


# KUISHI KATIKA BARAKA

KITABU CHA IBADA
BINAFSI KWA SIKU 365

Dkt. CHARLES "CHIC" SHAVER



***Maisha yamejaa milima na mabonde. Tunaweza kukubali kila tukio kwa furaha na ujasiri ikiwa tunaishi katika baraka.***

*Kuishi katika Baraka* ni kitabu cha ibada cha siku 365 kilichotokana na safari ya imani ya Dkt. Chic Shaver, ambaye amesafiri ulimwenguni akiwaleta watu kwa Yesu Kristo. Tafakari zimeandaliwa ili kuwahamashisha wasomaji watoke kwenye kanuni za msingi za Maisha ya Kikristo hadi kwenye utambuzi wa imani iliyokomaa na iliyo thabiti. Muundo rahisi na mwepesi unampa msomaji chaguo la kuyatumia kwa tarehe au kwa mpangilio wa kurasa.

Dkt. Charles “Chic” Shaver alimpokea Kristo akiwa mwanafunzi wa kujiandaa kusomea masomo ya sheria ya katika Chuo cha Dartmouth. Katika tajriba yake ndefu, amehudumu kama mchungaji, mwanzilishi wa makanisa, mwinjilisti, profesa wa seminari, na mwandishi. Anajulikana zaidi kupitia kitabu chake kinachoitwa *Basic Bible Studies for New and Growing Christians*, kilichouza zaidi ya nakala 750,000 za Kiingereza na kimetafsiriwa katika lugha 55. Dkt. Shaver amefanya mikutano karibu 900 ya uamsho, mahubiri na mafundisho ulimwenguni. Anaishi Leawood, Kansas, na mke wake Nancy. Wana watoto watatu ambao ni watu wazima, Rachel, Paul, na Miriam, na wajukuu na vitukuu kadhaa.

DINI/ Maisha ya Kikristo/ Ibada

ISBN: 978-0-8341-4084-4

# KUISHI KATIKA BARAKA

KITABU CHA IBADA
BINAFSI KWA SIKU 365

CHARLES "CHIC" SHAVER

THE FOUNDRY
PUBLISHING®

Hakimiliki © 2022 na Charles “Chic” Shaver
The Foundry Publishing®
PO Box 419527
Kansas City, MO 64141
thefoundrypublishing.com

978-0-8341-4084-4

Kimechapishwa
Marekani

... Hakuna sehemu ya kitabu hiki itatolewa tena katika mfumo wa aina yoyote, kutunzwa katika mfumo ambao kinaweza kusambazwa au kupatikana tena kwa namna au njia yoyote ile, au kubadilishwa katika namna yoyote ile, kwa mfano kielekroniki, kutolewa nakala kivuli, kurekodiwa, bila idhini ya maandishi kutoka kwa mchapishaji. Kinachoruhusiwa pekee ni nukuu fupi zilizochapishwa kwenye mapitio.

Msanifu wa sehemu ya ndani: Sharon Page

Data ya Uchapishaji katika Makataba ya Congress
Majina: Shaver, Charles, 1935- author.
Kichwa: Kuishi Katika baraka: Kitabu cha Ibada Binafsi kwa siku 365 / Charles “Chic” Shaver.
Maelezo: Kansas, MO: The Foundry Publishing, 2022. | Inajumuisha marejeo ya bibliografia na na faharisi. |
Muhtasari: “Kuishi katika Baraka ni Kitabu cha Ibada Binafsi kwa siku 365 kilichohamasishwa na safari ya imani ya Dr. Charles “Chic” Shaver, aliyesafiri ulimwenguni na kuwaleta watu kwa Yesu Kristo. Maombi na tafakari hizi binafsi zimeandaliwa kutokana na vidokezo vya maisha ya Kikristo kwenye tafakari za imani komavu na kubwa”— zilizotolewa na mchapishaji.
Vitambulisho: LCCN 2021038156 (print) | LCCN 2021038157 (ebook) | ISBN 9780834140844 | ISBN 9780834140851 (ebook)
Mada: LCSH: Kalenda za maombi ya kibinafsi.
Mpangilio: LCC BV4811 .S3763 2022 (print) | LCC BV4811 (ebook) | DDC 242/.2—dc23
Rekodi ya LC inapatikana kwenye https://lccn.loc.gov/2021038156
Rekodi ya kitabu pepe cha LC inapatokana kwenye https://lccn.loc.gov/2021038157

Isipokuwa imebainishwa vinginevyo, nukuu yote ya Maandiko imechukuliwa kutoka katika Biblia ya Kiswahili – Union Version iliyochapishwa na Chama cha Biblia cha Kenya na Chama cha Biblia cha Tanzania.® © 1997 Chama cha Biblia cha Kenya na Chama cha Biblia cha Tanzania. Haki zote zimehifadhiwa Ulimwenguni kote.

Maandiko yote yamenukuliwa kutoka katika Biblia ya Swahili Union Version

... ... ...

*Msisitizo wa mwandishi umeoneshwa kwa kutumia herufi zilizolala*.

Warner Sallman's *Christ at Heart's Door* © 1942, 1970 Warner Press, Inc., Anderson, IN, kimetumiwa kwa ruhusa.

Anwani za intaneti, anwani za baruapepe, na nambari za simu zilizo katika kitabu hiki zilikuwa sahihi wakati wa kuchapishwa kitabu hiki. Zimetolewa kama nyenzo. Kampuni ya Foundry Publishing haiwathibitishi au kutetea maudhui yao au kudumu kwake.

10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

***Kwa Nancy***

*Mbali na Yesu Kristo, umekuwa mtu muhimu zaidi na umeyagusa maisha yangu sana. Katika miaka ya uchungaji, huduma ya uinjilisti, kufundisha, na kuandika, umekuwa mtu aliyenitia moyo, mshauri wangu, msaidizi, na mwombeaji. Uwekezaji wako katika watoto wetu watatu ni wa hali ya juu sana. Tangu uimbe na kung'aa kama mwanafunzi wa uuguzi mwenye umri wa miaka ishirini katika mkutano wa uvuvio huko St. Joseph, Missouri, moyo wangu umeguswa. Bado unaguswa. Tumekuwa na vipindi vya kusisimua katika kumfuata Yesu pamoja nchini kote na ulimwenguni. Umekuwa sehemu ya yale yote niliyopitia na ukweli ulio katika kitabu hiki.*
*Asante kwa kuwa mpenzi wangu!*

***Kwa marafiki zetu** wapendwa ambao wameyarefusha maisha yetu na kutumiminia upendo mwingi sana.*

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Shukrani | 6 |
| Kuhusu Mwandishi | 7 |
| Pia na Mwandishi | 9 |
| Utangulizi | 11 |
| Ndani ya Siku Zijazo | 14 |
| Ibada Binafsi ya Kwanza | 15 |
| Faharasa ya Maandiko | 527 |

# Shukrani

❖

Asante Joy Parke—mwanamke wa Mungu, rafiki mpendwa wa Kikristo, aliyekuwa mkurugenzi katika Chic Shaver Center for Evangelism, na mpiga taipu na msanifishaji wa mswada wa kwanza wa vitabu hivi vya ibada binafsi. Joy, siwezi kukushukuru vya kutosha kwa uandaaji wako kwa uangalifu, masahihisho ya sarufi na mtindo, kuipienda kazi, kujitoa, na zaidi. Una sehemu ya baraka zote zinazotiririka kutoka ndani ya kitabu hiki.

# Kuhusu Mwandishi

Charles F. Shaver, Jr., alizaliwa Manchester, Connecticut, mnamo Januari 5, 1935. Ili kuweza kumtofautisha na jina la baba yake, alipewa jina la utani la "Chic" tangu akiwa mdogo. Alilelewa pamoja na dada yake Joanne katika familia nzuri, iliyojiweza. Baba yake alikuwa muuzaji kwenye Duka la Vifaa la Yale na Towne, kisha baadaye katika maisha yake, alimiliki na kuendesha hoteli ya wasafiri katika Treasure Island, Florida. Mama yake Chic, Vera, alikuwa mama anayesimamia nyumba yake vizuri.

Chic alisoma katika chuo cba Dartmouth College na kusoma kozi ya kujiandaa kusomea sheria na alipenda sana siasa. Kupitia ushahidi wa rafiki yake Peter Gunas, Chic alishuhudia kumpokea Kristo kwa namna ya ajabu mnamo Novemba 20, 1955. Alipohisi kwamba kuna hitaji la kuishi maisha ya ushindi zaidi kama Mkristo, mnamo tarehe 2 Septemba, 1956, alitakaswa kabisa kwa kujazwa na Roho Mtakatifu. Kufikia wakati wa kufuzu kwake kutoka chuo cha Dartmouth, alihisi wito wa kumtumikia Mungu.

Chic alipokuwa akihubiri kwenye mikutano ya uvuvio ya vijana huko St. Joseph, Missouri, msichana mmoja aliyekuwa ni mwanafunzi wa uuguzi aliitwa aimbe wimbo maalum. Basi Nancy Doro alipoimba, Chic alisema, "alikuwa anang'aa." Walifunga ndoa mnamo tarehe 1 Juni, 1959. Watoto wao ni Rachel, Paul, na Miriam.

Chic ana shahada ya BA kutoka Dartmouth College, MDiv kutoka Nazarene Theological Seminary, na DMin kutoka Fuller Seminary. Uchungaji wake wa kwanza aliufanyia katika kibanda cha farasi kilichokarabatiwa. Mnamo 1967, alianza kufanya huduma kama mwinjilisti wa kudumu wa kwenda hapa na pale; mwaka 1969, alihubiri kwa jumla ya Jumapili arobaini na sita wakati wa ibada za uvuvio. Mnamo mwaka 1970, aliitwa akafundishe uinjilisti katika Nazarene Theological Seminary. Aliendelea kutumika katika wadhifa huo, na hatimaye akateuliwa kuwa profesa wa Uinjilisti katika Frank and Gladys Cooper. Alistaafu mnamo mwaka 2000. Kuanzia mwak 1974 hadi 2003, pia alihudumu kama mchungaji katika First Church of the Nazarene huko Kansas City, Missouri. Aliendelea kufanya huduma yake ya uvuvio na uinjilisti hadi mwaka 2020, akiendesha takriban mikutano 900 ya uvuvio. Amehubiri na/au kufundisha uinjilisti nchini Afrika Kusini, Ufilipino, Korea, Urusi, na katika makao makuu ya Bill Graham.

Wasiwasi wake juu ya Wakristo wachanga ulimfanya aandike kitabu kiitwacho *Basic Bible Studies for New and Growing Christians*, ambacho

kiliuza zaidi ya nakala 750,000 za Kiingereza na kimechapishwa katika lugha zaidi ya hamsini na tano. Vitabu vyake vingine vinatumiwa namadhehebu mbalimbali na ni pamoja na *Witnessing without Fear, Living in the Power of the Spirit, The Bible Speaks to Me about My Witness,* and *Basic Bible Studies for the Spirit-Filled and Sanctified Life.* Tangu mwaka 1992, ametumika kama mkurugenzi mtendaji wa Chic Shaver Center for Evangelism.

Mnamo mwaka 2019, katika Kongamano la Church of the Nazarene's M19, Dr. Shaver na Nancy walipewa Tuzo ya Lifetime Achievement. Kama mume, baba na babu, mhubiri, mwalimu, mwandishi, mchungaji, na mwinjilisti, moyo wa Chic unang'aa kwa uwepo wa Mungu na kuwajali watu kila mahali wamjue Kristo katika ngazi ya mtu mmoja.



*Chic na Nancy wakiadhimisha miaka hamsini na tano ya ndoa yao*

# Pia na Mwandishi

❖

Nimekuwa na uhusiano mrefu, wa kutia moyo, na mzuri na The Foundry Publishing. Hapa kuna orodha ya vitabu vingine, CD, na DVD ambavyo vimechapishwa na kampuni hii kwa miaka kadhaa. Ukitaka kuagizia, unaweza kuwasiliana na Foundry kwa kutumia anwani ifuatayo:

The Foundry Publishing
PO Box 419527
Kansas City, MO 64141-6527
1-800-877-0700
orders@thefoundrypublishing.com

| | |
|---|---|
| 978-0-8341-2502-5 | *Who Is This Jesus? The Gospel of John Chapters 1–15* (2009) |
| 978-0-8341-2503-2 | *The Mission of Jesus: The Gospel of John Chapters 12–21* (2009) |
| 978-0-8341-0411-2 | *Conserve the Converts: A Manual to Help Conserve the Results of Personal and Mass Evangelism* (1976) |
| S-250 | *Living in the Power of the Spirit* (1986) |
| S-250LG | *Living in the Power of the Spirit, Leader Guide w/ DVD* (2004) |
| CDR-1 | *People, Sex, & God: A Biblical Approach (CD)* (2007) |
| CDR-2 | *A New Creation: My Personal Testimony (CD)* (2006) |
| DVD-1701 | *A Personal Evangelism Call (DVD)* |
| VE-80 | *Basic Bible Studies for New and Growing Christians* (1972) |
| VE-91 | *Basic Bible Studies for the Spirit-filled and Sanctified Life* (1991) |
| 978-0-8341-2058-7 | *Basic Bible Studies in Everyday English* (2003) |
| U-4040 | *Witnessing Without Fear* (2001) |
| CDR-1695 | *Sermons on the Spirit-filled and Sanctified Life* (2008) |
| CDR-1595 | *Lord, Teach Us to Pray (CD)* (2008) |

# Utangulizi

Nilipokuwa ninakua, hata ingawa nililelewa katika kanisa la Kiprotestanti, Mungu hakuwa halisi kwangu. Nilipokuwa nikisomea maandilizi ya kujiunga na chuo cha sheria cha Dartmouth College, nilikutana na Peter, kiongozi wa wanafunzi ambaye awali aliacha kusoma kwa sababu ya pombe lakini sasa alikuwa amerudi. Mara tu baada ya ibada chuoni, Peter alinipa mkono na kusema, "Chic, mimi ni mtu tofauti na jinsi nilivyokuwa awali kwa sababu nilimpata Bwana."

Maneno ya Peter yalinigusa. Sikuwa nimewahi kumsikia mtu yeyote akisema hivyo—Mungu alikuwa halisi kwake. Wiki chache baadaye, Peter alikuja kwenye bweni langu na kunisimulia kwa kina jinsi alivyokutana na Kristo na kumpokea. Alinialika kanisani kwake. Mnamo tarehe 20, Novemba mwaka 1995, katika ibada ya Jumapili usiku, Kristo aliingia moyoni mwangu na maishani mwangu. Nilijua nimesamehewa, na Mungu alikuwa halisi kwangu na alikuwa ndani yangu. Nilihisi furaha kubwa.

Nilikua kiroho katika muda wa miezi michache. Biblia ilikuwa hai kwangu, na nilishuhudia uhusiano wa karibu na Mungu katika maombi. Niliwashuhudia wengine juu ya imani yangu wakati mwingi, sikukosa ibada kanisani, na nilishuhudia mabadiliko makubwa katika maisha yangu ya kila siku.

Takriban miezi 6 katika maisha haya mapya, nilianza kuona nina hasira kali ikichipuka kutoka katika kilindi cha nafsi yangu—uchungu, wivu, kiburi, roho ya kukosoa, na ukosefu wa nguvu za kiroho katika kujaribu kuwashawishi wengine. Nguvu zangu mwenyewe hazikutosha kutatua matatizo haya.

Katikati ya wasiwasi wangu uliokuwa unaongezeka, nilianza kusikia na kusoma ahadi za maisha ya kiroho yenye kina—maisha ya ushindi. Maisha haya ya kina yalirejelewa kwa maneno kama: "kutakaswa kweli kweli;" "kujazwa kwa Roho Mtakatifu;" "mapumziko ya imani;" "kusulubiwa pamoja na Kristo;" "utakatifu;" "maisha ya utele." Nilianza kumtafuta Mungu anipe jibu lake.

Mnamo tarehe 2, Septemba, 1956, Mungu alinijibu maombi yangu kwa njia ya ajabu kwa ajili ya maisha haya mapya kwa kunitakasa moyo wangu kwa njia ya moto. Nilifia yule Chic Shaver wa zamani, na Roho Mtakatifu wa Mungu akanijaza na kunitakasa kweli kweli. Punde si punde, maisha yangu yote ya Kikristo yalibadilika kufikia kiwango kipya, na cha juu.

Nilikuwa na mambo mengi ya kujifunza. Zaidi ya kipindi kile cha kujazwa na Roho, kulikuwa na maisha ya kuishi na kuenenda kwa Roho. Wagalatia 5:25 kilikuwa kifungu changu kikuu: "Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho."

Kufikia wakati huu, nilikuwa nimepokea wito wa huduma, na nilianza kuhubiri na kufundisha maisha haya kwa wengine. Baada ya muda, niligundua kwamba Wakristo wengi walikuwa wamechanganyikiwa au hawana hakika na maisha haya ya kina. Nilipofikia sehemu fulani ya maisha yangu na huduma baadaye, msukumo mkubwa ulikua ndani yangu kuandika kitabu cha ibada ya kila siku juu ya maisha haya ya utakatifu kwa lugha ambayop ingeeleweka kwa watu wa kawaida. Nimejumuisha tafakari kadhaa zilizoandikwa na binti zangu, Rachel na Miriam, na mke wangu Nancy.

Sasa hivi umekishikilia mkononi kitabu hicho. Andiko na ukweli hutiririka kila siku. Nimejaribu kuonesha jinsi kweli hizi zinavyofanya kazi katika maisha ya kila siku. Katika kufanya hivyo, nimerejelea vitabu vingine na waandishi wengine; shuhuda za Wakristo wa zamani; mahojiano na Wakristo wa leo; na uzoefu wangu mwenyewe wa maisha.

Unaweza kutumia kitabu hiki cha kutafakari pamoja na usomaji wako wa Biblia; unaweza hata kuwa na jarida la mawazo yako, ufahamu, na maombi kadiri unavyoendelea. Unaweza kutumia kitabu hiki kila siku kulingana na tarehe za kalenda. Huenda wewe ni Mkristo mchanga na umeanza maisha yako na Kristo katikati ya mwaka kwenye kalenda. Utaona mfumo mbadala, ambao ni mfumo wa nambari wa kutoka 1 hadi 365. Unaweza kuanza na nambari 1 hata ukiwa katikati ya mwaka. Pengine umekuwa katika mafundisho ya Biblia pamoja na rafiki yako katika imani yako mpya. Baadhi yenu huenda mmepitia kitabu cha *Basic Bible Studies for New and Growing Christians*. Tafakari hizi zitaendana na kuongezea uzito yale ambayo umekuwa ukijifunza.

Kwa hiyo natuanze safari hii ya kusisimua pamoja, "mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu" (Waefeso 3:19). Usitishwe na agizo hilo gumu; vifungu vinavyofuata kutoka Waefeso 3 vinasema, "Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam, atukuzwe" (fungu la 20–21).

Kati ya umri wa miaka thelathini na mitatu na hamsini na nane, mtoto wangu wa kiume, jina lake Paul, alifanyiwa upasuaji mkubwa mara tano wa saratani, upasuaji ule mkubwa zaidi ulikuwa ni kuondoa koromeo lake. Na bado, ana furaha na anaishi maisha ya furaha. Watu wengi walimuuliza wakasema, "Inawezekanaje?"

Naye kwa sauti yake mpya, yenye mikwaruzo alijibu, "nilikuwa ninaishi chini ya baraka kabla sijapata saratani, nilikuwa chini ya baraka baadaye walipoondoa koromeo lake, na bado ninaishi chini ya baraka leo." Kwa sababu hii, nilipokuwa ninatafuta jina la kitabu hiki, Paul alipendekeza *Kuishi Katika Baraka*.

Wahubiri wa kwanza wa nyakati za Utakatifu walikiita "baraka ya pili." Wimbo wa utakaso "Yote kwa Yesu" unajumuisha kifungu kifuatacho:

*Yote namtolea Yesu,*
*Moyo wangu ni wake;*
*Ninavutwa na upendo,*
*Kwa hivyo najitoa.*[1]

Wengine wanaamini kwamba maneno ya Paulo katika Warumi 15:29—"Nami najua ya kuwa nikija kwenu nitakuja kwa utimilifu wa baraka ya Kristo."—kinazungumzia maisha yake mwenyewe yaliyotakaswa na kujazwa na Roho. Haijalishi ni kweli au si kweli, tuna hamu ya kumwona kila mtu akishuhudia utakaso kamili wa kujazwa na Roho. "Tukienenda kwa Roho" (Wagalatia 5:25) kila siku, tunaweza kusema kwa hakika, "Tunaishi katika baraka!"

Vitabu hivi vya ibada binafsi vimejaa simulizi za watu halisi. Katika mifano mingi nimebadilisha majina ya watu ili wasijulikane, lakini hadithi zenyewe ni za kweli.

Kitabu hiki kinajumuisha vitabu kadhaa vya ibada binafsi vilivyoandikwa na watu wengine; katika mifano kama hii, majina halisi ya waandishi yameorodheshwa. Aidha, kwa miaka mingi, mimi na mke wangu Nancy tumeandika vitabu vya ibada binafsi katika machapisho mbalimbali. Kwa ruhusa yao, tumejumuisha vitabu kadhaa vya ibada binafsi katika kitabu hiki.

1. Judson W. Van DeVenter (words), Winfield S. Weeden (music), 1896, "I Surrender All," *Sing to the Lord: Hymnal* (Kansas City, MO: Lillenas Publishing Company, 1993), #486.

# Katika Majaliwa Yako

❖

Mtume Paulo aliichukulia huduma yake kwa uzito. Alisema, "ili niwe mhudumu wa Kristo Yesu kati ya watu wa Mataifa, niifanyie Injili ya Mungu kazi ya ukuhani, kusudi Mataifa wawe sadaka yenye kibali, ikiisha *kutakaswa na Roho Mtakatifu*" (Warumi 15:16). Katika sura hiyo hiyo alisema, "Nami najua ya kuwa nikija kwenu *nitakuja kwa utimilifu wa baraka ya Kristo*" (kif. 29).

Katika Zaburi, Daudi anauliza, "Ni nani atakayepanda katika mlima wa BWANA? Ni nani atakayesimama katika patakatifu pake? Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe, Asiyeiweka nafsi yake katika uongo, Wala hakuapa kwa hila. Atapokea *baraka kwa BWANA* na haki kwa Mungu wa wokovu wake" (Zaburi 24:3–5).

Kwa Waefeso, Paulo alifurahi na kusema, "Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa *baraka zote za rohoni*, katika ulimwengu wa roho, *ndani yake Kristo*" (1:3).

Kwa kila mtu anayesoma kitabu hiki, naomba uishi katika masomo yake na uendelee *kuishi katika baraka*.

# Ni Mkuu Kuliko . . .

❖

*Ninyi, watoto wadogo, mnatokana na Mungu nanyi mmewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia.*
*1 Yohana 4:4*

Jambo la ajabu lilitokea kwako ulipompokea Yesu Kristo. Ufunuo 3:20 ina maneno haya: "Tazama! Nasimama mlangoni, nabisha. Mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami."

Tunaelewa kwamba mtu akimfungulia Kristo mlango wa moyo wake, Kristo huingia. Anasema atakula pamoja na mtu huyo, ambayo ndio njia yake ya kudhihirisha ushirika wa kina. Kwa sababu ya kweli hizi, unaweza kusema waziwazi, "Kristo anaishi ndani yangu."

Kabla andiko la leo katika 1 Yohana 4:4, Yohana anawaonya wasomaji juu ya pepo wachafu na manabii wa uongo ulimwenguni. Kisha Yohana anawahakikishia Wakristo wote wa kweli kwamba *Kristo kuishi ndani yao ni zaidi* ya nguvu yoyote ya uovu ulimwenguni. Kwa uwepo wake na nguvu zake, tunaweza kushinda uovu wowote.

Hebu fikiria juu ya faida zote ambazo sasa ni sehemu ya maisha yako kwa sababu Kristo anaishi ndani yako:

- Dhambi zako zote *zimesamehewa*. "Nawaandikia ninyi, watoto wadogo, kwa sababu mmesamehewa dhambi zenu, kwa ajili ya jina lake" (1 Yohana 2:12).
- Sasa uko *hai* kiroho. Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alitufanya kuwa hai pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema" (Waefeso 2:4-5).
- Sasa tunaweza *kufarijiwa* katika sehemu yote ngumu katika maisha. "Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo, tunazofarijiwa na Mungu" (2 Wakorintho 1:3-4).
- Sasa mko chini ya nguvu za Mungu *zinazothibitisha*. "Ambaye atawathibitisha hata mwisho, ili msilaumiwe siku ile ya Bwana wetu Yesu Kristo" (1 Wakorintho 1:8).

- Mungu atawabeba nyinyi na maisha yenu mapya hadi *yamalizike vizuri*. "Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu" (Wafilipi 1:6).

Maisha ya Peter yalijaa pombe na uzinzi. Kwa viwango vya leo, alikuwa akitumia dola elfu moja kwa mwezi kununua pombe. Hali ilikuwa mbaya sana kiasi kwamba alijiuzulu nafasi yake katika timu ya kandanda ya chuoni na pia akajiuzulu kama raisi wa kundi lake. Aliacha kusoma chuoni. Alianza kuishi hapa na pale kwenye pwani ya mashariki ya Marekani. Alilala upande wa nyuma wa gari lake na akakabiliana na polisi katika majimbo sita tofauti. Maisha yake yalivurugika.

Peter alipishana naWakristo wengine ambao maisha yao yalikuwa tofauti kabisa na yake. Mmoja wa Wakristo hawa alimwambia kwamba tofauti ni Yesu. Peter alijisemea moyoni, *Pengine huyo ndiye ninayemhitaji*.

Basi alianza kutafuta. Mnamo Jumapili moja, alipokuwa akisikiliza mahubiri, dhambi zake zilipita mbele yake kama mwanga, na Mungu akawa halisi kwake. Peter aliondoka pale kanisani kwa haraka sana na akaendesha gari hadi mahali ambapo palikuwa pametulia katika nchi. Akapiga magoti na akaziungama dhambi zake. Baadaye, alipokuwa akielezea hali ilivyokuwa wakati huo, Peter angesema, "Mungu alinibadilisha." Alikiri kwamba lilionekana kuwa jambo lisilokuwa la kawaida lakini alisema, "Nilitambaa kuelekea juu ya viti vya gari na nikalala—ulikuwa usingizi wa kwanza wa amani nilioupata tangu nikiwa na umri wa miaka minne." Peter alikombolewa.

Peter alikua kiroho na kuanza kuwaambia wengine yale Yesu alikuwa ametenda. Baada ya muda mfupi alisajiliwa tena katika chuo kilekile alichokuwa ameacha kusoma. Katika miaka iliyofuata, aliishi maisha ya Kristo ya furaha na akawa mtu anayeomba sana na mwalimu wa Biblia.

Peter ndiye mtu aliyenileta kwa Yesu.

Faida zote za kuwa Mkristo zilizorodheshwa hapo juu zilikuwa kweli katika maisha ya Peter; zinaweza kuwa kweli katika maisha yako pia. Kristo ndani yako ni mkuu zaidi ya nguvu zozote za uovu duniani. Unaweza kushinda.

# Mwaka Mpya, Mwanzo Mpya

*Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya: Ya kale yamepita, tazama yamekuwa mapya!*
2 Wakorintho 5:17

Kila Januari, watu wengi huweka maazimio ya Mwaka Mpya. Maazimio haya ni yale matumaini yanayodhihirishwa ya kutaka kubadilisha mambo mabaya ya zamani, na kuwa na mambo mazuri mapya. Mara kwa mara, watu hushindwa kutimiza waliyoahidi kuyatekeleza.

Njia ya Mungu ya kuanza upya ni kukusaidia kuwa na uhusiano binafsi na Kristo. Kuwa "ndani ya Kristo," kama kifungu kinavyosema, huleta njia mpya, maisha mapya, na kiumbe kipya.

Shuhuda mbalimbali zinazotolewa baada ya wiki ya uvuvio huko kanisa la Michigan zinadhihirisha jinsi Kristo anavyoweza kumfanya mtu kuwa mpya. Hizi hapa ni baadhi ya shuhuda hizo chache:

- Mama wa makamu alipata furaha mpya: "Nilifanyiwa upasuaji wa moyo wa papo hapo—Mungu aliuondoa uchungu wangu."
- Shemasi alipokea: utakaso kutokana na "roho ya kukosoa."
- Mama mwingine alisema: "Roho alinipa amani na nguvu."
- Mwanafunzi wa sekondari alishukuru kwa kuweza "kuwa katika hali nzuri tena."
- Nyanya mmoja alisema: "Si kuhusu mimi; ni kuhusu Yesu."
- Mshauri mmoja wa shule alitoa ushuhuda na kusema: "Neno moja hunijia akilini—kujisalimisha."
- Mtaalam wa mashine mwenye ujuzi mwingi aliguswa na ahadi ya Andiko isemayo "hakuna hukumu!"
- Mshirika mwingine alikumbuka chanzo endelevu cha nguvu za kiroho: "Nilisahau jinsi kwa kweli tulivyo watu wa kawaida . . . na jinsi nilivyohitaji kurudi katika uwepo wake."

Je, ni kitu gani kipya Kristo amekutendea katika mwaka uliopita? Je, ni kitu gani kipya Kristo atakutendea mwaka huu?

# Usimzuie Mteule wa Mungu

*Yoshua mwana wa Nuni, mtumishi wa Musa tangu ujana wake, akajibu akasema, "Ee bwana wangu Musa uwakataze!" Musa akamwambia, "Je! Umekuwa na wivu kwa ajili yangu? Ingekuwa heri kama watu wote wa BWANA wangekuwa manabii na kama BWANA angewatia roho yake!"*
*Hesabu 11:28–29*

Je, si ni vizuri kwamba Baba yetu wa mbinguni ameshika usukani? Ninasema natufurahi na kushukuru popote, wakati wowote, na vyovyote vile Mungu anavyochagua kufanya kazi. Natutoe, natuhimizane, tusaidiane, tushangaliliane, na tujaliane kadiri tunavyoendelea na kazi ya Baba yetu.

Mtu asituondelee furaha yetu. Mtu asisime ndoto zetu haziwezi kutimia. Mtu asilete mtazamo wake hasi kwenye maono yetu kutoka kwa Mungu, kwa sababu yeye huchagua watu wasiotarajiwa, huwatumia wale watu wanaopatikana, huchagua wale wazuri zaidi, huwagusa wale nisiodhani wako tayari, huwaita wale ambao tayari wana shughuli. Ananishawishi kwamba "ninaweza" kwa nguvu zake, ananitoa katika sehemu nilizozoea kwa sababu ananijali sana, na yeye hunipa nafasi ya pili wakati wote.

Kwa hiyo, na tuendelee mbele wakati tunapitia shida. Na tuendelee mbele wakati hatuoni vizuri. Na tuendelee mbele wakati tunakumbwa na mashaka na woga. Na tuendelee mbele hadi tufike nyumbani—kwa sababu tumechaguliwa.

Nancy Shaver[2]

---

2. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Septemba–Oktoba-Novemba 1998 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 91. Imetumiwa kwa ruhusa. (Chapisho hili liligeuka kuwa *Reflecting God*.)

# Je, Kuna Mungu?

*Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono yake. Mchana husemezana na mchana, Usiku hutolea usiku maarifa.*

*Zaburi 19:1–2*

Mtu asiyeamini kuna Mungu husema hakuna Mungu. Mkana Mungu huwa na mashaka na husema, "Sina hakika kama kuna Mungu." Mimi nilikuwa mkana Mungu wakati nikianza kuwa mtu mzima, hata ingawa nililelewa katika mazingira ya kanisani.

Nilipokuwa chuoni, nilisumbuka. Nilijisemea, *Kama kuna Mungu, afadhali nisuluhishe hili*. Nilihisi mimi ni mtu ninayependa mantiki na mwenye ari ya kuwaza na kuwazua. Hatimaye nilipata mawazo sita ya kimsingi:

1. Nina saa nzuri sana inayofanya kazi vizuri sana. Kama vile ilivyo vigumu kuamini kwamba kuna saa pasipo mtengenezaji saa, ndivyo ilivyo vigumu kuamini kwamba kuna dunia nzuri pasipo kuwa na muumba dunia.
2. Kama ulimwengu wote unaweza kuangamizwa kwa nguvu za atomiki katika mwaka mmoja (kama profesa wangu wa kemia alivyofundisha), basi hatimaye maisha hayana maana isipokuwa kuwe kuna Mungu na maisha baada ya kifo.
3. Kama hiyo ni kweli na kuna Mungu, basi kitu muhimu zaidi duniani kingekuwa ni kumjua yeye.
4. Kama Mungu si halisi kwangu (na hakuwa hivyo), lazima kuwe na kuzuizi kati yetu. Kuna uwezekano mkubwa kwamba kizuizi kinasababishwa na mimi kumpuuza au dhambi ninazomtenda.
5. Kama yeye ndiye mkosewa na kuna kizuizi kati yetu, basi ana haki ya kuniambia kukivuka kizuizi na kumwendea.
6. Hicho ni kitu cha hali ya juu alichofanya katika kumtuma Yesu Kristo hapa ulimwenguni—yeye ndiye daraja la kile kizuizi cha kumfikia Mungu.

Paulo anaangazia ukweli huu kwa uwazi sana anaposema, "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake" (2 Wakristo

5:19). Na zaidi ya hayo, "Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye" (kif.21).

Kutokana na mahitimisho haya, nilikwenda nje kumtafuta Mungu. Na baada ya miezi kadhaa, kwa ukarimu wa Mungu kwangu, nilimpata. Je, wewe uko wapi? Je, umetoka nje kumtafuta?

**JANUARI 5** **5**

# Kuongoka—Nini Kinachofuata?

*Lakini Barnaba akamtwaa, akampeleka kwa mitume.*
*akawaeleza jinsi alivyomwona Bwana njiani,*
*na ya kwamba alisema naye, na jinsi alivyohubiri kwa*
*ushujaa katika Dameski kwa jina la Yesu.*
*Matendo 9:27*

*Kisha akatoka akaenda Tarso kumtafuta Sauli; hata*
*alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Kwa hiyo kwa*
*mwaka mzima Barnaba na Sauli walikutana na kanisa.*
*Matendo 11:25-26*

Kuongoka pia kunaitwa "kuzaliwa mara ya pili" (Yohana 3:3). Kunalinganishwa na uzazi wa kimwili. Hebu fikiria, kama baada ya kuzaliwa, kile wazazi wako wangefanya ni kuongea juu ya wakati ule ulipozaliwa. Wasingekushikilia, kukuogesha, kukulisha, au kukutunza. Je, hali yako ingekuwaje baada ya wiki tatu? Ungeugua na kufa.

Kwa hiyo katika maisha ya kiroho, baada ya kuongoka—au kuzaliwa mara ya pili—lazima utunzwe, ulishwe kiroho, uongozwe. Barnaba, ambaye pia aliitwa "mwana atiaye moyo," ni mmoja wa wanafunzi wazuri zaidi, au mfanya kazi wa ufuatiliaji, katika Biblia. Yeye ndiye aliyemwendea Sauli (baadaye aliitwa Sauli), akajenga daraja lililomwingiza katika maisha ya kanisa, na akafanya kazi pamoja naye mara kwa mara hadi Sauli akawa kiongozi mkubwa wa kiroho. Barnaba na Sauli walihudumu pamoja huko Antiokia (Matendo 11:26) na wakatumwa na kanisa lote kwenda safari ya kimishenari (13:2-3).

Mambo hayo hayo ndiyo yanayofanyika leo. Dave, kijana aliyekuwa mtu mzima, alikuwa mgeni katika mji. Alipoona sehemu ya kuoshea magari iliyomilikiwa na kanisa la vijana, alisimama. Wale vijana walioosha gari lake walikuwa wacheshi sana kiasi kwamba aliamua kulitembelea kanisa lao

Jumapili. Baada ya safari yake hiyo, mchungaji mmoja alimpigia simu na akamwomba kama wanaweza kumpitia. Dave alikubali kwa furaha.

Basi yule mchungaji aliandamana na mwanafunzi mmoja wa chuo cha Biblia aliyeitwa Dan, ambaye alikuwa akimfundisha stadi za uchungaji. Wakati wa kumtembelea Dave kwake nyumbani, waligundua kwamba Dan alikuwa amempokea Kristo chuoni na sasa alikuwa mjini kufanya kazi ya uhandisi. Mchungaji akapendekeza kwamba Dave aanze mafundisho ya *Basic Bible Studies for New and Growing Christians*, na Dan akakubali kukutana na Dave kila wiki kupitia masomo yake. Dave alikua kiroho kupitia upendo na mwongozo wa Dan na baadaye alijiunga na kanisa kwa kuitangaza imani yake. Hatimaye alifunga ndoa na Linda, msichana aliyemcha Mungu na aliyekutana naye kupitia shughuli ya kanisani.

Dan alimaliza masomo yake seminari na kuanza uchungaji wake wa kwanza. David na Linda walihamia jimbo jingine, ambapo walihudumu kikamilifu katika kanisa lao. David alifanyika mweka hazina na hatimaye akachapisha kitabu chenye nguvu nyingi za kiroho.

Barnaba na Sauli. David na Dan. Utaratibu ni uleule: baada ya kuongoka/kuokoka huja ukuaji, nguvu, na huduma kwa sababu ya uanafunzi wa kiuaminifu. Je, wewe unaingia wapi katika kisa hiki?

**JANUARI 6** **6**

# Johnny na Penny Jar

*Tubu, kisha, mgeukie Mungu.*
*Matendo 3:19*

*Uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru,*
*waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate*
*msamaha wa dhambi zao na urithi miongoni mwao waliotakaswa*
*kwa imani iliyo kwangu mimi.*
*Matendo 26:18*

Baba yake alikuja nyumbani mara nyingi na kutumbukiza chenji zake zote za pesa kwenye “kibubu.” Lilikuwa birika kubwa lenye tundu ndogo kiasi. Pesa hii wakati wote ilihifadhiwa kwa ajili ya mradi maalum wa familia. Sheria ya familia ilikuwa kwamba hakuna mtu aliruhusiwa kutumbukiza mkono ndani

ya kibubu hadi Baba alipoona kuwa wakati wa mradi wa familia ulikuwa umefika.

Siku moja, Baba na Mama waliondoka nyumbani kwa muda mfupi kwenda kuchukua zawadi ya kumshangazia Jonny. Waliondoka nyumbani, wakitarajia kwamba atakuwa na tabia njema kabisa.

Mara tu walipoondoka, Johnny aliamua kutwaa pesa kutoka ndani ya kibubu, na kwenda kununua peremende kwenye duka lililokuwa karibu, ale, na ahakikishe kibubu kimerudishwa mahali pake kabla wazazi wake hawajarudi—hakuna mtu angaliyekuwa mwerevu zaidi. Ilikuwa vigumu kutumbukiza mkono wake kupitia tundu la kibubu, lakini alisukuma mkono wake na kuzifikia sarafu na kuchukua kiasi cha kutosha kujaza mkono wake. Lakini kulikuwa na tatizo—mkono wake uliojaa sarafu ulikuwa mkubwa zaidi kiasi kwamba haukuweza kuuchomoka kupitia tundu la kibubu hicho. Ghafla, akasikia mlango wa gari ukifungwa, na akatambua kwamba wazazi wake wangeingia ndani ya nyumba baada ya muda mfupi.

Kwa akili yake ya kitoto, akafikiria, "Ninaweza kushikilia zile sarafu za thamani kwa mkono wangu uliokwama kwenye kibubu, au ninaweza kuziachilia hizi sarafu na kuufanya mkono wangu uwe mdogo kiasi cha kuweza kuuvuta nje ya kibubu Ninaweza kupata uhuru wangu, au ninaweza kuendelea kushikilia sarafu na mkono wangu unaswe na nishikwe na wazazi wangu."

Basi Jonny alichagua uhuru, akaziachilia zile sarafu, na kurudisha kibubu mahali pake. Mama na baba yake walikuwa wamesisimka wakati walipoingia ndani na kuweka zawadi yake mezani. Kwa sababu alikuwa ameachiliza zile sarafu, mikono yake ilikuwa huru kabisa kupokea zawadi.

Toba ni kuachilia dhambi zetu. Wokovu ni kupokea karama ya msamaha wa dhambi. Huwezi kuendelea kuzishikilia dhambi zako na bado upokee msamaha wa Mungu. Ziache dhambi na umgeukie Mungu ili uweze kupokea.

**JANUARI 7** **7**

# Hakuna Hukumu

*Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.*
*Warumi 8:1*

Dhambi mbili nilipokuwa na miaka sita, dhambi nne nilipokuwa na miaka minane, dhambi nane nilipokuwa na miaka kumi . . . na kadiri nilivyokuwa karibu na wakati wa sasa, ndivyo nilivyoona dhambi na ubinafsi mwingi zaidi. Nilihisi hatia, hukumu, na kujisikitikia. Hebu wazia tukio hilo kwa muda.

Kwa nini tunahisi kuhukumiwa? Wengine wetu tunahishi kuhukumiwa kwa sababu tunashindwa kuelewa dhambi na makosa. Kutenda dhambi ni kuvunja sheria ya Mungu inayojulikana. Kosa linaweza kutofikia mapenzi makamilifu ya Mungu, lakini kwa sababu linatendwa kwa kutojua, au kwa nia njema, basi ni kosa. Hata Yakobo anatambua hili anapoandika na kusema, "Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi" (Yakobo 4:17). Lazima *ujue* habari zake ndipo iwe dhambi. Ukirundika dhambi na makosa pamoja, utajihukumu bila haja ya kufanya hivyo kwa kufanya makosa.

Wengine huhisi kuhukumiwa kwa sababu hawajioni kuwa watu wazuri. Mawazo wanayojiwazia juu yao, pengine yakitokana na wakati wakiwa watoto ni, "Sina thamani sana vile," au "Sina talanta sana vile." Lakini hivyo sivyo Mungu anavyowaza juu yao—Mungu anawathamini sana kiasi kwamba alimtoa mwanawe wa pekee ili kuwapa msamaha na wokovu wao: "Kwa maana jinsi hii mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16). Mungu anafundisha kwamba kila Mkristo ana angalau kipawa kimoja, lakini kwa sababu vipawa vinavyotoka kwa Mungu ni tofauti, tunatofautiana mmoja na mwingine. Hata Yesu alifundisha akasema, "Mpende jirani yako kama unavyojipenda *mwenyewe*" (Mathayo 19:19).

Lakini sababu kuu inayowafanya watu wahisi kuhukumiwa si kwa sababu wanakosa kuelewa dhambi na makosa; si kwa kwa sababu wanajiona hawana thamani—lakini ni kwa sababu wamekuwa wakitenda dhambi. Wana hatia; wanahisi kuhukumiwa; wanahukumiwa.

Kwa miaka mingi, nilidhani itanibidi nisubiri hadi kifo na hukuma ya mwisho—basi, hapo ndipo nitakapojua kama Mungu alinikubali. Lakini hivyo sivyo Neno linavyofundisha: "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu." Inasema *sasa*—hakuna hukumu ya adhabu sasa hivi. Unaweza *kujua* kwamba huhukumiwi, kwamba dhambi zako zimesamehewa, na kwamba umepatanishwa na Mungu.

Je, unatambua, "wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu?" (Warumi 2:4). "Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo" (5:1). Sasa hatuhukumiwi tena. Uhalisia huu ni kwa kundi moja la watu pekee. Hebu tazama andiko la

leo tena: "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao *walio katika Kristo Yesu*."

Usiku huo, nilizifikiria dhambi zangu tangu nikiwa na umri wa miaka 6, nikamwambia Mungu nilisikitika kwa kutomtii na kumpuuzilia mbali, na kwamba, kwa msaada wake, nilikuwa ninaziacha dhambi zangu. Kisha nikampokea Yesu Kristo na nikampokea moyoni mwangu na maishani mwangu kama Mwokozi na Bwana. Punde si punde, nilihisi msamaha kamili kutoka kwa Mungu—sikuhisi hukumu tena. Hakuna hukumu ya adhabu kwa mtu yeyote anayefika hapa—wapo "ndani ya Kristo Yesu."

**JANUARI 8** **8**

# Yeye Ashindaye

*Yeye ashindaye, nitamridhia kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.*
*Ufunuo 3:21*

Washindi wanasifiwa katika kitabu cha Ufunuo. Lakini ukiwasikia Wakristo wakiongea leo, mfumo wa maisha ya Kikristo unaonekana kuwa ule wa walioshindwa.

Tambua jinsi ushindi unavyosisitizwa katika nyaraka za Kristo kwa makanisa saba katika Ufunuo:

- "Yeye ashindaye, nitampa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu" (2:7).
- "Yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili" (v. 11).
- "Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa. Nami nitampa jiwe jeupe, na juu ya jiwe hilo limeandikwa jina jipya asilolijua mtu ila yeye anayelipokea" (kif. 17).
- "Na yeye ashindaye, na kuyatunza matendo yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa" (kif. 26)
- "Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe. Wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake" (3:5).
- "Yeye ashindaye, nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu. Wala hatatoka humo tena kabisa. Nami nitaandika juu yake

jina la Mungu wangu, na jina la mji wa Mungu wangu, huo Yerusalemu mpya, ushukao kutoka mbinguni kwa Mungu wangu, na jina langu mwenyewe, lile jipya" (kif.12).

- "Yeye ashindaye, nitamridhia kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi" (kif. 21)

Kushinda, au "ushindi," hufasiliwa katika Ufunuo 12 kama ushindi dhidi ya "mshitaki wa ndugu zetu" (kif. 10), "ibilisi" (kif. 12): "Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao" (kif.11). Wana ushindi leo, wanashinda dhambi na ibilisi kwa damu na kwa ushuhuda. Kwa mfano, hebu niwasimulie habari za Chuck.

Rafiki yangu alinihimiza nikamtembelee Chuck kwenye gereza la kaunti—alisema Chuck alikuwa amempokea Kristo hivi karibuni. Basi Chuck alipotambua kwamba mimi ni mchungaji, alinisalimia kwa uchangamfu na akanisimulia kisa chake: Alikuwa amejihusisha na dawa za kulevya, alifanya ujambazi ili aweze kununua dawa za kulevya, na akampokea Kristo kama Mwokozi na Bwana kwa njia ya ajabu. Papo hapo, alikombolewa kutokana na hamu yake ya dawa za kulevya. Alikwenda polisi, na kusema uhalifu wake, na sasa alikuwa jela. Imani yake ilikuwa inang'aa. Alianza mafunzo ya *Basic Bible Studies for New and Growing Christians*, na tukakubaliana kuwa na mkutano wa uanafunzi kila wiki ili kupitia mafunzo yake.

Katika mkutano wetu wa tatu, Chuck alikuwa anasumbuka. Aliniambia hamu yake ya zamani ya dawa za kulevya ilikuwa inarudi tena. Nilimkumbusha 1 Wakorintho 10:13, kifungu ambacho awali alikariri: "Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu. Ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita muwezavyo. Lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili muweze kustahimili."

Nikamwambia, "Chuck, Mungu hataruhusu ujaribiwe zaidi ya uwezo wako. Anajua kwamba kwa msaada wake, unaweza kulishinda. Nilikuwa na dhambi maishani mwangu, na zilinidhibiti; sikuzidhibiti. Lakini Kristo alipoingia maishani mwangu, alinipa nguvu ambazo sikuwa nazo awali. Sijarudia hizo dhambi zangu hata mara moja. Anaweza kufanya hivyo kwako!"

"Ndiyo!" Chuck akasema. "Ninaweza kufaulu!" Na Chuch aliendelea kutoka hapo katika ushindi. Alikamilisha vizuri mafundisho ya Biblia ya kila wiki. Aliwaleta wafungwa wengine kadhaa kwa Kristo. Alijawa na furaha na hali ya kujitoa. Hakurudia matumizi ya dawa za kulevya kamwe.

Hatimaye, Chuck alitolewa gerezani. Jaji alimtaka aishi katika nyumba ya mchungaji wa familia yao na awe chini ya ushawishi wake. Mara ya mwisho nilipoongea naye kwenye simu, nilimuuliza hivi, "Chuck, unaendeleaje?"

Akajibu, “Ninaendelea vizuri. Ninapanga kwenda kusoma chuo cha Biblia. Nafikiri Mungu ameniitia katika huduma.”[3]

“Ndiyo! Ninaweza!” Ni mshindi!

JANUARI 9 **9**

# Sithubutu Kukabiliana na Watu au Matatizo

*Lakini ninalilia msaada, Bwana; asubuhi maombi yangu yanakuja mbele zako.*
*Zaburi 88:13*

Je, huwa unakabiliana na mambo gani katika saa tatu za kwanza za siku yako? Je, huwa unafanya nini kujitayarisha kwa saa hizo?

Siku chache zilizopita, nilikuwa namsikiliza mtu niliyekuwa nimewekeza sana kwake maana alikuwa anafundisha darasa moja kanisani. Alisema, “Kama Mchungaji Shaver alivyosisitiza sana kwamba, “sithubutu kukabiliana na watu au matatizo hadi pale nitakapokabiliana na Bwana.” Alikuwa amejumuisha mazoea haya katika maisha yake mwenyewe. Maneno yake yalinikumbusha jinsi suala hili lilivyokuwa muhimu sana na bado ni muhimu kwangu.

Nilimpokea Kristo mwaka wangu wa kwanza katika chuo kisichokuwa cha Kikristo. Nilihisi nitakuwa ninaishi katika mazingira ya kiroho yasiyokuwa rafiki. Kati ya wanafunzi elfu tatu, takriban wanafunzi thelathini walikuja katika ibada ya kanisha la chuoni, na sita hadi wanane walikusanyika kwa ajili ya maombi. Ilikuwa muhimu kwangu kuamka asubuhi na kutumia muda kusoma Biblia na kuomba kabla ya kukabiliana na watu au matatizo. Niliuchukulia huo kuwa wakati wangu wa “Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani” (Waefeso 6:11).

Bila shaka, kama unafanya kazi ya usiku, basi siku yako huanza wakati wa alasiri. Ikiwa huwezi kumpa Mungu mwanzo wa siku yako, mpe wakati ule ambapo akili yako huwa makini. Mpe sehemu bora zaidi ya siku yako; usimpe masalio.

3. Imeripotiwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Septemba 2012).

Sasa, miaka sitini na tano baada ya kuokoka, bado ninafuata utaratibu huu: "Sithubutu kukabiliana na watu au matatizo hadi pale nitakapokabiliana na Bwana." Matunda ya utaratibu huu yamekuwa mengi sana.

Ungana nami katika utaratibu huu. Biblia inasema hivi juu ya Yesu, "Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko" (Marko 1:35). Utakuwa katika hali nzuri.

**JANUARI 10** **10**

# Toba ni Kitu Kizuri Sana

*Petro akawaambia, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu. Nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie".*
*Matendo 2:38-39*

Ikiwa Mungu ni mtakatifu—na kweli ni mtakatifu—basi ni jambo lenye mantiki kukubali kwamba watu wakizishikilia dhambi zao hawataweza kuishi naye katika maisha ya milele. Hili lipo wazi sana kiasi kwamba Petro anamnukuu Bwana: "Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu" (1 Petro 1:16).

Kwa hiyo, tutafanya nini juu ya dhambi tulizotenda? Petro anasema, "tubuni." Toba maana yake ni kusikitikia dhambi zako na kumwomba Mungu akusamehe na uziache dhambi katika siku zijazo. Pia ni muhimu kwamba wakati huo umgeukie Yesu Kristo. Kwa kumwendea Kristo, sasa unawezeshwa kuishi maisha mapya—ya utakatifu. Warumi 3:22 inasema, "ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio." Waraka wa pili kwa Wakorintho 5:17 inasema, "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya." Kristo hukufanya kuwa mpya; sasa unaweza kuishi maisha tofauti na ya utakatifu.

Mungu anakupenda sana kiasi kwamba alimtuma Kristo akusamehe maisha yako ya zamani na akamtuma Roho Mtakatifu akuwezeshe kwa siku zijazo. Brennan Manning anasema, "Je, Mungu anakupenda kwa kiasi gani? Anakupenda sana hivi kwamba afadhali afe kuliko kuishi bila wewe—kwa

hiyo alifanya hivyo."[4]

Hivi ndivyo Michael Henderson anavyofasili Mkriso: "Mkristo ni mtu ambaye kwa sasa anamfuata Yesu na anatenda yale aliyosema atende."[5] E. Stanley Jones anasema kwamba kumtii Mungu kwa sababu huenda atatuumiza ni sifa ya Mkristo asiyekomaa; kumtii Mungu kwa sababu huenda tutamuumiza ni sifa ya Mkristo aliyekomaa.[6]

Mtoto wangu, Paul, alipatwa na melanoma kwenye bega lake, na ikawa anahitajika kufanyiwa upasuaji. Mpasuaji aliingia ndani na kukata sehemu kubwa ya bega lake. Je, mnadhani nilimkasikiria yule daktari? Je, nilifoka na kusema, "Una haki gani ya kuuvamia mwili wa mwanangu na kukata sehemu kubwa ya bega lake?" Hapana—nilifurahi kwamba daktari aliingia ndani, na kuipata ile saratani, na kuyarefusha maisha ya Paul. Nilifurahi.

Toba ndivyo ilivyo—Mungu anaingia ndani zaidi kukabiliana na dhambi zako. Na hebu fikiria, dhambi zako zote zinaweza kusamehewa, na unaweza kuwa mtu mpya. Ndiposa Warumi 2:4 inasema, "Au waudharau wingi wa wema wake na ustahimili wake na uvumilivu wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu?" Toba ni kitu kizuri sana.

**JANUARI 11** **11**

## Je, Unawezaje Kumtambua Nabii wa Kweli?

*Mungu wa milele ndiye makazi yako, Na mikono ya milele i chini yako.*
*Kumbukumbu La Torati 33:27*

Mtoto wetu alipoitwa kutuambia kwamba atafanyiwa upasuaji wa kuondoa saratani shingoni mwake, upasuaji ambao yamkini ungeondoa koromeo lake, mama yake alijibu. Haya ndiyo yale maneno aliyoandika:

> *Nilikuwa nimesimama jikoni niliposikia kwa mara ya kwanza Paul akituambia juu ya saratani yake ya kooni, na nilianguka chini kwa ghafla na nikakaa hapo. "Bwana, unawezaje kuruhsu hili litokee? Tafadhali, Bwana, huyu ndiye mwana wetu wa kiume wa pekee!" na akasema, "Ndiyo, Nancy, ninataka kumtumia." Kwa hiyo, nikasalimu amri papo hapo, na*

4. Quotation from sermon notes. Original source unknown.

5. D. Michael Henderson, *Making Disciples—One Conversation at a Time* (Kansas City, MO: Beacon Hill Press of Kansas City, 2006), 28.

6. Nukuu kutokana na kumbukumbu za mahubiri. Chanzo asili hakijulikani.

*baada ya muda mfupi, akanimiminia amani moyoni mwangu. Amani hiyo ilikaa nami muda huo wote wa upasuaji uliochukua saa kumi na tatu; na ulipomalizika, waliitoa ile saratani, wakafanya trakeotomi, na kujenga upya umio lake. Siku ya pili yake alikuwa anaweza kusimama na kutembea, na mnajua hayo mengine yaliyofuata. Unaweza kumwamini Mungu wakati wote. Ninajua hili kwa sababu Mungu aliniinua na kunishikilikia mikononi mwake siku hiyo, na alinipenda na kunitunza na kunijaza kwa nguvu za kukabiliana na siku zijazo na mambo yatakayotokea kwa sababu anajua jina la Paul na lako na langu. Unaweza kuamini hili kabisa pasipo kuwa na wasiwasi wowote. Anatufanya tuwe na nguvu zaidi na hodari kwa sababu hakuna woga katika upendo.*[7]

Maisha ya ushindi ya Paul baada ya kuondolewa koromeo yamesimuliwa katika makanisa ishirini na nane, na Paul alitoa ushuhuda wake kwa watu 2,200 huko Kanisa la Kibaptisti la South Carolina.

Na kwa Nancy, "chini kuna mikono ya milele."

**JANUARI 12** **12**

# Mwanasayansi na Mungu

*Inueni macho yenu juu.*
*Isaya 40:26*

Kwa wengine, sayansi na imani ni maadui. Ilihali, kwa wengine, sayansi na imani ni vitu vinavyokumbatiana.

Mtazamo wa kulipinga kanisa ulikuwa umejengeka ndani ya Joe—yale mabaya aliyopitia baba yake kanisani yalichangia hali hii. Lakini, Joe alipokutana na Doris wakati wakiwa chuoni, mtazamo wake ulianza kubadilika. Doris alilelewa katika familia ya Kikristo, akampa Mungu maisha yake wakati alipokuwa na umri wa miaka 14 wakati wa ibada ya uvuvio, na alifurahia kuishi katika uhusiano na Kristo. Doris alipomfafanulia Joe habari za Kristo na kanisa, akili yake ilifunguka, na akampokea Kristo moyoni na kanisa moyoni mwake.

Walioana muda mfupi kabla hawajamaliza chuo. Joe alijua kwamba kwa sababu ya vita nchini Korea, angejumuishwa katika huduma ya kijeshi.

---

7. Barua ya Krismasi kutoka kwa Shaver, 2015.

Katika wakati wake wa kuwa jeshini, alimaliza mafunzo yake ya msingi kama kamanda wa gari lenye silaha, aliendelea mbele na kuwa afisa wa mafunzo, na hatimaye akatumwa kufanya kazi katika maabara ya kemikali ya jeshi.

Baada ya kuruhusiwa kuondoka jeshini, Joe alifanyia kazi kampuni ya Standard Oil iliyoko California kwa muda wa miaka tisa. Kisha alipata kazi katika maabara ya Bayer huko Kansas City, ambapo alifanya kazi kama mwanakemia mkuu kwa miaka ishirini na tano. Kwa Joe na wale wanakemia wengine kumi na wanne waliofanya kazi chini yake, lengo lilikuwa kuendeleza, kuendeleza tena, na kuboresha viungo mbali mbali vya dawa ya kuua wadudu iliyokuwa ikiuzwa na Bayer.

Baada ya kustaafu, Joe alianzisha maabara yake mwenyewe. Mmoja wa wateja wake alipiga simu kutoka Ulaya, akieleza kwamba wanakemia wao walikuwa wametengeneza viungo maalum kwa muda wa miaka mitatu, lakini walikuwa na tatizo: kontena zao ziliendelea kulipuka. Joe alichukua wajibu wa kulitatua tatizo lao. Jioni hiyo, alimwendea Mungu na kumwomba amsaidie. Mungu alimwambia alijua jibu tayari, na atumie maarifa yake ya kemia kwenye tatizo hilo. Ndani ya siku tatu, Joe alipata jibu kutokana na mafunzo ya kimatibabu ya awali.

Pasipo kuamini, rais wa kampuni ya mteja na mfanyakazi walifika kwenye maabara ya Joe kujionea wenyewe. Hawakuamini kwamba hakuna hata chupa moja iliyokuwa inalipuka, mbali na kiwango cha joto zilimokuwa zimehifadhiwa au kwa muda gani zimehifadhiwa.

Joe sasa hivi anamiliki hataza kumi na tano za msingi na jumla ya hataza 253, ikiwa ni pamoja na zile zinazohusiana na kampuni mbalimbali duniani kote.

Mseto mzuri ulioje—mwanasayansi wa kemia na imani katika Mungu anayejibu maombi. Ndiyo maana Isaya alisema, "Inueni macho yenu juu: Ni nani aliyeziumba hizi? Aletaye nje jeshi lao kwa hesabu; aziita zote kwa majina" (Isaya 40:26).

**JANUARI 13** **13**

# Je, Nini Maana ya "Kuamini"?

*Abramu alimwamni BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki.*
*Mwanzo 15:6*

"Mwamini Yesu pekee na utaokolewa" ni wazo linalorudiwa sawa katika sehemu kubwa ya Ukristo. Na bado kuna tundu, kuna kitu fulani kinakosekana katika kauli hiyo. Jibu liko katika uelewa mzuri wa neno "kuamini."

"Kuamini" ni zaidi ya kukubali kiakili kwamba Yesu yupo. Hata Yakobo anasema hiyo haitoshi anapoandika na kusema, "Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja. Watenda vema! Mashetani nao waamini na kutetemeka" (Yakobo 2:19). Bila shaka, mashetani "wanaamini" kuna Mungu, lakini ni dhahiri hawajaokolewa. Victor Hamilton anasema, "Kumwamini Bwana ni kumtumaini Bwana. Kuelewa imani kama kutumaini husongeza kule kuamini kutokana na kitu tunachokikubali akilini mwetu hadi kitu ulicho tayari kukifanya kwa maisha yako."[8]

Biblia inarudiarudia kuunganisha pamoja wazo la kuamini au kumtumaini Bwana na maisha ya huduma, kujitoa, kujituma, na maisha ya kishujaa. Yakobo 2:22–24 anafafanua hivi: "Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale. Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, Abrahamu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu. Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake."

Nina njia rahisi ya kuelewa dhana ya kuamini au imani. Nikikwambia, "Nina imani na mke wangu, Nancy," je, ninamaanisha tu kwamba yuko? Au imani yangu inamaanisha ninamwamini, ninamtegemea, natafuta kumpendeza, kumhusisha katika maamuzi yangu, kumtunza, na kujitoa kwake?

Je, wewe unaamini imani gani?

**JANUARI 14** **14**

# Jambo la Ajabu, Jambo Zuri Sana

*"Kwa maana rahisi ni lipi, ni kusema, Umesamehewa dhambi zako, au ni kusema, Ondoka, uende? Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi." Amwambia yule mwenye kupooza, "Inuka, ujitwike kitanda chako, uende nyumbani*

8. Victor Hamilton, "Commentary Genesis 14:17–15:6," *Illustrated Bible Life*, Septemba–Novemba 2015 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 7.

*kwako." Akaondoka, akaenda zake nyumbani kwake. Makutano walipomwona, walishikwa na hofu, wakamtukuza Mungu, aliyewapa watu amri ya namna hii.*
*Mathayo 9:5–8*

Binti yangu mwenyewe alinipa changamoto na kusema, "Baba, angalau mara moja kwa wiki, andika angalau kitu kimoja cha ajabu, kitu kimoja kizuri sana, kilichotokea wiki hiyo." Basi nikaamua kuikubali changamoto hiyo. Watu wa wakati wa Yesu walipoona kwamba Kristo anaweza kusamehe dhambi na kuponya waliopooza, walijawa na hofu na *wakamtukuza Mungu*. Nilihisi zoezi hili lingenifanya niwe makini zaidi kwa kazi ya Mungu maishani mwangu, niwe na shukrani zaidi, na kumpa Mungu sifa. Lingenizuia kuangazia yale mabaya na kuyakumbuka yale mazuri. Kwa hiyo nilianza kuorodhosha yale mambo mazuri sana. Hapa ni baadhi ya mambo hayo:

- Nilishiriki moyo wa furaha wa Siku ya Krismasi na familia yangu.
- Baada ya kumwomba Bwana atume hela kwa ajili ya mahitaji ya mwisho wa mwaka ya Kituo cha Uinjilisti, tulipokea zawadi za kifedha za jumla ya dola elfu sita.
- Watu mia moja walikuja kusherehekea kustaafu miaka arobaini ya kufundisha darasa la uanafunzi na kumbukumbu yangu ya siku ya kuzaliwa ya miaka themanini na tano. Mimi na familia yangu tumehisi kupendwa, kusaidiwa, kushukuriwa, na kutiwa moyo.
- Nimeandika makala ya maombi ya kibinafsi na kutafakari ndani ya siku saba.
- Nimeona *Charlie and the Chocolate Factory* huko Kauffman Center. (Kwa miaka mingi, nilitaka kwenda Kauffman angalau mara moja.)
- Nimepokea ujumbe wa maandishi wa kimapenzi kutoka kwa Nancy ambao ningeuomba.
- Jumamosi moja, nilikutana na Wakristo wenzangu wengine, mmoja wa Wakristo hao alithibitisha imani yake katika Kristo na akakubali kufanya *Basic Bible Study*, na wengine walikubali kuwa wabia wa kufanya ufuatiliaji.
- Jumapili, nilihubiri ujumbe wenye kichwa cha "Moyo wangu—ni nyumbani kwa Kristo" kwa kundi la watu wapatao 186. Baadaye, watu 33 walimtafuta Kristo.
- Nimepata fursa ya kushuhudia uzuri wa Naples Botanical Gardens.
- GPS imeharibika, lakini Rachel alikuwa amenifundisha kutumia Siri kwenye simu janja. Programu tumizi iliweza kunionesha njia.

Baadhi ya mambo haya yalikuwa majibu mazuri sana ya maombi; mengine yalikuwa ni kufurahishwa kwangu na uzuri wa asilia; mengine yalikuwa ya kuitendaji, kama vile Siri kunionesha njia vizuri kwenda nyumbani. Na moyo wangu uliinuliwa nilipopita—ni ajabu, mazuri sana. Kwa hiyo najiunga na uzao wa Yakobo: "Bali atakapowaona watoto wake, walio kazi ya mikono yangu, katikati yake, wao watalitakasa jina langu; naam, watamtakasa Mtakatifu wa Yakobo, nao watamcha Mungu wa Israeli" (Isaya 29:23).

Je, mngependa kujaribu kufanya hivyo—kitu kimoja kizuri sana kila wiki?

**JANUARI 15** **15**

# Ahadi za Mungu Kwa Ajili Yako

*Naam, nijapopita kati ya bonde la kivuli cha mauti,*
*Sitaogopa mabaya; Kwa maana Wewe upo pamoja nami.*
*Zaburi 23:4*

Ni barua ya mapenzi kutoka kwa Mungu kwa ajili yako. Hiyo ni njia moja ya kuilezea Biblia.

Njia moja nzuri ya kusoma Biblia ni kuanza kwa kitabu kimoja maalum, kama vile Injili ya Yohana. Njia moja ya kusoma Biblia kwa mwaka ni kununua na kusoma kitabu cha *One Year Bible*, kinachokupa somo la kila siku ya mwaka. Masomo haya yana takriban sura mbili za Agano la Kale, na sura moja ya Agano Jipya, nusu Zaburi, na vifungu vitatu kutoka Mithali. Kwa kuifuata kalenda yako, utamaliza kusoma Biblia kwa mwaka mmoja.

Ili uweze kusoma na kuelewa vizuri, fuata ushauri wa Earl Lee, aliyefundisha "SMU." Hizi herufi hazisimamii Southern Methodist University, lakini "Inasema *nini*? Inamaanisha *nini*? Ninaweza *kuitumiaje*?" Kwa kupata matumizi mahususi ya Biblia, utashuhudia ukuaji mkubwa sana.

Biblia inatoa maagizo, ushauri, na ahadi. Ahadi zinatupatia msaada mkubwa wakati tunapokumbana na changamoto. Bila shaka, ahadi maalum ziliwekwa katika nyakati maalum zilizopita kwa mtu maalum au kundi maalum—lakini mara nyingi ahadi hizi pia ni kanuni zinazodumu zinazoendelea kutumika kwa watu leo.

Dorothy Hamilton ana orodha ya ahadi ambazo hasa zinaweza kutusaidia. Hizi hapa ni baadhi ya ahadi hizo—zitumie kwa ajili yako:

- “Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako. Nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kulia wa haki yangu” (Isaya 41:10).
- “Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake” (Warumi 8:28).
- “Maana sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso. Sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana” (1 Wakorintho 13:12).
- “Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima . . . , ili maombi yenu yasizuiliwe na chochote” (1 Petro 3:7).
- “Huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu” (1 Petro 5:7).
- “Neema yangu yakutosha; maana uwezo wangu hutimilika katika udhaifu” (2 Wakorintho 12:9).

Shinikizo la makataa lilikuwa juu yangu. Ulikuwa mradi wangu wa mwisho kwa ajili ya shahada yangu ya uzamivu katika huduma huko Fuller Seminary. Ninaandika mafundisho ya uanafunzi yenye masomo kumi na mawili, na ilikuwa lazima nimalize kufikia mwisho wa Disemba.

Shinikizo halikutokana na mradi huu pekee. Nilikuwa nahudumu kama profesa wa uinjilisti na kama mchungaji wa uinjilisti, pamoja na kuhusika katika majukumu mengi ya kwenda kuhubiri. Nilihisi kuwa na msongo sana. Niliweka kichwa changu juu ya meza yangu na nikahisi kana kwamba nilikuwa narukwa na akili. Nilikuwa nimeandika swali la mafundisho ya uanafunzi muda mchache uliopita: “Je, matarajio ya kibiblia ya nguvu za kushinda magumu kwa ajili ya Kristo ni nini?” Pamoja na swali hilo nilijumuisha rejeleo la Wafilipi 4:13: “Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.” Nafikiri kichwa changu kilikuwa bado kimeegemea mezani nilipomsikia Roho Mtakatifu, “Kwa nini usiuweke mradi wako wa chuoni hapo?”

Nilisoma kifungu hicho tena na nikaongeza neno “mradi”: “Ninaweze kufanya mradi huu katika yeye [Kristo] anitiaye nguvu.” Nilipofanya hivyo, nguvu zilitiririka ndani yangu—nilijua ninaweza kuufanya. Roho alinena tena, akasema, “Utakamilika kwa wakati, na utachapishwa.” Mradi ulifika Fuller mapema, na ulichapishwa kwa kichwa *Living in the Power of the Spirit*. Nilijua ahadi ya Mungu ilikuwa imefanya kazi maishani mwangu—ninatarajia iwe vivyo hivyo kwako.

# Wakati Hatuelewi

*Akawaambia, "Kwa nini mnitafute? Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?" Nao hawakuelewa neno hilo alilowaambia. Akashuka pamoja nao mpaka Nazareti, naye alikuwa akiwatii; na mamaye aliyaweka hayo yote moyoni mwake. Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu.*
*Luka 2:49–52*

Mmoja wa wanawake wacha Mungu zaidi katika historia ya ulimwengu alikuwa Mariamu, mama yake Yesu. Kama Luka 1:28 asemavyo, "[Malaika] Akaingia nyumbani kwake akasema, Salamu, uliyepewa neema. Bwana yu pamoja nawe."

Naye akafadhaika sana kwa ajili ya maneno yake, akawaza moyoni, Salamu hii ni ya namna gani? Malaika akamwambia, "Usiogope, Mariamu. kwa maana umepata neema kwa Mungu. Tazama, utachukua mimba na kuzaa mtoto wa kiume; na jina lake utamwita Yesu. Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye Juu. Na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake, ...na ufalme wake utakuwa hauna mwisho" (kifungu cha 30–33). Malaika akajibu akamwambia, "Roho Mtakatifu atakujia juu yako, na nguvu zake Aliye Juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu" (kif.35).

Baadaye, Yesu alipofikisha umri wa miaka kumi na miwili, yeye, Mariamu, na Yusufu walikwenda Yerusalemu kwa ajili ya sherehe ya Pasaka. Basi jamaa zao waliposhika njia kwenda nyumbani, wazazi wa Yesu waligundua kwamba Yesu hakuwa pamoja nao. Basi walirudi Yerusalemu, na kumpata Yesu, na wakamhoji wakitaka kujua kwa nini amefanya hivyo. Aliwajibu kwamba ilimbidi kuwa nyumbani mwa Baba yake, lakini *hawakuelewa*.

Inapokuwa Malaika wa Mungu alikuwa ameongea na Mariamu waziwazi kabisa, kufikia wakati huu wa ukuaji wa Yesu, bado hawakuelewa. Ndiyo, inawezekana kwamba kuna masuala ambayo wacha Mungu hawayaelewi.

Kwa mfano, mwaka 2020 nilikuwa nikijiuliza, "Kwa nini kuna COVID-19?" Je, ni kwa sababu katika historia yote ya ulimwengu, tunakumbwa na magonjwa makubwa kila baada ya mufa fulani? Je,

ni hukumu kutoka kwa Mungu kwa wale wasiotii? Wale Waisraeli waliolalamika na kunung'unika jangwani walimchukiza Bwana, "kawapiga watu kwa pigo kuu mno" (Hesabu 11:33). Je, ni kwa sababu tunaishi katika ulimwengu ulioharibika, ulimwengu usiokuwa na uadilifu tangu dhambi iwaingie wanadamu? Hata hivyo, tunaishi katika tumaini, "kuwa viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu." Zaidi ya hayo, "Tukikutazamia kufanywa wana, yaani, ukombozi wa mwili wetu" (Warumi 8:21 na 23). Sijui, sielewi, lakini nimekuwa nikiomba kwamba Mungu atatumia mfufulilzo huu wa matukio ya majanga kuwavuta watu kwake—Mwokozi, asameheaye, mponyaji, Bwana.

Mamilioni ya watu walijitenga na wengine kwa kuamua kujitenga wenyewe ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa miongoni mwa wanadamu. Je, wale watu ambao kwa kawaida huzongwa na shughuli za kazi, shule, michezo, burudani, na manunuzi watafanya nini wakati kila kitu kimesimama? Wanapokaa nyumbani siku hadi siku, nini kinaendelea akilini mwao? Je, wanawaza nini? Je, inawezekana kwamba Mungu anapata usikivu wao?

 17

# Kuishi kwa ajili ya Malimwengu Mawili

*Lakini tuna moyo mkuu; nasi tunaona ni afadhali kutokuwemo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana. Kwa hiyo, tena, ikiwa tupo hapa, au ikiwa hatupo hapa, twajitahidi kumpendeza yeye. Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee malipo ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, yawe ni mema au mabaya.*
*2 Wakorintho 5:8-10*

Mnamo tarehe 1 Aprili, 2020, Dr. Anthony Fauci alitabiri kwamba mamia na maelfu ya Wamarekani wangekufa kutokana na janga la virusi vya korona. Kwa kuzingatia hayo, je, si lingekuwa jambo la busara kama kila mtu angekuwa na hakika kwamba wanaishi kwa ajili ya malimwengu mawili—huu wa sasa na ule ujao? Mtume Paulo alizungumzia juu ya, "kutokuwemo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana." Matokeo yake, ni kwamba "twajitahidi kumpendeza

yeye." Suala hili ni kubwa sana kiasi kwamba lazima sote tusimame mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.

Yesu alifasili uzima wa milele katika Yohana 17:3: "Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma." Ni uhusiano wa sasa, na wa muhimu na Mungu wa kweli na Yesu Kristo. Lakini matokeo yake ya mwisho hutupeleka kwenye uzima baada ya kifo. Yesu anafafanua zaidi hili zaidi katika Yohana 10:27: "Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata." Hapa, njeo ya kitenzi hiki "kufuata" inamaanisha "sasa wananifuata." Yesu anasema, "Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu" (kifungu cha 28).

Maisha ya sasa yanapaswa kuwa ya uaminifu na ya huduma. Matthew 25:34–36 inasema, "Kisha Mfalme atawaambia wale walioko katika mkono wake wa kulia, 'Njooni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu. Kwa maana nilikuwa na njaa, mkanipa chakula; nilikuwa na kiu, mkaninywesha; nilikuwa mgeni, mkanikaribisha; 36 nilikuwa uchi, mkanivika nilikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nilikuwa kifungoni, mkanijia.'"

Zaidi ya hayo, maisha haya ya kuwa pamoja na Kristo yamejaa hali ya kutosheka sana. Katika Yohana 10:10, Yesu anasema, "Mimi nilikuja ili wawe na uzima, tena wawe nao tele." Paulo anasema katika Warumi 14:17 inasema ufalme wa Mungu unahusu "haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu."

Lakini pia kuna maisha yanayofuata. Kristo anasimulia kisa cha tajiri mmoja ambaye alipanda na kuvuna mavuno mengi. Alisema hivi, "Akasema, Nitafanya hivi; nitazivunja ghala zangu, nijenge nyingine kubwa zaidi, na humo nitaweka nafaka yangu yote na vitu vyangu. Kisha, nitajiambia, Ee nafsi yangu, una vitu vyema vingi ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi" (Luka 12:18-19). Lakini dosari ya falsafa yake ilikuwa kwamba aliishi kwa ajili ulimwengu huu. "Lakini Mungu akamwambia, Mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka roho yako! Na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nani?" (kif.20).

Kuna maisha yanayofuata. Mtume Paulo aliandika hivi kutoka gerezani, "Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida. Ila ikiwa kuishi katika mwili, kwangu mimi ni matunda ya kazi. Basi nitakalolichagua silitambui. Ninasongwa katikati ya mambo mawili: Ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo maana ni vizuri zaidi sana" (Wafilipi 1:21–23). Paulo anaridhika na maisha yake ya duniani hivi kwamba anasema, "Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda. Baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa

siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake" (2 Timothy 4:7–8).

Na tunaweza kuyaona vizuri maisha yajayo—sauti kubwa inanena, "Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao. Nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao. Wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita" (Ufunuo 21:3-4).

Sasa, natuwe na busara. Jiandae kuishi kwa aina hizo mbili za ulimwengu.

**JANUARI 18** **18**

# Kama Ayala Aioneavyo Shauku Mito ya Maji

*Vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu.*
*Zaburi 42:1*

Dalili ya kwanza ni sauti miti inavyovunjwa kichakani. Na kisha unamwona ayala akijitokeza—kiumbe mzuri kando ya kijito cha maji. Ayala amelowana jasho, lakini koo lake linatamani maji. Kile kijito kinakata kiu yake; anaburudishwa kwa maisha mapya. Lakini kwa mbali anaona kundi la mbwa na linamfanya misuli yake ijikaze tena, na ghafla anajitosa ndani ya kijito. Kile kijito ndicho usalama wake—wale mbwa hawawezi kuipata harufu yake ndani ya maji.

Tunahitaji kuburudishwa, tunahitaji uzima, na usalama. Mbwa wawindaji wametukimbiza kwa muda mrefu sana. Tunaona kiu! Ah, lakini Mungu yuko hapa—anaikata kiu yetu, anatupa maisha mapya, na katika usalama wa uwepo wake, wale mbwa wanapotea njia. Kaka yangu, dada yangu, naomba unywe kutoka kwenye kijito cha Mungu. Vyanzo vingine vyote vya maji vinaweza kuwa vimechafuliwa au havitoshi, lakini Yesu alisema, "Lakini yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele" (Yohana 4:14).[9]

9. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Januari–Februari–Machi 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 39. Imetumika kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

# Linatokea

*Lakini ilipokuwa karibu usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza. Ghafla pakawa tetemeko kuu la nchi, hata misingi ya gereza ikatikisika. Akataka taa ziletwe, akarukia ndani, akitetemeka kwa hofu, akawaangukia Paulo na Sila; kisha akawaleta nje akasema, "Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?"*
*Matendo 16:25–26a, 29–30*

Kuomba na kuimba nyimbo za kumsifu—hivyo ndivyo walivyokuwa wanafanya walipoketi gerezani kwa kuhubiri habari za Yesu katika mji wa Filipi. Walikuwa wamepigwa sana na miguu yao ilikuwa imefungwa kwa mikatale—bado, waliimba na kuomba. Kisha, tetemeko la ardhi likalitikisa lile gereza.

Ule mtazamo wa wafungwa, kuomba na kuimba kwao, na tetemeko la ardhi yote yalivuta usikivu wa yule mlinzi. Mungu aliweza kusikilizwa kama alivyotaka. Kabla macheo, yule mlinzi wa gereza na familia yake yote walimpokea Bwana. Baada ya mlinzi wa gereza kuyasafisha yale majeraha ya wafungwa, yeye pamoja na familia yake walibatizwa. Kisha ile familia ilimwandalia Paulo na Sila chakula cha jioni.

Wiki mbili kabla niliandika kurasa hizi, niliandika masombo ya kuomba na kutafakari #16 kwa Januari 16, "Tunapokosa Kuelewa." Katika somo hilo niliandika, "Kwa nini kuna COVID-19?" Aya ya mwisho ya somo hilo ilisema hivi: *Mamilioni ya watu walijitenga na wengine kwa kuamua kujitenga wenyewe ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa miongoni mwa wanadamu. Je, wale watu ambao kwa kawaida huzongwa na shughuli za kazi, shule, michezo, burudani, na manunuzi watafanya nini wakati kila kitu kimesimama? Wanapokaa nyumbani siku hadi siku, nini kinaendelea akilini mwao? Je, wanawaza nini? Je, inawezekana kwamba Mungu anapata usikivu wao?*

Katika sehemu ya michezo ya gazeti la *The Kansas City Star* Aprili 2020, Nilisoma hadithi juu ya Rex Hudler, anayetangazia Kansas City Royals. Mnamo 1978, Hudler alisaini kandarasi na Yankees mara tu baada ya kumaliza shule ya sekondari. Alianza kucheza katika mechi kubwa mwaka 1984, na akastaafu mwaka 1998. Muda mfupi baadaye, alianza kutangazia Los Angeles

Angels, na mnamo 2009 alijiunga na timu ya matangazo ya Royals. Janga la virusi vya korona lilimfanya Hudler kuwa na kipindi kigumu, COVID-19 ilifunga mchezo wa besiboli, na kama wengi wetu, Hudler alisalia nyumbani kwa saa nyingi na kupokea msururu wa habari mbaya zisizokoma. Wakati wa "kuzuiwa kutoka nje", Hudler alisema alijitahidi awezavyo kutoangalia habari za asubuhi kwenye TV, akaelezea jinsi ratiba yake ilivyobadilika:

> Nimeweza kuwa karibu na Mungu wakati huu na, unajua, mimi si mtu wa dini sana, ni mtu wa kiroho. Na kwa hiyo ninapoamka asubuhi, ninafungua macho yangu na kumshukuru Mungu kwa uzima . . . Unajua jinsi tunavyokumbushwa mambo kupitia ujumbe kwenye simu? Fox, CNN, vyombo hivi vyote viko kwenye simu yako, vikisubiri uanze siku yako hapa. Uh-uh. Ninaanza na Mungu. Nitatafuta Andiko na nisome Andiko na nianze siku yangu pamoja naye, si pamoja na ulimwengu.[10]

Je, inawezekana kwamba Mungu anapata usikivu wa watu? Linatokea!

JANUARI 20 **20**

## Paul Shaver—Kabla na Baada ya Saratani, Sehemu ya 1

*Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.*
*Wafilipi 4:6–7*

Niruhusu nikusimulie hadithi ya kile kilichotokea kwa familia yangu mwaka 2014.

Mtoto wetu wa kiume, Paul, anaishi Muncie, Indiana, pamoja na mkewe, Lori. Ana umri wa miaka hamsini na miwili na anaendesha matrela katika maeneo ya majimbo sita, akipeleka chakula kwenye maduka ya chakula ya Kroger. Paul na Lori wana watoto wawili nyumbani, wasichana wawili

10. Pete Grathoff, "Rex Hudler Is Missing More Than Baseball These Days," *For Pete's Sake* (column), *The Kansas City Star*, April 2, 2020, https://www.kansascity.com/sports/spt-columns-blogs/for-petes-sake/article241714041.html.

walioolewa, na wajukuu watatu wanaoishi karibu nao. Paul na familia yake wanahudumu katika kanisa lao.

Mnamo mwishoni wa Septemba 2014, Paul alinipigia simu na kuniambia alikuwa na shimo shingoni mwake na sauti ilikuwa inakwaruza. Alifikiri asubiri kwa miezi kadhaa ndipo akamwone daktari—bima yake mpya ilikuwa itaanza kufanya kazi Januari. Kwa sababu awali alikuwa amefanyiwa upasuaji wa saratani, nilimwambia lazima akamwone daktari mara moja.

Alipopimwa alionekana kuwa na seli ya saratani shingoni. Basi upasuaji ukawekewa tarehe ya mwisho wa Oktoba. Daktari alitabiri kwamba upasuaji ungechukua saa kumi hadi saa kumi na mbili; na kwamba itawabidi waondoe koromeo la Paul; kwamba Paul angelazwa hospitali kwa siku kumi na mbili hadi kumi na nne.

Niliposikia jinsi hali ya mwanangu ilivyo mbaya, nilianza kuomba kwa njia maalum. Nilikuwa sijaomba hata kwa dakika mbili nilipohisi *amani* ya ajabu, inayofariji ndani yangu—hali ya kuwa mzima. Bwana hakuniambia kwamba Paul angepona, au hata kwamba koromeo lake lingeweza kuponywa. Badala yake alisema hivi: "Nitatembea pamoja nawe katika hii hali yote ngumu." Nilipoomba hivyo katika ibada ya uvuvio katika jimbo lingine, mke wangu, Nancy, aliombea nyumbani, na *amani* ikamshukia na yeye. Amani hii haijatuacha.

Wakati huo, Paul alianza kushuhudia kazi ya Mungu kwa njia ya ajabu. Wakati mmoja, alikutana na mfanya kazi wa ujenzi na akamsalimia, "Unaendeleaje?"

Yule mfanya kazi akajibu, "Safi! Nina Yesu!"

*Ndiyo*, Paul akawaza, *hiyo ndiyo siri*.

Katika moja ya safari zake za kupeleka bidhaa, Paul alipokuwa akimpa stakabadhi mteja, alimwangalia na akamuuliza, "Uko sawa?" Akasema ndiyo lakini ilikuwa wazi kwamba hakuweza kumshawishi kwamba ni mzima kwa sababu alimuuliza swali lile lile mara mbili. Kisha yule mteja akasema, "Ninaweza kukuombea?" na akaomba ombi refu, na lenye ari kwa niaba yake. Paul alishangaa.

Paul alimwomba mchungaji wake amruhusu kuimba na kutoa ushuhuda katika ibada ya Jumapili asubuhi tarehe 19 Oktoba. Aliimba wimbo usemao, "Nothing between My Soul and the Savior," "Learning to Lean," na "Jesus Loves Me." Alitoa ushuhuda mbele ya washirika, na kusema, "Mimi ndiye mtu sahihi kwa changamoto hii; ninaweza kukabiliana nayo vizuri sana; na ninaamini hili litamletea Mungu utukufu."

Paul alilia alipokuwa akitoa ushuhuda, na washirika vilevile walilia. Kisha akapiga magoti madhabahuni na akaomba, "Ikiwa kuna dhambi zozote moyoni

mwangu, nisamehe." Pia aliiombea familia yake. Mchungaji alipomwagia mafuta na kumwombea Paul, takriban washirika wote walimzunguka kumuunga mkono.

Washirika wengine walianza kumwomba mchungaji awapake mafuta na kuwaombea—kama alivyosema mchungaji baadaye, "Mungu alikuwa kila mahali." Mwanamke mmoja aliyekuwa ametoka Wisconsin alisema, "Hili ndilo kanisa zuri zaidi nililowahi kuhudhuria. Ukiniambia kuna kanisa kama hili Wisconsin, nitaenda huko."

Siku chache baadaye, mimi na Nancy tuliendesha gari kwenda Muncie. Usiku huo, tulimnasa Paul kwenye video kwa sababu tulidhani huenda ndiyo mara ya mwisho kusikia sauti yake tena. Lakini Paul alituambia haogopi: Alisema, "Niko tayari." Aliimba na kutoa ushuhuda wake wa jinsi Mungu alivyokuwa karibu naye. Kisha akaimba wimbo wa watu watatu na binti zake. Ilionekana *amani* ya ajabu ilikuwa imesambaa maishani mwa Paul. Alikuwa hodari sana.

Ilipofika saa kumi na moja asubuhi, tulifika Chuo Kikuu cha Indiana huko Indianapolis. Yule daktari wa upasuaji wa saratani na mpasuaji wa kubadili maumbile walielezea kinaganaga kile ambacho wangefanya, na ilipofika kama saa moja na nusu, Paul alipelekwa kwenye chumba cha upasuaji kwa gari la magurudumu. Kila baada ya dakika tisini, muuguzi alikuja kutupa taarifa. Yule mpasuaji wa saratani alikuja kutupa ripoti saa tisa alasiri; na mnamo saa tatu kasoro dakika ishirini, alikuja yule mpasuaji wa maumbile. Kwa jumla, Paul alifanyiwa upasuaji kwa saa kumi na tatu.

Wale wapasuaji waliondoa saratani na nyama kutoka kidevuni mwake hadi sehemu ya chini ya shingo; waliondoa koromeo lake. Walitoa nyama ya kupandikiza kutoka kwenye misuli ya kifuani na minofu. Pia madaktari walituambia, "Tutamsaidia atembee na kumfundisha kupumua, kumeza, kula—na hatimaye, kuongea." Daktari alisema hakuwa amewahi kuona kisa kama cha Paul.

# Paul Shaver—Kabla na Baada ya Saratani, Sehemu ya 2

*Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.*
*Wafilipi 4:6–7*

Siku iliyofuata, tulimtembelea Paul katika chumba cha wagonjwa mahututi. Alikuwa amefunikwa na mipira mingi, na shingo lake lilikuwa limefura. Lakini uso wake ulikuwa unapendeza alipotabasamu. Hakuweza kuongea, lakini alituonesha ishara kwa mikono na akaandika ujumbe kwenye tableti. Muuguzi alituambia kwamba alikuwa akitembea kwa kusaidiwa na amekuwa akiketi kwenye kiti kwa muda wa saa tatu—alikuwa anaendelea vizuri sana. Kufikia wakati tulipoondoka, walikuwa wanampeleka kwenye wadi ya utunzaji endelevu.

Wakati huo huo, Lori alikuwa akiandika taarifa juu ya Paul kwenye Facebook. Karibu katika taarifa zote, aliandikwa kwamba tulitarajia kwamba Mungu angetukuzwa katika tukio hili. Zaidi ya watu mia mbili walitoa maoni, kuanzia watu waliosoma pamoja shule ya upili na chuoni; hadi washirika wa kanisani kwake; hadi marafiki zake wa riadha kutoka enzi yake alipokuwa refa. Karibu wote walisema, "Tunakuombea."

Kadiri nilivyoendelea kuiweka hali ya Paul, mbele za Mungu, nilihisi nasukumwa kumwombea mtu ajitokeze kuongoza juhudi za kuchangisha pesa kwa ajili ya familia na gharama za matibabu wakati Paul hawezi kufanya kazi. Baada ya saa kadhaa, rafiki fulani alinijia na akasema alitaka kuwachangia pesa. Kanisa la Paul lilianzisha mfuko na wakamletea kiti maalum kilichoinama na iPad Mini ili imsaidie kuwasiliana.

Binti yetu Rachel alikuwa kwenye ngazi kazini aliposikia maneno yafuatayo katika roho yake: "Mungu wangu atakutana na mahitaji yako." Dakika kumi baadaye, alipokea simu iliyomwambia juu ya matoleo yasiyotarajiwa, ya ukarimu ya kufadhili kanisa la Paul. Kanisa lilipowapa pesa walizochanga, Paul na Lori walilia machozi.

Paul alirudi nyumbani baada ya kukaa siku nane hospitalini—ambazo ni chache kuliko zile siku kumi na nne alizokadiria daktari. Kufikia wiki ya kwanza ya Disema, alikuwa anaongea kwa sauti yake mpya na nzito, na alikuwa amerudia kufanya kazi yake ya kudumu.

Nashangaa jinsi Mungu atakavyotumia haya yote. Ninakumbuka Joni Eareckson Tada hakuwa maarufu wakati akiwa na afya njema, lakini baada ya kupooza kwake na kutojiweza kwake, alianza huduma ya ulimwengu mzima na kudhihirisha neema ya Mungu inayotosha. Je, inawezekana ndivyo ilivyo kwa Paul? Anaishi karibu na Mungu sana, na kupitia kwa kila kitu, ile *amani* haijaondoka.

**JANUARI 22** **22**

# Mifumo ya Maombi

*Na bado habari zake zilienea hata zaidi, hivi kwamba makundi ya watu walikwenda kumsikiliza na kuponywa magonjwa yao. Lakini Yesu mara kwa mara akijiepua na kwenda mahali pasipokuwa na watu na kuomba.*
*Luka 5:15–16*

Hata ingawa alikuwa Mungu katika mwili, Yesu Kristo bado alihisi ni muhimu sana kuomba kwa Baba wa mbinguni bila kukoma. Unapoendeleza maisha yako ya maombi, tiwa moyo na mfumo wa maombi wa Yesu.

Luka 11:1 inasema, "Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipomaliza, mmoja katika wanafunzi wake alimwambia, Bwana, tufundishe sisi kusali, kama vile Yohana alivyowafundisha wanafunzi wake." Tambua kirai cha "mahali fulani"—hiki kinaweza kumaanisha Yesu alikuwa na mahali maalum alipoenda kuomba. Tunajua alipokuwa Yerusalemu, "Akatoka akaenda mpaka mlima wa Mizeituni kama *ilivyokuwa desturi yake*" (Luka 22:39), na katika kifunga cha 41, he "akapiga magoti akaomba."

Itakuwa vizuri kama utapata mahali maalum pa kuomba. Mimi nina kiti ninachokipenda ambapo hukaa na kikombe cha kahawa, na kusoma Biblia, kisha kuandika mawazo makuu kwenye daftari, ikiwa ni pamoja na kifungu kikuu nilichosoma, mambo ya kushukuru, na maombi. Kisha, huwa ninakwenda kwenye afisi chini ya nyumba yangu na kuomba maombi maalum.

Kulingana na Luka 3:21–22, "Ikawa, watu wote walipokwisha kubatizwa, na Yesu naye amebatizwa. Naye anaomba, mbingu zilifunuka; Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua. Sauti ikatoka mbinguni: 'Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe.'"

Huyu hapa Yesu mwanzoni mwa maisha yake ya utu uzima, mwanzoni mwa huduma yake. Je, anafanya nini? Haponyi. Hahubiri. Anaomba. Huu ujumbe unanena nami: lazima tuanze siku zetu kwa maombi. Katika maisha yangu ya kwanza kama Mkristo, nilihisi ni lazima nimwendee Mungu kwanza, kabla sijakabiliana na watu au matatizo ya siku. Ningeamka mapema asubuhi na kutumia sehemu muhimu ya siku kuwa pamoja naye. Ikiwa kwa sababu fulani huwezi kutumia muda wako wa asubuhi na Mungu, basi mpe sehemu muhimu zaidi ya siku yako—usimpe masaza.

Unaposoma Luka 5:15–16, tambua kwamba Yesu alikuwa anafaulu sana na halaiki ya watu, akihubiri, na kuponya. Lakini mara nyingi Yesu alijitenga na hayo yote na kutafuta mahali pa faragha kuomba. Hii inatuambia kwamba maombi yalikuwa muhimu zaidi kushinda chochote kile. Maombi aliyapa kipaumbele, na alikuwa alijitia nidhamu kufanya hivyo. Vivyo hivyo, sote tunahitaji *kuamua* kutenga *muda* kuomba.

Luka 9:18 inasema, "Ikawa alipokuwa akisali kwa faragha, wanafunzi wake walikuwapo pamoja naye, akawauliza, Je! Makutano hao wanasema ya kuwa mimi ni nani?" Tambua tamathali ya usemi hapa: Yesu alikuwa "faraghani" na wanafunzi wake walikuwapo "pamoja naye." Kuna njia kadhaa za kuelezea hili, lakini somo kuu ni kwamba wale wanafunzi walijifunza kuomba kwa kumsikia Yesu akiomba—alikuwa akifundisha kwa mifano. Je, unakutana na nani ili muombe pamoja ili ujifunze kutokana na mfano wake?

Luka 6:12–13 inasema, "Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha akimwomba Mungu. Na kulipokucha aliwaita wanafunzi wake; akachagua kumi na wawili miongoni mwao, ambao aliwaita mitume." Je, unadhani Yesu alikuwa anamwomba Mungu nini usiku mzima? Ninaamini aliomba hivi, "Ewe Mungu, kati ya wanafunzi wengi, nimchague nani awe mmoja wa wanafunzi wangu kumi na wawili?" Kwa maneno mengine, Yesu aliomba na kutafuta mwongozo wa Mungu kwa mambo muhimu aliyochagua katika maisha—na tupaswa kufanya hivyo pia.

Je, utaruhusu mfumo wa Yesu wa maombi ukuongoze? Anza hatua kwa hatua. Ni sawa kuanza kidogo—pengine kama dakika 10 kila asubuhi. Kadri unavyokua katika maombi, utaanza kuhisi kwamba Mungu anaongea nawe utakapomwomba akuongoze.

Jambo linalosisimua kiasi gani! Tambua kwamba Yesu alipoomba katika Luka 3:21, "mbingu zilifunguka." Ikiwa unataka kuishi na mbingu zilizofunguka, tenga muda uombe.

JANUARI 23 **23**

## Musa na Bwana—Uhusiano Binafsi Sana

*Musa akapanda .... mpaka mlima Nebo, hata kilele cha Pisga kukabili Yeriko. BWANA akamwonesha nchi yote... BWANA akamwambia, "... Basi nimekuonesha kwa macho yako, lakini hutavuka huko." Basi Musa, mtumishi wa BWANA, akafa huko, katika nchi ya Moabu, kwa neno la BWANA. Akamzika bondeni Moabu . . . . . Musa alikuwa mtu wa miaka mia moja na ishirini alipokufa; jicho lake halikupofuka, wala nguvu za mwili wake hazikupunguka . . . . Wala hajainuka tena katika Israeli nabii kama Musa, ambaye BWANA alimjua uso kwa uso; katika ishara zote na maajabu yote, ambayo BWANA alimtuma kuyatenda katika nchi ya Misri, kwa Farao, na kwa watumishi wake wote, na kwa nchi yake yote. Na katika ule mkono wa nguvu wote, tena katika ule utisho mkuu wote, alioutenda Musa machoni pa Israeli wote.*

*Kumbukumbu La Torati 34:1, 4–6a, 7, 10–12*

Je, unaweza kuwa na uhusiano binafsi kwa kiwango gani? Uhusiano binafsi kati ya Musa na Mungu ni wa ajabu sana—na unaochangamsha moyo. Kutoka kileleni mwa Pisga, "Bwana akamwonyesha nchi yote" (kif. 1). *Bwana alimwonesha*. Hivi ndivyo Musa alivyokuwa amefanyia kazi na ilimsababishia miaka arobaini ya shida. Sasa, ndoto yake ilitimia machoni mwake.

Kumbukumbu La Torati inasema, "Kisha BWANA BWANA akasema, 'Hii ndiyo nchi niliyoahidi.'" *Bwana akasema*—oh, alikuwa amenena na Musa mara nyingi sana. Kisha, Mungu anaendelea kusema, "Basi nimekuonesha kwa macho yako, lakini hutavuka huko." *Hutavuka huko*.

Kizuizi kilichomfanya Musa asivuke kilikuja mapema huko Kadeshi juu ya tatizo la maji. Kulipokuwa hakuna maji ya kunywa kwa watu wa Musa wapatao mamia elfu jangwani, Bwana alimwambia Musa aongee na mwamba, na maji yangemwagika. Musa aliwakusanya watu, akawakemea, na akasema, "Tuwatokezee maji katika mwamba huu?" (Hesabu 20:10). Aliupiga ule mwamba mara mbili kwa fimbo yake, na maji yakatiririka.

Mara tu Bwana akanena, akasema kwamba kwa sababu Musa na Haruni hawakumheshimu Bwana kama mtakatifu, hawataruhusiwa kuwafikisha Waisraeli katika nchi ya ahadi. Haijulikani hasa kosa lao lilikuwa nini—je, ilikuwa hasira ya Musa kwa watu wake waliokuwa wanalalamika? Je, ilikuwa ni kule kutofuata maagizo ya Bwana yaliyokuwa wazi? Au pengine madai yake ya "*tuwatokezee* maji," hivyo akajua sifa kwa muujiza wa *Bwana*? (Angalia Hesabu 20:1–12.)

Musa alikuwa amemsihi Bwana amruhusu "nivuke, nikaione hiyo nchi nzuri iliyoko ng'ambo ya Jordani, mlima ule mzuri, na Lebanoni," ingawa Bwana alikuwa tayari amesema kwamba haitaingia katika hiyo nchi (Kumbukumbu La Torati 3:25). Katika kujibu, BWANA alisema, "na ikutoshe" (kif. 26). Alimwambia Musa kwamba angeiona nchi, lakini "huuvuki mto huu wa Yordani" (kif. 27). Mungu alikuwa amemwagiza Musa amwagize Yoshua awaongoze watu katika (kif. 28). Mazungumzo ya kina kati ya Musa na Bwana yanaonesha uhusiano wao wa karibu kimaongezi—hii haikuwa mara ya kwanza ya Musa kumsihi Bwana.

Bwana alikuwa wazi katika kuelezea mustakabali wa Musa: "Ukafe katika kilima, huko ukweako, ukusanywe uwe pamoja na jamaa zako" (32:50). Je, ni mara ngapi tunaambiwa hali na wakati wa kifo chetu? Lakini Musa haoneshi dalili za huzuni juu ya tangazo hili. Anamwagiza Yoshua na kumhimiza yeye na watu: "Uwe hodari na moyo wa ushujaa, maana utakwenda pamoja na watu hawa hata nchi BWANA aliyowaapia . . . . Naye BWANA yeye ndiye atakayekutangulia" (31:7b, 8a). Maneno yake hayaoneshi hali ya kujisikitikia—ila anajali tu kufaulu kwa kazi hiyo.

Baada ya Musa kufa, Kumbukumbu la Torati linatupa hitimisho hili: "Wala hajainuka tena katika Israeli *nabii kama Musa*, ambaye *BWANA alimjua uso kwa uso*, katika *ishara zote na maajabu* yote, ambayo *BWANA alimtuma* kuyatenda katika nchi ya Misri, kwa Farao, na kwa watumishi wake wote, na kwa nchi yake yote. Na katika ule mkono wa nguvu wote, tena katika ule *utisho* mkuu wote, alioutenda Musa machoni pa Israeli wote" (34:10–12).

Musa aliiona nchi ya ahadi lakini hakuingia. Musa, "mtumishi wa BWANA" (34:5); Musa, "nabii" (kif. 10); Musa, "ambaye BWANA alimjua uso kwa uso" (kif. 10); Musa, "mtu wa Mungu" (33:1). Musa hakuingia katika nchi ya ahadi, lakini alipokufa huko Mlima Nebo, alipandishwa juu kwenye uwepo wa Bwana, ambayo ni ahadi kubwa zaidi.

Je, uhusiano wetu na Bwana ni wa karibu kiasi gani?

# Je, Ombi Lilijibiwa?

*Kwamba niokolewe kutoka kwa wale wasioamini katika Yudea, na tena huduma yangu niliyo nayo huko Yerusalemu ikubalike kwa watakatifu; nipate kufika kwenu kwa furaha, kama apendavyo Mungu, nikapate kupumzika pamoja nanyi.*
*Warumi 15:31–32*

Je, umewahi kuomba na usipokee majibu? Paulo aliwaomba Warumi waombee mambo matatu: (1) kwamba aokolewe kutoka kwa wale wasioamini Yudea; (2) kwamba huduma yake aliyo nayo huko Yerusalemu ikubalike kwa watakatifu; (3) kwamba kwa mapenzi ya Mungu, aweze kufika kwao kwa furaha.

Sehemu ya kwanza ya ombi la Paulo haikujibiwa—kusema kweli, wale Wayahudi wasioamini walikuwa ndio wa kulaumiwa kwa kupigwa kwake, kushtakiwa, na kusindikizwa na wanajeshi hadi Rumi. Lakini ombi la kwanza la Paulo ambalo halikujibiwa lilikuja kuwa njia ya kujibiwa kwa ombi la tatu.

Gordon Wetmore alisema, "Maombi si kule kuongea tu, lakini ni jinsi tunavyosikiliza." Na Paulo alisema, "Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea" (Warumi 8:26). Katika majaribu, Mungu alimwambia Paulo, "Uwe na moyo mkuu; kwa sababu, kama ulivyonishuhudia habari zangu Yerusalemu, imekupasa kunishuhudia vivyo hivyo Rumi nako" (Matendo 23:11).

Alipokuwa amefungiwa nyumbani, alinena na watu wengi waliokwenda kumsikiliza (28:23). Alipokuwa gerezani, Paulo hakuweza kuwakwepa askari wake, lakini hao askari wake pia hawakuweza kumwacha, na hatimaye askari wote wa kasri hiyo walijua habari za Kristo (Wafilipi 1:13).

Mungu alinena na Paulo, na kazi yake ikatimia. Ombi lake la tatu lilijibiwa![11]

11. *Reflecting God* Juni–Julai–Agosti 2010 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 18. Imetumiwa kwa ruhusa.

# Si Haki

*Kufundishwa matendo ya busara, katika haki na hukumu na adili.*
*Mithali 1:3*

*Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yoyote, na katika mambo yoyote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa. Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.*
*Wafilipi 4:12–13*

Akapiga kelele akisema, "Si haki!" Yule msichana wa miaka minne alitoa malalamiko yake kwa wazazi huku ndugu yake wa kiume mwenye miaka minane akitazama.

Wanandoa walimwandikia mhariri wa Miss Manners juu ya chakula cha jioni walichokuwa wanakiandaa kwa marafiki wachache wa bwana fulani aliyeaga dunia hivi majuzi. Watu wachache ambao hawakualikwa kwenye mlo huo wa jioni waliudhika kwa sababu walidhani walifaa kuwa hapo. "Si haki," wakasema.

Niliipigia simu kampuni yangu ya simu—ambayo kazi yake kuu ni mawasiliano yenye ufanisi kwa njia ya simu—ili warekebishe makosa kwenye bili yangu ya simu. Baada ya kuongea na mtu mmoja (hakuwa mtu anayefaa) kwa dakika mbili na kuachwa nisubiri kwa dakika hamsini na tatu, ilibidi nikate simu niendelee na kazi: "Si haki."

Mfalme Sulemani aliyekuwa na hekima aliandika na kusema lengo la mithali zake ni "kufundishwa matendo ya busara, katika haki na hukumu na adili" (Mithali 1:3). Itakuwa haki kusema kwamba hilo ndilo lengo la Mungu kwa wanadamu. Tunataka haki; tunarajia haki; lakini katika ulimwengu ulioharibiwa na dhambi, hivyo sivyo ilivyo.

Yesu anasimulia mfano wa mwenye shamba aliyeajiri vibarua kwa siku. Kila mmoja wao alimlipa dinari moja, ambao ndio uliokuwa mshahara wa siku. Wale wafanyakazi waliofanya kazi kwa saa kumi walilalamika kwamba wale waliofanya kazi kwa saa moja walipokea ujira ule -ule kama walivyopokea: "Si haki." Kama idadi ya saa walizofanya kazi ndio tatizo pekee, wangekuwa wanasema ukweli. Yule mwenye shamba alijibu akasema aliwalipa wale wafanyakazi waliofanya kazi kwa saa kumi kile kiwango

cha pesa walichokubaliana. Hakukuwa na udanganyifu wowote; kilikuwa ni kitendo cha wazi ambacho msingi wake ni makubaliano. Yule mwenye shamba alihisi kwamba kama alitaka kuwa mkarimu kwa mtu, ni haki yake kufanya hivyo. Huku wakiwa wale wafanyakazi waliofanya kazi kwa saa kumi wakikasirika kwa sababu ya kudhania kwao na matarajio yao, yule mwenye shamba alikuwa anafanyia kazi makubaliano yao ya wazi. Tunapokuwa tunatarajia haki wakati wote, tunajiandaa kuudhika.

Mtume Paulo alikuwa na jibu la suala hili: "Katika hali yo yote, na katika mambo yo yote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa" (Wafilipi 4:12). Alikuwa amepigwa, kupigwa mawe, na kufungwa jela kwa kumhubiri Kristo, na mapato yake yalikuwa yanabadilika-badilika. Haikuwa haki! Lakini aliridhika. Alikuwa amepata siri ya kuridhika: "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu" (kif. 13). Kristo aliyeishi ndani yake alimpa nguvu za kukabiliana na hali za maisha zisizokuwa za haki—na nguvu zake zinapatikana kwetu leo.

**JANUARI 26** **26**

# Aina Zote

*"Naye akasema, Mimi ndimi Yesu unayemtesa." "Lakini simama, uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda."*
*Matendo 9:5*

*Mwanamke mmoja, jina lake Lidia, mwenye kuuza rangi ya zambarau, mwenyeji wa Thiatira, mcha Mungu, akatusikiliza. Alikuwa a kimwabudu Mungu. Ambaye moyo wake ulifunguliwa na Bwana, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo.*
*Matendo 16:14*

Akiwa na umri wa miaka 15, Bekah aliweza kuchapishiwa makala yake katika jarida la *Holiness Today*. Sehemu ya makala yake ilisema hivi: "Baba yangu ndiye amekuwa akinipa changamoto na mama yangu ndiye amekuwa akinitia moyo. Yeye ndiye amekuwa akinifundisha jinsi ya kukabiliana na ulimwengu na mama yangu ndiye amekuwa akiniandaa kufanya hivyo. Amenipa changamoto ya kuwa na ndoto, kujaribu mambo mapya, na kumtumaini

Mungu hata katika mambo yasiyojulikana . . . . Karama ya kuweza kuchongwa na wazazi Wakristo haitapoteza nguvu zake maishani mwangu."[12]

Ni nzuri sana, sivyo?

Sauli, ambaye baadaye alijulikana kama Paulo, aliokoka kwa njia ya ajabu akiwa barabarani kwenda Dameski. Mwanga kutoka mbinguni ulimmulika, akaanguka chini na hasa akasikia sauti ya Yesu Kristo ikinena naye na kusema, "Mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe."

Baadaye, baada ya Paulo kuhudumu kama mmishenari wa Mungu, alifika Filipi, akatembelea sehemu ya mto, na akakuta kundi la wanawake huko, akiwemo Lidia. Paulo aliponena, "moyo wake ulifunguliwa na Bwana, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo" (16:14). Kuongoka kwa Lidia kulikuwa kuzuri na kwa unyenyekevu, lakini wa kweli. Alimwalika Paulo na wenzake wakae nyumbani kwake, nao wakakubali. Na baadaye, baada ya Paulo na Sila kufungwa gerezani kwa sababu ya kufundisha na kuwaponya watu, walikwenda nyumbani kwa Lidia. Watu walikuwa wamekusanyika nyumbani kwa Lidia (pengine lilikuwa kanisa la nyumbani), na huko, Paulo na Sila waliwafariji wale ndugu (kif. 40).

Somo ni hili: Kuongoka na kumfuata Kristo kunaweza kuwa kwa ajabu na kwa kushangaza au kuzuri na kwa unyenyekevu. Lakini kuongoka kote kunaweza kuwa halisi.

Katika huduma ya Paulo kwa Wafilipi, Bwana alimkomboa msichana aliyepagawa na pepo. Mungu alimwokoa Lidia, mwanamke aliyekuwa tajiri. Yule askari wa gereza Mfilipi aliokoka baada ya tetemeko kubwa la ardhi. Na baada ya askari kumpeleka nyumbani kwa ajili ya chakula cha jioni, mke wake na watoto wake walimpokea Bwana. Hapa katika mji huu watu wa matabaka matatu wanaokolewa—na katika mfano wa askari wa gereza, tunapata uongofu wa watu wazima na watoto.

Tunapata mfumo mwingine wa mwitiko wa familia Paulo anapomwandikia mchungaji kijana aitwaye Timotheo katika 2 Timotheo 1:5: "Nikiikumbuka imani uliyo nayo isiyo na unafiki, ambayo ilikaa kwanza katika bibi yako Loisi, na katika mama yako Eunike, nami nasadiki wewe nawe unayo." Kuna uwezekano mkubwa kwamba Timotheo aliongoka wakati akiwa mtoto kwa sababu ya ushawishi wa kiungu wa bibi yake na mama yake. Huenda hata ilikuwa katika nyumba ambamo mume/baba hakuwa muumini.

---

12. Bekah Rainey, "Kingdom Shapers," *Holiness Today* Mei–Juni 2020 (Lenexa, KS: Church of the Nazarene), 38.

Haijalishi yale uliyopitia wakati wa kuokoka kwako, jambo muhimu zaidi ni kwamba unaweza kusema, “Kristo yuko moyoni na maishani mwangu sasa hivi, na ninamfuata.”

Kuna ukweli wa Biblia ambao unazungumzia hakikisho na uhakika:

- 1 Yohana 5:11–12—“Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima.”
- 2 Timotheo 4:7–8 (Ushuhuda wa mwisho wa maisha ya Paulo)—”Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda. baada ya hayo nimewekewa taji la haki.”
- Warumi 8:16—“Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu.”

Nilipoongea na Bekah mwenye umri wa miaka kumi na mitano, aliyeandika makala nzuri sana iliyonukuliwa hapo juu, nilimuuliza jinsi alivyompokea Kristo. Akasema, “Nilipokuwa na umri wa miaka minne, mama yangu alikuwa akinisimulia hadithi. Nilimuuliza maswali juu ya ni nini maana ya kumpokea Kristo. Kisha nikasema nilitaka kumpokea Yesu moyoni mwangu. Mama yangu alisimamisha gari kwenye kituo cha mafuta, na tukaomba papo hapo. Nilihisi nimempokea Yesu wakati huo. Kadiri nilivyokuwa mtu mzima, maswali yaliibuka. Maswali hayo yalijibiwa yote wakati nilipotakaswa, jambo lililonitia nguvu zaidi.”

Kwa hiyo, *kila aina* ya watu wanampata Yesu. Na wanashuhudia uongofu *kwa njia za kila aina*. Lakini ashukuriwe Mungu, kila mtu *anaweza kumjua Yesu* kwa njia binafsi.

JANUARI 27 **27**

# Kuziba Gurudumu Lililotoboka

*Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki. Naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote.*
*1 Yohana 2:1*

Mpango wa Mungu, nia yake, matarajio aliyo nayo kwako ni "msitende dhambi." Lakini je nikitenda dhambi, hata nikiwa Kristo aliyetakaswa? Je, nifanye nini?

Kwa Mkristo aliye makini, kuna majaribu mengi ya kutukatisha tamaa. Lakini ujumbe u wazi: Achia hapo ulipo. Usisubiri hadi ibada ya kanisa inayofuata au hata asubuhi yake. Hapana, papo hapo, lipeleke suala hilo kwa Kristo. Yeye ndiye Mwombezi aongeaye na Baba kukutetea wewe. Iungame hiyo dhambi, iache, na uombe uhusiano wako na Mungu urejeshwe upya. Kristo "sadaka ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu" (1 Yohana 2:2) atakutakasa upya.

Hebu chukulia kwa mfano unaendesha gari kutoka Columbus hadi Dayton, Ohio. Kisha, ghafla gurudumu lipate pancha. Utafanya nini? Kuna mambo matatu unayoweza kufanya:

1. Unaweza kutoka nje ya gari, ukaangalia lile gurudumu lenye pancha, na kusema, "Hili gurudumu limepata pancha. Ninakata tamaa. Sitaweza kufika Dayton. Kwa kuwa ni hivyo, nitaacha kuendesha gari kabisa."
2. Unaweza kusema, "Gurudumu limepata pancha. Nitaendelea kuendesha gari hadi nitakapofika kwenye kituo cha mafuta." Kufikia wakati wa kuendesha gari mwendo mrefu hivyo, utahitaji gurudumu jipya, pangine rimu mpya, na nani ajuaye, pengine utakuwa umeharibu sehemu ya chini ya gari lako uliendelea kuliburuta.
3. Unaweza kusimama mara moja unapopata pancha, na kushuka chini, kuchukua gurudumu la akiba, na kulibadilisha, na kuendelea na safari yako huku ukiwa umekatizwa tu kidogo.

Wakristo waliojikwaa katika dhambi sharti wasiamue kuacha maisha ya Kikristo kabisa. Wala hatupaswi kusubiri hadi ibada ya Jumapili inayofuata, au hata siku inayofuata—tukifanya hivyo, tutaishia kuhitaji ukarabati mkubwa wa kiroho. Badala yake, sharti tuichukue ile dhambi mara moja na kuipeleka kwa Bwana na kuitubu, na kumtumaini Kristo atusamehe, atusafishe, na aturejeshe upya. Kwa njia hii, tunaweza kuendelea na safari yetu pasipo ushirika wetu na Mungu kukatizwa. Huu ukweli mmoja kutoka katika 1 Yohana 1:7: "Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake yesu, mwana wake, yatusafisha dhambi yote." Kwa hiyo kumbuka kirai cha "kama" katika 1 Yohana 2:1.

# Anajua Hitaji langu

*Baba yako anajua kile unachojitaji kabla hujamwomba.*
*Mathayo 6:8*

Mimi na Nancy tulikuwa tumekutana mara nyingi na Wakristo wawili wachanga, Myra na Christopher, ili tuwafundishe uanafunzi. Walikuwa wamechumbiana na wanapanga harusi. Mnamo Jumanne moja, Christopher alichelewa kutoka kazini na Myra peke yake ndiye aliyeweza kuja kutuona. Basi nikamwomba Mungu ayaongoze mazungumzo yetu. Mara kwa mara katika mikutano yetu, nilikuwa na mada maalum, lakini usiku ule, sikuwa nayo.

Kwa hiyo nikaomba, "Sasa, Bwana, tumwambie Myra nini?" Nilikuwa nimeguswa na Andiko nililosoma kutoka Hesabu 1 siku hiyo, kwa hiyo ikaonekana hilo ni jambo linalofaa kushiriki naye. Hasa, nilitaka kuzungumzia juu ya ukweli wa ajabu uliofunuliwa na maagizo ya Mungu katika Hesabu 1—Mungu anajua jina langu Kabla hatujakutana, Nancy pia alinipa kitabu ambacho sikuwahi kukiona mbeleni, ambamo ndani yake mna mwanamke Mkristo anayewaandikia wanawake wengine kuhusu kujipenda na kujithamini.

Tulipokuwa tukishiriki wazo kwamba "Mungu analijua jina langu" na kile kitabu juu ya kujipenda na kujithamini, uso wa Myra ulichangamka na kuanza kung'aa. Alituambia kwamba alikuwa akisumbuka sana juu ya hali ya kuwa na thamani. Akasema, "Umenipa kile nilichohitaji hasa."

Nikasema, "Myra, Mungu ndiye amefanya hivyo. Myra, analijua jina *lako*. Zaidi ya hayo, anajua hitaji *lako*."

Na wewe, unayesoma maneno haya—anajua *jina lako*. Anajua *hitaji lako*. Na andiko la leo linasema, "Baba yako anajua kile unachohitaji kabla hujamwomba."

# Walishiriki

*Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza; naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele. Mtu akinitumikia, na anifuate; nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu.*
*Yohana 12:25–26*

Alipokuwa akikabiliana na msalaba, akiwa tayari kuyatoa maisha yake kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu, Kristo aliwapa changamoto wafuasi wake. Aliwaita wayatoe maisha yao yote kwa Kristo, wamfuate, na wajitoe kwa Mungu (Yohana 12:23–26).

Nimesoma habari za watu ambao wanafanya hivyo —Vilevile wengine ninawajua binafsi.

Bob na Bessie Black, ambao ni wakulima kutoka Marekani ya magharibi ya kati, walijisalimisha kwa Yesu na wakajitoa kwa Mungu kuhamia Papua New Guinea, ambako Bessie alifanya kazi kama mwalimu na Bob alikuwa akikarabati na kutunza kituo cha umishenari.

Keith Fitzsimmons, ambaye ni mhasibu, alianza kumfuata Yesu na kuhisi wito wa Mungu wa kutoa sehemu ya muda wake kuhudumu kama mlezi wa kanisa.

Bev Burgess alishuhudia neema ya Yesu iokoayo na nguvu zake za uponyaji. Baadaye, aliamua kutumia maisha yake kuwaambia wengine waje wamjue Yesu.

Rees Howells kutoka Welsh alikuwa mchimba migodi wa makaa ya mawe. Baada ya kukutana na Kristo, alihisi anaitwa kuwa mwombezi, na alitumia saa nyingi kuomba kila siku. Hatimaye, aliomba hadi Bible College of Wales kikaanzishwa.

Hobby, mchapishaji wa magazeti, alimpokea Yesu akiwa na miaka sitini. Kisha alijifunza ukweli wa Malaki 3:10: "'Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu. Mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la.'" Kwa furaha Hobby alianza kutoa zaka, akisema, "Kwa sababu ya yale Yesu amenitendea,

hicho ndicho kitu cha chini ninachoweza kumfanyia." Hobby alijitoa kwa Mungu.

Charles Colson, wakili na mmoja wa washauri wa karibu wa Rais Richard Nixon, alikutwa na hatia na akafungwa kwa sababu ya uhalifu unaohusiana na kashfa ya Watergate. Muda mfupi kabla hajafungwa jela, alimpokea Kristo. Colson alisema mambo yafuatayo juu ya wakati mgumu katika kifungo chake:

> Ulikuwa ule usiku nikiwa katika chumba changu kilichokuwa kimya nilipojisalimisha kabisa, na kukamilisha kile nilikianza kwenye barabara ya Tom Phillips' miezi kumi na minane iliyopita: Nikasema, "Bwana, kama hivi ndivyo mambo yalivyo, basi nakushukuru. Ninakusifu kwa kuniacha jela, kwa kuwaruhusu wachukue leseni yangu ya uanasheria, ndiyo—hata kwa mwanangu wa kiume kukamatwa. Ninakusifu kwa kunipa upendo wako kupitia kwa watu hawa, kwa kuwa Mungu, kwa kiniruhusu tu nitembee na Yesu."
>
> Maneno hayo yalifuatiwa na furaha kubwa—kuwekwa huru, kumwachia Mungu kila kitu kama ndugu yangu Harold alivyokuwa ameniagiza kufanya. Na katika saa zilizofuata nilipokea nguvu zaidi kuliko nilivyowahi kupokea kabla. Huu ndio uliokuwa ushuhuda halisi kileleni mwa mlima. Ulimwengu ulijaa furaha na uzuri juu yangu na karibu yangu. Kwa mara ya kwanza nilihisi niko huru kweli kweli, hata ingawa hali zangu za kimaisha zilionekana kudorora sana.[13]

Saa arobaini na nane baadaye, Jaji Gerhard Gesell alitangaza kufunguliwa kwa Colson kutoka gerezani. Colson aliyatoa maisha yake aliyoyasalimisha kwa Mungu kwa kuanzisha shirika liitwalo Prison Fellowship, ambalo aliliongoza maisha yake yote yaliyosalia. Shirika hili limekuwa nguvu kubwa zaidi katika kuleta mabadiliko ya magereza Marekani.

Hadithi hizi zote zilitokea kwa sababu watu walijitoa kwa Mungu.

**JANUARI 30** **30**

# Bwana, Umetenda Tena!

*Kwa sababu BWANA, Mungu wenu aliyakausha maji ya Yordani, mbele yenu, hadi mlipokwisha kuvuka kama BWANA Mungu wenu, alivyoitenda Bahari ya Shamu, aliyoikausha mbele yetu hata tulipokwisha*

13. Charles W. Colson, *Born Again* (Old Tappan, NJ: Fleming H. Revell, 1977), 339–40.

*kuvuka. Watu wote wa duniani wapate kujua mkono wa BWANA, ya kuwa ni mkono wenye uweza, na ili nanyi mpate kumcha BWANA, Mungu wenu, milele.*
*Joshua 4:23–24*

“Tumainia wakati wako mzuri na Mungu.” Nafikiri V. Raymond Edman alisema hivyo, lakini bila kujali nani aliyasema hayo, ni maneno ya hekima na ya kweli. Yamkini kipindi kilichokuwa kizuri zaidi kwa Waisraeli ulikuwa ule muujiza wa kuigawanya Bahari ya Shamu na kuwafungulia njia ya kutoroka utumwa wa Misri. Sasa, baada ya miaka arobaini ya kusafiri, walikuwa wamevuka mto Yordani hadi katika nchi ya ahadi.

Safari yao ilikuwa ya shida. Matatizo yao mara kwa mara yalikuwa ni ya kujisababishia wenyewe. Walikuwa wamelalamika, waliasi, na kukaidi, na matokeo yake, Mungu alikuwa amewakemea na kuwahukumu. Ingawa kulikuwa na miujiza kama ya manna, kware, na maji kutoka mwambani, mtazamo wa Waisraeli ulikuwa hasi na wa kushindwa. Lakini Mungu alikuwa anajitahidi kuwaongoza, kuwawezesha, na kuwatia moyo. Kisha akafanya tena—aliukausha Mto Yordani kama alivyoifanya ile Bahari ya Shamu. Waisraeli walikumbushwa kwamba Mungu alikuwa amefanya hivyo. Alikuwa ametengeneza njia kupitia Bahari ya Shamu, na sasa alikuwa amewatengenezea njia kupitia Yordani. Yoshua aliita “mambo ya ajabu” (3:5). Aliwaambia Waisraeli, “jambo hili mtajua ya kuwa Mungu aliye hai yu kati yenu” (kif.10).

Ukidhani kuvuka mto si jambo la kuvutia kama kuvuka bahari, ngoja kidogo—sikiliza kabla hujadumisha kazi ya Mungu hapa. Matini inatuambia kwamba mto Yordani ulikuwa kwenye kiwango cha kufurika (kif. 15), na “ndipo hayo maji yaliyoshuka kutoka juu yakasimama, yakainuka, yakawa kichuguu kirefu sana” huko mji wa Adamu (kif. 16). Katikati ya mto Yordani, kuhani “akasimama imara mahali pakavu” hadi taifa zima likavuka “katika nchi kavu” (kif. 17).

Baada ya kuvuka vizuri, Yoshua aliwakumbusha Waisraeli—Mungu amefanya tena! Mara tatu katika 4:23–24, anatumia kirai cha, “BWANA Mungu wenu.” Uhusiano binafsi zaidi, yu karibu, karibu sana, na halisi. Bila shaka ujasiri wa Waisraeli uliongezeka sana. Kwa Waisraeli, hili lingekuwa kumbukumbu ya kumcha Bwana; pia lingekuwa ushuhuda kwa watu wa duniani.

Kwa kweli huu ni ujumbe wako na wangu leo: Chochote kile unachokumbana nacho leo, hata ikiwa kinaonekana kuwa giza sana, Mungu aliyefanya kazi katika maisha yako awali atafanya kazi tena. Mtegemee kabisa.

Kuwa wazi kuisikia sauti yake na kupokea mwongozo wake na uwe macho. Nini kingine? Ikiwa una kipindi cha Bahari ya Shamu, unaweza kuwa kwenye kipindi cha ukingoni mwa Mto Yordani. Usiwe na mashaka gizani juu ya kile alichokwambia Mungu nuruni.

JANUARI 31 **31**

# Siku Mbaya

*Eliya alikuwa anaogopa na akakimbia ili aokoe maisha yake . . . .*
*Akafika mahali penye kichapukizi, akaketi chini yake na akaomba afe.*
*"Yatosha; sasa, Ee BWANA, uiondoe roho yangu; kwa kuwa*
*mimi si mwema kuliko baba zangu." Naye akajinyosha*
*akalala chini ya mretemu.*
*1 Wafalme 19:3a, 4b–5*

Mara moja moja, huwa ninakuwa na siku mbaya. Kwa hiyo Eliya—alikuwa na siku mbaya sana.

Alikuwa mtu mkubwa wa Mungu. Alikuwa amemsuta Mfalme Ahabu aliyekuwa mwovu na akaandaa shindano miongoni mwa manabii wa uwongo wa Baali wapatao 450, ambao wote waliasaidiwa na mke wa mfalme, Yezebeli. Kuni ziliandaliwa; wale manabii wa uwongo walichinja fahali na wakamwita Baali aichome kwa moto ile dhabihu. Walimwita kuanzia asubuhi hadi saa sita mchana, lakini Baali hakusema kitu. Wakati huo huo, Eliya alijenga upya madhabahu ya Bwana, akaweka kuni na akatoa dhabihu ya fahali juu yake, na akaimwagia maji. Yule Mungu ambaye angejibu kwa moto ndiye angekuwa Mungu wa kweli. Eliya aliomba ombi fupi, na moto wa Bwana ukashuka. Wale watu waliwakamata wale manabii wa Baali na wakawaua.

Kisha, Eliya alimwambia Ahabu atafute kitu cha kula kwa sababu, mvua ya miujiza na kubwa ilikuwa inakuja kuondoa ukame. Eliya alienda Karmeli, akakaa mkao wa dua, na akamtuma mtumishi wake kwenda kuangalia mawingu mara saba. Hatimaye, wingu—Ahabu alipanda gari lake la farasi na kwenda kwa Yezebeli. Mvua ilimwagika, na Eliya akakimbia mbele ya Ahabu. Ahabu alimwambia Yezebeli kile kilichotokea, na akamtisha Eliya kwa kifo. Ndiposa Eliya aliogopa (I Wafalme 18:1–19:3).

Maneno ya Eliya yanaonyesha kwamba alikuwa amefadhaika. Sababu ya kufadhaika huko huenda kulikuwa pamoja na woga wa kifo chake mwenyewe;

kuchoka kwa mwili; na uchovu wa kiakili na kihisia baada ya kutuma nguvu nyingi sana za kiroho.

Kwa hiyo Eliya anafanya nini? Analala kidogo. Malaika wa Bwana anamtembelea, na anakula kitu. Kisha analala tena, malaika anamtembelea tena, na anatii maagizo ya malaika kwa kwenda mahalai pa faragha. Hapo, yeye na Mungu wanakutana na kuwa na mazungumzo mazuri. Kuna tetemeko la ardhi na moto, lakini Mungu hayuko katika matukio hayo; badala yake, yu ndani ya mnong'ono wa upole. Mungu anampa Eliya kazi, naye anatii—mfadhaiko ulikuwa umepita (I Wafalme 19:3–21).

Ninapokuwa na siku mbaya, ninadumisha mambo yafuatayo:

1. Bado ninasoma Neno. Ahadi zake zote bado ni za kweli. Najitia moyo katika maneno aliyoambiwa Yoshua na malaika: "Iweni hodari na moyo wa ushujaa, msiogope wala msiwahofu; kwa maana BWANA, Mungu wako, yeye ndiye anayekwenda pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha" (Kumbukumbua La Torati 31:6).
2. Bado ninaomba. Ninatambua kwamba ingawa kusikia kwangu sauti ya Mungu—kusikia kwangu kwa kiroho—kuna kufifia kwa sababu zozote zile, bado Mungu yuko na bado anaongea hata wakati kusikia kwangu si kubaya.
3. Bado ninaandika shajara yangu. Katika kuandika kwangu shajara, ninataja zile siku mbaya.
4. Ninauchunguza moyo wangu kuona ikiwa kuna dhambi yoyote inayozua mawasaliano yangu na Mungu.
5. Ninachunguza shughuli zangu za hivi karibuni. Je, nimelala vizuri na kula chakula kizuri?
6. Ninachunguza niliyomfanyia Bwana hivi karibuni. Kama imekuwa nyingi, basi kupumzika kihisia kunaweza kuwa jambo la kawaida. Mapumziko yanasaidia sana.
7. Ninafanye kile Hazel Lee alifanya alipopata habari kwamba mtoto wake Gary alikuwa amekamatwa na kufungwa jela wakati wa kutekwa kwa Ubalozi wa Marekani huko Irani. Alikufa ganzi kihisia. Aliomba na kusema, "Bwana, nifanye nini?" Mungu akamjibu, "Chukua hatua inayofuata." Kwa hiyo Hazel aliendelea kufanya shughuli zake za kawaida—alihudhuria shule ya Jumapili, akafundisha darasa lake, na akaenda kanisani. Mimi vilevile, nitaendelea kufanya shughuli zangu za kawaida.

Ninapodumisha utaratibu huu, sitashangaa ikiwa, baada ya muda, nitatembelewa na Mungu au nitasikia neno kutoka kwa Bwana. Na litakapotokea, nitakuwa na siku ya furaha.

# Mungu Hutoa Msaada Wakati wa Matatizo

*Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, Ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari, maji yake yajapovuma na kuumuka. BWANA wa majeshi yu pamoja nasi; Mungu wa Yakobo ni kimbilio letu.*
*Zaburi 46:1–3, 11*

Kwangu, sikuwa na maswali yoyote juu yake—nilipokuwa Mkristo, ilibidi nijitenge na kikundi changu cha chuoni na matatizo yake ya ubaguzi, pombe, na siri. Lakini nilipokea barua kutoka kwa baba yangu iliyoniumiza vibaya sana—ilionekana kana kwamba ardhi "ingepasuka." Mpenzi wangu aliniandikia barua na akaniita mwenda wazimu, na akauvunja uhusiano wetu—"Ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari." Kundi langu lilinishinikiza—"maji yake yananguruma."

Lakini vumilia, nafsi yangu. Hizi ni hali; kisha kuna Bwana, "kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso." Ndani ya saa ishirini na nne, katika matukio matatu tofauti, Mungu alinipatia kifungu ambacho sikukijua awali: "Hata baba yangu na mama yangu wakiniacha, Bali BWANA atanikaribisha kwake" (Zaburi 27:10). Ndani ya miezi sita, mama yangu aliokoka. Ndani ya miezi kumi na mitano, lile kundi langu la marafiki lilinialika kunena nao kuhusu jinsi ya kuwa Mkristo. Ndani ya miaka minne, Bwana alinielekeza kwa msichana mrembo Mkristo ambaye alikuja kuwa mke wangu. Ndani ya miaka mitano, baba yangu alimpokea Yesu Kristo na sasa yuko mbinguni akinisubiri: BWANA wa majeshi yu pamoja nasi."[14]

---

14. Awali kilichapishwa katika C*ome Ye Apart* Machi–Aprili–Mei 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 38. Imetumiwa kwa ruhusa. (Chapisho hili liligeuka kuwa*Reflecting God*.)

# Vipi kuhusu Yule Mtu ambaye Hajawahi Kumpokea Kristo?

*Kwa hiyo, wewe mtu uwaye yote uhukumuye, huna udhuru;*
*kwa maana katika hayo umhukumuyo mwingine wajihukumu mwenyewe*
*kuwa na hatia; kwa maana wewe uhukumuye unafanya yale yale.*
*Warumi 2:1*

Ikiwa Biblia inafundisha kwamba mtu anaweza kwenda kwa Baba na kupata wokovu kupitia kwa Kristo pekee (Yohana 14:6), je, yule mtu ambaye hajamsikia Kristo atafanya nini? Inaonekana si haki. Je, Maandiko yanasemaje juu ya swali hili?

1. "Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru" (Warumi 1:20). Uumbaji unatupa ushahidi mkubwa sana wa nguvu *zote* za Mungu na asilia, na wanadamu wote wanaweza kushuhudia ulimwengu ulioumbwa.
2. "Kwa maana katika hayo umhukumuyo mwingine wajihukumu mwenyewe kuwa na hatia; kwa maana wewe uhukumuye unafanya yale yale" (2:1). Je, hili hufanyikaje? Hebu fikiria mtu anayeishi katika kabila lililotengwa. Hajasikia habari za Kristo na anaishi katika utamaduni unaoruhusu wake wengi. Basi mtu huyu anapokuwa amekusanyika na wanaume wengine karibu na moto wa kambini, anawakemea na kusema, "Si vizuri kuwapiga wake zenu!" Usiku uliofuata, mke wake wa pili alitia chumvi nyingi kwenye nyama yake ya kuchoma, na akakasirika na kumtandika. Anahukumiwa na yuko chini ya hukumu ya Mungu kwa sababu amevunja vigezo vile alivyowawekea wengine—amejihukumu mwenyewe. Hata ingawa yule mtu hajawahi kusikia habari za Kristo, kuna kigezo cha haki ambacho kwacho anahukumiwa.
3. Si ajabu Warumi inaongezea kusema, "wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu" (2:4).
4. Na zaidi: "Hao waionesha kazi ya torati iliyoandikwa mioyoni mwao" (2:15). Mawazo ya watu yanaweza kuwashtaki au kuwatetea "katika

siku ile Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu, sawasawa na Injili yangu, kwa Kristo Yesu" (2:16). Bado hiki ni kigezo cha haki!

5. Hata hivyo, ukikata tamaa kwamba, licha ya kigezo cha haki, "kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (3:23), je, kuna njia ambayo kwa kiasi fulani mtu anaweza kupata haki mahali pa dhambi? "ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio" (Warumi 3:22).
6. Si ajabu ni muhimu sana kutoa ujumbe wa Kristo kwa kila mtu ninayemjua, na kufanya sehemu yangu ya kuutuma ujumbe ulimwenguni kote.

**FEBRUARI 3** **34**

# Kupanga Njia

*Akamwuliza,"Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?"*
*Marko 10:17*

Maili elfu tatu na mia tano na vituo kumi vya kusimama vinavyodumu kuanzia usiku mmoja hadi wiki moja, maili zote hizo ni kwa gari—huo ulikuwa mradi wangu leo. Iligharimu maandalizi mazuri, ikiwa ni pamoja na kutafuta na kuhifadhi hoteli ya wasafiri kwa kila mwisho wa siku. Pia ilijumuisha kuwatembelea mpwa wangu, kukaa huko siku kadhaa na rafiki yangu wa muda mrefu, kuendesha mikutano ya uvuvio, na kuchukua wiki moja ya likizo. Nilikuwa ninapanga ile njia nitakayotumia, lakini wakati wote nikiwa na lengo la kutafuta na kufika mahali fulani maalum.

Kupanga njia na kuyafikia malengo ni mifumo ya kawaida katika maisha. Unaweza kuchagua chuo au shule ya kiufundi ili kulifikia lengo la kazi fulani au taaluma. Unaweza kutenga mapato yako ya kila wiki kwenye maafao ambayo hayatozwi ushuru ili uweke akiba kwa ajili ya kustaafu kwako. Unaweza kununua bima ya afya ili kukimu mahitaji ya wapendwa wako utakaowaacha nyuma.

Mtu mmoja alimkimbilia Yesu na akamwuliza, "Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?" Katika akili ya huyu bwana, "nifanye nini" ndiyo iliyokuwa njia, na "uzima wa milele" ndilo lililokuwa lengo. Yesu alimwambia sharti azifuate Amri Kumi; yule bwana akasema

alikuwa amefanya hivyo. Yesu, kwa nguvu zake za miujiza, aliuona moyo wa huyu bwana na akalitambua tatizo, ile sehemu ambayo hakuwa nayo. Alimwambia auze vitu alivyo navyo na awape maskini hizo hela—kisha angekuwa na hazina mbinguni. Vilevile, alimwambia yule mtu, "kisha, njoo, unifuate" (Marko 10:21).

Vifungu vingine vya Maandiko zinafafanua uelewa wetu wa lengo hili la uzima wa milele:

- Yesu, katika Yohana 17:3 anasema—"Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma."
- Yohana 3:16—"Kwa maana jinsi hii mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."
- Paulo, katika Warumi 6:23—"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."
- Yohana anasema tena katika 1 Yohana 5:11–12—"Na huu ndio ushuhuda: ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."

Sisi sote hupanga njia zetu kwa majini kuyafikia malengo ambayo mwisho wake ni maisha haya tunayoishi. Je, ni wangapi miongoni mwetu tumepanga njia inayotupeleka kwenye uzima wa milele—lengo litakalo yachonga maisha haya na yale yajayo?

**FEBRUARI 4** **35**

# Mungu Alitupenda Kwanza

*Hakuna woga katika upendo. Lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu. Na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo.*
*1 Yohana 4:18*

"Lazima aniombe msamaha kwanza. Niko tayari kumsamehe na kusahau. Lakini baada ya kuongea nami kwa njia hiyo, naona anapaswa kuniomba msamaha." Je, umewahi kumsikia mtu akisema hivyo?

Najiuliza nini kingetokea kwa yule mwanamke Msamaria pale kwenye kisima cha Yakobo kama Yesu angekuwa na mtazamo huo juu yake. Bila shaka yule mwanamke alipaswa kumwomba Mungu msamaha—zaidi ya hayo, alihitaji kutubu. Lakini haonekani kuwa katika hali ya "kuungama" vile hadi Mwokozi alipomwendea kwanza. Hiyo ni ishara ya upendo—upendo utamtafuta yule anayehitaji msaada.

Lakini kabla upendo haujakamilika, lazima kuwe na mtu wa kuweza kuupokea na kuurudisha. Upendo ndicho kiwango cha pekee ambacho kwacho watu na Mungu wanaweza kuwasiliana kikamilifu. Kwa sababu sisi ni binadamu, tuna mipaka inayotokana na uwezo wetu mbalimbali. Hata hivyo, lengo na madhumuni yetu, yakihamasishwa vilivyo kwa upendo wa Mungu, yanaweza kubarikiwa kwa ukamilifu. Hili linawezakana "yeye alitupenda kwanza" (kif. 19).[15]

**FEBRUARI 5** **36**

# Kuwaambia Wengine

*Yesu . . . alisema, "Nenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu,*
*kawahubirie ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana,*
*na jinsi alivyokurehemu."*
*Marko 5:19*

Yule mtu mwenye kichaa aliyeishi makaburini alipokutana na Yesu ana kwa ana, Yesu alitambua kwamba alikuwa amepagawa na pepo. Yesu alipomweka huru dhidi ya mapepo, yule mtu alibadilika—, baada ya muda mfupi alikuwa "ameketi, amevaa nguo, ana akili zake" (Marko 5:15). Alishukuru sana kwa yale Yesu alimtendea kiasi kwamba alimwomba Yesu ikiwa inawezekana asafiri naye wakati Yesu alipozuru mji mmoja hadi mwingine akihubiri na kuponya. Yesu alisema hapana na akampa kazi ya kufanya. Hebu natuyachambue yale maagizo aliyompa Yesu kirai kwa kirai:

- "Nenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu"—Nenda kwa wale unaowajua tayari, wale unaowaelewa, wale wanaokujua, ikiwa ni pamoja na maisha yako ya zamani.

15. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Machi–Aprili–Mei 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 37. Imetumiwa kwa ruhusa. (Chapisho hili liligeuka kuwa*Reflecting God*.)

- “Kawahubirie ni mambo gani makuu”—Elezea yale mabadiliko ya nguvu, mazuri ambayo Kristo ameleta katika maisha yako.
- “Aliyokutendea Bwana”—Ni yale Kristo aliyokutendea, bali si yale uliyomtendea Kristo.
- “Aliyokutendea”—ni hadithi yako binafsi, si yale yaliyonenwa au kushuhudiwa na mtu mwingine.

Mwaka mmoja na nusu baada ya kuwa mlevi kupindukia chuoni na kuacha shule, rafiki yangu aitwaye Peter alikuja kwenye ibada ya chuoni. Tulipokutana hapo, alinitolea ushuhuda wa sentensi moja: “Chic, mimi ni mtu tofauti kuliko nilivyokuwa kwa sababu nilimpata Bwana.” Maneno ya Peter yalifungulia mlango ushuhuda mwingine kamili: ndani ya saa ishirini na nne za kusikia hadithi ya Peter, nilimpokea Kristo.

Rafiki yangu Jolene alifafanua kumpokea kwake Kristo namna hii: “Maisha yangu yalikuwa kama fumbo na Mungu ndiye aliyekuwa mfumbua fumbo.”

Tom Phillips, rais wa Raytheon Corporation, alitoa ushahidi mbele ya wakili wa White House aitwaye Charles Colson:

> Sikuona nina kitu chochote kilichokuwa cha maana. Yote yalikuwa wazi. Vitu vyote katika maisha havina maana ikiwa mtu hajatambua kuna nini chini ya vitu hivyo . . .
>
> Usiku mmoja nilikuwa New York kwa ajili ya shughulia ya kibiashara na nikaona Billy Graham alikuwa na Mkutano Mkubwa wa Injili katika Madison Square Garden . . . Nikahudhuria—nikiwa na maswali, nadhani—nilitumai pengine ningepata majibu. Yale aliyosema Graham usiku ule yalinifanya nikaelewa kila kitu. Niliona kile nilichokuwa sina, uhusiano binafsi na Yesu Kristo, kule kutomkaribisha katika maisha yangu, sikuwa nimempa maisha yangu. Kwa hiyo nikafanya hivyo—usiku uleule kwenye ule Mkutano Mkubwa wa Injili.
>
> . . . Nilimwomba Kristo aingie maishani mwangu na niliweza kuhisi uwepo wake ukiwa nami. Nilihisi amani yake ndani yangu. Niliweza kuhisi Roho wake akiwa hapo nami. Kisha nikaenda kutembea peke yangu kwenye mitaa ya New York. Sikuufahamu mji wa New York hapo kabla, lakini usiku huo ulikuwa mzuri. Nilitembea kutoka sehemu moja hadi nyingine. Kila kitu kilionekana tofauti kwangu. Kulikuwa kunanyesha kiasi na taa za mjini ziliunda mwanga wa dhahabu. Kitu kilikuwa kimetendeka kwangu na nilikijua.[16]

16. Charles W. Colson, *Born Again* (Old Tappan, NJ: Fleming H. Revell, 1977), 110.

Tambua kwamba Phillips alisisitiza ile tofauti kati ya maisha yake kabla ampokee Kristo na baada ya kumpokea Kristo.

Mnamo Jumatano usiku, nilishiriki imani yangu na njia ya uzima wa milele na Lyle, aliyekuwa naibu wa msimamizi wa shule. Lyle aliniambia alikuwa ni mtu makini na mfikirivu na asingeweza kumpokea Kristo usiku ule—alikuwa hana budi kufikiria juu ya hilo. Mnamo Ijumaa, alikwenda kwenye duka la kuuzwa vifaa vya ujenzi kununua bawaba kwa ajili ya kabati za jikoni alizokuwa akijenga. Alipoegemea vile vifaa vilivyokuwa vinaoneshwa, alisikia sauti ikisema, "Unanunua kitu kitakachoshika kutu. Ninataka kukupa kitu kitachodumu milele." Kwa hiyo Lyle alikwenda pale palipokuwa gari lake, akaomba, na kumpokea Yesu Kristo na uzima wake wa milele. Ndani ya mwaka mmoja, Lyle alijiunga na kanisa lake kwa kukiri imani yake na akateuliwa kuwa msimamizi wa shule ya Jumapili ya kanisa lake.

Je, unajua nani aliongea na Lyle katika lile duka la vifaa vya ujenzi? Alikuwa ni Roho Mtakatifu. Yesu alisema, "Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia. Nanyi pia mnashuhudia" (Yohana 15:26–27). Roho Mtakatifu ndiye mwinjilisti mkubwa wa Utatu. Atasaidia na kutilia mkazo ushahidi na ushuhuda wako, hata kama unaogopa.

**FEBRUARI 6** **37**

# Hadithi Yako ya Kiroho

*Yesu . . . alisema, "Nenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu,*
*kawahubirie ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana,*
*na jinsi alivyokurehemu."*
*Marko 5:19*

Tunapotumia Marko 5:19 katika maisha yetu leo, tunaona kwamba maneno ya Yesu yanaelezea shuhuda zetu wenyewe.

**Hadithi yako ya kiroho:**

- Ni nzuri—"kwa kiasi gani"
- Inamtukuza Bwana—"Bwana"
- Ni ya uhusianobinafsi—"amekutendea"
- Ni ya maneno—"waambie"

**Inajumuisha Kabla, Jinsi, na Tangu Lini:**

- Jinsi nilivyokuwa *kabla* sijakutana na Kristo
- *Jinsi* Nilivyompokea Kristo
- Maana ya Yesu Kristo katika maisha yangu *tangu hapo*

Na sasa ninawahimiza—katika mazungumzo ya ana kwa ana na katika ibada za umma semeni, "yale Bwana amekutendea."[17]

FEBRUARI 7 **38**

# Kuwaandaa Wanafunzi Wanaowafanya wengine kuwa Wanafunzi

*Nendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi.*
*Mathayo 28:19*

*Nyingine zikaanguka penye udongo ulio mzuri zikazaa—*
*moja mia, moja sitini, moja thelathini.*
*Mathayo 13:8*

*Na mwenye hekima huvuta roho za watu.*
*Mithali 11:30*

Jukumu la kanisa ni kuwafanya watu kuwa wanafunzi ambao watawafanya wengine kuwa wanafunzi—haya yalielezwa tena na tena na mchungaji mcha Mungu na rais wa chuo cha Biblia Gordon Wetmore. Na tumeona kazi hiyo ikidhihirishwa!

Mnamo mwaka 1968 vuguvugu la Roho Mtakatifu liliwagusa vijana waliokuwa watu wazima katika kanisa la Shawnee, Kansas. Mwalimu wa shule ya umma aitwaye Kathy alimwambia mwalimu Mike habari za Kristo. Mike na mke wake, Linda, walilitembelea lile kanisa. Mchungaji Melvin na mkewe, Jeanie, walikwenda kwenye nyumba yao. Wakawahubiria injili, na wote wawili wakampokea Kristo. Baada ya kwenda kanisani mara kadhaa na kusoma Biblia, Mike aliimwaga pombe yake chini na akasema, "Sidhani Mkristo anapswa kunywa pombe." Siku ya Jumapili ya Mitende iliyofuata, watu ishirini na wanane walibatizwa, wengi wao walikuwa vijana

17. *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (March 2014).

watu wazima. Baada ya muda mfupi Mike alimwambia mchungaji wake, “Ninaamini Mungu ananiongoza kuingia kwenye huduma.”

Haikuchukua muda mrefu, Mike alijiunga na chuo cha Biblia ili ajiandae. Wakati alipokuwa katika darasa la uinjilisti, alipewa kazi ya kuwasiliana na mtu au familia ambayo haijawahi kwenda kanisani, Mike alikwenda mitaani na kuongea na Jan kwenye ngazi ya mbele ya nyumba yake. Curt na Jan walikuwa wamehama kutoka Indiana siku kumi zilizopita. Kwao, Aprili 1972 ilimaanisha si tu makazi mapya lakini pia juhudi za kuyajenga maisha yao upya. Watoto wao wa kiume, Scott na Chip, walikuwa na umri wa mwaka mmoja na mwingine miaka mitatu tu.

Jumapili hiyo asubuhi, walikuwa katika kanisa la Shawnee, na mkutano wa uvuvio ulikuwa unaendelea. Basi mwinjilisti alipokuwa akihubiri, Curt alihisi mguso, akalia, na kujitokeza mbele kuombewa, akatubu, na kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana. Jan awali alikuwa ameomba ili ampokee Kristo wiki chache zilizopita huko Indiana lakini hakuwa anajua nini kingine cha kufanya. Sasa Curt na Jan walikuwa kwenye ukurusa mmoja. Usiku huo, Curt aliuambia ule umati wa ibada ya Jumapili jioni upatao watu takriban mia tatu kile Kristo alichokuwa amemtendea asubuhi hiyo.

Siku tano baadaye, mchungaji aliwatembelea Curt na Jan nyumbani kwao na kuwaingiza kwenye mafundisho ya *Basic Bible Studies for New and Growing Christians*. Curt na Jan walikua kiroho. Curt alikombolewa kutoka kwenye matumizi ya tumbaku na pombe mara hiyohiyo. Baada ya muda mfupi walianza kutoa zaka. Kile mafundisho ya Biblia yalisema, walikifanya. Kama meneja wa Kmart, Curt alipewa duka lingine karibu kila mwaka, na kila mwaka walihama. Kila mahali walipata makanisa mazuri, viongozi wazuri wa watoto, viongozi wazuri wa vijana, na wachungaji wazuri. Curt na Jan waliwafundisha watoto wao kuwa wanafunzi, na kanisa liliifanya familia nzima kuwa wanafunzi. Katika kuhama kwao, kanisa wakati wote lilikuwa ndiyo kambi yao ya kirafiki.

Scott alipofikisha umri wa miaka mitatu na nusu, alioongozwa na mama na baba yake kumpokea Kristo nyumbani kwao. Alipofika gredi ya sita shuleni, Scott alishuhudia nguvu kuu za Roho zikimtakasa kabisa. Baada ya kumaliza masomo chuoni, Scott alihisi Mungu akimwita kuacha taaluma yake ya matibabu na kuanza kufanya huduma. Baada ya kufuzu mnamo mwaka 1993, alimwoa Jenni, na wakaanza kazi za huduma huko Fort Wayne, Indiana. Nilimpigia simu Scott, na kumwalika kwenda chuo cha Biblia, nikampa ufadhili wa kusomea uinjilisti, na kumwomba anifanyie kazi fulani katika kanisa la Kansas City. Kutokana na mafundisho yake ya uinjilisti, tuliwaona watu wengi wakimpokea Kristo.

Baada ya kutoka chuo cha Biblia, Scott alirudi Fort Wayne kama mchungaji wa uinjilisti. Baada ya muda mfupi, aliitwa kuwa mchungaji mkuu katika kanisa moja Houston ambalo lilinawiri sana chini ya uongozi wake. Ndani ya miaka minane na nusu, washirika waliongezeka kutoka watu mia nne hadi watu mia saba, wakajenga jengo jipya, wakapanda kanisa, na zaidi. Katikati ya kukua huko kwa kanisa, Mungu aliwakatiza na kuiita familia ya Scott wawe wamisionari. Mnamo mwaka 2012, Scott, Jenni, na binti zao, Bekah na Sarah, walifika Kiev, Ukraine, na mnamo mwaka 2015, Scott alitawazwa na dhehebu lake kama mratibu wa mikakati wa uwandani wa Jumuiya ya Madola ya Mataifa Huru. Scott alisimamia mafundisho ya wachungaji, uanafunzi, na uinjilisti kwa mataifa kumi na mawili ya Ulaya na Asia. Mwaka 2018, Scott alichaguliwa kuwa mkurugenzi wa kimataifa wa shule ya Jumapili na uanafunzi. Sasa, ushawishi wake unaenea katika makanisa yote ya dhehebu lake duniani kote.

Kuanzia mwak 1968 hadi 2020. Kutoka kwa Kathy, hadi kwa Mike, hadi kwa Linda, akisaidiwa na Kasisi McCullough. Kwa Curt na Jan. Hadi kwa Scott na Chip (ambao wote sasa wako katika huduma). Kwa wachungaji na waumini wapya huko Ukraine, Urusi, Armenia, na ulimwenguni: “Nyingine zikaanguka penye udongo ulio mzuri zikazaa—moja mia, moja sitini, moja thelathini” (Mathayo 13:8). Kuwaandaa Wanafunzi Wanaowafanya wengine kuwa Wanafunzi.

**FEBRUARI 8** **39**

# Kupanda Kumpendeza Roho

*Yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele.*
*Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna*
*kwa wakati wake, tusipozimia roho.*
*Wagalatia 6:8–9*

“Habari, mkuu,” baruapepe ilianza namna hiyo. Ujumbe uliendelea hivi: “Jina langu ni Joe Kumor. Nimeshiriki leo katika bodi yangu ya kuweka wakfu huko Hastings, Nebraska. Natumai nitakuwa kasisi wa jeshi. Mchungaji, Kasisi John Whitsett, aliniuliza ikiwa ninawajua Frank na Peggy Kumor. Hao ni wazazi wangu, ingawa mama yangu aliaga dunia miaka kadhaa iliyopita. Aliniona ni jambo la ajabu sana kwamba alikumbuka darasa la uinjilisti

ulilofundisha yapata miaka thelathini na tano iliyopita lililotaja wazazi wangu na sasa alikuwa anamsaili mtoto wao katika bodi ya kuweka wakfu."

Je, ninawakumbuka Frank na Peggy Kumor kweli! Mnamo mwaka 1975, walitembelea lile kanisa nililohudumu kama mchungaji wa uinjilisti. Walikuwa wazi na wacheshi sana kiasi kwamba niliwauliza ikiwa tunaweza kuwatembelea zaidi na kusikia habari zao na imani za kanisa letu. Wakasema ni sawa, hivyo ndivyo walivyotaka!

Alhamisi hiyo usiku, washirika wawili wa kawaida waliandamana nami kuwatembelea kina Kumor nyumbani kwao. Roho Mtakatifu alifungua milango na mioyo yao na ilipofika saa 5:00 usiku, mwezi Februari 13, 1975, Frank na Peggy walimpokea Yesu mioyoni mwao na maishani mwao kama Mwokozi na Bwana (Ufunuo 3:20). Kufikia usiku uliofuata, walikuwa wote wamekamilisha mafundisho ya *Basic Bible Studies for New and Growing Christians*. Ilikuwa ajabu sana—hawakuwa wamewahi kujifunza Biblia kwa njia hii. Wiki nane baada ya kumpokea Kristo, walimaliza mafundisho yote vizuri. Ukuaji wao wa kiroho ulikuwa wa haraka na wenye nguvu—waliweza kushinda matumizi ya tumbaku, walianza kutoa zaka kwa furaha, na wakajiunga na kanisa kwa kuikiri imani. Peggy alianza kuandika kweli nzuri sana za kiroho. Wiki tatu baada ya kuokoka, aliandika maneno haya, "Februari 13, saa 5:00 usiku., nilifurahi kuliko nilivyowahi kufurahi mbeleni. Ninaamini kile kilichozidisha furaha ni kule kujua kwamba furaha hii maalum haina mwisho. Kujua kwamba Yesu amenipa mahali mbinguni hunipa furaha ya kila siku."

Baada ya muda mfupi Frank alimaliza mafunzo yake ya ufundi wa saa huko Kansas City. Baadaye, walihamia tena kule kwao Nebraska. Frank alianza kufanya kazi katika duka la vito, na wakawa viongozi kanisani kwao. Frank hatimaye alikuwa mmiliki wa hilo duka, na wakajaliwa watoto saba.

Mwaka 1996 niliwasiliana na akina Kumor nilipokuwa nikihubiri katika kanisa la Omaha. Peggy alikuwa amepigana na saratani, na muda mfupi baadaye, alikumbana na vita vingine. Aliniambia kwamba alifurahi sana aliweza kuwafundisha watoto wake juu ya uzima wa milele. Baada ya muda mfupi, Peggy angesimama katika uwepo wa Bwana.

Muda ulipita, na mnamo mwaka 2015, nilipokea baruapepe ya Kumor, ilinibidi nimpigie ili nijue hali ya familia yake. Niligundua mambo kadhaa ya ajabu. Joe ni mchungaji msaidizi katika kanisa. Frank, sasa amemuoa Pat na bado anamiliki lile duka la vito, na anahudumu kanisani. Mmoja wa ndugu wa kiume wa Joe, ni daktari jeshini, alihudumu kwa kipindi kifupi katika hospitali ya kimisheni huko Papua New Guinea. Six of the kwa watoto are active kanisani.

Niliposikia haya yote, nilimsifu Mungu tu. Bila shaka neema ya Mungu ilikuwa kila mahali katika familia hii, na walikuwa wanaenda katika neema hiyo. Ni jambo la kutia moyo sana kwamba kile kilichopandwa mwaka 1975 kilileta mavuno kama hayo miaka arobaini baadaye. Natupande sasa—na, tutavuna kwa wakati wake.

**FEBRUARI 9** **40**

# Mpira wa Theluji!

*Yesu akawajibu, Amin, amin, nawaambia, Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi.*
*Yohana 8:34*

Kwa mtoto aitwaye Jacob, theluji iliyo kandoni mwa mlima ilikuwa mwaliko wa kutoka na kwenda kucheza. Aliamua kuumba mpira mkubwa zaidi wa theluji aliowahi kuumba. Aliikusanya pamoja ile theluji kwa mikono yake, na mpira wake wa theluji ulipokuwa na ukubwa ufaao, aliuweka chini na akaanza kuubingirisha. Kadiri alivyoubingirisha mbali, ndivyo ulivyozidi kuwa mkubwa. Punde si punde, ule mpira wa theluji ukawa mzito kiasi kwamba ilikuwa vigumu kuubingirisha. Jacob alikumbuka kwamba, badala ya kuubingirisha *hapo* kandoni mwa mlima, kuubingirisha *kwenda chini* ya mlima ingekuwa rahisi. Alipokuwa akiubingirisha chini, ule mpira wa theluji ulianza kubingirika wenyewe na kuanza kushika kasi. Ilibidi akimbie mbio kuufikia. Kisha akajikwaa na mwili wake huo mdogo ukaanguka chini mbele ya mpira wa theluji uliokuwa ukibingirika. Katika mzunguko mmoja, theluji safi ilimfunika. Kabla hajaweza kujinasua, ule mpira wa theluji ulibingirika tena, na akafunikwa na rusu nyingine ya theluji. Haraka na haraka, rusu baada ya rusu. Jacob alinaswa kabisa. Ule mpira wa theluji uliomfungia Jacob ulibingirika chini ya mlima hadi kwenye mawe huko chini. Uligonga yale mawe, na Jacob akauawa. Mchezo wake ulianza bila shida yoyote. Lakini uamuzi mmoja wa kuubingirisha mpira wa theluji *chini* ya mlima ulimpeleka Jacob mahali ambapo hakunuia kwenda.

Dhambi ndivyo ilivyo—itakupeleka mahali ambapo hukunuia kwenda. Hebu fikiria kile hutokea unapodanganya kisha uhojiwe juu yake: inakubidi useme uongo mwingine kuufunika ule wa kwanza. Ndiposa Yesu alisema dhambi itakufanya uwe *mtumwa* wake. Nilipofikiria juu ya maisha yangu

ya zamani, nilikuwa sina budi kukubali kwamba, “Dhambi ilinitawala; Sikuitawala.”

Na je, matokeo ya utumwa huu wa dhambi ni nini? Warumi 6:23 inatuambia, “Mshahara wa dhambi ni mauti”—kama Yakobo chini ya mlima. Kama dhambi ina nguvu jinsi hiyo, tunaweza kufanya nini? Nguvu kubwa zaidi zinahitajika. Jibu la pekee ni kuja kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliyesema, “Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli” (Yohana 8:36).

**FEBRUARI 10** **41**

# Ufalme wako Uje

*Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa mhuri hata siku ya ukombozi.*
*Waefeso 4:30*

*Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele.*
*Ufunuo 11:15*

*Ufalme wako uje.*
*Luka 11:2b*

Mwaka 2020 ulikuwa mwaka wa matatizo nchini Marekani. Janga la korona lilivamia nchi (kama lilivyofanya katika nchi nyingine nyingi), lakini juu ya hayo, kule kufungiwa kwenda mahali na kujitenga kulizidisha matatizo ya wale wanaopambana na uraibu na matatizo ya kiakili. Wamarekani wengi walikosa subira na wakakaidi kanuni zilizopendekezwa na serikali. Mivutano ya ubaguzi wa rangi pia iliongezeka kwa kuuawa kusikokuwa kwa haki kwa mwanaume mweusi huko Minneapolis. Wamarekani wa kila tabaka waliungana katika kutafuta haki, lakini umoja na maandamano ya amani yalididimizwa na vurugu na wizi kila mahali nchini.

Nilisumbuka, nikawa na huzuni, na nikaomba. Mafundisho ya Ukristo yalikuwa na ushawishi hapo awali nchini Marekani. Baada ya miaka mingi, kudorora kwa maadili haya kunaonekana wazi. Maadili binafsi na tabia zilizidi kuwa chafu. Watu wamemhuzunisha Roho Mtakatifu, ambaye ameleta ushawishi wake sana katika taifa letu. Inasemekana kwamba neno

“kuhuzunisha” ni neno la upendo. Tunapomhuzunisha Roho, yeye huondoka. Mungu aliyehuzunishwa anapoondoa mikono yake, uozo na kudorora kwa jamii yetu huingia. Ni kana kwamba Mungu anasema, “Sawa, fanya vile unavyotaka, na uone jinsi maisha yalivyo wakati nimeachwa nje.”

Hatimaye, tutatambua suluhisho letu pekee ni Bwana. Si ajabu sauti za mbinguni zilikuwa za juu: “Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele.” Na wale wazee ishirini na wanne wa mbinguni wanajibu kwa kusema, “umeutwaa uweza wako ulio mkuu, na kumiliki. Mataifa walikasirika, hasira yako nayo ikaja” (Ufunuo 11:17–18). Wakristo bado wanaomba na kusema, “Ufalme wako uje.”

**FEBRUARI 11** **42**

# Alikuwa Shahidi

*Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na kote katika Yudea, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*
*Matendo 1:8*

Hakumaliza gredi ya sita. Umaskini na mahitaji aliyowekewa kama mtoto mkubwa katika familia yalimfanya atafute kazi haraka kadiri iwezekanavyo. Mafundisho yake ya kina ya kanisani yalipuuziliwa mbali alipokuwa huko nje duniani, akiwa ameolewa na kulea watoto.

Katika umri wake uliokuwa unakaribia miaka hamsini, Yesu alikuja kumtembelea Vera tena. Katika ibada ya uvuvio, alipiga magoti, akaomba, akaungama, na kumpokea Mwokozi. Baada ya ibada, Vera alikubali kwamba alikuwa akifikiria kuyatamatisha maisha yake. Sasa mzigo wake wa hatia uliondolewa. Yesu alikuwa hakuiokoa nafsi yake tu, bali alikuwa pia ameyaokoka maisha yake.

Alikua kiroho, akapata ushindi dhidi ya uraibu wake wa tumbaku na pombe, na akahudumu kanisani. Aligundua kwamba anaweza kuwa na uhusiano wa dhati na Mungu. Baada ya muda mfupi, huku akiwa amejisalimisha kikamilifu, Vera alishuhudia kazi ya utakaso na kazi ya Roho Mtakatifu inayowezesha.

Akajisemea, *Familia inahitaji kusikia juu ya haya*. Kwa hiyo Vera aliendesha gari kutoka nyumbani kwake Florida hadi kaskazini mwa New York. Aliwatembelea ndugu zake, wapwa zake wa kike na wa kiume, kadiri alivyoweza.

Dadake Mary hakuwa akienda kanisani sana vile, lakini Vera alishiriki imani yake na kumshawishi Mary kwenda pamoja kwenye ibada huko Watertown. Na Mary alimpokea Kristo! Akaanza kwenda kanisani mara kwa mara na akakua kiroho.

Mary na marafiki zake wapya kutoka kanisani walioishi LaFargeville waliona mwendo wa maili ishirini na tano kwa gari kwenda kanisani Watertown kuwa mgumu hususan katika wakati wa theluji ya kina cha futi tatu. Waliwaza, *Kwa nini tusianzishe kanisa la Holiness katika mji mdogo wa LaFargeville?* Kwa hiyo wakafanya hivyo!

Kadiri miaka ilivyosonga, Mary aliendelea kuwashuhudia kwa dhati wapwa zake wa kike na wa kiume. Alipokuwa na umri wa miaka themanini na saba, moyo wake ulianza kudhoofika, na alikuwa anakaribia mwisho. Jamaa zake walikusanyika karibu naye.

Mpwa wake alisikia juu ya hali yake na akapiga simu kutoka umbali wa maili elfu moja. Aliongea na Mary kwa kifupi—alikuwa mdhaifu sana. Alisema, "Kuna jua huku, lakini afadhali huko."

Asubuhi iliyofuata, yule mpwa alipiga simu tena, na familia ikasema alikuwa ameaga dunia asubuhi hiyo. "Je, alisema kitu chochote kingine?" akauliza.

Wakasema, "Ndiyo, usiku mzima alilala kwenye mto akiwa mdhaifu sana. Ghafla asubuhi ya leo, aliketi, akainua mikono yake juu ya kichwa chake na kusema, 'Oh, oh, wamenizunguka. Malaika, wamenizunguka.' Kisha akalala chini juu ya mto wake na akaaga dunia."

Kwa nguvu za Roho, Vera alikuwa shahidi. Kwa nguvu za Roho, Mary alikuwa shahidi. Naijua hadithi hiyo vizuri. Vera alikuwa mama yangu; Mary alikuwa shangazi yangu.

FEBRUARI 12 **43**

# Watu Watatu au Wanne Waliojazwa Roho

*Ikawa, watu wote walipokwisha kubatizwa, na Yesu naye amebatizwa. Naye anaomba, mbingu zilifunuka; Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua. Sauti ikatoka mbinguni: "Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe."*
*Luka 3:21–22*

Alikuwa ni Yesu, Mungu katika mwili, na bado Roho Mtakatifu akamshukia. Na Maandiko yanatuambia zaidi juu ya Roho katika maisha ya Yesu:

- Luka 4:1—"Yesu, *akiwa amejaa Roho Mtakatifu*, alirudi kutoka Yordani."
- Luka 4:1—"Kisha Yesu*alipandishwa na Roho* nyikani."
- Luke 4:13—"Na Yesu, akiwa *amejaa Roho Mtakatifu*, alirudi kutoka Yordani."
- Luka 4:18—"The *Roho wa Bwana yu juu yangu*,Kwa maana *amenitia mafuta* kuwahubiria maskini Habari Njema."

Kama Yesu alihitaji kujazwa Roho, vipi kuhusu wafuasi wake? Siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu aliwashukia wafuasi 120 wa Yesu waliokuwa wakiomba. Matendo 2:4 inatuambia, "Wote wakajazwa Roho Mtakatifu," na kuleta uamsho mkubwa wa kiroho ulioenea Yerusalemu yote.

Miaka mitano baadaye, kukatokea tatizo kanisani juu ya ugawaji wa chakula kwa wajane. Wale mitume, walitaka kusaidiwa kulitatua tatizo hili, basi waliomba kanisa liwateue viongozi wa kawaida wasimamie mradi huu. Tambua sifa walizopaswa kuwa nazo viongozi hawa: "Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, *wenye kujawa na Roho*, na hekima" (6:3). Wakristo pekee waliozaliwa kwa Roho, *waliojulikana kujazwa na Roho*, ndio walioweza kuchaguliwa.

Nini kilichofuata? Matendo 6:5 inatuambia, "wakamchagua Stefano, mtu *aliyejaa* imani na *Roho Mtakatifu*." Stefano aliposimama na kuongea kwa ujasiri kwa ajili ya Kristo, kundi la watu lilimshambulia na hatimaye wakamuua. Na bado Stefano aliweza kukabiliana na dhuluma hii kwa nguvu na upendo wa ajabu. Inawezekanaje? Matendo 7:55 inatuambia, "Lakini yeye *akijaa Roho Mtakatifu*, akakaza macho yake, akitazama mbinguni, akauona utukufu wa Mungu, na Yesu akisimama upande wa mkono wa kulia wa Mungu." Stefano

alikuwa amejaa upendo na msamaha sana hivi kwamba muda mfupi kabla akate roho, aliomba hivi, "Bwana, usiwahesabie dhambi hii" (kif. 60).

Wakristo wengi leo wanatambua hitaji la kuwa na uhusiano wa dhati na Mungu kupita uhusiano wao wa sasa na Kristo. Wanatamani kumfanyia Mungu kazi zaidi, lakini hawana nguvu za kufanya hivyo wenyewe. Wanajua wamezaliwa kwa Roho (Yohana 3:5), lakini sasa wanahitaji kujazwa Roho.

Sherwood Wirt, mhariri mstaafu wa jarida la *Decision* la shirika la Billy Graham, alitambua kwamba maisha yake ya Kikristo yalijaa misukosuko ya ndani—hususan hisia za uchungu na kisasi na kukosa upendo. Katika Isaya 61:1, 3, alisoma, "Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu...kuwaagizia hao waliao katika Sayuni, wapewe taji la maua badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito" Alimngojea Bwana, na kisha baadaye akatoa ushuhuda:

> Nilikuwa nimekiachilia kiti cha enzi cha maisha yangu (yaani, maisha yangu ya Kikristo) . . . Nilipomwomba anisulubishe, alikubali kauli yangu na kutimiza ombi langu. Kwa wakati wake na kwa raha zake, alituma kiyeyusho cha kiungu katika moyo huu uliosumbuka . . . Sijui jinsi Upendo ulivyoingia, lakini ninajua kwamba uchungu wote niliokuwa nao dhidi ya wengine—ikiwa ni pamoja na wale waliokuwa karibu nami—ulipotea. Kisasi—ukatili—hisia za kuumia—na kadhalika. Yote yalipotea. Yaliyeyuka. Yalienda.[18]

Upendo ndio ulikuwa mada ya Sherwood Wirt. Na si ajabu! Warumi 5:5 inasema, "Na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi."

Yesu, Stefano, Sherwood Wirt—wote walijaa Roho Mtakatifu. Je, jina lako linapaswa kuongezwa kwenye orodha hiyo?

---

18. Sherwood Eliot Wirt, *Afterglow: The Excitement of Being Filled with the Spirit* (Grand Rapids: Zondervan, 1976), 17–19.

# Uhusiano wa Upendo

*Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye.*
*naye anipendaye atapendwa na Baba yangu;*
*nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.*
*Yohana 14:21*

Mimi na Jared tulikutana Maryland wakati wa mkutano wa uvuvio kanisani na tukawa na gumzo zuri sana. Huko, alisimulia hadithi ya safari yake ya kiroho:

*Nililelewa kanisani. Nilikuwa nikiishi maisha yaliyoonekana kuwa ya Kikristo kwa watu wa nje, lakini ndani yangu, nilikuwa vuguvugu. Nilikuwa na uhusiano na Kristo, lakini si uhusiano wa upendo. Sikumwona baba yangu akisoma Biblia, na hakuonesha hisia katika imani yake. Kisha, miaka minne iliyopita, alitakaswa. Aliinyoosha mikono yote miwili hewani na akaanza kuimba. Siwezi kuamini jinsi maisha yake yalivyobadilika. Sasa, kila asubuhi huwa anasoma Biblia yake na kuandika kwenye daftari lake. Uhusiano wake na mke wake na watoto ulibadilika na kuwa mzuri sana. Akawa kiongozi wa kiroho.*

Muda mfupi baadaye, Jared alikuwa akitembea kando ya barabara. Jared anaendelea na ushuhuda wake:

*Mungu alinena waziwazi, "Je, haya ndiyo yote utakayonipa?" Nilikuwa mchoyo na watu wangu, na sikumpa kipaumbele Mungu. Hili lilinigusa sana.*

*Nikamjibu Mungu nikasema, "Mimi ni wako. Fanye kile unachotaka nami." Hicho ndicho kitu cha kutisha zaidi nilichowahi kusema.*

*Nilihisi naitwa katika huduma. Basi nilikwenda nyumbani kumwambia mke wangu. Nilikuwa ninalia machozi sana! Akaniuliza akisema, "Una shida gani?"*

*Nikasema, "Mpenzi, ninaogopa sana. Naogopa Mungu atatuta hapa."*

*Akasema, "Jared, ulinioa, na ninamtumikia Mungu yule yule unayemtumikia. Tuko pamoja. Ninamwamini, na ninakuamini."*

*Nilitakaswa katika mkutano wa uvuvio mwaka mmoja uliopita. Mungu alianza kupogoa mambo fulani kwangu. Waebrania 12:1 inatuambia "na tuweke kando kila mzigo mzito." Aliniondolea vipindi kadhaa vya TV na*

*chochote kile kilichokuwa kinanizuia kuwa karibu na Bwana. Nilikuwa vile vyote nilivyohitaji kuwa.*

Jared alitumika katika huduma ya vijana. Ushuhuda wake unaendelea:

*Ule mpango wa vijana ulikuwa na kufikia zaidi ya vijana thelathini. Baadhi ya vijana waliwaka moto. Mungu alinipa amani moyoni mwangu. Mungu anapokuongeza utafanikiwa. Ninapoongea, ninaweza kujua wakati Mungu ananena nami. Hii ndiyo maana ya kujazwa Roho.*

*Ni jambo la kuridhisha. Maombi mengi yamejibiwa wiki tangu siku ya Jumapili. Ninajua hivyo kwa sababu nimemwacha Mungu atawale.*

Kama unavyoona, Jared ameingia katika uhusiano wa upendo na Yesu. Maneno ya Yesu katika Yohana 14:21 ni sehemu ya ahadi yake ya kumtuma Roho Mtakatifu kwa wanafunzi wake (kif.15-21). Fursa iliyoje kwamba uhusiano huo wa upendo unapatikana kwetu leo.

**FEBRUARI 14** **45**

# Kutakaswa na Roho Mtakatifu

*Niifanyie Injili ya Mungu kazi ya ukuhani,*
*kusudi Mataifa wawe sadaka yenye kibali,*
*ikiisha kutakaswa na Roho Mtakatifu.*
*Warumi 15:16*

Watu wengine walimchekelea Jeff na Melissa kwa kuhudhuria mkutano wa mafundisho ya Biblia juu ya Roho Mtakatifu siku ya Ijumaa usiku. Watu walisema walikuwa watoto sana, kiasi kwamba wanapaswa kuwa nje ya mji wakifanya mambo ya kufurahisha.

Hata hivyo, Melissa anasema, "Mimi na Jeff tumekuwa na nyakati za kufurahisha sana kwa *Living in the Power of the Spirit*." Kisha anaendelea kusema:

*Nimejifunza maana ya kutakaswa kabisa na kujazwa Roho . . . Nimejifunza jinsi asili yangu ya ubinafsi inavyoyatawala maisha yangu na jinsi ya kujikana nafsi na kumwacha Roho aniongoze na kunitawala . . . Nimeweza kuwasamehe kabisa marafiki zangu walioniumiza hapa zamani na kuweza kurekebisha mahusiano hayo yaliyovunjika. Nimeweza kuanzisha utaratibu mpya wa kila siku wa kutumia muda katika Neno na katika maombi . . . Nimeuona mwongozo wa Roho katika kufanya maamuzi*

*muhimu ya shule na ya kitaaluma. Na nimeona jinsi kuishi katika nguvu za Roho kunavyoweza kuyatajirisha maisha ya mtu . . . kwa sababu hayo ndiyo yaliyotokea kwangu.*

Hata leo, haya ni kweli katika huduma ya Paulo—Jeff na Melissa ni "dhabihu inayokubalika kwa Mungu, na kutakaswa na Roho Mtakatifu."[19]

**FEBRUARI 15** **46**

# Pasipo Kunung'unika

*Yatendeni mambo yote pasipo manung'uniko wala mashindano, "mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi kilichopotoka;." ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu, mkishika neno la uzima.*
*Wafilipi 2:14-16*

"Kazini nalalamika wakati wote," alisema kwa ghafla. Elgin alikuwa sehemu ya kundi zito la uanafunzi lililokuwa linatumia wiki kumi na mbili kujifunza kazi ya Roho Mtakatifu. Alikuwa amefanya kazi kwa miaka mingi katika kampuni ya Kikristo ya uchapishaji. Alishangaa na kuaibika alipotambua jinsi alivyokuwa akilalamika.

Kwa kiasi kikubwa, Elgin aliishi maisha ya Kikristo ya kujitolea, na alisoma Biblia yake. Lakini pengine kwa mara ya kwanza, kifungu hiki kilivuta usikivu wake. Alikuwa katika kundi hili la uanafunzi kwa ajili ya ukuaji wake wa kiroho, kwa hiyo aliazimia kubadilisha mazoea yake ya kulalamika. Kufikia wiki ya kumi na mbili ya mafundisho, alikuwa anatoa ripoti na kufurahia kwamba aliweza kukaa siku nzima pasipo kulalamika.

Rafiki yangu ilimbidi aende kwenye nyumba kitalu iliyokuwa chini ya nyumba yake kuchukua mimea na kuileta juu. Basi pale kwenye mtaro wa sakafu, alipata kidimbwi cha maji. Alijua kulikuwa na tatizo la maji taka kukwama na kurudi ndani mara kwa mara, lakini ilikuwa imepita miezi minane tangu yeye na majirani zake walipomwita fundi bomba kuja kusafisha mabomba. Alikuwa anapitia changamoto kadhaa hivi karibuni, ikiwa ni

19. Imetolewa kutoka Taken *Reflecting God* June–July–August 2010 (Kansas City, MO: *WordAction* Publishing Co.), 12. Imetumiwa kwa ruhusa.

pamoja na changamoto za kifedha, mabadiliko makubwa katika hali yake ya kazi, na ukarabati mwingine wa nyumba uliohitaji kushughulikiwa.

"Oh Bwana, kweli!" akasema kwa mshangao. "Sihitaji tatizo lingine. Nitavunjika."

Lakini Bwana alimkatiza: "Baba yako amepiga simu sasa hivi. Anakutumia cheki. Kwa hiyo hili nimelishughulikia Huna haja ya kulalamika."

Papo hapo, mtazamo wake ulibadilika. "Ndiyo. Asanteni, Bwana," akapumua.

Ule ukarabati wa bomba ulikuwa ufanyike siku ya Jumapili Ile cheki ilifika siku ya Jumatatu, lakini saa kumi na nusu alasiri badala ya ule muda wake wa kawaida wa saa sita. Licha ya kuchelewa huko, alipompigia yule fundi bomba, alisema angefika baada ya nusu sasa. Basi yule fundi alisafisha ule uchafu, na baada ya kumlipa $79, alibaki na $121.

Watu hawa wawili walibadilika kutoka kuwa watu wa kulalamika na kunung'unika hadi kuwa nyota zing'aazo. Vivyo hivyo, Wakristo wenye mioyo safi, iliyojazwa Roho sharti walione kuwa jambo la kawaida kufurahi na kung'aa. Hili hutuma ujumbe kwa kila mtu tunapofanya hivyo!

**FEBRUARI 16** **47**

# Chakula Usichokijua

*Yesu alisema, "Chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yale aliyenituma nikaimalize kazi yake."*
*Yohana 4:34*

Mnamo Novemba tarehe 20, mwaka 1995, saa tatu za usiku, Yesu Kristo aliingia moyoni mwangu. Nilifurahi sana kuwa naye kama mgeni kiasi kwamba nilimwalika atembelee sehemu zote za moyo wangu, makazi yake mapya.

Tulikaa mezani pamoja katika chumba cha kulia chakula—chumba cha hamu na shauku. Bwana Yesu hakugusa kile chakula kilichowekwa mbele yake, ambacho bado kilikuwa na ladha ya ulimwengu ndani yake.

Nilipomuuliza kwa nini hakukigusa kile chakula chake, aligeuka, na kunitazama moja kwa moja machoni, na akasema, "Mimi ninacho chakula msichokijua ninyi . . . . Chakula changu . . . niyatende mapenzi yale aliyenituma" (kif. 32, 34).

Hapo hapo ndani ya meza ya moyo wangu, alinionjesha utamu wa maana ya kutenda mapenzi ya Mungu. Tangu wakati huo, nimeona kila kitu chochote kingine kuwa hakiridhishi.[20]

**FEBRUARI 17** **48**

# Upendo Mkuu

*Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.*
*Waefeso 3:17-19*

Je, unaweza kumudu upendo wa kiasi gani? Mwingi, kusema kweli. Paulo anawaombea Waefeso na sisi mambo yafuatayo:

- Wawe na shina na msingi katika upendo
- Wafahamu upana wote wa upendo wa Kristo
- Waujue upendo upitao ufahamu

Unapotambua upana wa upendo wa Kristo—upendo ulio wa kina kiasi kwamba alikwenda msalabani kufa kwa ajili ya dhambi zetu—unaweza kuwa na shaka kwamba unaweza kupenda jinsi hiyo. Na bado Paulo anatuonesha kwa kiasi kikubwa hakikisho kwamba Mungu ana nguvu za kutuleta kwenye upendo wa aina hiyo.

Anasema kwamba Mungu ana “utajiri wa utukufu wake” ambao kutokana nao anaweza kutoa ili atutie nguvu kwa Roho wake katika utu wetu wa ndani (Waefeso 3:16). Anaomba kwamba Kristo akae mioyoni na ajihisi kuwa nyumbani (kif. 17). Ni fursa yetu “utimilike kwa utimilifu wote wa Mungu” (kif. 19). Na ikiwa bado unafikiria hili ni agizo kubwa sana, Paulo anamalizia kwa kutuambia kwamba Mungu anaweza “zaidi ya yote tuyaombayo au tuyawazayo” (kif.20).

Inasaidia ikiwa tunaweza kumwona mwanadamu wa sasa akiishi na upendo wa aina hiyo. Nimebarikiwa kwa sababu nimewaona. Katika

20. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Machi–Aprili–Mei 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 35. Imetumiwa kwa ruhusa. (Chapisho hili liligeuka kuwa*Reflecting God*.)

kongamano huko Manila, Philippines, nilikutana na mtu kama huyo—Carl, mmishenari alikwenda Smoky Mountain. Jiji la Manila lilikuwa limegubikwa na kiwango kikubwa cha taka walizozalisha hadi wakaanza kuzitupa katika Mto Pasig. Baada ya muda mfupi, pale mahali palikuwa mlima wa taka, kwa hiyo maafisa wa jiji wakazitia moto zile taka kupunguza ukubwa wake. Taka haziteketei vizuri, lakini zinatoa moshi mwingi—hivyo, pale mahali palikuja kujulikana kama Smoky Mountain.

Watu elfu ishirini walio maskini hohehahe walifurika mlimani kutafuta mahali pa kuishi. Walijenga vibanda vya karatasi ngumu, mbao nyembamba, au mikebe iliyotupwa. Sakafu zao zilikuwa chafu, na ilibidi watembee mwendo wa robo maili kutafuta maji kutoka kwenye bomba la jumuiya.

Carl alisisimka juu ya yale Bwana alikuwa anafanya katika kazi ya huduma aliyopewa. Alituambia alikuwa na wanaume kumi waliokuwa wamekuwa wafuasi wa Kristo. Walikuwa wamebadilishwa: walipata ushindi dhidi ya tumbaku, pombe, na kamari; walikuwa wanawatendea wake zao kwa upendo na ukarimu; Carl alikuwa anawasaidia kujenga familia bora zaidi. Aliwapenda hawa wanafunzi kumi.

Tulipomuuliza Carl kile alipanga kufanya baada ya hapo, alifurahi. Baada ya muda mfupi alikwenda kwa ajili ya likizo ndefu kwao Sweden, ambapo aliweza kuwaona jamaa zake.

Kisha? Kwa msisimko mkubwa, alisema, "Oh, natamani sana kurudi Smoky Mountain!" Siku hiyo, katika mwanadamu halisi anayeishi, niliuona upendo kama ule wa Kristo—upendo unaovuka mipaka.

**FEBRUARI 18** **49**

# Kuletwa Mbele Zake Watakatifu

*Katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake,*
*ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu,*
*wasio na mawaa wala lawama.*
*Wakolosai 1:22*

Kama ningalikuwa nitaletwa mbele za Mungu, ningevalia mavazi yangu mazuri zaidi. Lakini bado kwa kiasi fulani, sidhani ataenda kuangalia mambo hayo. Nimekuwa nikiishi katika ufalme kwa miaka sasa na nimeona kasoro nyingi. Nimeyaweka katika ubongo wangu.

Kuna njia ya msamaha nyumbani kwetu, njia iliyochakaa. Wakati mwingine ni afadhali nisiitumie kwa sababu ni rahisi "kuwatendea wengine kama wanavyonitendea." Si rahisi kuchagua upendo, lakini kunafanya kazi. Si rahisi kuitikia badala ya kukasirika, lakini kunafanya kazi. Si rahisi kukabiliana na tatizo linalohitaji suluhisho wakati napendelea kutokabiliana nalo, lakini inafanya kazi. Si rahisi kuachilia mambo, lakini inafanya kazi.

Mungu lazima aangalie na asione mawaa yoyote, kama vile nilivyomtazama kila mmoja wa watoto watu watatu wachanga na nikasema, "Ni wakamilifu." Kwa sababu ya karama ya Mungu kwangu, nimepatanishwa. Kile kilichovunjika kimekarabatiwa. Kile kilichotenganishwa kimeletwa pamoja. Kile kilichokuwa hakiko sasa kiko. Inafanya kazi!

Nancy Shaver[21]

**FEBRUARI 19** **50**

# Ulikuwa Peke Yako

*Na mlishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu; tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane ninyi— kwa kadiri muonavyo siku ile kuwa inakaribia.*
*Waebrania 10:23-25*

"Tunahitajiana" kilikuwa kirai maarufu cha Reuben Welch kinachonukuliwa mara kwa mara. Mwandishi wa Waebrania aliamini hilo vilevile—na hata sisi tunaamini.

Kanisa la kwanza mara kwa mara lilikutania katika nyumba za watu binafsi. Yule mwanamke tajiri, Lidia, alimpokea Kristo chini ya huduma ya Paulo (Matendo 16:14–15). Baadaye, tunasoma, "Nao wakatoka gerezani wakaingia nyumbani mwa Lidia; na walipokwisha kuonana na ndugu wakawafariji, wakaenda zao" (16:40). Kitu kilichoangaziwa zaidi katika mikutano ya kanisa ya nyumbani kilikuwa: "....wakawafariji."

---

21. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Machi–Aprili–Mei 1996 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 29. Imetumiwa kwa ruhusa. (Chapisho hili liligeuka kuwa*Reflecting God*.)

Hatimaye, makanisa yalikuja kuanzishwa mara kwa mara katika sehemu za umma—mara kwa mara, katika jengo lililotengwa kama nyumba ya ibada. Hata katika mpangilio huu mpya, lengo kuu la mikusanyiko hii ilikuwa bado ni "kuhimizana katika upendo na kazi nzuri."

Mtu mmoja alimwendea mchungaji aliyewekwa wakfu na kusema kwamba hakuona haja ya kanisa lenye mpangilio. Aliendelea kuelezea kwamba alimwita mke wake na watoto pamoja kila siku ya Jumapili, na kuwahubiria, na kuwapa Sacramenti mara moja moja—na hiyo inatosha. Lakini kwa kuwa kusanyiko hili lilikuwa la familia moja ndogo, walikuwa wanatoa hesabu kwa nani? Je, nani walimpa zaka zao? Si ajabu mwandishi wa Waebrania alituonya kwamba tusiache kukusanyika pamoja. Zaidi ya kuwa familia moja, "kwa kweli tunahitajiana."

Wakati wa kufungiwa kutoka wakati wa COVID-19, serikali nyingi zilitangaza watu wasikaribiane na wakawahimiza au hata kutaka makanisa yaache kukutana. Makanisa mengi yaliendesha ibada kukiwa na mchungaji, wanamuziki wachache, na kanisa tupu, wakitumia teknolojia kuwasiliana na washirika majumbani mwao. Hili lilikuwa tendo zuri kwa kuzingatia hali ya wakati huo, lakini kila mahali Wakristo walikuwa wakisema, "Natamani sana kurudi kanisani na kukutana pamoja."

Mchungaji mmoja alikuwa mnenaji mgeni katika kanisa moja lililo nje ya parokia yake. Gary, ambaye alikuwa mmoja wa wachungaji wa kanisa hilo, alimwendea yule mnenaji na akasimulia jambo aliliopitia yapata miaka arobaini iliyopita, wakati Gary na mke wake walipokuwa wameanza kazi ya kanisa katika wilaya mpya. Wakati huo, yule mnenaji mgeni alikuwa akihudumu katika wilaya hiyo moja. Gary anakumbuka na kusema hivi, "Tulipofika, hatukumjua mtu yeyote. Wewe peke yako ndiye uliyetusikiliza. Wewe na mkeo mlitupeleka kwenda kula chakula cha mchana." Hii ni ajabu sana. Natumai hili halitatokea tena.

Kwa hiyo fanya sehemu yako. Jitose katika kanisa ambalo linafuata Biblia na linamheshimu Yesu Kristo. Jiunge na wale waliokaribu nawe "kuhimizana katika upendo na kazi nzuri" na "kufarijiana." Baadaye, watu wasije wakasema, "Wewe ulikuwa ni wewe tu," lakini badala yake waseme, "U mmoja wa watu waliotupenda na kutusikiliza."

# Hakuna Jina Jingine

*Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote,*
*kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa*
*wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*
*Matendo 4:12*

Ni nadra kwa mtu kujitolea kuteseka jela kwa jambo lisilo la kweli au kwa hisia. Petro na Yohana, watu waliofungwa jela kwa kumhubiri Kristo, walikuwa wamemjua Yesu katika maisha yake, kifo, na ufufuo—walijua kwa hakika kwamba Yesu alikuwa Mungu katika mwili.

Hata ingawa yule kiwete kila siku alikuwa mahali pa dini akizungukwa na watu wa kidini waliokuwa wakiomba kila mara, alikuwa hajapona kupitia kwao. Lakini katika jina la Yesu, aliponywa mara hiyohiyo (Matendo 3:6–7).

Ingawa viongozi walimpa changamoto, Petro alikuwa jasiri kwa ujazo wa Roho (4:8), na akahubiri kwamba Kristo hatoi tu uponyaji lakini pia wokovu. Petro alikuwa wazi kabisa: "Kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (4:12).

Mchungaji kutoka Vietnam alikuwa jela kwa zaidi ya wiki arobaini. Alihubiri Jumapili nyingi, kisha maafisa wa serikali wakaja kumkamata na kumtupa jela. Alipoachiliwa huru, alipewa stakabadhi rasmi iliyonakili kukamatwa kwake. Mchungaji alihifadhi stakabadhi hizi kwa sababu, huko Vietnam, kanisa linaweza kusajiliwa tu baada ya kuweko kwa miaka kumi na mitano—na stakabadhi zake za kukamatwa zinathibitisha hiyo miaka kumi na mitano. Wakati huu wote amekuwa akihubiri, "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote" isipokuwa Kristo.[22]

22. Awali kilichapishwa katika *Reflecting God* Juni–Julai–Agasti 2010 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 23. Imetumiwa kwa ruhusa.

FEBRUARI 21 **52**

# Je, Jumapili ni Takatifu Kiasi Gani?

*Usiwe na miungu mingine ila mimi.*
*Ikumbuke siku ya Sabato uitakase.*
*Kutoka 20:3, 8*

Mungu wa kweli na wa ajabu, Mungu pekee ndiye alikuwa amewakomboa Waisreli kutoka utumwani. Walikuwa watakuwa watu wake pekee. Katika mkutano mkubwa aliokuwa nao na Musa huko Mlima Sinai, Mungu alitoa zile Amri Kumi. Mara moja, aliwaambia watu wasiwe na miungi mingine—isipokuwa "Bwana Mungu wako." Alitoa sheria nyingine za ziada kuwalinda watu wake na kuwasaidia kumpa nafasi ya kwanza katika mioyo na maisha yao. Moja ya sheria ilikuwa kuikumbuka siku ya Sabato.

Baada ya Yesu kusulubiwa, Mariamu Magdalena na yule Mariamu mwingine walikwenda kaburini. Mathayo 28:1 inataja saa maalum: "Na sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Walipokuwa hapo, malaika alitangaza na kusema, "Hayupo hapa; maana amefufuka kama alivyosema" (kif.6). Kufufuka kwa Yesu Kristo kulikuja kuwa tukio muhimu zaidi katika maisha na huduma ya Yesu. Kadiri vuguvugu jipya la Kikristo lilivyoenea, Wakristo walianza kukutana siku ya Jumapili, siku ya kwanza ya juma. Katika 1 Wakorintho 16:2, Paulo anawahimiza Wakristo, "Siku ya kwanza ya juma kila mmoja wenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja." Katika ulimwengu wa kisasa, yamkini asilimia 95 ya Wakristo huichukulia Jumapili, kuwa siku ile Yesu alifufuka kutoka kifoni, kuwa siku yao ya ibada.

Alikosolewa mara kwa mara kwa jinsi alivyoichukulia Sabato; mafarisayo hata walipanga njama ya kumuua kwa sababu alimponya mtu siku ya Sabato, ambalo ni jambo lililokiuka sheria kali za Wayahudi walizoziunda ili kuitakasa siku ya Sabato (Marko 3:2–6). Yesu alijibu hasira yao kwa kuwauliza maswali yasiyohitaji majibu: "Ni halali siku ya sabato kutenda mema, au kutenda mabaya? Kuponya roho au kuiua?" (3:4). Katika wakati wake duniani, Yesu alifunua uelewa mpya wa Sabato—alituonesha kwamba "kufanya mema" ni tukio zuri katika siku ya kuabudu.

Wakati mwingine, Yesu alishughulikia suala hilo zaidi kwa kutumia swali lingine: "Akawaambia, Ni nani miongoni mwenu, ikiwa ng'ombe wake

au punda wake ametumbukia kisimani, asiyemwopoa mara hiyo siku ya sabato?" (Luka 14:5). Ni sawa kushughulikia dharura ya watoto au wanyama wako katika siku ya ibada.

Katika maisha yangu ya kwanza, niliichukulia Siku ya Bwana hivi hivi. Tatizo kidogo tu lingenizuia kwenda kanisani. Lakini baada ya kumjua Kristo kwa uhusiano binafsi, nilianza kuwa makini juu ya kuiheshimu Siku ya Bwana. Nilikuja kuamini kwamba ni siku ya ibada, ushirika, huduma, na kupumzika.

Siku moja, nilikuwa nimeenda nyumbani kwa rafiki yangu wa utotoni na familia yake. Basi tukaenda kanisani. Mama yake rafiki yangu alikuwa ameweka nyama kwenye oveni kabla hatujaondoka. Tulipofika nyumbani, tulikuta ile nyama ilikuwa imeungua, na ule moshi uliotokana na kuungua huko uliacha mashata kila mahali kwenye fanicha. Mwanzoni, nilisumbuka—je, ilikuwa siku ya kuabudu ama siku ya kazi? Lakini nilijua nilihitaji kujitosa mzima mzima na kusaidia, kwa hiyo sote tulifanya kazi pamoja kusafisha fanicha. Kilikuwa kisa cha "kumtoa ng'ombe kisimani."

Hadi leo, niko makini juu ya kutunza siku ya Jumapili kama siku ya ibada. Watu wakija kunitembelea, wanakaribishwa kuja kanisani kwetu. Wakikataa kuja kanisani, basi wanajua kwamba jambo ninalolipa kipaumbele ni kwenda katika nyumba ya Bwana. Kama nasafiri, huwa naandaa ratiba ambayo inatenga Jumapili kama siku za kuabudu.

Siku moja nilisikia msemo wa zamani: "Wayahudi waliikumbuka Sabato, na Sabato iliwakumbuka." Ninaamini ninaweza kusema wazi kwamba katika zaidi ya miaka sitini na tano tangu nilipompokea Kristo kwa mara ya kwanza, "Nimeikumbuka Siku ya Bwana, na Siku ya Bwana imenikumbuka." Na kukumbuka huko kumekuwa kuzuri sana, kumekuwa kwa furaha, utele na unayotiririka.

Hapa kuna zoezi zuri—malizia sentensi ifuatayo kwa kujaza pengo lifuatalo: "Bwana, sitakwenda kanisani asubuhi ya leo kwa sababu kukutana nawe si muhimu kama _________."

**FEBRUARI 22** **53**

# Je, Nitakuwa Kama Wewe?

*"Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu."*
*Yohana 3:3*

*Naomba watoto wangu wakue katika neema na kumjua*
*Bwana na Mwokozi Yesu Kristo.*
*2 Petro 3:18*

"Nikimpokea Yesu Kristo usiku wa leo, je, nitakuwa kama wewe usiku wa leo kwa kuwa umemfuata Yesu kwa miaka mingi?" Hili ndilo lililokuwa swali zito na la wazi aliloniuliza Peggy. Mimi na watu wawili wengine kutoka kanisani tuliketi na Frank na Peggy sebuleni kwao. Tulijadiliana kwa kina maana ya kumpokea Kristo na kumfuata. Tuliwaeleza kwamba mtu anapompokea Kristo kweli katika maisha yake, mtu huyo hubadilika sana kiasi kwamba Yesu aliita hali hiyo "kuzaliwa mara ya pili."

Sasa Peggy alitaka kujua, kama dakika moja baada ya kumpokea Kristo, angekuwa kama mimi—mtu aliyemfuata Kristo kwa miaka mingi. Sehemu iliyofuata ya mazungumzo yetu ilikuwa hivi:

"Peggy, umeniambia habari za mtoto wako, Brent. Ana miaka mingapi?"

"Mitatu."

"Je, anaendeleaje katika aljebra?"

Huku akiwa ameshtuka, alijibu akasema, "Hasomi aljebra."

"Ndiyo. Amezaliwa. Yuko hai. Anaongea, anatembea, anakimbia, anacheza. Ana afya njema na yuko hai kabisa. Yuko jinsi anavyopaswa kuwa kwa miaka mitatu. Lakini bado hajakuwa vyote anavyopaswa kuwa. Siku moja atakwenda shule, atajifunza hesabu, atajifunza kujumlisha na kutoa, kisha kuzidisha na kugawany. Na siku moja atajifunza aljebra."

Nikaendelea kusema, "Unapozaliwa mara ya pili kiroho, unafanyika kuwa hai kweli na kikamilifu katika Kristo. Sasa una maisha halisi ya kiroho. Lakini una maisha kamili ya kukua mbele yako. Mungu atakuvumilia. Atakuongoza hatua kwa hatua, kama uwezavyo, hadi uwe na maisha ya ukomaavu na yenye nguvu. Kuna masomo kadhaa aliyonifundisha katika wiki yangu ya kwanza, mengine alinifundisha mwaka mmoja baadaye, na mengine wiki iliyopita tu. Ni njia ya kusisimua ya kuishi, na Mungu mwenyewe akikukuza wiki baada ya wiki."

Peggy aliridhika. Usiku ule, Frank na Peggy walimpokea Kristo maishani mwao na wakaanza safari na Yesu. Na walikua kiroho sana!

Si ajabu tuna maonyo yote mawili: "Zaliwa mara ya pili," na, "Kua katika neema na maarifa ya Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo."

# Kua

*Naomba watoto wangu wakue katika neema na kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo.*
*2 Petro 3:18*

Ninafanyiwa upasuaji kesho asubuhi. Si upasuaji mkubwa—ni upasuaji wa jicho. Na bado kuna hatua nyingi sana za kufika huko. Huku zikiwa zimesalia saa ishirini na nne, nimepimwa kimatibabu na kupewa vipimo vitatu vya dawa ya kutia machoni. Bado ninahitaji kunawa uso wangu vizuri usiku na asubuhi; sina chakula wala maji baada ya usiku wa manane; kutumia dawa fulani nilizoandikiwa ninapoamka; kuwa na mtu wa kunipeleka kwa gari kwenda kwenye kituo cha upasuaji na kurudi; kuacha vitu vyangu vya thamani nyumbani; kutoa hati zenye historia yangu ya afya, leseni ya udereva, kadi ya bima, na kadi ya mkopo kwenye meza ya wagonjwa wanaolazwa; na zaidi.

Hatua hizi zote ndogo zinachukuliwa ili upasuaji uweze kufaulu, kisha niweze kuona vizuri maisha yangu yote. Nimechukua kila hatua kwa mtazamo chanya kwa sababu ninapenda matokeo ya mwisho. Ninaamini hili ni muhimu kwa sababu tayari nilipasuliwa vizuri jicho moja, na maisha ni mazuri zaidi.

Petro alikuwa na mambo mengi ya kusema katika barua zake mbili alizowaandikia Wakristo. Anazungumzia "kutakaswa na Roho" (1 Petro 1:2); "alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima" (kif. 3); "urithi" mbinguni (kif. 4); "mtakuwa watakatifu" (kif. 16); na "Basi, wekeni mbali uovu wote na hila yote" (2:1). Anasema, "Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu" (2:2).

Kuna wakati katika maisha ya kiroho unapopiga hatua za kitoto, huku ukijua utaweza kuleta maendeleo na ushindi katika siku zijazo. Kama Mkristo mchanga, mimi husoma historia za maisha ya Wakristo wakubwa na wakomvu kama vile kitabu cha Hudson Taylor *Spiritual Secret* and Rees Howell's *Intercessor*. Wanaume hawa walipokea majibu ya ajabu ya maombi yao na walipata ushindi mkubwa. Nilivutiwa na mengi katika maisha yangu ya kiroho kwa sababu ya hayo, lakini nilijua ingechukua miaka mingi ya kukua ndipo nifike hapo. Lakini sikuvunjika moyo kwamba sijafika hapo bado.

Hata unaposoma kurasa hizi za maombi ya kibinafsi, utaona mambo mengi makuu yaliyotendwa na Mungu. Hebu hili naliwahamasishe kufikia malengo makubwa zaidi, badala ya wasiwasi kwa sababu huo sio uzoefu wako.

Katika maisha yangu ya Ukristo ya kwanza, nilikuwa naweza kuomba kwa dakika kumi kwa siku na kusoma sura moja ya Agano Jipya kwa siku. Lakini nilijua kuna mambo mazuri zaidi mbele yangu. Wakati mmoja, nilihisi majaribu makubwa na nikajaribu kuomba niyashinde, lakini sikuweza. Nilipokimbilia hadi kwenye chumba cha bweni la mshauri wangu wa kiroho na kuumimina moyo wangu kwake nilipata jibu.

Katika kanisa ambalo nilikuwa nimempata Kristo karibuni, nilimwona Mkristo aliyenizidi umri akiishi maisha yasiyokuwa na msimamo na nikamlalamikia mchungaji wangu juu yake. Mchungaji wangu alinitia moyo, akanishauri kuwa na subira, na akanionya dhidi ya kuwa na roho ya kuwahukumu watu. Hatua hizi ndogo zimeyachonga maisha yangu ya sasa.

Ninayasema haya yote ili uweze kukua katika neema ya Mungu. Ninajua unaweza kufanya hivyo.

**FEBRUARI 24** **55**

# Kubishwa Mlangoni

*Tazama! Nasimama mlangoni, nabisha. Mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.*
*Ufunuo 3:20*

Picha inaweza kuwa njia ya mtu kumpokea Yesu moyoni na maishani mwake.

Hapo juu ni picha maarufu ya Warner Sallman ya Kristo akibisha mlangoni. Picha ya Sallman ya *Head of Christ*, *Christ at Heart's Door*, na picha nyingine zimetokea katika picha bilioni moja za Kristo zilizosambazwa duniani kote.

Picha ya *Christ at Heart's Door* msingi wake ni rufaa ya kanisa huko Laodicea katika Ufunuo 3:20. Hata ingawa wito ni kwa wale walio vuguvugu kufungua makanisa yao na maisha yao upya kwa Kristo, vilevile wito huu unaimarisha kanuni pana ya kiroho: palipo na mlango uliowazi, kutakuwa na Kristo anayeingia. Hivyo, maandiko haya yanaweza kutumiwa kwa Wakristo wanaohitaji wokovu.

Huu hapa ni muhtasari wa mazungumzo yangu na Fred na Patty baada ya majadiliano ya awali kuonesha uelewa wao wa injili:

**Chic Shaver:** Fred na Patty, hapa kuna picha maarufu ya Kristo akibisha mlangoni mwa moyo. Msingi wake ni Ufunuo 3:20, "Nasimama! Nasimama mlangoni, nabisha. Mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami." Je, unauona ule mwangaza kwenye tao la mlango la mawe, na kisha upande wa kushoto ulio chini ya tao la mbao? Kisha mwangaza unafifia chini miguuni mwa Yesu. Ukitumia ukifirivu wako, unaweza kuona umbo la moyo. Unaweza kuliona?

**Fred:** Ndiyo, tunaweza!

**Chic Shaver:** Hebu tuchukulie hilo kuwa ni Yesu akibisha mlangoni mwa moyo wako. Tambua ile miba inayokua karibu na miguuni pa Yesu, kana kwamba amekuwa akibisha kwa muda mrefu. Inaonekana kwangu kwamba Kristo amekuwa akibisha kwenye mlango wa moyo wako kwa muda mrefu. Je, unaelewa hilo?

**Patty:** Nafikiri sote itatubidi tuseme ndiyo—amebisha mlango kwa muda mrefu.

**Chic Shaver:** Unaliona lile dirisha dogo? Kuna giza ndani kwa sababu maisha kwa kawaida huwa giza wakati Kristo ameachwa nje. Kisha, tambua Kristo anabisha pekee; hajaribu kuusukuma huo mlango. Hii ni kwa sababu ule mlango lazima ufunguliwe kutoka ndani.

**Fred:** Ninaelewa.

**Chic Shaver:** Njia ya kawaida ya kufunga milango siku hizo ilikuwa ni kuweka kipande cha boriti katika mabano ya chuma pande zote mbili za mlango. Ili uufungue mlango, yule mtu aliye ndani ilimbidi kusukuma nje ile boriti itoke kwenye yale mabano na kwenda upande mmoja wa mlango. Kifungu kilicho nyuma ya Ufunuo 3:20, kifungu cha 19, kinaishia kwa neno "ukatubu." Ikiwa tutafungua mlango wa mioyo yetu kwa Kristo, lazima tumwambie Mungu tunasikitika kwa dhambi zetu na, wa msaada wa Mungu, tuziache dhambi zetu. Katika mfano huu wa picha, ikiwa kweli tunataka kumfungulia Kristo mlango, lazima tuiondoe ile boriti ya dhambi. Je, unayaelewa haya?

**Fred:** Ndiyo.

**Patty:** Ndiyo, nayaelewa.

**Chic Shaver:** Ukimfungulia Kristo mlango wa moyo wako, anaahidi kuingia ndani. Lakini lazima uelewe kwamba unapofungua mlango, unampokea kama Mwokozi, anayesamehe dhambi zako zote, na kama Bwana, kiongozi wa maisha yako. Hiyo inaamanisha kuanzia sasa, utafanya yale anayotaka ufanye. Unamruhusu akuongoze. Je, uko tayari kufanya hivyo?

**Fred:** Ndiyo, niko tayari.

Patty anatikisa kichwa kukubali.

Masomo ya kesho yatakueleza nini kilichofuata.

**FEBRUARI 25** **56**

# Nguvu za Picha

*Wote niwapendao ninawakemea na kuwarudi. Basi uwe na bidii, ukatubu. Tazama! Nasimama mlangoni, nabisha. Mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.*
*Ufunuo 3:19–20*

**Chic Shaver:** Ninaona, Fred na Patty, kwamba Kristo anakuomba sasa hivi ikiwa ungependa kumpokea na karama yake ya uzima wa milele kwa kumfungulia Kristo mlango wa moyo wako. Kama ninaweza kukusaidia kufanya hivyo kwa kuomba nawe, je, ungependa kufanya hivyo?

**Patty:** Hakika, ndiyo!

**Fred:** Hivyo ndivyo ninavyotaka kufanya.

**Chic Shaver:** Je, ungependa ombi lako mwenyewe, au urudie nyuma yangu ikiwa kweli unamaanisha?

**Fred:** Omba, kisha tutarudia nyuma yako.

Niliomba ombi lifuatalo, na wakarudia nyuma yangu.

**Chic Shaver:** Ewe Mungu, ninajutia dhambi zangu, na kwa msaada wako, ninaziacha. Sasa hivi, ninakufungulia mlango wa moyo wangu. Yesu. Ninakupokea kama mtu anayesamehe dhambi zangu zote na kama yule anayeyatawala maisha yangu. Sasa hivi, ninakupokea moyoni mwangu na maishani mwangu. Amina.

Kisha nikawaomba wainamishe vichwa vyao huku nikiwauliza maswali kadhaa.

**Chic Shaver:** Fred, je, ulimaanisha wakati ulipomwambia Mungu kwamba unajutia dhambi zako na kuziacha dhambi hizo?

**Fred:** Ndiyo, nilimaanisha.

**Chic Shaver:** Je, ulikuwa unamaanisha wakati ulipomwalika Kristo aingie moyoni mwako na kuwa kiongozi wa maisha yako?

**Fred:** Ndiyo, nilimaanisha.

**Chic Shaver:** Yesu alisema kwamba mtu yeyote akifungua mlango wa moyo wake, ataingia ndani. Je, unadhani alimaanisha hivyo?

**Fred:** Ndiyo, alimaanisha hivyo.

**Chic Shaver:** Kama umeziacha dhambi zako na ulimaanisha; kama umeufungua mlango wa moyo wako na ulimaanisha; na ikiwa Yesu alisema ukiufungua mlango, ataingia; basi Yesu yuko wapi sasa hivi?

**Fred:** Yuko moyoni mwangu.

Mwishoni wa mazungumzo yetu, Fred alililichukulia kwa uzito na nikamuuliza Patty maswali yale yale. Akaniambia, “Yuko moyoni mwangu,” na akaanza kulia.

Sote tuliinua vichwa vyetu. Niliwapa mikono na nikasema, “Karibuni katika ufalme wa Mungu!” Walitabasamu sana. Tabasamu la mwaka.

Basi nikaanza mchakato wa uanafunzi pamoja nao uliokuwa ni pamoja na kuanza mafundisho ya *Basic Bible Studies for New and Growing Christians*. Nilichukua ile picha ya Yesu na nikaandika nyumba yake: “Fred Smith alimfungulia Kristo moyo wake mnamo Februari 13, 2018—Ufunuo 3:20.” Nilimwomba Fred atie saini cheti cha kuzaliwa kiroho na nikawaomba wote walioandamana nami watie saini pia. Vile vile nilimpa Patty picha kama hiyo na kauli.

Picha ya Kristo akibisha mlangoni ni mfano wa kiasilia wa ujumbe wa injili ambao kila kipengele cha picha kinakukumbusha kile utakachofuatia kusema. Nguvu za picha! Kubisha mlangoni! Je, umemwalika Kristo moyoni na maishani mwako? Je, unamjua mtu ambaye anahitaji umwelezee maana ya picha hii?

**FEBRUARI 26** **57**

# Mungu Akubariki

*BWANA akamtokea usiku uleule, “akasema, Mimi ni Mungu wa Abrahamu baba yako. Usiogope, maana mimi ni pamoja nawe, nami nitakubariki, na kuzidisha uzao wako kwa ajili ya Abrahamu mtumishi wangu.” Akajenga madhabahu huko, akaliitia jina la BWANA. Akapiga hema yake huko, na watumwa wa Isaka wakachimba kisima huko.*
*Mwanzo 26:24–25*

Hebu natufupishe muktadha wa kitini kilicho hapo juu:

- Bwana alikuwa na mkutano binafsi na Isaka.
- Bwana alimwambia Isaka asiogope. Kwa nini? Kwa sababu Bwana angekuwa pamoja naye.
- Mungu aliahidi *kumbariki* Isaka na kumpa kizazi kikubwa.
- Isaka hakuuchukulia mkutano huu kwa juu juu. Alijenga madhabahu na akamwabudu Bwana.
- *Baraka* ya Isaka ilikuwa ni pamoja na uwepo wa Mungu; afueni ya papo hapo ya mateso ya kimwili (kisima cha maji mahali pakavu sana); na msururu wa uzao unaotokana na kuzaliwa kwa Yesu Kristo.

Katika Biblia, baraka inatolewa kwa wema—mara kwa mara vitu vizuri vya kimwili na kiroho.

Mathayo 7:11 inasimulia juu ya mafundisho ya Yesu kuhusu maombi: “Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu zawadi nzuri, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa roho mtakatifu hao wamwombao!” Luka 11:13 inaendelea kufafanua zaidi kile Yesu alisema wakati huo: “Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu zawadi nzuri, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa roho mtakatifu hao wamwombao!” Ni wazi, Roho Mtakatifu ndiye karama bora zaidi ya karama zote. Si ajabu tunasema mtu yeyote anayempokea Roho Mtakatifu amebarikiwa kweli. Unapokuwa na Roho Mtakatifu, una Mungu mwenyewe.

Ni baraka iliyoje kumpokea Roho katika ukamilifu wake utakasao. As Wagalatia 5:25 inasema, “Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho.” Hili lkwa kweli linaweza kuitwa “kuishi katika baraka.” *Mungu akubariki*.

**FEBRUARI 27** **58**

# Kujikana Nafsi

*Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye; si kama apigaye hewa; bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiria wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.*
*1 Wakorintho 9:26-27*

Je, unaweza kuamini kwamba yule mtu aliyesema, “Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu” (Waefeso 2:8), na, “Lakini katika mambo hayo yote sisi ni zaidi ya washindi, kupitia kwake yeye aliyetupenda” (Warumi 8:37),

na, "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu" (Wafilipi 4:19) angetilia mkazo kujikana nafsi sawa na kusema, "bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha"?

Nilimwambia rafiki yangu ambaye ni kijana na aliyekuwa amempokea Kristo na alikuwa na historia ya kunywa pombe kupindukia, "Usijaribu kunywa hata chupa moja." Rafiki yangu mwingine alikuwa mara kwa mara amehisi kushindwa na tatizo la kula kupita kiasi na uzito wa ziada, lakini hatimaye nilimwona akijitia nidhamu ya kula na kuweza kuudhibiti uzito wake.

Niliamua kumheshimu Mungu katika mawazo yangu kwa kukabiliana na sehemu za vipindi vya TV zilizo chafu kwa kanuni ya sekunde mbili: ndani ya sekunde mbili, ningetumia kitanza mbali kubadilisha stesheni.

Huenda Mungu amekupa moyo safi, lakini itakubidi ujitie nidhamu juu ya hisia zako juu ya kuumizwa katika maisha. Dr. Jim Diehl siku moja alisema kwamba usipompa Yesu moyo wako, kule kuumizwa kunaweza kuwa uchungu, ambao unaweza kugeuka kuwa kisasi, ni kisasi kinaweza kuwa chuki. Alisema, "Ikiwa hutajikana nafsi, hutaendelea kuwa mshindi." Hata mtume Paulo alijitia nidhamu ili asiweze "kuikosa thawabu."

Na je, nini matokeo ya kujikana nafsi? Yule mwanamke aliyepoteza uzito aliniambia alihisi vizuri juu yake, alihisi kuwa mshindi, na akapata furaha. Hebu fikiria jinsi *utakavyohisi* utakapoona matunda ya nidhamu katika maisha yako mwenyewe. Unapotumia neema ya Mungu kujikana nafsi, ushindi hupatikana. Utakimbia mbio ukiwa na lengo na utamaliza vizuri.

**FEBRUARI 28** **59**

# Kwa Nini Kuna Mauaji Mengi?

*Wakati BWANA, Mungu wako, atakapowatoa mbele yako, nawe utawapiga; wakati huo ndipo uwaondoe kabisa. Usifanye agano nao, wala kuwahurumia; wala usioane nao. Binti yako usimpe mwanawe mume, wala usimtwalie mwanao mume binti yake. Kwa kuwa atamkengeusha mwanao mume asinifuate, ili wapate kuabudu miungu mingine; ndipo itakapowaka hasira ya BWANA juu yenu, naye atakuangamiza upesi.*
*Kumbukumbu 7:2–4*

*Usiseme moyoni mwakoBwana Mungu wako, atakapokwisha kuwasukumia nje mbele yako, ukasema, "Ni kwa haki yangu alivyonitia Bwana niimiliki nchi hii." kwani ni kwa ajili ya uovu wa mataifa haya Bwana anawafukuza nje mbele yako.*
*Kumbukumbu La Torati 9:4*

"Kwa nini kuna mauaji mengi katika Agano La Kale?" ni swali nililoulizwa mara nyingi kwa miaka mingi. Nakubali kwamba linatatiza. Hapa kuna mawazo juu ya suala hilo:

1. Waisraeli wazitwae mali za mataifa si kwa sababu ya haki ya Waisraeli lakini kwa sababu ya uovu wa mataifa hayo (Kumbukumbu La Torati 9:4). Ni waovu.
2. Waisraeli wanapaswa kuwaangamiza hawa watu kabisa. Wasipofanya hivyo, na wale binti wa mataifa waoelewe na wavulana wa Kiisraeli, ushawishi wa wale binti hatimaye utawavuta Waisraeli waabudu miungu wa uwongo. Mungu ananuia kuianzisha nchi mpya ambapo ataheshimiwa kama Mungu wa pekee aliye wa kweli (Kumbukumbu la Torati 7:3-4).
3. Kuangamizwa kabisa kwa mataifa maovu ni taswira ya jinsi maisha ya kiroho yanavyopaswa kuwa—kuondolewa kwa dhambi *zote* kutoka mioyoni na maishani mwetu, na kujiachilia kikamilifu kwa Mungu mmoja wa kweli. Hakuwezi kuwa na washindani—mioyo yetu lazima iwe ya Mungu kwa asilimia 100.

Baada ya Yesu kuja katika ulimwengu wetu, tunaona msisitizo mpya. Anatimiza yale yaliyodhihirishwa na Agano la Kale, na sasa tuna Agano Jipya.

1. Yesu anafundishwa, "Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi" (Mathayo 5:44). Hatujaitiwa vita, bali upendo: "Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema" (Warumi 12:21).
2. Hatupaswi kuacha alama za dhambi katika maisha yetu, isije zikatuvuta nyuma na kurudia maisha ya dhambi: "Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi. Na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu" (Waebrania 12:1)
3. Mungu anawaagiza Wakristo tuyasalimishe maisha yetu yote *kikamilifu* kwake: "Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana" (Warumi 12:1). Agano Jipya hata linazungumzia juu ya kuua uovu wote katika maisha yetu. Kama Paulo

anavyosema, “Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu” (Wagalatia 2:20).

Haya ndiyo mauaji ambayo ningeyajali zaidi leo—kuua dhambi. Mathayo 5:8 inasema, “Heri wenye moyo safi; Maana hao watamwona Mungu.” Je, uko tayari kuwa mmoja wa wale wenye moyo safi?

**MACHI 1** **60**

# Mungu Alitupenda Sana

*Wapenzi, na mpendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu.*
*1 Yohana 4:7*

Chumba cha Rees Howells kilikuwa sehemu ya chini ya nyumba ya umishenari. Yeye ndiye aliyekuwa mtu pekee katika nyumba hiyo. Lakini Rees alisema alitembelewa na wageni wakati wa usiku—vitu vinavyotambaa na kunawiri katika majira ya joto. Siku moja wakati wa asubuhi, alipokuwa akiandaa kula kifungua kinywa chake cha shayiri na jibini, alikuta wadudu wameshamwahi. Mwanzoni, Rees hakuweza kujizuia kuwa na hisia mbaya dhidi ya rafiki yake aliyekuwa amempa mahali hapo pa kuishi. Kisha Mungu akaongea na Rees, akisema kwamba Yesu alimpenda wakati alipomtendea Yesu vibaya zaidi kuliko jinsi rafiki yake alivyomtendea Yesu

Akiwa juu ya vilima hivyo vya kisiwa chenye joto, Rees aliomba. Hakuweza kumwona rafiki yake na alimwona Mwokozi aliyewapenda wale waliomuua! Kufikia wakati Mungu ameishughulikia hali ya ndani ya Rees, Roho Mtakatifu ndani yake alimpa upendo kamili kwa yule aliyekuwa amemkosea. Hakuna msamaha wa kuigiza hapa—Rees alipoona kwamba “Mungu anampenda sana”, aliweza kuwapenda wale waliokuwa vigumu kuwapenda.[23]

23. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Machi–Aprili–Mei 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 36. Imetumiwa kwa ruhusa. (Chapisho hili liligeuka kuwa*Reflecting God*.)

# Na ndugu yako akikukosea, nenda...

*Na ndugu yako akikukosea, nenda ukamwonye,*
*wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo.*
*La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili.*
*Mathayo 17:15-16a*

Kile ambacho kifungu hicho hapo juu kinasema inaonekana jambo zito, gumu sana, na limejaa hatari—wengi wataepuka kufanya kile kinachosemwa na hicho kifungu. Na bado ukweli huu unajitokeza wazi kuhusu tukio la kaka au dada anayekutwa katika dhambi:

- Dhambi inahukumu, na mtu huyu anathaminiwa.
- Wakristo wanajaliana.
- Mtu anayetenda dhambi anarejeshwa.

Hili lilikuwa suala zito sana kiasi kwamba Yesu alifundisha kwamba mchungaji mwema angeacha kondoo tisini na tisa mahali na kwenda kumtafuta kondoo aliyepotea. Kisha akahitimisha kwa kusema, “Vivyo hivyo haipendezi mbele za Baba yenu aliye mbinguni kwamba mmoja wa wadogo hawa apotee” (Mathayo 18:14).

Nilikuwa mchungaji mchanga, na Cal alichaguliwa kama msimamizi wa Shule ya Jumapili katika kanisa letu jipya. Usiku mmoja, nilipokea simu kutoka kwa mtu nisiyemjua. Mtu huyu asiyejulikana alisema, “Je, unajua Cal ni mlevi na sasa hivi yuko nyumbani kwa mwanamke mwingine?”

Baada ya simu hiyo, nilihisi ilinibidi niende kwenye nyumba hiyo, nilikutana na Cal mlangoni na alikuwa mlevi na akanitukana. Nilimkuta akitenda dhambi. Nilirudi nyumbani na kumpigia simu msimamizi wangu wa wilaya anipe ushauri. Aliniambia, “Watu wa kanisa lako jipya wamemfahamu Cal kwa muda mrefu zaidi kushinda muda ule wamekujua wewe. Hawataamini neno lolote utakalosema juu yake. Iambie bodi yako ya kanisa kile ulichokigundua. Andamana na wanaume wawili au watu hivi. Mwombe Cal akiri tatizo lake la kunywa pombe mbele za watu ulioandamana nao. Mwambie ajiuzulu kama msimamizi wa Shule ya Jumapili.”

Ile bodi ya kanisa ikakubali; tukawachagua wanaume watatu. Bodi ilimwombea Cal usiku ule, na wale wanaume watatu walisema walitaka kumwombea Cal hapo nyumbani kwake. Kwa hiyo tukaenda kumtembelea.

Tulipofika nyumbani kwake, Cal, ambaye sasa alikuwa macho makavu, aliungama tatizo lake la pombe. Nilimwomba ajiuzulu na akinisihi akisema, "Naomba nibaki kazini, na nitapata ushindi dhidi ya unywaji pombe."

Nikasema, "Hapana, wewe pata ushindi wa tatizo lako la kunywa pombe kisha baadaye kanisa litaamua ikiwa utahudumu katika wajibu huu." Akakubali kwa shingo upande. Na, oh, natamani ungeyasikia yale maombi ya huruma waliyomwombea wale wana bodi.

Tulimteua msimamizi mpya, na wale wanaume wa kanisani walimzunguka Cal kwa upendo, maombi, na uwajibikaji. Cal alibaki kanisani, na mke wake aliendelea kuhudumu kama mwanabodi na kuwa mfano wa uaminifu kwa wengine. Mtoto wao wa kiume aliyekaribia kubalehe aliokolewa kwa ajili ya kanisa na ufalme.

Ilikuwa vigumu, lakini tulifuata kanuni za Biblia katika kumkabili huyo ndugu aliyekuwa ametenda dhambi. Na kwa hiyo kondoo aliyepotea alirejeshwa zizini.

**MACHI 3** **62**

# Ninaenda—Anakuja

*Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke,*
*kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu;*
*bali mimi nikienda zangu, nitamtuma kwenu.*
*Yohana 16:7*

Thomas Edison alijulikana kwa kumiliki zaidi ya hataza elfu moja—zaidi ya mtu yeyote katika historia ya dunia. Alivumbua balbu ya mwangaza wa umeme. Lakini balbu yake ya mwangaza imepotea, na ni kwa faida yetu kwamba tunatumia balbu za LED na balbu nyingine za kisasa zilizoboreshwa.

Wakati mmoja, Henry Ford alimpa Edison gari la 1916 Ford Model-T. Katika siku hizo za Model-A na Model-T, ungeweza kununua Ford mpya kwa $450. Sasa Model-T limepotea na, kwa faida yetu, gari nzuri zaidi zinapatikana.

Yesu aliendesha huduma yake ya nguvu kwa miaka mitatu, lakini hakuvuka ile sehemu tunayoijua kama Palestina. Alipokuwa anakaribia mauti msalabani, wanafunzi wake walikuwa wamehuzunika sana. Aliwafariji kwa kusema, "yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo

Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitamtuma kwenu." Roho Mtakatifu angeweza kuwako na kufanya kazi mahali popote duniani kwa wakati mmoja.

Yesu alisema, "Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia" (Yohana 15:26). Kazi kuu ya Roho ni kutuelekeza kwa Yesu, kumwakilisha Yesu. Unapomkea Kristo kama Mwokozi wako, ni Roho anayemfanya Kristo awe halisi kwako. Yohana 3:8 inaita hilo "kuzaliwa kwa Roho." Warumi anamwita Roho Mtakatifu, "Roho wa Kristo."

Mchukulie Roho Mtakatifu wa Mungu kuwa faida yako kubwa. Hebu fikiria juu ya baraka zote anazotaka kukupa:

- "Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu" (Yohana 14:16-17).
- "Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atamtuma kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia" (Yohana 14:26).
- "Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu" (Yohana 16:8).
- "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake (Yohana 16:13).
- "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu...na hata mwisho wa nchi" (Matendo 1:8).
- "Basi kanisa...likajengwa. Likiendelea na kuongezeka katika kicho cha Bwana, na faraja ya Roho Mtakatifu" (Matendo 9:31).
- "Basi watu hao, walipotumwa hadi Kipro na Roho Mtakatifu wakateremkia Seleukia" (Matendo 13:4).
- "Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake" (Matendo 20:28).
- "Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu" (Warumi 8:14).
- "Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa" (Warumi 8:26).

• Na hata zaidi!

Rees Howells, mshirika wa kawaida wa asili ya Welsh (1879–1950), mwasisi wa Bible College of Wales, alikuwa mtu aliyeomba sana. Ingawa alimpokea Kristo na kuzaliwa kwa Roho, alishuhudia juu ya jinsi baadaye alivyokutana kwa undani na Roho Mtakatifu: "Aliniambia, 'Kama vile Mwokozi alivyokuwa na mwili, kwa hiyo ninaishi katika hekalu la muumini lililotakaswa. Mimi ni Mtu. Mimi ni Mungu, na nimerudi kukuomba uutoe mwili wako kwangu ili nifanye kazi kupitia huo. Ninahitaji mwili kwa ajili ya hekalu langu (1 Kor. 6:19).' Ilimaanisha kila chembe ya asili yangu iliyoanguka ilikuwa niiende msalabani, na angeleta maisha yake mwenyewe na asili yake mweneywe."[24]

Je, ungependa Roho Mtakatifu akufanyie nini sasa hivi? Je, umezaliwa kwa Roho? Je, umejazwa Roho? Baraka iliyoje—Roho Mtakatifu amekuja.

**MACHI 4** **63**

# Chochote kile!

*Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote,*
*fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.*
*1 Wakorintho 10:31*

Mtu anaposema, "neno lolote," kwa kawaida inamaanisha kutojali. Lakini hivyo sivyo Paulo alivyomaanisha aliposema, "Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo, *neno lolote* fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu." "Neno lolote" la Paulo lilimaanisha kujali kikamilifu kwamba maisha yote sharti tuyaishi kwa utukufu wa Mungu.

Hata ingawa waliruhusiwa kula nyama iliyonunuliwa sokoni, Wakristo waliokuwa na wasiwasi walikataa kuila kama ingekwaza dhamira ya mtu mwingine. Tunaweza kufupisha ujumbe wa Paulo kwa kanisa kwa njia hii:

• Fanya kila kitu kwa utukufu wa Mungu, hata kile kitu kidogo zaidi.
• Tafuta kuwaona wengine wakifanikiwa.
• Jambo zuri zaidi ni kwamba watu waokoke.
• Fuata mfano wangu, kama ninavyofuata mfano wa Kristo.

---

24. Norman Grubb, *Rees Howells, Intercessor: The Story of a Life Lived for God* (Philadelphia: Christian Literature Crusade, 1952), 36.

Baada ya kumpokea Kristo, mtu mmoja alikuwa makini sana. Alimshukuru Mungu hata kwa glasi ya maji ya kunywa. Hakuweza tena kuweka sigara mdomoni mwake na kuomba na kusema, "Ewe Mungu, asante kwa sigara hii. Ibariki iutie nguvu mwili wangu na inisaidie kukutumikia." Kwa hiyo aliacha kuvuta sigara.

Mwanamke mmoja ninayemjua alijitahidi awezavyo kutenga muda wa kuwa pamoja na watu waliokuwa karibu naye, kuwatunza, na kuwaburudisha. Sasa rafiki yake na mume wa huyo rafiki yake wamempokea Kristo na wanahudumu kanisani. Dr. Larry Garmin alitoka kwao na kwenda kuwafikia Wahindi katika misitu ya Peru. Katika mifano yote miwili, waumini hawa "wanatafuta.... mafanikio ya wengi, ili waweze kuokolewa." Wanafanya "neno lolote", "kwa utukufu wa Mungu."[25]

**MACHI 5** **64**

# Tarajia Ushindi

*Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.*
*Ufunuo 21:2*

*Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu.*
*Ufunuo 21:7*

"Je, una ushindi?" ndilo swali ambalo mchungaji wangu anipendaye Ferrioli aliniuliza kila Jumapili nilipofika kanisani. Nilikuwa Mkristo mchanga, niliyeishi katika eneo la kidunia la chuo cha Ivy League, na kuzungukwa na shinikizo na majaribu. Swali la mchungaji lilikuwa zuri kwa mujibu wa kujali kwake maisha yangu endelevu ya Kikristo. Swali hili vilevile lilikuwa zuri kwa Yohana, mwandishi wa Ufunuo. Aliona kwamba kundi moja la watu lingerithi Mji Mtakatifu, mbingu mpya, na nchi mpya (21:1–2),"washindi."

Mapema, katika sura ya 2 na ya 3, Yohana alisisitiza suala hili mara nyingi katika kunakili ujumbe wa Kristo kwa makanisa saba:

25. Awali kilichapishwa katika *Reflecting God* Juni–Julai–Agasti 2010 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 14. Imetumiwa kwa ruhusa.

- Kwa Efeso—Tubu kwa kupoteza upendo wako wa kwanza kwa Kristo; kisha, utakuwa mshindi (Ufunuo 2:7).
- Kwa Smirna—Uwe mwaminifu kwa Kristo hata wakati wa mateso na hata kiasi cha kuwa tayari kufa; kisha, utakuwa mshindi (2:10–11).
- Kwa Pergamo—Tubu kwa kufuata mafundisho ya uwongo; kisha, utakuwa mshindi (2:14–17).
- Kwa Thiatira—Fanya mapenzi ya Mungu hadi mwisho; kisha, utakuwa mshindi (2:26).
- Kwa Sardi—Amka. Umekufa kiroho na matendo yako hayajakamilika. Tubu; kisha, utakuwa mshindi (3:1–5).
- Kwa Filadelfia—Shika sana ulicho nacho; kisha, utakuwa mshindi (3:11–12).
- Kwa Laodikia—Tubu uvuguvugu wako na ufungue moyo wako, maisha yako, na kanisa kwa Kristo upya; kisha, utakuwa mshindi (3:15–21).

Mwanzoni, Yohana huyuhuyu aliandikia barua kwa Wakristo wa kwanza. Katika Yohana 1:7, alisema, "Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, mwana wake, yatusafisha dhambi yote." Hii ni njia moja ya kuelezea maana ya kuwa mshindi. Kwa hiyo, unasemaje? Je, una ushindi?

**MACHI 6** **65**

# Mungu ana Jeshi

*Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia; basi, iweni na akili, mkeshe katika sala. Zaidi ya yote iweni na bidii kubwa katika kupendana; kwa sababu upendano husitiri wingi wa dhambi. Mkaribishane ninyi kwa ninyi, pasipo kunung'unika; kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu.*
*1 Petro 4:7–10*

Mnamo mwaka 2020, agizo lilitolewa na jiji letu na kaunti zinazozunguka likiwataka watu wakae nyumbani isipokuwa iwe shughuli zao ziwe ni muhimu kwa afya na usalama wao wenyewe au wengine. Agizo hilo lilikuwa jaribio la kupunguza kasi ya kuenea kwa virusi vya korona ambavyo vilienea ulimwenguni kote mnamo mwaka 2020.

Katika siku nyingine ya mateso mazito na changamoto nyingi, Petro aliwaandikia Wakristo maagizo ya kusali, kupenda, kuwa wakarimu, au kutumia karama yoyote waliyokuwa nayo kuwatumikia wengine. Katika siku zao na katika nyakati zetu, katika nyakati ngumu zaidi, Mungu angali ana jeshi: mamilioni ya Wakristo waaminifu wanaotumia karama zozote walizonazo kuwatumikia wengine.

Katika janga hili, Wakristo wengi wameniambia kwamba wanaomba kwamba Mungu atatumia mgogoro huu kuwavuta watu kwake; kwamba atawawezesha wanasayansi kupata tiba au chanjo; kwamba atawapa nguvu wafanyakazi wa matibabu na wengine wanaowahudumia wagonjwa; na kwamba atafanya haya yote kwa ajili ya taifa letu na kwa dunia nzima.

Nilihisi kupendwa wakati mchungaji wangu aliponipigia simu ili kuona jinsi tulivyokuwa tunaendelea wakati wa janga hili. Ibada za kanisa zilisitishwa kwa sababu ya hatari ya virusi kuenea katika umati wa watu. Kwa hiyo niliamua kwamba kwa siku thelathini zilizofuata, ningempigia simu angalau mtu mmoja kwa siku kutoka katika darasa langu la shule ya Jumapili au mtaani kwetu na kuwatia moyo.

Agizo la awali la serikali lilituambia kwamba mikusanyiko lazima iwe na watu kumi au wachache zaidi. Rafiki yangu Scott alisema kwamba, kwa kuwa huduma za kanisa zilikatishwa, alikuwa akiwaalika watu wanane, waumini na wasioamini, nyumbani kwake ili kumtazama mchungaji wetu akihubiri akiwa mbali. Kisha wageni wake wote wangealikwa kwenye chakula cha jioni cha Jumapili. Huu ni ukarimu wa hali ya juu!

Jirani yangu John alinipigia simu kuniambia niko huru kumwomba anifanyie kazi yoyote, hata ikiwa ni kukimbia usiku sana kwenye duka la dawa. Wakristo kila mahali walitumia karama zozote walizoweza kuwahudumia wengine wakati wa janga hilo.

Mungu ana jeshi, na wakati wa shida, linabadilika na kuchukua hatua. Na ikiwa juhudi za jeshi hili hazionekani kuwa za kutosha, kumbuka jambo lingine: Mfalme wa Aramu mwenye chuki alipozingira jiji la Dothani ili kumkamata nabii Elisha, mtumishi wa Elisha aliona jiji hilo limezingirwa na farasi na magari ya vita. "Oh, Bwana wangu! Tutafanya nini?"

"Akamjibu, Usiogope; maana walio pamoja nasi ni wengi kuliko wale walio pamoja nao. 17 Elisha akaomba, akasema, Ee BWANA, nakusihi, mfumbue macho yake, apate kuona. BWANA akamfumbua macho yule mtumishi; naye akaona; na tazama, kile kilima kilikuwa kimejaa farasi na magari ya moto yaliyomzunguka Elisha pande zote" (2 Wafalme 6:14–17).

Jiunge na jeshi la Mungu la watumishi leo. Na kumbuka kwamba Mungu ana jeshi la akiba la kikosi cha miujiza ya moja kwa moja: "farasi na magari ya moto."

MACHI 7 66

# Kondoo Wawili Waliopotea

*Ni nani kwenu, mwenye kondoo mia, akipotewa na mmojawapo, asiyewaacha wale tisini na tisa nyikani, aende akamtafute yule aliyepotea hadi amwone? Nawaambia, Vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na tisa ambao hawana haja ya kutubu.*
*Luka 15:4, 7*

Mojawapo ya mambo yanayonisumbua sana ni watu waliomkubali Kristo zamani lakini, miaka mingi baadaye, wanaonyesha ushahidi mdogo wa kumfuata Bwana. Paulo alikuwa na wasiwasi wa kutosha juu ya suala hili hadi akaandika haya yafuatayo kwa Wakolosai (2:6–7): "Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, ishini vivyo hivyo katika yeye; wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani."

Yesu vile vile, alilichukulia jambo hili kwa uzito aliposema, "Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea" (Yohana 15:6).

Zaidi ya miaka kumi na miwili iliyopita, Alan na Martha walihusika sana katika shughuli za kanisa letu. Walidhihirisha ushahidi wa kujituma kwa Kristo na kuwa na bidii kwa ajili yake. Sijui jinsi ilivyotokea hasa, lakini waliteleza, wakaacha. Niliwafikia, lakini sikupata majibu. Katika miaka hiyo kumi na miwili, niliwasiliana nao mara kwa mara.

Hapa kuna barua mbili kutoka kwa Alan na Martha kuhusu kile kilichotokea katika miaka mitatu iliyopita:

*Mchungaji Shaver,*

*Asante kwa kuwa kielelezo kizuri sana cha Kristo na upendo wake kwetu.*

*Miaka michache iliyopita, Mungu alianza kunikumbusha na kunena nami moyoni mwangu kwamba ulikuwa wakati wa kurudi kanisani. Niliona*

*kwamba baada ya kukosa kazi za kwenda kufanya siku za Jumatatu–Ijumaa, ilikuwa vigumu zaidi kujua ilikuwa siku gani ya juma. Kila mara aliponikumbusha, niliuliza ikiwa angechukua hatua thabiti kwa ajili yetu, kwa kuwa nilitaka sisi sote tutamani uhusiano wa dhati zaidi na Kristo.*

*Kila wakati nilipotuma hundi kanisani, niliomba kwamba siku moja tungerudi kanisani. Ilifanyika tu kwamba baada ya wewe kututumia kadi ya kutualika turudi, utakuwa unafundisha siku iliyofuata. Nilimsomea Alan kadi hiyo, na jibu lake lilikuwa kusema, "Tunaenda kesho."*

*Ninashukuru sana kwa kujitolea kwako kwa kondoo waliopotea au waliopotoka. Tulikuwa tunatangatanga kwa muda. Tulikuwa tukisoma Biblia zetu kwa uaminifu lakini tulikosa mwongozo. Darasa la uanafunzi ni mahali pazuri kwetu kwa wakati huu, na tunafurahia vipengele vyote vya nyumba yetu ya kanisa.*

*Tunakupenda na tunamshukuru Mungu kwa ajili yako na msukumo wako wa kuwavuta wengine kuwa na uhusiano wa kina na Bwana wetu.*

*Mungu akubariki!*

*Alan na Martha*

*Chic na Nancy,*

*Wow! Huu ni mwaka mzuri sana ambao Mungu ametubariki. Mnamo Januari mwaka 2019, Alan alifanyiwa upasuaji wa moyo; Februari, akarudi kwenye maabara ili awekwe bomba; mwezi Julai, alirudi tena kwenye maabara kuwekwa mabomba mawili; na uwepo wa Mungu umekuwa nasi wakati wote. Hali ya yeye kuwa hajavuta sigara tangu Januari 23, 2019, ni muujiza ambao ni Mungu pekee angeweza kutimiza.*

*Tunawashukuru nyote na darasa la shule ya Jumapili kwa kusimama nasi katika haya yote kwa maombi na chakula na kadi. Mungu ni mwema sana, na tunajisikia kuwa tumebarikiwa sana.*

*Wako wapendwa,*

*Alan na Martha*

Alan na Martha wamepatikana; wamerudi; kondoo wawili wamerudi. Wamekuwa viongozi wa kiroho wenye nguvu—na kuna shangwe hapa na mbinguni.

# Utiifu na Uhodari

*Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi?*
*2 Wakorintho 6:14*

*Basi, kusudieni mioyoni mwenu, kutofikiri-fikiri kwanza mtakavyojibu; kwa sababu mimi nitawapa kinywa na hekima ambayo watesi wenu wote hawataweza kushindana nayo wala kuipinga.*
*Luka 21:14–15*

Ndiyo, maisha yaliyojazwa na Roho yatahitaji mara kwa mara utiifu kwa Mungu, na Roho huyohuyo atakuwezesha uwe na ujasiri wa kutii!

Nilizidi kukosa raha kutokana na uamuzi nilioufanya katika mwaka wangu wa pili chuoni. Sasa, katika mwaka wangu wa kwanza, nikiwa mfuasi mchanga wa Yesu, uamuzi huo uliendelea kunijia na kunisumbua.

Nilikuwa nimejiunga na kundi liitwalo Greek letter. Sasa, nilikuwa nahisi lazima nitoke kwenye kundi hilo! Kulikuwa na sababu tatu za uamuzi huu:

- Shirika hili la siri lilikuwa linanidhibiti kwa kiasi fulani. Nilihisi nimefungwa nira isivyo sawa.
- Nilitakiwa kulipa ushuru wa kawaida wa jamii. Pesa hizo zilikuwa hasa za kununulia pombe. Hata hivyo, nilihisi nimeguswa kuacha kunywa pombe.
- Maamuzi mengi katika kundi hilo yalitokana na ubaguzi na chuki.

Nilipomwendea makamu wa rais kumjulisha kuwa nataka kujiuzulu kutoka kwenye hicho kikundi, aliniambia hilo halikuwa chaguo langu. Ningelazimika kuutetea uamuzi wangu mbele ya Baraza la Muungano wa Vikundi.

Basi tarehe iliwekwa. Baraza hili lilikuwa na wanachama kumi na wawili au kumi na wanane - nusu yao walikuwa marais wa kundi hilo, nusu yao walikuwa wa kitivo na ambao walikuwa wamewekeza sana kwa wanachama wa kikundi. Nilikuwa nimeandika barua iliyohitajika kwa baraza nikiomba kuruhusiwa kujitoa kutoka kwenye kikundi changu "kwa sababu ya imani yangu ya kidini." Nilipokuwa chumbani kwangu, nikijaribu kujitayarisha kiakili kwa ajili ya mkutano huu wa baraza, nilikuwa na woga. Je, wanachama

hawa wa baraza wangeitikiaje nitakaposema, “Ninajiondoa kwenye kikundi kwa sababu nimekuwa Mkristo”? Niseme nini?

Nilikuwa nikisoma Maandiko nilipoona kifungu ambacho sikuwa nimewahi kukiona hapo awali: “Basi, kusudieni mioyoni mwenu, kutofikiri-fikiri kwanza mtakavyojibu: Kwa sababu mimi nitawapa kinywa na hekima.” Nilihisi kwamba sikupaswa kutayarisha hotuba badala yake nimtegemee Roho wa Mungu kunipa maneno ya kusema.

Baada ya muda mfupi, nilikuwa nimeketi katika chumba cha kusubiria nje ya milango mizito ya mwaloni ya mkutano wa baraza la makundi mbalimbali. Muda kwa mkutano ulikuwa umepita kwa dakika ishirini na tano, na nilihisi kuwa mwoga sana.

Ghafla, Bwana akaingia chumbani. Alionekana kuwa na ndoo kubwa ya amani ambayo aliimimina moyoni mwangu. Pamoja na hayo, ule woga wote ulitoweka mara moja.

Wakati huo huo, milango ya mwaloni ilifunguliwa, na msemaji akasema, “Bw. Shaver, tuko tayari kwa ajili yako.” Na nilikuwa tayari kwa ajili yao.

Wale wanachama wa baraza waliponiomba nieleze kwa nini nilitamani kutoka kwenye kikundi, nilisema nilikuwa nimempata Kristo kama Mwokozi na Bwana wangu, na sasa nilikuwa ninajali sana masuala ambayo hayakuwa yakinisumbua hapo awali. Basi wale wanaume waliojitolea kabisa katika kikundi walikasirika na wakanifokea. Hatimaye wakasema, “Unaweza kuondoka. Tutakujulisha baada ya siku chache ikiwa tutakuruhusu kujitoa katika kikundi.”

Siku chache baadaye, nilipokea barua iliyonipa ruhusua ya kujitoa kwenye kikundi.

Baadaye, katika mwaka wangu wa mwisho chuoni, mnenaji mzuri sana kutoka InterVarsity Christian Fellowship alipangiwa kutembelea chuo chetu. Niliwasiliana na ndugu zangu wa zamani kwenye kikundi na kuwaomba kama wangependa mtu huyu anene nao kuhusu maana ya Ukristo. Nao wakakubali—kwa masharti kwamba ningeandamana na mnenaji na kusimulia hadithi yangu mwenyewe ya jinsi nilivyompokea Kristo. Nilifanya hivyo!

Yesu aliahidi kwamba wsingeweza “kupinga au kukataa.” Wasingeweza! Alinipa ujasiri wa kuwa mtiifu!

# Nguvu ya Injili

*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye,*
*Warumi 1:16a*

Paulo hakuwa mdhaifu wa kiroho. Tambua ujasiri wake: "nawiwa" (Warumi 1:14), "ni tayari" (kif. 15), na "siionei haya" (kif. 16). Hii ilikuwa ni kwa sababu injili ilikuwa na nguvu ya ajabu.

Roy na Doris Baker walikuwa mfano wa leo wa nguvu hizi. Katika sehemu kubwa ya maisha yake, Roy alikuwa mpinzani mkubwa wa dini. Na bado alifanikiwa sana, kwa kupata shahada ya PhD huko Harvard na kazi ya uprofesa wa uhasibu katika Chuo Kikuu cha Missouri-Kansas City.

Roy na Doris walitembelea kanisa moja na kuanza kuuliza maswali. Marafiki zao wapya wa Kikristo walipowatembelea nyumbani kwao na kushiriki nao injili, walivutiwa. Mgeni mmoja aliwafafanulia ule msamaha uliotajwa katika Isaya 53:6: "Bwana AMEWEKA juu yake makosa yetu yote."

Alisema, "Roy, Doris, nini kitatokea kwa dhambi zangu? Zote zimewekwa juu ya Kristo. Nimesamehewa na niko huru."

Roy na Doris walipiga magoti yao, wakalia, na kuziacha dhambi zao, na kumfungulia Kristo mioyo yao. Walikua, na kudhihirisha hali waliyopokea kutoka kwa Mungu, na wakawa viongozi kanisani.

Baadaye Roy aliponena baadaye katika darasa la seminari, mwanafunzi mmoja aliuliza swali akasema, "Dr. Baker, je, ni ukweli gani alionena Dr. Shaver ambao ulikushawishi?"

Roy alijibu akasema, "Yesu alinifia!"

Hii ndiyo injili: "nguvu ya Mungu iletayo . . . wokovu."[26]

26. Awali kilichapishwa katika *Reflecting God* Juni–Julai–Agasti 2010 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 19. Imetumiwa kwa ruhusa.

# Jihusishe

*Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, Habari Njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa mhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake.*
*Waefeso 1:13-14*

Wanandoa wanaposimulia hadithi zao, moja ya nyakati kuu za uchumba wao daima ni wakati wa kuvishana pete. Baadhi ya matukio ya kuvishana petehutokea baada ya kutembea kwenye bustani nzuri; nyingine hufanyika kwenye maeneo ya kuvutia zaidi katika jiji; nyingine hata hutokea kwenye viwanja vya riadha mbele ya maelfu ya mashabiki. Mara chache tukio husahaulika.

Katika Kigiriki cha kisasa, neno "amana" ni neno lilelile la "pete ya uchumba." Ulipotiwa muhuri na Roho Mtakatifu aliyeahidiwa, akawa amana yako ya kitu bora zaidi cha kufuata. Kama vile pete ya uchumba ni ahadi ya kitu bora kufuata (ndoa), hivyo Roho Mtakatifu ni ahadi ya kitu bora zaidi kitakachokuja-karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo mbinguni.

Wazo hili la kutia muhuri pia linaonyeshwa katika 2 Timotheo 2:19: "Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama, wenye mhuri huu: Bwana awajua walio wake. Na tena, Kila aliitaye jina la Bwana na auache uovu." Ujumbe hapa ni umiliki na utakatifu. Kama umejaribiwa kuwa na mashaka na uhusioano wako na Mungu, kumbuka Matendo 15:8-9, ambayo inazungumzia suala la mataifa kujazwa Roho. Kujazwa huku kulithibitisha kwamba Mataifa vilevile walikubaliwa na Mungu: "Na Mungu, ajuaye mioyo ya watu, akawashuhudia, akiwapa Roho Mtakatifu vilevile kama alivyotupa sisi; wala hakufanya tofauti kati yetu sisi na wao, akiwasafisha mioyo yao kwa imani." Hata ikiwa huelewi kina kamili cha moyo wako, Mungu anajua. Matokeo ya matendo yake katika mioyo yetu ni usafi, umiliki, na utakatifu. Roho anapokutia alama kwa mhuri, anakufanya ufanane na Yesu zaidi.

Mhudumu mmoja aliwahi kumlalamikia E. Stanley Jones kwamba kutajwa kwa Roho Mtakatifu kulimfanya aingiwe na baridi kali; aliogopa kwamba kujadiliana kuhusu Roho kungesababisha hisia nyingi kwa washirika. Jones alijibu, "Rafiki yangu, unamfananisha Roho Mtakatifu na watu fulani

ambao wamevuka mpaka katika suala hilo. Kristo ndiye kielelezo chetu. Alijazwa zaidi na Roho Mtakatifu kuliko mtu ye yote aliyewahi kuikanyaga dunia hii. Je, unaogopa kufanana na Kristo?"[27]

Roho Mtakatifu ndiye arabuni yetu ya kwenda mbinguni. Wakati Dan, mwanafunzi wa chuo niliyemjua, alipojazwa na Roho Mtakatifu, alisema, "Loo, kama mbinguni ni kitu kama hiki!"

Ni kana kwamba Mungu anakuambia, "Mwanangu, siwezi kukuleta mbele yangu kwa sasa. Nina unayotakiwa kuifanya kwanza: kuishi kwa sifa ya utukufu wangu. Lakini nitafanya jambo linalofuata ambalo ni bora zaidi. Nitakupa uwepo wangu katika nafsi ya Roho Mtakatifu, naye atakaa na kuishi ndani yako—atakuwa hapo usiku na mchana, katika ugonjwa na afya, katika furaha au katika huzuni. Siwezi kukuleta mbinguni bado, lakini nitaiweka mbingu kidogo ndani yako."

**MACHI 11** **70**

## Bwana, Unipe Maji Hayo

*Yule mwanamke akamwambia, "Bwana, unipe maji hayo,*
*nisione kiu, wala nisije hapa kuteka."*
*Yohana 4:15*

Alitembea chumbani, mikono ikiwa nyuma yake. Alimwambia rafiki yake, "Oh, Bwana Judd, Mungu amenifanya niwe mtu mpya! Mungu amenifanya niwe mtu mpya!" Hudson Taylor kwa muda mrefu amekuwa Mkristo na mmishonari mwenye bidii nchini China, lakini hivi majuzi alikuwa ameshuhudia hali mpya ya kiroho.

Chini ya shinikizo la kazi yake, Taylor alipokea nuru mpya kutoka kwa Bwana: "Lakini yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi *hataona kiu milele*" (kif. 14). Kufikiria kwamba "*hataona*" linamaanisha *hataona*, kwamba "milele" linamaanisha *milele,* na kwamba "kiu" linamaanisha *hitaji lolote ambalo halijatoshelezwa*! Kuanzia siku hiyo na kuendelea, kulikuwa na nguvu mpya katika huduma ya Taylor, kulikuwa na imani kuu katika maombi yake, na pumziko kubwa zaidi katika nafsi yake.

27. Kumbukumbu za mahubiri, chanzo chake hakijulikani.

Si ajabu yule mwanamke Msamaria alimsihi Yesu akisema, “Bwana, Unipe Maji Hayo.” Sisi sote tuna kiu: kiu za moyo, kiu za nafsi, kiu za akili. Kwa hivyo yeye pia alikuwa na kiu. Bado alikuwa anachanganya mambo ya kimwili na ya kiroho (kif. 15), lakini alikuwa akimwomba mtu anayefaa kumpatia mahitaji ya maisha yake. Ikiwa unaendelea kunywa kutoka kwenye chanzo katika Yesu, “utaona kiu milele.”[28]

MACHI 12 **71**

# Usitende Dhambi—Itakuwaje Ukitenda?

*Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba- Yesu Kristo mwenye haki.*
*1 Yohana 2:1*

Kukata nyasi za bustani, hiyo ilikuwa kazi yangu. Nilikuwa na umri wa miaka kumi au kumi na miwili, na nyasi bado zilikuwa za kijani. Siku moja, nilikusanya safu za majani ili yaje yachukuliwe. Baba yangu kisha aliwasha moto kuzichoma kwa haraka zile safu za nyasi. Nilikasirishwa sana na kitendo hiki hadi nikamfokea na kumwadhibu vikali. Sitasahau kamwe sura yake—jambo la kuvunja moyo. Ningewezaje kumfanyia hivyo baba ambaye alinipenda sana?

Kisha kuna Baba yetu wa mbinguni. Hebu fikiria jinsi anavyohisi tunapomwasi, tunapomtenda dhambi. Yohana anasema, “ili msitende dhambi” (2:1), na anasisitiza jambo hili kabisa: “Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi” (3:6). Baadaye, anaandika na kusema, “Atendaye dhambi ni wa Ibilisi... Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi” (3.8).

Yesu alimponya yule mtu aliyepooza pele kwenye Birika la Bethesda na akamwamuru, “Angalia, umekuwa mzima, usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi” (Yohana 5:24). Kusema wazi, Yesu alidhani anaweza kuacha kutenda dhambi-vinginevyo mtu huyu alikuwa sasa chini ya laana mbaya. Mimi na wewe hatuhitaji kutenda dhambi.

---

28. Awali kilichapishwa katika C*ome Ye Apart* Machi–Aprili–Mei 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 33. Imetumiwa kwa ruhusa. (Chapisho hili liligeuka kuwa*Reflecting God*.)

Lakini ukitenda dhambi-oh hapa kuna rehema za ajabu: Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba-Yesu Kristo" (1 Yohana 2:1). Ikiwa utamwasi au kutompendeza Bwana, simama hapo ulipo na umwombe Mungu akusamehe, akurejeshe, na akutie nguvu umfuate. Kristo atakuombea msamaha. Ndiyo maana tuna hii ahadi: "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu" (1:9).

Siku moja nilipokuwa nikiendesha gari kwenda nyumbani, nilijisemea, "Oh, nimesahau kuwaita watu mbele waokoke."

Nikamsikia Mungu akisema, "Utukufu wangu sitaugawa kwa mtu yeyote."

Basi nikatubu kiburi changu, na Mungu akanisamehe.

Nikiongea na mke wangu kwa ukali, kwa haraka humwomba Mungu na Nancy wanisamehe.

Mtume Petro alimkana Bwana na akatenda dhambi. Alisamehewa na kurejeshwa kisha akaja kuwa kiongozi mkubwa, mwenye nguvu, mtakatifu wa kanisa hilo changa. Mungu bado anatoa msamaha wa aina hii—Nilimwona akimfanyia hivyo mtu ninayemjua ambaye alimfuata Kristo, akarudi dhambini kwa miaka ishirini, kisha akatubu, na akarejeshwa upya, na sasa ni mtumishi wa Mungu leo.

**MACHI 13** **72**

# Mungu Analijua Jina Langu

*Haya ndiyo majina ya wanaume watakaokusaidia; Wa Reubeni; Elisuri mwana wa Shedeuri. Wa Simeoni; Shelumieli mwana wa Suri-shadai. Wa Yuda; Nashoni mwana wa Aminadabu.*
*Hesabu 1:5–7*

Musa na Haruni walikuwa watu wenye majina makubwa katika tendo la kimuujiza la Mungu la kuwakomboa Israeli kutoka Misri na kuwaanzishia safari yao ya jangwani kwenda nchi ya ahadi. Ilikuwa mwezi wa pili wa mwaka wa pili tangu Waisraeli watolewe utumwani Misri (1:1). Mungu anazungumza na Musa na kumwambia awahesabu wanaume wote wenye umri wa miaka ishirini na zaidi ambao wanaweza kuhudumu katika jeshi. Kwa kuwa hii ni kazi kubwa, Bwana anamtajia Musa wanaume kumi na wawili ambao watasaidia katika kazi hiyo. Kundi hili la wanaume mahususi linajumuisha

Elisuri, Shelumieli, na Nashoni. Wanapomaliza kuhesabu, wanapata kuna wanaume 603,550 wenye uwezo wa utumishi wa kijeshi.

Jambo hili lilinishangaza mwanzoni, kwamba kati ya wanaume 603,550, Mungu alitaja wanaume kumi na wawili mahususi, na hata akamwambia Musa majina ya baba zao. Elisuri, Shelumieli, na Nashoni kati ya watu 603,550—hebu fikiria hilo. Wanaume hawa hawakuwa maarufu kama Musa au Haruni, lakini Mungu aliyajua majina yao.

Katika Luka 10:20, Yesu anawaambia wanafunzi sabini na wawili miongoni mwa wafuasi wake, kwamba, "Furahini kwa kuwa majina yenu yameandikwa mbinguni." Hitimisho pekee linalowezekana ni kwamba Bwana anajua jina *lako* pia.

Wakati wowote watu wanapouliza mwanangu, Paul, jinsi anavyoweza kufanya kazi baada ya kufanyiwa upasuaji wa saratani mara tano na kuondolewa kwa koromeo lake la sauti, ananukuu maneno ya wimbo ambao una maana sana kwake: "He knows my name, he knows my name-Anajua jina langu, anajua jina langu." Wakati mwingine, ananukuu maneno ya wimbo mwingine maarufu: "His eye is on the sparrow, and I know he watches me-Macho yake yamtazama shomoro, na ninajua ananilinda."

Analijua jina lako. Ndiyo, jina lako!

**MACHI 14** **73**

# Hatimaye

*Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, ishini vivyo hivyo katika yeye; wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani.*
*Wakolosai 2:6-7*

*Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka.*
*Mathayo 24:13*

Tom na Agnes walijua kwamba walipaswa kufanya jambo fulani—kuongezeka kwa shinikizo la Wakomunisti katika hali ya kisiasa ya Guyana ilikuwa ikiyafanya maisha kuwa magumu sana huko. Mpango wao ulikuwa kuwachukua watoto wao wanne na kwenda nao Marekani. Hata hivyo, serikali iliwekea vizuizi kuondoka kwao—watoto hao wawili wakubwa wasingerushishisiwa kuondoka. Kati ya rasilimali zao zote, Tom na Agnes waliruhusiwa kubeba

$400 pekee na kila mtu kubeba sanduku moja. Walipata nyumba katika Jiji la Kansas, wakapanda basi, na wakatembea mwendo uliosalia na kukwea hadi kanisani.

"Tunakaribishwa hapa?" Waliuliza.

Yule aliyetusalimia akasema, "Mnakaribishwa sana!"

Tom na Agnes walianza kuzoea maisha ya kanisa, na kanisa liliwaombea kwa ajili ya watoto wao wawili wakubwa walioachwa huko Guyana. Mwaka mmoja baadaye, mnamo Julai 7, 1978, watoto wote wawili waliingia kanisani pamoja na wale watu wengine wa familia yao—na kanisa likapiga makofi!

Je, historia ya familia hii ya kishujaa ilikuwa ni ipi? Acha nikusimulie kisa cha Agnes. Bibi yake alitaka kumlea awe Mhindu. Baba yake akasema, "Haiwezekani!" Alianza kuhudhuria kanisa la Wesley karibu na nyumba yake huko Guyana. Akiwa mtoto, alimpokea Kristo na kujiunga na kanisa. Baba yake alipofariki na mama yake akaenda kazini, Agnes mwenye umri wa miaka kumi na miwili alibeba majukumu makubwa na akaacha shule ili awatunze wadogo zake sita.

Kwa maisha yake yote, Agnes alimtumikia Kristo. Akiwa na umri wa miaka themanini na tisa, Agnes alipokaribia mwisho wa maisha yake, mwanawe wa kiume alisema, "Baba na Mama yangu ndio waliokuwa daraja letu la kutufikisha kwa Yesu."

Agnes alisali kila asubuhi, wakati wa kula chakula, na kila usiku. Kama ulikuwa na kitu chochote kilichokuwa kikikusumbua, Agnes alikuhimiza uombe. Mtoto wake wa kiume aliyekuwa mtu mzima alipokufa ghafula, Agnes hakuonyesha uchungu wala kumlaumu Mungu kamwe. Alihudhuria mahafali ya chuo kikuu ya mjukuu wake huku akiwa dhaifu, kwenye kiti cha magurudumu, bila kulalamika.

Afya yake ilipodhoofika na kuhamia kwenye makao ya wazee, Agnes alisema, "Hapa ndipo ninapopaswa kuwa." Siku chache kabla ya kifo chake, alikuwa akirudia kusema, "Nampenda Yesu," na akiomba kwa bidii, aliomba maombi ya upako kwa ajili ya mchungaji wake na kanisa.

Je, unapata taswira? Alisimama kidete hadi mwisho. Haya ndiyo maisha ya Kikristo yanayofundishwa na Biblia.

# Kanisa Lenye Upendo wa Kutosha wa Kuwachangamsha

*Na Sauli alipofika Yerusalemu, alijaribu kujiunga na wanafunzi, nao walikuwa wakimwogopa wote, wasisadiki ya kuwa yeye ni mwanafunzi. Lakini Barnaba akamtwaa, akampeleka kwa mitume. Akawaeleza jinsi alivyomwona Bwana njiani,na ya kwamba alisema naye, na jinsi alivyohubiri kwa ushujaa katika Dameski kwa jina la Yesu.*
*Matendo 19:26-27*

*Na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.*
*Waefeso 3:19*

Karibu tumpoteze. Sauli, ambaye baadaye aliitwa Paulo, alikuwa amempokea Bwana, lakini kanisa la Yerusalemu lilikuwa linamwogopa—na bila sababu yoyote. Kabla hajakutana na Yesu, alikuwa akiwakamata Wakristo na kuidhinisha kuuawa kwao. Basi mtu mmoja mwenye upendo mwingi na hekima alimwendea Sauli na “kumpeleta” kwa wale mitume. Basi kwa kuwa alihisi anapendwa na kukubaliwa, alibaki kanisani. Hatimaye Sauli (Paulo) huyu alikuja kuwa kiongozi wa vuguvugu la Kikristo. Matendo 14:21–22 inasema, “wakarejea mpaka Listra na Ikonio na Antiokia, wakifanya imara roho za wanafunzi na kuwahimiza wakae katika ile imani.” Basi Paulo alikuwa bingwa wa ufuatiliaji, unawirishaji, na msaada.

Siku za kwanza katika huduma yangu, mwinjilisti Modie Schoonover alinifundisha kujiuliza hivi: Je, kanisa langu lina upendo wa kutosha wa kuweza kuwachangamsha? Kama vile mtoto mchanga anavyohitaji kuangaliwa, kupendwa, kutunzwa kwa njia maalum, hivyo ndivyo kanisa jipya linavyohitaji. Niliyaona haya yakitimizwa kwa jinsi Dan na Judy walivyoishi.

Dani alilelewa katika nyumba ya wachungaji, lakini alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili, alikuwa akivuta sigara; kufikia miaka kumi na sita, alikuwa na uchungu na chuki. Alipomuoa Judy, alimwonya asithubutu kuwa Mkristo. Dan alipokuwa jeshini, mama yake aliugua sana, na akamtuma Judy amfariji. Judy alishangaa kuona mazingira ya upendo katika nyumba hiyo ya wachungaji. Alienda kanisani na wakwe zake Jumapili na akaokolewa.

Dan alikasirishwa na habari hiyo. Baada ya kutoka hospitali, walihamia mji wa Midwester huko Marekani. Muda mfupi baadaye, Judy aliugua na akagundua kwamba alikuwa na uvimbe. Kwa hofu, aliwaita wazazi wa Dani wamwombee. Katika chumba cha upasuaji, daktari alimchunguza Judy kabla ya kumkata na kusema kwa mshangao, “Saratani tuliyokuja kuiondoa tayari imetoweka.” Dan aliposikia taarifa hiyo, alikiri kuwa ilikuwa jibu la maombi, na hakujua kwa nini alikuwa na uchungu sana.

Dan na Judy waliamua kwenda kanisani Jumapili hiyo. Lakini watu wa kanisa walikuwa na shughuli nyingi wakifurahia ushirika wa marafiki zao wa zamani wa Kikristo na hawakuwaona Dan na Judy. Waliketi peke yao. Watu wachache waliwasalimia; hakuna aliyewaalika kwa ajili ya chakula cha jioni cha Jumapili. Dan alishangazwa na jinsi kulivyokuwa hakuna urafiki. Wiki iliyofuata, walijaribu kwenda kuabudu katika kanisa lingine. Walikwenda kutafuta kanisa lenye watu wachangamfu na hawakupokewa vizuri.

Basi marafiki zao kadhaa waliwatia moyo, wakajaribu kanisa lingine lililowasalimia kwa furaha. Kufikia siku ya Ijumaa, washirika wawili waliokuwa mtu na mkewe waliwatembelea nyumbani. Mchungaji alipowatembelea, Dan alijivunia upendo wa kanisa hilo. Jumapili iliyofuata, walirudi, na Dan alipanda madhabahuni, huku akiwa analia machozi. Mchungaji alipomuuliza kama alikuwa amesamehewa, alijibu na kusema, “Niliomba msamaha mara moja tu.”

Baadaye, Dan alimpigia simu baba yake na kumwambia, “Nimekutana na rafiki yako wa zamani.”

“Ni nani huyo?”

“Bwana Yesu Kristo.”

Jumapili uliyofuata, Dan na Judy walitakaswa. Jumapili iliyofuata baada ya hiyo, walijiunga na kanisa. Baada ya hilo, waliwaleta marafiki katika kusanyiko la Billy Graham. Na baada ya hayo, kanisa lilikuwa na mkutano wa uamsho—walihudhuria ibada zote isipokuwa moja.

Siku za baadaye, wandoa wageni walijitokeza. Mara moja, Dan na Judy walikuwa karibu nao, wakiwakaribisha nyumbani kwao. Walikuwa wamekuwa kanisa lenye upendo wa kutosha wa kuchangamsha.

# Roho Wa kubadilisha Moyo

*Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda.*
*Ezekieli 36:26-27*

Bill alikuwa amedhohofika na mnyonge sana. Hatimaye, ilibidi ifanyike—upasuaji wa moyo. Siku chache zilizopita, niliketi kando yake wakati wa kiamsha kinywa na kuiona nguvu yake, mawazo yake kamili na maongezi, furaha yake mpya ya kuishi. Tofauti kubwa iliyosababishwa na upasuaji wa moyo.

Nabii wa Agano la Kale Ezekieli alisema Israeli walilitia unajisi jina kuu takatifu la Mungu. Kwa sababu ya dhambi zao, walikuwa wametiwa mateka Babeli. Lakini sasa Mungu aliahidi kuwatwaa kati ya mataifa, na kuwakusanya na kuwatuoa katika nchi zote, na kuwarudisha katika nchi yao. (Ezekieli 36:24). Walihitaji kupata mabadiliko moyo na kuishi ndani ya roho ili jambo hili litendeke. Utashi wao haungetosha; msamaha wa Mungu unaoondoa hatia ya dhambi za zamani haikutosha. Ndani yao, mioyo yao ingebadilishwa. Roho atakaa ndani yao ili awaongoze kutii.

George alitoa ushuhuda wake wa kuwekwa wakfu kwa ajili ya huduma:

> Daima, nilijihisi nina hekima kuliko mtu yeyote yule. Kwa hivyo, hakuna mtu angeweza kunihubiria. Hali hii ilikuwa imezama ndani sana kiasi kwamba sikuweza kuhisi nipo hivyo. Lakini huwezi kumpenda mtu kama Yesu anayopenda unapojiona kuwa wewe ni bora kuliko wao.

Kisha, akaelezea kuhusu utakaso wake: "Ikiwa Mungu asingefanya hivyo, kanisa hili lingekuwa limeharibika. Ilinibidi niwe mtumishi; nilihitaji kukaa muda mrefu ili niuone ushindi. Kwa kweli Bwana ananimiliki."

Alitafutwa na Roho. Akatakaswa ili ahudumu. Moyo mpya.

Msomaji, ukiwa katika safari yako ya kiroho, je, utaufungua moyo wako kwa ajili ya mabadiliko ya Roho Mtakatifu?

# Viungo Vinafanya Kazi

*Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo.*
*1 Wakorintho 12:12*

*Akawaambia, Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu. Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata.*
*Mathayo 4:19-20*

Bill na Irene walimjua Laura kutokana na uhusiano wa kazini. Lazima walimwalika Laura na mumewe, Keith, kanisani mara nane kabla ya mwaliko wa "kanisa na chakula cha mchana" kukubalika. Kisha mtu kutoka kanisani alimpelekea Kethi na Laura biskuti zilizo tengenezwa nyumbani kwao. Kiongozi wa watoto alipendezwa na mtoto wao, Andy, alianza kuhudhuria Shule ya Jumapili. Mwalimu wa Shule ya Jumapili ya Watu Wazima alimwalika Keith na Laura kwenye darasa la watu wazima na kubaki baada ya ibada kwa ajili ya chakula cha kuletwa na kila mtu.

Marafiki wapya kutoka kanisani waliwatembelea Keith na Laura kwa miadi na kujadili masuala ya kiroho yaliyosababisha Keith na Laura kuanza kuwaza kwa kina. Walihidhuria mafuzo ya Bibilia kuhusu Injili ya Yohana, ambapo Mungu alizungumza na Laura walipokuwa wakisoma kuhusu yule mwanamke kisimani.

Tarehe 28 Agosti, mmoja wa wachungaji kanisani, pamoja na Scott na Angie, walihubiri injili nyumbani kwa Keith na Laura, na wote wawili walimkubali Kristo. John na Helen waliwaongoza kwa wiki nane ya mafunzo ya *Basic Studies for New and Growing Christians* kuwakuza. Baada ya kuongozwa na washirika, Keith na Laura walijiunga na kanisa.

Keith alianza darasa la uinjilisi lililofaadhiliwa na kanisa. Alifanya urafiki na mfanyikazi mwenzake Marta na mume wake, Waynard, akashiriki injili na wao na kuwaongoza kwa Kristo. Hatimaye walijiunga na kanisa.

Leo hii, Keith na Laura ni viongozi wa kiroho kanisani kwao kwa sababu viungo vingi vya mwili wa Kristo katika kanisa hilo vilifanya kazi kwa pamoja kutangaza injili, kukuza na kufunza.

# Manukato yako Hewani

*Basi wakamwandalia karamu huko; naye Martha akatumikia; na Lazaro alikuwa mmojawapo wa wale walioketi chakulani pamoja naye. Basi Mariamu akatwaa ratili ya marhamu ya nardo safi yenye thamani nyingi, akampaka Yesu miguu, akamfuta miguu kwa nywele zake. Nayo nyumba pia ikajaa harufu ya marhamu.*
*Yohana 12:2-3*

Nilikuwa nikihubiri katika kanisa moja kule Bedford-Stuyvesant huko Brooklyn, New York, ambapo waumini wengi walikuwa watu wa visiwa—kutoka Trinidad, Bahamas, Barbados, Jamaica. Karibu kila mwanamke alikuwa amevaa kofia. Na kusanyiko lilikuwa likiimba daima!

Mchungaji alikuwa akiwaendesha wanawake wanne na mimi kurudi nyumbani kwetu wakati ambapo mwanamke mmoja alisema, "Aaah, Ndungu Shaver, mahubiri yako ni kama chapa kutoka kwenye chupa ya manukato." Sikuwa na uhakika wa kile alichokuwa akimaanisha, lakini nadhani ilikuwa sifa nzuri.

Katika maandiko ya leo, Yohana anaelezea mandhari ya chakula cha jioni pamoja na Yesu ambapo harufu ya manukato ilijaa hewani. Yesu alikuwa anaelekea kufa msaalabani—lakini wakati huo, ulikuwa wakati wa kufurahia mapumziko makubwa yenye kuinua ya kijamii.

Fikiria juu ya vipengele vyote. Chajio, iliyotayarishwa na Martha, kwa heshima ya Yesu. Lazaro, karibu na Yesu, anyejulikana sasa kwa sababu alifufuliwa hivi karibuni kutoka kwa wafu. Watu waliokuja kumwona Lazaro (12:9).

Katika shuguli hii yote, Mariamu, kwa ishara kuu ya upendo, aliitwaa ratili ya marhamu ya nardo safi yenye thamani nyingi, akampaka Yesu miguu. Hata kwa heshima ya Yesu, furaha juu ya Lazaro, karamu kubwa, ushirika mchangamfu, na manukato mazuri, uovu ulishindwa. Yuda Iskarioti alilalamikia kuhusu kutumiwa vibaya kwa marhamu yenye thamani nyingi, lakini kifungu kinatuonyesha tabia yake ya kweli inasema kuwa alikuwa akiiba kutoka kwenye hazina (12:6).

Kuna mafunzo katika haya yote. Pamoja na mahitaji ya maisha ya kila siku—pengine pia mahitaji ya huduma ya Kikristo—tunahitaji kutenga

wakati wa kufurahia na kusherehekea. Furahia, pumzika na mwinue Yesu! Tunapaswa kumheshimu Yesu; kupata ushirika wa mlo; kufurahi ushahidi wa neema na miujiza ya Mungu, kama Lazaro. Tunafaa kutoa upendo wetu kwa wingi. Na hata ingawa uovu hunainua kichwa chake kibaya, haturuhusu hilo lizuie sifa na furaha yetu. Rafiki Mkristo, hakikisha unajumuisha matukio kama haya.

Nilimaaliza mazungumzo kwa simu na Kasisi Jack Hamilton. Amekuwa mpweke kidogo baada ya jirani yake na ndugu yake mpendwa kufa, Dkt. Jim Hamilton, akiwa na umri wa tisini na nne. Jack alikuwa mwalimu wa shule ya umma na mwinjilisti aliyefanya mikutano zaidi ya 250 ya uamsho katika majimbo ya Missouri na Kansas peke yake. Jack ana miaka tisini na tisa sasa.

Kwenye mazungumzo yetu, tulizungumza kuhusu Bwana, kanisa, familia, nyakati za kale, na ushindi wa sasa. Nilijifunza zaidi kuhusu Jack kwa dakika ishirini na tano zaidi ya vile nilivyo mfahamu. Tulifurahia; tulitiwa moyo. Kulikuwa na harufu ya manukato isiyo ya kwaida kwenye mazungumzo yetu.

Ikiwa unafikiri kupumzika huku kwote, kukumbuka, na kufurahia si cha kiroho cha kutosha, nakukumbusha juu ya Ufunuo 19:7 na 9: "Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-kondoo imekuja, na mkewe amjiweka tayari . . . . Heri walioalikwa katika karamu ya arusi ya Mwana-kondoo!"

MACHI 19 **78**

# Janga hadi Ushindi

*Nanyi kweli mlinikusudia mabaya, bali Mungu aliyakusudia kuwa mema, ili itokee kuokoa taifa kubwa, kama ilivyo leo.*
*Mwanzo 50:20*

Tarehe 28 Aprili 2020, kati ya umri wa miaka themanini na nane na tisini na moja, Mincaye alikufa nyumbani kwake katika kijiji cha Ecuadorian. Aliishi na mke wake, watoto kumi na watatu, na wajukuu zaidi ya hamsini. Mtu huyu, aliyezaliwa katika tamaduni yenye dhulma ya msitu wa mvua ya Amazon mashariki ya Ecuador, alijulikana ulimwenguni kwa sababu maelfu ya mia ya watu walimwona kama udhihirisho wa nguvu za Mungu za kuokoa na kubadilisha.

Mincaye alikuwa mmoja wa wapiganaji sita waliowachoma mikuki wamishenari Nate Saint, Jim Elliot, Pete Fleming, Roger Youderian, na Ed McCully wakafa kwenye mto wa sandar mwaka 1956. Karibu vyombo vyote vya habari vilitangaza mauaji hayo kama janga kubwa. Je, tukio kama hili lingewezaje kusababisha ushindi?

Katika maandiko ya leo, Yusufu, aliyekuwa waziri mkuu wa Misri, anawaambia ndugu zake waliomuuza utumwani, "Nanyi kweli mlinikusudia mabaya, bali Mungu aliyakusudia kuwa mema." Mungu alimtumia Yusufu kuwapa ndugu zake na familia zao chakula na mali wakati wa kiangazi. Kwa maneno mengine, Mungu alimtumia Yusufu kutimiza uokoaji wa maisha ya watu wengi. Ndugu zake walimtakia mabaya, na Mungu aliyakusudia mema.

Baada ya mauaji hayo ya watu watano, wake na wanafamilia ya wamishenari waliouawa walirudi kwenye kabila hilo. Hatimaye, baadhi ya watu wa kabila hilo walimjua Yesu Kristo. Maisha mapya ya Mincaye ndani ya Kristo yalikuja kuonekana katika *End of the Spear*, kitabu kilichobadilishwa kuwa filamu. Filamu hiyo imefasiriwa katika lugha za robo moja ya watu duniani.

Mincaye, aliyeweza tu kuhesabu hadi ishirini (akitumia vidole vyake vya mikono na miguu), alitangaza neno kote Marekani na Canada kwa umati mkubwa wa watu elfu arobaini na tano. Kwa mara nyingi alisema, "Tuliishi kwa hasira, chuki na kuua bila sababu, mpaka walipoleta ishara za Mungu. Sasa, sisi tunaoishi kwa njia za Mungu tunaishi kwa furaha na amani."

Steve Saint, mwana wa mmoja wa wamishenari waliouawa, amekuwa msafiri wa mara kwa mara wa Mincaye. Anasema, "Nimemjua Mincaye tangu nikiwa kijana mdogo, aliponipa hifadhi na wana wake kunifunza kufyatua risasi kuwinda. Alikuwa mmoja wa marafiki zangu wa dhati duniani. Ndio, alimuua baba yangu, lakini alinipenda mimi na familia yangu." [29]

Ndio, "ulinikusudia mabaya, bali Mungu aliyakusudia kuwa mema." Imekuwa zaidi ya miaka sitini sasa tangu mauaji hayo, kwa hivyo tukumbuke kumpa Mungu muda ili atimilize sehemu ya mwisho ya sentensi: "Bali Mungu aliyakusudia kuwa mema."

Je, umetazama na kusikiliza kwa muda wa kutosha kuona mema ya Mungu?

29. Steve Saint, "Remembering Mincaye: Obituary for Mincaye," ITEC, itecusa.org/mincaye/.

# Hali

*Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yoyote niliyo nayo. Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yoyote, na katika mambo yoyote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa. Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.*
*Wafilipi 4:11-13*

Wakati Ralph aliiacha kazi nzuri na kukubali mwito kuwa mchungaji, alilichukua kanisa dogo ambalo lilikuwa likikutana katika karakana ya magari mawili iliyorekebishwa. Hali yake ilibadilika, lakini aliridhika.

Peter alitoka katika maisha yake ya kila siku na kuanza kumhudumia mke wake aliye kuwa mgonjwa sana. Hali yake ilibadilika, lakini aliridhika.

Rachel alitoka katika kufurahia ndoa yenye furaha hadi kuomboleza kifo cha mapema cha mume wake. Hali yake ilibadilika, lakini ajifunza siri ya kuwa radhi.

Scott alitoka katika kuhudumia kanisa nzuri iliyostawi kwenye jiji zuri la Marekani hadi kuanza kuhudumu kama mishonari kwa mataifa manane yenye uvutano wa kikomunisti na wasio Wakristo. Hali yake ilibadilika, lakini aliridhika.

Mtume Paulo alifungwa gerezani kwa sababu ya kumhubiri Yesu, na katika kifungu hapo juu, analiandikia kanisa alilolipanda huko Filipi. Huku amefungwa minyororo na ulinzi mkali. Hangeweza kuwaponyoka—lakini kwa upande mwingine, hawangeweza kwenda mbali naye. Kwa hivyo Paulo aliwashuhudia kuhusu Kristo, na walinzi wengi walimfahamu mwokozi. Paulo hangeweza kutoka nje kuhubiri, lakini alikuwa na wakati mwingi wa kuandika barua kwa makanisa yake. Kwa kweli, barua hizi baadaye zilikuwa zikawa sehemu kuu ya Agano la Jipya.

Wakati wa huduma kuu ya Paulo huko Listra, palikuwa na mtu mmoja, asiyeweza kutumia miguu yake na aliyekuwa kiwete tangu kuzaliwa kwake, aliponywa, alirukaruka, na akaanza kutembea. (Matendo 14:8-10). Paulo mwenyewe alikuwa mgonjwa, “nilipewa mwiba katika mwili” alivyo iita (2 Wakorintho 12:7). Kwa mara tatu alimsihi Mungu aiiondoe. Lakini Mungu hakumponya, alimwambia Paulo maneno hayo: “Neema yangu yakutosha;

maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu" (12:9). Kwa neema, katika hali hii, aliridhika, hata akapata ushindi. Hata gerezani, akiwaandikia Wafilipi, alipata sababu ya msingi ya kutosheka kwake kama, "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu" (Wafilipi 4:13).

Bi. Dutcher alikuwa mwanamke aliyebatizwa aliyemcha Mungu alikuwa maelazwa kitandani. Lakini alikuwa mchangamfu, mwenye furaha, na alizidi kuwa katika huduma ya uombezi. Siku moja, aliniomba nimpigie simu kijana mmoja aliyekuwa akimwombea. Chuck alikuwa gerezani, lakini Bi. Dutcher aliamini kuwa alikuwa amemkubali Kristo. Nilimpigia Chuck, tukaelewana, na tukaanza mafunzo ya masomo ya Bibilia. Alikua, akishi maisha ya kumcha Mungu akiwa gerezani, akawaleta wengine kwa Kristo, na mwishowe akafunguliwa. Kwa ripoti ya mwisho, alikuwa anaelekea Chuo cha Bibilia kusomea huduma.

Samuel na Gladys walikuwa wenyeji wa England na Wales lakini walitumia muda mwingi wa maisha yao kama wamishenari huko Marekani Kusini, wakati wa uwakilishi wao nchini Marekani, waliishi karibu na mtaa wetu, na tukawa karibu nao pamoja na watoto wao watatu. Baada ya wao kustaafu, tulizidi kuwasiliana nao.

Niliposikia kuwa Samuel amefariki, nilimpigia simu Gladys. Kuonyesha huruma yangu, niliuliza, "Unaendeleaje katika hali hii?"

Kwa lafudhi yake ya Kiwelsh, alisisitiza, "Aaa, Ndugu Shaver, siko chini ya hali, niko juu ya hali zote!"

Inawezekanaje? Katika Kristo atutiyaye nguvu.

**MACHI 21** **80**

# Ikiwa Unaamini

*Na yoyote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea.*
*Mathayo 21:22*

Binti yetu, aliyelelewa kanisani, alitalikiwa na mume wake na akaaingilia maisha ya ulimwengu. Mke wangu na mimi tulianza kuwa na vidonda vya tumbo na moyo uliovunjika kwa wakati mmoja. Kwa miaka mitano tuliomba na kushuhudia harakati za kiroho lakini hakuna kurudi kwa njia ya wazi kwa Kristo na maisha mapya.

“Kuwa na imani” au “amini” ni masharti yaliyotajwa sana kwa maombi kujibiwa kwenye Agano Jipya. Je, jitihada zangu za kibinadamu ya imani au kuamini ni yote yaliyopo? J.G. Morrison alikuwa akifunza kuwa zaidi ya imani yenye kuokoa na imani ya kutakasa, pia kuna imani ya kutimiza. Kwa hii, alimaanisha imani anayotumia Mungu kutimiza miujiza zaidi ya mahitaji yetu kibinafsi ya kiroho.

Kuna mafundisho mengi kwenye Maandiko kuhusu kumngoja Mungu na kuwa na wakati mbele zake katika maombi. Mambo haya humruhusu Mungu kufanya kazi ndani yetu. Imani ni zawadi ya Mungu pia ni uwezo ambao mwamini lazima kuutumia. Katika Mathayo 21:22, kifungu “na yoyote mtakayoyaomba katika sala mkiamini mtapokea,” inasisitiza haja ya kuwa na imani. Katika 1 Wakarintho 12:9, Imani ni zawadi kutoka kwa Mungu kupitia Roho.

Katika barua kwa Theophilus Lessey, John Wesley pia natupa ufahamu wa muhimu: “Tunapoomba mtu kuamini, tunamaanisha, *Kubali hiyo imani ambayo Mungu yuko tayari kutoa*. Kwa kweli, kuamini ni kitendo cha mwanadamu, lakini ni zawadi ya Mungu. Kwa kuwa hakuna aliyeamini amini isipokuwa Mungu kumpa uwezo.”[30]

Siku moja, baada ya miaka mitano ya kumwombea binti yangu, Mungu alimsaidia kuwa na imani, na niliona maono ya binti yangu akienda madhabahuni kuomba. Ilikuwa kweli kiasi kwamba nilikimbia juu kumwambia mke wangu, “Nimemwona Rachel akiokoka.”

Usiku huo, nilipokea simu kutokaa kwa binti yangu aliyekuwa akilia, “Baba,” alisema, “nimekuwa nikisikiliza hadithi yako ya uongofu, na kwa nusu saa iliyopita nimekuwa nikiomba na kukiri dhambi zangu. Kristo amerejea moyoni mwangu, na Mungu amekuwa wa kweli kama alivyo sasa usiku huu.” Alikuwa tofauti tangu siku ile na ni mfuasi wa Yesu mpaka sasa.

---

30. John Wesley, *The Works of John Wesley* (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House, nd), XIII, 136.

MACHI 22 **81**

# Nitakuwa Mwaminifu Hata Kufa

*Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji la uzima.*
*Ufunuo 2:10*

Ilikuwa siku ngumu zaidi ya maisha yangu ya Ukristo. Baba yangu alinikasirikia kwa kuwa mfuasi kamili ya Yesu Kristo. Labda ni kwa sababu sikuwa nimeelezea vizuri maisha yangu mapya. Labda ilikuwa kutokana na maisha yake yasiyo ya kumcha Mungu. Au labda yalikuwa masikitoko yake kuwa nisingeweza kutimiza ndoto *yake* ya maisha yangu—kwamba ninaweza kuwa daktari au wakili.

Bila shaka, shinikizo aliloweka juu yangu ilikuwa kubwa sana. Hakunihudumia kifedha nilipokuwa nikimaliza mwaka wa mwisho katika shule ya msingi, akijua ya kuwa hakuna njia ambayo ningeweza kupanya fedha za kutosha kutumia katika shule yangu ya upili ya gharama kubwa ya Ivy League. Alimwambia rafiki mmoja kuwa heri niwe mhalifu kuliko niwe Mkristo. Aliajiri timu ya kisheria ya mume na mke, wote wasiomwamini Mungu, waniweke katika kipindi cha mahojiano makali na kuthibitisha kuwa haiwezekani kwa mwanadamu kumjua Mungu.

Mawakili hawa wawili walinialika nyumbani kwao kwa ajili ya chakula cha jioni cha minofu ya nyama. Walikuwa marafiki wa baba yangu, hivyo nilidhani nilialikwa kwa ajili ya njioni nzuri ya kutangamana. Walianza kunihoji kuhusiana na uongofu wangu wa ajabu. Ingawa, hawakungojea majibu yangu—badala yake, walinirushia maswali makali kwa mfululizo wakilenga kunifanya nisalimu amri, au nikanganyikiwe.

Hatimaye, mmoja wao akasema, “Unaweza kuwa kipindi cha kushangaza, lakini yote ni kisaikolojia tu.”

Kwa maneno mengine, “Ilikuwa tu hisia—haiwezi kuwa Mungu.”

Nilikuwa na wiki chache tu katika Bwana, na nilitikiswa. Tukio hili lilitendeka nilipokuwa likizoni. Siku chache baadaye, kwenye chumba changu cha chuo, nilikuwa na wakati wangu wa ibada asubuhi na Bwana. Nilikuwa bado ninasumbuliwa na maongezi makali ya mawakili wale. Nilipofikiria

kuhusu mazungumzo yangu na mawakili wale, nilisikia sauti mbaya ikisema, *Lakini yote ni ya kisaikolojia tu*.

Nilishangaa, *Je hii ni kweli? Je nimefanya makosa? Je hii ni hisia tu, ya kisaikolojia inayoinuka kutokana na tabia yangu? Je kweli huyu alikuwa Mungu? Je nitupilie mabali haya yote?*

Kisha nikasikia mnong'ono wa sauti ya upendo: *Chic, unajua kilichokutokea*.

Moyo wangu ukajibu, *Ndiyo, Bwana, ninajua kuwa ilikuwa wewe*. Niliitazama tena kifungu nilichokuwa nikisoma kwenye Bibilia yangu: "Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba" (Mathayo 7:24-25).

Moyo wangu ulifurahi. Ndiyo, niliwaza, *maisha yangu yako kwenye mwamba! Nimekuja kumjua Kristo! Mungu yuko! Nitasikia neno lako na kulifanya! Sitarudi nyuma!*

Mkutano huu na mawakili na sauti mbaya ziliweka chuma rohoni mwangu. Je ni kitu kigani kibaya anachoweza kunifanyia mtu? Kuniua. Kwa hivyo, niliamua, "nitakuwa mwaminifu hata kufa." Nitakuwa miongoni mwa umati wa Ufunuo, "Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji la uzima. "Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji la uzima." (2:10) Mwelekeo huo haujawahi kutoka ndani yangu.

**MACHI 23** **82**

# Hakimu Huyu ni Wa Haki

*Nimekutenda dhambi Wewe peke yako, Na kufanya maovu mbele za macho yako. Wewe ujulikane kuwa una haki unenapo, Na kuwa safi utoapo hukumu.*
*Zaburi 51:4*

"Wewe, Daudi, ndiwe huyo mtu," alisema nabii Nathani. Na mara moja Daudi alianza safari kwelekea kilindini mahali ambapo hakuna mtu anayeruhusiwa kuingia bila ruhusa, isipokuwa Mungu. Alienda nyuma ya ukuta wa ulinzi,

nyuma ya kinyago, nyuma ya hukumu, nyuma ya *mambo* na *wajibu* hadi mahali ambapo alisemama amevua nguo kisingizio.

Daudi hakusema, "Dhambi za baba yangu ziliwacha doa katika maisha yangu."

Hakusema, "Mimi ndiye mfalme—niko juu zadi ya kufuata sheria za Mungu."

Hakusema, "Nilikuwa mwathiriwa wake."

Hakusema, "Nasema uongo gani nitasema ndiposa Mungu aamini kuwa haikuwa makosa yangu?"

Hakusema, "Je, na wewe, Nathani?"

Alisemama tu pale, uchi kwa aibu yake, na akakubaliana na Mungu. Akaomba rehema, huruma na msamaha, akijua kuwa hakimu mwenye haki alikuwa na upendo usio na kikomo—akitambua kuwa hakuna njia nyingine ya kupokea utakaso kwa nafsi yake ya ndani.

Wakati Mungu alikuja, Daudi aliinua ishara inayosema, "Nina hatia."

Wakati Mungu aliondoka, Daudi aliinua ishara inayosema, "Nimesamehewa."

Ndani yako kabisa, ishara *yako* inasemaje?

Nancy Shaver[31]

MACHI 24 **83**

# Wakristo wa Kweli—Wafanyakazi Bora

*Ninyi watumwa, watiini hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote, si kwa utumwa wa macho, kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali kwa unyofu wa moyo, mkimcha Bwana. Lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu, mkijua ya kuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi. Mnamtumikia Bwana Kristo.*
*Wakolosai 3:22-24*

Utumwa ulikuwa taasisi iliyokuwa imeimarika katika Milki ya Roma (na mfumo tofauti kabisa na mfumo wa utumwa wa kawaida wa Marekani

31. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Machi–Aprili–Mei 1996 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 26. Imetumiwa kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

ambayo ilikomeshwa karne ya kumi na tisa). Kwa kweli, labda nusu ya idadi ya watu ya Milki ya Roma walikuwa watumwa. Watumwa wengi walikuwa watu wenye elimu ya juu ambao walitekeleza majukumu makubwa katika nyumba za matajiri, na hata kuelimisha watoto wao. Baadaye kidogo katika barua hii, mabwana wanaambiwa kuhusu jukumu lao la kuwatendea watumwa kwa haki na usawa.

Wakati huo, Ukristo ulikuwa kikundi kidogo kilichokuwa na mamlaka madogo ya ksiasa. Kadiri kanisa na ushawishi wake uliendelea kukua, hatimaye kanisa lilikuha kuwa kisababishi kikuu cha kumaliza utumwa.

Hivi leo, uhusiano katika ya utumwa na bwana wake unaweza kuwa kielelezo cha uhusiano kati ya mfanyakazi na bosi wake. Kwa hakika, Ukristo wa mfanyakazi utamfanya awe mfanyakazi bora na mwenye ufanisi zaidi. Kumfanyia bosi kazi inaoneana kama kumfanyia Mungu kazi.

Najua mwanamke Mkristo ambaye amefanyia kampuni yake kazi kwa zaidi ya miaka ishirini na mitano na ameshinda tuzo ya Rais mara mbili. Huwa anaombea na anafanya kazi na mkubwa wake na wafanyakazi wenza, kuonyesha huruma (kama hundi ya ukarimu kwa mfanyikazi mwenza anayekabiliana na saratani), na anashiriki imani yake kwa ufanisi.

Hivi majuzi, bosi wake alimwambia, “Uaminifu wao kwa hii kampuni haina kifani; ni sawana uaminifu wako kwa wafanyikazi wenzako. Wawakilishi wa mauzo wanakupenda.”

Mfanyakazi huyu alijibu, “Ni kawaida yangu kwa sababu huwa nawekeza kwa watu.”

Hivi karibuni, mwanamke huyu alipokuwa anasoma mojawapo ya mamia ya barua pepe zake, aliona mmoja kati ya wafanyakazi wenzake walimuomba msaada. Alisema angetuma barua ya haraka sana, ambayo ingekubalika. Badala yake, alimpigia mfanyikazi mwenzake simu na, kwa dakika ishirini, alimpa ushauri kamili na wa kujali.

“Je, maadaili haya ya kazi yalitoka wapi?” Nilimuuliza.

Alijibu, “Nililelewa katika nyumba ya Kikristo. Niliyaona kwa wazazi wangu.”

Nawasihi mwende na mtindo wa maisha yenu ya Ukristo kwa sehemu zenu za kazi.

Kwa muktadha wa barua ya Paulo, watumwa hawakuwa wanaruhusiwa kumiliki mali. Lakini ajabu ni kwamba, Mingu aliahidi wafanyakazi hawa wa Kikristo wenye nidhamu “ujira wa urithi kutoka kwa Bwana” (3:24). Naam, hii ni kama tuzo la Rais, lakini kubwa zaidi—ni zawadi ya Yesu.

# Mkamilifu?

*Basi ninyi iweni wakamilifu, kama Baba yenu*
*wa mbinguni alivyo mkamilifu.*
*Mathayo 5:48*

Kila sekunde tatu, bomba la jikoni kwetu lilidondosha maji. Lilikuwa na mojawapo ya hicho kishikio ambacho kingeweza kuzunguka pande zote. Upande wa kulia kulikuwa na maji baridi, na upande wa kushoto ilikuwa baridi. Unapofunga maji, usingeweza kuvuta hadi chini moja kwa moja—ungelazimika kuipigisha kona kuelekea kulia. Lakini ilitona kila wakati.

Wakati mwendeshaji wa mashine ya uchimbaji, mchimba mitaro hodari na Rafiki yangu Dave aliniambia Rafiki yake mzuri Jim alikuwa fundi wa bomba ningeweza kuweka maisha yake juu yake, nilikuwa karibu nipige kelele za furaha. Dave na Jim alikuja Jumamosi, na tuliwapatia kila kazi ya ufundi katika nyumba yetu. (Tungekuwa tumeiweka kwa muda mrefu.) Lakini kazi kubwa ilikuwa mfereji wa jikoni.

Mke wangu, Nancy, alikuwa amenunua mfereji wa pesa kiasi na vifaa vyake vyote kutoka wa jirani Lowe. Dave na Jim walifanya kazi kwa muda mrefu na kwa bidii, na mfereji mpya uliwekwa. Tuliufungua—kulikuwa na mtiririko mzuri wa maji. Lakini tulipoufunga, ulitona.

Tulirudi dukani na kununua aina hiyohiyo ya bomba katika kisanduku kipya kilichokuwa kimefungwa. Lakini tulipofungua kisanduku, tuliona bomba hilo limeharibika, kishikio kimekatika. Tulirudi kwenye duka kwa mara ya pili.

Bomba la tatu lilihitaji kazi nyingi, lakini mwishowe liliwekwa. Tuliufungua—maji yakatiririka. Tukafunga—na *halikuvuja*! Nikawaza, *hiyo imekamilika*! Halikuwa bomba la bei ghali au la kuvutia sana, lakini lilikuwa kamilifu kwa sababu lilitimiza jukumu lililoundwa litekeleze.

Haikushangazi kwamba Mungu anatuambia, “Basi ninyi kuweni wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu” (Mathayo 5:48)? Katika mstari wa 43-47, Yesu alituambia tupendane jinsi Baba anavyopenda.

William Barclay anasema, "Mtu ni mkamilifu anapogundua kusudi ambayo aliumbiwa na kutumwa ulimwenguni."[32]

Huenda wewe si mwenye talanta kubwa zaidi, mwerevu zaidi, au mzungumzaji mkuu, lakini unaweza kutimiza kusudi la upendo. Unaweza kuwa mkamilifu katika kuonyesha wengine upendo—hilo ndilo kusudi wewe na mimi tuliumbwa. Aina hii ua upendo ni wa hali ya juu, lakini kwa neema ya Mungu, tunaweza ifanya.

Hata hivyo, imekuwa siku chache—bomba halijavuja au kudondosha maji. Hiyo ni kamilifu! Nina furaha kwa sababu inatekeleza jukumu lake.

**MACHI 26** **85**

# Inaweza Kuwa Maalum Sana

*Naye akamjibu, "Fuata; kwa kuwa hakika utawapata,*
*nawe hukosi utawapokonya wote."*
*1 Samweli 30:8b*

Utambuzi wa ugonjwa wa Alzheimer huleta shida nyingi katika familia. Umeathiri familia yetu. Tunasikia mengi ya "Siwezi pata . . ." Inaogopesha moyo wako kama ni kadi yako ya mkopo.

Jumatatu moja, Nancy alinipigia simu kuniambia kwamba alikuwa anatoka dukani akielekea nyumbani. Jumamosi hio, akaniambia, "Siwezi kuona simu yangu." Tulijaribu kurudi alikoanzia safari yake. Ilikuwa imepotea tangu siku aliponipigia akiwa dukani, lakini alikuwa mvivu wa kuniambia kwa sababu hakutaka kunikasirisha. Jumamosi usiku, nilikuwa nimetafuta katika vibeti vine na kupekua kwa nyumba yote. Kadiri nilivyotafuta, ndivyo nilishikwa na wasiwasi.

Jumapili asubuhi na mapema, nilikuwa nasoma kutoka 1 Samweli. Mji wa Daudi wa Ziklag ulikuwa umeshambuliwa, na wavamizi walibeba mabibi, wana, na wasichana wa Daudi na askari wake. Daudi alitafuta mwongoza wa Mungu: "Daudi akauliza kwa BWANA, akasema, Je! Nikiwafuata jeshi hili, nitawapata? Naye akamjibu, Fuata; kwa kuwa hakika utawapata, nawe hukosi utawapokonya wote" (1 Samweli 30:8).

32. William Barclay, *The Gospel of Matthew*, Vol. I (Philadelphia: Westminster Press, 1975), 177.

Maneno haya, ukweli huu, ulikuwa na athari sana kwangu. Nikaandika katika shajara yangu, *Bwana, najihisi kama Daudi. Nancy amepoteza simu yake. Je, utaniongoza? Je, utaniambia ipo wapi? Je, utanisaidia niipate?*

Baadaye kidogo, nilipokuwa najitayarisha kuingia garini ili niende shule ya Jumapili na kanisani, nilihisi nasukumwa kutafuta katika gari yetu—ambayo Nancy aliiendesha Jumatatu. Nilitafuta katika viti vya mbele na sehemu za kuhifadhi—hapakuwa na simu. Vipi kuhusu viti vya nyumaa? Kwenye sakafu, karibu na kituo cha video, *simu ilikuwa hapo*. Nilienda na simu hiyo ndani na kumwonyesha Nancy, na sisi sote tukasema, "Asante kwa Bwana!" kitulizo kilichoje.

Ni ajabu jinsi Mungu anayeishi anaweza na atazungumza nasi na kutuongoza. Anatupatia hali ya furaha na hakikisho kuwa yupo nasi—na, kwa wakati, mwongozo wake unaweza kuwa maalumu kwa mahitaji yetu!

**MACHI 27** **86**

# SemaKwaheri Kutengwa!

*Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu.*
*Waefeso 2:19*

Sema kwaheri kutengwa!

Je, mambo hayo yanavutia? Inamaanisha hatimaye unapata mahali unapojumuishwa, unapendwa, unakubalika na kufurahiwa. Inamaanisha kuwa na maahali salama ulimwenguni—ulimwengu ambao uliona ni vigumu kuishi kwa ajili ya Mungu.

Nimeona watu wengi wakisitasita kuuliza kuhusu ushirika katika ufalme wake, kwa sababu nyingi. Wengine hawaamini wanastahili kuwa katika ufalme wa Mungu. Wengine hawajazoea kupendwa. Wengine wanaogopa kile ambacho Mungu atawaagiza wafanye. Wengine wanadhulumu wengine na kusababisha waathiriwa; wengine wenyewe ndio waathiriwa. Wengime wanaamini wanapaswa kuwa katika udhibiti wakati wote; wengine wamepoteza mwelekeo. Wengine wanakana kwamba wanahitaji chochote—hata upendo wa Mungu. Wengine huja na kuta na milango yao imefungwa na kuzuiwa. Wengine wapo katika maumivu na wanaamini kuwa hakuna kitulizo. Wengine wamekufa kiroho na hawaamini kwamba kweli wanaweza

ishi kabla ya kufa kweli. Wengine wamejawa na hasira na aibu. Wengine ni watunzaji wa ulimwengu waliochoka.

"Je, Mungu atakubalia waingie?" unauliza. Naam, ikiwa watafungua milango ya mioyo yao. Unaona, nilikuwa kama baadhi ya waliotajwa hapo juu, *akanikubalia* ndani. Kutengwa Nenda salama!

Nancy Shaver[33]

**MACHI 28** **87**

# Mbingu

❖

*Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; "kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hakuna bahari tena. .... Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita."*
*Ufunuo 21:1, 3-4*

"Hey Siri!" Nilisema. "Je, hali ya anga ya kesho ikoje?"

Akajibu, "Uwezekano wa asilimia arobaini wa mvua ya radi, kiwango cha juu cha digrii themanini na nane, na kiwango cha chini cha digrii sabini na saba."

Ajabu! Anaweza kukwambia hali ya anga ya kesho.

Vipi Ufunuo! Je, umilele wetu wa wakati ujao ukoje?

Ajabu! Ufunuo anaweza kukwambia kuhusu hali yako ya baadaye mbinguni.

Mkristo anapofariki leo, roho yake huenda kuwa na Bwana mara hiyo. Paulo alithibitisha, "Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida.... Ninasongwa katikati ya mambo mawili; ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo maana ni vizuri zaidi sana" (Wafilipi 1:21, 23). Alizidi

33. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Machi–Aprili–Mei 1996 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 28. Imetumiwa kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

kuandika, "Lakini tuna moyo mkuu; nasi tunaona ni afadhali kutokuwemo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana. Kwa hiyo, tena, ikiwa tupo hapa, au ikiwa hatupo hapa, twajitahidi kumpendeza yeye" (2 Wakorintho 5:8-9).

Baada ya hapo, siku inawadia ambapo miili yetu itakombolewa. 1 Wathesolonike 4:16-17 inatuambia kuwa, "Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele."

Mtu mmoja alipoulizwa, "Kwa nini Mungu anapaswa kukuacha uingie mbinguni?" jibu lilikuwa, "Kwa sababu nataka kumwona mama yangu tena."

Hiyo inaweza kuwa shauku nzuri, lakini simsingi wa kuingia mbinguni ambao Ufunuo inatuambia anayeingia na asiyeingia: "Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu. Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili." (Ufunuo 21:7-8).

Au, "Na ndani yake hakitaingia kamwe chochote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-kondoo." (Ufunuo 21:27).

Au, "Heri wazifuao nguo zao, ili wawe na haki ya kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake. Huko nje wako mbwa, na wachawi, na wazinzi, na wauaji, na hao waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uongo na kuufanya" (Ufunuo 22:14-15).

Ufunuo inasema kwamba mji wa mbinguni ni kama maili 1,400, marefu yake na mapana yake na kwenda juu kwake ni sawasawa; kuta zake ni dhiraa 200; malango kumi na mawili yana majina ya jamii kumi na mbili za Israeli; walinzi wake ni Malaika; msingi wake umejengwa kwa mawe yenye majina ya watumwa kumi na wawili; kuta zake zimepambwa na vitu vya dhamani; malango yake ni ya lulu; nan jia zake ni za dhahabu; ni hekalu lake Bwana Mungu na Mwanakondoo; mwanga wa mji huo ni utukufu wa Mungu. Utakuwa na maji ya uzima, na mti wa uzima, mimea kumi na miwili ya matunda, uponyaji wa mataifa, na mwanga mwangavu.

Maneno ya mwisho ya shangazi yangu Mary kabla hajafariki yalikuwa, "Ah, ah, ah, malaika, malaika, wamenizunguka!" Ah, kuna mbingu.

Roho na Bibi arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure. (Ufunuo 22:17).

# Nilicho nacho, Ndicho Nikupacho

*Lakini Petro akasema, "Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende."*
*Matendo 3:6*

Mmishenari wa Ethiopia Howie Shute aliripoti kwamba miongoni mwa watu elfu moja waliokusanyika kwa ajili ya Mkutano wa Utakatifu walikuwa Waislamu wenye shaka walioshuku nguvu za Kristo. Mchungaji alipokuwa anahubiri, Waislamu wanne walileta Rafiki yao aliyekuwa amelemaaa maisha yake yote na alikuwa mashuhuri katika jamii. Wakamlaza kwenye madhabahu. Wakati wa maombi, misuli yake iliyokufa ilikua, miguu yake ikawa na nguvu, na mtu huyo alianza kukimbia na kumsifu Mungu. Waislamu arubaini walikimbia na kuja mbele na kupaaza sauti, "Tunamhitaji Yesu."

Bado inatendeka. Nguvu za kiroho huja kwa wafuasi wa Kristo waliojitoa kikamilifu—nguvu kutoka kwa ukamilifu wa Roho (Matendo 1:8; 2:4). Kwa muktadha wa neno la leo, mtu amelemaa na anapaswa kubebwa kwenda mahali kuombaomba (3:2)—alikuwa mnyonge na asiyejiweza. Kama mifuko yao haikuwa tupu, Petro na Yohana wangempa mtu huyo pesa kwa ajili ya mahitaji yake ya siku hiyo. Lakini kwa sababu walikuwa wanawasiliana na nguvu za Kristo, badala yake walimpatia alichokuwa anahitaji zaidi, na matokeo ya muda mrefu.

Kama kawaida, uponyaji huu, tendo kama hili, linatendwa ili kuelekeza kwa Kristo kama Mwokozi. Mashahidi wameshangaa (3:10), nafasi za kuhubiri na uinjilisti zimefunguka, na watu wengi wamemkubali Kristo (4:4). Hivyo hivyo, katika nguvu ya Roho, wacha tutoe tulicho nacho (3:6).

*Imeripotiwa na Howie Shute, Holiness Summit, Colorado Springs, Colorado, Septemba 7, 2008. [34]

---

34. Awali kilichapishwa katika *Reflecting God* Juni–Julai–Agosti 2010 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 20. Imetumiwa kwa idhini.

# Alijishusha Sana

*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuko na namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.*
*Wafilipi 2:5-8*

Nilikuwa Moscow kwa wiki moja tu kuwafundisha Warusi kumi na saba, saa nane kwa siku, jinsi ya kuwa shahidi bora wa Yesu. Nilipelekwa katika nyumba ndogo ya kukaa. Nilipokuwa nafungua mizigo yangu, niliona ndoo ya takataka imejazwa uchafu. Sikujua itifaki za nyumba hizo za kupangisha kuhusu kutupa taka, kwa hivyo niliuliza mmishenari mwenyeji kuhusu ndoo hiyo. Kwa namna ya kupendeza, alipiga magoti chini na kuweka mikono yak echini, akaondoa taka kwa mikono yake na kusugua ndoo hiyo.

Ningeweza kulia. Hapa alikuwa mmshenari wa maisha yote ambaye alitoka nyumbani kwao Marekani na kujitoa kikamilifu kwa Yesu, ili kuwaleta Warusi kwa Mwokozi. Sasa, tena alikuwa amepiga magoti akisafisha ndoo yangu ya taka ili kufanya vitu viwestarehe zaidi kwa ziara yangu ya wiki moja.

Tazama Yesu Kristo, ambaye ni Mungu kweli lakini alikuja duniani kama mwanadamu; ambaye kwa hiyari yake alikwenda msalabani na kufa ili dhambi zako na dhambi zangu ziweze kusamehewa. Ili kujifananisha na wanadamu hata kikamilifu zaidi, aliangikwa kati ya wezi wawili na akafa jinsi tu walivyokuwa wanakufa. Ebu Fikiria! E. Stanley Jones alisema, "Hii inamaanisha alienda chini sana ili aweze kufikia mwenyedhambi wa chini kabisa na kumwinua mpaka kwa kiwango kisichofikirika." [35]

Alifanya hivi kwa ajili yako na mimi!

35 Eli Stanley Jones, *How to Be a Transformed Person* (New York: Abingdon-Cokesbury Press, 1951), 12.

# Akasulubiwa

*Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*
*Wagalatia 2:20*

Yesu Kristo alisulubishwa kwa ajili ya dhambi zetu. Wakristo kila mahali wanatambua ukweli huu. Lakini unajua kuwa inawezekana kwako kusulubishwa pia? Kwa kweli Paul alidai hivyo: "Nimesulubiwa na Kristo."

Katika Giriki, neno la Paul ya "Mimi" ni "Kiburi." Tunapomwelezea mtu kwa kusema, "Anajiona sana," tunamaanisha kuwa ni mbinafsi. Hivyohivyo, Paul anapotaja, "Nimesulubishwa," na marejeleo "Na uhai nilio nao sasa katika mwili," Paulo anamaanisha kwamba ubinafsi wake umekufa. Unapopitia haya, ubinafsi wako unasulubishwa lakini si sifa zako za maana—bado utakuwa na ubinafsi wako. Na sasa bado utapitia vizuizi, unyonge na majaribu. Utaishi kwa "Imani katika Mwana wa Mungu," na kufanya chaguo zilizondani ya Kristo. Paul anafichua siri ya nguvu kama hizo: "Kristo anayeishi ndani yangu." Halali wala kusinzia—anaishi.

Ikiwa unamwacha akusulubishe, utashika vitu kwa ulegevu, kwa kuwa ni vogumu kushika chochote na chembe mkononi mwako. Dennis Kinlaw anasema kuhusu kusikia mwamke anayeitwa Mary akicheza zeze kwa njia maridadi sana na kwa utukufu wa Mungu. Mary alimwelezea kwamba uhusiano wake na zeze hio siku zote hujawa wa kumtukuza Mungu.

Bwana alimwambia, "Mary, nipatie violini lako."

Akajibu, "Bwana, ndiyo nimebaki nayo pekee."

"Nipatie zeze yako."

"Lakini Bwana, ni maisha yangu."

"Najua. Nataka niwe maisha yako."

Mary alimwelezea Kinlaw, "Zeze hilo lilinimiliki. Sikulimiliki. Kwa hiyo nilimpatia Bwana. Kwa mara ya kwanza nilikuwa huru. Alinirudishia—sasa naimiliki kwa sababu ananimiliki. Na niko huru!"

Nikasulubishwa, lakini bado nina uhai kwa wingi. Matokeo ni—muziki wa kupendeza zaidi.

# Mazuri Zaidi Yatokanayo na Mabaya Zaidi

*Yese akamzaa mfalme Daudi. Daudi akamzaa*
*Sulemani kwa yule mke wa Uria.*
*Mathayo 1:6*

Mathayo anatoa ripoti ya nasaba ya Yesu Kristo, Masihi, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu, ana rudi nyuma mpaka kwa Ibrahimu, anayetii mwito wa Mungu wa kuondoka katika nchi yake na kuanzisha taifa jipya. Mathayo anaangazia Daudi, aliyekuwa mfalme mkuu wa Israeli. Hii ni muhimu kwa sababu wakati wa huduma yake, Yesu anaitwa mara kwa mara "Mwana wa Daudi."

Lakini ona anachofanya Mathayo: anaporipoti kuwa Daudi ni babake Sulemani, anabainisha kuwa mamake Sulemani alikuwa mke wa Uria. Sasa hii inakuwa mbaya sana – Mfamle Daudi alikuwa na wake wengi (2 Samweli 5:13), utamaduni ambao ulionekana kukubalika siku hiyo.

Kisha, siku moja, kutoka kwenye paa la kasri lake, Daudi akamwona mwanamke mrembo anaoga na akamtuma mtumishi amchukue. Mwanamke huyo, Bathsheba, akaja kwa mfalme, na Daudi akalala naye. Akamtuma arejee nyumbani, na hatimaye akatuma ujumbe kuwa ana mjamzito wake.

Baada ya kujua haya, Daudi akamwita mume wa Bathsheba, Uria, kutoka vitani, na kupangaa arejee nyumbani kwa matumaini kuwa ata lala na mkewe. Lakini Uria anakataa kwenda nyumbani na badala yake, pamoja na jeshi lake, akachagua kulala kwenye mkeka pamoja na watumishi wa mfalme. Daudi alimtuma Uria tena vitani na kumwamuru jemedari wake, Yoabu, amweke mbele ya watu, Uria ameuwawa. Kisha Daudi akamuoa Bathsheba, akamzaa mtoto wa Daudi. Kwa hivyo, Daudi anafanya uzinzi na kupanga kifo cha Uria.

Kwa hivyo, kama Mathayo anavyoripoti nasaba ya Yesu Kristo, kwa kweli anamworodhesha Mfalme Daudi mwenye kasoro katika ukoo, na zaidi anamtambulisha Bathsheba kama mamake Sulemani. Sababu moja ninaamini maandiko ni kweli na ya kuaminika ni kwa sababu haifichi mabaya, ukweli wa dhambi. Hii hapa ni bora kutoka kwa mbaya zaidi: Mwokozi wa ulimwengu alitoka katika msururu uliojumuisha dhambi mbaya sana. Hii inaniambia kuwa Mungu anaweza kuchukua mabaya zaidi kutoka katika maisha yako au yangu na kufanya kitu kizuri kutoka kwayo.

Mungu haichukulii dhambi ya Daudi kwa wepesi- Nambii wa Mungu Nathani alimjia Daudi kufichua dhambi yake na kumkemea (2 Samweli 12:7). Wakati wa mkutano huu Daudi mara moja anakiri, "Nimemfanyia Bwana dhambi" (12:13). Nathani akajibu kwa msamaha wa Mungu, lakini akamwambia Daudi kuwa mtoto atakayezaliwa kwake atakufa. Maombi kamili ya Daudi ya toba yameandikwa katika Zaburi 51: "Usitiri uso wako usitazame dhambi zangu na uzifutie hatia zangu zote. Ee Mungu, uniumbie moyo safi, na uifanye upya na kuidhibiti roho yangu" (kf. 9-10).

Baada ya hali hii, Daudi akamfuata Mungu kwa uaminifu. Tufikapo Agano Jipya, Petro anahubiri kuhusu Daudi na anakumbuka tathmini ya Mungu juu yake: "Nimemwona Daudi mwana wa Yese, mtu anayeupendeza moyo wangu, atakayefanya mapenzi yangu yote" (Matendo 13:22). Daudi anakuwa mfalme mkuu katika historia ya Israeli, na hatimaye, anakuwa njia ya Mwokozi wa ulimwengu.

Bora kutoka kwa mbaya zaidi!

**APRILI 2** **92**

# Alizichukua Dhambi Zetu

*Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa. Kwa maana mlikuwa mnapotea kama kondoo; lakini sasa mmemrudia Mchungaji na Mwangalizi wa roho zenu.*
*1 Petro 2:24-25*

Ilikuwa kama mzaha- nilifanya kazi wakati wote wa majira ya joto na nikahifadhi sehemu kubwa ya mshahara wangu. Katika vuli, nilirudi kwenye Chuo changu cha Ivy League kwa mwaka mwingine na kutumia yote niliyoweka kwa ajili ya masomo, karo, chumba na chakula. Bado, ilikuwa kidogo sana. Vipi kuhusu salio langu kubwa?

Subiri kidogo, nilikumbuka kuwa nilibeba hundi kubwa mfukoni kutoka kwa baba yangu. Unaona, alikuwa amefanya kazi kwa bidii na kuhifadhi kiasi kikubwa. Sasa, kwa sababu ya upendo wake mkubwa kwangu, aligharamia gharama yangu ya chuo mwenyewe ili niwe huru kabisa kifedha.

Damu nyingi ilimwagika kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Ukisoma Agano la Kale, utaona kwamba maelfu kwa maelfu ya mafahali, kondoo-

dume, wanakondoo walitolewa dhabihu kwa ajili ya ondoleo la dhambi za wanadamu. Hata hivyo, damu hii yote haikutatua tatizo la dhambi. Njia pekee ya kulitatua ilikuwa ni Mungu ajitokeze.

Hii ndio maana Mungu alimtuma Mwanawe wa kiungu. Kristo alisema, "'Nimekuja nifanye mapenzi yako'... katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu" (Waraka kwa Waebrania 10:9-10). Kafara moja, inatosha kabisa, hakuna kurudiwa. Dhambi zangu, zimeondolewa kabisa. Dhambi zangu zote zimesamehewa mara moja. Upendeleo wangu, kufia dhambi. Hatima yangu, kuishi kwa haki! Kwa sababu alizichukua dhambi zetu!

**APRILI 3** **93**

# Kuletwa Karibu kwa Damu

*Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo.*
*Waefeso 2:13*

Yesu alipoubisha mlango wangu, aliupata umefungwa kwa nguvu. Ingawa nilimtaka aingie, sikujua jinsi ya kumpa kiingilio. Sikujua jinsi ya kumruhusu aingie. Nililipitishia ujumbe chini ya mlango wenyezangu ya sifa yangu zote nzuri- sababu zote kwa nini ningekuwa mali ya ufalme na si wajibu.

Hakukuwa na jibu. Kwa hiyo, niliwasilisha orodha ya wajibu wangu, kwa nini sikustahili upendo wa Mungu, kwa nini sikustahili kuwa mshiriki wa ufalme. Inasikitisha kwamba, orodha hii ilikuwa ndefu kuliko ya kwanza. Tena, hakuna jibu.

Kwa hivyo niliita na kumuliza mtu ambaye tayari alikuwa mshiriki anionyeshe njia. Mtu huyu alinielezea kuhusu msalaba ambao Yesu alitundikwa kwa gharama kubwa binafsi na alitoa zawadi yake kuu, damu ya uhai wake, ili nijumuishwe katika familia yake.

Ulikuwa muda wa thamani nilipouliza kupitia mlangoni, "Kwa ajili yangu pia?"

"Ndiyo, kwa ajili yako pia."

Niliufungua mlango wazi, kengele zikalia, bendi ilicheza, na upendo ukaingia.

Je, unahitaji kuomba mtu akuonyeshe njia? Je, kuna mtu *anayekuomba* umwonyeshe njia?

Nancy Shaver[36]

APRILI 4 — 94

# Kuu Sana

*Na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu.*
*Warumi 1:4*

Je, umewahi kufikiri kuhusu mambo ambayo ni makuu sana? Nimefikiria machache:

- Kuendesha gari kwenye Mlima wa Mwamba kutoka Red Lodge, Montana, hadi Mbuga ya Kitaifa ya Yellowstone
- Kushuhudia milipuko ya kila saa ya Old Faithful
- Kuona nyati wa kiume akipanga kivuko cha barabara kwa dazani ya kike na watoto wao.
- Kuwasikia Wakristo wakiomba kwa lugha nyingine
- Kumwona mama yangu akiokolewa
- Kutambua neema ya Mungu katika ndoa yangu

Tunamtumikia Mwokozi mkuu, Warumi 1 inatupa picha yake. Natuichambue kwa maneno:

- "Injili ambayo Mungu amekwisha kuiahidi kwa kinywa cha manabii wake katika Maandiko Matakatifu" (Warumi 1:2). Mamia ya miaka kabla ya Kristo kuja, manabii walitueleza kumhusu.
- "Yaani, habari za Mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili" (1:3) Kristo alikuwa mwandamu kweli na, kama ilivyoahidiwa, alitoka katika ukoo wa mfalme mkuu wa Israeli.
- "Na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu" (1:4) — Roho—ambaye ni mtakatifu kweli na muumba wa utakatifu kwa wengine—anafanya kazi kwa nguvu. Kristo kweli ni Mungu.

36. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* March–Aprili–Mei 1996 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 27. Imetumika kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

- “Kwa ufufuo wa wafu” (1:4) — Ufufuo, uliothibitishwa kuwa jambo kuu la kihistoria na mashahidi zaidi ya mia tano, ulikuwa ushindi wa adui mkubwa wa wanadamu, kifo.
- “Yesu Kristo Bwana wetu” (1:4)—mioyo yetu ya jitoa kumwabudu.
- “Ambaye katika yeye” (1:5) —Mengi huja kwetu kupitia kwake, kupitia yeye tu—anatupa kile ambacho hakuna mwingine anaweza.
- “Tulipokea neema” (1:5) —Tunaweza kufikiri kuhusu hii kupitia kwa kifupisho, ambapo G.R.A.C.E. inawakilisha “God’s Riches at Christ’s Expense.” Mungu hututendea yale ambayo hatustahili—na zawadi yake inapokeleka.
- “Na utume ili mataifa yote wapate” (1:5) — Sisi ni wawakilishi wa Kristo, wenye jukumu la kuwaita wengine waje kwake.
- “Kijitiisha kwa imani” (1:5) —Inawezakana kumtii Mungu, na tunaweza kufanya kwa nguvu ya Imani—si kwa njia nyingine yoyote.

Huyu ndiye unayemjua na kumtumikia—Yesu Kristo *mkuu*, aliye pamoja nawe sasa hivi.

**APRILI 5** **95**

# Kupitia kifo hadi Ufufuo

*Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka katika wafu. Tazama, awatangulia kwenda Galilaya; ndiko mtakakomwona. Haya, nimekwisha waambia.*
*Mathayo 28:7*

Zaidi ya mara sitini nimewasikia Wakristo wenye Furuha wakiimba, “kutoka kaburini alifufuka, kwa ushindi mkubwa dhidi ya maadui wake,”[37] au nyimbo kama hiyo siku ya Jumapili ya Pasaka. Tukio hili lilikuwa la maana sana kiasi kwamba Warumi 1:4 inamwelezea Yesu kuwa ndiye “na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu na ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu.”

Kifo chako, kifo changu, kinaweza kuwa kitu cha kuogofya. Hata hivyo, Paulo anasema, “Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti” (1 Wakorintho

37. Robert Lowry, “Christ Arose” (1874), *Sing to the Lord Hymnal* (Kansas City, MO: Lillenas Publishing Co., 1993), #258.

15:26). Lakini pia, kuna jibu la mwisho: "Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo" (v. 57).

Nimemwomba Mungu ajipatie utukufu kupitia kila sehemu ya maisha yangu ya kikristo—hata katika kifo changu. Kusema kweli, nimekuwa na wasiwasi kuhusu kufa. Nimepitia changamoto nyingi katika miaka zaidi ya sitini na tano ya maisha yangu ya kikristo: kushinda changamoto za kifedha kwa maombi, kushinda magonjwa, ushindi licha ya upinzani mkali, kukombolewa kwa wale waliotawaliwa na mihadarati, upendo na amani unapokumbwa na ugonjwa wa Alzheimer na mengi zaidi. Kila mmoja kati ya ushindi huu wa zamani unanipa mwonekano wa uhakika nitakapokabiliana nazo tena.

Bali, kufa—sijawahi kupitia hali hiyo. Lakini ninakumbushwa kuhusu huyu Mwokozi aliyekuwa mwanadamu kamili— "Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa" (Waraka kwa Waebrania 2:18). Kwa kweli, Bwana "Yeye anatujua umbo letu, Na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi" (Zaburi 103:14). Kama Frances Ridley Havergal anavyosema, "anakumbuka kila wakati," na, "hatujawahi pita njia hii, lakini Bwana Yesu amepita."[38]

Ingawa sijawahi kupitia chochote ambacho kinaweza kunitayarisha kwa kifo changu, Bwana wangu Yesu mwenyewe amepitia kifo—na alifufuka. Kwa kuwa niko katika uhusiano hai naye, anatanivusha katika kifo changu: "Hatujawahi pita njia hii, lakini Bwana Yesu amepita." Je, utapokea uhakikisho huo pia?

**APRIL 6** **96**

# Ikiwa Unateseka

*Kama mimi nilivyoona, hao walimao maovu, Na kupanda madhara, huvuna yayo hayo.*
*Ayubu 4:8*

Joni alikuwa kijana mahiri, mwenye bidii. Alikuwa Mkristo kwa miaka miwili. Mambo mengi yalikuwa sawa katika maisha yake, lakini alitatizwa

38. Quoted in Mrs. Charles E. Cowman, *Streams in the Desert: 366 Daily Devotional Readings* (Grand Rapids: Zondervan, 1996), 112.

na kurejea kwa baadhi ya tabia zake za hapo awali— hasira, wivu, chuki, uchoyo— kwa hivyo alimwomba Mungu ambadilishe.

Julai 30, 1967, Joni aliruka ndani ya ziwa lenye kina kifupi, akavunjika shingo, na kupooza kutoka shingoni kwenda chini. Alianza kuwa na uchungu, kumkasirikia Mungu, na maombi yasiyojibiwa. Polepole aligunduwa kuwa, ingawa Mungu hakusababisha ajali yake, alikuwa akiitumia ili amtegeme zaidi. Alisema Mungu aliitumia ajali "kumgeuza mtoto mkaidi, msumbufu, mwasi kuwa mwanamke ambaye angeonyesha tabia ya subira, tabia ya uvumilivu, tabia ya ustahimilivu,"[39] Hatimaye, Joni Eareckson Tada alikuwa msanii aliye paka rangi kwa kushikilia mswaki kwa meno yake; mwandishi, mtetezi wa walemavu; na msemaji mkuu wa Mungu.

Lakini subiri kidogo! Je, mateso ya Joni hayathibitishi kuwa kulikuwa na dhambi ambayo haikuungamwa katika maisha yake? Hiyo ilikuwa hoja ya "mfariji" wa Ayubu, Elifazi, aliposema, "Kama mimi nilivyoona, hao walimao maovu, na kupanda madhara, huvuna yayo hayo." Kwa sababu mifugo wote wa Ayubu walikuwa wamepotea kwa siku moja kwa kufa au kuibiwa, kwa sababu watoto wake wote walikufa kwa siku moja kutoka na mporomoko wa nyumba; kwa sababu Ayubu aliteseka kwa vidonda vichungu kutoka kichwani hadi miguuni-lazima kuna dhambi ya siri inayosababisha haya yote.

Ni kweli kwamba Wagalatia 6:7 inasema, "Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna" (Wagalatia 6:7). Lakini mstari huo ni kweli tunapojumuisha umilele, si tu maisha haya. Nilihitimisha kuwa ndiyo, wote watendao dhambi watateseka— lakini si wote watesekao wametenda dhambi. Yesu alifafanua suala hili katika Yohana 9:2-3 wakati wanafunzi wake, walikuwa wanaashiria mtu kipofu, waliuliza, "Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu?"

Yesu akajibu, "Huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake; bali kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake."

Hapa kuna baadhi ya sababu zinazowafanya watu wateseke:

- *Dhambi yako husababisha mateso*. Rafiki yangu alifuatwa na mtu asiyemjua aliyempiga ngumi na kumsababishia kupoteza fahamu. Mtu aliyempiga ngumi sasa *anateseka* gerezani.
- *Dhambi yako husababisha mateso kwa wengine*. Kama kijana, mke wangu alikumbwa na mahangaiko na hisia za kukataliwa kwa sababu baba yake aliiacha familia kwa ajili ya pombe na mwanamke mwingine.

39. Imenukuliwa katika Rick Williamson, "Adult Leader," Mike Wonch, editor, Juni–Julai–Agosti 2014, Vol. 37, No. 4 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 74–75.

- Dhambi yako husababisha mateso kwa taifa au shirika. Kwa miaka mingi, tumeona mifano mingi ya suala hili kwenye vichwa vya habari, ambapo matendo ya mtu mmoja—mwanasiasa au kiongozi wa dini—yanaweza sababisha mateso kwa kundi kubwa la watu.
- *Adamu na Hawa walitenda dhambi, na ulimwengu wetu wote umekuwa ukiteseka tangu wakati huo*, Mungu akawaambia Adamu, "Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako" (Mwanzo 3:17). Pia tunauona uchungu huu unajitokeza katika Warumi 8:18–23, mstari wa 22: "Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina uchungu pamoja hata sasa." "Kwa kuwa viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu" (8:21), lakini kwa sasa, bado tunakabiliwa na vimbunga, tsunami, moto, mafuriko, tufani na mengine.

Dr. Orval Nease, kiongozi wa kanisa, alikuwa katika uchungu mwingi juu ya matatizo ambayo yalionekana hayawezi kutatulika. Anasoma Warumi 8:28 kwenye Bibilia yake: "Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake" (Warumi 8:28). Mateso yake yalikuwa makubwa sana kiasi kwamba maneno haya kuonekana kuwa kweli. Alichukua Agano lake Jipya la Kigiriki na kuusoma mstari kwa lugha yake asilia. Inasema, "Nasi twajua ya kuwa mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake." Kwa wakati huo, nuru ilionekana kwa Dr. Nease. Alifahamu kuwa si kuwa "Mambo yote hufanyika," bali, "katika mambo yote *Mungu hufanya kazi*." Mungu huweza kuchukua hata kile shetani amekituma na, akipewa muda, hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema—kwa Joni; kwa Dr. Nease; kwako; na kwangu.

**APRILI 7** **97**

# Kwa Unyenyekevu Panda Juu!

*Katika yeye tunao ujasiri na uwezo wa kukaribia katika tumaini kwa njia ya kumwamini.*
*Waefeso 3:12*

Nikiwa na Baba yangu wa mbinguni katika mahali salama tunapopaita nyumbani, ninaweza kumzungumzia naye kuhusu jambo lolote. Ninaweza kwenda kwa ujasiri kwa sababu:

Ananialika.

Ana sera ya kufikiwa kwa urahisi.

Hajawahi kusema, "usije."

Alikuwepo wakati ule.

Hajawahi kukosa wakati wa kusikiliza.

Ana orodha yangu ya "mambo ya kufanya."

Naichukua mizigo yangu (ikiwa nitaitua).

Anaganga majeraga yangu.

Ananifunza kuhusu maisha.

Sihitaji paspoti.

Sihitaji "kupita kwenda."

Sihitaji kufikia kiwango.

Sihitaji kupitia kwa karani.

Sihitaji kuwa wa maana, na mada yangu ya mazungumzo si lazima iwe muhimu.

Sihitaji mada ya mazungumzo—ninaweza kukaa na Mungu na *nitulie tu*.

Ninaweza kwenda huko kwa ujasiri kwa sababu ninajua ananipenda, na pendo lililokamili huitupa nje hofu. Nimemtumaini Mungu, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?

Nancy Shaver[40]

**APRILI 8** **98**

# Ujasiri Ni . . .

*Ndipo akawaambia, Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa;*
*kaeni hapa, mkeshe pamoja nami.*
*Mathayo 26:38b*

40. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* March–Aprili–Mei 1996 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 31. Imetumika kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

*Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniondokee;lakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe.*
*Mathayo 26:39b*

*Kisha akawajia wanafunzi wake, akawaambia, Laleni sasa, mpumzike tazama, saa imekaribia, na Mwana wa Adamu anatiwa katika mikono ya wenye dhambi. Ondokeni, twende zetu! Tazama, yule anayenisaliti amekaribia.*
*Mathayo 26:45b-46*

Yesu Kristo alinena maneno hayo yote hapo juu alipokuwa akiomba Gethsemane, akijua kwamba karibuni atakwenda kutundikwa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu.

Hapa, tunapata kuona ubinadamu wa Yesu: anahisi huzuni nyingi. Anapendelea njia rahisi, isiyo na uchungu mwingi kufanya mapenzi ya Mungu. Anaogopa. Lakini anachagua kufanya mapenzi ya Mungu licha ya unyenyekevu na uchungu: "Twendeni!"

Mtazamo huu wa aliyopitia Yesu unadhihirisha kuwa waweza kuwa karibu sana na Mungu na bado usipate kile unachoomba. Inafundisha umuhimu wa maombi wakati mambo ni magumu. Yesu anaomba maombi yale yale mara tatu mpaka anapofikia ombi la mwisho: "Mapenzi yako yatimizwe" (26:42).

Mwanzoni mwa maisha yangu ya ukristo, nilifikiri kwamba mkristo yeyote aliyejazwa roho kweli atakuwa huru dhidi ya hisia za hofu. Lakini sasa nina fasili mpya ya ujasiri. Ujasiri wa Agano Jipya si kutokuweko kwa hofu—ni kufanya kile ambacho Mungu anataka ufanye hata kama una hofu.

Yesu alihisi huzuni, na pengine hofu, lakini alichagua mapenzi ya Mungu. Pia, mtume Paulo aliyejawa na roho alisema, "Nami nilikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na kwa kutetemeka sana" (1 Wakorintho 2:3). Lakini katika mstari unaofuata, anasema kuwa ujumbe wake uliwajia Wakorintho "kwa dalili za Roho na za nguvu." Licha ya hofu yake, Paulo alifanya mapenzi ya Mungu.

Kama Mkristo mchanga, licha ya hofu yangu, nililazimika kurudi kwa bosi wangu wa zamani na kuomba msamaha kwa fitina zangu kumhusu. Licha ya hofu yangu nililazimika kukabiliana na Baraza la Udugu ili kufafanua kwa nini nilitaka kuondoka kwenye chama hicho. Hadi leo hii, inanibidi nikabiliane na hofu yangu kila ninapomshuhudia Yesu Kristo.

Kwa bahati nzuri, kuna msaada kwa sisi wenye hofu. Hata wakati wa mateso ya Yesu huko Gethsemane, Luka 22:43 inaeleza katika sentensi hii ndogo "Malaika kutoka mbinguni akamtokea akamtia nguvu." Paulo anasema

"Basi, wapendwa wangu, kama vile mlivyotii siku zote . . .utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema" (Wafilipi 2:12-13).

Kwa hiyo muwe na ujasiri licha ya hofu zenu. Fanya kile Mungu anataka ufanye.

**APRIL 9** **99**

# Yesu Yu Hai!

*Yesu akamwambia. Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini nenda kwa ndugu zangu ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu. Mariamu Magdalene akaenda, akawapasha wanafunzi habari ya kwamba, Nimemwona Bwana, na ya kwamba amemwambia hayo.*
*Yohana 20:17-18*

Kitu gani ni halisi? Kitu gani ni kweli? Ulimwengu wetu unategemea kabisa mbinu za kisayansi kiasi kwamba tunaweza kuamini kuwa mambo yanayoweza kupimwa ndiyo ya kweli. Kwenye hisabati, kuanzia hesbabu rahisi za kujumlisha hadi kanuni changamani za hisabati, tunategemea matokeo maalum. Lakini sayansi na hisabati hayatoi majibu yote ya maisha. Je, unaamini kuna kitu kinaitwa haki? Je, unaaamini upendo upo? Basi tafadhali nionyeshe mahali penye haki au upendo mwingi. Huwezi—kwa sababu vitu hivi viwili haviwezi kupimika kisayansi au kihisabati. Kotini, tunakubali ushahidi. Ushuhuda binafsi ni muhimu sana. Uamuzi hufikiwa ushahidi unapotoa uthibitisho usio na shaka yoyote.

Ukristo hutoa maelezo ya ajabu kuhusu kiongozi wake, Yesu Kristo," na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu Yesu Kristo Bwana wetu" (Warumi 1:4). Vitabu vinne vya Injili ni ripoti makini ya maisha ya Yesu Kristo na huduma yake. Injili ya Mathayo na Yohana ziliandikwa na wawili kati ya mitume kumi na wawili waliochaguliwa kwa makini na Yesu na walikuwa karibu naye sana kwa miaka mitatu. Marko alikuwa mfuasi wa Kristo na alisafiri na Paulo na Barnaba wakifanya kazi kubwa ya uinjilisti; Luka alikuwa mwanahistoria makini aliyewahoji mashahidi wenye kuyaona na kuandika historia taratibu ya Kristo (Luka 1:1-4). Baadaye vitabu

vya Agano Jipya viliandikwa na viongozi wakuu wa Kikristo waliokuwa katika uhusiano hai na Kristo na kwa uaminifu walitangaza neno lake.

Kristo aliwaeleza wafuasi wake mara kwa mara kuwa atauawa na atafufuka. Tazama Luka 18:31-33: "Akawachukua wale Kumi na Wawili, akawaambia, Tazameni, 'Tunapanda kwenda Yerusalemu, na mabo yote, Mwana wa Adamu aliyoandikiwa na manabii yatatimizwa. Kwa kuwa atatiwa mikononi mwa Mataifa, atafanyiwa dhihaka; atatendwa jerui, na kutemewa mate; nao watampiga mijeledi, kasha watamwua; na siku ya tatu atafufuka." Yesu pia aliahidi kuwatumia wanafunzi Roho Mtakatifu baada ya kifo chake, ufufuo, na kupaa ili kumshuhudia Yesu, ili awe halisi kwa watu (Yohana 15:26-27).

Msalabani, Yesu alisema, "Imekwisha," akainamisha kichwa, akaisalimu roho yake (19:30). Muda mchache baada ya hali hii, "wakaona ya kuwa amekwisha kufa," (19:33).

Waandishi wa injili wako wazi; hawafichi shauku ambayo wafuasi wa Yesu walipata. Licha ya mafundisho yake yote, Mariamu Magdalene alipogundua kuwa kaburi la Yesu lipo wazi, hakudhani yu hai. Lakini, alienda mbio akafika kwa Petro na kusema, "Wamemwondoa Bwana kaburini, wala hatujui walikomweka!" (20:2). Lakini hatimaye, Mariamu alimwona.

Tomaso, mmoja wa wale Kumi na Wawili, alikataa kuamini kuwa Yesu amefufuka wanafunzi wengine walipomwambia, "Tumemwona Bwana!" (20:25). Ni pale tu ambapo Yesu alipowatokea wanafunzi wake, na milango imefungwa, akasimama katikati, akasema, Amani iwe kwenu. Kisha akamwambia Tomaso, lete hapa kidole chako; uitizame mikono yangu; ulete na mkono uutie ubavuni mwangu, wala usiwe asiye, ndipo Tomaso aliamini (20:26-28).

Baada ya mikutano hii mitakatifu kuisha, wanafunzi wote Kumi na Wawili (pamoja na Mariamu Magdalene na wanawake wengine kadhaa) walikuwa wamemwona Bwana. Baada ya Yesu kupandishwa hadi mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, Baba na Mwana waliwamwagia Roho Mtakatifu wanafunzi 120 waliokuwa wakisali. (Matendo 2:33). Nguvu kuu za Roho Mtakatifu ziliwashukia watu wafuasi wa Yesu waliposimulia kumhusu. Baadaye, mtumishi Stefano alipokuwa anapigwa mawe, alitazama juu mbinguni na kumwona Yesu "amesimama mkono wa kulia wa Mungu" (7:56).

Sauli alipokuwa akielekea Dameski kuwatesa Wakristo ghafla, nuru kutoka mbinguni ikamwangaza kotekote. Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, Sauli, Sauli, mbona wanitesa? Akasema, U nani wewe, Bwana? Naye akasema, "mimi ndimi Yesu, unayemtesa" (9:5). Sauli akawa mtume

Paulo, kiongozi mkuu wa harakati za Kikristo duniani. Baadaye, Paulo aliripoti kuwa Kristo aliyefufuka "baadaye aliwatokea ndungu zaidi ya mia tano pamoja; katika hao wengi wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala" (1 Wakorintho 15:6).

Tunaweza kusema nini? Ni hili tu: Yesu yu hai!

Watu wawili walikuwa wakienda katika kijiji kimoja, jina lake Emau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo wa saa mbili, nao walikuwa wakizungumza wao kwa wao habari za mambo hayo yote yaliyotukia. Ikawa katika kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao. Macho yao yalifumbwa wasimtambue. Baadaye, alipokuwa ameketi nao chakulani, aliitwaa mkate, akaubariki, akaumega akawapa. Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua. Wakaondoka saa ileile, wakarejea Yerusalem, wakawakuta wale kumi na mmoja wamekutanika, wao na wale waliokuwa pamoja nao, "wakisema, Bwana amefufuka kweli kweli, naye amemtokea Simoni" (Luka 24:34).

Kutokana na ukweli kuwa Yesu yu hai, ni watu wangapi hii leo wanahitaji kuwa makini wanapojishugulisha na maisha yao ya kila siku—ili kumtazamia yule anayetutangulia katika kila hatua? Ingekuwa busara kuomba, "Jidhihirishe kwangu, Bwana Yesu."

**APRILI 10** **100**

# Kuwa na Hatima ya Kiti cha Enzi

*Yeye ashindaye, nitamridhia kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.*
*Ufunuo 3:21*

Ni nini lengo kuu na kusudi la maisha yako? Mungu ana jukumu gani na kusudi gani katika maisha yako? Kwa kipimo kamili cha tendo la ukombozi, anawatayarisha watu kuketi na Kristo kwenye kiti chake cha enzi. Unanipata? Kusudio la Mungu ni kuketi kwenye kiti cha enzi cha Kristo.

Dhambi ni kizuizi kikuu cha mpango huu. Kwa hivyo Mungu anafanya kazi kupitia katika maisha ya Kristo, kifo, ufufuo, na maombezi, na huduma ya Roho Mtakatifu kusamehe na kusafisha dhambi zetu na ubinafsi—yote hiyo tuweze kuketi pamoja na Yesu. Kukubaliana na ukweli kwamba Mungu

anafanya kile awezacho kukutengeneza na kukusafisha kwa ajili ya hatima yako.

Sikia Maneno ya Bwana juu ya ukweli huu:

Warumi 8:29: "Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi."

Waraka kwa Waebrania 2:10-11: "Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wana wengi waufikie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso. Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake."

Waraka kwa Waebrania 11:16: "Lakini sasa wanaitamani nchi iliyo bora, yaani, ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; maana amewatengenezea mji."

Waraka kwa Waebrania 13:12-13: "Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango. Basi na tutoke tumwendee nje ya kambi, tukichukua shutuma yake."

Waraka kwa Waebrania 12:10-11: "Maana ni hakika, hao kwa siku chache walituradi kama walivyoona vema wenyewe; bali yeye kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu wake. Kila adhabu wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha, bali cha huzuni; lakini baadaye huwaletea wao waliozoeshwa nayo matunda ya haki yenye amani."

Fikiria kuhusu hilo—mimi na wewe tumekusudiwa kiti cha enzi! Usikivu wetu kwa Roho Mtakatifu wa Mungu utatutayarisha.

**APRILI 11** **101**

# Nguvu ya Kusamehe

*Neno hili likapendeza machoni pa mkutano wote; wakamchagua Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho Mtakatifu, na Filipo, na Prokoro, na Nikanori, na Timoni, na Parmena, na Nikolao mwongofu wa Antiokia. Matendo 6:5*

*Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, Bwana Yesu, pokea roho yangu. Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, Bwana, usiwahesabie dhambi hii. Akiisha kusema haya akalala. Na Sauli alikuwa akiona kitendo cha kuuawa kwake kuwa sawa.*
*Matendo 7:59-60*

Inashangaza kwamba watu wanaotendewa mabaya wana nguvu ya kuwasamehe wanaowadhulumu. Stefano alifanya hivyo! Yesu alifanya hivyo! Akiwa msalabani Yesu aliwaaombea waliomsulubisha na mkutano ulioshangilia, "Yesu akasema, Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo. Wakagawa mavazi yake, wakipiga kura" (Luka 23:34).

Tunaona hii pia katika hadithi ya Jacob DeShazer, aliyefungwa gerezani na kuteswa na Wajapani kwa miaka mingi wakati wa Vita vya Pili vya Dunia, kisha akawasamehe walinzi wake. Gerezani alimpokea Yesu, alitakaswa na kujazwa Roho Mtakatifu, na kuhisi wito wa kuhubiri. Baada ya vita, alirudi Japani kama mmishenari kuhubiri kuhusu msamaha na upendo wa Kristo.

Na nguvu hii ya kusamehe bado inafanya kazi hata leo. Kathy Cagg, mwanamke aliyetakaswa na kujazwa Roho Mtakatifu, alitoa na kuupokea msamaha huo. Hadithi yake hii hapa:

> Mnamo Aprili 2007, ndugu yangu Dave alifyatua risasi nyingi kwenye Maduka ya Ward Parkway katika Jiji la Kansas, Missouri. Watu wanne walipoteza maisha yao akiwemo ndugu yangu, aliyelazimika kusitishwa na polisi.
>
> Miezi minne baadaye, sikuweza kuhisi huzuni yoyote kuhusiana na kifo cha Dave, niliweza tu kuhisi huzuni kwa aliowaua na familia zao. Nilichokuwa nikiwaza ni, *Angewezaje kuleta uchungu mwingi katika maisha ya watu wengi!* Iligharimu mkono wa Mungu kunisaidia kushugulikia hisia zangu. Nilifanya mkutano na waandishi wa habari mbele ya kanisa langu siku moja baada ya ufyatuaji. Mchungaji wangu aliomba, kisha nikatoa baadhi ya kauli nikikusudia kutoa rambirambi zangu na kuomba msamaha kwa kitendo cha ukaidi cha ndugu yangu. Mama wa mmoja wa waathiriwa wa ndugu yangu alikuwa akitazama, na kuniona nikitoa kauli hizo kwa namna fulani alianza uponyaji ndani yake.
>
> Miezi kadhaa baadaye, alizungumza na mchungaji wangu na kuomba kukutana nami. Tulikutana katika ofisi ya mchungaji, tukakumbatiana, tukalia, tukazungumza, na tukaendelea na kujitolea kwetu kwa ajili ya uponyaji wetu kwa kwenda mahali pa shambulio pamoja. Kwenye gari nyingi katika maegesho ya jengo, nafasi ilikuwa tupu ambapo binti wa thamani wa Carolee, Leslie, alipoagia dunia. Tulisimama katikati ya

nafasi hiyo tukiwa tumeshikana na kulia. Wakati wa mazungumzo yetu, alinieleza kuwa alimsamehe ndugu yangu, akijua kuwa Yesu anatuhitaji tufanye hivyo. Hadi wakati huo, sikuwa nimejiruhusu kuona kiwango cha hasira niliyokuwa nayo kwa ndugu yangu.

Mara moja, nilijua ninajukumu la kumsamehe Dave mbele yangu. Usiku huo, nyumbani kitandani, nilimwomba Mungu anisaidie nisamehe, na alifanya hivyo. Kwa miezi minne kabla ya shambulio, nilikuwa nikilala kichwa changu kikielekea kwenye miguu ya kitanda, na wasiwasi kwamba Dave angejaribu kunipiga risasi kupitia dirisha la chumba changu cha kulala. Nilifikiri, *Heri miguu yangu kuliko kichwa changu*. Baada ya shambulio, sikuweza kubadilisha nilivyo kuwa ninalala. Baada ya kumsamehe Dave, niliweza, na usiku huo nilipata usingizi bora zaidi—pumziko la amani la mtoto mtiifu!

Baada ya kugundua hasira yangu na kuchagua msamaha. Bado nilikuwa na majonzi ya kushugulikia. Ilichukua muda, na mwishowe, ilinileta mahali pa Mungu kuweka wito wa huduma katika maisha yangu ili kuongoza ahueni ya majonzi katika kanisa langu. Ni heshima ya thamani na baraka kutembea na watu katika safari yao ya majonzi hadi furaha. Msamaha mara nyingi huwa sehemu ya uponyaji wao. Msamaha ni chaguo tuna uwezo wa kufanya tunapofanya uhusiano wetu na Yesukuwa mkubwa kuliko maumivu.

Carolee alimsamehe Dave. Kathy pia alimsamehe. Hata la kustaajabisha zaidi, Carolee ambaye mtoto wake aliuawa, na Kathy, dadake muuwaji, walikuwa marafiki wazuri. Carolee aliamua kujiunga na Shule ya Jumapili ya Kathy. Ungewaona wakiketi pamoja kila Jumapili wakiwa na nuru ya Mungu kwenye nyuso zao. Walikuwa wamegundua nguvu ya kusamehe.

**APRILI 12** **102**

# Nguvu ya Ufufuo

*Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika*

*Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka katika mkono wake wa kulia katika ulimwengu wa roho.*
*Waefeso 1:18-20*

John alilelewa katika familia ya wachimba madini. Kwa siku alizokaa shuleni kwa ajili ya mazoezi ya soka, mara nyingi alifika nyumbani na kupata chakula cha jioni chote kimeliwa na famila yake.

Alikuwa mwanariadha mkuu. Alikuwa mshindi wa mpira wa kikapu katika mashindano ya mwisho wa mwaka. Alijiuanga na timu ya mbio na kupata ushindi mara tatu katika ubingwa wa wilaya: 220, 440, na kama kinara kwenye timu ya kupokezana vijiti. Katika Jimbo la Colorado alichaguliwa kwenye timu ya soka ya wanazuoni. Sasa yuko kwenye Pennsylvania Football Hall of Fame, Eastern Conference. Na kwa miaka thelathini na tatu, alifanya kazi kama mwalimu wa shule ya upili, kocha wa soka, na kocha wa miereka.

Mimi na Nancy tulikaa katika nyumba nzuri ya John na Gloria wakati wa ibada ya uamsho katika kanisa lao mahalia. Sasa John mwenye miaka themanini na nane, alinieleza kuwa, hadi shule ya darasa la tisa, alikuwa ameenda kanisani mara moja tu. Baada ya hapo, alianza kuwa na shughuli nyingi. Moja ya mambo alivyoniambia ni, "Nisaidie katika dini."

Tarehe 2 Aprili, mimi na mchungaji wa eneo hilo tulishiriki habari njema za Yesu Kristo na John. Mapema katika mjadala wetu, John alisema, "Sidhani kama ninaweza kwenda kwa Bwana kwa sababu nina shughuli ambayo sijakamilisha."

Asubuhi hiyo, John aliomba na kumpokea Yesu katika moyo wake na maisha yake. Sasa chache zilizofuata, alisema yafuatayo:

- "Ninahisi tofauti sasa."
- "Ninaweza kumkabidhi Mungu shida zangu zote."
- "Kwa sababu ya yale Bwana amenitendea."
- "Nilihisi kitu mwilini mwangu—kwenda tu kanisani haikutosha."
- "Najihisi tofauti—nafikiri nimempata—amenipata."
- "Ulinisaidia sana."

Usiku huo alitoa ushuhuda kwenye ibada wa uamsho: "Nilikuwa na futi tano inchi kumi na moja, lakini nimepungua mpaka futi tano inchi nane. Sasa najihisi futi tano na inchi kumi na moja tena—nilihisi siko sakafuni."

Siku mbili baadaye, alipokuwa anapanga safari nje ya mji, John alimwendea rafiki yake kumwomba amsaidie kumwanagalia mbwa wake, "Ray, nina kitu kizuri cha kukuambia. Mimi ni Mkristo aliyeokoka."

Mabadiliko haya yangewezekanaje? Badaa ya miaka themanini na nne, John alibadilishwa kutoka kufa katika dhambi hadi kuishi ndani ya Kristo.

Ni kwa sababu ya nguvu kuu iliyopo kwa sisi tuaminio—nguvu hiyo hiyo iliyomfufua Yesu kutoka kwa wafu. Nguvu ya ufufuo ipo kwa John, kwako, kwangu!

**APRILI 13** **103**

# Kufungasha Kwenda Nyumbani

*Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; baada ya hayo nimewekewa taji la haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake.*
*2 Timotheo 4:7-8*

Tunafungasha vitu vyetu—vitu vyote tulivyodhani tutahitaji kutumia tutakapokuwa pamoja na wanafamilia ishirini katika kisiwa chetu tunachokipenda cha Treasure, Florida. Mapema kesho asubuhi, tutaanza safari yetu kuelekea nyumbani. Kama zilivyokuwa nzuri wiki zetu mbili hapa, ninaweza kusema kwa kweli itakuwa vizuri sana kurudi nyumbani.

Mtume Paulo alipokuwa akijifungasha kwenda nyumbani kwake mbinguni, ushuhuda wake ulikuwa mkuu. Hakusema, "*Kama* nimevipiga vita vilivyo vizuri," au, "*Pengine* mwendo nimeumaliza," au, "*Nimejaribu* kuilinda imani." Bali, alisema kuwa nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda.

Paulo alipokuwa akijiandaa kwa safari yake, hakufungasha vitu vya kimwili, Badala yake, alifungasha rekodi ya yale Mungu aliyofanya katika maisha yake. Tayari alikuwa amewaeleza Wafilipi suala hili alipoandika, "Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo,na kufa ni faida . . .ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo maana ni vizuri zaidi sana (Wafilipi 1:21, 23).

Hakutakuwa na wakati au ghala la vitu vya kimwili tutakapofika mbinguni. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza, kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa paomja na Bwana milele (1 Wathesolonike 4:16–17). Wafuasi wa Bwana leo wanaokufa kabla ya kurudi kwa Kristo wataingia katika uwepo wake, kama Paulo anavyosema.

Hapana, hatutachukua vitu—kuna lengo muhimu zaidi tunapaswa kukumbuka kabla ya kwenda nyumbani mbinguni. 1 Yohana 3:2–3 inatueleza wazi, “Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini tunajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo. Na kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu.” Kwa hivyo usifungashe vitu kwa ajili ya mbinguni —hakikisha kuwa una moyo safi.

APRILI 14 **104**

# Mtakatifu Anapokwenda Nyumbani

*Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa*
*Mungu wake, naye atakuwa mwanangu.*
*Ufunuo 21:7*

Dkt. Robert Coleman, mtumishi wa Mungu mwenye neema, kiongozi wa Kikristo, na mwandishi wa *The Master Plan of Evangelism*, aliandika barua kwa marafiki mwaka 2017. Hii hapa sehemu ya barua hiyo:

> Mke wangu mpendwa, Marietta, alifariki asubuhi mapema tarehe 3 Januari.
>
> Alipoelezwa kuwa ana saratani ya kufisha miezi minne mapema, Marietta alimwangalia daktari kwa upole na kusema, “Kwa hivyo naenda nyumbani mbinguni.”
>
> Katika kipindi hiki cha kusubiri huku akiwa bado na kiasi fulani cha faraja, tunasoma tena kitabu anachopenda zaidi, *The Pigrim's Progress*, maelezo ya safari ya Mkristo kwenda mbinguni. Hujaji alipokuwa akisafiri, aliulizwa mara kwa mara alitoka wapi na anaenda wapi. Alijibu mara kwa mara alikuwa anatoka Mji wa Uharibifu na alikuwa njiani akielekea Mji wa Mbinguni
>
> Alianza safari yake kama msichana mdogo alipompenda Yesu. Imani yake ya Kikristo ya kina na ya kuvutia ilitiririka katika maisha yake kama chemichemi ya maji ya kuburudisha.
>
> Nyumba yetu ikawa mlango wa mbinguni. Ukarimu ulikuwa shauku yake, na alifanya nyumba yetu kuwa nyumba ya wageni ya kweli kwa wanafunzi, wamishenari, marafiki mara nyingi waliketi kwenye meza yetu. Kwa miaka sitini na tano, mimi na Marietta tulihudumu pamoja.

Katika miezi ya mwisho ya ugonjwa wake, nilifutilia mbali mikutano yote ili nikae naye. Alifia nyumbani mikononi mwangu. Sasa kwa kuwa hayupo, ni wakati wangu sasa kurudi kazini, kuhubiri, na kufundisha. Kwa kweli, nitamkosa Marietta karibu yangu! Wakati mwingine naweza kuhisi mguso wake laini kwenye mkono wangu. Kwa bahati nzuri, binti yangu, Angie na mume wake wanaishi umbali wa dakika kumi. Popote nilipo, kuna kitanza mbali jichoni mwangu, kwa sababu niko njiani kuelekea mji wa mbinguni ambapo kutakuwa na muungano wa ajabu tukikizunguka kiti cha enzi cha Mungu.

Asante kwa maombi yenu na ukumbusho wa upendo.

Robert Coleman

Wewe na mimi pia tunaweza kuwa sehemu ya muungano huo.

**APRILI 15** **105**

# Usiitupe! Kamwe!

*Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu.*
*Waraka kwa Waebrania 10:35*

Niliweza kusikia mmoja wa kundi la Wormwood akisema, “Yuko chini. Sidhani kama ataamka. Mshale niliomrushia ulimchoma moyo wake ndani kabisa, na wamemalizana na Mungu.”

Nilipokuwa nimelala pale katika uchungu wangu, kuchanganyikiwa na kukata tamaa, Mungu alikuja na kunichukua. Nililala kifuani mwake, na alinishikilia tu.

“Bwana, nilidhani uchungu wangu wote ulikuwa katika siku za nyuma.”

“Uchungu,” alisema, “ni sehemu ya maisha, lakini furaha pia. Simlazimishi mtu yeyote upendo wangu. Kila mtu ana uhuru wa kuchagua. Ilikuchukua muda kunichagua.”

“Ndiyo, Bwana, na wewe ni hazina yangu ya kipekee. Nina uhusiano na wewe ambao hakuna mtu mwingine anayeweza kuharibu. Kundi la Wormwood limepata mshangao leo, Bwana. Alirudi kunitafuta, na akapata nyayo zako. Je, hajui kwamba wewe huwalinda walio wako, iwe hapa chini, au juu? Ninahisi vizuri zaidi. Nadhani ninaweza kutembea sasa. Nadhani niko tayari kuganga jeraha la mtu mwingine, kumsaidia mtu kusherehekea kwa sababu amegundua upendo wako, kumsimulia mtu huyo hadithi, au . . .”

Hapo zamani, Mungu alitazama chini—na kumtuma mwanawake.

Nancy Shaver[41]

APRILI 16 **106**

# Malipo ya Mateso

*Wala si hivyo tu, ila na mfurahi katika dhiki pia; mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta subira; na kazi ya subira ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini; na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.*
*Warumi 5:3-5*

Hata mashabiki wa kawaida wa soka walifurahishwa sana na mchezo huu—timu mbili. Houston wanacheza na Kansas City—walikuwa wanaelekea kuwa washindi wa mwisho wa michuano ya Super Bowl ya mwaka 2020. Mwisho wa robo ya kwanza, Houson iliongoza 24-0.

Mchezaji mkuu kijana wa Kansas City, Patrick Mahomes, alikwenda kando na wachezaji wake. Kwa hekima zaidi ya umri wake, hakuwakemea, kuwafokea, au kukasirika. Badala yake, aliwatia moyo, aliwaunga mkono na kuwapa tumaini—wakati wote akiwa mtulivu. Alitoa changamoto kwa timu na umati kwa kusema, "Tutapigana hadi mwisho," na "Twendeni tufanye kitu cha kipekee." Mahomes alikuwa mfano wa uvumilivu na utulivu.

Kisha, kutokana makosa yao na upungufu wa pointi 24, Kansas City waliamka, wakafunga mabao manne chini ya dakika kumi na sita, na wakashinda mchezo 51-31.

Tabia zinazoonyeshwa wakati wa mchezo huo wa kulipiza zinapigwa baragumu kwenye Neno la Mungu. Mateso, yanapotumiwa na kusimamiwa kwa msaada wa Mungu, huzaa uvumilivu, ambayo huzaa tabia, ambayo huzaa matumaini. Na tumaini hili halitatuaibisha au kutukatisha tamaa, kwa sababu linatarajia tuzo bora kuliko ushindi wa ajabu wa soka. Ni kuhusu upendo wa

41. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* March–Aprili–Mei 1996 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 32. Imetumika kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

Mungu uliomiminiwa (si kudondoshwa) mioyoni mwetu (ambapo tunaihitaji zaidi) kupitia kwa Roho Mtakatifu (uwepo wa Mungu binafsi) tuliopewa sisi.

Ndio, kuna malipo ya mateso tukishirikiana na msaada wa Mungu na kuwa na tabia nzuri. Na kisha kuna malipo mengine makubwa zaidi—tumaini la utukufu wa Mungu, ambapo siku moja tutaishi katika uwepo wake wa milele mbinguni.

**APRILI 17** **107**

## Barua ya Kweli

*Mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoiandaa,*
*iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa Mungu aliye hai; si katika*
*vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama.*
*2 Wakorintho 3:3*

Barua—tunapokea mafurushi mengi. Unapenda kupokea barua za aina gani? Pengine aina inayosema:

"Tuna tukio zuri—njoo tusherekee pamoja."

"Asante, ulifanya kazi nzuri! Tusingeweza kuifanya bila wewe."

"Pole. Nisamehe."

"Tabia yako inanihuzunisha, lakini bado ninakupenda."

"Hatimaye utapata kitu kizuri katika dhoruba hii."

"Nilitaka kukujulisha: Nilikutana na Yesu wako na mimi ni mshiriki wa ufalme pia."

"Ni sawa—sote hufanya makosa. Ulijifunza nini kutokana na hili?"

"Hakuna kisichowezekana. Mungu hazuiliki. Mwamini."

"Ninajua ninaweza kukutegemea; ninajua kwa sababu umesimama kwenye mwamba."

"Je nimekwambia hivi majuzi kuwa ninakupenda zaidi ya utakavyowahi kujua?"

Ikiwa ni hivyo, ichukue barua ya Mungu. Jina lako liko kwenye kurasa zake.

"Vaa silaha zako zote leo" (Tazama Waefeso 6:13).

"Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini" (Isaya 26:3 SRUV).

Na, je, unajua kuwa wewe pia ni barua? Upendo wa Mungu, unapochorwa juu ya mioyo yetu, upo kwa ulimwengu wote kuu soma.

Nancy Shaver[42]

APRILI 18 **108**

# Kuhusiana na Moshi, Zima Moto

*Mvue mwenendo wenu wa kwanza, utu wa zamani unaoharibika, kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu;na mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.*
*Waefeso 4:22-24*

Kasisi wa shule alinikasirikia. Wanafunzi waliohudhuria ibada ya voluntary chapel mara nyingi waliulizwa kuhubiri, na aliniuliza mimi, Mkristo mchanga kabisa. Nilihubiri juu ya mstari, "Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu" (Warumi 14:17). Nilikuwa na furaha katika kuonyesha maisha yangu mapya, yaliyobadilika katika Kristo.

Kasisi alizungumza nami baada ya ibada: "Ikiwa unadhani wewe ni bora sasa kuliko ulivyokuwa hapo nyuma, wewe ni mbaya sasa kuliko ulivyokuwa hapo nyuma." Aaah! inaonekana, alikubaliana na mafundisho kuwa hata Mkristo anaweza kuwa mwenye dhambi. Nini kilichotokea kwa Mungu kutuwezesha Ya kwamba atatujalia sisi, tuokoke mikononi mwa adui zetu, "na kumwabudu pasipo hofu, kwa utakatifu na kwa haki mbele zake siku zetu zote" (Luka 1:74-75)? Hata hivyo, zaidi ya dhambi zetu za nje, kuna suala la kina zaidi.

E. Stanley Jones anashuhudia kuwa alipata wongofu wa kubadilisha maisha. Anaandika kuwa katika Kristo, "Maisha yana msingi mpya yanayozunguka kwa huo. Lakini nguvu zote za maisha na hisia hazijakusanywa karibu na Kristo. Kuna wale ambao hawasalimu amri na kukubali utii huu mpya." Kuna

42. Awali kilichapishwa katika C*ome Ye Apart* March–Aprili–Mei 1996 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 30. Imetumika kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

tamaa ambazo “zimekuwa zikishinda—zimekuwa zikishinda kwa muda mrefu.” [43]

Paulo aliwaandikia Waefeso, “Mvue mwenendo wenu wa kwanza, utu wa zamani unaoharibika, kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu na mkavae utu mpya.” Mungu anatupa changamoto twende kilindini mwa mioyo yetu kwa utakaso kamili. Tafsiri ya SRUV inaelezea mstari wa 22 hivi: “Mvue mwenendo wenu wa kwanza, utu wa zamani unaoharibika, kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya.” Nyuma ya matendo yako kuna tabia; nyuma ya vitendo, mtazamo, nyuma ya mienendo, nia; nyuma ya dhambi, ubinafsi. Kuyashinda haya, tunapaswa huchukua hatua kali—“vua”—matendo mema—“vaa utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.”

Kuhusiana na moshi, zima moto. Kuhusiana na tabia zako za zamani, vua mwenendo wako wa kwanza.

Muda baada ya kumkubali Kristo kama Mwokozi wa maisha yake, Rees Howells, mshirika wa Welsh aliyeanzisha Chuo cha Bibilia cha Wales, alikuwa na mkutano wa kina na Roho Mtakatifu. Kutokana na mkutano huo, alisema, “Ilimaanisha kila sehemu ya utu wangu ulipaswa kurejea msalabani, na angeleta maisha yake mwenyewe na asili yake mwenyewe.” [44]

**APRILI 19** **109**

# Ongeza Ushuhuda wako

*Mimi nikijishuhudia mwenyewe, ushuhuda wangu si kweli. Yuko mwingine anayenishuhudia; nami najua ya kuwa ushuhuda wake anaonishuhudia ni kweli.*
*Yohana 5:31-32*

“Wapendwa, Injili ziliandikwa na watu ambao *walidhani* Yesu alikuwa Masihi. Tunafaa kuichukulia kama *propaganda*.” Haya yalikuwa maneno ya ufunguzi ya profesa wangu wa Chuo cha Bibilia.

Maneno yake yaliitia kichefuchefu roho yangu iliyoongoka hivi karibuni. Ni ushuhuda mbaya! Kweli zaidi na kusisimua zaidi yalikuwa maneno

43 E. Stanley Jones, *Abundant Living* (New York: Abingdon, 1942), 150.
44 Norman Grubb, *Rees Howells, Intercessor: The Story of a Life Lived for God* (Philadelphia: Christian Literature Crusade, 1952), 36.

niliyosikia wiki chache zilizopita kutoka kwa mtu aliyeniongoza kwa Kristo: "Chic, mimi ni tofauti na nilivyokuwa kwa sababu nilimpata Bwana."

Kushuhudia ni kumweleza mtu mwingine kile ambacho Yesu amekutendea—kushuhudia nikuwathibitishia wote kuwa Yesu kweli yupo.

Katika kukabiliana na watu wabaya wa siku zake, Yesu alisema kuwa angejishuhudia mwenyewe, usingekuwa ukweli tosha—asingekubalika. Kisha Yesu akaanza kuwaorodhesha watu wengine na ukweli ulioshuhudia utambulisho wake. Je, ingewezekana kuwashawishi wapinzani wake?

Kwanza alimtaja Yohana Mbatizaji aliyejulikana vyema kuwa nabii siku hiyo: "Ninyi mlituma watu kwa Yohana, naye akaishuhudia kweli. Si kwamba ninaupokea ushuhuda wa wanadamu; lakini ninasema haya ili ninyi mpate kuokoka" (Yohana 5:33-34).

Pili, alitaja kazi, ishara, na miujiza aliyotenda kama ushahidi kamili: "Lakini ushuhuda nilio nao mimi ni mkuu kuliko ule wa Yohana; kwa kuwa zile kazi alizonipa Baba ili nizimalize, kazi hizo zenyewe ninazozitenda, zanishuhudia ya kwamba Baba amenituma" (5:36).

Tatu,Baba mwenyewe alishuhudia ujumbe wa Kristo "Lakini ushuhuda nilio nao mimi ni mkuu kuliko ule wa Yohana; kwa kuwa zile kazi alizonipa Baba ili nizimalize, kazi hizo zenyewe ninazozitenda, zanishuhudia ya kwamba Baba amenituma" (5:37).

Mwisho, kuna ushahidi wa maandiko: "Mnayachunguza maandiko kwa sababu mnadhani kuwa ndani yake ninyi mna uzima wa milele; na maandiko yayo hayo ndiyo yanayonishuhudia" (5:39).

Yesu alitoa shuhuda nne nzito zilizoheshimika kana kwamba alikuwa katika mahakama ya sheria. Na wasikilizaji wake waliitikiaje ushahidi huu? Aliutoa Yesu kuwahusu, "Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu, wala ninyi hamnipokei; mwingine akija kwa jina lake mwenyewe, mtampokea huyo" (5:43). Inasikitisha sana!

Kisha, shahidi mwingine akitokeza: mtu aliyeponywa akawaambia wapinzani wa Yesu, Yohana 5:15 inasema, "Yule mtu akaenda zake, akawapasha habari Wayahudi ya kwamba ni Yesu aliyemfanya kuwa mzima."

Ni raha iliyoje kuwasikiliza watu kama Jolene. Tarehe 30 Septemba, alimkubali Kristo na kusema, "Ilikuwa ya ajabu. Nilibadilika mara moja."

Akisimulia wakati ambapo Mungu aliangusha ukuta wake wa mwisho wa upinzani, Mike alisema, "Nilihisi kwamba nilihitaji kuondoka kwa watu usiku huo; na nikiwa pekee yangu saa 5:00 usiku, nilipaza sauti na kumwomba Yesu aingie moyoni mwangu." Baadaye, alisema, "Mungu amenisaidia kwa namna ya ajabu."

Shahrzad alikuwa amefadhaika tarehe 14 Aprili kwa sababu ya kodi ya mapato. Lakini wakati baadhi ya marafiki wa Kikristo walimweleza kuwa Kristo yu mlangoni mwa moyo wake anabisha, aliomba na kuufungua mlango. Alianza kufurahi na kusema, "Aah, aah. Aah, Nina amani! Nina mani!"

Alikimbia chumbani na kumkumbatia mume wake, akishangaa, "Albert, tufanye nini?"[45] Tumsaidie kujibu—nenda umwambie mtu!

Je, ungependa kujiunga na washuhudiaji?

APRILI 20 **110**

## Kusimama kwenye Ahadi

*Bali tukienenda katika nuru, kama yeye alivyo katika nuru, tunashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.*
*1 Yohana 1:7*

Kama mwimbaji mashuhuri na mcheza piano hodari, Frances Ridley Havergal angeweza kuwa na kazi ya kuvutia mbele ya umati uliokuwa unashangilia. Hata hivyo, alishawishika kuwa vipaji vyake vilikuwa vya mkopo kutoka kwa Bwana. Hivyo, kwa lengo la kushinda nafsi, aliimba tu muziki mtakatifu.

Frances alizaliwa mwaka 1836 na akaanza kuandika akiwa na umri wa miaka saba. Alisomea Uingereza na Ujerumani na mahiri katika Kigiriki na Kiebrania cha Biblia. Mwaka 1874, alienda nyumbani ambapo watu kumi walikuwa wakiiishi hapo hawakumjua Mungu wala hawakuwa Wakristo wenye furaha. Kufikia wakati aliondoka nyumbani, wote kumi walikuwa Wakristo wenye furaha. Baadaye, alijazwa na furaha kiasi kwamba hakuweza kulala. Usiku huo, aliandika "Ever, Only, All for Thee," ambayo ilikuwa sehemu ya wimbo.

Wakristo ambao hutafuta maisha ya kiroho kwa undani hupitia utakaso wa ajabu. Utafutaji wa Frances hukuwa na ajabu sana. Frances alimjua na alimpenda Mungu lakini bado alikuwa anatamani uhusiano wa kina zaidi na yeye. Hatua kwa hatua, alikaribia kile ambacho alikiita "uzoefu wa pili."

Kukumbuka tarehe 2 Desemba, 1873, Frances aliandika:

45. Sehemu za ripoti hii zimetoka Holiness Today, October 2000 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 3–4. Imetumiwa kwa idhini.

> Niliiona mara ya kwanza kwa haraka . . . Lazima kuwe na kujitoa kabisa kabla ya kuwa na heri kamili . . . Nilionyeshwa 'damu ya Yesu Kristo mwana wake husafisha kutoka kwa dhambi zote' . . . Basi yule alikuwa amenisafisha alikuwa na uwezo wa kunifanya niwe safi . . .Neno hilo moja 'kusafisha' . . . Sikuwa nimewahi ona nguvu ya hali awali, wakati uliopo unaendelea, wakati uliopo sikuzote, si wakati uliopo ambao muda ujao utakuwa uliopita. Inaendelea kusafisha . . . si kuja kwa kisima tu, bali kudumu kwenye kisima, ili iendelee kusafisha.
>
> Alimalizia kwa furaha, "Ninayaona yote na nina baraka." [46]

Kutokana na ujazo mwingi wa kiroho, aliandika mamia ya nyimbo, na maneno yake ya furaha bado yanaweza kupatikana katika vitabu vya nyimbo leo.

Huenda unasumbuka; huenda unamwomba Mungu akutakase. Unaweza kusimama kwa ahadi kwamba ataifanya – atakusafisha, kutakaswa, na kufanywa watakatifu. Jisongeze kwake unapozidi kusimama kwa ahadi zake.

**APRILI 21** **111**

# Kuteka Nyara Kila Fikra Ipate Kumtii Kristo

*Tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo.*
*2 Wakorintho 10:5*

Nina hofu kidogo nilitia ushuhuda binafsi wa Ed hapa. Hata kama hadithi yake ni chungu, inaonyesha ukombozi wa Mungu wenye nguvu na haja ya nidhamu isiyobadilika.

> Nilipelekwa kanisani kwa mara ya kwanza nikiwa na umri wa siku kumi. Baada ya hapo, utoto wangu wote, wazazi wangu walinipeleka kanisani kila wakati milango ilikuwa imefunguliwa. Nililelewa katika shule za Jumapili na nikasomeshwa katika vyuo vya Kikristo. Hata nilienda katika seminari kwa miezi kumi na nane. Nilikuwa nimeyatoa maisha yangu kwa Mungu mwaka 1966, nilipokuwa umri wa miaka kumi na nne-lakini kabla ya hapo, niliweka msingi wa uraibu wa kingono.

46. J. Sidlow Baxter, *His Deeper Work in Us* (Grand Rapids: Zondervan, 1967), 70.

Mwishoni wa miaka yangu ya ujana, nilikuwa nimeunda maisha ya kisiri. Katikati ya ndoa yangu ya kwanza akili yangu ilikuwa imepotoka kiasi kwamba chaguo langu la dhambi imethibitishwa. Tabia yangu ya ngono isiyoweza kudhibitika ilinigharamu ndoa mbili na kazi moja. Niliumiza watu wengi sana.

Mwishoni mwa msimu wa kiangazi mwaka 1992, nilikuwa na fikra za kujiua, katika juma hilo, kasisi wangu aliniitisha bunduki yangu, na tabibu wangu alijitolea kuniweka kwa hospitali ya kiakili. Lakini Mungu alikuwa na mipango mingine!

Mnamo Mei 1993, nilihudhuria mapumziko ya kumi na mbili na nikakiri kuwa nilikuwa mraibu wa ngono. Hlafu Mungu akaniongoza katika kupata uponyaji kwa njia ya makongamano ya kikanisa na mapumziko. Lakini kwa sababu nilidhani niliweza kuzidhibiti, tabia yangu ya ngono isiyoweza kudhibitika iliendelea kuongezeka.

Mnamo Juni 2000, nilihudhuria kikundi changu cha kwanza cha usaidizi wa uponyaji kutokana na uraibu wa ngono. Kwa wakati huu, nilijua sikuwa na uwezo kutokana na fikira zangu za kingono, na maisha yangu yalikuwa karibu kuharibika. Dhana yangu kuhusu Mungu ilikuwa ile ya hukumu na adhabu, vipi Mungu kama huyo angeweza kunisamehe mambo yangu niliyoyafanya. Lakini ndugu zangu katika uponyaji walinikubali na kunipenda. Niliamua kwamba wangeweza kunikubali, huenda Mungu angeweza pia.

Kupitia kundi langu la uponyaji na mahubiri ya biblia katika kanisa langu, nilijifunza kuwa Mungu wa Neno alikuwa Mungu wa upendo, neema, ukombozi na kukubali. Nilikuja kugundua kuwa alikuwa Mungu wa nafasi ya pili, ya tano, ya kumi, na ishirini. Lakini fikira zangu za kulazimisha bado zilisukuma tabia yangu ya ngono.

Mwaka wa 2001, usiku wa Jumapili kabla ya Dominika ya matawi, kasisi wangu aliongoza kanisa kwa ibada ya komunio. Vipingee vilipokuwa vinapitishwa, niliona taswira ya Kristo msalabani, na akaniambia, “Nipatie hatia zako na aibu yako.”

Baada ya miaka thelathini na tano ya uraibu wa ngono, nilikuwa na hatia nyingi na aibu kwake. Niling’ang’ana na uamuzi huo, lakini Kristo alizidi kuongea na mimi. Hakukubali—ilinilazimu nimwachie.

Wakati ambao niliweka makosa na aibu yangu kwake, nguvu za uraibu ziliondoka. Minyororo ya dhambi ilivunjwa—nilikuwa huru!

Lakini kweli nilikuwa huru? Neno linasema shetani huwinda kama simba akitafuta mtu wa kumeza. Bado anatafuta kunimeza. Bado nina

hayo mawazo na taswira katika akili—nilizitia katika akili yangu miaka mingi. Kila siku, shetani huwa anajaribu kuyatumia dhidi yangu.

Lakini neno linaniambia kwamba njia pekee ambayo naweza kumshinda shetani ni kupitia damu ya mwanakondoo na neno la ushuhuda wangu. Kristo tayari amemwaga damu yake, na neno la ushuhuda linapatikana katika 2 Wakorintho 10:4-5: "maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome; tukiangusha mawazo ya kila kitu kinachoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo."

APRILI 22 **112**

# Chaneli ya Upendo

*Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye.*
*1 Yohana 4:9*

*Na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.*
*Warumi 5:5*

*Wapenzi ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana.*
*1 Yohana 4:11*

Mama yake Bill aliaga dunia katika umri wa miaka arobaini na nne, Bill alipokuwa na miaka kumi na mitano. Mwaka uliofuata, baba yake alikufa. Dada mkubwa wa Bill na ndugu zake wawili katika nyumba yake, na katika mwaka wa kumi na saba, Bill aliendа jiji la Kansas kutafuta kazi. Alipata kazi katika kampuni ya mbao na akaenda shule ya uhasibu usiku.

Dick alifanya urafiki na Bill na akaihisi kampuni yake imwajiri Bill. Baadaye, Dick alianza kumpeleka Bill katika mikutano ya wafanyibiashara mashuhuri wa Kikristo. Katika mikutano ya mapumziko, baada ya kusikia shuhuda za mwezake, Bill alienda katika chumba chake na kuomba, "Nisamehe dhambi zangu. Nataka kuwa sehemu ya familia yako. Ongoza maisha yangu."

Kazini, Bill alimwambia Dick, ambayo hakuhudhuria mkutano kutokana na ugonjwa, kuhusu maombi yake. Kwa mwongozo zaidi, Bill aligundua kuwa amezaliwa tena.

Bill alianza katika kampuni ambapo Dick alimtafutia kazi mwaka 1966, akawa mshirika mwaka 1976, na akawa mmiliki binafsi mwaka 1986. Baadaye, kwa miaka mitatu mfulilizo, *jarida la kibiashara la jiji la Kansas* liliangazia kampuni ya Bill kama mojawapo ya bishara kumi kuu za Kansas City zinazokuwa kwa haraka. Hatimaye Bill alioa mwanamke mchamungu aliyeitwa Gwen. Mwaka 1990, baada ya miaka ya ukuaji wa kiroho, Bill alishushudia neema ya utakaso wa Mungu.

Bill ana uhusiano uliobarikiwa na Mwokozi wake unaofasiliwa na upendo:

- Upendo wa Kristo kwake (1 Yohana 4:9).
- Upendo wa Kristo ndani yake (Warumi 5:5).
- Upendo wa Kristo kupitia kwake (1 Yohana 4:11).

Bill huwekeza kwa watu, anawashauri kiroho, na anadumisha urafiki wa muda mrefu. Zaidi ya miaka arobaini iliyopita, yeye na Jim walikuwa marafiki. Kila Jim alipopata miezi miwili ya mapumziko kutoka katika kazi yake ya ubaharia, alikaa kwa Bill. Mpaka leo, huwa wanashiriki katika maombi, na Bill humtembelea Jim na mke wake mara kwa mara huko New Jersey, ambapo Jim hufanya kazi katika shule ya Kikristo.

Dave na Bill alikuja kuwa marafiki Dave alipohudhuria seminari. Walipigia wageni simu pamoja katika kanisa lao mahalia. Dave alisaidia katika kujenga nyumba ya Bill; Bill alimtembelea Dave katika uchungaji wake huko Maine; na Bill alihudhuria harusi ya Dave kwake Maybeth huko Washington. Mpaka leo, Dave anaporudi kutoka kazi za umeshenari huko Georgia (nchi ya Ulaya) ama Poland, huwa anaishi kwa Bill.

Bill alikuja kuwa Rafiki na Michael, mwanafunzi wa seminari, alipokuwa wakipigia wageni wa kanisa simu pamoja. Michael sasa ni kasisi, na Bill amemtembelea, mke wake, na watoto wao watano katika kazi ya kijeshi huko Savannah, Georgia, na Monterrey, California. Bill na Michael husaidiana katika maombi.

Bill ni upatano wa ajabu wa chaneli ya upendo wa Kristo kwa watu wengi. Wewe pia unaweza kuwa chaneli ya upendo wa Kristo.

# Kujazwa kwa Ujasiri

*Basi walipoona ujasiri wa Petro na Yohana, na kuwajua ya kuwa ni watu wasio na elimu, wasio na maarifa, wakastaajabu, wakawatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu.*
*Matendo 4:13*

*Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.*
*Matendo 4:31*

Je, umewahi tupwa katika hali isiyofurahisha ambayo ilijua kila mtu aliye karibu na wewe hakuwa na huruma katika Imani yako? Je, umewahi kutishiwa sababu ya Imani yako?

Kama umewahi kuwa katika mojawapo ya hali hizi, unajua kile Peter, John, na wafuasi wa awali walipitia kwa kumfuata Yesu. Peter na John walikutana na mwombaji kilema hekaluni, na katika jina la Yesu Kristo, aliponywa. Ghafla alipoanza kutembea, akiruka na kumsifu Mungu, mtu huyo alivutia uangalifu mkubwa katika koti ya hekalu (Matendo ya mitume 3:1-10). Peter alitumia tukio hilo kuhubiri kuhusu Yesu. Padri, kapteni wa mlinzi wa hekalu, Masadukayo walisumbuliwa sana kwa hili, na wakakamata na kutia Peter na John jela.

Siku iliyofuata, wenye mamlaka walimwomba Peter ajielezee. Peter alieneza ujumbe wa utafutaji. Kivipi? "Kujazwa na roho," Peter alitiwa nguvu kwamba wasikilizaji wake walishangazwa n aujasiri wake. Mwishowe, Peter na John walitishiwa zaidi na wakaachiliwa. Walirudi kwa wafuasi wenzao na wakasimulia matukio haya. Kundi kubwa lilienda katika maombi, na "walijazwa na Roho Mtakatifu na kunena neno la Mungu kwa ujasiri."

Iwe Mkristo anaishi katika hali ya kujazwa na roho ama anapitia kumwagiwa na kujazwaRoho, matokeo ni ujasiri. Wakati mwingine ujazo wa Roho ni wa utakaso (Matendo ya mitume 15:8-9), lakini hapa, ni wa ujasiri.

Kitambo katika maisha yangu ya Kikristo, nilikutana na suala la ujasiri. Nilikuwa katika mwaka wangu wa mwisho katika chou cha Ivy League. Kabla tu ya kurudi chuoni, nilipitia utakaso, ujazo wenye kutia nguvu wa Roho Mtakatifu. Kila mkufunzi alihitajika kuhudhuria kozi ya "suala kuu", ambapo

watu mashuhuri walikuja na kutufunza kutoka katika ustadi wao katika mada kuu katika biashara, serikali, mahusiano ya kimataifa, fedha, na dini.

Utawala ulikuwa umechagua Waziri wa muungano kuwasilisha uprotestanti. Kwa chukua Zaidi Kotoka kwenye saikolojia, aliendeleza wazo kuwa utu ni mzuri kwa kawaida. Siku iliyofuata, wanafunzi walirudi darasani na kumuuliza mzungumzaji maswali.

Katika chumba chake, Mungu alianza kunichochea: "Huwezi kuacha ujumbe wake upite bila kumpa changamoto." Nilijua kuwa siku iliyofuatia, nililazimika kumuuliza mnenaji swali mbele ya wakufunzi wote.

Siku iliyofuatia, niliuliza swali lifuatalo kwa mwasilishaji: "Je, vipi unaweza kusema kuwa ubinadamu ni mzuri kimsingi Biblia inaposema, 'Wote wametenda dhambi'; na Freud anaposema, 'Binadamu ana moyo tupu uliojazwa na uchafu'; na ambapo, katika uzoefu wangu, nilikuwa mwenye dhambi na mbinafsi mpaka nilipomweka Kristo katika moyo wangu na maisha?"

Watu katika umati walilalamika bila huruma. Mnenaji tena alijaribu kujibu swali kwa kuzingatia saikolojia.

Nakiri kuwa katika muda huo nilisimama kuuliza hilo swali, nilikuwa na hofu. Lakini nilikuwa tayari kufanya kile Mungu alikuwa ameniagiza nifanye. Ujasiri katika nguvu ya Roho—inawezekana leo.

APRILI 24 **114**

# Ndio, Ikimbieni Zinaa

*Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wezi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi. Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, Lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiswa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo na katika roho wa Mungu wetu.*
*1 Wakorintho 6:9-11*

Ingawa Steve na Jackie walikuwa wameenda kanisani mara chache, walikuja katika ibada ya asubuhi ya ufufuo siku ya Jumapili. Baada ya ibada ya usiku Jumamosi, Steve alikuja kuzungumza nami. Alisema kitu kama, "Nilifurahishwa na hadithi uliyoisema katika ibada ya asubuhi Jumapili.

Nilifikiri nimeishi maisha mazuri—sijawahi tumia tumbaku, pombe, ama madawa, lakini, kweli, naapa. Sana. Lakini nilipoapa katika kazi yangu ya ujenzi leo, nijihisi mwenye hatia sana. Angalia mikono yangu, inatetemeka tu." Nilijitolea kuomba na Steve, lakini hakuwa tayari kwa hilo. Alisema tu atarudi kwa ibada nyingine.

Steve na Jackie walirudi Jumatatu. Kati ya vitu vyote, nilihubiri huo usiku kuhusu "Watu, Ngono, na Mungu," kutoka katika 1 Wakorintho 6. Katika mahubiri hayo, nilifasili uzinifu kuwa mtu anayeishi katika uhusiano wa kingono na mwanamke ambaye hawajaoana—ambayo ilikuwa hali ya wachumba hawa.

Usiku wa Jumanne, walirudi tena. Wakati wa wito wa madhabahuni, Steve na Jackie waliungana mikono na wakasogea mbele. Nilipopiga magoti kando ya Steve, alikuwa anaomba kwa bidii. Alipaza sauti kwangu na kusema, "Dhambi zangu, dhambi zangu, zote zimesamehewa. Zimeondoka."

Nilimuuliza Steve mahali Kristo yupo, na kwa ujasiri akajibu, "Yupo moyoni mwangu."

Kwa kujazwa na furaha, Steve na Jackie walikuwa wameanza kutembea kutoka kwenye madhabahu ambapo, baada ya hatua chache, Steve alipinduka na akarudi kwangu. Akauliza, "Na hizo dhambi zingine—zimesamehewa zote pia?"

Nilijua kile ambacho alikuwa anazungumzia—mada ya mahubiri ya usiku uliopita. Nikasema, "Ndio, zote zimesamehewa pia."

"Tumekuwa tukiishi pamoja," Steve alisema. "Hatujaoana—sote tuna talaka. Ingawa tunapanga kuoana. Tayari tuna pete."

Kwa kujibu, nilimsihi Steve azungumze na mchungaji wake na amwoe Jackie mapema kadiri iwezekanavyo.

Kumbuka kile ambacho mtume Paulo alisema kwa Wakorintho: Baada ya orodha yake ya tabia za dhambi, aliandika, "Hicho ndicho wengi wenu walikuwa. Lakini mmeoshwa, mmetakaswa, mmethibitishwa katika jina la Bwana Yesu Kristo na kwa Roho wa Mungu wetu" (kif. 11). Kwa sisi sote ambao tumejihusisha na uzinzi hapo awali, tunaweza kusamehewa; tunaweza kubadilishwa; tunaweza kuwa safi; tunaweza kuwa wapya. Roho wa Mungu anaweza kufanya jambo hilo litokee. Aliwatendea Wakorintho; anaweza kututendea mimi na wewe.

Mbele yangu, nina picha ya Steve na Jackie wakitoka kwenye kanisa baada ya harusi yao. Wiki tatu baada ya maombi yao kwenye madhabahu; walifanya harusi yao inavyofaa baada ya ibada asubuhi ya Jumapili. Na tabasamu iliyoje katika uso wa Jackie!

Tangu harusi yao, Steve amebatizwa, na wote wawili wamejiunga na kanisa na kukamilisha *Basic Bible Studies for New and Growing Christians*. Sasa Steve anajifunza jinsi ya kucheza gitaa la besi ndiposa aweze kuchangia katika timu ya kuabudu.

Kwa hivyo ndio, "Ikimbieni zinaa" (kif. 18). Ikiwa unafikiria hili ni suala gumu kwako kutenda, kumbuka kwamba mwili wako ni hekalu la Roho Mtakatifu (kif. 19), na Roho huyo anakupa nguvu.



# Neema Inaonekana!

*Naye, alipofika na kuiona neema ya Mungu akafurahi, akawasihi wote waambatane na Bwana kwa moyo wote.*
*Matendo 11:23*

Neema inaonekana hadharani Mungu anapofanya jambo ndani. Wakati mwingine naweza kuona kwamba mioyo iko chini, inahofu, inaumia, inasononeka, inaficha, imeshikiliwa kwenye tumaini kiasi, au inaishi katika njia ya hatari. Nyingine imeweka chuki na ina majivuno, inataka makuu, na ina kiburi sana kuamini kuwa inahitaji Mungu. Je, hawafai kuuliza? Je, hawaoni ni jambo la maana kuuliza? Nyingi ni kuta ambazo hutufanya tuwe tumetengana na upendo wa Mungu.

Yesu anapokuja, anaondoa uchafu na ubaya wa maisha na anatupandisha kwenda utukufu. Upendo wake unatupatia maisha mapya na unaturuhusu kuishi tukijua anatupatia nguvu ya siku nyingine. Anastahili na anakufanya ustahili. Anavuta machozi yetu na anaondoa hofu yetu, kisha anacheka kwa sababu mioyo yetu imejazwa nay eye.

Nancy Shaver[47]

47. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Julai–Agosti–September 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 90. Imetumiwa kwa idhini (Chapisho hili lilikuja kuwa Reflecting God.)

# Alikuwa Mtoaji

*Nilikuwa uchi, mkanivika nilikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama;*
*nilikuwa kifungoni, mkanijia.*
*Mathayo 25:36*

Suzie alikuwa muwazi sana au karibu sana na mchungaji wake. Siku moja, katikati ya mazungumzo, alimwambia, "Je, unajua umeanza kupata upaa?" Usijali, alichukulia kama utani mzuri—ni yeye aliyesema hadithi yenyewe.

Hadithi nyingi za Suzie ziliibuka tulipokuwa tukizungumza na familia yake kuhusu ibada ya makumbusho yake. Alikuwa amefariki ghafla katika umri wa miaka sabini na miwili.

Suzie alipokuwa na umri wa karibu miaka kumi na miwili, alienda mbele madhabahuni kuomba, na siku hiyo, alimkubali Kristo. Miaka baadaye, baada ya kuolewa na kupata watoto watatu, wakati mwingi alikuwa mama wa nyumbani. Katika mkutano wa maombi, Suzie alisikia Mungu akiongea naye: "Nina vitu vingi nimeweka kwa ajili yako." Waliomjua wanasema alitakaswa katika mkutano wa maombi—labda kama huu.

Hatimaye Suzie akawa karani wa Kansas kwa ajili ya huduma za Prison Fellowship na mhudumu aliyetawazwa. Alianzisha *In His Service Ministries* na aliendesha mtandao ambao uliwasaidia wafungwa gerezani na familia zao kutafuta kazi, nyumba na ushauri.

Kwa angalau matukio kama matatu, Suzie na Rafiki yake Chaplain Vickie walinialika kuhubiri gerezani huko Lansing, Kansas. Nilishangazwa na vile walikuwa wanajua wafungwa kwa kiwango cha uhusiano binafi. Uwazi na heshima ya wafungwa hawa iliwafanya washirikiane na wanawake hawa.

Wasiwasi wa Suzie ulikuwa kwamba wafungwa wangeweza kumjua Kristo kwa namna ya uhusiano binafsi kama mwokozi na Bwana wao. Na wale ambao walikuwa Wakristo, aliwaombea na wakapata utakaso wa Mungu. Suzie na Vickie pia walihakikisha kuwa waumini wapya walijiunga na mafunzo ya Biblia ili waweze kuendelea kukua na kukomaa katika imani yao.

Mahusiano ya kifamilia ya Suzie yalikuwa ya upendo wa ajabu. Mume wake, Harry, alisema, "Alikuwa kitu chema zaidi kilichowahi kunitokea. Wakati wote anafanya jambo kwa wengine."

Kijana wake Stephen alisema, “Tuliongea kwa simu kila siku kwa miaka kumi na minane. Mama yangu alikuwa Rafiki wa dhati.”

Kijana wake Paul alizungumza juu ya furaha ya mama yake alipofanya safari ya utume kwenda Argentina.

Mwaka 2007, Suzie alipata ugonjwa mbaya wa maini. Ingawaalilazwa hospitalini aghalau mara moja kwa mwezi, hakuacha kuwa na bidii ama kuwa na huzuni. Badala yake, alitenga muda kwa wale waliokuwa karibu naye na kuwasikiliza. Alikuwa na furaha nyingi ya kutoa.

Kijana wake Stephen alisema, “Sikuweza kubadilisha wakati hata mmoja nilipokuwa nakua .”

Kijana wake Paul alisema, “Alipofariki, nilikuwa na amani, hakuna shaka kuhusu mahali alipo.”

Kwa nini tuende katika maelezo mengi vile kuhusu mtu mmoja? Kwa sababu ni muhimu kuona kile Mungu anaweza fanya kupitia maisha ya mtu mmoja. Miaka kumi na mitano baadaye alisikia Mungu akisema, “Nina vitu vingi nimeweka kwa ajili yako,” huduma ya Suzie ya gerezani ilikuwa imechanua na kuwa kamili. Mtoaji aliyeje! Je, unadhani nini Mungu atafanya kupitia maisha yako?

**APRILI 27** **117**

# Kwa Miaka Ishirini Kamili

*Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, ishini vivyo hivyo katika yeye; wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani.*
*Wakolosai 2:6-7*

Ingawa alilelewa kanisani, kama kijana, John alikuwa mwasi. Alianza kutumia dawa za kulevya akiwa na miaka kumi na miwili na pombe akiwa na miaka kumi na mitano. Aliweka rekodi ya miaka ishirini ya kuvuta sigara. Katika umri wa miaka kumi na nane, alioa mchumba wa umri wa miaka kumi na mitano. Alijaribu kuwa mume, lakini alifurahia sana uwindaji, uvuvi na sherehe za usiku.

Siku moja kazini, John aliona dereva wa lori akishindwa kufaulu upimaji wa dawa ya kulevya na akapoteza kazi yake. John alikuwa amempatia dawa

hizo! Hilo lilimshitua—John aligundua kwamba hilohilo lingemtokea. Kwa hivyo John akapanda katika lori lake na akaomba. Siku hiyo aliokolewa.

Wiki hiyo, kanisa la mke wake lilikuwa na ufufuo. Hapo, John alienda madhabahuni kwa ajili ya uthibigisho tena, kisha kwa ajili ya utakaso. Alishuhudia kwamba utakaso wake uliondoa hamu ya tabia zake za awali.

Katika ufufuo huo, Bwana alimjaribu kwamba atoe $50 yake ya mwisho kama sadaka. John alisitasita—hiyo ilikuwa pesa yake ya gesi, na aliihitaji. Lakini Bwana akamwambia, "Nitakuhudumia." Kwa hivyo John alifanya vile Mungu alivyomwagiza. Siku iliyofuatia, alipokea fidia ya matumizi ya $120 ambayo hakutarajia.

Mara hiyo John aliona mabadiliko katika maisha yake: alikombolewa kutoka katika dawa za kulevya. Tayari alikuwa ameachana na tumbaku. Alianza kutumia muda mwingi na familia yake, pamoja na watoto wake wawili. Alianza kuhudhuria kanisani mara kwa mara, kusoma Biblia, na kusali. Mke wake alisema, "Amekuwa mtu tofauti mara moja."

Siku hizi, John na mke wake bado wanashiriki katika ibada za ufufuo za kanisa. Sasa anasema, "Imekuwa miaka ishirini kamili." John amekuwa akimfuata Kristo na amekuwa ndani yake kwa muda mrefu. [48]

**APRILI 28** **118**

# Kwa nini Mungu Haondoi Kila Baya?

*Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, "Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, Lakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika."*
*Mwanzo 2:15-17*

Bill na Donna walikuwa ni kati ya wenzi wa kupendeza wanaomcha Mungu unaoweza kuwafikiria. Bill alikuwa mchungaji na hatimaye kiongozi wa madhehebu ambaye alizalisha machapisho ya shule ya Jumapili ya watu wazima ambayo ilibariki mamia ya maelfu ya watu.

48. Imenukuliwa na kurekebishwa kutoka *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Juni 2014).

Miaka kadhaa iliyopita, wakiwa njiani wakielekea katika Shule ya Jumapili, Bill na Donna alipokuwa umbali wa jengo moja tu kutoka kanisani, gari lao liligongwa na dereva mlevi. Bill na Donna walifariki kutokana na ajali hiyo.

Lisilo haki kwa namna gani—mbaya kiasi gani. Mungu asingeweza kuzuia ajali hiyo?

Mwanzoni, Mungu alipoumba wanadamu, alisema, "Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula; lakini matunda ya ujuzi wa mema na mabaya usile."

Ilipofikia kwa uumbaji wake mkuu—binadamu – Mungu alichagua kudhibiti nguvu yake mwenyewe kwa kutupatia uhuru wa kuamua ("Matunda ya kila mti wa bustani *waweza* kula"). Mungu aliwapa haki ya uchaguzi. Lakini kwa hakika, maamuzi yetu yana matokeo ("Lakini matunda ya ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika"). Hivyo, ulimwengu wetu ni zao la upendo wa Mungu na uchaguzi wa binadamu.

Mpango wa Mungu kwa ulimwengu ulileta aina mbalimbali ya uchaguzi mwema na wenye afya—nyingi mno za kumridhisha kila mtu ("kula kutoka kwa *kila* mtu"). Ni chaguo moja tu lilikuwa limekatazwa.

Peter Marshall, mchungaji mlezi wa Bunge la Marekani, alikabiliana na masuala haya katika hotuba yake wakati wa Vita vya pili vya ulimwengu. Hii ni sehemu ya mahubiri hayo:

> Hakuna haja ya kujaribu kuepuka suala hili. Kuna nyakati ambapo Mungu haingilii kati—ukweli kwamba hafanyi chochote ni mojawapo ya mafumbo yanayotatanisha sana katika maisha ya Kikristo. Ni H. G. Wells ndiye alitaja utata ambao mioyo mingi yenye shaka imepitia wakati wa vita: "Ama Mungu ana uwezo wa kusimamisha mauaji haya yote na hajali au labda anajali, nah ana uwezo wa kuyasimamisha." Lakini hilo silo jibu . . . . Mradi kuna dhambi ulimwenguni. Almradi kuna tamaa, uchoyo, chuki katika mioyo ya wanadamu, kutakuwa na vita . . . .
>
> Ni kwa sababu tu Mungu ni Mungu kwamba hajali kiasi kwamba aliruhusu binadamu wawe na chaguo huru ambalo limesababisha ulimwengu kuwa na janga hili sasa. Mungu angezuia hiyo vita! Je, unakuwa na shaka kwamba Mungu hana nguvu? Lakini tuseme angezitumia? Wanadamu basi wangekuwa wamepoteza nguvu zao za kuwa huru.... Wasingekuwa a tena nafsi zilizojaliwa na uwezo wa kuchagua . . . . Tena badala yake wangekuwa vikarangosi, roboti, mashine, wanasesere. La, Mungu anacheza mchezo mkubwa zaidi. Bado anangojea mzinduko wa

akili wa jukumu la undugu katika mioyo ya wanaume na wanawake kila mahali. Hatatutendea mambo ambayo tunaweza kujitendea.[49]

Licha ya machafuko tumefanya katika ulimwengu wetu, Mungu atakuwa na neno lingine. Anajitahidi kutufunza tujipange kwa ajili ya malimwengu mawili—huu na ujao. Ambapo kumekuwepo na maovu duniani kutokana na uasi wa binadamu katika bustani ya kwanza, atawezesha kuwepo kwa bustani ya pili kwa wale watakaoimiliki. Bustani ya pili ni mahali ambapo maovu yatafanywa mema. Ufunuo 22:1-5 inaielezea:

> Kisha akanionesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwanakondoo, katikati ya njia yake kuu. Na upande huu na huu kando ya ule mto, ulikuwepo mti wa uzima, uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi. Na majani ya mti huo ni ya kuponya mataifa. Wala hapatakuwa na laana yoyote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na Mwanakondoo kitakuwamo ndani yake na watumishi wake watamtumikia. Nao watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. Wala hapatakuwa na usiku tena. Wala hawana haja ya taa wala nuru ya jua, kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru. Nao watatawala hata milele na milele.

Huu ndio mji, bustani ambapo Bill na Donna wataishi.

Watu wengi wametumia uhuru ambao wamepewa na Mungu kutimiza mambo makubwa sana. Fikiria kuhusu mashujaa wafuatao:

- Martin Luther King, Jr., aliyetoa wito wa upatanisho wa migogoro ya ubaguzi wa rangi.
- Charles Colson, mfungwa aliyempata Kristo na akawa nguvu inayoongoza ulimwenguni kwa mageuzi ya gereza.
- William na Catherine Booth ambao walianzisha Jeshi la Wokovu ili kuinua wanyonge na kuokoa nafsi zao.
- John Wesley ushawishi wake katika Uingereza, Marekani na zaidi ulihamasisha mamilioni wamgeukie Kristo.

Kuna watu ambao walitumia uhuru wao kwa kushirikiana na uhuru wa Mungu—kwa ushirika wao na Roho, wagonjwa walipona. Hali kadhalika, wewe na mimi tuna fursa ya kuamua namna ya kutumia uhuru wetu wa kuchagua—chagua vyema.

---

49. Catherine Marshall, *Beyond Our Selves* (New York: McGraw Hill Book Company, 1961), 26–27.

# Upendo Hutimiza Sheria

*Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria.*
*Warumi 13:10*

Rafiki yangu wakili Albert anakadiria kwamba vitabu vya sheria vya Marekani vina sheria milioni hamsini zinazonuia kufanya watu wema. Lakini Ukristo una sheria moja tu: "Upende."

Mwanasheria mmoja alimuuliza yesu, "Katika torati ni amri ipi kuu?" Yesu akamjibu, "Mpende Bwana Mungu wako na moyo wako wote na akili zako zote. Hii ndio amri kuu na tena ni ya kwanza. Na ya pili inafanana nayo: 'Mpende jirani yako kama nafsi yako.' Katika amri hizi mbili hutegemea Torati yote na vitabu vya Manabii" (Mathayo 22:36-40).

Katika kitabu cha Mungu, upendo huu si upendo wa kizembe. Kabla ya kusema kuwa "upendo ndio utimilifu wa sheria" (Warumi 13:10), Paulo ananukuu kutoka katika Amri Kumi Kuu (kif. 9). Kama unampenda Jirani yako, hutazini na mke wake. Ikiwa unampenda jirani yako hutamuua, kumwibia, ama kutamani mali yake. Ikiwa una upendo wa kweli, bila shaka utatimiza Amri zote Kumi kuu.

Paulo anawaambia Wakristo wa Galatia kuwa vita vinaweza kuwa bado viko katika roho zao: "Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka" (Wagalatia 5:17).

Kisha Paulo anatoa mfululizo wa kauli ili kufafanua zaidi kuhusu suala la sheria na upendo. Katika Wagalatia 5:14, anaandika, "Maana torati yote imetimilika katika neno neno moja, nalo ni hili: 'Umpende jirani yako kama nafsi yako."

Lakini kama mwili au asili ya dhambi inapigana dhidi ya Roho Mtakatifu na inasababisha tabia zisizokuwa na upendo, tunaweza kufanya nini? Paulo anatoa majibu yafuatayo:

- Galatians 5:24—"Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake."
- Galatians 5:16—"Basi nasema, Nendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili."

- Galatians 5:22–23—“Lakini tunda la Roho ni upendo . . . juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.”

Yesu alikuwa na maneno makali kwa viongozi wakosoaji wa Kiyahudi waliojiona kuwa ni wataalamu wa sheria: “Lakini ni nimewajua ninyi. Ya kuwa hamna upendo wa Mungu ndani yenu” (Yohana 5:42). Hili lilikuwa shtaka halali dhidi ya viongozi ambao walionyesha unafiki mwingi. Bali Wakristo wengi wenye kujitahidi ambao hukubali amri ya kupenda wengine pia hupambana na vita vya kindani vya kiroho wanapoendelea katika tabia na mitazamo isiyo ya Kikristo. Wanajaribu kupenda zaidi, lakini hawawezi kuleta upendo wa kutosha kwa nguvu zao wenyewe.

Angalia katika vifungu vya Wagalatia vilivyonukuliwa hapo awali. Ona marejeo ya Paul yanayorudiwa kwa nguvu ya nje; chanzo cha kimungu; kazi ya Roho Mtakatifu. Kwingineko katika Warumi 5:5, Paulo anatupatia jibu lililo kamili zaidi kwa haya mashaka: “Na tumaini halitutahayarishi, kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminiwa katika mioyo yet una Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.” Wakati huwezi kujipa upendo wa kutosha, Roho Mtakatifu wa Mungu ataumimina katika moyo wako.

Ushuhuda wa Dr. Daniel Steele, profesa katika Chuo kikuu cha Boston, anadhihirisha hoja hii. Alikuja kumjua Kristo kama Mwokozi wake alipokuwa na miaka kumi na minane, lakini alikuwa na mapambano katika maisha yake ya Kikristo. Alihisi kuwa alikuwa “huru dhidi ya hatia na mamlaka ya dhambi, lakini si dhidi ya mielekeo yenye nguvu ya ndani, na hatimaye, alianza kumtafuta Mungu kwa nguvu zaidi.” “Kisha,” akasema, “Roho aliweka waziwazi kwa macho yangu maovu ambayo bado yamebaki katika uhalisi wangu.”

Usiku mmoja wa Novemba, alikuwa akimtafuta Bwana kwa bidii wakati, kama anavyosema, “Ghafla nilihisi nguvu ya ajabu ikijipenyeza kwenye hisia zangu . . . kama mkondo ya umeme ulikuwa unapita kwenye mwili wangu kwa mtikiso usio na maumivu, ukiuyeyusha mwili wangu wote katika mkondo wa moto wa upendo.” Alisema hii ilielezewa vyema kama “Upendo wa Mungu uliomwagiwa kote moyoni na Roho Mtakatifu.”

Akawa na uhakika zaidi juu ya upendo wa Mungu kwake kuliko uwepo wa ardhi chini ya miguu yake. Aligundua kuwa hii ilikuwa “kuondolewa kwa kanuni ya dhambi kwa nguvu ya utakaso wa Roho Mtakatifu.” Alikuwa ameshuhudia “pendo lililo kamili linalotupa nje hofu.” Dkt Steele aliendelea

na kuishi katika kiwango kingine cha ushindi na akawa kiongozi mkuu wa kiroho na mwandishi. [50]

Kama hadithi ya Dkt. Steele inayoonyesha, "Upendo hutimiza sheria." Ujazo wa Roho Mtakatifu na uwepo wake na nguvu zake zitafanya itimie katika maisha yako pia!

**APRILI 30** **120**

## Vipi kuhusu Wanafiki?

*Wakati Simoni alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha akisema, Nipeni na mimi uwezo huu, ili kila mtu nitakayemweka mikono yangu, apokee Roho Mtakatifu.*
*Matendo 8:18-19*

*Roho akamwambia Filipo, "Sogea karibu na gari hili, ukaribiane nalo."*
*Matendo 8:29*

Je, umewahi kumsikia mtu akisema, "Vipi kuhusu wanafiki kanisani?" Swali hili mara nyingi huja kabla ya sababu kwa nini mtu huyo haji kanisani. Napenda kuwauliza watu hawa kuhusu kazi zao: "Je una wafanyakazi wenzako ambao huzungumza sana kuhusu wanavyotia bidii, lakini unawaona wamesimama karibu na kipoza cha maji wakipunga upepo, wanacheza michezo ya video kwenye meza zao, na wanapoteza muda mwingi? Kwa kweli ni wanafiki, sivyo? Je, ukweli kwamba una wanafiki kazini mwako unakuzuia kwenda kazini?"

50. Nukuu kutoka kwa Daniel Steele zimetoloewa kutoka J. Sidlow Baxter, *His Deeper Work in Us* (Grand Rapids: Zondervan Publishing House, 1967), 71–73.

Huwa, wanaelewa.

Katika Matendo 8:14-40, tunahadithi ya watu wawili, Simoni na Filipo. Wote walimtamani Roho Mtakatifu, lakini kuna tofauti kati yao:

- Simoni alitakakukumtumia Roho Mtakatifu; Filipo alitaka Roho Mtakatifu amtumie.
- Simoni alitaka kulipia Roho Mtakatifu; Filipo alijitoa kwa Roho Mtakatifu.
- Petro alimkemea Simoni na kumwambia kuwa moyo wake si mnyofu mbele ya Mungu; ni mateka wa dhambi na lazima atubu. Mungu anamtunuku Filipo kwa kumtumia kuongoza Towashi wa Ethiopia wa hazina ya Kristo.

Kumbuka kwamba hadithi za watu hawa wawili ziko katika Bibilia. Bibilia iko wazi, na kwa kuelezea hadithi ya Simoni, inatambua kuwa kuna wanafiki kanisani. Bibilia hiyo hiyo pia inatueleza hadithi ya Filipo kuonyesha kuwa kuna Wakristo wa kweli kanisani. Hivyo basi, mtazamo wetu unapaswa kuwa upi?

Tuna mwongozo wa kufafanua: "Mtawatambua kwa matunda yao" (Mathayo 7:16). Tunapaswa kuwa na utambuzi na kujifunza kutofautisha kati ya wanafiki na wakweli. Kisha, tunapaswa kuamua kutowaruhusu wanafiki watuzuie na badala yake tufuate mfano wa Wakristo wa kweli. Ninajua maelfu ya Wakristo kama hawa, na ninataka niwe kama wao.

**MEI 1** **121**

# Maneno Yatokayo Kinywani Mwako

*Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia. Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa mhuri hata siku ya ukombozi. Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matusi yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.*

*Waefeso 4:29-32*

Katika jitihada za kunipa "hekima," mshiriki wakati mmoja alinishauri, "Hutafanikiwa katika dhehebu hili kwa sababu huna jamaa yeyote katika kanisa hili." Labda alikuwa ameumizwa; labda alikuwa mbishi; lakini

alinambia kwa maneno ya hakika kwamba kama unataka kupanda katika ngazi za kanisa, ni lazima uwe na watu wa familia yako katika vyeo vyenye mamlaka.

Maneno yake kwa hakika hayakunijenga, lakini pia hayakunivunja moyo—sikuwa ninajali kuhusu kupanda ngazi. Nilikuwa ninafurahia kuchunga hilo kanisa dogo nililokuwa ninahudumia. Wakati mwingine, huyu mtu alikuwa na maneno mengi zaidi kwa ajili yangu: "Utapandishwa cheo lini?"

Nilijua kanisa letu lilikuwa na mazingira ya chini—tulikutana katika zizi la farasi lililofanyiwa ukarabati. Lakini watu wapya walimpokea Yesu; wengine walikuwa wanatakaswa; kanisa letu lilikuwa linakua; na tulikuwa njiani kwenda katika jengo zuri jipya, lenye kanisa na kitengo cha elimu. Nikamjibu, "Niko katikati ya mapenzi ya Mungu. Siwezi kwenda juu kuliko hapo."

Ili tupate kuishi kulingana na mahimizo ya Waefeso 4:29–32, tunaweza kuuliza maswali yafuatayo kuhusu maneno yetu:

1. Je, ni ya kweli?
2. Je, ni ya lazima?
3. Je, ni hekima kuwaambia watu?
4. Je, yatamjenga anayesikia?
5. Je, yatamsaidia au kumwumiza mtu mwingine?

Maneno yetu kwa watu wengine yanaweza kumhuzunisha Roho Mtakatifu. Wakati mmoja Jessie Penn Lewis alisema kwamba "huzuni" ni neno la upendo. Unapompenda Roho Mtakatifu wa thamani, hutataka kumhuzunisha. Inawezekana hata umhuzunishe na kumtoa maishani mwako. Tafadhali kumbuka vifungu vilivyotangulia na vilivyofuata kifungu cha 30 vinavyoeleza njia za kumhuzunisha Roho.

Ninashtuka ninapotambua jinsi maneno ya mtu yanavyokaa kwa muda mrefu moyoni au akilini mwangu. Maneno, "Hutafanikiwa kamwe katika hili kanisa," yana zaidi ya miaka sitini. Maneno, "Ninakuombea wewe na Nancy kila siku," ni ya zaidi ya miaka arobaini iliyopita. Ninafurahi jinsi sentensi moja pekee inaweza kubeba uzito mkubwa sana.

Mbele yangu kuna ujumbe kutoka kwa mtu aliyenishukuru kwa maneno yangu:

> Mpendwa Chic,
>
> Kwa karibu miaka ishirini na mitano iliyopita, maneno yako kule seminari siku ile yalinipa tumaini kwamba nilikuwa nimefanya jambo sahihi. Hakuna mtu mwingine aliyenisaidia—naamini ni Mungu ndiye aliyekutuma uongee na mimi. Siku zote nimekuwa na *shukrani* nyingi sana!

Maneno yangu yalimbariki miaka ishirini na mitano iliyopita, na ujumbe wake unanibariki leo. Mfanye mtu mwingine afurahi kwa maneno yako. Mfanye Roho Mtakatifu afurahi kwa maneno yatokayo kinywani mwako.

**MEI 2** **122**

## Ni Kwa Jinsi Gani Unakuwa Hivi Ulivyo?

*Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo; na neema yake iliyo kwangu ilikuwa si bure, bali nilizidi sana kufanya kazi kupita wao wote; wala si mimi, bali ni neema ya Mungu pamoja nami.*
*1 Wakorintho 15:10*

Kama neema ingekuwa inaweza kuwekwa kwenye chupa na kuuzwa, watu wengi wangeuza vyote na kuinunua hiyo—lakini kwa kuwa ni bure, hawawezi kuamini kwamba ina thamani yoyote. Wengi wetu tungesema, "Pale lakini kwa neema ya Mungu ninaenda," maanake ni kwamba kama nilikuwa sijawahi kusikia au kutoa mwitikio kwa neema, ningekuwa bado nimepotea na kumtumikia bwana wangu wa zamani.

Jim Elliot alisema, "Yeye atoaye kile ambacho hawezi kukiweka ili apate kile ambacho hawezi kukipoteza, si mjinga." Vivyo hivyo, mtume Paulo hakuacha kutoa ule upendo ambao Mungu aliutia ndani yake. Hakuacha makosa yake ya zamani na kushindwa kwake kumfanye asitumike katika wakati wa sasa. Hakuacha vikwazo vya sasa, upinzani wa sasa, au mateso yamfanye asifikie lengo lake. Alitoa yake yote kila siku, akitumaini kwamba kama kutakuwa na kesho, Mungu angemtosha.

Je, Mungu anatutosha? Ndio, kwa sababu neema yake, haijawahi kupungua kamwe. Yeye yupo masaa ishirini na manne kwa siku. Kama waumini, vyote tulivyo navyo ni kwa sababu ya neema yake ya ajabu.

Nancy Shaver[51]

---

51. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Julai–Agosti–Septemba 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 93. Imetumiwa kwa ruhusa (Chapisho hili likawa *Reflecting God*.)

# Kutoka "Naweza Kupata Nini?" hadi "Naweza Kutoa Nini?"

*Ndipo Petro akajibu, "akamwambia, Tazama, sisi tumeacha vyote tukakufuata; tutapata nini basi?"*
*Mathayo 19:27*

Petro hakuwa mfuasi wa Kristo peke yake aliyejiuliza, *Naweza kupata nini*? Mamake Yakobo na Yohana alisema, "Agiza kwamba hawa wanangu wawili waketi mmoja mkono wako wa kuume, na mmoja mkono wako wa kushoto, katika ufalme wako" (Mathayo 20:21). Marko anasema kwamba Yesu alipowauliza wanafunzi wake kile walichokuwa wanashindania, "wakanyamaza kwa maana njiani walikuwa wakibishana wao kwa wao, ni nani aliye mkubwa" (Marko 9:34). Lakini kitu fulani lazima kiwe kimebadilika katika kilindi cha mioyo yao, kwa sababu katika kuwaeleza wanafunzi hawahawa miezi michache baadaye, Matendo inasema, "Hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu chochote alicho nacho ni mali yake mwenyewe, bali walikuwa na vitu vyote shirika" (4:32).

Niliona mtindo uo huo katika maisha ya Frank na Peggy. Walimpokea Kristo kama wana ndoa wachanga. Kanisa letu la nyumbani liliwazunguka na upendo na kujali wakati walipokuwa wanakua kiroho. Hatimaye, baada ya Frank kumaliza mafunzo yake ya kutengeneza saa za mkono, walirudi nyumbani kwao Omaha, Nebraska, ili Frank akaanze kazi kama mtu wa kukarabati saa. Baada ya kutumia wiki kadhaa kutafuta kanisa kule Omaha, walitutumia ujumbe: "Hatuwezi kupata kanisa hapa Omaha lenye upendo kama wenu."

Wakasafiri kuvuka majimbo a wakaingia Iowa. Na hata huko nako hawakuweza kupata kanisa lenye upendo kama wetu. Nikaanza kuwa na wasiwasi nao. Nikawahimiza watu wa kanisa letu wawaombee na wawapigie simu.

Hatimaye, Frank na Peggy wakasema, "Tumeamua tuache kutafuta kanisa lenye upendo kama kanisa lako. Badala yake, tutatafuta kanisa linalohitaji upendo na tulipe upendo kama kanisa lako lilivyotupa." Walifanya hivyo—na wakawa viongozi wakuu wa kiroho katika hilo kanisa.

Sote—Petro, Yakobo, Yohana, Frank, Peggy, wewe, na mimi—tutapata ushindi wa kiroho tutakapotoka katika "Naweza Kupata Nini?" hadi "Naweza Kutoa Nini?"

MEI 4 **124**

## Je, Kijana Anaweza Kutakaswa?

*Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo*
*kwao waaminio katika usemi, na mwenendo,*
*na katika upendo na imani na usafi.*
*1 Timotheo 4:12*

*Ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu—si kwa kadiri ya*
*matendo yetu sisi bali kwa ajili ya makusudi yake yeye na neema yake.*
*Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele.*
*2 Timotheo 1:9*

Kwa mwaka mmoja, nilipewa kazi ya kuhubiri na kufundisha katika mkutano 137 wa kila mwaka wa sikukuu za vibanda wa Iowa Holiness Association. Changamoto yangu ya kila siku ilikuwa kufundisha utakaso, utakatifu, na maisha ya kujazwa na Roho kwa njia ambayo kila mtu angeweza kuelewa.

Usiku mmoja, kijana aitwaye David alitoa ushuhuda, "Siku ya Jumanne, nilienda madhabahuni—nikajisalimisha, nikamwomba Mungu anisafishe na anijaze Roho Mtakatifu. Nimemwona Roho katika siku kadhaa zilizopita, na namshukuru Mungu kwa uwezo wake wa utakaso."

Nilikutana na kijana wa miaka kumi na sita aitwaye Donna mwanzo wa hiyo kambi. Alikuwa mtu peke yake katika familia yake aliyeenda kanisani, na mara ya kwanza alionekana ana haya, anasitasita, na hana uhakika. Mwisho wa hiyo kambi, aliandika hii ripoti. *Wiki kadhaa kabla ya Iowa Holiness Association, nilikuwa ninamwomba Mungu kwamba kutakuwa na ushindi mkubwa wa kiroho na kwamba Mungu angeyabadilisha na kuyageuza maisha yangu. Halafu nikaona kwamba Kasisi Chic Shaver angehubiri ujumbe juu ya utakaso, na Mungu akanionyesha kwamba huo ulikuwa kwa ajili yangu. Jumatatu, nikatoa moyo wangu na maisha yangu kabisa kwa Bwana, na Roho Mtakatifu alifurika nafsini mwangu katika wiki yote. Nilijazwa sana kiasi kwamba mimi ni mtu mpya. Nimefia kabisa Donna wa zamani na mimi ni mpya katika Bwana na Roho wake Mtakatifu. Kisha baadaye katika hii wiki, nilikuwa*

*namwomba Mungu kwamba angenijulisha mapenzi yake kwa ajili ya maisha yangu, na Jumatano, Mungu akaniambia anataka mimi niwe mmishenari. Bado ninaomba Mungu ananiita katika idara gani. Roho Mtakatifu wa Mungu amekuwa tu pamoja nami katika wiki yote. Nalisifiwe jina lake takatifu.*

Oo ndiyo, kijana anaweza kutakaswa![52]

**MEI 5** **125**

# Tatizo Moja, Sehemu ya 1

*Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu, aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa, basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.*
*1 Wakorintho 6:19—20*

Wakati mwingine kushinda pambano moja tu hukusukuma mbele kwa ujasiri na ushindi mkubwa katika maeneo mapana zaidi ya maisha yako ya Kikristo. Kukabiliana, kupigana, na kusambaratisha hicho kizuizi hukupa uwezo wa kushinda hata changamoto kubwa zaidi.

Mara tu tunapowaona wengine wakipata ushindi, tunaamini vivyo hivyo vinaweza kufanyika kwetu. Yoshua alipokabiliana na Mto Yordani, jiji kuu la Jeriko, na Waisraeli milioni mbili nyuma yake waliomtegemea yeye kwa uongozi, Mungu alimtia moyo kwa kumkumbusha kuhusu kazi yake katika maisha mengine, "Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe; sitakupungukia wala sitakuacha" (Yoshua 1:5).

Nitachukua suala moja tu—kutawaliwa na tumbaku. Nitazidi hata kuwa maalum zaidi na nichague uvutaji wa sigara. Hili linaweza kuwa ndilo pambano lako au la, lakini nivumilie. Sikia na kuona jinsi watu wengine walivyopata ushindi dhidi ya hilo wazo moja na kunawiri katika maeneo mengine mengi sana.

Wakati Jerrold Atchison alipokuwa kijana, aliamua kubadilisha mabwana. Alikuwa ametawaliwa na pombe na tumbaku; sasa amemchagua Yesu Kristo kama Bwana wake. Baada ya uamuzi wake kwa ajili ya Kristo, aliacha kunywa pombe mara moja, lakini kuvuta sigara kulionekana kuwa na mvuto mkubwa

52. *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Septemba 2015).

zaidi. Siku moja, kiu ya tumbaku ilionekana kuwa kali sana kuliko kawaida, na akaogopa angeshindwa kuvumilia. Papo hapo, simu ikalia, na rafiki yake mpya Mkristo akamwonyesha jinsi alivyokuwa anamwamini. Jerrold akatambua kwamba asingeweza kushindwa huku Mungu akiwa amempenda sana na marafiki zake walikuwa wamemwamini. Akafungua Biblia yake katika Yuda 1:24 (SUV) na akasoma, "Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu." Alimtumaini Mungu, naye akamhifadhi, na hakurudia tabia yake kamwe.[53]

Walter Jackson alikuwa ametawaliwa na sigara kweli kweli—alivuta kama pakiti tatu kwa siku. Kisha akamkubali Kristo kama Mwokozi na Bwana wake na akapata kwamba alikuwa Bwana ambaye angeweza kumtegemea kabisa. Akaacha kuvuta sigara mara moja, lakini mke wake akasema kwamba, kwa wiki mbili, alikuwa na wasiwasi sana. Baada ya wiki mbili kiu ikakoma kabisa—Walt alikuwa ameshinda vita. Alikubali kwamba bado kulikuwa na wakati ambapo bila kujitambua alitia mkono wake mfukoni ili atoe sigara. Lakini kila alipotia mkono huo mfukoni siku zote alikumbuka mabadiliko yaliyokuwa moyoni mwake, kwa kuwa katika mfuko uleule ulio juu ya moyo wake, alikuwa sasa anaweka nakala ndogo ya Agano Jipya—kama kiasi cha pakiti ya sigara lakini yenye uwezo mwingi zaidi. "Kwa nini nivute sigara huku nikiwa ninaweza kuvuta elimu ya Bwana?" Walt akajiuliza.[54]

Walter alielewa pale mahali katika Agano Jipya lake ambapo Paulo aliandika, "Bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha, isiwe nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa" (1 Wakorintho 9:27).

**MEI 6** **126**

# Tatizo Moja, Sehemu ya 2

*Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu, aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa, basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.*
*1 Wakorintho 6:19—20*

53. Charles "Chic" Shaver, *You Can Quit Smoking* (Kansas City, MO: Beacon Hill Press of Kansas City, 1975), 18–19.
54. Charles "Chic" Shaver, *You Can Quit Smoking* (Kansas City, MO:

Kwa ofisa wa polisi Vincent Hutchens, ilikuwa kama kila aina ya muujiza. Kwa miaka ishirini na miwili, alivuta pakiti mbili hadi tatu kwa siku. Lakini baada ya miaka ishirini ya kumtazama mke wake akiishi maisha ya Kikristo yenye uthabiti, Vincent hatimaye aliacha uasi na akamkubali Yesu Kristo. Mungu sasa alikuwa halisi kwake, na mambo ambayo awali yalikuwa ya maana sana kwake yakapoteza umuhimu wake. Kwa Vincent, sigara zilikuwa katika hili kundi.

Aliacha, lakini haikuwa rahisi. Alikuwa ametawaliwa sana kiasi kwamba, wakati mapenzi yake yaliyotiwa nguvu yalipomwambia asimame imara, alivumilia kile alichokieleza dalili za kujiondoa. Lakini Mungu hakuruhusu hilo jaribu lizidi kile Vincent alichoweza kuvumilia. Kwa kweli, Mungu alimpa muujiza mdogo wa kimwili umsaidie: Siku za nyuma, usingizi wa Vincent mara nyingi ulikatizwa kwa kuamka kila wakati. Sasa alitumia usiku kulala usingizi mzito, usiokuwa na bughudha. Kwa kushukuru alikubali kipawa hiki kutoka mikononi mwa Mungu. Kilimpa nguvu ya mwili aliyohitaji na kumwezesha kuendeleza ushindi wake.[55]

Vincent aliiishi ahadi ya Paulo kwa Wakorintho: "Jaribu halikuwapata ninyi isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu. Ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo. Lakini pamoja na lile jaribu, atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kusitahamili" (1 Wakorintho 10:13).

Robert Ferguson alipompata Kristo, alihisi kusadikishwa kuhusu wizi wake—alikuwa amefanya kazi katika kitengo cha kujalidi vitabu kwa miaka, na alikuwa anaiba kitabu kimoja kila wiki. Alijua atalazimika kukabiliana na bosi wake, akiri makosa yake, na avilipie hivyo vitabu. Kwa hakika, Robert alitishika sana. Lakini alifanya hivyo.

Huyo bosi alishangazwa na uaminifu wake na akamtendea kwa neema. Robert alitoka ofisini kwa bosi akiwa ametiwa moyo. Akafikiri, *Kama Mungu anaweza kunipa ujasiri wa kufanya hivyo, anaweza kunipa ujasiri wa aina nyingine*. Akiwa na hilo, alichukua pakiti ya sigara kutoka mfukoni mwake, akaziangusha chini na akazikanyaga kanyaga na kuzipiga mateke katika hicho chumba, na hakuvuta sigara tena.

Robert aliuona ukweli wa 1 Yohana 4:4: "Ninyi, watoto wadogo, mnatokana na Mungu nanyi mmewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Na punde baadaye, Robert akajifunza ukweli mwingine: "Ulikuwa mwaminifu kwa machache; nitakuweka juu ya mengi"

55. Charles "Chic" Shaver, You Can Quit Smoking (Kansas City, MO: Beacon Hill Press of Kansas City, 1975), 25-26.

(Mathayo 25:23). Robert aliitwa katika huduma na akawa nguvu kubwa kwa ajili ya Mungu.

Linaweza kuwa tu "suala moja"—lakini kumbuka kwamba mwili wako ni hekalu la Roho Mtakatifu. Ufanyie mambo mazuri!

MEI 7 **127**

# Mahali Wanapoponya Mioyo Iliyovunjika

*Nami nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi; nitawatakaseni na uchafu wenu wote, na vinyago vyenu vyote. Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda.*
*Ezekieli 36:25–27*

Msichana mmoja wa Kikorea aliuliza katika kituo cha umishenari, "Je, hapa ndipo mahali wanapoponya mioyo iliyovunjika?" [56] Mioyo mingi sana inahitaji uponyaji—msamaha, tumaini, kutiwa moyo, nguvu, upendo, kukubaliwa.

Mama yangu mwenyewe alihitaji uponyaji kwa ajili ya moyo uliovunjika. Dhuluma za baba yangu na kutawaliwa na pombe vilikuwa vimemponda kabisa kwa miaka. Akaacha kwa kiasi kikubwa usuli wake wa Kimethodisti uliojaa miamsho, kuitwa madhabahuni, na mikutano ya kambini alipokuwa anajaribu kuenenda katika ukingo wa shinikizo na matakwa ya ulimwengu. Katika mchakato huo, alifanya dhambi mbaya sana. Akaishi akihisi kuwa na hatia—kwa sababu alikuwa nayo. Alihitaji msaada. Mara nyingi alimtembelea jirani yake Mkristo, ambaye alimchukulia kama rafiki yake mzuri zaidi, na wakazungumza kwa masaa. Hata alitembelea kanisani mara chache na huyo huyo jirani. Jumapili moja, akapata ujasiri wa kutosha wa kuinua mkono wake akitaka aombewe.

Majira ya joto baada ya kumkubali Kristo, mamangu akaanza kuja kanisani. Usiku mmoja, wakati wa ibada ya uamsho ya vijana, akapata kwamba asingeweza tena kuvumilia huko kuvunjika kwake. Akakimbia madhabahuni, akamimina dhambi zake, na akampokea Yesu, anayeishi, anayependa,

56. E. Stanley Jones, *Abundant Living* (New York: Abingdon, 1942), 94.

anayeponya katika maisha moyo wake na maisha yake. Tulipokuwa tunatoka kanisani, akaniambia kisiri kwamba alikuwa amejaribu kuwaza kuhusu kujinyonga. Hapo pekee ndipo nilipotambua jinsi moyo wake ulivyokuwa umevunjika sana.

Mara moja Yesu akaanza kuukarabati moyo wake. Alijua kwamba dhambi zake *zote* zilisamehewa—ni afueni iliyo je! Mara moja akawa na furaha, amani, na uwepo wa Mungu.

Akaanza kuyapanga upya maisha yake yote. Akatupa sigara zake chooni na akawa huru dhidi ya tumbaku. Akaacha kunywa pombe. Akaingia katika Neno la Mungu. Akaanza kuwaombea wanafamilia wengine wamwone Bwana. Aliingia ndani kwa kina zaidi katika maisha yake ya Kikristo na kupata kwamba Mungu angemjaza na Roho wake na amtakase tabia zake za ndani. Aliwashuhudia wanafamilia wengi na akamleta dadake kwa Kristo.

Mungu akaupa nguvu moyo wake, na akamshuhudia babangu kwa upendo na hekima. Alipojaribu kumshawishi akubali mambo mengine katika imani yake juu ya masuala fulani, akamjibu, "Kumbuka, ulikuwa ukinambia kwamba sikuweza kujifikiria mwenyewe. Sasa ninajifikiria!" Hatimaye, hakuweza kuchukua mchanganyiko wake wa upendo na nguvu—na mwishowe, akamkubali Bwana.

Mama yangu hakurudia kamwe mambo yake ya zamani—alikuwa ana moto kwa ajili ya Yesu maisha yake yote yaliyosalia. Alikuwa kiongozi katika kanisa lake, anawashuhudia wengine, na mtu mwenye ushawishi katika jumba la sehemu nyingi ilimokuwa nyumba yao. Alipokuwa na miaka tisini na mbili, aliomba, "Ninapokuwa mzee, usiniache nikawa mtu mwenye kulalamika." Na hilo ombi lilijibiwa. Alipokuwa na umri wa miaka 103, alienda kuwa na Yesu kwa amani. Alikuwa amepata mahali—mwanadamu Yesu, anayeponya mioyo iliyovunjika.

**MEI 8** **128**

# Familia

*Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno.*
*Waefeso 5:25–26*

*Lakini kila mtu ampende mke wake kama nafsi yake mwenyewe,*
*wala mke asikose kumstahi mumewe.*
*Waefeso 5:33*

*Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki.*
*Waefeso 6:1*

*Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali*
*waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana.*
*Waefeso 6:4*

Crawford Loritts anasema, "Eneo la muhimu zaidi la maisha ambalo unawatayarisha watoto wako kwa hilo ni ndoa na familia, na matayarisho yao bora zaidi ni kuishi na baba yao anayempenda mama yao." [57] Ningeongeza, "na kuishi na mama yao anayempenda baba yao."

Kulingana na Waefeso 5:25, Kristo ndiye mfano wa upendo wa mume. Upendo wake ni wa kujitoa sadaka, wa kujitoa mwenyewe, wa kutakasa. Huu upendo hautaangusha, haudunisha, hautadanganya, au kudhoofisha uadilifu. Kama Kristo alivyojitoa mwenyewe kulitakasa kanisa, pia mume naye anapaswa kumhimiza mke wake awe mtakatifu. Wazo ni kuendelea kupenda.

Mimi na Nancy tulifikia mahali pa changamoto katika mwaka wa thelathini na tatu wa ndoa yetu. Tulizungumza pamoja na tukaibuka na kauli ya maono ifuatayo kwa ajili ya mwaka wetu wa thelathini na nne.

> *Kwa sababu sisi ni muhimu, tunashiriki vile siku zetu zilivyokuwa. Kuwa na mambo ya kufurahia pamoja ni jambo la kupewa kimbaumbele cha juu. Tunafurahia ngono yenye mahaba. Kila mara tunazungumza na kusikilizana, tunaonyesha upendo wetu kwa maneno na vitendo, na tunaonyesha mawazo yetu na hisia zetu za ndani. Katika baadhi ya masuala tunayafunga kwa kukubaliana kwamba ni sawa kutokubaliana. Tunaungana mkono katika amali na jitihada za binafsi. Tunakuwa wepesi wa kuhisi mahitaji yanayobadilika ya mwingine. Tunachukua wakati kumweka Mungu pahali pake sahihi maishani mwetu, na bado tunapeanamahali petu sahihi.*

Sasa baada ya zaidi ya miaka sitini, ndoa yetu ina mambo mengi mazuri na iko hai.

Leo, tunatambua kwamba nyumba nyingi hazina mume na mke pamoja. Kwa maana fulani, ndoa zote ni za muda—mwenza anaweza kufa au, la kusikitisha, wanandoa wanaachana. Hivyo basi, ni muhimu sana kujenga ndoa juu ya msingi wa Kristo. Mwenzako akienda, bado unakuwa na msingi

57. Crawford W. Loritts, Jr., "Ten Ways to Be a Better Father" (Garland, TX: American Tract Society, 1993), https://jhfamilysolutions.com/10-ways-to-be-a-better-father/.

wako. Kama ndoa yenyewe ndio msingi wako, utaondoka wakati mwenzako anapoondoka.

Watoto wajifunze kuwa watiifu kwa wazazi wao. Hili huboresha ubunifu wao wa kumtii Mungu wakati nafasi inapotokea. Kina baba, watieni nidhamu watoto wenu, lakini msiwavunje roho zao. Toeni zaidi "Mnaweza kufanya hivyo," na "Ninajivuna kwa sababu yenu." Kwa kila haoana, toa ndiyo. Yesu, mama, na baba na wawe viongozi wao wakuu wanaowashangilia.

Kama kijana, mwana wetu, Paul, aliishi ukingoni. Tulimpenda na kumwombea. Ilikuwa furaha iliyoje usiku ule katika mkutano wa kambini alipokimbia madhabahuni, akaomba, akaruka, na akasema, "Baba, Mungu ameniokoa"—kisha, huku akinikumbatia, "Baba, ninakupenda."

MEI 9 **129**

## Ubebaji wa Kangaruu

*Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana,*
*enendeni vivyo hivyo katika yeye.*
*Wakolosai 2:6*

*Onjeni mwone ya kuwa Bwana yu mwema;*
*heri mtu yule anayemtumaini.*
*Zaburi 34:8*

Mpendwa Dr. Ralph Earle alikuwa akifundisha kwamba kuna njia tatu watu huelewa maisha ya Mkristo: ubebaji wa paka, ubebaji wa tumbili, au ubebaji wa kangaruu.

Nadharia ya Ukristo wa ubebaji wa paka msingi wake ni tabia ya mama paka. Akifikiri kuwa mwanawe yuko hatarini, anamuuma tu ngozi ya kikosi cha shingo na kumwondoa. Yule mtoto analegea kabisa—hafanyi lolote ili ajiepushe na hatari. Wengine wanaelewa Ukristo namna hii—Mungu hutuchukua na kutubeba. Hatuna lolote tunaloweza kufanya, hatuna wajibu wowote, na labda hata tunabebwa kinyume na matakwa yetu—Mungu ndiye kila kitu.

Nadharia ya ubabaji wa tumbili msingi wake ni jinsi mtoto wa tumbili husafirishwa. Wakati mama tumbili yuko tayari kusafiri, mtoto wake anawajibika kikamilifu kwa kupanda mgongoni mwake na kujishikilia kwa

ajili ya maisha yake anayoyapenda. Wakristo wengine huangalia imani kuwa ni wajibu wetu wote kumshikilia Mungu—zote ni jitihada zetu.

Hatimaye, nadharia ya ubebaji wa kangaruu msingi wake uko juu ya ukweli kwamba mama kangaruu ana mfuko unaotoa usalama, ulinzi, na malezi kwa mtoto wake. Hata baada ya mtoto wa kangaruu kukomaa vya kutosha kujiongoza mwenyewe, ana wajibu na nafasi ya kurudi kwa mfuko wa mama yake wakati anapokuwa hatarini. Ni uamuzi na hatua ya mtoto, pamoja na ulinzi na usaidizi kamili wa mamake—mtoto huyo anaruka na kuingia mfukoni kwa imani. Huu ndio mlinganisho bora zaidi wa Ukristo: Mungu ndiye msaidizi na mlinzi wetu, lakini wakati uo huo, ni lazima tuchague kuingia (na kukaa) ndani ya mfuko.

Kwa hakika, Maandiko hutoa vielelezo vingi mbalimbali vya maisha ya Mkristo. Viwe vinaonekana katika barua au katika mifano ya Yesu, vielezo hivi hutofautiana kulingana na mahitaji ya wasomaji. Wakati mwingine huweka mkazo juu ya neema ya Mungu, wakati mwingine huangazia hiari ya mwanadamu, wajibu, na utiifu. Lakini kulingana na ujumbe wa jumla wa Maandiko, kwa hakika ubebaji wa kangaruu unaeleza mchakato huu kwa ubora zaidi.

Baada ya kufundisha kwamba kondoo wake ni wale wanaosikiliza sauti yake na kumfuata yeye, Yesu anaahidi kwamba kundi lake litakuwa na uzima wa milele. Anawaahidi wasikiaji wake kwamba "hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa baba yangu" (Yohana 10:29). Hata hivyo Mkristo binafsi anaweza kuchagua kuuacha mkono wa Baba.

Kukaa katika mkono wa Baba! "Ishini maisha yenu ndani yake," na "mkimbilieni yeye." Ubebaji wa Kangaruu!

**MEI 10** **130**

# Kiambato Kinakosekana

*Samweli akamwendea Sauli; naye Sauli akamwambia, "Ubarikiwe na Bwana! Nimeitimiza amri ya Bwana." Samweli akasema, "Maana yake nini, basi, hiki kilio cha kondoo masikioni mwangu? Na huu mlio wa ng'ombe ninaousikia?"*
*1 Samweli 15:13–14*

Lilikuwa jaribio lake la kwanza kutengeneza biskuti za unga wa shayiri zenye vibanzi vya chokoleti. Akatoa maelezo ya upishi ya kina na kuanza kumwaga viambato katika bakuli la kuchanganyia. Ooh—hakuwa na hamira. Akamtuma mwanafamilia mmoja dukani akanunue. Hatimaye, akachanganya viambato, akaipasha moto oveni, na akapanga hayo matonge kwenye mabamba mawili. Alipoangalia biskuti katika oveni, kuna kitu kilionekana hakiko sawa. Hatimaye, akazitoa kutoka kwenye oveni na akazipanga—kitu fulani kilikuwa na mwonjo tofauti.

Kuna tatizo gani? Akalinganisha maelezo ya upishi na vile alivyokuwa amefanya. Kisha akaona hilo tatizo—alikuwa amesahau kuongeza robo tatu za kikombe cha sukari nyeupe. Kiambato kimoja pekee ndicho kilichokuwa kimepungua—bado, zile biskuti zilizokuwa na mwonjo usiokuwa wa kawaida zilitupwa kwenye pipa la taka. Kiambato kimoja pekee!

Linapokuja suala la kumjua, kumpenda, na kumtumikia mwenyezi Mungu, ni lazima tufanye uamuzi ulio wazi: kama Bwana ndiye Bwana, je, tutachukua maelezo yake ya upishi, mwongozo wake, uelekezi wake moyoni, na kumfuata asilimia 100?

Kwa uongozi wa kiungu, Sauli alichaguliwa kama mfalme wa kwanza wa Israeli. Mzuri, wa kupendeza, mwenye uwezo, maarifa, uongozi dhahiri, alikuwa na kila kitu alichotakiwa kuwa nacho.

Amri ya Bwana ilimjia kupitia kwa nabii Samweli: "Basi sasa, enda ukawapige amaleki, na kuviharibu kabisa vitu vyote walivyo navyo. Wala msiwaachilie" (1 Samweli 15:3). Sauli na jeshi lake wanapata ushindi mkubwa. Lakini Sauli anamwacha hai Mfalme Agagi na kondoo na ng'ombe wazuri. Sauli anadai kwamba ametii agizo. Samweli anauliza kwa nini anasikia milio ya kondoo. Ni kama Sauli aliweka kile tunayoweza kuita hekima yake juu ya amri ya wazi ya Bwana. Samweli akasema, "Kisha Bwana akakutuma safarini, akasema, 'Enenda ukawaangamize kabisa wale Waamaleki wenye dhambi.' . . . Mbona basi hukuitii sauti ya BWANA?" (15:18–19). Sauli anadai kwamba aliwahifadhi wanyama ili amtolee Bwana sadaka. Naye Samweli akajibu, "Kutii ni bora kuliko dhabihu" (15:22). Na, "Bwana NAYE amekukataa wewe usiwe mfalme wa Israeli!" (15:26).

Kiambato kimoja pekee hakikuwapo—utiifu kamili.

Oo, Mungu, nisaidie nikutumaini wewe, Bwana, kama Bwana na nikupe utiifu kamili.

# Wavulana Sita kwenye Safu ya Mbele

*Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako, Kabla hazijaja siku zilizo mbaya, Wala haijakaribia miaka utakaposema, "Mimi sina furaha katika hiyo."*
*Mhubiri 12:1*

Ni kitu gani kilikuwa nyuma ya kile kisa kisichokuwa cha kawaida katika usiku wa mwisho wa umsho kanisani kule Bowling Green, Missouri? Naweza kusema ilikuwa Nick Stumbaugh, mmoja wapo wa wale vijana. Majira ya joto yaliyopita, katika mkutano wa kambini wa wilaya, Nick alimwona Mungu kwa undani zaidi. Aliporudi nyumbani, mchungaji wake alihisi kwamba kuna kitu maalum kilichofanyika kwa Nick. Wakati mchungaji wake alipomwongoza katika *Basic Bible Studies for the Spirit-filled and Sanctified Life*, Nick alitambua kwamba Mungu alikuwa amemtakasa na kumjaza Roho.

Nick alikuwa mchezaji wa kandanda, mchezaji wa mpira wa vikapu, na alikuwa maarufu shuleni. Alipokuwa anaanza kunena na marafiki zake shuleni kuhusu injili, mamake alisema, "Amekuwa katika misheni."

Mchungaji wake alisema, "Nick anawaka moto."

Baada ya ile ibada ya uamsho, wengine walipokuwa wanapiga magoti madhabahuni, wale vijana sita walisimama kuizunguka madhabahu na kuongea. Nilipokuwa ninafunga mizigo yangu niondoke, mmoja wao alinifuata.

Kwa upole kabisa, Nathan Kneib alisema, "Simaanishi kukubughudhi, Dr. Shaver. Nilikuwa tu nataka ujue leo usiku nimemkubali Kristo." Nilifurahi na kumhimiza aanze kujifunza Biblia.

Tarehe 12 Aprili, nilizungumza na mchungaji wa hilo kanisa tena. Alitoa ripoti kwamba mambo yasiyokuwa ya kawaida yalikuwa yanafanyika tangu uamsho huo. Alikuwa amekutana na vijana watano kila mmoja kwa nafasi yake na akaupitia mpango wa wokovu pamoja nao ili aimarishe kujitoa kwao. Wiki mbili baadaye, watu sita walioitikia uamsho walibatizwa. Wale wazazi wa hao mabarobaro walikuwa wanaanza kwenda kanisani. Nick alikuwa anaongoza ibada ya vijana ya Jumatano usiku kwa kujitoa na kwa hamu. Bodi ilikuwa imemwita mchungaji wa vijana.

Mungu asifiwe kwa ajili ya Nick, wale vijana sita kwenye safu ya mbele, na wengine kama wao.[58]

Je, ungetaka kuwa sehemu ya picha kama hii?

MEI 12 **132**

# Shuhuda za Washiriki, Dennis Kinlaw, na Paul

*Ni mapenzi ya Mungu kwamba mtakaswe.*
*1 Wathesalonike 4:3*

Baada ya ibada, hicho chumba kililipuka kwa shuhuda.

Vickie akasema, "Nilikuzwa katika dhehebu la Utakatifu. Nimekuwa nikiandika maelezo usiku mzima na kusafisha nyumba." Baadaye, alitangaza, "Huu ni utakaso. Nimetakaswa! Nimetakaswa!"

Melissa alitoa ushuhuda, "Nimekuwa Mkristo kwa miaka kumi, lakini leo usiku aliingia katika kabati langu lote. Nilimpa uchafu wote, na nimetakaswa."

Juu ya hiyo mada, msomi Dennis Kinlaw aliandika: "Kwa hakika hatuwezi kuitakasa mioyo yetu wenyewe, kwa kuwa nia ile ile ambayo ingechagua kuwa safi hiyo yenyewe ni chafu . . . . Utakaso ni matokeo ya imani kama tu vile kufanywa wenye haki kulivyo kwa sababu ni jambo ambalo ni Mungu pekee ambaye anaweza kufanya . . . . Hivi ndivyo Paulo alivyokuwa anawaambia Wathesalonike alipoomba kwa ajili ya utakaso wao. Alijua hawangeweza kamwe kujitakasa wenyewe."[59]

Paulo aliomba, "Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa. Nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya" (1 Wathesalonike 5:23–24).[60]

58. *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (June 2010).
59. Dennis Kinlaw, *This Day with the Master* (Grand Rapids: Zondervan, 2002).
60. This devotional was previously published in *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (September 2013).

MEI 13 **133**

# Jambo la Kufanya Mungu Anapokuambia . . .

*Kisha Mungu akasema, "Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye— Isaka—ukaende zako mpaka nchi ya Moria. Ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmoja wapo nitakaokuambia."*
*Mwanzo 22:2*

*Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu, Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni. Kisha akamfunga Isaka mwanawe, akamweka juu ya madhabahu, juu ya zile kuni.*
*Mwanzo 22:9*

Steve mwenye urefu wa futi sita na nchi saba alicheza mpira wa vikapu kule Ufaranza. Alilelewa katika nyumba isiyokuwa ya Wakristo, lakini Steve alipoenda katika chuo cha Kikristo, aliona dhihirisho la Kristo katika michezo. Katika ibada ya kanisa, alikuwa ukungu katika hiyo njia alipokuwa akikimbia madhabahuni kuutoa moyo wake kwa Kristo. Aliendelea na akawa mkufunzi mkuu wa mpira wa vikapu katika chuo cha Kikristo. Hapo, aliwaongoza wanafunzi kwa Kristo, akawa na vipindi vya uanafunzi, na kuongoza mikutano ya maombi. Steve alisema haya maisha yalikuwa ya furaha zaidi kuliko yale aliyokuwa nayo awali. Ni wazi kabisa, alikuwa ameyaweka maisha yake yote juu ya madhabahu.

Ibrahimu alikuza uhusiano wa karibu na Mungu, na akatii amri ya Mungu ya kuhamia nchi mpya (Mwanzo 12:1-3). Japokuwa Ibrahimu alikuwa mzee, Mungu alimwahidi mtoto wa kiume (15:1-6). Licha ya hayo, katika agano lake na Ibrahimu, Mungu aliahidi kwamba kupitia kwa huyu mwana, Ibrahimu angekuwa baba wa mataifa (17:1-27).

Miaka kadhaa baadaye Mungu alimjaribu Ibrahimu kwa kumwambia amtoe dhabihu mwanawe—mwana yuleyule ambaye Mungu alikuwa amemwahidi. Mungu anapokwambia umpe kitu chako kilicho bora zaidi, unaweza kutii tu pekee kama una uhakika kwamba Mungu ni mwaminifu, anakupenda, anakutunza, na ana lengo kwa ajili yako. Ibrahimu aliamini haya yote. Lakini wakati alipokuwa tu karibu na kumtoa sadaka mwanawe, Mungu alimpa kondoo dume amtoe badala yake. Mungu akasema, "Sasa ninajua ya

kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee" (22:12).

Kama Mungu alivyoahidi, mataifa mengi yametoka kwa Isaka mwana wa Ibrahimu. Yesu Kristo, Mwokozi wa ulimwengu, pia alitoka kwa Isaka. Baba wa mbinguni alimruhusu Mwanawe wa pekee, Yesu Kristo, afe ili apate kukuokoa na wote wanaompokea.

Mungu atakwambia uweke kila kitu juu ya madhabahu. Kisha, unapofanya hivyo, chunguza vile anavyokupa vitu.

Baada ya kulelewa katika nyumba ya Kikristo, Jim alijenga biashara yake kutoka chini hata akawa milionea. Alitoa mafungu yake ya kumi, lakini hakuwa na furaha. Alikuwa na utupu. Hata hivyo, aliona kujitoa na upendo ndani ya mchungaji wake. Jim alitambua kwamba alikuwa akiweka mitazamo mibaya na kupoteza maisha yake.

Usiku mmoja, Jim alipokuwa amekaa katika Mercedes yake, Mungu alimpa changamoto kwa kumwuliza, "Jim, je unanipenda kweli?"

"Kwa hakika."

"Je, ungenipenda kama ningechukua vitu vyote? Kama ningechukua uwezo wako?"

"Mungu, ninakubali. Nionyeshe kitu chochote ambacho ningekuzuia usifanye kazi kupitia mimi."

Kufikia wakati wa kwenda kulala, Jim alikuwa ametengeneza orodha ya vitu ambavyo vilikuwa vinazuia uwezo wa Mungu kufanya kazi kupitia kwake, na akaanza kuvichukulia hatua. Hatimaye kila kitu kilikuwa juu ya madhabahu. Familia ya Jim ilianza kuitikia mabadiliko aliyokuwa anafanya. Mungu akaanza kumfungulia milango ya kuzungumza na maelfu ya watu kila mwaka, na kanisa lake la nyumbani likakua kutoka 250 hadi 2,000. Jim anapokumbuaka njia zote ambazo Mungu amefanya kazi ndani yake na kupitia kwake, anasema, "Sikuota kamwe kwamba ingekuwa na utimilivu mwingi namna hiyo."

# Paka Wangu Lucky

*Kama vile Baba alivyonipenda mimi, nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu. Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake.*
*Yohana 15:9–10*

Lucky ndiye paka mwenye upendo zaidi, mwema, lakini wakati mwingine anaweza kuwa mwasi na kukosa kutii. Nilikutana na Lucky baada ya jirani yangu kuhama na akachagua kumwacha Lucky asiende naye. Alimtoa tu Lucky nyumbani mwake. Akaendelea kuja kwenye dirisha langu lililokuwa wazi, akilia kutaka kuingia ndani. Wakati wowote nilipokuwa nje, alikuja na akaonekana kuniomba nimpe makao na usalama. Niliamua kumchukua Lucky na kumfanya sehemu ya familia yake. Amekuwa pamoja nami kwa kama miaka kumi na mitano sasa.

Wiki chache zilizopita, Lucky alikuwa mkali na asiyetii siku nzima. Nikiwa nimechoka kutokana na kukabiliana na fadhaa na mashinikizo ya kila siku, nilijipata nikimtolea hotuba hii: “Lucky, niliokoa maisha yako! Ulikuwa huna chochote—huna makao, huna chakula, hakuna usalama, huna ulinzi. Ninakupa *kila kitu*. Ninafanya bidii kutengeneza pesa ili uwe na makao na chakula. Ninakupa wakati wangu, nguvu zangu, na upendo wangu. Nimekupa kila kitu. Je, angalau huwezi kufanya kile ninachotaka ufanye? Je, huwezi angalau kunitii?”

Kisha, kimya—Roho wa Mungu anaponiangukia na kunionyesha usambamba wa moja kwa moja katika maisha yangu mwenyewe. Mungu akasema, *Hufikiri nami huwa ninahisi vivyo hivyo kuhusu wewe*?

Ni kweli kabisa. Mungu aliniokoa, na hunipa vitu na kila kitu ninachohitaji. Siku zote amekuwa wa kutegemeka. Ananifariji, ananilinda, na anayakimu mahitaji yangu yote. Hata alitoa uhai wake kwa ajili yangu.

Kwa nini nisimtii asilimia 100 ya wakati? Kwa nini simtii mara moja siku zote, na nijue kwamba yeye ananilinda, na nimtegemee kikamilifu?

Miriam Burch

# Waliupata Uhuru Wao—na Kupoteza Maisha Yao

*Yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe,*
*bali atakuwa na nuru ya uzima.*
*Yohana 8:12*

Thafi, thangu, na pono, na wengine wengi waliishi katika tangisamaki langu nilipokuwa darasa la saba. Niliwafanyia vizuri sana samaki wangu—ningewawashia mataa au kuwazimia, hali ya joto ilidhibitiwa kati ya nyuzi sabini na sabini na nane, na kuwaingizia hewa kuwapa oksijeni yao. Konokono wa ajabu walisafisha glasi ya tangisamaki, na kambare wa Mto Amazoni walifanya sakafu ya mchanga iwe tupu. Niliwalisha chakula kikavu, lakini pia nilikuza viluwiluwi vya mbu na mabuu meupe ili samaki wangu wapate kula—mnofu na mbavu kubwa za ulimwengu wa samaki. Nina hakika wale samaki walikuwa na furaha.

Kawaida, samaki mmoja aliibuka kama bosi au mkandamizaji wa lile tangisamaki, kawaida akimiliki mahali maalum apendapo sana na kuwafukuza samaki wengine. Usiku mmoja, kabla tu wakati wangu wa kulala kufika, nilimwona bosi akiwa na wasiwasi, lakini sikuweza kujua ni kwa nini.

Wakati wa usiku, bosi aliitisha mkutano wa samaki wote katika hilo tangi. Sina hakika ya jinsi samaki wanavyozungumza, lakini ninadhania alisema kitu kama hiki: *Nyote mnajua kwamba kwa kweli tumefanyiwa mambo mazuri sana na Shaver. Tuna mwangaza, joto, oksijeni, tunahudumiwa kila mara, na chakula bora zaidi. Mnajua nimekuwa na furaha, nikaoa samaki wa ndoto zangu, nikapata watoto na sasa wajukuu. Lakini kuna jambo moja ambalo sikulipenda kuhusu Shaver—anaendelea kutufungia katika hizi kuta za glasi. Jambo hili limenichosha, na mimi nimefika mwisho kuhusu hili. Ni nani anaungana na mimi?*

Kesho yake nilipoteremka gorofa ya chini kwa ajili ya kifungua kinywa, nikampata bosi na samaki wengine watatu wakilala sakafuni katika sebule, wakiwa wakavu na wamekufa. Kwa kuruka kutoka kwenye lile tangi, walipata uhuru wao—lakini wakafa.

Nilihuzunika. Kuta za glasi za tangisamaki hazikuwekwa pale ili iwe kizuizi cha furaha ya samaki. Zilikuwa tu mipaka iliyowaweka hao samaki katika mazingira ya pekee ambapo wangeweza kuendelea kuishi na

kufanikiwa—maji ya moto ya hilo tangi. Nilikuwa nimewapa kwa utunzaji wa hali ya juu kwa ajili yao.

Nimetambua kwamba watu wengine wanachukulia amri za Mungu kama vizuizi vikali vya furaha yao. Ukweli ni kwamba, Mungu katika upendo wake na hekima yake visivyokuwa na mwisho, anajaribu kutuweka katika mazingira ambayo tunaweza kuendelea kuishi na kufanikiwa. Nje ya mapenzi yake, kuna hatari za kufisha maisha yetu ya kimwili na ya kiroho.

Mipaka ya Mungu kama ilivyofunuliwa kupitia kwa Musa ilikuwa zile Amri Kumi (Kutoka 20:1–17). Musa akawaambia Waisraeli, "Endeni njia yote aliyowaagiza BWANA, Mungu wenu, mpate kuwa hai, na kufanikiwa, mkafanye siku zenu kuwa nyingi katika nchi mtakayoimiliki" (Kumbukumbu la Torati 5:33).

Mungu alituagiza kupitia kwa Paulo, "[Neema] yatufundisha 'kukataa' ubaya na tamaa za kidunia, tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa katika ulimwengu huu wa sasa" (Tito 2:12).

Yesu akasema, "Yeye anifuataye [kizuizi] hatakwenda katika giza kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima [baraka]" (Yohana 8:12).

Uhuru wa uongo na kifo viko nje ya amri za Mungu. Ndani ya amri zake, tunapata nuru ya uzima.

**MEI 16** **136**

# Yesu Anapokuombea

*Akasema, Simoni, Simoni, tazama, Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano. Lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike. Nawe utakapoongoka, waimarishe ndugu zako.*
*Luke 22:31–32*

"Ninakuombea wewe na Nancy kila siku," rafiki yangu mmoja alinambia. Kisha akaonyesha amekuwa akifanya hivyo kwa miaka. Hilo liliuchangamsha moyo wangu sana.

Yesu alilitaja jina la Simoni Petro mara tatu katika kutangaza kwamba alimwombea. Hilo linagusa sana, hilo lina uwezo sana, kwamba hata alipokuwa anakabiliana na msalaba na uzizo wa ulimwengu mzima mabegani mwake, Yesu alimwombea mtu mmoja maalum. Aliomba kwa kujua kwamba Petro angemsaliti hivi karibuni. Yesu pia alikuwa anajua juu ya ushawishi mbaya

wa Shetani katikati ya wanafunzi wote. Yesu aliomba na uhakika kwamba Petro angerudi katika imani, na kwamba matokeo ya mwisho ya hadithi hii yangekuwa bora zaidi kwa sababu Petro angewaimarisha wale ndugu Wakristo. Uzoefu wake wa kuanguka na kurudi katika imani kungempa hekima na mkakati wa kuwashughulikia wengine katika wale Kumi na Wawili. Zaidi ya hilo, ungemtayarisha kushughulikia maelfu ya waumini Wakristo wa siku za usoni alipokuwa anakuwa mmoja wapo wa viongozi wakuu wa kanisa jipya. Si ajabu baadaye Petro aliandika, "Mwe na kiasi na kukesha. Kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani, mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani" (1 Petro 5:8–9).

Wakati Yesu alipoomba ombi lake la kuhani mkuu kabla ya kwenda msalabani, alikujumuisha wewe. Kwanza alinena kwa ajili ya wanafunzi wake wa kwanza: "Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu. Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu. Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli. Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni" (Yohana 17:15–18). Lakini kisha, Yesu alikuombea akasema, "Wala si hao tu ninaowaombea. Lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao, wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako" (kif. 20–21).

Yesu aliahidi kwamba angemtuma Roho Mtakatifu kwa wafuasi wake, na huyo Roho Mtakatifu angemwakilisha yeye. Katika Warumi 8:26 tunasoma, "Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu. Kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa." Roho, mwakilishi wa Yesu, hutusaidia kuomba ingawa tuna mipaka yetu.

Sasa Yesu amepaa kwa Babake na Baba yetu. Yesu anafanya nini leo? Waebrania 8:1 inasema, "Tunaye kuhani mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni." Na kazi yake maalum ni ipi? Waebrania 7:25 inatwambia, "Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee."

Je, unaelewa hilo? Yesu Anakuombea.

# Kutubu na Kuburudishwa

*Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana.*
*Matendo 3:19*

Wakati mmoja nilihusika katika semina ya siku tano iliyohudhuriwa na kama watu sitini. Baada ya kukaa chini na kusema na wengi wa wahusika, nilijiuliza, *Kwa nini wana uchungu sana dhidi ya dini na kanisa*? Nilipokuwa ninasikiliza hadithi zao zaidi na zaidi, hatimaye nilipata jibu. Hawa watu walikuwa wamelelewa katika makanisa ambayo yalihubiri, "Umefanya dhambi, na Mungu atakuhukumu." Na huo ndio uliokuwa mwisho—hakukuwa na ahadi ya msamaha. Si ajabu walikuwa na uchungu mwingi hivyo.

Ujumbe wa Petro ulikuwa tofauti. "Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana" (Acts 3:19). Katika kauli hii, anaahidi kwamba dhambi zetu zitafutwa, na kwamba Bwana atatuburudisha, na kwamba toba yetu itatengeneza njia ya kuja kwa Kristo mara ya pili (3:20–21).

Mwana wetu, Paul, alipokuwa na saratani ya ngozi begani mwake, daktari mpasuaji akakata ndani sana na akaondoa kipande kikubwa cha nyama yake. Je, nilimkasirikia daktari? Je, nilidai, "Ulikuwa una haki gani kuuvamia mwili wa mwanangu?" Hapana kwa hakika—nilifurahi kwamba huyo daktari aliitoa hiyo saratani yote kupitia kwa huu upasuaji mkali. Matokeo yake ni kwamba mwanangu aliishi.

Si ajabu Warumi 2:4 inasema, "Wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu." Kwa kutubu, Mungu huondoa hiyo saratani ya dhambi ili uweze kubarikiwa na kuburudishwa.[61]

61. Awali kilichapishwa katika *Reflecting God* Juni–Julai–Agosti 2010 (Kansas City, MO: `WordAction Publishing Co.), 22. Imetumika kwa idhini.

# Mahali Uwezo Unakuwa Muhimu Zaidi

*Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani.*
*Waefeso 3:16*

Waefeso walikuwa wakristo wazuri. Lakini Paulo anaomba ombi la nguvu kwa ajili ya uhalisi wa kujazwa nguvu kupitia kwa kazi ya Roho Mtakatifu mwenye nguvu. Roho atafanya kazi katika "utu" wao na "utu" wako "wa ndani." Mtu mmoja aliueleza kama "mahali uwezo unakuwa muhimu zaidi kwa yule anayemaanisha zaidi."

Kila Mkristo wa kweli ana Roho Mtakatifu (Warumi 8:9) na amezaliwa kwa Roho. Lakini kuna maeneo ya ndani zaidi kwa kazi ambayo Roho anataka kufanya katika moyo wa Mkristo. Roho hukutia nguvu ndani yako, na hata anaweza kukufikisha mahali ambapo "unatimilika na utimilifu wote wa Mungu" (Waefeso 3:19, SUV).

Grant alijaribu kujiokoa mwenyewe kwa akili yake na matendo yake mazuri, lakini alikuwa malimbikizo ya dhambi yaliyochanganyika na jitihada zake. Hatimaye siku ikafika alipoacha matendo na dhambi na akaokolewa kwa neema pale madhabahuni. Mabadiliko makubwa yalitokea maishani mwake—lakini kulikuwa na ukosefu wa usalama kuhusu imani yake uliokuwa unamsumbua. Alikuwa na hakikisho la wokovu lakini alikuwa hana ujasiri. Aliogopa kushindwa. Katika ibada ya mkutano wa kambini, alimsikia mhubiri akinukuu Wafilipi 1:6: "Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu" (SUV). Roho akatembea katika moyo wa Grant. Akaenda akaomba na, ule usiku, akakubali ahadi ya kipawa cha Roho Mtakatifu na akatakaswa.

Nimetazama maisha yake kwa miaka ishirini na mitano tangu wakati huo. Ameendelea kuishi kwa uthabiti katika uwezo wa Roho na utulivu lakini uhakika wa kweli na nguvu. Ameleta mabadiliko makubwa kwa wengine—ana uwezo mahali unapokuwa muhimu zaidi.

# Kipande cha Maisha

*Katika hili tumelifahamu pendo: Yesu Kristo aliutoa uhai wake kwa ajili yetu. Imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu. Lakini mtu akiwa na riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia huruma zake, je! Upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo?*
*1 Yohana 3:16–17*

Katika baadhi ya nchi, kifo ndicho gharama wanayolipa watu wengine kwa kumfuata Yesu. Mimi binafsi ninawajua baadhi ya watu waliolipa gharama ya kufungwa gerezani. Nchini kwetu, kumfuata Yesu kunaweza kukuletea mateso ya kimaneno au ya kisheria—lakini yamkini si kifo.

Baada ya kutukumbusha kuhusu upendo mkuu wa Kristo katika kuutoa uhai wake kwa ajili yetu, Yohana anasema tunapaswa tuwe tunapenda tutoe maisha yetu kwa ajili ya wengine. Kisha Yohana anaweka mkazo juu ya umuhimu wa kuchukua sehemu mali zetu na kumpa ndugu au dada mwenye mahitaji makubwa zaidi. Kwa kufanya hivyo, Yohana anaeleza wazi kwamba hata wakati ambapo hatujaitwa kutoa maisha yetu ya kimwili kwa ajili ya injili, tutaitwa kutoa "sehemu ya maisha yetu."

Nimefanya hivi mara nyingi sana. Katika kazi yangu ya uchungaji na kama Mkristo ninayeishi maisha yangu ya kila siku, nimeitwa nitoe sehemu ya maisha yangu.

Mfano ulio wazi unatoka katika jambo moja wapo nililokumbana nalo kama mchungaji. Wana ndoa wazee kidogo, Roy na Nora walikuwa wahusika waaminifu katika kanisa letu la nyumbani. Walikuwa hawana watoto lakini walikuwa na ushawishi mkubwa wa kiroho kwa mpwa wao aliyekuwa amempokea Kristo. Wakati mmoja wa Krismasi, Nora alilazwa hospitalini, na mguu wake ukakatwa kwa sababu ya ugonjwa sugu.

Asubuhi ya Krismasi, tulikuwa tunajitayarisha kufungua zawadi na watoto wetu watatu, ambao wote walikuwa chini ya miaka sita. Kisha simu ikalia—Roy alikuwa amepatwa na mshtuko mkubwa wa moyo tu hivi punde alikuwa katika hospitali ileile aliyokuwa Nora.

Nifanye nini? Je, napaswa niache asubuhi hii ya kufurahia Krismasi na watoto wangu na niende nikawe na Roy na Nora? Walikuwa hawana watoto

wa kuwasaidia. Nikamwuliza Nancy, mke wangu, awaeleze watoto kwamba tungefungua zawadi baadaye kidogo mchana huo. Nililazimika kuwa na Roy na Nora.

Kwa kutoa sehemu ya wakati wangu wa familia, nilikuwa na wakati mtamu ulioguswa na Mungu, na Roy na Nora. Wote walipona na punde walikuwa kanisani tena wakifanya kazi. Nancy, watoto, na mimi tulikuwa na wakati wa kufurahia kufungua zawadi baadaye mchana ule. Mpaka leo, watoto wetu watatu watu wazima husema kuhusu kuona kujitoa kukileta baraka kwa wengine.

Fikiri kuhusu hili—unaweza kuwa hutaitwa kutoa maisha yako yote ya kimwili mara moja, lakini ni sehemu gani za maisha ambazo Yesu atakuita utoe kwa ajili yake na kwa ajili ya wengine?

**MEI 20** **140**

# Roho Mtakatifu Alitutembelea

*Itakuwa siku za mwisho asema Mungu,*
*nitawamwagia watu wote Roho yangu.*
*Matendo 2:17*

Mwaka wa sabini na tano wa Nazarene Theological Seminary kule jini la Kansas, watu waliosoma chuo hicho waliombwa wasimulie hadithi kuhusu chou hicho. Nilipokuwa ninatafakari kuhusu hiyo miaka yangu mitatu kama mwanafunzi na miaka thelathini kama profesa wa uinjilisti, tukio moja lilijitokeza juu ya mengine yote.

Ilitokea Februari 1970—nilikuwa nimemaliza tu wiki chache za mwaka wangu wa kwanza wa kufundisha hapo. Tulikuwa tumekusanyika kwa ajili ya ibada kwenye kanisa dogo, na Kasisi Paul Cunningham ndiye aliyekuwa mnenaji. Alikuwa amerudi tu kutoka kunena katika ibada maalum za wiki nzima. Katika hizo ibada, wanafunzi wawili kutoka Chuo cha Asbury kule Wilmore, Kentucky, walikuwa wametoa shuhuda zao. Hizi zilifanya kuwe na mzunguko wa nguvu wa Roho Mtakatifu katikati ya wale wanafunzi elfu moja kule Asbury, pamoja na ibada ya kanisa dogo iliyochukua saa 185 bila mapumziko.

Kasisi Cunningham alipokuwa anatoa ripoti ya huo mzunguko wa Roho, Roho Mtakatifu aliwajilia wale watu katika ule umati wa seminari wa kanisa

dogo. Ghafla, mwanafunzi akaacha kiti chake na akapita katikati ya safu kwendea kushoto kwa huo umati, huku akiwa amefunika uso wake kwa mikono yake, akilia. Bila kuona kule alipokuwa anaenda, akagonga kinanda, akakiangusha naye akaanguka pale penye madhabahu ya maombi akilia. Kwa dakika mbili, karibu wanafunzi wengine ishirini walikuwa wamekuja madhabahuni, wengi wao wakilia. Kasisi Cunningham alimtazama huyo rais kana kwamba angesema, *Sasa tufanye nini?* Alikuwa katikati ya ujumbe wake. Waliamua kuimba wimbo wa mwaliko, na Kasisi Cunningham akawahimiza wengine waje mbele. Kama ishirini wengine walikuja. Hapakuwa na nafasi katika hiyo madhabahu, kwa hivyo wanafunzi walipiga magoti tu katikati ya madhabahu yaliyokuwa yamejaa na safu ya kwanza ya viti.

Kama mwalimu wa kitivo, ingekuwa kawaida kwangu mimi kusonga mbele na kuwasaidia wanafunzi kuomba. Lakini siku ile, nilikuwa na hisia takatifu, ufahamu wa uwepo wa Roho Mtakatifu, kiasi kwamba sikuthubutu kutoka kitini pangu, nisije nikatatiza kazi ya Roho Mtakatifu. Hakuna mwalimu hata mmoja aliyeenda popote.

Yule mwanafunzi aliyekuja mbele kwanza alimaliza kuomba, akaenda kwenye kipaza sauti, na akaomba ruhusu ya kuzungumza. Akatoa ushuhuda kwamba ameweza kuendelea kusoma katika hicho chuo kupitia kuuza Biblia, lakini alikuwa ameweka malipo ya mwisho aliyokuwa amekusanya—alikuwa hajayatuma kwa kampuni. Aliuhakikishia huo umati kwamba kutokuwa mwaminifu kulisamehewa na kwamba angetuma hizo pesa baada ya masaa machache.

Alipokuwa amemaliza, wanafunzi wengine walikuwa wanapanga laini ili wanene. Mwanafunzi mmoja alikubali kwamba alikuwa amedanganya kuhusu kukamilisha ripoti ya usomaji ambayo kamwe hakufanya, na akamwomba profesa msamaha. Mwanafunzi mwingine alisema kuwa alikuwa anamchukia profesa mmoja. Mwanafunzi mwingine akakiri kwamba alikuwa amekosana na mwanafunzi mwingine, na akaomba msamaha. Kabla ya kuondoka kwenye kipaza sauti, yule mwanafunzi aliyekosewa alikuwa juu ya jukwaa, na wao wawili wakakumbatiana. Kulikuwa na sifa na kuimba na kufurahi. Ijapokuwa kengele ya mwisho wa ibada ya kanisa dogo ilipigwa, hiyo ibada iliendelea kwa masaa mawili.

Baada ya ibada hiyo, muhula wote ulikuwa tofauti. Ibada za kanisa dogo zilihudhuriwa vizuri na zikajawa na sifa. Wakati mwingine vipindi vya masomo viliingizwa katika maombi kiasi kwamba hawakuingia katika somo. Vipindi vingine vilijawa na kuimba. Wanafunzi walifanya mambo yao kwa upendo na uaminifu.

Hiyo ibada bado ipo akilini mwangu kama ibada kubwa zaidi ambayo nimewahi kuwa sehemu yake. Nilijifunza mengi zaidi kuhusu Roho Mtakatifu katika masaa mawili kuliko nilivyokuwa nimejifunza katika masaa mengi ya mafunzo. Mazingira ya upendo na kuelewa katika muhula wote uliosalia vilikuwa vinatia moyo sana. Roho Mtakatifu Alikuwa Ametutembelea

MEI 21 **141**

# Mungu Atajua

*Kwa maana ni lazima sote tuonekane mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo. Ili kila mmoja wertu aweze kupokea kile tunachostahili kwa ajili ya vitu vinavyofanywa wakati tunapokuwa katika mwili, vizuri au vibaya.*
*2 Wakorintho 5:10*

*Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi, na vitabu vikafunguliwa. Na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima. Na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao. Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.*
*Ufunuo 20:12, 15*

Nilipoteza hati ya kuzaliwa ya mke wangu. Kwa sababu aliihitaji ili apate hati nyingine za kisheria, ilikuwa muhimu sana kupata nyingine. Nikapiga simu kwa ofisi ya takwimu muhimu, nikafanya ombi langu, na nikatoa taarifa za kuzaliwa kwa mke wangu—lakini hilo halikutosha. Makarani wapole na wa kusaidia nilioongea nao walitaka kuwa na hakika kwamba hitaji la mke wangu na jinsi nilivyomwakilisha kwao vilikuwa halali.

Huyo karani akaanza kuniuliza maswali kadhaa ya ajabu. Alinisomea anwani tano za barabara na akaniuliza kama nimewahi kuishi katika moja wapo kati ya hizo. Hizo zote sikuwa nazijua, kwa hivyo nikasema hapana.

Kisha akaorodhesha majiji matano kule Texas na akaniuliza kama niliwahi kuishi katika jiji lolote kati ya hayo. Aliposema Houston, nikajibu, “Ndiyo, nilifanya kazi kwa miezi minne huko.” Alipendezwa na akakamilisha hatua za kututumia hiyo hati mpya ya kuzaliwa.

Baada ya mazungumzo haya, nilianza kufikiri kuhusu swali la Texas. Nilitambua kwamba huyu wakala wa serikali aliyajua maisha yangu vizuri

sana, alikuwa na nakala kamili, hata walijua kwamba, katika safari yangu ya maisha ya miaka themanini na mitano, nilikuwa nimekaa Houston kwa miezi minne.

Nikatambua kwamba kama ofisi ya takwimu muhimu ilijua mengi sana kuhusu mimi, ingekuwa hakuna tatizo kwa Mungu mwenyezi kujua kwa kinamaisha yangu yote. Kwa hivyo tafadhali kuwa tayari, rafiki yangu, kwa kile kitakachotokea mwisho wa maisha yako. Maandiko yanatuambia, “Na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu sawasawa na matendo yao” (Ufunuo 20:12), na, “Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya” (2 Wakorintho 5:10).

MEI 22 142

# Hii ni Sheria ya Namna Gani?

*Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti.*
*Warumi 8:2*

Baraza la jiji lako linakutana. Mwanachama mmoja wa baraza, aliyeudhiwa na uendeshaji wa gari usiokuwa na uangalifu, anabisha kwamba faini ya kupita ilani ya simama inapaswa kuongezwa kutoka $150 hadi $300. Baraza linapiga kura saba kwa sita kwamba, usiku wa manane wa Alahamisi, sheria ya ilani ya simama itabadilika, na faini itaongezwa hadi $300.

Mwanachama mwingine wa baraza ana wasiwasi kuhusu sheria tofauti ambayo imekuwa ikimtatiza na anawashawishi wenzake kuifuta kabisa. Kwa hivyo, baraza linapiga kura kumi na tatu kwa sifuri kwamba, Alahamisi ijayo, jiji lako litaahirisha sheria ya mvutano.

Kwa hakika, isingejalisha hata kidogo kama wangeahirisha sheria ya mvutano. Ingawa sheria ya ilani za simama ni sheria iliyowekwa na wanadamu iliyokusudiwa kuhimiza uendeshaji wa usalama, sheria ya mvutano haiamuliwi na watu. Haya ni maelezo ya nguvu inayofanya kazi katika ulimwengu wetu.

Kwa hivyo tusisumbuke kwamba mwisho wa Warumi 7 na mwanzo wa Warumi 8, mtume Paulo anatumia neno “sheria” kwa njia sita tofauti: “Sheria ya Mungu” (7:22); “katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali” (7:23);

"sheria ya akili zangu" (7:23); "sheria ya dhambi" (7:23); "sheria ya Roho wa uzima" (8:2); na, "sheria ya dhambi na mauti" (8:2). Sheria ya Mungu imefupishwa katika Amri Kumi; sheria nyingine zinataja nguvu zinazofanya kazi katika haiba ya mwanadamu.

Sheria ya dhambi na mauti ni nguvu, nguvu inayotawala, sheria inayofanya kazi katika haiba ya mwanadamu. Inaitwa sheria ya dhambi na mauti kwa sababu hivyo ndivyo dhambi inayozaa siku zote—mauti. Kama Warumi 6:23 inavyothibitisha, "Mshahara wa dhambi ni mauti." Kama sheria ya mvutano inavyowafanya watu waanguke, ndivyo sheria ya dhambi na mauti inavyofanya watu watende dhambi.

Sheria ya Roho wa uzima ni nguvu inayofanya kazi, nguvu inayotawala, sheria inayofanya kazi katika haiba nyingine. Kama Warumi 8:2 inavyosema, sheria ya Roho wa uzima itakuweka huru dhidi ya sheria ya dhambi na mauti. Tafsiri nyingine zinasema "itaniweka *mimi* huru," ambalo lingefanya huu uwe ushuhuda binafsi waPaulo —kivyovyote, tunawekwa huru.

Ezekieli 36:27 anaeleza hii sheria ya Roho: "Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda." Paulo pia anafupisha athari za hii sheria katika Wafilipi 2:13: "Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema."

Neno la Kiyunani la "weka huru" ni neno zito. Katika Warumi 6:18 na 6:22, linaonekana katika kirai "kuwekwa huru mbali na dhambi." Katika Warumi 8:2, muundo wa kitenzi chake linaonyesha jambo ambalo hufanywa wakati fulani. Tafsiri ya The- New Living Translation ya Warumi 8:2 ni, "Kwa sababu ninyi ni wake, uwezo wa Roho atoaye uzima umewaweka huru dhidi ya uwezo wa dhambi inayoleta mauti."

Watu wengi hawapendi kuambiwa la kufanya. Hata hivyo, chukulia kwamba nilihubiri kanisani mwenu Jumapili asubuhi kuanzia saa 5.00 na kumaliza saa 9.00, kisha nikawapa amri ifuatayo: "Sasa nendeni kwa ajili ya mlo wa mchana." Mngefurahi sana kufanya kama nilivyowaambia—sheria ya njaa iliyoandikwa juu ya tumbo lako lote ingeinuka na kukubali hiyo amri.

Nimekutana na baadhi ya Wakristo ambao hatimaye wanamtii Mungu kwa inda, chuki, na kutokubali, kwa sababu nguvu ya ndani yenye ubinafsi humpinga Bwana. Hawa watu wanaweza kusema kwa matwezo, "Sawa, Mungu, nitalifanya."

La! Hivyo sivyo Mungu anavyofanya mambo. Roho wake Mtakatifu atafanya kazi sana ndani yako kiasi kwamba utasema pamoja na mtunzi wa zaburi, "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu" (40:8). Utatii kwa raha na furaha

kwa sababu kuna kitu kimefanyika ndani yako: "Uwezo wa Roho atoaye uzima umekuweka huru dhidi ya uwezo wa dhambi inayoleta mauti."

MEI 23 **143**

# Unaweza Kuwa Huru Kwa Jinsi Gani?

*Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti.*
*Warumi 8:2:*

Mamangu alipozidi kuwa mzee, niliazimia kumtembelea mara nyingi zaidi. Aliishi kule Sanford, Florida, nami niliishi kule Leawood, Kansas. Januari moja, baada ya eneo la Jiji la Kansas kuwa na viwango vya joto ishirini na sita vya chini ya sifuri, nilifikiri kwamba ulikuwa wakati wa kumtembelea. Nilikuwa nimepanga wiki tatu za ibada za uamsho katika sehemu tofauti tofauti na nilikuwa na wiki moja pekee niliyokuwa huru.

Nikajiuliza, *Je, kutakuwa na maana yoyote ya kutoka Kansas hadi Florida na nirudi—maili 2,600—ndani ya wiki moja?* Nikitembea, sitaweza kufika. Nikikimbia, sitaweza kufika. Kama nikitembea kwa kupiga misamba mikubwa mikukwa, sitaweza kufika. Unaona, tangu nilipozaliwa, nimefungwa na sheria ambayo sijaweza kuivunja—sheria ya mvutano. Nguvu yote ya kuvuta chini ya hiyo sheria ingemaanisha kuwa, hatua ndefu zaidi, hatua za haraka zaidi ambazo ningezichukua siku zote zingekuwa na upungufu mkubwa wa kunifanya nisimalize hizo maili 2,600 kwa wiki moja. Nikafikiri kwamba kulikuwa hakuna haja hata ya kujaribu kwenda Florida kwenda kumwona mamangu.

Kama wakati huo huo, rafiki yangu mmoja akaupata usikivu wangu: "Je, hujawahi kusikia juu ya sheria ya juu zaidi—sheria ya elimu mwendo ya hewani? Wakati huu tuna ndege za jeti zenye mwendo wa kasi." Akaendelea, "Ukiwa utajitolea kikamilifu kuamini hii sheria mpya, utawekwa huru dhidi ya hiyo sheria ya zamani." Nikaamua kuijaribu.

Punde tu, nilikuwa ndani ya jeti yenye nguvu ikienda kwa kasi uwanjani ikitaka kuondoka. Ghafla, nguvu ya kuvuta chini ya mvutano ikaishiwa nguvu na sheria ya elimu mwendo ya hewani ikaniweka huru. Baada ya dakika kumi na tano, nilikuwa nimeenda juu futi 32,000, na baada ya masaa matatu

nikatua vizuri sana kule Orlando. Ndiyo, sheria ya elimu mwendo ya hewani iliniweka huru dhidi ya sheria ya mvuto wa chini!

Mtume Paulo ananitaka mimi na wewe tujue uwezo kama huo wa "kutuweka huru."

- "Sheria ya dhambi na mauti"—nguvu ya kiroho inayofanya kazi katika mioyo
- "Sheria ya Roho wa uzima"—nguvu ya kiroho inayofanya kazi mioyoni mwa wanadamu
- "Weka huru"—neno lenye nguvu, linalofanana na Warumi 6:18 ("kuwekwa huru dhidi ya dhambi").
- "Weka huru"—jambo linalofanyika wakati mmoja, si kidogo kidogo

Kama nilifurahi kuwa hatimaye nilijua kwamba "sheria ya elimu mwendo ya hewani" iliniweka huru dhidi ya "sheria ya mvuto wa chini," ingekuwa furaha nyingi zaidi iliyoje ule usiku wa tarehe 2 Septemba wakati ambapo, baada ya mwaka mmoja wa maisha yangu mapya ya Kikristo na mapambano na mvuto wa chini wa ubinafsi uliobaki katika mtazamo na msimamo, sheria ya Roho wa Mungu anayetakasa iliuweka huru moyo wangu Dhidi ya sheria ya dhambi na mauti.

**MEI 24** **144**

# Ikiwa tu Unatembea

*. . . ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho.*
*Warumi 8:4*

*. . . ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho.*
*Warumi 8:4, SUV*

Kuna kundi moja tu peke yake la watu ambalo linatimiza kikamilifu matakwa ya haki ya sheria. (Kumbuka kwamba Warumi 8:4 haisemi "sehemu"—inasema "kikamilifu.") Hilo kundi ni wale ambao "wanaishi" au "wanaenenda" kulingana na Roho. Mara tu Roho anapokuweka huru dhidi ya "sheria ya dhambi na mauti," baada ya hapo utatakiwa kuenenda hatua kwa hatua katika Roho. Au, kama Wagalatia 5:25 inavyosema, utahitaji "ufuate

hatua za Roho." Ni watu wangapi ambao wakati mmoja walikuwa wamejazwa Roho na wameshindwa kuenenda katika Roho?

Naturudi kwenye mfano wa ndege ya jeti wa jana. Hebu fikiri kwamba baada ya sheria ya elimu mwendo ya hewani kuniweka huru dhidi ya sheria ya mvuto wa chini, nimeenda juu futi 32,000 kwa ndege kwa masaa mawili. Huku nikipita juu ya jimbo la Georgia, ninaanza kuhisi kutotosheka katika mambo mengi:

- Watu kumi na wawili hawajanijia kuniambia jinsi nilivyo mzuri sana.
- Ndege inahitaji mabadiliko ya ndani.
- Ubora wa chakula cha ndani ya ndege umeenda chini (kama unaweza kuita njugu mlo).
- Yamkini rubani anahisi kuwa mkuu kwangu kwa sababu ameendesha mamilioni ya maili, na mimi sijaendesha hata nchi moja. Nafikiri ana mtazamo wa kujua kila kitu.

Sina haja ya kuchukua hili—mimi ni mwerevu sana. Sijawahi kuendesha jeti, lakini nina hakika ningeweza kama ingenibidi. Papo hapo, ninatambua mlango wa dharura karibu na kiti changu. Ninavuta kishikio chekundu, ninavuta hicho kibanio upande mmoja, na kuruka kutoka kwenye ndege, huku nikitangaza, "Nitapeperuka peke yangu hadi Orlando!"

Kwa hakika, nitaanguka na kufa. Kwa nini? Kwa sababu moja tu rahisi: punde tu ninapojiondoa kutoka kwenye sheria ya elimu mwendo ya hewani, sheria ya mvuto wa chini ndiyo nguvu ya pekee iliyobaki inayotawala maisha yangu.

Na hivyo ndivyo ilivyo kwa ulimwengu wa kiroho. Ni sawa na kama tumekuwa watendaji katika kazi ya Mungu, lakini hatukuridhishwa na kanisa kwa sababu zifuatazo:

- Watu kumi na wawili walishindwa kunijia Jumapili asubuhi kuniambia jinsi nilivyo mzuri sana.
- Kanisa liliweka zulia la kijani kibichi wakati nilipokuwa ninajua kuwa rangi ya waridi ingekuwa bora zaidi.
- Kile chakula cha kuletwa na kila mtu hakiko vile tulivyokizoea.
- Kiongozi wa kanisa ana hakika kwamba yeye yuko sahihi. Siku zote anasukuma ajenda hii au ile. (Unatakiwa kuamua kama yule kiongozi ni Bwana au ni mchungaji.)

Ni kitu gani kinachofanyika hapa? Ni rahisi: Punde tu tunapojiondoa kutoka kwenye "sheria ya Roho wa uzima," sheria ya dhambi na mauti ndiyo nguvu ya pekee iliyobaki ya kutawala maisha yetu.

Je, unaiona? "Matakwa ya haki ya sheria" yanaweza tu "kutimizwa *kikamilifu* ndani yetu" kama tukienenda katika Roho.

# Marashi Mazuri

*Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo, mbele za Mungu, katika wao wanaookolewa, na katika wao wanaopotea.*
*2 Wakorintho 2:15*

Vyungu kumi na vinne vya pilipili katika sherehe yetu ya mapishi ya kila mwaka vilieneza harufu nzuri ya kudondosha mate katika jengo lote la kanisa. Kwa upande mwingine, kulikuwa na harufu mbaya ya mayai yaliyovunjika yaliyoachwa juu ya meza ya jikoni kwa siku mbili—ilikuwa mbaya.

Katika kila kisa, harufu mbaya iliyotoka msingi wake ulikuwa juu ya kile kilichokuwa kinafanyika katika kiwango cha ndani zaidi. Kwa wale kati yetu ambao, kwa neema ya Mungu, wanamfuata Kristo kwa ushindi, "na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu" (2 Wakorintho 2:14, SUV). Tunapoachilia kila kitu kwa Kristo na misheni yake katika kiwango cha ndani ya moyo, harufu nzuri inasikiwa na Mungu na pia wanadamu. Harufu nzuri ambayo watu walio karibu na sisi kusikia inategemea na kujitoa kwa mioyo yao wenyewe (2:16).

Sasa imekuwa siku kumi na moja tangu Evan na Jody wamkubali Kristo. Evan amesema kwamba ana maana mpya ya amani, na Jody anasema anahisi utulivu. Jody alionyesha mshangao wake kwa hili, akisema, "kwa miaka, nilikuwa nimedanganywa kufikiri kwamba usingeweza kutangaza imani yako—kwamba lilikuwa jambo la siri. Lakini kwa wiki yote nimekuwa nikiwaambia watu kule kazini kile ambacho Bwana ametufanyia, na hakuna mtu aliyekasirika."

Kuna harufu nzuri katika maisha ya Evan na Jody, kama tu ilivyo kwa wale walioambiwa habari za Kristo. Ni harufu nzuri ya aina gani unayoacha?[62]

62. Awali kilichapishwa katika *Reflecting God* Juni–Julai–Agosti 2010 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 15. Imetumiwa kwa idhini.

MEI 26 146

# Mwaminifu kwa Mambo Machache, Sehemu ya 1

*"Vema mtumwa mwema na mwaminifu! Umekuwa mwaminifu*
*kwa machache, nitakuweka juu ya mengi.*
*Ingia katika furaha ya bwana wako!*
*Mathayo 25:21*

Uaminifu ni jambo muhimu sana kwa Mungu. Wazo hili limetajwa tena mahali pengine katika Maandiko:

- Mathayo 24:46–47—"Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo. Amin, nawaambieni, atamweka juu ya vitu vyake vyote."
- Luke 16:10—"Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia."
- Luke 19:17—"Kwa vile ulivyokuwa mwaminifu katika neno lililo dogo, uwe na mamlaka juu ya miji kumi."

Katika visa hivi vyote, uaminifu wa sasa huleta matokeo ya matunda mengi zaidi.

Paulo aliitwa katika huduma, lakini alikuwa akihangaika katika seminari. Hatimaye akajitoa mwenyewe kwa Mungu kikamilifu, na Mungu aliendelea kumtakasa wakati wote. Wakati wa kufuzu, makanisa kadhaa yalimwita akawe mchungaji. Mwishowe, akaacha miito kutoka makanisa makubwa zaidi kwa sababu alihisi alikuwa anaongozwa kwenda kuchunga kanisa la washiriki arobaini na sita.

Hilo kanisa lilikuwa na watu wazuri sana—lakini lingekua kidogo kisha likaanguka kidogo. Paulo akajiingiza kwa moyo mmoja katika kazi yake na akaanza kuomba, kujifunza, kuhubiri na kuita. Siku moja alisihi katika maombi, "Oo, Mungu libariki hili kanisa."

Bwana akamjibu: *Kama kweli unataka kubariki kanisa, unaweza kuanza kwa kuchanga angalau dola elfu moja kwa ajili ya Misheni*.

Hili lilikuwa miaka kadhaa iliyopita, na kanisa lilikuwa halijawahi kuchanga dola elfu moja kwa ajili ya Misheni. Paulo akajibu, "Bwana, kama ni lazima tuchange dola elfu moja kwa ajili ya Misheni, itanibidi nitoe dola mia moja." Alikuwa ameshtuka—hakuwa na dola mia moja.

*Bwana akasema, la, nitakwambia utoe dola mia mbili.*

Paulo akatatizika. Hakuwa na dola mia mbili pia. Lakini akafikiri, kama alitaka kununua gari na hakuwa na pesa, angechukua mkopo. Kama akitaka kumheshimu Mfalme Yesu, kwa nini asichukue mkopo kwa ajili ya Misheni? Akaenda katika benki yake, na mahojiano yake na raisi wa benki yakapangwa. Raisi wa benki akamwuliza, "Kwa nini mhubiri atake kuomba dola mia mbili?"

Unawezaje kumweleza raisi wa benki ambaye mvuto wake uko katika uwekezaji wa biashara za nyumbani, kwamba utazitoa kwa kanisa lako na kwamba watazitumia kwa ajili ya kazi za umishenari kule Musumbiji, Papua New Guinea, na Peru? Paulo tu kirahisi alimwambia kuhusu hospitali, shule, makanisa, na Mungu kubadilisha maisha ya watu katika zaidi ya mataifa 160. Yule mkuu wa benki akampa huo mkopo na akasema, "Ninaamini katika programu kama hiyo. Hundi yangu ya kwenda katika hayo matoleo ndiyo hii."

Paulo akachukua hizo hundi zake, akalihamasisha kanisa, na wakachanga zaidi ya dola elfu moja. Mungu alikuwa anatazama, na akaona kanisa na mchungaji aliyekuwa mwaminifu katika jambo dogo. Sasa angeweza kuwaamini na jambo kubwa zaidi.

**MEI 27** **147**

# Mwaminifu kwa Mambo Machache, Sehemu ya 2

*Vema mtumwa mwema na mwaminifu! Umekuwa mwaminifu*
*kwa machache, nitakuweka juu ya mengi.*
*Ingia katika furaha ya bwana wako!*
*Mathayo 25:21*

Baada ya matoleo ya misheni, kanisa la Paulo lilianza kukua—uhudhuriaji ukaongezeka hadi watu sabini na, themanini na, tisini na, kisha likaongezeka hadi mia na ishirini. Kanisa ikawa halina nafasi ya kutosha, kwa hivyo Paulo akakusanya viongozi wa kanisa pamoja na akawauliza, "Je, tupunguze jitihada zetu, au tutafute nyenzo kubwa zaidi?" Viongozi walitaka kukua.

Dhehebu la Paulo lilikuwa maarufu kwa kujenga vyuo vya sanaa huru vya Kikristo katika maeneo muhimu nchini kote, na walikuwa wanapanga kujenga chuo kipya katika eneo la katikati la Marekani—eneo lilimokuwa kanisa la Paulo. Paulo akakutana na raisi wa benki yake, na pamoja, wakaamua kuwaomba viongozi wa biashara wenyeji watoe ardhi kwa ajili ya hicho chuo kipya. Punde, viongozi wenyeji walikuwa tayari kutoa ardhi—ekari themanini

zilizokuwa karibu tu na mpaka wa jimbo, zenye thamani ya mamilioni ya dola—kama zawadi kwa hilo dhehebu kama wangejenga chuo chao kipya hapo.

Viongozi wa dhehebu walitafutwa, mipango ikafanywa, majengo yakajengwa, na sheria ikawekwa kuwa kanisa la Paulo liwe na kipande cha hiyo ardhi. Kanisa likatumia nafasi hiyo kujenga jengo kubwa zaidi. Chuo kipya kikakua, kanisa la Paulo likakua, na punde walihitaji jengo kubwa zaidi. Raisi wa benki akatoa zawadi ya $100,000 kwa ajili ya hilo.

Chuo kilipokuwa kinakua, mji pia ukakua, na watu wengi zaidi na zaidi wakavutiwa na kanisa. Baada ya miaka ishirini na tisa ya uongozi wa Paulo, washiriki walikuwa wameongezeka, na kanisa likawa limekuwa moja wapo ya makanisa makubwa zaidi katika hilo dhehebu.

Katika Mkutano Mkuu wa Mwaka 1993, wa Dhehebu, Paulo, ambaye katika maisha yake alikuwa amechunga kanisa moja pekee, alichaguliwa kuwa askofu mkuu—cheo kikuu na muhimu zaidi ulimwenguni, cha uongozi wa hilo dhehebu. Alitekeleza uongozi wenye uwezo katika cheo hicho kwa miaka kumi na sita. Mungu alikuwa amempata mtu aliyekuwa mwaminifu kwa mambo machache, kwa hivyo Mungu akamweka juu ya mambo mengi. Paulo alikuwa mtu ambaye Mungu aliweze kumwamini.

Huyo mtu alikuwa Paul Cunningham; chuo ni MidAmerica Nazarene University; kanisa lilikuwa College Church of the Nazarene kule Olathe, Kansas.

Mungu anaweza kukuamini kwa kiasi gani?

**MEI 28** **148**

# Kile Roho Atakachofanya kupitia Wewe

*Lakini yeye akijaa Roho Mtakatifu, akakaza macho yake, akitazama mbinguni, akauona utukufu wa Mungu, na Yesu akisimama upande wa mkono wa kuume wa Mungu. Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, "Bwana Yesu, pokea roho yangu." Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, "Bwana, usiwahesabie dhambi hii." Akiisha kusema haya akalala. Na Sauli alikuwa akiona vema kwa kuuawa kwake.*
*Matendo 7:55, 59–60, 8:1a*

Tarehe 11 Septemba, 2001, ndege nne za bishara zilitekwa nyara na maharamia katika mashambulizi yaliyopangwa dhidi ya Marekani. Ndege mbili zikapiga World Trade Center kule Jiji la New York, na zaidi ya watu elfu mbili wakauawa. Ndege nyingine ikapiga Pentagoni kule Washington, DC.

Saa 3:28 asubuhi, ndege ya nne, Flight 93, ilitekwa nyara na maharamia waliokusudia kuiangusha katika jiji kuu la taifa. Saa 3:57, abiria Todd Beamer alilia kwa sauti kubwa, "Natuchukue hatua!" na akaongoza nguvu ya kudhibiti ndege hiyo kutoka kwa hao maharamia. Saa 4:03, ndege hiyo ilianguka kule Shanksville, Pennsylvania, katika mwendo wa maili 563 kwa saa. Abiria wote waliokuwamo walikufa. Walikuwa bado tu dakika kumi na nane za mwendo wa ndege wafike Washington, DC—jiji kuu na watu wake wakapona.

Ni kitu gani kinachowafanya watu wengine wanakuwa na uwezo sana na kuweza kufanya mambo makuu, hata mambo ya kishujaa? Sasa tunajua kwa kina kuhusu Todd Beamer: Alilelewa katika nyumba ya Kikristo iliyomcha Mungu. Alihitimu kutoka Wheaton College, shule ya Kikristo. Alimwoa Lisa, mwanamke mcha Mungu. Muda mfupi kabla ya ndege kuanguka, alikuwa anajifunza *A Life of Integrity* na kundi lake la uanafunzi la wanaume. Akampigia Lisa Jefferson, an air-phone operator in Chicago, na wakakariri Sala ya Bwana pamoja. Katikati ya utekaji nyara aliomba, "Yesu, nisaidie." Muda mfupi baada ya hilo ombi ndipo aliposema, "Natuchukue hatua," na akaongoza mashambulizi kwenye chumba cha rubani. Nyuma ya ushujaa wa Todd Beamer, tunavumbua uhusiano wake na Yesu Kristo.

Ijapokuwa si matendo yote ya ujasiri ni ya kishujaa, Maandiko yanatuonyesha mifano mingi ya watu waliokamilisha kazi nzuri kwa msaada na uwezo wa Roho Mtakatifu:

- Tunaona hili katika Petro (Matendo 4:8–12). Akiwa amejaa Roho, kwa ujasiri alikabiliana na wakuu watesi na akatangaza wokovu kupitia kwa Kristo peke yake.
- Tunaona jambo hili katika Stefano (Matendo 7:55–60). Akiwa amejaa Roho, alimwona Yesu kule mbinguni na akaomba kwa ajili ya msamaha wa wale waliokuwa wanampiga mawe.
- Tunaona hili katika kundi la Wakristo (Matendo 4:31–35). Wakiwa wamejaa Roho, waligawanya mali zao mpaka kukawa katikati yao hakuna mtu aliyehitaji kitu.
- Tunaona hili katika Barnaba (Matendo 11:24). Akiwa amejaa Roho, aliwatia moyo watu wengi sana walioletwa kwa Bwana.
- Tunaona hili katika Paulo (Matendo 13:9–12). Akiwa amejaa Roho, alimkazia macho Elima mwovu na akamkemea.

- Tunaona hili katika Filipo (Matendo 6:1–5; 8:26–30). Akiwa amejaa Roho, alimwongoza mwandishi wa hazina ya malkia wa Ethiopia kwa Kristo.
- Tunaona hili katika Sauli, aliyemwona Stefano aliyekuwa amejaa Roho akipigwa mawe hadi kufa na aliathiriwa sana hivi kwamba akamkubali Kristo na kuwa Paulo.

Hii orodha inaweza kuwa ndefu sana. Roho Mtakatifu huwatia watu nguvu ya kufanya mambo makubwa, mazuri, na ya neema.

Jambo hili ni halisi kwa Jenee. Wazazi wake walimwacha alipokuwa na miezi miwili. Alianza kutumia mihadarati akiwa na miaka kumi na mmoja. Kama kijana, alitiwa mbaroni zaidi ya mara ishirini na nne. Jenee alitiwa mbaroni na FBI na alikuwa anakabiliwa na kifungo cha maisha wakati alipokutana na Yesu kupitia kwa mtu aliyekuwa Mkristo maisha yake yote, mnamo tarehe 6 Machi 2005. Kristo akamkomboa dhidi ya kutawaliwa na mihadarati kwa miaka kumi na tisa na kwa neema ya Mungu akambadilisha. Miezi mitano baada ya kuokoka, Jenee alipokuwa anajifunza *Basic Bible Studies for the Spirit-filled and Sanctified Life* na kumaliza siku zake thelathini za mwisho katika programu ya detox, alikubali kipawa cha ujazo wa Roho Mtakatifu na akapata utakaso kamili.

Leo, Jenee ni mhudumu aliyewekwa wakfu na anatumika kama mchungaji anayelipwa katika kanisa la Jiji la Kansasi. Wakati wa kuandika hili, alikuwa amemaliza tu kuongoza vijana kumi na wawili kupitia mafunzo ya utakaso yaliyomwathiri sana. Alishinda Tuzo ya Uinjilisti katika seminari anayohudhuria. Maisha na huduma ya Jenee hutiwa nguvu na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu atafanya nini kupitia kwako wewe?

**MEI 29** **149**

# Kipawa Bora Zaidi

*Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao!*
*Luka 11:13*

*Je! Si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao!*
*Mathayo 7:11*

Ni zawadi gani bora zaidi ambayo mtu mwingine amewahi kukupa? Mungu atakupa wewe zaidi kuliko hiyo aina ya zawadi—atakupa Roho Mtakatifu. Fungu letu lililo sambamba katika Mathayo inatwambia kwamba Mungu hutoa "vipawa vizuri." Hivyo basi, tunaweza kuchukulia kwamba Roho Mtakatifu ndicho kipawa bora zaidi kuliko vipawa vizuri vyote. Kwa huyu Roho Mtakatifu, unaweza kuzaliwa kwa Roho, ukajazwa Roho, na ukaongozwa na Roho.

Pengine jibu la kuvutia zaidi la maombi ambalo nimewahi kulipata lilitokea wakati nilikuwa ninachunga kanisa langu la kwanza. Kanisa letu lilikuwa linakua, na nilikuwa nimewekeza sana katika Bev na Floyd. Floyd alikuwa ameokoka, akajiunga na kanisa, na akachaguliwa katika bodi.

Baada ya kuhusika kikamilifu katika kanisa kwa zaidi ya mwaka mmoja, Floyd aliomba akutane nami Jumapili moja wakati wa mchana. Nilipata mshtuko kabisa, aliposema, "Mimi na Bev tunaondoka kanisani."

"Kwa nini?" Nikajibu. "Je, mmenikasirikia kuhusu jambo fulani?"

Floyd akasema, "Ndiyo, lakini sikwambii kuhusu nini."

Nikasema, "Kama huwezi hata kunambia ni kitu gani, ni vigumu kulishughulikia. Kile ninachoweza kusema ni kuwa nitaliombea."

"Unaweza kuomba vyote unavyotaka. Sisi tunaondoka." Alipomaliza kusema hivyo, Floyd akanipa rekodi za mwekahazina kutoka katika moja lapo la mashirika yetu ya ziada.

Nilifadhaika nilipokuwa narudi katika nyumba ya mchungaji na nikamwambia mke wangu. Hivi karibuni tulikuwa tumealikwa kuchunga kanisa kubwa zaidi—mara mbili kwa ukubwa, nyumba ya mchungaji yenye ukubwa mara mbili, na mshahara wa mara mbili. Niliukataa mwaliko huo, nikiamini mapenzi ya Mungu kwetu yataendelea katika kazi yetu tuliyo nayo sasa. Lakini baada ya mazungumzo yangu na Floyd, nikamwambia Nancy, "Kama hivyo ndivyo watu wanavyohisi kuhusu sisi hapa, basi labda ni wakati wetu sisi kuondoka."

Nancy akajibu, "Nisingependa ibilisi akulaghai hata ufikiri hivyo ndivyo kila mtu anavyohisi. Hivi ndivyo watu wawili wanavyohisi."

Nikatambua kwamba alikuwa sahihi. Nikaenda katika chumba changu cha maombi na nikafunga mlango.

Nikaomba, "Bwana, niko tayari kuacha hili kanisa katika aibu kama hivyo vitaendeleza ufalme wako—au nitakaa na kupigana. Niambie la kufanya."

Wakati uo huo, mfano wa mbwa mume ukapita katika jicho la akili yangu. Nilijua sifa za mbwa mume: hushikilia hivyo hata iwe nini.

Nikasema, "Ni sawa, Bwana, nitakaa." "Lakini kuhusu Floyd je?"

Bwana akanambia, *Nitasema na Floyd*.

"Vyema!" Nikasema kwa sauti kubwa.

Kisha Mungu akanipa agizo la ziada: *Usimwambie mtu yeyote kuhusu hili kwa siku saba*.

Kwa hakika kabisa, siku ya saba, Floyd alikuja kwangu. Akauliza, "Je, umemwambia mtu yeyote kwamba nimeondoka kanisani?"

Nikamwambia sikuwa nimemwambia mtu yeyote.

Floyd akasema, "Kama hujamwambia mtu yeyote, mimi na Bev tumeamua kukaa hapa. Nitarekesja rekodi zangu za mweka hazina."

Nikakaa katika lile kanisa kwa miaka mitatu zaidi. Kufikia mwaka wa mwisho, kanisa lilikuwa na uhudhuriaji wa juu zaidi, washiriki wengi zaidi, na utoaji wa kifedha wa juu zaidi. Floyd aliingia kanisani ndani kabisa na akawa nguvu kuu katika programu yetu ya ujenzi. Mwaka uliofuata, tulikuwa na kanisa jipya zuri na kitengo cha elimu.

Ninafurahi nilikaa na kungojea kwa siku saba. Ninashukuru Mungu alinena na Floyd. Na nimeona maombi mengine mengi ambayo Mungu amejibu tangu nilipojazwa na Roho.

**MEI 30** **150**

# Roho Mtakatifu Alikuwa Hajamaliza

*Na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi,*
*mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu. Basi atukuzwe yeye*
*awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au*
*tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu.*
*Waefeso 3:19–20, SUV*

Nilijifunza mengi sana kwa kuona uongozi wa Roho juu ya Floyd na Bev. Unapofadhaika, ni rahisi kutoa kauli ya jumla. Waliponambia wanaondoka kanisani, nilifikiri, *Kama hivyo ndivyo watu wanavyohisi kuhusu sisi*—huku, katika uhalisi, hivyo vilikuwa tu jinsi Floyd na Bev walivyohisi. Nilijifunza kwamba hupaswi kufanya uamuzi mkubwa wakati unapokuwa umechoka, una wasiwasi, u mgonjwa, au umefadhaika. (Ijapokuwa, kama mtu mmoja alivyotoa mzaha wakati mmoja, "Hilo ni wakati wote.")

Sehemu ya ombi langu imekuwa, "Vipi kuhusu Floyd?" Karibu na wakati tulipomaliza kujenga kanisa jipya, Floyd alikuja kwangu na akasema, "Mchungaji, nimepewa kazi nzuri kule Michigani. Ninahisi natakiwa

kuichukua. Sasa tuna watoto watatu. Sijasoma vizuri, na kazi zangu hapa ni za mshahara wa chini. Tunahitaji kuondoka."

"Floyd, ninachukia kukuona unaenda—wewe kwangu ni kama mwangangu. Lakini ninaelewa."

Kabla Floyd na Bev hawajaondoka, walitupeleka kwenye mkahawa mzuri zaidi ambao hatujawahi kuingia na kula tangu tulipokuja Jiji la Kansas. Kule katika nyumba ya mchungaji, Floyd alitembeahuku na huku kwa wasiwasi. Baada ya muda kidogo, hatimaye alinambia, "Mchungaji Shaver, wewe ndiwe mtu mzuri zaidi ninayemjua." Haikuwa kweli, lakini kulingana na vile alivyokuwa akihisi kuhusu mimi awali, ninashukuru alihisi ilikuwa hivyo.

Hiyo familia ikaenda Michigan, na Floyd akaanza kazi yake mpya. Baada ya siku chache, ilimbidi aiache. Kazi ilikuwa ya juu kuliko yeye. Akalalamika kwa Bev—wanapaswa kufanya nini tena? Alihisi kwamba maarifa yake yalikuwa na upungufu.

Floyd akaenda benki na akapata kazi ya kufuta sakafu baada ya masaa. Kisha akapata kandarasi ya kupeleka matambara ya kutiwa kemikali ya kuwekwa njiani kwenye milango ya benki. Alilazimika kupeleka hayo matambara kwa dobi mwingine kwa kuwa mashine ya Bev haikuweza kwa kuwa yalikuwa mazito sana. Alipokuwa huko, alitambua hali ya hiyo dobi na akapata kandarasi ya kufuta sakafu *zao* na kuwaletea matambara yao ya njiani. Lililofuata, alipata duka la vyuma na duka la vyakula.

Wakati uo huo, familia ilihusika katika kanisa lao la nyumbani, ambalo lilikuwa kubwa kuliko langu kwa mara mbili. Floyd alichaguliwa katika bodi ya kanisa na kuongoza kamati muhimu.

Nilipowapigia nijue wanaendeleaje, Bev alisema Floyd alikuwa anatumika sana kanisani. Nikamwuliza Floyd biashara yake ya uhudumu wa ofisi ilivyokuwa inaendelea.

Akasema, "Oo, niliiuza. Sasa ninamiliki duka kubwa zaidi hapa jijini. Katika hilo duka kubwa, ninaendesha duka la nguo. Nina duka lingine la nguo hapa jijini kaskazini mwa hapa."

Muda fulani huko nyuma, nilikutana na Bev na Floyd katika mkutano wa kambi wa Michigan. Wote walikuwa wanafurahi na wana moto kwa ajili ya Yesu.

Katika ombi langu la mwanzo, nilimwomba Mungu, "Vipi kuhusu Floyd?" Katika kujibu, Bwana "aliweza kutimiza kwa wingi zaidi sana kuliko yale tunaweza kuomba au kudhania." Roho Mtakatifu alikuwa bado hajamalizana na Floyd. Na bado hajamalizana na wewe pia!

# Unahitaji Nguvu za Roho

*Na tazama, waletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu.*
*Luka 24:49*

Wanawake wawili walikaa katika safu ya mbele ya kanisa la D. L. Moody. Wakati wa kufunga ibada, wakamwambia, "Tumekuwa tukikuombea."

"Kwa nini hamwaombei watu?" Moody akauliza.

Wale wanawake wakajibu, "Kwa sababu unahitaji nguvu za Roho." Wakaja kuongea na Moody na wakamwombea kwamba ajazwe nguvu za Roho Mtakatifu.[63]

Yesu alikuwa na shauku iyo hiyo kwa ajili ya wanafunzi wake. Alikuwa tayari amewafundisha kuhusu kuja kwa Roho Mtakatifu aliyeahidiwa (Yohana 14–16). Uaminifu wao katika kumfuata Yesu ulikuwa umekuwa wa kugeukageuka. Wakati mwingine walikuwa ndani wote; wakati mwingine, walibishana juu ya ni nani mkubwa, wakatafuta heshima za juu, au kumwacha Kristo wakati shinikizo lilipokuwapo. Katika Luka 24, Yesu alifufuka na akawapa wanafunzi maagizo ya mwisho. Alijua ilikuwa bora kwao kwenda mahali maalum na wakamngojee Bwana—wangehitaji uwezo wa Kristo kwa ajili ya kazi kuu ya kuwa mashahidi wake. Walitii na wakajazwa nguvu za Roho (Matendo 1:8 na 2:1–4).

Akiwa na umri wa kama miaka kumi na minane, Dwight Moody aliongozwa kwa Kristo na mwalimu wake wa shule za Jumapili, Bw. Mr. Kimball, kule nyuma ya duka la viatu ambapo Moody alikuwa akifanya kazi. Baada ya hapo, maisha yake yote yalibadilika. Alisema, "Kabla ya kuokolewa, nilifanya kazi kuendea msalaba, lakini tangu hapo nimefanya kazi kutoka msalabani; kisha nikafanya kazi ili niokolewe, sasa ninafanya kazi kwa sababu nimeokoka."[64]

Moody akahamia Chicago na akaanzisha shule ya Jumapili iliyokua hadi 1,500. Hatimaye, akaanza kuhubiri.

---

63. James Gilchrist Lawson, *Deeper Experience of Famous Christians* (Anderson, IN: Warner Press, 1911), 347.

64. Lawson, *Deeper Experience of Famous Christians*, 342.

Akaenda Uingereza kujifunza njia za wafanyakazi Wakristo katika hiyo nchi. Alianza kuwa na njaa ya kuona Ukristo wa kina alipomsikia Henry Varley akisema, "Ulimwengu bado haujaona kile atakachofanya Mungu na, kwa ajili ya, na kupitia kwa na katika na kwa mtu aliyewekwa wakfu kikamilifu kwake."[65]

Moody akaenda Jiji la New York kukusanya pesa za kujengea Chicago baada ya moto wake mkubwa. Lakini moyo wake haukuwa katika hiyo kazi. Baadaye alisema, "Nilikuwa ninalia wakati wote kwamba Mungu angenijaza Roho wake. Mm, siku moja, katika jiji la New York . . . Ninaweza kusema tu kwamba Mungu alijifunua kwangu, na nikauona upendo wake hivi kwamba ikanibidi nimwombe aendelee kuuweka mkono wake. Nikaenda kuhubiri tena. Mahubiri hayakuwa tofauti . . . lakini mamia ya watu waliokolewa."[66]

Moody akasafiri huko na huko kati ya Uingereza na Marekani. Watu wengi kama elfu arobaini walimsikia akihubiri kule Glasgow. Mkutano wake wa injili wa mwisho kule Jiji la Kansas; huko, alishikwa na matatizo ya moyo akaenda kufa nyumbani. Mwaka wa 1899, baadhi ya maneno yake ya mwisho yalikuwa, "Huu ni ushindi wangu. Hii ni siku yangu ya kutawazwa. Nimeitarajia kwa miaka mingi."[67]

Uwezo wa Roho Mtakatifu upo kwa ajili ya wanafunzi wa Yesu; kwa ajili ya Dwight Moody; kwa ajili yangu mimi na wewe.

**JUNI 1** **152**

# Starehe

*. . . ili Kristo aweze kukaa mioyoni mwenu kupitia kwa imani.*
*Waefeso 3:17a*

Hapa kuna kirai kilichonitatiza kutoka kwa ombi kuu la Paulo kwa ajili ya Waefeso, 3:14–21. Kanisa la Efeso halikuwa kanisa la matatizo, hawa watu walikuwa Wakristo wazuri na wa kweli. Paulo aliowaombea watiwe nguvu na Roho (3:16) na kwamba na kwamba wangeimarika katika upendo (3:17). Hilo linaeleweka, lakini kuomba "kwamba Kristo akae mioyoni mwenu" kwa watu ambao walikuwa wamempokea Kristo tayari halieleweki.

65. Lawson, *Deeper Experience of Famous Christians*, 345–46.
66. Lawson, *Deeper Experience of Famous Christians*, 348.
67. Lawson, *Deeper Experience of Famous Christians*, 351.

Jibu limo katika kuelewa utajiri wa neno “kaa.” Msomi wa Biblia Willard Taylor anasema: “Neno la Kiyunani la ‘kaa’ linatoka katika neno linalomaanisha ‘kufanya makao,’ ‘kufanya makao ya kudumu.’ Kwa hivyo Kristo haji kama mgeni, au kuwekwa kizuizini kihatari, lakini kama mkazi Mkuu nyumbani mwake halisi.”[68]

Katika nchi yetu tunatumia tamko hili: “Starehe.” Huwapa wageni ruhusa ya kujifanya wawe watulivu na wenye kustarehe kama ambao wako nyumbani kwao.

Kama mwinjilisti, nimesafiri sana; nimetia vitu vyangu kwenye sanduku na kukaa katika nyumba za washiriki. Nashukuru kwa mamia ya watu walionifungulia nyumba zao kwa upendo usiokuwa na ubinafsi. Kila mara, ninapoingia, ninaonyeshwa chumba cha wageni na kuambiwa, “Dkt. Shaver, tafadhali starehe.” Ninaanza kutoa vitu vyangu na kuchukua suti na makoti mawili na kuning’iniza kwenye kabati, na kupata kwamba hiyo kabati imejaa nguo ambazo hiyo familia itazitumia katika mabadiliko ya majira yatakayofuata. Ninaweka suti yangu na makoti yangu juu ya hicho kitanda mpaka nipate suluhisho. Ninatoa shati zangu, zikiwa zimekunjwa kwa uangalifu ili zisiwe na mikunjo. Ninachukua shati nne na kuzipeleka kwa watoto wa meza na kutambua kuwa kila mtoto wa meza kati ya watoto wanne amejaa kabisa. Nifanye nini? Mkutano wa mwamsho unapoisha na kurudi nyumbani kwangu mwenyewe, kabati iliyojaa au mwana wa meza aliyejaai si tatizo. Kama mwenye nyumba, nina uhuru kamili kutoa nguo katika kabati au mwana wa meza ili nipate nafasi. Katika hapa mahali, kwa kweli ninajifanya niwe na starehe.

Kwa hivyo, Paulo anaomba kwamba Waefeso waliompokea Kristo mioyoni mwao wataingia ndani zaidi—kwamba watamruhusu akae ndani na ajisikie starehe kabisa mioyoni mwao kupitia kwa imani. Wakati mmoja mtu fulani alisema kwamba katika maisha ya Wakristo wengi, “Kristo ni mkazi, lakini bado si raisi.” Kwa maneno mengine—je, Kristo ni mgeni, au yeye ndiye mwenye nyumba?

Hivyo basi, Wakristo wanapaswa kuingia katika kiwango cha kina zaidi cha maisha ya Kikristo ambamo wanapewa uwezo na Roho (3:16) na kujazwa utimilifu wa Mungu (3:19)—wanapaswa kumpa Kristo umiliki kamilifu wa mioyo yao na maisha yao. Je, kwa uaminifu kabisa unaweza kumwambia Yesu, “Starehe moyoni mwangu”?

---

68. Willard Taylor, *Beacon Bible Expositions Vol. 8, Galatians and Ephesians* (Kansas City, MO: Beacon Hill Press of Kansas City, 1981), 165.

# Kutoa Kabati ya Ukumbini

*Ili Kristo aweze kukaa mioyoni mwenu kupitia kwa imani.*
*Waefeso 3:17a*

Mmoja wapo wa maprofesa wanaomcha Mungu zaidi ambao nimekaa chini yao ni Robert Boyd Munger. Yeye ni maarufu kwa sababu nyingi, lakini anajulikana sana zaidi kwa maelezo yake ya wazi ya maisha ya Kikristo katika kijitabu chake *My Heart—Christ's Home*.

Katika *My Heart—Christ's Home*, mwanamume anamkaribisha Kristo moyoni mwake, kisha anamchukua Kristo katika safari ya vyumba vya moyo wake. Maktaba inawakilisha maisha ya fikira; chumba cha kulia, hamu na tamaa; sebule, maisha ya ibada, waasha, vipawa na vipaji; programu ya michezo iitwayo rec, maisha ya kijamii. Mtu anatoa kila eneo la maisha yake kwa Kristo. Hatimaye kuna kabati ya ukumbini, inayofungwa kwa ufunguo, yenye vitu vilivyokufa na vinavyooza. Hatimaye, mtu anatoa hata hiyo kwa Kristo ili aweze kutakaswa na kumilikiwa. Kisha, anatia sahihi ya mali yote na kumpa Kristo kama mmilkaji kamili, si mgeni tu. Inapitisha ujumbe wa nguvu.

Siku moja baada ya kipindi, Dkt. Munger alinialika kwa ajili ya mlo wa mchana. Wakati wa mlo huo, Dkt. Munger kwa upendo aliniuliza: "Unawezaje kusema utakaso ni upeo wa tatizo wa kitambo kidogo, huku wainjilisti wengine wanajua ni mchakato?"

Nikajibu, "Dkt. Munger, je, unakumbuka wakati mtu anapomruhusu Kristo achukue kabati ya ukumbini ya moyo wake?"

Akasema, "Ndio."

Nikaendelea, "Je, hilo hufanyika tu kwa kitambo kidogo, au ni mchakato?"

Akasema kwa mkazo, "Oo, hilo hufanyika kwa kitambo kidogo!"

"Dkt. Munger, hilo ndilo tunalozungumzia—unafanyika kwa kitambo kidogo. Si hilo tu pekee, nimehubiri hadithi yako nchini kote na tumeona mamia ya watu wakijitokeza kwa kitambo kidogo, wakipiga magoti, wakiomba, na kutoa kabati yao ya ukumbini kwa Kristo."

Mara moja, machozi yanatiririka kutoka machoni mwa Dkt. Munger—kwa nguvu sana hata nikafikiri yangenipiga. Wakati huo, sote tulijua kwamba wakati tulipolizungumzia kwa upendo, sote tuliamini jambo lilo hilo moja—

kutoa vyote na kutakaswa hufanyika kwa kitambo kidogo, na mchakato kabla na baadaye.

Baada ya mlo wa mchana, nilirudi na nikasoma hadithi ya kabati ya ukumbini tena. "[Kristo] nikaenda hati mlangoni, nikaifungua, nikaingia, nikatoa vitu vinavyovunda ambavyo vilikuwa vinaoza humo, na nikavitupa. Kisha akaisafisha hiyo kabati, akaipaka rangi, na akaitengeneza kila kitu kwa kitambo kidogo."[69]

Je, ni wakati wako kutoa kabati yote ya moyo wako kwa Kristo ili aisafishe na kuimiliki kikamilifu? Linaweza kufanyika sasa hivi—inategemea chaguo lako.

**JUNI 3** **154**

# Zaidi ya Yote Tuyaombayo au Tuyawazayo

*Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu*
*mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo,*
*kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu . . .*
*Waefeso 3:20*

Wakati mmoja, mchungaji wa kanisa la nyumbani alinipa orodha ya washiriki ambao kila mmoja wao alikuwa amebobea katika eneo fulani. Kila msitari ulianza na "si kila mtu."

Si kila mtu anaweza kuoka keki ya kahawa kama Kathy.

Si kila mtu anaweza kutatua mambo kama Ed.

Si kila mtu anaweza kuandaa milo ya jioni kama Stacy na Shirley.

Si kila mtu anaweza kuimba na kucheza timu yetu ya kuongoza sifa.

Si kila mtu anaweza kuvua samaki kama Ken.

Si kila mtu anaweza kufundisha watoto kama Susan.

Si kila mtu anaweza kusalimia watu kama Kevin.

Si kila mtu anaweza kutembelea watu kama John na Lester.

Lakini siku ya Pentekoste, Maandiko yanasema juu ya wafuasi wa Yesu 120, "Wote wakajazwa Roho Mtakatifu" (Matendo 2:4). Si kila mtu anaweza . . . lakini *wote* wakajazwa Roho Mtakatifu.

---

69. Robert Boyd Munger, *My Heart—Christ's Home* (Downers Grove, IL: InterVarsity Press, 1986), 25–26.

Je, unatambua kwamba kila mtu aliyekuja kwa Kristo na amezaliwa kwa Roho anaweza kwenda ndani zaidi na ajazwe Roho? Awali, katika ombi letu la Waefeso 3:14–21, kifungu cha 19 kinatafsiriwa, "mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu" (SUV).

Wakati mmoja, baada ya kuwahimiza Wakristo wakazani na "wajazwe Roho," kijana mmoja aliyekuwa ni kama amekasitika aliniuliza. Alipiga kelele, "Unamaanisha nini, 'kujazwa na Royo? Je, unafikiri Roho Mtakatifu amegawanyika? Je, unapata nusu ya Roho Mtakatifu unapookoka na Roho Mtakatifu kamili wakati unapotakaswa?"

Nikajibu, "La, sidhani kama Roho Mtakatifu amegawanyika. Kuanzia wakati unapookoka, Roho anataka kummiliki nyingi nyote. Lakini ilimradi kuna sehemu ya moyo wako ambayo unaizuia isiwe katika udhibiti wake kamili, huwezi kujazwa. Tatizo si tatizo la Roho—ni tatizo lako."

Fikiri kuhusu yote ambayo Paulo amewaombea Wakristo Waefeso na wewe:

- Ili *mpate kufanywa imara kwa nguvu* kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani (3:16)
- Ili *Kristo akae* na astarehe *mioyoni* mwenu kwa imani (3:17)
- Ili *ili mpate kufahamu jinsi* upendo wa Kristo ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina (3:18)
- Ili *mpate kutimilika* kwa utimilifu wote wa Mungu (3:19, SUV)

Hivi vitenzi vyote vinaonyesha kile ambacho Mungu atafanya hivi punde.

Mjibizo wako unaweza kuwa kitu kama, "Hayo ni mengi kupita kiasi—siwezi kufika mahali hapo katika maisha yangu ya kiroho." Hata hivyo, Neno linatwambia, "Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu" (3:20). Anaweza kufanya hivyo—na hata zaidi ya yale uyaombayo au unayoyawaza. Utamwamini lini?

**JUNI 4** **155**

# Nitakuongoza

*Ninatakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea:*
*Nitakushauri, jicho langu likikutazama.*
*Zaburi 32:8, SUV*

Nikiwa na hofu kiasi fulani, nilikaa katika ofisi ya mkuu wa kitivo kujadili kazi yangu mpya ya kufundisha. Raisi William Greathouse alikuwa amenipigia simu miezi kadhaa awali na akanialika niende katika seminari nikafundishe uinjilisti. Nilikuwa nimefurahi katika kazi yangu kama mwinjilisti wa wakati wote, nikihubiri katika kanisa tofauti kila wiki. Lakini, hiyo simu ilipopigwa, nilihisi mara moja kwamba haya yalikuwa mapenzi ya Mungu kwa ajili yangu.

Sasa nilikabiliana na uhalisia na Mkuu wa Kitivo Mendell Taylor. Nikasema, "Sijawahi kupanga kufundisha. Sikuwahi kamwe kusoma hata darasa moja la elimu—lakini nafikiri hivi ndivyo Mungu anavyotaka nifanye."

Huyo mkuu wa kitivo akanisukumia boksi iliyokuwa na vifungu vya Maandiko ndani yake. Akasema, "Chukua moja." Elewa, nilikuwa na nimepewa vilasi vya muda wa mihula miwili na sikuwa na mhadhara hata mmoja uliokuwa tayari. Nikatoa kifungu kimoja kwa kubahatisha. Kilisema, "Ninatakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea: Nitakushauri, jicho langu likikutazama."

Na je, Mungu aliwahi kunielekeza. Usiku wa manane katika meza yangu, na nikiwa nina uongozi wa kiungu uliokuwa wazi, niliunda mihadhara yangu. Na je, wanafunzi waliwahi kutoa mwitikio! Miaka thelathini ya kufundisha, iliyojaa neema, na furaha ilifuata.

Kile kilichotokea katika ofisi ya mkuu wa kitivo siku ile kilifunua haki ya kimsingi ya maisha yaliyojazwa Roho—kuongozwa na Roho wa Mungu. Kama Warumi 8:14 inasema, "Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu."

Katika kumwelekeza Filipo kwa yule Mwiethopia, "Roho akamwambia Filipo, 'Sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo'" (Matendo 8:29). Filipo alikuwa ameelezwa tayari katika Matendo 6:3: "Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili."

Je, umejazwa na Roho? Je, unaongozwa na Roho? Je, unajua inamaanisha nini Mungu anaposema, "Nitakuongoza"?

# Msaidizi

*Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine,*
*ili akae nanyi hata mileler—ndiye Roho wa kweli.*
*Yohana 14:16–17*

Wanafamilia ishirini walikuwa wamekusanyika kwa ajili ya mkutano wa mwaka kule Treasure Island, Florida. Wengine walikuwa wanaendesha magari, na wengine walisafiri kwa ndege. Familia ya Chad—watu wazima wawili na watoto wanne—walikuja kwa ndege. Mwangangu alinipigia simu akaniuliza kama ningemwazima Chad gari yetu ili waweze kufanya ununuzi wa vyakula. Mwanangu, aliyekuwa na uhusiano wa karibu na mimi kuliko Chad, alikuwa ananisihi kwa niaba ya Chad na familia yake—alikuwa anawatetea.

Yesu angewaacha wanafunzi wake muda si mrefu, kwa hivyo akamwomba Baba yake awape Roho Mtakatifu, ambaye alimweleza kwa wanafunzi kama "mtetezi mwingine wa kuwasaidia." Kama Yesu alivyomsihi Baba kwa niaba ya wanafunzi, Roho Mtakatifu angechukua nafasi ya Yesu na kuwasaidia kama Yesu alivyofanya.

Roho Mtakatifu hangeweza kukubaliwa na ulimwengu (watu wanaoishi bila Mungu), lakini anakubaliwa na wale waliomfuata Yesu peke yao. Kwa kweli, huyu Roho angeishi ndani yao.

Zaidi ya hayo, Yesu alisema, "Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia" (Yohana 14:26). Baadaye alitoa utondoti zaidi: "Lakini ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba—, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba—yeye atanishuhudia" (15:26).

Neno "msaidizi" linatumiwa tena katika 1 Yohana 2:1: "Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki." Sasa Kristo ni Msaidizi wetu. Wakristo wanapaswa watarajie kuishi katika ushindi juu ya dhambi—lakini tukifanya dhambi, tunaweza kupeleka jambo hilo kwa Kristo mara moja, ambaye atatuombea mbele yra Baba. Tunaweza kuwa na hakika kwamba "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohana 1:9).

Hebu fikiri—Roho Mtakatifu ni Msaidizi wako. Yesu Kristo ni Msaidizi wako.

JUNI 6 **157**

# Unaweza Kujua

*Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu.*
*1 Yohana 5:13*

Larry, mkazi mwenza katika chumba kule chuo, alikuwa amekuwa akitafuta. Ijapokuwa alilelewa kanisani, akawa na maadili mazuri, na akajali kuhusu mambo ya kiroho, hakuwa na *hakika* yeye alikuwa Mkristo. Baada ya kuhudhuria mafunzo ya Biblia ya kundi kule chuo, alitambua kwamba watu wengi katika hilo kundi walikuwa na hakika na wokovu wao.

Akipanga kuwa mwanasayansi mtafiti, Larry aliuendea uhusiano wake na Mungu kiurazini. Katika chumba chake cha kusoma kule maktaba, alizima taa ili mtu yeyote mwingine asimwone, na akapiga magoti. Akasoma ahadi kama, "Wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe" (Yohana 6:37, SUV), na "Mimi hapa! Nasimama mlangoni nabisha. Mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami" (Ufunuo 3:20).

Larry akaomba, "Kama wewe kweli uko vile unavyodai kuwa katika Injili, ninakupa ruhusa ya kuja maishani mwangu na kujifunua kwangu. Na siweki mipaka yoyote ya wakati."

Miezi sita baadaye, Larry alisema, "Nilikuwa na ushahidi wote niliohitaji. Maombi yalikuwa yanakuwa mazunguzo yaliyo hai na Mungu, na Biblia ikawa kitabu kinachobadilisha maisha cha kufurahisha, kama ambaye Mungu alikuwa ananena nami ana kwa ana. Mtazamo wangu wote na hulka yangu yote vilikuwa vinabadilishwa." Nikiwa na Neno la Mungu, maisha yaliyobadilika, na ushahidi wa Kristo ukiwa unafanya kazi maishani mwake, Larry alipata *kujua* kwamba alikuwa Mkristo kweli. Leo, yeye ni mhudumu wa injili na mtu mwenye nguvu za Roho zisizo na kifani.

Mungu anataka ujue kwamba wewe ni Mkristo. Ni dhamira inayotawala katika 1 Yohana, kama vile katika 5:13: "Nimewaandikia ninyi mambo hayo,

ili *mjue* ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu."

Unaweza *kujua* wewe ni Mkristo kwa:

- Ushahidi wa Neno: "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohana 1:9). Kumbuka kwamba Mungu ni mwaminifu kusamehe na kusafisha.
- Ushahidi wa kupenda: "Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote" (1 Yohana 1:7). Wakati kujitoa kwangu binafsi kwa hiari yangu kunaweza kusema, "Ninatembea katika nuru yote inayojulikana ambayo Mungu amenipa," ninaweza kuwa na hakika kwamba mimi ni Mkristo.
- Ushahidi wa mwenendo—"Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua" (Mathayo 7:20). Maisha yako yatauonyesha.
- Ushahidi wa Roho—"Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" (Warumi 8:16). Roho hutoa hakikisho la ndani, amani, na kumjua Mungu ili wewe *ujue* wewe ni mtoto wa Mungu.

Wiki kumi na nne zilizopita hadi naandika hili, Rob alimkubali Yesu Kristo. Siku chache zilizopita, nilimwuliza Rob jinsi alivyojua kwa hakika kwamba yeye ni Mkristo. Maneno yalitiririka kutoka kwake:

> Nilitoa maisha yangu kwa Kristo. Nilijua hili moyoni mwangu. Nina amani na uhakika. Ninaenenda na kunena na Yesu. Mwenendo wangu uko tofauti. Sijawahi kuwa na shaka kamwe tangu Februari 19.

Ukweli wa kushangaza na wa ajabu ni kwamba unaweza kujua kwamba wewe ni Mkristo, kwamba umeokolewa, na kwamba huna tatizo na Mungu. Ni bora sana wakati mashahidi wote wanne wakiungana pamoja katika maisha. Inamfurahisha Mungu kwako wewe kuwa na hili hakikisho.[70]

70. Awali kilichapishwa katika *Standard*, Juni 5, 2016 (Kansas City, MO: WordAction Publishing). Imetumiwa kwa idhini.

# Hakikisho la Utakaso Pia

*Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya.*
*1 Wathesalonike 5:24*

Katika miaka mia moja iliyopita, mmoja wapo wa mtu aliyekuwa na uwezo mkubwa zaidi katika Kanisa la Kimethodisti alikuwa E. Stanley Jones. Kwa mwaka mmoja baada ya yeye kuokolewa na Kristo, aliishi katika furaha kuu. Kisha, aligundua kwamba hasira kali, hali mbaya, na migongano ya ndani ilianza kuinuka kutoka katika misingi ya nafsi yake. Alimtafuta Mungu kwa ajili ya uhusiano wa ndani zaidi.

Bwana akamwuliza, "Je, utanipa mambo yako yote?"

Jones akajibu, "Ndiyo, Bwana, kwa hakika nitafanya hivyo. Nitakupa mambo yangu yote—yote ninayojua na yote nisiyojua."

Bwana akajibu, "Basi chukua yangu yote—chukua Roho Mtakatifu."

Jones aliona hili kama "yangu yote kwa yake yote." Akajibu kwa hamu, "Nitamchukua Roho Mtakatifu." Akainuka kutoka kwa maombi bila ushahidi wa hii ahadi isipokuwa neno la Mungu. Mashaka yalianza kukaribia, lakini akayasukuma nyuma na maombi.

Alipokuwa anatembea katika hicho chumba, Roho wa Mungu alitoa ushahidi wa moyo wake. Baadaye, alitoa ushuhuda, "ghafla nikajazwa—nikajazwa na Roho Mtakatifu. Wimbi baada ya wimbi yalionekana yakinipitia kama moto wa kusafisha . . . Nilijua huu haukuwa mhemko uliokuwa unapita; Roho Mtakatifu alikuwa amekuja kukaa na mimi milele."[71]

John Wesley alisema, "Kwa hivyo, hakuna mtu ayepaswa kuamini kuwa kazi imefanywa mpaka kuwe na ushuhuda wa ziada wa Roho akitoa ushahidi wa Roho akishuhudia utakaso wake wote wazi wazi kabisa kama kuhesabiwa haki kwake."[72] Wakati Petro alipokuwa anathibitisha ukweli kwamba Mungu aliwakubali watu wa mataifa pia waliomcha yeye, Petro alijenga juu ya kile ambacho Roho alikuwa amefanya kwa wafuasi wa kwanza wa Yesu: "Na Mungu, ajuaye mioyo ya watu, akawashuhudia, akiwapa Roho Mtakatifu

---

71. E. Stanley Jones, *A Song of Ascents* (Nashville: Abingdon Press, 1968), 52–53.

72. Kama ilivyonukuliwa katika H. Orton Wiley, *Christian Theology II* (Kansas City, MO: Beacon Hill Press, 1953), 514.

vile vile kama alivyotupa sisi. Wala hakufanya tofauti kati yetu sisi na wao, akiwasafisha mioyo yao kwa imani" (Matendo 15:8–9). Baadaye, Yohana alitangaza, "Katika hili tunafahamu ya kuwa tunakaa ndani yake, naye ndani yetu: Kwa kuwa ametushirikisha Roho wake" (1 Yohana 4:13).

Gary alikuwa msimamizi wa duka la kwao la vyakula. Alikuwa amemjua Kristo kwa mwaka mmoja, na mchungaji wake alifurahi juu ya ukuaji wake wa Kikristo. Wakati wa ibada za kanisa za kufanywa upya kiroho, alisikia mahubiri juu ya utakaso mzima kutoka 1 Wathesalonike 5:23–24. Baadaye, alitoka mbele apate kuomba.

Yule mhubiri aliuliza, "Unataka Mungu akufanyie nini?"

Gary akajbu, "Ninamtaka anitakase."

Wakasoma 1 Wathesalonike 5:23–24: "Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa . . . Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya." Yule mhubiri akamhimiza Gary aachilie maisha yake yote yaliyosamehewa kwa Mungu na amwombe Mungu amsafishe dhidi ya kujipenda mwenyewe kokote kulikokuwa kumesalia. Alimwambia afikie watu kwa imani na kuamini Mungu atafanya. Gary akauliza maana ya imani ni nini.

Huyo mhubiri akamwuliza, "Gary, kwa nini umekuja hapa chini kuomba?"

Gary akajibu, "Mungu ameniita."

"Kwa nini Mungu amekuita?"

"Ili anitakase."

"Mm, Biblia inasema Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya. Unafikiri atafanya lini?"

"Sasa hivi!" Gary akasema kwa mshangao.

Baada ya sekunde thelathini za maombi zaidi, Gary alikuwa anatabasamu. Akasema, "Oo, *ninajua*." Hii inaogofya."

Kama E. Stanley Jones, John Wesley, na Gary, unaweza *kujua* kwamba Mungu anakutakasa; unaweza *kujua* kwamba Roho anakujaza sasa. Nijaze sasa![73]

73. Awali kilichapishwa katika *Standard*, June 5, 2016 (Kansas City, MO: WordAction Publishing). Imetumiwa kwa idhini.

# Mungu Alimtuma Huyu Musa

*Musa huyo waliyemkataa, wakisema, "Ni nani aliyekuweka kuwa mkuu na mwamuzi?" Ndiye aliyetumwa na Mungu kuwa mkuu na mkombozi, kwa mkono wa yule malaika aliyemtokea katika kile kijiti.*
*Matendo 7:35*

Ni kejeli, sivyo, jinsi watu wanavyowakataa wawakilishi wateule wa Mungu? Waisraeli walimkataa Musa; manabii wengi walipata kwamba hakuna mtu aliyewasikiliza; watu pia walimkataa Stefano, wakati alipokuwa anawakumbusha kwamba Yesu, waliyemsulubisha, alitumwa na Mungu.

John Wesley alijua kukatazwa kusikiwa kilikuwa kitu gani. Wakati mmoja ilikuwa kupigwa mawe; wakati mwingine, maadui zake walijaribu kumpiga na rungu. Mara nyingi, alipokea ilani kutoka kwa mchungaji au mashemasi kuhusu usomaji wa kanisa, "Bwana, hupaswi kuhubiri tena hapa mahali." Lakini wale waliomsikia waliokoka. Na sasa, historia inatwambia kwamba uamsho uliofuata mahubiri ya Wesley yaliokoa Uingereza kutoka kwa mapinduzi mabaya.

Hata katika makabiliano na upinzani ya fujo, mtu ambaye ametumwa kutoka kwa Mungu kweli hupata njia ya kuwasilisha ujumbe. Musa aliwaongoza watu wake kutoka katika utumwani; Stefano alinena maneno yake ya mwisho kuwa ushahidi wa kushangaza; Wesley alihubiri hata ingawa kulikuwa na uhasama dhidi yake.

Usiwe na hatia ya kupuuza ujumbe wa Mungu kwa kuwapuuza wale anaowatuma wanene kutoka juu ya jukwaa.[74]

74. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* July–Agosti–Septemba 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 18. Imetumiwa kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa Reflecting God.)

# Kwa Nini Bwana Anakawia

*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake,*
*kama wengine wanavyokudhani kukawia. Bali huvumilia kwenu,*
*maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.*
*2 Petro 3:9*

*Imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu*
*na utauwa, mkitazamia*
*hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza.*
*2 Petro 3:11b–12a*

Kuna angalau sababu mbili kwa nini Bwana amekawia kuja mara ya pili:

1. Apate kuruhusu wakati kwa ajili ya watu wengi zaidi watubu, kujumuisha na wale utakaowashuhudia wewe.
2. Apate kutupa nafasi "kuwa watu wenye mwenendo mtakatifu na utauwa."

Ninafurahi sana kuwa Yesu alikawia kuja kidogo zaidi.

Naona angekuwa amekuja 1954—lakini ninafurahi sana alingojea kwa sababu nilimpokea kama Mwokozi wangu mwaka wa 1955, kama mwanafunzi wa chuo mwenye umri wa miaka ishirini.

Ninafurahi alingojea kwa sababu, mwaka uliofuata, nikiwa na miaka arobaini na miwili mamangu alimkubali Kristo.

Ninafurahi alingojea kwa sababu, miaka minne baadaye, babangu alimkubali Kristo akiwa na miaka hamsini na tisa.

Ninafurahi alingojea kwa sababu, babu yangu alimpokea Kristo akiwa na miaka themanini na minane.

Ninafurahi alingojea kwa sababu, nyanya yangu alimpokea Kristo akiwa na miaka tisini na miwili.

Ninafurahi alingojea kwa sababu, mwanangu alimkubali Kristo akiwa na miaka kumi na saba.

Ninafurahi alingojea kwa sababu, binti yangu alimrudia Bwana akiwa na miaka ishirini na saba.

Ninafurahi alingojea kwa sababu, binti yangu aliyefuata alimrudia Bwana akiwa na miaka thelathini.

Si ajabu Petro alisema, "Uvumilivu wa Bwana wetu kuwa ni wokovu" (2 Petro 3:15). Hakika ni kweli kwa familia yangu.

Lakini kuna kipengele cha pili: "Imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa, mkitazamia hata ije ile siku ya Mungu." Petro alithibitisha suala hili awali zaidi alipoandika, "Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu" (1 Petro 1:16). Lakini moyo wangu unawezaje kufanywa mtakatifu—unaopenda sana kuficha, usiojua kabisa kuhusu ubinafsi wa ndani unaovizia? Kwa mara nyingine, Petro ananena: "Na Mungu, *ajuaye mioyo ya watu*, akawashuhudia, akiwapa Roho Mtakatifu vile vile kama alivyotupa sisi. Wala hakufanya tofauti kati yetu sisi na wao, *akiwasafisha mioyo yao kwa imani*" (Matendo 15:8–9).

Roho aliingia katika kilindi cha moyo wangu, na akausafisha kwa imani. Sasa, kila siku, "Ninafanya bidii ili nionekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake" (2 Petro 3:14) na kukua katika neema (3:18). Asante Bwana kwa kungojea.

**JUNI 10** **161**

# Kwa Kila Njia . . . Okoa Wengine

*Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao.*
*2 Mambo ya Nyakati 7:14*

Mwaka 1949, katika jumuiya inayoitwa Barvas iyoko katika visiwa vya Hebrides katika pwani ya Uskochi, washiriki sita Wapresbiteri na mchungaji wao walikutana. Waliomba kwa ajili ya uamsho wa kiroho wa miji jirani, ambako ilikuwa ni nadra sana vijana kwenda kanisani. Ahadi yao ilikuwa 2 Mambo ya Nyakati 7:14.

Kwa miezi kadhaa, siku tatu usiku kwa wiki kwa masaa sita kila usiku, wale watu walimtafuta Mungu bila matokeo ya wazi. Hatimaye, usiku mmoja, mwanamume mmoja katika lile kundi aliwakumbusha kwamba ni wanaume wenye mikono safi na mioyo sagi peke yao ndio wanaoweza kupokea baraka kutoka kwa Bwana (Zaburi 24). Wakapiga magoti tena na wakaungama hitaji lao wenyewe—na kisha, Mungu na uamsho ukaingia.

Wiki mbili baadaye, katika usiku wa kwanza ibada zao za uamsho, kulionekana kama hakuna matokeo—lakini Wakristo wakashikilia katika imani. Ibada ya usiku iliyofuata ilikatizwa na askari polisi. Akamwomba yule mhubiri aende kituo cha polisi kuwahudumia umati wa watu wanaolia huko. Usiku huo, karibu watu mia sita walimtafuta Mungu karibu na kile kituo cha polisi—watu ambao roho zao zilikuwa zimesadikishwa wakiwa njiani kwenda katika ibada. Kwa wiki tano, mwamsho uliingia katika parokia hiyo na ibada nne usiku mmoja. Kisha ukaenea hadi miji mingine.

Vijana kumi na wanne waliokuwa wakinywa katika kile kilabu cha pombe waliokoka. Katika kijiji kimoja, karibu kila kijana kati ya miaka kumi na miwili na ishirini walikuwa wamejitoa kwa Kristo katika saa arobaini na nne.

Kufikia mwaka 1952, matokeo ya uamsho yaliweza kuonekana katika ibada za familia katika kila nyumba. Kati ya wale mamia waliomgeukia Kristo katika wimbi la kwanza la huyo Roho, ni wanne peke yao walioacha kuhudhuria mikutano ya maombi. Zaidi ya nyimbo themanini zilitungwa na wale waliookoka. Katika mahali pamoja, mwamsho huo uliongeza uhudhuriaji kutoka 27 Jumapili asubuhi hadi 875 katika mkutano wa maombi. Haya yote kwa sababu wengine wanaamini: "Ikiwa watu wangu . . ."[75]

**JUNI 11** **162**

# Kungojea

*Mungu amesema, "Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa."*
*Waebrania 13:5*

*Na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*
*Mathayo 28:20*

*Nilimngojea Bwana kwa* SUBIRA*; akaniinamia na kusikia kilio changu.*
*Zaburi 40:1*

75. Awali kilichapishwa katika *Herald of Holiness* (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House, Septemba 30, 1970), 20. Imetumiwa kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Holiness Today*.)

Daktari mpasuaji alikuwa amechelewa. Yule mgonjwa alikuwa tayari lakini bado alikuwa wa tatu katika foleni ya upasuaji. Kile alichoweza kufanya ni kungojea.

Binti yake akamtumia ujumbe mzuri wa maneno ya kumtuliza: "Samahani sana kwa kukawia. Yesu anangojea pamoja na ninyi."

Mara nyingi sana, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba angekuwa pamoja nao, mara nyingi kwa kupitia uwepo wa Roho Mtakatifu. Kulingana na kusulibishwa kwake kulikokuwa kunakuja, aliwahakikishia kwamba angekuwa pamoja nao katika hali zao zote. Alikuwa anangojea twende pamoja leo kwa mkutano muhimu ulioombewa wa mlo wa mchana na mtu mkuu.

Sisi pia tunaambiwa tungojee—tunapaswa kumngojea Bwana kwa subira. Wakati tunapongojea mbele za Bwana, hiyo inampa nafasi ya kutafuta sehemu za ndani zaidi za mioyo yetu. Na huku tukiwa tunangojea, tunaweza kusikia sauti yake. E. Stanley Jones aliwahimiza Wakristo wahakikishe wanaendeleza "kituo cha kusikiliza" na Bwana.

Kungojea mbele za Bwana ni muhimu hasa kwa Mkristo anayetafuta mjazo wa Roho unaotakasa. Watu wengi hunena kuhusu nyongeza ya wakati wa kumtafuta Bwana kuhusu hili kabla hawajapokea jibu la Mungu. Vivyo hivyo, Yesu aliwaambia wanafunzi wa wakati wake, "Msitoke Yerusalemu, bali mwingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu. Ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache" (Matendo 1:4–5).

Yesu anangojea pamoja na ninyi; Mungu anawangojea ninyi. Mnamgojea Bwana.

JUNI 12 **163**

# Umbali wa Kunong'onezana

*Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote. Kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.*
*Yohana 16:13*

*Na baada ya tetemeko la nchi kukawa na moto; lakini BWANA hakuwamo katika moto ule. Na baada ya moto sauti ndogo, ya utulivu. Ikawa, Eliya alipoisikia, alijifunika uso wake katika mavazi yake,*

*akatoka, akasimama mlangoni mwa pango. Na tazama, sauti ikamjia, kusema, "Unafanya nini hapa, Eliya?"*
*1 Wafalme 19:12–13*

Katika miaka yetu ya uzeeni, mke wangu mpenzi, Nancy, amelazimika kukabiliana na changamoto ya kudhoofika kwa kumbukumbu. Tunajaribu kufanya kazi pamoja ili tuweze kusimamia maisha yetu ya kila siku.

Tuliamua ni vizuri zaidi kwa sote wawili kuangizia bangili za MedicAlert, ambazo zina orodha ya namba za simu unazoweza kupiga saa ishirini na nne kupiga kama mtu yeyote atagundua kuwa tuna msongo. Baada ya kuingia katika tovuti mara kadhaa na kujadili mipango yetu kwa wiki kumi, siku ilifika ambayo ninge ningepiga simu na kuagiza. Lakini kwanza ilinibidi nijaze maswali mengi ya kidadisi na nipige simu kule ofisini Kalifonia. Nilihisi mfadhaiko juu ya kupiga hii simu, lakini zaidi na zaidi, nimejifunza kuombea kila jambo—hata mambo ya kila siku. Kwa hivyo niliomba kwamba Bwana anipe mshauri sahihi ninapopiga simu. Katika mazungumzo chanya ya saa moja, yaliyokuwa na huruma, mshauri mzuri sana alipata taarifa alizozitaka kutoka kwangu na nikajibu maswali yangu. Kabla hata wiki kuisha, tulikuwa na bangili zetu zilizonakishiwa.

Kila majira ya kuchipua, Nancy hupamba ua na bustani yetu na maua yanayoishi ambayo yeye hununua na kupanda. Baada ya kufanya hivyo kisawasawa majira haya ya kuchipua, alihisi msukumo wa kununua maua zaidi kila alipoona mauzo. Baada ya siku kadhaa za ununuzi wa aina hiyo, alikuja nyumbani kunionyesha ua lingine zaidi. Nilihisi kujaribika kueleza kuhusu maua mengi kupita kiasi, kazi nyingi zaidi, na makadirio ya maua. Badala yake nikasita kidogo nikamwuliza Mungu anionyeshe la kusema. Kisha nikasikia mnong'ono: "Furahi pamoja naye juu ya hilo ua lake. Mwambie jinsi lilivyo zuri sana. Usijali kuhusu ua moja zaidi. Limemfanya awe na furaha. Na zaidi ya hilo, halikugharimu pesa nyingi sana."

Kwa hivyo tukafurahi pamoja. Unaona, nilisoma yafuatayo katika kitabu cha ibada binafsi cha Samuel Logan Brengle, *Take Time to Be Holy*: "Sasa kama unataka kuweka hizo baraka [utakaso wote], ni lazima kila mara uinue moyo wako kwa Mungu ili upate nuru, si katika matatizo ya maisha peke yake, lakini katika kila kipengele chake. Kwa kujizoeza, unaweza kuingia katika tabia hiyo hivi kwamba itakuwa kama jambo la kiasili kwako kama kupumua. Kuwa katika umbali wa kunong'onezana na Mungu siku zote."[76]

---

76. Samuel Logan Brengle, *Take Time to Be Holy*, ed. Bob Hostetler (Carol Stream, IL: Tyndale Momentum, 2013), 200.

Hivyo ndivyo ninavyotaka kufanya: "Kuwa katika umbali wa kunong'onezana na Mungu siku zote."

JUNI 13 164

# Jazwa—Endelea Kujazwa

*Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi. Bali mjazwe Roho.*
*Waefeso 5:18*

*Afterglow: The Excitement of Being Filled with the Spirit* ni kichwa cha kitabu kilichojipambanua cha Sherwood Wirt, aliyekuwa mhariri wa gazeti la *Decision* la shirika la Billy Graham. Ni hadithi ya uzoefu wake mwenyewe wa kujazwa Roho, na wa wengine ambao ameshirikiana nao, au aliowahudumia.

Himizo la Paulo kwa Waefeso katika in 5:18, "Mjazwe Roho," liko katika njeo ya sasa. Wazo ni *kuendelea* kujazwa Roho. Kwa hakika, huwezi kuendelea kujazwa bila kuwa na wakati ambapo unajazwa mara ya kwanza. Lakini wakati unapojazwa mara ya kwanza, ni muhimu sana kwamba uendelee kujazwa. Sherwood Wirt yuko na uhakika kuhusu wakati aliojazwa:

> Nilipokuwa ninasoma Maandiko, wakati wa kuokoka kwangu, Roho wake alikuwa amenipa uwezo wa kufikia zana zote za uwezo wa Mungu. Sikuwa tu ninazitumia!
>
> Na je ninajua wakati *nilipojazwa* Roho Mtakatifu? Ninajua kwa hakika. Ilifanyika wakati nilipomwomba Bwana aniondoe njiani, anisulibishe msalabani, na anijaze kwa upendo wake.
>
> "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu" (Wagalatia 2:20).[77]

Sherwood Wirt alitambua ukweli wa Matendo 1:8: "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu." Wirt pia alitoa ushuhuda: "Kijana mmoja aliyekuja katika nuru alimwomba Mungu amfanye shahidi bora zaidi wa Kristo kwa watu asiowajua. Siku iliyofuata alisimama apate kifungua kinywa katika mkahawa mmoja. Mwanamume aliyeketi kando yake katika kaunta akasema, 'Unaonekana

77. Sherwood Wirt, *Afterglow: The Excitement of Being Filled with the Holy Spirit* (Grand Rapids: Zondervan, 1976), 39.

kama ambaye usiku uliopita ulikuwa nje na ukawa na wakati mzuri sana.' Ulikuwa mlango ulio wazi naye akaingia ndani mara moja."[78]

Wirt aliathiriwa na uwezo wa upendo ambao Roho aliuweka ndani yake: "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote. Tukipendana, Mungu hukaa ndani yetu, na pendo lake limekamilika ndani yetu. Katika hili tunafahamu ya kuwa tunakaa ndani yake, naye ndani yetu: kwa kuwa ametushirikisha Roho wake" (1 Yohana 4:12–13). Wirt anasema, "Kama hilo ni kweli, basi Roho Mtakatifu ni upendo. Uwezo wa Roho ni uwezo wa upendo. Pumzi ya Roho ni pumzi ya upendo. Moto wa Roho ni moto wa upendo. Upako wa Roho ni upako wa upendo. Ubatizo wa Roho ni ubatizo wa upendo. Ujazo wa Roho ni ujazo wa upendo."[79]

Huu upendo pia ndicho kipengele kikuu katika uongozi wa kichungaji. Tena, Wirt anaandika, "Mhudumu anapopenda kundi lake, anapowapenda watu kweli na kuwasilisha huo upendo hivi kwamba wapate huo ujumbe, anaweza tu kujiandikia tikiti yake mwenyewe. Yaani, uwezekano wa kanisa hilo kuleta matokeo tarajiwa hauna mipaka."[80]

Kuendelea kujazwa na Roho ni muhimu sana. Wirt anasimulia hadithi fupi ifuatayo kuhusu mchungaji mmoja:

> Mchungaji mmoja rafiki yangu aliyekuwa amepata uamsho aliulizwa na mshiriki wa kanisa lake, "Kasisi, kwa nini unasisitiza kuongea wakati wote kuhusu kujazwa na Roho?"
>
> Rafiki yangu alionekana kuwa na makini. "Kwa sababu," alisema, "Ninavuja."[81]

Warumi 5:5 inasema, "Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi." Hili andiko pia lilileta athari kubwa juu ya Wirt. Alilieleza hivi:

> Nilianza kufikiri kuhusu hilo tamko *kumiminwa*. Ilionekana kwangu kwamba maisha yangu yanaweza kuelezwa kama glasi. (Hapo zamani yamkini kingeitwa "chombo.") Niliona kwamba Mungu ana jagi la dhahabu, na anapendekeza kuijaza hiyo glasi kwa maji ya uzima. Anataka aijaze na aendelee kuijaza mpaka ifurike. Anataka ifurike na kujaza glasi nyingine zilizo karibu nayo, na huko ni kushuhudia.
>
> Maji yanapofurika kwenye mdomo, kunena kuhusu Yesu kunakuwa rahisi. Bwana hutayarisha kila kitu; anaweka miadi, anapanga mahojiano, analeta mvuto, analeta matokeo.

78. Wirt, *Afterglow*, 65.
79. Wirt, *Afterglow*, 93.
80. Wirt, *Afterglow*, 95.
81. Wirt, *Afterglow*, 71.

Tatizo lilikuwa, Mungu hakuweza kuijaza glasi yangu. Hapakuwa na tatizo lolote kwenye chanzo; visima vya chemchemi visivyokuwa na mipaka haviishi maji. Tatizo lilikuwa ni mimi. Glasini mwangu mlikuwa na maji tayari, na yalikuwa yamechafuliwa. Masimbi yalikuwa huko chini. Ilikuwa ni lazima ipinduliwe juu chini na maji yake yamwagwe yote.

Yesu alisema katika Yohana 7:38, 39 kwamba maji ya uzima yangebubujika kutoka kwa wale waliomwamini yeye. Alikuwa anazungumza kuhusu Roho Mtakatifu.

Lakini Mungu hawezi kuchanganya maji machafu na maji safi. Hatamwaga kutoka kwenye jagi lake la dhahabu mpaka glasi yetu imwagwe na kuwa tupu. Hatatuma upendo wake katika moyo ambao tayari unajipenda wenyewe, au uwezo wake katika maisha yanayoendeshwa na nguvu za mwanadamu.

Sasa niliona kwa uwazi zaidi kile ambacho Paulo alimaanisha kwa kusema, "Nimesulibiwa pamoja na Kristo."[82]

Unangojewa na maisha ya upendo na mbubujiko ulioje wakati unapojazwa Roho—unapoendelea kujazwa Roho.

JUNI 14 **165**

# Watu Wakaamini

*Na wakaamini. Na waliposikia ya kuwa BWANA amewajilia wana wa Israeli, na ya kuwa ameyaona mateso yao, wakainama vichwa vyao wakasujudu.*
*Kutoka 4:31*

Alikuwa tu mhubiri mchanga, na mfanyakazi mwenzake katika kuhubiri alikuwa mzee kidogo tu. Kwa kweli, walikuwa wameogopa. Ulikuwa uamsho tu wa wikiendi pia—hapakuwa na wakati mwingi. Lakini walitambua kwamba watu walikuwa wanazungumza kuhusu huo uamsho. Na uwezo wa maombi ulikuwa wazi. Vijana walikuwa wameomba na kufunga.

Jumamosi walihubiri wote wawili, na ushindi ulikuja. Jumamosi asubuhi, mhubiri mchanga alihubiri. Alipofikia wakati wa kuwaalika watu

82. Wirt, *Afterglow*, 114–115.

madhababuni, alifikiri, *Sijui hata kuwaalika watu madhababuni*. Lakini kwa kutetemeka, aliwaalika watu madhababuni.

Kabla wimbo wa mwisho haujaisha, mtafutaji wa kwanza alikuja—mtu mkubwa aliyegonga madhabahu kwa nguvu sana hata ikavunjika. Halafu wakaja kutoka kila mahali—katika kila ubeti wa huo wimbo—huo wimbo ulipoimbwa kwa mara ya tatu. Madhabahu zote zilijaa, na nyuma yao, viti vya mbele vilijaa pia. Hiyo asubuhi, talaka sita zilisitishwa kwa neema—wale wenza walimpenda Mungu na wakapendana wenyewe. Wengi waliokoka na dhambi zao zote zikasamehewa—"Na wakaamini."

Musa na Aaroni walikuwa timu ya kuhubiri ya awali zaidi. Hawakuwa vijana, lakini waliogopa. Lakini ngoja kidogo! Mungu aliyewaita alitayarisha watu na njia. Wakaamini—na kukawa na ushindi![83]

JUNI 15 **166**

# Kutoka KuwaMabomu hadi kuwa Upendo

*Na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.*
*Warumi 5:5*

Tarehe 7 Disemba, 1941—"siku ambayo itabaki kuwa siku mbaya," kama alivyoiita Rais Roosevelt kwa umaarufu—Jemadari Mitsuo Fuchida aliongoza ndege 360 za Kijapani kupiga mabomu meli za Marekani kule Pearl Harbor. Tarehe 18 Aprili, 1942, ndege za Marekani zilizojulikana kama Doolittle Raiders ziliondoka kutoka *USS Hornet* kwenda kupiga bomu Japani. Sajini Mkuu Jacob DeShazer aliangusha mabomu yake na, baada ya saa kumi na tatu kuwa hewani, alianguka na mwavuli juu ya China iliyokuwa imeshikwa na Japani. Alishikwa na akateswa gerezani kwa miezi arobaini.

Ijapokuwa alikuwa amelelewa katika nyumba ya Kikristo, DeShazer hakujali, alikuwa baridi, alikuwa na shauku, na mdhaifu katika kiasi na dhamira. Kufikia mahali fulani, mmoja wa walinzi alimpitishia Biblia mikononi mwake. Aliisoma kwa undani na kwa hamu kabisa kwa wiki tatu, kisha akalazimika kuipitisha kwa mfungwa mwingine. Kufahamu kifo cha

83. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Julai–Agosti–Septemba 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 17. Imetumiwa kwa ruhusa (Chapisho hili likawa *Reflecting God*.)

Kristo cha kujitoa sadaka kwa dhambi zake kilimwathiri. Tarehe 8 Juni, 1944, alimwomba Mungu: "Unajua ninatubu dhambi zangu. Hata ingawa niko mbali na nyumbani na ijapokuwa nimo gerezani, ni lazima niwe na msamaha."[84]

Nafsini mwake mliingia furaha ya kiungu—shahidi wa ndani kwamba Mungu, alikuwa amemsamehe, kwa ajili ya Kristo. DeShazer alisema, "Ni furaha kubwa iliyoje kujua kwamba nilikuwa nimeokoka."[85] Njaa haikuweza tena kumtisha, wala ukosefu wa chakula, wala gereza lenye baridi kali sana. Sasa, kama Mkristo, DeShazer alijua ilikuwa ni lazima apende watu wengine—hata maadui zake. Alijua Mungu alitarajia utiifu.

Siku moja, mmoja wa walinzi alimharakisha na akamwingiza katika selo yake na akafunga mlango kwa nguvu juu ya mguu wake uliokuwa pekupeku. Kisha huyo mlinzi akaupiga teke mguu wa DeShazer na njumu zake. Baadaye, akahisi uchungu na chuki dhidi ya yule mlinzi.

DeShazer alijua ilimbidi aingie katika kiwango cha ndani zaidi cha maisha yake ya Kikristo—kwa hivyo akaamua amfanye huyo mlinzi awe rafiki yake. Alihisi kwamba asili yake ilikuwa imebadilika. Alitambua kwamba, kama Mkristo, angeweza kuishi maisha ya ushindi.

Baadaye, ugonjwa ulipokuwa umemzidia kule gerezani, DeShazer alikuwa karibu kufa. Alipokuwa anaomba, akasikia sauti ikisema, "Roho Mtakatifu amekuweka huru dhidi ya dhambi."[86]

Akaanza kusikia ushirika usiokuwa wa kawaida na Mungu. Siku zikapita, na akaongozwa kuombea amani. Kisha ile sauti ikanena naye tena: "Umeitwa uende ulawafundishe Wajapani."[87] Kuhusu makabiliano haya, baadaye DeShazer alisema, "Ninajua nilibatizwa kwa Roho Mtakatifu na kwamba mafuriko makuu ya upendo yaliingia moyoni mwangu."[88]

Tarehe 28 Disemba, 1948, DeShazer, mkewe, Florence, na watoto wao walianza huduma yao ya umishenari kule Japani. Mapema mwaka 1950, DeShazer alihisi kuongozwa kufunga siku arobaini kwa ajili ya mwamsho wa kiroho katika hiyo nchi.

Moja wapo kati ya matunda ya kwanza ya huo mfungo lilikuja tarehe 14 Aprili, 1950, ambapo Jemadari Mitsuo Fuchida alimkubali Kristo. Mwezi uliofuata, Fuchida na DeShazer walikuwa pamoja, wakitoa shuhuda zao

---

84. C. Hoyt Watson, *DeShazer: The Doolittle Raider Who Turned Missionary* (Winona Lake, IN: Light and Life Press, 1950), 95.
85. Watson, *DeShazer*, 96.
86. Watson, *DeShazer*, 118.
87/ Watson, *DeShazer*, 123.
88. Watson, *DeShazer*, 142.

katika ukumbi mkubwa zaidi kule Osaka. Watu mia tano walikuja mbele kumtafuta Kristo. Fikiria—mlipuaji wa Pearl Harbor na mlipuaji wa Japani, wote kusamehewa, kufanywa upya katika Kristo, na kuhubiri msamaha na upendo.

Ungekuwa umefanya hivyo? Ni uwezo na usafi wa utimilivu wa Roho Mtakatifu pekee ndio unaoweza kufanya hilo litokee.

JUNI 16 **167**

# Wapweke Majasiri

*Naye akawamo humo gerezani. Lakini BWANA akawa pamoja na Yusufu, akamfadhili, akampa kibali machoni pa mkuu wa gereza.*
*Mwanzo 39:20–21*

Angekuwa na uchungu. Mara mbili alifanyiwa vibaya sana: kwanza, ndugu zake walimwuza utumwani; kisha mke wa Potifa akamshitaki kimakosa. Huyu mtu mmoja sasa alikuwa gerezani. Lakini *Bwana akawa pamoja naye*. Kwa kumfuata Bwana, alikuwa waziri mkuu wa Misri na akasimamia mradi wa chakula uliookoa nchi na jamaa zake dhidi ya njaa.

Natuwapongeze wapweke majasiri. Lisa alikuwa amepitia talaka mbaya; mume wake alikuwa amemwacha na watoto na kiti kimoja. Hiyo Jumapili, alitembelea kanisa la Nazarene, na kufikia mwisho wa wiki, kanisa likampelekea fanicha. Lisa akasema, "Ilikuwa na rangi zilizoendana. Mungu amekuwa mwema sana. Ningeweza kuhisi mikono yake ikinikumbatia. Je, ningekuwa nimeagizia hili? La, lakini Mungu analitumia." Badala ya kusikia uchungu, Lisa aliamua kuwa vizuri zaidi alipokuwa akikabiliana na maisha yake yaliyosalia.

Baada ya ndoa ya Kelli kuvunjika, yeye na mwanawe Brian walianza kwenda kanisani. Mchungaji wa vijana akawa na mvuto maalum kwa Brian. Kelli akasema, "Tulikuwa hatuna familia, lakini sasa tumepata familia."

Corrie ten Boom, Mdachi mtengeneza saa, alichukuliwa na kupelekwa katika kambi ya wafungwa ya Nazi kwa sababu familia yake ilikuwa ikiwaficha na kuwalinda Wayahudi wakati wa vita. Baada ya babake na dadake kufa katika hiyo kambi, Corrie alitoka kambini kwa neema ya Mungu nyingi sana kiasi kwamba aliweza kuwasamehe watekaji wake. Aliandika kitabu cha nguvu chenye kichwa *The Hiding Place*, na kufikia umri wa miaka themanini,

alikuwa amefanya kazi na kunena katika nchi sitini na moja za ulimwengu. Akiwa peke yake, aliweza kufanya kile ambacho yamkini hangeweza kufanya kama angekuwa na mume na watoto.

Mungu huwatumia wapweke kwa njia maalum. Akiwa na umri wa miaka arobaini na mitatu, chaplaini Oswald Chambers alikufa kutokana na ugonjwa wa kidole tumbo. Mke wake aliyebaki peke akakusanya maelezo yake ya mahubiri yake na akayachapisha kwa jina la *My Utmost for His Highest* mwaka wa 1927. Hicho kitabu bado kinachapishwa kama kitabu maarufu zaidi cha ibaada ya kila siku ulimwenuni kote.

Historia ya Ukristo haiko wazi juu ya kama mtume Paulo alioa au la. Ushahidi mwingi unapendekeza kwamba kamwe hakuoa. Na kwa hakika, alikuwa nguvu kuu katika kueneza ujumbe wa Yesu katika siku zake.

Wapweke majasiri, tunawapa heshima.

**JUNI 17** **168**

# Kuuelewa Uinjilisti

*Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo: mpatanishwe na Mungu.*
*2 Wakorintho 5:20*

Ninasaidiwa na "u" nne za ndoa:

Uwepo—Kuishi maisha ya wema, huruma, na matendo mema; kuweka usikivu kwake, na kukuza uhusiano na yeye.

Utangazaji—"Ninakupenda."

Ushawishi—"Je, unakubali nikuoe?"

Uhifadhi—Kulea na kukuza uhusiano wako wa ndoa katika maisha yako yote.

Vivyo hivyo, hizi "U" nne ni sehemu ya uinjilisti kamili na wa kujumuisha sehemu zote:

Uwepo—Kuishi maisha ya wema, huruma, na matendo mema; kuweka usikivu kwa yule ambaye hajaokoka na kukuza uhusiano na yeye.

Utangazaji—"Mungu anakupenda"; kuwatangazia wengine ukweli wa injili katika kuhubiri na ushuhuda wa kibinafsi.

Ushawishi—"Je, utampokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wako?"

Uhifadhi—Kulea, kukuza, na kuendeleza Mkristo katika ukomaavu na huduma.

Ni kama hakuna hata Mmarekani mmoja niliyekutana naye ambaye ameoa bila swali la ushawishi: "Je, unakubali nikuoe?" Kuishi maisha ya upendo na kutangaza huo upendo bila kuuliza swali la uamuzi haviwezi kuleta ndoa. Na mkakati wa misheni au uanafunzi bila swali la kusudi—"Je, ungependa kumpokea Kristo kama Mwokozi na Bwana?"—kutakatisha misheni yetu ya Kikristo.

Uinjilisti kamili wa kibiblia utajumuisha "U" zote nne. Paulo alisihi kwa ajili ya huduma ya upatanisho katika 2 Wakorintho 5:11–21. Katika ombi lake alisema, "Basi tukiijua hofu ya Bwana, *twawavuta* wanadamu" (kif. 11). Pia alisema, "Upendo wa Kristo *watubidisha*" (kif. 14), na "*Twawaomba* ninyi kwa ajili ya Kristo: Mpatanishwe na Mungu" (kif. 20).

Basi nawahimiza ninyi, ndugu zangu na dada zangu Wakristo, mjumuishe huo "ushawishi"—jumuisha "U" zote nne![89]

JUNI 18 **169**

# Katika programu ya Fishbowl—"Waacheni Watazame"

*Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu, kuishuhudia Habari Njema ya neema ya Mungu.*
*Matendo 20:24*

Anakimbia mbio za mita 400, anaruka chini, ana ujuzi wa mashindano ya mbio na yasiyokuwa ya mbio. Lakini zaidi ya hayo, ameazimia kumaliza mbio ambazo Kristo amemwekea.

Kelly ana miaka kumi na saba. Ni mwanafunzi wa kidato cha juu cha shule za upili, na sana sana anafundishwa nyumbani, na vilasi kadhaa katika shule ya umma. Wazazi wake wote ni wahudumu na wamechunga kwa upendo na kwa ushawishi kwa miaka kumi na minne katika maeneo ya mashambani ya Pensilivania. Kelly ndiye mdogo zaidi kati ya watoto wanane, ambao wengine wamemaliza chuo, wengine ni wanafunzi wa vyuo, na kwa

89. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (March 2012).

Kelly, yeye atajiunga na chuo mwaka ujao. Atakuonyesha kwamba yeye ni mtu wa kutabasamu, kufurahi, kung'ara, amani, na amejaa nguvu tulivu.

Kelly huamka 8:15 usiku, siku nne kwa wiki, anakuwa na wakati wa ibada na Kristo, na huenda kazini saa 9:00 usiku. Akiwa na msaidizi mmoja, hukamua ng'ombe 130. Hutoka saa 1:00 asubuhi. Kwa nini anafanya kazi ngumu namna hiyo? Anasema, "Nataka niwe wa msaada, nifanye kazi ambayo hakuna mtu mwingine anayetaka kuifanya, na nifanye kazi na wanyama. Na hizo pesa husaidia."

Kelly alimpata Kristo kama Mwokozi alipokuwa na miaka minne kule Vacation Bible School. Tangu wakati huo, uhusiano wake na Kristo umekuza tumaini lililoongezeka. Anapenda ukweli kwamba anaweza kumwendea Mungu wakati wowote, na Mungu hamwangushi. Anaona thamani katika kutambua kwamba Mungu hajibu maombi siku zote kama anavyoomba—kwa sababu vinamfanya aendelee kurudi kwa Mungu.

Alisema, "Watu wanajua mimi ni Mkristo na ninafanya mambo kitofauti karibu nami." Hivi karibuni alishuhudia kule kazini, na mfanya kazi mwenza akajibu kwamba hakuna wakati wa kwenda kanisani, na Kelly akajibu, "Ukimwambini Bwana na wakati wako, atakubariki."

Safari yake ya misheni kule Peru katika umri wa miaka kumi na saba ilikuwa kivutio cha maisha yake ya ujana. Alinena na kusanyiko kuhusu kupinga hofu, alisimulia hadithi ya jinsi, hakufanya mchango wowote ingawa safari yake iligharimu $1,550—watu walikuja tu na kumpa pesa.

Alishinda zawadi ya nafasi ya kwanza katika tukio la Sherehe za Maisha na uchoraji wake wa rangi wa kwanza. Anapenda maswali ya Biblia, na kifungu chake anachokipenda zaidi alichokikariri ni Matendo 20:24.

Haoni haja ya kuanza uhusiano wa kimapenzi akiwa shule ya upili. Anasema ataanza uhusiano atakapokuwa mkubwa; hata inaweza kuwa kwamba mtu wa kwanza atakayekuwa na uhusiano naye ndiye atakayemwoa. Kwa Kelly, kuona wanafunzi wa darasa la saba wakishikana mikono shuleni inaonekana kuwa jambo lisilofaa.

Moja wapo kati ya ndoto zake za siku za usoni ni kufanya kazi katika hifadhi za kitaifa. Dhana ya kufanya huduma za Kikristo katika hifadhi inamvutia.

Vifungu ambavyo wazazi wake walimchagulia Kelly wakati wa kuwekwa wakfu alipokuwa mchanga vilikuwa 1 Wathesalonike 4:11–12: "Tena mjitahidi kutulia: Na kutenda shughuli zenu, na kufanya kazi kwa mikono yenu wenyewe, kama tulivyowaagiza, ili mwenende kwa adabu mbele yao walio nje, wala msiwe na haja ya kitu cho chote." Unayaishi Kelly!

Hivi karibuni, wakati wa ibada ya uamsho ya Jumatatu usiku katika kanisa lake la nyumbani, Kelly alitoka mbele apate kuomba na kumtafuta Mungu katika kiwango cha ndani zaidi. Alikuwa tu amesikia uigizaji wa *My Heart—Christ's Home na Robert Boyd Munger*. Kelly alishuhudia: "Nilitoa kila kitu kwa Bwana jana usiku. Nilimwomba asafishe vyumba vyote vya moyo wangu. Nilimpa kila kitu, na nikahisi vizuri. Nikahisi hisia za amani nikijua nilitakaswa. Sasa, kwa ajili ya uthabiti na ukuaji wa kiroho wa siku za usoni, nitauliza, *Ni vyumba gani ambavyo mimi na Bwana hasa tunafanyia kazi leo?*"

Mng'ao na ushawishi wote wa kiroho wa Kelly wa hapo awali vitatiwa nguvu sana kwa kujitoa kwake kikamilifu na utakaso kamili wa Mungu.

Mtu mmoja aliposema kwamba kuwa katika familia ya mchungaji ni kama kuishi katika bakuli la samaki, kaka yake Kelly akasema, "Nawatazame!"

Kelly akaongeza, "Hainisumbui kuwa katika bakuli la samaki."

**JUNI 19** **170**

# Baba Yenu wa Mbinguni

*Basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao!*
*Mathayo 7:11*

Ulimwengu wetu una Baba wa mbinguni anayekupenda na anataka upate mambo bora zaidi. Anatamani awe karibu na wewe na akupe vipawa vizuri.

Ungana Nami katika Hadithi ya Linda: Kati ya umri wa miaka kumi na minne na kumi na sita, alikuwa amehudhuria kanisani mara mbili au tatu peke yake, kupitia kwa ushawishi wa mjomba na shangazi. Mamake aliondoka alipokuwa na miaka mitano. Babake alijaribu kumlea kwa msaada wa bibi yake aliyekuwa amezeeka.

Usiku mmoja, huku akiwa anamsaidia bibi yake jikoni, Linda alisikia mshindo. Akaingia sebuleni na kumwona babake akiwa ameanguka sakafuni kifudifudi, gazeti likiwa limekunjwa-kunjwa chini yake—akifa kwa shambulizi la moyo akiwa na umri wa miaka arobaini na miwili.

Usiku huo, alimwita mchungaji wa kanisa akamwuliza, "Je, utamzika baba?"

Baadaye, aliandika, "Nilihisi nisingeendelea kuishi kwa sababu babangu kwa kweli ndiye mtu pekee niliyekuwa naye."

Pale mazishini, mchungaji alinukuu Zaburi 23:4 (SUV): "Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya: kwa maana Wewe upo pamoja nami." Alieleza haya maneno yanaweza kuwa kweli peke yake kama tutamruhusu Bwana awe mchungaji wetu.

Linda alichukua huo ukweli. Yeye na mashangazi zake, wajomba zake, na nyanya zake, na binamu zake walikuja katika ibada ya usiku wa Jumapili iliyofuata. Kufikia mwisho, Linda na jamaa zake sita walikuwa wamekuja madhabahuni kumtafuta Bwana. Akiwa ameudhiwa kabisa na maisha kutokuwa na maana yoyote, Linda alisema, "Kwa mara ya kwanza Kristo kwa kweli alionekana *halisi* kwangu."

Wiki chache baadaye, mchungaji alipozungumza naye kuhusu maisha ya ndani ya utakaso, Linda alimwambia kwamba alikuwa amepokea tu hilo tukio hilo. Punde, Linda na binamu zake wawili walijiunga na kanisa kwa kurikiri imani.

Nyanya ya Linda alipohama mji ule, Linda alienda kuishi na shangazi yake mmoja. Ilimbidi aiendeleze hiyo Ford aliyokuwa amerithi kutoka kwa babake na alipe gharama za maisha kutoka kwa $96.80 kwa mwezi alizopokea kama mtoto katika malipo ya uzeeni ya babake. Ulipofika wakati wa mipango ya chuo, Linda na rafiki yake Lois (ambaye Linda alikuwa amemwongoza kumpokea Kristo) walipata kazi za muda mfupi ili wapate kupokea pesa za kulipia gari ya kwenda chuo cha Kikristo kule Bethany, Oklahoma. Muda si muda, Linda akawa mwanafunzi huko.

Linda hakuweza kunyamaza kuhusu kile Yesu alichomfanyia. Alileta watu wapya zaidi kanisani kuliko mtu mwingine yeyote. Wakati wa uamsho wa vijana wa siku tano, alileta vijana kumi na mmoja tofauti—wote wapya kwa kanisa—na wanne kati yao walimtafuta Mungu katika hizo ibada.

Linda alikutana na Paul kule chuo; wakapendana na wakafunga ndoa. Paul alikuwa anatoka katika jamaa ya wanamuziki, na punde Linda alikuwa anaimba nyimbo za injili katika kikundi cha watu wanne kilichozunguka kusini kaskazini mwa Marekani. Hatimaye wakafanya makazi yao kule Florida na wakafanya kazi katika kanisa lao la nyumbani, ambapo Paul aliongoza muziki na Linda akafundisha watoto na vijana kutoka kwenye familia zilizovunjika.

Linda anapotazama nyuma katika maisha yake, hutangaza, "Nilimpoteza baba yangu wa duniani, lakini nikampata Baba yangu wa mbinguni!" Baba huyo anakupenda na angependa wewe pia, umpate kwelikweli.

# Chanzo cha Mafanikio

*Maana alikuwa mtu mwema amejaa Roho Mtakatifu na imani, watu wengi wakaongezeka upande wa Bwana.*
*Matendo 11:24*

Thomas Edison alimiliki zaidi ya hataza elfu moja—yamkini zaidi ya mtu yeyote mwingine katika historia—lakini anajulikana zaidi kwa kuvumbua balbu. Unapotembelea nyumbani kwake na makavazi yake kule Fort Myers, Florida, utashangaa sana—ni kitu gani kilikuwa motisha yake ya ndani, nguvu yake ya ndani, msukumo wake binafsi, uliomfanya awe mvumbuzi mkubwa namna hiyo?

Tunaweza kuuliza maswali kama hayo kuhusu motisha ya ndani na maisha ya kiroho ya mashujaa wa Biblia. Tunapoona matokeo makubwa, matunda makubwa, ubora mkubwa, na mafanikio makubwa tunauliza—ni kitu gani kilikuwa nyuma yao?

Mtazame Barnaba, aliyekuwa chanzo kikuu cha kumfanya Sauli (baadaye Paulo) mwokofu mpya akubaliwe na kanisa (Matendo 9:26–28; 11:25–27). Barnaba alikuwa anajulikana kama “mwana wa faraja” (4:36) na aliwatia moyo watu wengine mara nyingi. Yeye ni mmoja wa mifano mizuri sana ya Biblia ya “ufuatiliaji” wa Wakristo wapya. Alikuwa mtoaji mkarimu na “mzuri” kweli. Matendo 11:24 inafunua chanzo cha maisha ya of aina hii ya uzima: “Maana alikuwa mtu mwema amejaa Roho Mtakatifu na imani.”

Mtazame Filipo. Alikuwa mshiriki na mwinjilisti mkubwa wa kujitegemea. Alimwongoza katibu wa hazina ya Ethiopia kwa Kristo, na huyo mtu akapeleka Ukristo Ethiopia. Alikuwa sehemu ya bodi ya kanisa la kwanza la nyumbani na huduma ya huruma akijitolea kuwalisha wajane. Katika Matendo 6, tunajifunza kuhusu chanzo chake cha ndani ya nguvu: “Chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima . . . Wakamchagua Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho Mtakatifu, na Filipo” (vif. 3, 5).

Hiki kifungu pia kinavuta usikivu wetu kwa Stefano. Yeye ndiye mfia dini wa kwanza kwa ajili ya Kristo, wa kanisa la kwanza kunakiliwa Alipokuwa akipigwa mawe hadi kufa kwa kumhubiri Yesu, aliomba, “Bwana, usiwahesabie dhambi hii” (7:60), anawasamehe wauaji wake kama Kristo

alivyofanya. Maandiko yanatwambia kile kilichoushika usikivu wake kabla ya kushambuliwa na umati uliokuwa umekasirika. “Lakini yeye akijaa Roho Mtakatifu, akakaza macho yake, akitazama mbinguni, akauona utukufu wa Mungu, na Yesu akisimama upande wa mkono wa kuume wa Mungu” (7:55).

Kisha kuna mtume Paulo, ambaye ni Sauli aliyeokolewa kimiujiza katika njia ya kwenda Dameski. Alifanya mengi kulipanua kanisa kuliko mtu mwingine yeyote katika historia. Chanzo chake kilikuwa nini? Tunakiona anapokabiliana na Elima mtu mwovu: “Lakini Sauli, ambaye ndiye Paulo, akijaa Roho Mtakatifu, akamkazia macho, akasema, ‘Ewe mwenye kujaa hila na uovu wote, mwana wa Ibilisi, adui wa haki yote, huachi kuzipotoa njia za Bwana zilizonyoka? Basi, angalia, mkono wa Bwana u juu yako, nawe utakuwa kipofu, usilione jua kwa muda.’” (13:9–11).

Katika historia ya hivi karibuni zaidi, kuna mmoja katika viongozi wenye nguvu zaidi katika Kanisa la Kimethodisti, E. Stanley Jones. Aliacha mafanikio mengi, pamoja na vitabu vyake, vinavyojumuisha *How to Be a Transformed Person*; *Christian Maturity*; *Way to Power and Poise*; *Victorious Living*; *Victory Through Surrender*; *Abundant Living*; *Unshakable Kingdom*; *Song of Ascents*; na *The Divine Yes*. Mwaka mmoja baada ya kuokolewa na Kristo, Jones alitoa ushuhuda, “Ghafla nikajazwa—nikajazwa na Roho Mtakatifu. Wimbi baada ya wimbi yalionekana yakinipitia kama moto wa kusafisha.”[90]

Hawa mashujaa wote wa imani walipata nguvu zao, na uvumilivu wao, na tumaini lao kutoka kwa Roho wa Mungu.

**JUNI 21** **172**

# Malezi ya Kukusudia

*Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako. Nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii. Na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo.*
*Kumbukumbu la Torati 6:6–7*

Sikia ombi lenye hamasa kutoka kwa kiongozi wa kidhehebu kwenda kwa wazazi kwa ajili ya watoto wao. Haijalishi usuli wako wa kidini ni wa namna gani, sikia moyo wake.

90. E. Stanley Jones, *A Song of Ascents* (Nashville: Abingdon Press, 1968), 53.

"Sikiza, Ee Israeli: BWANA Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja. 'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote" (Kumbukumbu la Torati 6:4–5). Kwa hakika Yesu, alinukuu hiyo *Shema* alipoulizwa, "Amri kuu zaidi ni ipi?" Akiongeza amri ya "kumpenda jirani yako kama ujipendavyo" (Mambo ya Walawi 19:18), Yesu alifunua kwamba amri nyingine zote hutoka katika hizi amri mbili!

Hizi amri mbili zinaendelea kushikilia nafasi muhimu zaidi katika mioyo ya watakatifu leo. Kama Wanazorayo, tunashikilia kwa uthabiti imani katika kazi yote ua utakaso. Inabaki kuwa wazo letu lenye tofauti ya kitheolojia katikati ya makanisa mengi ya Kiprotestanti, na ilikuwa sehemu ya sababu ya kuzaliwa kwa Kanisa la Wanazarini mwaka wa 1908. *Mwongozo wa Kanisa la Nazarini* unasema, "Tunaamini kwamba utakaso wote ni kile kitendo cha Mungu, kinachofuata uongofu, ambao kwa huo waumini wanafanywa kuwa huru kutoka kwa dhambi asili, au upotovu, na kuletwa katika hali ya kujitoa kwa Mungu kikamilifu, na utiifu mtakatifu wa upendo uliofanywa kuwa kamili" (Makala ya Imani X). Kumpenda Mungu na kuwapenda wengine ndiyo maonyesho makuu ya maisha ya muumini aliyetakaswa kikamilifu.

Katika miaka yangu ishirini na sita ya uchungaji, hata hivyo, ni lazima nikubali kwamba sijaona ari hii na kusudio katika wazazi wa Nazarene inapofikia mahali pa kuwasaidia watoto wao wakione kipawa cha Mungu cha utakaso mkamilifu. Huku tukiwa tunaamini katika hii kazi ya pili ya neema, inahuzunisha, hatuonekani kujitoa kuwasaidia watoto wetu kuona furaha ya kuenenda katika uhusiano mzuri sana wa kujitoa kwa Mungu kikamilifu. Sisikii wazazi wakimwomba Mungu kwa ajili ya watoto wao watakaswe kikamilifu. Ni nadra kusikia shuhuda za watoto walioingia katika huu uhusiano mzuri sana wa uzima teletele katika Kristo. Hebu fikiri kuhusu hili kwa dakika moja: Je, tunataka watoto wetu wajue msamaha wa dhambi lakini wasiuone "utiifu mtakatifu wa upendo kufanywa kuwa kamili"?

Tumeunda mfumo mpya wa ulimwengu kwa ajii ya uanafunzi. Huu mfumo utatumika kuelekeza jitihada zetu za uanafunzi kwa kukusudia. Mfumo wetu mpya hufasili uanafunzi wa Nazarini kama safari ya neema. Tunatambua kwamba uanafunzi ni safari ambayo inachukua maisha yote. Katika hiyo safari, tunakutana na neema ya Mungu na tunaitwa kuitikia neema yake. Safari ya neema inajumuisha neema ya Mungu ya kukuzuia, ya kukuokoa, na ya kukutakasa. Kupitia kwa neema ya kukuzuia, Mungu anatutangulia kutengeneza njia na kutuvuta katika uhusiano. Kupitia kwa

neema ya kuokoa, Yesu anatuokoa kutoka dhambini na kutuongoza katika kweli inayotuweka huru. Kupitia kwa neema ya kutakasa, Roho hututia nguvu za kuishi maisha yalitowekwa wakfu kwa Mungu kikamilifu. Wanazorayo wanapohusika katika misheni ya Mungu katika ulimwengu huu, tunajitoa kuungana na wengine katika safari kutoka neema hadi neema kupitia kwa neema.

Mimi na mke wangu, Jenni, tunataka kutangaza tamanio letu la binti zetu wote wawili, Bekah na Sarah, wasione tu neema ya wokovu peke yake katika Kristo, lakini pia kazi ya Roho Mtakatifu ya utakaso kamilifu kwa neema kupitia imani. Tunaomba kwamba binti zetu, "wapate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu" (Waefeso 3:19). Tunaomba kwa juhudi, "usiku na mchana . . . tupate . . . na kuyatengeneza mapungufu ya imani yenu" (1 Wathesalonike 3:10). Tunaomba "Mungu wa amani, awatakase [binti zetu] kabisa. Nafsi zao na roho zao na miili yao na ihifadhiwe wawe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo" (1 Wathesalonike 5:23). Tumejitoa kuwafundisha watoto wetu jambo hili na kuwahimiza wazazi wengine wafanye vivyo hivyo. Hatutagemea huduma ya watoto ya kanisa la nyumbani kuwaongoza katika uhusiano huu na Mungu, lakini tutashukuru kwa msaada tunaopokea kutoka kwa jumuia ya kanisa letu. Tunapokea wajibu kibinafsi kama wazazi, na tunajitoa kuwafanya wanafunzi watoto wetu kupitia kwa safari yote ya neema! Je, mtaungana nasi katika kufanya kujitolea huku kuwe malezi ya kukusudia?[91]

Scott Rainey

**JUNI 22** **173**

# Mafunzo Makubwa Zaidi katika Miaka Hamsini ya Ndoa

*Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake,*
*ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja.*
*Waefeso 5:31*

91. Adapted from *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (March 2020).

Katika shule ya Jumapili, mimi na Nancy tulifundisha "Mafunzo Kumi Makubwa Zaidi Tuliyojifunza katika Miaka Hamsini ya Ndoa." Haya ndiyo hayo mafunzo, kwa muhtasari kabisa (manne ya kwanza yanatoka kwa Nancy, na yaliyosalia yanatoka kwangu):

1. Ufanyeni upendo wenu uendelee kuwa hai wakati wote wa ndoa yenu.
2. Hisia ya usalama inatakiwa ili ndoa iwe na nguvu, nasi tunapana usalama huo—lakini tafuteni hata usalama wa juu zaidi katika kumtegemea Bwana.
3. Jengeni undani unaomruhusu kuwa karibu kwelikweli ninyi kwa ninyi, katika kiwango cha moyo.
4. Kujitoa—ninyi kwa ninyi, 'mpaka kifo kiwatenganishe—ndiyo njia ya hekima zaidi na yenye nguvu zaidi. Lakini zaidi ya yote, kujitoa kwa Bwana ndiyo siri kubwa zaidi ya kuwa na upendo wa kina katika ndoa.
5. Ndoa ni sehemu ya mpango mkubwa zaidi—mpango wa Mungu. Msingi wako ni Yesu Kristo, si ndoa yako.
6. Usimchukulie mkeo hivi hivi. Kila siku, sema asante; mpongeze; mwambie nakupenda; na umkumbatie mara saba kwa siku.
7. Katikati ya majaribu ya ulimwengu wa ponografia, Bwana aliniambia, "Huna haki ya kutazama mwili mwingine wowote [katika picha, mtu mwenyewe] ila mwili wa Nancy."
8. Nyakati ngumu zaidi zinapokuja, kama talaka ya binti yetu, mimi na Nancy tulivunjika mioyo na kushikwa na vidonda vya tumbo kwa wakati mmoja. Pia tulijifunza, "Mwisho wa ndoto zilizovunjika, yeye ndiye mlango ulio wazi." Baada ya Mungu kuiponya mioyo yetu, tulitambua kwamba katika huo mchakato, pia aliipanua mioyo yetu. Leo, tunaweza kushikilia upendo zaidi na Mungu zaidi kuliko tulivyowahi kuweza.
9. Endelezeni huduma ya kuandikiana ujumbe—kwenye sanduku, juu ya meza ya jikoni, kwenye kadi.
10. Unapokuwa na wakati mgumu kumwelewa mwenza wako, acha hili swali liongoze mwitikio wako: "Yesu Kristo angemchukulia namna gani?"
11. Bahashishi: Tunaendelea kucheza mchezo ambamo ninajaribu kuwa mzuri kwake kuliko anavyokuwa kwangu. Anajaribu kuwa mzuri kwangu kuliko ninavyokuwa kwake. (Nancy husema ninashinda.)

Haya ndiyo hayo—masomo kumi na moja katika miaka hamsini. Ni safari ya namna gani na mwanamke mzuri namna hii. Asanteni nyote mliotusaidia

katika hii safari, na asante kwa Yesu Kristo aliyetubariki sana katika hii safari hata ikafanikiwa![92]

JUNI 23 **174**

# Tunda Litakalodumu, Sehemu ya 1

*Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda—na matunda yenu yapate kukaa—ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni.*
*Yohana 15:16*

Lazima ilikuwa kama mwaka 1989 wakati First Church ilipoanza mradi wa Jirani-hadi-Jirani. Lengo lake lilikuwa kujijulisha wenyewe na kuwaalika majirani wa karibu kanisani kupitia kwa pakiti iliyoachwa katika kila mlango. Nancy na binti yake, Jennifer, waliitikia. Sasa Jennifer huyo huyo na mumewe, Jonathan, wanafundisha darasa hapo kanisani. Hili lilifanyika namna gani katika kipindi cha zaidi ya miaka thelathini? Hii ndiyo hadithi kwa maneno yao wenyewe:

**Jennifer**

*Hadithi yangu inaanzia wakati nilipokuwa na umri wa kama mtoto wa darasa la tano au la sita. Wazazi wangu waliamua kuhamia nyumba mpya kule Jiji la Kansas mwaka ule nilipokuwa darasa la tano, na ilifanyika tu kwamba nyumba yetu mpya ilijengwa barabara chache kaskazini mashariki mwa kanisa lililoitwa First Church. Wakati ule, kanisa halikuwa vile lilivyo sasa; halikuwa na mnara wala jengo, na mamangu hata alinambia kwamba, kwa muda, alidhani kuwa ilikuwa kampuni ya stima. Hadi kufikia wakati huo katika maisha yangu, nilikuwa nimeenda kanisani mara chache tu.*

*Kisha siku moja, mimi na mamangu tulirudi nyumbani na tukapata pakiti tu ya kawaida mlangoni kwetu. Tulipoifungua, tuligundua kuwa ilikuwa imetoka First Church kama sehemu ya programu ya kuifikia jamii. Ninakumbuka ilitosha kuwasha moto wazo kwa mamangu kwamba isingekuwa vibaya kujaribu First Church.*

92. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Septemba 2009).

*Kwa kuwa babangu alifanya kazi Jumapili, mimi na mamangu ndio tulioanza kuhudhuria. Ninakumbuka kuanzia hiyo Jumapili ya kwanza tulihisi kukaribishwa sana kwa upendo na hilo likatufanya tujisikie nyumbani. Huyo mchungaji katika hiyo miezi ya kwanza ya uhudhuriaji wetu alikuwa Keith Wright, na ninakumbuka kwa kusikiliza mahubiri yake kwa hamu Jumapili na kuziingiza jumbe zake akilini mwangu nikiwaza kwamba kanisa lilikuwa halichoshi kabisa! Baada ya wiki chache, nilianza kuhudhuria shule ya Jumapili. Ninakumbuka kwenda katika idara ya watoto na mara moja kumtambua msichana kutoka darasa langu la tano shuleni. Mmoja wapo kati ya walimu wangu wa kwanza wa shule ya Jumapili alikuwa Beulah Postlewait, ambaye pia alimfundisha mwanangu, Jackson, na wakati huu anamfundisha binti yangu, Hadley, katika darasa la watoto wa miaka minne. Katika huo mwaka wa kwanza wa First Church, akili yangu ilikuwa inakuwa inafunguka kwa mipango ambayo Mungu alikuwa nayo kwa ajili yangu.*

*Katika wakati huu, mamangu alifuatwa na mchungaji aliyekuwa anataka kuja nyumbani kwetu na kujifunza mengi zaidi kuhusu sisi. Ninakumbuka akituonyesha kadi ya Yesu akiwa amesimama mlangoni akibisha. Alieleza kwamba mlango uliwakilisha mlango wa mioyoni mwetu na kwamba Yesu alitaka kukaribishwa ndani. Nilisikia kusisimka kufanya hivyo, na mimi na mamangu, sote tukaomba na Mchungaji Shaver ili Bwana aingie ndani. Tangu wakati huo imekuwa safari ndefu!*

*Sina shaka akilini mwangu kwamba Mungu alikuwa anatuongoza na kutuelekeza kwake wakati wote katika hatua yetu ya kwanza, pakiti ilikutwa mlangoni petu, na kupitia watu wengi wazuri sana wa First Church.*[93]

**JUNI 24** **175**

# Tunda Litakalodumu, Sehemu ya 2

*Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda—na matunda yenu yapate kukaa—ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni.*
*Yohana 15:16*

93. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (March 2017).

**Jonathan**

*Hadithi yangu ya kumkubali Yesu Kristo moyoni mwangu ilitokea wakati nilipokuwa na umri wa miaka ishirini na mmoja—baadaye kidogo katika maisha kuliko hadithi ya mke wangu.*

*Nilikuzwa Mkatoliki. Familia yangu ilihudhuria kanisani kila mara kwa muda, lakini kwa sababu yoyote ile, hiyo ikafifia kwa muda katika miaka yangu ya baadaye ya shule ya msingi.*

*Sikwenda kanisani mpaka nilipokutana na Jennifer ndipo nikaanza kwenda kanisani tena. Nilianza kuambatana naye mara kwa mara katika miaka yetu ya uhusiano. Wakati huo, nisingeweza kusema nilikuwa mtu wa dini, lakini nilikuwa huru kuhudhuria na yeye. Ibada tulizokuwa tukihudhuria kule First* Church *mara nyingi zilikuwa na athari na maana kwangu, na imani yangu ilikuwa inakua, lakini nilikuwa bado sijajitoa kikamilifu kwa Bwana.*

*Baada ya kumwomba Jennifer tuoane katika majira ya joto ya 2000, tulijua tunataka kufunga ndoa kule First Church. Tulimchagua Mchungaji Shaver atufungie ndoa yetu na tukakutana naye mara nyingi kujadili maisha yetu ya kiroho tunapoingia katika hiyo ndoa yetu na vipengele vya hiyo sherehe yetu. Nikiwa bado sijamkubali Kristo kikamilifu wakati huo, Mchungaji alituhimiza tufanye mafunzo ya Biblia na wanandoa wengine, Fabian na Kandy Pearson, nyumbani kwao. Fabian alikuwa na amali katika tasnia ya fedha sawasawa na ile yangu, na alikuwa anafanya kozi kupitia seminari ili awe mchungaji, kwa hivyo Mchungaji alifikiri tunaweza kuwa wenza wazuri. Katika msururu wa mikutano yetu kwa miezi mingi, nilipata kuelewa maana ya kuwa Mkristo na kuwa na Yesu kama kama kitovu chamaisha yangu. Katika mmoja wapo wa hiyo mikutano, tukikaa katika meza ya jikoni ya Pearsons, nilihisi uhitaji wa kuomba na kumkubali Yesu katika maisha yangu na moyo wangu. Katika huo wakati, nilihisi kutosheka kwa ndani na upendo ambao nilikuwa sijawahi kuusikia awali. Ninashukuru sana kwa njia ambayo Mungu aliniweka na natarajia chochote kile ambacho siku zangu za usoni zimeniwekea, vitu vizuri na vibaya, kwa sababu ninajua ninaweza kumtegemea ili aniongoze.*

Fikiri tu—mtoto wa darasa la tano asiyeenda kanisani aliyekuja kwa Kristo sasa anafundisha watoto wa darasa la tano kuhusu Yesu, zaidi ya miaka thelathini baadaye. Hayo yalikuwa ni malipo mazuri kwa kanisa linalohusika na kufikia watu na kuwashuhudia. Au kama Yesu alivyosema, “Si ninyi

mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matundat—na matunda yenu yapate kukaa."[94]

JUNI 25 **176**

# Alijaribiwa—Lakini Hakutenda Dhambi

*Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasikatika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwasawasawa na sisi katika mambo yote—bila kufanya dhambi.*
*Waebrania 4:15*

Marafiki zetu wapendwa walikuwa wanahamia nyumba yao waliyonunua hivi karibuni. Katika zile dakika thelathini waliondoka kurudisha lile lori waliloazima, nyumba yao ikashika moto, na sehemu nyingi zikaharibiwa. Katika ushauri wa chama cha wenye nyumba, waliajiri mkandarasi. Baada ya kuondoa uharibifu wote na kabla hawajaanza kujenga upya, huyo mwanakandarasi akapotea na pesa zao za ukarabati. Kesi zikaanza, na nikamwomba wakili wangu awasaidie. Wakati alipotambua yule mwanasheria wa wilaya wa serikali alihusika, rafiki yangu wakili alisema tushikane na yeye—alikuwa ana uwezo wa kushawishi kuliko wakili mwingine yeyote waliyeweza kuajiri.

Yesu Kristo ndiye kuhani wetu mkuu mbele ya Mungu, na ana ushawishi mkuu wa kutoa hoja za kesi yetu kuliko mtu mwingine yeyote. Ili usije ukafikiri kwamba yeye ni mkuu sana na mtakatifu hata hawezi kukuelewa, tafadhali jua kwamba katika ubinadamu wake, Yesu alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote. Hata mara moja hakushindwa; hakutenda dhambi. Kuna tofauti kati ya majaribu na dhambi: Kila mtu, pamoja na Yesu, anajaribiwa, lakini yeye hakutenda dhambi, na huna haja ya kutenda dhambi.

Majaribu mengine huja kutoka nje na ni ya wazi sana, kama Shetani alipomjaribu Yesu kule nyikani (Luka 4). Wakati mwingine Shetani hushupaa na hushambulia kama simba angurumaye (1 Petro 5:8). Nyakati nyingine, anakuwa mwerevu na mdanganyifu, akijifanya malaika wa nuru (2 Wakorintho 11:14).

94. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (March 2017).

Lakini majaribu pia yanaweza kuja kutoka ndani. Mungu ametuumba tukiwa na misukumo na matamanio fulani kama sehemu ya ubinadamu wenye afya na imara. Hii misukumo ina nguvu na ni mizuri kama ina nidhamu na inaongozwa.

Kuna msukumo wa kijamii—tamanio la nguvu ili watu wakupende. Lakini kama huo msukumo ukiruhusiwa kutoka nje ya udhibiti, unaweza kumwasi Mungu ili uwafanye watu wakupende.

Kuna msukumo wa ngono, ambao ni sehemu ya mpango wa Mungu wa kuendeleza jamii ya wanadamu, na ulikusudiwa uwe tukio la mapenzi kati ya mwanamume na mwanamke waliofunga ndoa. Lakini kama huo msukumo hauna nidhamu, na unauchukulia kama kitu cha kukufurahisha, inakuwa ni dhambi.

Kuna msukumo wa usalama, unaolinda maisha yako. Huu msukumo unakusababisha uruke kutoka katika njia ya gari inayoenda kwa kasi. Lakini pia unaweza kupotoshwa na kukufanya kuwa mtu wa kunyakua, kumiliki, na mbinafsi. Katika kisa hiki tena, msukumo mzuri umekuwa dhambi.

Kuwa mwerevu. Kuwa macho. Misukumo yako ya ndani ni mizuri—usiiache ikageuzwa. Huku Yesu akiwa kuhani wetu mkuu huko juu, Roho Mtakatifu aliyepo "hutusaidia katika udhaifu wetu" (Warumi 8:26).

Paulo alitumia maneno ya nguvu katika 1 Wakorintho 9:27 alipoandika, "Bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha, isiwe nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa". Alijaribiwa, ndio, hata kutoka ndani—lakini na nidhamu ya kiungu, huna haja ya kutenda dhambi.

JUNI 26 **177**

# Bila Kutarajiwa

*Akamwona Myahudi mmoja, jina lake Akila, mzalia wa Ponto; naye amekuja kutoka nchi ya Italia siku za karibu, pamoja na Prisila mkewe, kwa sababu Klaudio amewaamuru Wayahudi wote watoke Rumi. Paulo akaenda kuwaona na kwa kuwa kazi yao ya ufundi ilikuwa moja, akakaa kwao, wakafanya kazi pamoja.*
*Matendo 18:2–3*

"Bila Kutarajiwa" ni msemo tunaotumia kuelezea tukio ambalo halitarajiwi kabisa. Mungu anafanya kazi yake hapa ulimwenguni, na ijapokuwa tunajaribu kuelewa mapenzi ya Mungu na kuyafuata, wakati mwingine atatushangaza.

Unaweza kueleza mkutano wa Paulo na Akila na Prisila kama tukio "lisilotarajiwa." Paulo alikutana na wenza hao kule Korintho kwa sababu Mfalme Klaudio alikuwa amewaamuru Wayahudi wote waondoke Rumi—Mungu atatumia matukio ya kisiasa na ya kijamii hata maovu, kuendeleza ufalme wake. Muungano wa kwanza wa hawa watu watatu yalikuwa katika kazi yao isiyokuwa ya kidini kama watengenezaji wa mahema.

Paulo alitoka sinagogini kwake kuhubiri kule Korintho kwa sababu ya upinzani kutoka kwa Wayahudi. Kisha, bila kutarajia, Kripo mkuu wa sinagogi, akamkubali Bwana, pamoja na familia yake yote (Matendo 18:7–8). Punde baadaye, "Bwana akanena na Paulo"—tena, inaonekana bila kutarajiwa—akimwambia asiogope kwa sababu alikuwa na "watu wengi katika mji huu" (kif. 9–10).

Marafiki zake watengenezaji mahema wapya, Prisila na Akila, sasa walifanya kazi na Paulo katika hiyo huduma na wakaambatana naye katika safari yake ya kwenda Efeso. Mwishowe, akawaacha huko wakihudumia (kif. 18–19). Prisila na Akila walimfundisha msimulizi wa nguvu Apolo, ambaye hatimaye aliendа Akaya kumtangaza Yesu kama Masihi (kif. 26–28). Maendeleo kama hayo yanaweza kuwa yalionekana kuwa mambo yasiyotarajiwa, lakini Mungu aliyafanya yakatendeka.

Vivyo hivyo, matendo yako kwa ajili ya Mungu yanaweza kuleta matokeo bila kutarajiwa. Mimi na Nancy tulitembelea kanisa la nyumbani kuimba, kufundisha, na kuhubiri. Tulipokuwa huko, tulikutana na washiriki ambao ni wafanyakazi wa kichungaji. Kufikia mahali fulani, mmoja wapo wa wachungaji, Gary, alitujia na kutukumbusha kuhusu mkutano wetu wa kwanza. Alisema jambo kama hili: "Tulipofika ili tuchunge kanisa dogo, ni kama hakuna hata mtu moja aliyenena nasi chochote. Ninyi mlikuwa watu pekee mliotukaribisha. Wewe na Bi. Shaver mlitupeleka kwenye mlo wa mchana."

Nilikuwa sijakumbuka huu muungano huu—Gary siku zote alikuwa ananena kuhusu mkutano ambao ulikuwa umefanyika kama miaka hamsini na mitano iliyopita. Nilishangaa na kunyenyekezwa kujifunza kwamba wema wetu rahisi ulikuwa umeleta athari kama hizo. Hii ripoti ilikuja kwetu bila kutarajiwa kabisa.

Jitayarishe kwa ajili ya tukio lako la bila kutarajiwa kutoka kwa Bwana; kuwa tayari kuwa ushawishi kama huo kwa ajili ya Mungu ili ripoti kama hizi zitakurudia bila kutarajiwa.

# Neema—Wa neema

*Kwa maana ikiwa kwa kukosa kwake yule mmoja wengi walikufa, zaidi sana neema ya Mungu, na kipawa kilicho katika neema yake mwanadamu mmoja Yesu Kristo kimezidi kwa ajili ya wale wengi!*
*Warumi 5:15*

Kimbunga cha sekunde kumi kilipasua katikati ya Jiji la Pierce, kule Missouri, saa 12:45 jioni tarehe 4 Mei, 2003. Mtu mmoja alikufa. Zaidi ya hayo, ukumbi wa jiji, biashara arobaini na mbili kati ya arobaini na tano za humo mjini, na nyumba themanini na moja viliharibiwa kabisa.

Mwenye duka kubwa la mjini alilazwa hospitalini kule Springfield wakati wa hicho kimbunga. Yeye na mke wake walikuwa wanamiliki hilo duka kwa miaka kumi na sita. Aliporudi hapo mahali ambapo palikuwa hilo duka lake, lilikuwa linachotwa na kujazwa kwenye lori la taka.

Hatimaye, mara tu mji uliporudi tu kidogo katika hali ya kawaida, mwenye duka la vyakula aliendea Kanisa la Baptisti na akauliza kama angenunua uwanja wao. Awali hilo kanisa lilikuwa limepanga kujenga kanisa jipya nje ya mji. Baada ya bodi ya kanisa kukutana, walikataa kumwuzia huyo mwenye duka la vyakula—badala yake, wakampa hicho kiwanja. Hata hivyo, huo mji ulihitaji duka la vyakula.

Daktari wa madawa pia alihitaji sehemu mpya, kwa hivyo akamwendea mwenye duka la vyakula kuhusu kununua uwanja *wake* wa zamani. Huyo mwenye duka la vyakula hakuweza kumwuzia; alimpa tu.

Ukumbi wa jiji ulikuwa ni lazima ujengwe tena, kwa hivyo meya akamwendea daktari wa madawa kuhusu kuhusu kuuza uwanja *wake* wa zamani. Huyo daktari wa madawa akasema jiji linaweza kuuchukua bure.

Inashangaza kwa namna gani kwamba katika mahali pa uharibifu, matendo ya neema yalizidi kuwa mengi. Hakuna mtu aliyelazimishwa.

Tunapoona neema ya Mungu ikionyeshwa katika Biblia, ni wazi kwamba yanaelekea kuwafanya wapokeaji wake wawe wenye neema pia. Neema ya

Mungu na neema ya Yesu Kristo vinawafurikia watu wengi leo. Je, umeshikwa katika huo mtiririko?[95]

JUNI 28 179

## Mahali Hapo ni Nchi Takatifu

*Tena akasema, "Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo." Musa akaficha uso wake; kwa maana aliogopa kumwangalia Mungu.*
*Kutoka 3:6*

Alikuwa na hamu ya kumjua Mungu vizur zaidi. Nyakati zote, jambo ovu lilikuwa bado linavuma ndani yake. Akiwa Peke yake kule nyumbani alikaa apate kuomba.

Kisha, Mungu akamjia kama moto—kama "nuru nzito." Nafsi yake ikabadilishwa, ikainuliwa juu hadi viwango vipya vya kiroho, na mahitaji yake yakatimizwa.

Akaanza kuhubiri utakatifu wa Mungu na hitaji la watu kuwa watakatifu kuliko walivyowahi kuwa. Makanisa aliyochunga baada ya hapo yalikua na nguvu ya ajabu—zaidi ya mara moja, makanisa yake yalikuwa na washiriki maradufu katika mwaka mmoja. Dkt. Phineas F. Bresee hivyo basi akawa mtu wa Mungu wa kuwakomboa watu kwa ajili ya Mungu. Muda si muda, moto mtakatifu uliwaka katika bara lote la Marekani katika kundi jipya lililoitwa Church of the Nazarene.

Yule mtu aliyepokea Amri Kumi kutoka mkononi mwa Mungu kwanza alijifunza kwamba Mungu ni mtakatifu. Ili uweze kujibu kilio cha watu walio utumwani (Kutoka 2:24), Bwana alinena na Musa kutoka kwenye moto kwenye ardhi iliyofanywa kuwa takatifu na uwepo wake (Kutokas 3:5). Oo, natamani kwamba leo wengi zaidi wangetoa viatu vyao baada ya kusikia sauti na kuhisi huo moto! Basi wangeweza kuwaongoza watu.[96]

95. Drawn heavily from a report in Marilyn Meberg, *Assurance for a Lifetime* (Nashville: W Publishing Group, 2004), 55–57.

96. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Julai–Agosti–Septemba 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 14. Imetumiwa kwa ruhusa (Chapisho hili likawa *Reflecting God*.)

# Jinsi ya Kujua Mapenzi ya Mungu

*Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu—ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*
*Warumi 12:1–2*

Cheri alilia huku akisema, "Ninaogopa Mungu hataniruhusu niwe naye." Huyo msichana kijana alikuwa katikati ya mgongano: Mapenzi ya Mungu dhidi ya mapenzi ya Cheri.

Hatua ya kwanza ya kutafuta mapenzi ya Mungu ni kuhakikisha umejitoa kwake kama sadaka iliyo hai. Mara tu unapokuwa katika hiyo hali ya kujitoa, kuna njia tano za utendaji za kupambanua mapenzi ya Mungu:

1. **Biblia**. Neno la Mungu linatoa kanuni fulani zinazokuwa juu ya kila kitu, kama vile Warumi 12:1–2. Biblia haikwambii kama unapaswa kuwa daktari au dereva wa lori—hata hivyo, inaweka wazi kwamba uchaguzi unaofanya lazima utoke katika maisha yaliyotolewa kwa Mungu kikamilifu.
2. **Uongozi wa Roho katika Maombi**. Hapa ndipo Roho anaweza kukupa mwongozo maalum zaidi: ni kazi gani, mtu gani, ni chaguo gani. Sauti ya Roho inasikika kama kitu gani? Kulingana na A. J. Russell, "Sauti ya kiungu haitamkwi kwa maneno ya kusikika siku zote. Huwa inajulishwa kama ufahamu wa moyo."[97]
3. **Milango Iliyo Wazi na Iliyofungwa**. Hii inapaswa kusaidia uongozi wa Roho. Kama unahisi kuwa mhandisi lakini umeanguka kozi zako zote za hesabu na sayansi, huo unasikika kama mlango uliofungwa.
4. **Ushauri wa Marafiki Wakristo Wakomaavu**. Nilipoalikwa kwenda kufundisha katika seminari, niliwauliza watano kati ya marafiki zangu Wakristo ninaowaamini wanipe maoni yao. Wanne walisema ninapaswa kukubali hicho cheo. (Kwa hakika, pia nilitafuta ushauri kutoka katika Maandiko na nikaomba kuhusu huo uamuzi.)

---

97. A. J. Russell, *God Calling* (New York: Arthur James Ltd., 1953).

5. **Sababu Iliyotakaswa**. Unapaswa kutumia mantiki yako na ufahamu kuelewa ukweli wa hiyo hali. Haya ni mazoezi ya sababu "iliyotakaswa"—yaani, sababu ambayo inahifadhi mahali pakubwa kwa ajili ya Mungu. Hivi sasa, mmoja kati ya wapendwa wangu anajaribu kuamua kama ataongeza mkopo wa nyumba yake ya rehani. Katika huo mchakato, anatumia sababu iliyotakaswa kutengeneza orodha ya machaguo yote ya kifedha.

Katika kupitia tena hizi rasilimali, ninakumbushwa rafiki mmoja ambaye amekuwa na mfululizo wa maamuzi muhimu sana mbele yake. Katika mchakato huo, ametumia miongozo yote mitano ya kupambanua mapenzi ya Mungu. Matokeo yake ni kwamba, anaweza kufanya jaribio na kuthibitisha mapenzi ya Mungu—yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu. Na ni vizuri sana.

JUNI 30 **181**

# "Kamilifu"—Je, Unafanya Mzaha?

*Katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.*
*Waebrania 10:10*

*Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.*
*Waebrania 10:14*

Inawezekana kuleta mchanganyiko karibu na maneno, virai, au dhana nzuri na kamilifu. Ni kama Seattle mwanafunzi wa darasa la tano aliyefanya mtihani wa sayansi juu ya mwili wa mwanadamu. Badala ya kutambua fuvu la kichwa, kifua, na mvungu wa tumbo, akaandika "fuvu la mchwa," "tifua," na "uvungu wa kuchukiza."

Neno "kamilifu" limekuwa na historia yenye matatizo. Kisingizio cha kila mara cha mwanangu kijana cha kufanya makosa kilikuwa, "Hakuna mtu mkamilifu, Baba."

Waebrania inaonyesha ukuu wa sadaka ya Kristo juu ya mfumo wa sadaka wa zamani—"mara moja tu" dhidi ya "tena na tena." Kuhani wa Agano la Kale anabaki *kusimama* siku baada ya siku; Kristo alikufa mara moja tu kwa ajili ya wote na sasa *ameketi* mkono wa kuume wa Mungu (Waebrania 10:11–13).

Inaonekana kipengele cha kwanza cha mapenzi ya Mungu ni kwamba tunapaswa kutakaswa (kif. 10)—lakini hatuwezi kufanya hivi sisi wenyewe. Ni kwa kupitia mwili wa Kristo peke yake. Sadaka yake kamilifu imeleta ukamilifu kwa wale wanaotakaswa. Katika kifungu cha 16–17, Mungu anakabiliana na dhambi kwa njia mbili: katika kifungu cha 17, hazikumbuki dhambi tena (yaani, yeye husamehe dhambi); katika kifungu cha 16, anatia sheria katika mioyo yetu. Katika huo mchakato, anasafisha na kuweka mfanano wa Kristo mioyoni mwetu. Sasa Mungu ameipita tabia ya nje ili abadilishe nafsi zetu za ndani.

Katika Agano Jipya, neno "kamilifu" maana yake ni iliyokamilika; kuletwa katika kiwango kilichotakiwa; kutimiza lengo ambalo kile kitu kilikusudiwa au kilipangwa kilitimize. Inatuleta sisi katika upendo kamilifu, ambamo tunampenda Mungu na mioyo yetu yote, akili zetu zote, na roho zetu zote. Yohana wa kwanza 4:17–18 inaeleza aina hii ya upendo inaposema, "Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu; kwa kuwa, kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu. Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu."

Ukamilifu huu una mipaka. Si nguvu kamili, ujuzi kamili, hekima kamili, mawasiliano kamili, hukumu kamili—lakini upendo kamili. Maneno "mara moja tu" na "wakati wote" katika maandiko ya leo huweka mkazo juu ya ukuu wa sadaka ya Kristo.

Fikiri kwamba baada ya kujifunza kwa muda mrefu na kwa bidii, mvulana mdogo anapokea 100% katika mtihani wake wa herufi. Analeta mtihani wake nyumbani na kumwonyesha babake kwamba mwalimu wake amendika, "Karatasi kamili" juu ya hilo karatasi. Mungu huliangalia kwa muda kidogo, kisha anasema, "Lakini mwanangu, hufikiri kwamba unaweza kuboresha mwandiko wako?" Kwa hakika, huko ni kukosa hilo wazo kabisa—huyo mwana alikuwa kamili katika hilo eneo alilojaribiwa.

Si ajabu Warumi 13:10 inasema, "Pendo ndilo utimilifu wa sheria" na Warumi 5:5 inasema, "Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi." Mungu ametuumba ili tumpende yeye na wengine—sasa lengo ambalo tuliumbwa kwa hilo linatimizwa na kazi ya Roho Mtakatifu.

Hatufanyi mzaha! Kama Waebrania 10:14 inavyoshuhudia, Mungu "amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa."

# Bwana, Anayeamsha Mioyo

*Ikawa katika mwaka wa kwanza wa Koreshi, mfalme wa Uajemi, ili kwamba neno la BWANA alilolisema kwa kinywa cha Yeremia lipate kutimizwa, BWANA akaamsha roho yake Koreshi, mfalme wa Uajemi, hata akapiga mbiu katika ufalme wake wote, akaiandika pia, akisema, Koreshi, mfalme wa Uajemi asema hivi; "BWANA, Mungu wa mbinguni, amenipa falme zote za dunia; naye ameniagiza nimjengee nyumba katika Yerusalemu, ulioko Yuda."*
*Ezra 1:1-2*

Rais Harry Truman alitambua Israeli kama taifa mwaka 1948, Wayahudi ulimwenguni kote walimiminika wakirudi katika taifa lao lililoanzishwa upya. Je, hili linawezakuwa kisa cha Bwana kuamsha moyo wa rais?

Fungu letu linatuambia kwamba Bwana aliamsha moyo wa Koreshi, mfalme wa wapagani. Kushindwa kwa Yuda mwaka 586 KK kuliwafanya Wayahudi wengi wahamishwe kwenda Babeli. Yuda ilishindwa kwa sababu ya dhambi yake; kisha Koreshi, mfalme wa Uajemi, aliishinda Babeli. Lakini mwaka 538 KK, Koreshi alitoa amri ya kuwaruhusu watu wa Israeli warudi katika nchi yao na walijenge upya hekalu. Walirudi watu elfu arobaini na mbili.

Manabii walikuwa wametabiri kwamba Mungu angewarudisha watu wake katika nchi yao. Yeremia 32:37 inasema, "Nitawaleta tena hata mahali hapa, nami nitawakalisha salama salimini." Vivyo hivyo, Isaya 45:13, "Mimi nimemwinua katika haki . . . ataujenga mji wangu, naye atawaacha huru watu wangu." Ndiyo, Mungu ndiye anayeamsha mioyo, anayechochea mioyo hata ya watu wakuu—hata ya watu ambao bado hawamtumikii.

Ninamjua mwanamke mmoja ambaye biashara ya sasa ya mwajiri wake imeuzwa—sasa kuna chumba kipya cha maonyesho na kikubwa zaidi, mpango wa kukipanua, na mmiliki mpya. Punde, yule mfanyakazi atakutana na yule mmiliki mpya ili wajadili wajibu wake, saa, na mshahara. Marafiki zake wanaomba kwamba Bwana atauamsha moyo wa mmiliki mpya kumfanyia huyu mfanyakazi anayesemwa, kwa kumjali ya kumfanyia ifaavyo.

Siku moja Ijumaa asubuhi, nilikuwa na wanaume kumi na wawili katika maombi ya asubuhi ya wanaume. Wakati huo, nilikuwa ninahudumu kama

profesa wa uinjilisti katika Nazarene Theological Seminary. Mwanamume aliyekuwa amekaa karibu nami, makamu wa rais wa taasisi ya kifedha yenye sifa hapo mjini, aliinama kunielekea na akaninong'onezea, "Niko katika bodi ya hazina ya misaada, na tunataka kutoa pesa kwa ajili ya shughuli za Kikristo, hasa uinjilisti. Tuma ombi kwetu kwa ajili ya msaada wa masomo ya uinjilisti." Kisha akapanga miadi ya mimi kukutana na rais wa hiyo hazina. Mwishowe, kati ya dola nusu milioni na milioni za pesa za msaada wa masomo ulienda kwa wanafunzi wengi ambao leo wanawaleta watu wengi kwa Yesu Kristo. Kwa wakati huo sikuwa nimejitayarisha, lakini Mungu akaamsha moyo wa yule mwanamume aliyekaa karibu nami katika yale maombi.

Unahitaji kumwombea nani—ambaye Munga ataamsha moyo wake?

JULAI 2 — 183

# Mkristo Anapokuudhi

*Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakatifu, pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali, Bwana wao na wetu.*
*1 Wakorintho 1:2*

*Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa subira katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi katika mkono wa kulia wa kiti cha enzi cha Mungu.*
*Waraka kwa Waebrania 12:1-2*

Alipoandika waraka kwa kanisa la Korintho, Paulo aliwaita "waliotakaswa." "Waliotakaswa" ina maana mbili za kimsingi: kutengwa kwa ajili ya huduma takatifu; na kusafishwa au kufanywa safi. Lakini mambo hayakuwa sahihi sana kwa Wakorintho—vifungu vichache baadaye, Paulo, anaudhiwa na wao, anaomba "wala pasiwe kwenu faraka" (1 Wakorintho 1:10). Tunaweza kuliita tukio lao "utakaso wa kwanza"—hicho kiwango cha kutengwa na kusafishwa kunakofanyika wakati mtu anapookoka na kumkubali Kristo.

Lakini Wakorintho walihitaji kwenda ndani zaidi na kukabiliana na kujipenda wenyewe kuliko baki ndani yao. Paulo alipokabiliana na utakaso

wa ndani zaidi wa Wathesalonike, aliomba, "Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa" (1 Wathesalonike 5:23). Huu unaitwa "utakaso wote." Leo, wahubiri wanapoita watu watakaswe, kawaida humaanisha "utakaso wote." Ni wazi kwamba hilo ndilo walilohitaji Wakorintho, na kile wanachohitaji Wakristo wengi leo.

Jambo moja la kutatiza zaidi ambalo Mkristo anaweza kupitia ni wakati Mkristo mwenzake anamwudhi kwa machaguo ya kutojali ya mtindo wa maisha au kwa kumwacha Bwana. Hili lilitokea kwangu: Mwanamume niliyemchukulia kama mtu mcha Mungu zaidi, rafiki yangu mpendwa, na mtu niliyemtazama kwa ajili ya uongozi, alimwacha Bwana. Nilifadhaika, lakini nilijua kwamba Yesu Kristo alikuwa halisi sana kwangu hivyo basi *nisingeweza kumwacha* Bwana. Nilikaza macho yangu kwa Yesu na nikaendelea kupiga mbio katika mashindano.

Kwa miaka mingi, niliendelea kuwa na mawasiliano na huyu rafiki—alinambia nilikuwa mmoja wa wale wachache waliofanya hivyo. Miaka kadhaa baadaye, alimrudia Bwana na akaishi maisha nguvu yenye nyingi za kiroho na ushawishi.

Kama mtu amekuudhi, wewe endelea kumtazama Yesu—yeye hatakuangusha kamwe. Na badala ya kuweka usikivu wako wote kwa yule aliyeanguka, kwa nini usiwaangalie wale wanaosimama kweli? Hata hivyo, tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi.

JULAI 3 **184**

## Bwana Alikuwa Pamoja Naye

*Lakini BWANA akawa pamoja na Yusufu, akamfadhili,*
*akampa kibali machoni pa mkuu wa gereza.*
*Mwanzo 39:21*

Katika mkutano wa maombi wa wanaume, wa alfajiri, Kim aliripoti kwamba saratani yake ya utumbo mkubwa ilikuwa imeingia katika mapafu yake na ini. Alikuwa anawaza kushiriki katika kujaribu dawa ya majaribio. Lakini pia aliripoti, "Hivi ninavyohisi ndivyo vizuri zaidi nilivyowahi kuhisi katika miaka mitatu. Ninamshukuru Mungu kwa kila kitu. Maisha ni mazuri."

Mwanangu, Paul, baada ya kufanyiwa upasuaji mkubwa wa saratani mara tano kuanzia umri wa miaka thelathini na mitatu hadi thelathini na mitano,

alisema katika sauti ya kukwaruza, katika simu, “Baraka za Mungu zilikuwa juu yangu kabla ya saratani yangu. Baraka za Mungu zilikuwa juu yangu baada ya kutoa boksi ya sauti yangu. Baraka za Mungu ziko juu yangu leo.”

Mimi na mke wangu Nancy, tulipoingia katika kipindi cha kuhuzunisha zaidi maishani mwetu baada ya talaka ya binti yetu na mtindo wake wa maisha usiomcha Mungu, Mungu alinena nasi mara nyingi kupitia maneno ya wimbo ulitungwa na Steve Green unaoitwa “Watu Wanamhitaji Bwana”: “Mwisho wa ndoto zilizovunjika, yeye ndiye mlango ulio wazi.”

Rafiki yangu Tim aliripoti kutoka gerezani kwamba rafiki Mkristo “alinitembelea siku ileile nilipotazama video ya mazishi ya mamangu, ambayo ilikuwa na mihemko kwangu. Tena, huyu ndugu Mkristo, kupitia upendo na wakati wa Mungu, alikuwa hapo kunifariji. Watu wengine hilo wangeliita sadifa. Hilo mimi siliiti ajali. Upendo na wakati wa Mungu ni kamilifu. Gereza linaweza kuwa mahali pa upweke, lakini kupitia upendo wa Mungu nimekuwa nikikua kama Mkristo. Ijapokuwa uhuru wangu umefungwa na uzio wa waya wa wembe, nimekuwa nikijihisi kuwa mtu huru zaidi, na hilo ni kwa sababu nimejazwa upendo wa Mungu moyoni mwangu.”

Katika mahali pagumu sana maishani, Bwana atakuwa pamoja nawe. Kupitia mahali pagumu haimaanishi kwamba Mungu ametoka maishani mwako—anaweza kuwapo na halisi katika hizo sehemu ngumu.

Inafaa kukumbukwa kwamba katika Mwanzo 39:3, “Potifa . . . akaona ya kwamba Bwana yu pamoja na Yusufu, na ya kuwa BWANA anafanikisha mambo yote mkononi mwake.” Potifa alitambua hili wakati Yusufu alipokuwa mtumwa, ambalo kwa hakika ulikuwa wakati wa dhuluma na mgumu katika maisha ya Yusufu. Baadaye, Mwanzo 39:21 linathibitisha hili: “Lakini Bwana akawa pamoja na Yusufu kule gerezani na akamwonyesha upendo wake aminifu.”

Vivyo hivyo, Bwana anaweza kuwa *pamoja nawe* katika kila hali. Uwepo wa Bwana ulio hai ndilo jambo muhimu zaidi katika maisha yote.

# Kanuni ya Sekunde Mbili

*Hatimaye, ndugu zangu, mambo yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya heshima, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote, yatafakarini hayo.*
*Wafilipi 4:8*

Katika karibu miamsho mia tisa na kusafiri maelfu ya maili, nimekuwa na heshima ya kukaa katika nyumba nyingi na hoteli nyingi. Nikilala hotelini, lengo langu la kurudi chumbani kwangu baada ya kuhubiri jioni, kuomba na watu wanaomtafutaMungu, na kuwashauri wengine, lilikuwa ni kustarehe na kupumzika.

Katika hiyo miaka sitini na tano ambayo nimekuwa nikifanya hivi, ulimwengu wetu umeona mabadiliko na maendeleo mengi katika teknolojia. Wakati fulani katika maisha ya nyumbani mwetu, tulikuwa na TV ya kawaida iliyopokea idhaa sita au nane kupitia antena. Lakini nilikaa katika hoteli fulani, kwa mara ya kwanza, niliona idhaa za waya. Kwa nguvu za rimoti uliyoishika mkononi, ningeweza kuingia katika idhaa nyingi kwa muda mfupi. Vipindi vyangu nilivyopenda sana vya kunituliza vilikuwa michezo na vipindi vya wanyama. Kufikia mahali fulani, bila kupanga, niliona idhaa za waya ambazo zilikuwa ni za ngono. Ninasikitika kusema kwamba nilitazama baadhi ya hivi vipindi.

Wingu lilianza kushuka juu ya uhusiano wangu na Bwana. Wakati mmoja, nilihisi kama Bwana aliniambia, *Ukiendelea kufanya hivi, utapoteza roho yako.*

Mara moja nikaomba nisamehewe na nitakaswe. Nilijua mapitio yangu hayakuwa yanakubalika na kwamba lazima nichukue hatua ya wazi. Kisha nikaanzisha (na bado ninaendeleza) Sheria ya Sekunde Mbili: kama nikiona chochote chenye maudhui ya ngono kwenye TV, ni lazima nibadilishe idhaa katika sekunde mbili. Ni baraka iliyoje wakati huu kutumia rimoti!

Mtume Paulo asingejua kuwa kutakuwa na TV ya waya, mtandao, Facebook, rununu, au vifaa vingine vya kisasa ambavyo sasa vina uwezo wa kutuma video. Lakini alifahamu kwamba chochote kile kinachoshika macho au akili yako hatimaye kingeweza *kuiteka* akili yako, mapenzi yako, matendo yako. Kwa hivyo, akatengeneza orodha ya sifa—ya kweli, ya staha, sahihi, safi,

ya kupendeza—na akasema, “tafakarini hayo.” Chochote kile kinachoishika akili yako hukushika wewe—kwa hivyo kwa ajili ya roho yako, chagua yaliyo safi, yenye staha, na ya kweli. Katika vifungu vya awali (4:6–7), Paulo alitoa suluhisho la kuwa na wasiwasi. Ni wazi kwamba ni lazima kuna uhusiano kati ya kifungu cha 8 (maisha ya fikira) na kifungu cha 6 na cha 7 (kuishi bila wasiwasi).

Chaguo moja wapo bora zaidi nililowahi kufanya ni kutumia Kanuni ya Sekunde Mbili. Leo, ninaishi na kufurahi katika uhusiano na Mungu ambao ni mzuri zaidi, wa ndani zaidi, wa kuinua zaidi niliowahi kuujua. Asante Bwana! Je, unahitaji kuchukua Kanuni hii ya Sekunde Mbili au mkakati kama huo?

JULAI 5 **186**

# Hatuwezi Kuacha!

*Maana sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia.*
*Matendo 4:20*

Kwa nini Wakristo hawashuhudii zaidi? Katika zaidi ya semina 250 za Kushuhudia Bila Woga nilizofundisha, majibu mawili, maarufu zaidi ni haya yafuatayo:

- Watu wanaweza kunikataa.
- Sijui nitasema nini.

Yote, kwa sehemu, ni masuala ya woga. Lakini Petro na Yohana wanajulikana kwa ujasiri wao (Matendo 4:13).

Bado, kuna sababu nyingine kubwa kwa nini Wakristo hawashuhudii: Hawasisimki vya kutosha kuhusu yale Yesu aliyowafanyia.

Hobby alikuwa sehemu ya kanisa kwa miaka kadhaa, na akaishi kwa vigezo vyote, maisha mazuri na ya heshima. Lakini, kufikia umri wa miaka sitini, alimkaribisha Kristo moyoni mwake kwa njia ya uhusiano binafsi. Kwa mara ya kwanza, Mungu alikuwa halisi kwake.

Tulipoenda kufanya ununuzi pamoja kwa ajili ya ratiba ndogo za kanisa, alimchukua mwuzaji kando kabla sijamaliza ununuzi wangu. Baadaye, nilipomwuliza alifanya hivyo kwa nini, Hobby alisema, “Oo, nilipata nafasi ya kumwambia kile ambacho Mungu aliifanyia familia yetu.” Hobby alibubujika

tu. Au, kama Petro alivyosema, “Maana sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia” (4:20).[98]

JULAI 6 **187**

# Kudanganywa!

*Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa uongo.*
*Yohana 8:44*

Kwa siku moja, nimepokea simu tano:

- “Hujambo babu . . . Nimepata ajali na nipo katika kituo cha matibabu . . .”
- “Ununuzi wa $999 kwa ajili ya simu ya Apple umetozwa katika akaunti yako, isipokuwa ughairi . . .”
- “Ninapiga kwa niaba ya AT&T. Je, ungependa kupunguziwa bei?”
- “Ununuzi wa $599 kwa ajili ya simu ya Apple umetozwa kwenye akaunti yako . . .”
- “Je, ungependa kiasi chako ya mkopo kipunguzwe?”

Kama ningekuwa nimejibu simu yoyote katika hizi, nina hakika wangejaribu kuchukua taarifa zangu au wanifanye niahidi kitu fulani, hatimaye wangeniibia pesa zangu. Kila ombi linaonekana lenye manufaa kwangu, lakini yote ni uongo—mwisho wake siku zote ni wapate kitu chenye manufaa kwao, bila kujali hilo litaniumiza kwa kiasi gani.

Hili linanikumbusha juu ya jinsi Shetani anavyofanya kazi. Anatoa ombi, akipiga apate huruma yako au akuahidi manufaa fulani. Hana tatizo na kukudanganya. Mwisho wake, lengo lake ni kuiba, kuua na kuharibu (Yohana 10:10). Mwishowe utaumizwa, labda uachwe ukiwa na kauti yako ya benki imetolewa pesa zote au kadi yako ya mkopo imetumiwa yote.

Shetani anaweza kuwa mwovu—1 Petro 5:8 inasema, “Kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze.” Shetani anaweza kuonekana mzuri, hata mcha Mungu. Lakini

98. Awali kilichapishwa katika *Reflecting God* Juni–Julai–Agosti 2010 *(Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 24. Imetumiwa kwa ruhusa.*

2 Wakorintho 11:14 inatuonya, “Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru.”

Kwa hivyo, “Mwe na kiasi na kukesha” (1 Petro 4:7). Usimwache shetani akudanganye.

JULAI 7 **188**

# Kupunguza Pengo la Uwezo, Sehemu ya 1

*Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.*
*Yohana 14:12*

Kama umefuata siasa za Marekani na maisha ya kitamaduni katika miaka sitini iliyopita, yamkini umesikia kuhusu pengo la kombora, pengo la kuaminika, na pengo la kizazi. Ningetaka kupendekeza neno lingine—pengo la maadili. Lakini pengine pengo muhimu zaidi ni pengo la uwezo kanisani. Ni pengo kati ya yale aliyoahidi Yesu na uwezo unaodhihirishwa katika maisha ya Wakristo.

Yesu aliahidi kwamba wale waliomwamini yeye wangefanya kazi kubwa zaidi kuliko zile alizofanya. Ingawa kuna njia nyingi za kufasili ahadi yake, tunajua kwamba ingawa wafuasi wa Yesu walikuwa wanahesabika, Petro aliona maelfu wakiokolewa katika mahubiri yake, na Paulo alileta maelfu kwa Kristo kupitia makanisa aliyoanzisha.

Yesu anatoa funguo tatu za kufungulia uwezo huu wa kiroho:

1. Ufunguo wa Maombi: “Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya” (Yohana 14:13).
2. Ufunguo wa utiifu wa upendo: “Mkinipenda, mtazishika amri zangu” (14:15).
3. Ufunguo wa huduma ya Roho Mtakatifu: “Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele—ndiye Roho wa kweli” (14:16–17).

Nilitaka kupunguza pengo la uwezo katika maisha yangu. Katika mchakato huo Mungu alinifundisha hili somo moja: Nilipowaita watu kama mchungaji katika nyumba isiyojua kanisa, nilikutana na Clark. Alikuwa mkomavu sana, mkubwa, mwenye miraba minne hata nikafikiri yeye ndiye aliyekuwa baba

katika hiyo familia. Kumbe alikuwa mwana, na alicheza katika timu ya kandanda ya shule ya upili. Alianza kuja kanisani. Muda si muda, akamwona Bwana, akabatizwa, na akaungana na kanisa. Aliishi maisha yaliyong'aa na hata akaanza kuwaleta binamu zake kanisani. Baada ya masomo, akajiunga na jeshi na akapelekwa Ulaya. Sikumwona kwa miaka sita—niliwasiliana naye kwa barua. Alipokuja nyumbani, alikuja na msichana wa Kijerumani aliyeitwa Rhonda. Alikuwa mtafsiri, alikuwa akizungumza lugha nne kwa ufasaha. Walitaka kufunga ndoa.

Nikamwuliza Clark mahali alipokuwa kiroho. Akajibu, "Niko vizuri. Sifanye chochote kibaya. Ninafanya kila kitu ninachopaswa kufanya." Maneno yake yalikuwa baridi; mng'ao ulikuwa umeenda. Rhonda alinihakikishia alikuwa vizuri kwa sababu alikuwa mshiriki wa German State Church.

Baada ya ndoa yao, Clark na Rhonda walihudhuria Jumapili asubuhi ila hawakufanya kitu kingine chochote. Nikawasihi, nikaomba, na nikahubiri lakini sikupata mwitikio wowote. Katika wakati huo, mwinjilisti mmoja akaniambia, "Kama kwa kweli unataka kuwafikia watu, ni lazima uwazunguke na upendo na maombi." Hiyo ndiyo njia ya nguvu niliyohitaji ili Bwana afanye kazi kubwa zaidi.

Siku moja, nikapokea simu kuhusu kulazwa hospitalini kwa Rhonda. Walikuwa wanatarajia mtoto, lakini hakuumwa na uchungu—alikuwa anafanyiwa upasuaji wa tumbo.

Nikamtembelea Rhonda kule hospitali. Alikuwa amechanganyikiwa. Mtoto alikuwa azaliwe muda si mrefu, lakini asingeweza kuvumilia uchungu baada ya upasuaji. Ilionekana kama angefanyiwa upasuaji wa kutolewa mtoto usiokuwa umepangwa. Nilieleza kwamba Bwana alielewa hali yake, na nikapendekeza tuombe.

Kama Bwana hutembelea watu hospitalini, basi siku hiyo alimtembelea Rhonda katika chumba chake. Alitazama kutoka kwa maombi na akasema, "Mungu amekuja, Mungu amekuja" katika lafudhi yake ya Kijerumani. Nilipokuwa ninatoka kwenye kile chumba, akaita akisema, "Asante, asante, Mchungaji Shaver."

# Kupunguza Pengo la Uwezo, Sehemu ya 2

*Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.*
*Yohana 14:12*

Niliendelea kumzunguka Clark na Rhonda kwa upendo na maombi. Baadaye, niliporudi hospitali, nilimkuta Rhonda amekaa akipata mlo wa jioni wa kuku wa kukaanga mbele yake. Alikuwa amemzaa mtoto wake kawaida na alikuwa hana maumivu tena kabisa kutoka kwa upasuaji na kujifungua. Tulikubaliana kwamba ulikuwa muujiza.

Siku iliyofuata, huku nikiwa ninasoma katika ofisi ya kanisa, nilisikia kelele. Kule nje katika sebule ya kanisa, Clark alikuwa anajivunia mtoto wake binti. Tukafurahi pamoja. Kwa maombi nikarusha kitanzi kingine cha upendo na nikauliza, “Clark unaendeleaje kiroho?”

Akajibu, “Mungu kwa kweli hayuko vile alivyokuwa awali.”

Katika wakati huo, Roho Mtakatifu alinipa kipawa cha upambanuzi. Nilijua ni dhambi gani iliyokuwa imevunja uhusiano wa Clark na Mungu. Nikasema, “Clark, ninajua dhambi ni ipi, lakini nikikwambia, utanikasirikia.”

Akasema, “La, Mchungaji Shaver, Sitakasirika. Wewe ni rafiki yangu, kwa hivyo unaweza kuniambia.” Kwa hivyo nikaitaja dhambi yake.

Ghafla, mchezaji mkali wa kandanda akaangua kilio. Akasema, “Nimekuwa mbaya sana, nimekuwa ninaogopa kuomba.”

Sote tukaelekea madhabahuni kule kanisani. Huko, Clark akamwaga moyo wake na akamrudia Mungu. Kisha akasimama, akarusha ngumi hewani kwa nguvu, na akasema, “Sasa ninaamini mimi ni Mkristo halisi!”

Kisha mtazamo wa mshangao ukatokea usoni mwake. Akasema, “Lakini ni lazima nitoe fungu la kumi . . . lakini siwezi kumudu kutoa fungu la kumi . . . lakini ni lazima nitoe fungu la kumi.” Akabishana na yeye mwenyewe akisema hivi na vile. Mwishowe, ingawa alikuwa na malipo ya nyumba, malipo ya gari, na mtoto mchanga, Clark kwa furaha aliamua kutoa fungu la kumi. Nilipomwuliza kama ataenda kumwambia mkewe kile kilichofanyika kwake, alienda zaidi ya hilo na kusema, “Inanibidi nimwambie baba na mama.” Wazazi wake pia walihudhuria kanisani.

Aliposema hivyo, akatoka nje ya kanisa upesi, akaingia katika gari yake ndogo nyeusi ya michezo, na akaondoka mbio kwenda katika misheni yake.

Punde nikapigiwa simu nyingine. Mmoja wapo wa wanawake pale kanisani alikuwa amezungumza na Rhonda, aliyekuwa ameuliza, "Ni kitu gani kimefanyika kwa mume wangu? Jana usiku alikuja kuniona, lakini chumba changu kilikuwa kimejaa watu, hatukupata nafasi nzuri ya kuzungumza. Lakini anafanya mambo kitofauti, anazungumza kitofauti."

Niliposikia hili, nikarudi katika chumba cha Rhonda na kumwambia, "Clark amempata Bwana."

Rhonda akaanza kulia, akavuta shuka akajifunika uso wake, na kusema, "Oo, nimesitasita."

Jumapili iliyofuata, Clark, Rhonda, na mtoto wao wote walikuwa kanisani. Asubuhi hiyo Rhonda alipiga magoti madhabahuni kwa mara ya kwanza na akamkubali Yesu Kristo.

Wiki chache baadaye, Rhonda aliungana na kanisa kwa kukiri imani, na Clark akahakikisha tena viapo vyake vya mshiriki vilivyovunjika. Waliendelea kuishi maisha ya utumishi na uwezo wa kiroho.

Rhonda alimpata Kristo; Clark akaurudisha mng'ao wake na akajifunza kwamba, kwa kuwazunguka wengine kwa upendo na maombi, ningeweza kulipunguza hilo pengo la uwezo.

**JULAI 9** **190**

# Msaada Wangu Unatoka Wapi?

*Nayainua macho yangu niitazame milima, Msaada wangu utatoka wapi?*
*Msaada wangu hutoka kwa BWANA, Aliyezifanya mbingu na nchi.*
*Zaburi 121:1-2*

*Nafsi yangu yamngoja Mungu peke yake kwa utulivu, Wokovu wangu hutoka kwake. 2 Yeye tu ndiye mwamba wangu na wokovu wangu, Ngome yangu, sitatikisika.*
*Zaburi 62:1-2*

Sauli alipokuwa ameghadhibika, akiwa amedhamiria kumwua Daudi—

Waisraeli walipokuwa wanakimbia kutoka Misri, walifika Bahari ya Shamu, na wakatambua kwamba jeshi la Farao lilikuwa linawafuata—

Yoshua alipokuwa anajaribu kuwaongoza Waisraeli waingie katika nchi ya ahadi na walikabiliwa na mji wa Yeriko uliozingirwa na ukuta na ngome—

Paulo alipotiwa gerezani kwa kumhubiri Yesu—

—wote walipata msaada wao kutoka kwa Bwana.

Waisraeli walipoikataa ripoti ya Yoshua na Kalebu kuhusu nchi ya ahadi, hukumu ya Mungu iliwaangukia wale wapelelezi wengine kumi waliowavunja moyo Waisraeli wasiingie hiyo nchi. Baada ya hiyo hukumu, Waisraeli waliamua kuingia nchi ya ahadi na waichukue, lakini Musa akawaonya, "Msikwee, kwa kuwa BWANA hayupo kati yenu. Msipigwe na kuangushwa mbele ya adui zenu" (Hesabu 14:42). Kwa hakika, katika kiburi chao, Waisraeli walishindwa (kif. cha 44–45).

Kwa sababu uchaguzi unaofanywa na wengine, mimi ni raia wa Marekani, ambayo ina sifa ya kuwa taifa lililoendelea zaidi katika historia ya ulimwengu. Tuna ustadi mkubwa wa kiufundi, mfumo wa kimatibabu wa kipekee, nguvu kubwa ya kifedha, nafasi kubwa za elimu, na nafasi za kuendelea kisayansi. Lakini, kufikia wakati nilipokuwa ninaandika hili, kirusi hatari cha korona kilichoanza Disemba 2019 kilienea kote ulimwenguni. Shule zilifungwa, biashara zikafungwa, watu wakapoteza kazi, soko la hisa likaporomoka, na watu wengi ulimwenguni walikumbwa na kufungiwa na karantini.

Nina simu ya Apple iPhone. Kwa kunena na hiyo simu kwa maneno, "Hey, Siri," ninaweza kupata majibu ya kila aina ya maswali. Kufikia sasa, imenambia kiwango cha joto cha leo; hali ya hewa ya kesho; majira ya ligi kuu ya Beziboli yatakapoanza; njia nzuri kutoka Naples, Florida, kurudi jiji la Kansasi; na hata jinsi ya kutaja tahajia za neno, "kirusi cha korona." Ni nzuri sana kiasi kwamba niliamua kuiuliza, "Hey, Siri, tiba ya kirusi cha korona ni ipi?"

Ikajibu kwamba, kwa sasa, "hakuna tiba ya kirusi cha korona."

Mungu, katika rehema zake, aliwapa baadhi ya wanasayansi wazuri sana maarifa ya kutengeneza chanjo ambayo ilianza kutolewa mapema mwaka 2021, na labda tiba ya hakika zaidi iko upeoni. Lakini juu ya mambo mengine yote, ni lazima tukumbuke kuwa, hata tufikiri kuwa sisi ni werevu au tuna uwezo wa namna gani, kuna matatizo ambayo hatuwezi kuyadhibiti au kuyatatua—hatupaswi kabisa kudhania tunaweza kuvifanya peke yetu.

Basi "msaada wangu unatoka wapi? Msaada wangu u katika Bwana." Kwa kweli kama mtunzi wa zaburi anavyoandika, "Kweli yeye tu ndiye mwamba wangu na wokovu wangu, Ngome yangu, sitatikisika sana."

# Musa Akakimbilia Midiani

*Basi akatazama huku na huko, na alipoona ya kuwa hapakuwapo mtu, akampiga na kumwua Mmisri yule, akamfukia mchangani.*
*Kutoka 2:12*

Kwa upanga wake alikuwa ameua watu kumi na wawili. Lakini sasa Gikita, mtu wa kabila ya Huaorani ya kule Ekwado, alikuwa hana furaha kwa sababu ya aliyofanya zamani. Hakuwa amefanya mambo mazuri. Sasa kwa kuwa alikuwa amemjua Mungu, machoni mwake mlikuwa na machozi.

Siku zilizopita, ghadhabu yake ilimfanya aongoze mashambulizi dhidi ya wamishenari watano kule Palm Beach. Katika hayo mashambulizi, Nate Saint alikuwa ameuawa. Lakini sasa, dadake Nate, Rachel, alisikia huo ushuhuda wa nguvu—Gikita alikuwa anawaongoza Wahuaorani wengine kwenda kwa Kristo.

Hii haikuwa mara ya kwanza Mungu kusababisha "ghadhabu ya mwanadamu . . . kumsifu" yeye (Zaburi 76:10). Musa, aliyekuwa amemwua Mmisri, alikutana na Mungu kule Midiani. Kule Misri, alikuwa amejaribu kusahihisha udhalimu kwa kuchukua sheria mikononi mwake. Lakini baada ya kukutana na Mungu mtakatifu, Musa alikomaa kwa miaka arobaini katika nchi ya ugenini. Kufikia wakati Mungu alikuwa amemaliza kumtayarisha, Musa angefanya zaidi sana kuliko kumwokoa Mwebrania mmoja kutoka kwa Mmisri mmoja kwa nguvu za mkono wake mwenyewe—sasa, angeokoa taifa zima kutoka katika utumwa kwa nguvu za mkono wa Mungu unaofanya kazi kupitia kwake.

Je, ushaona hilo? Mungu anataka kuchukua kushindwa kwako kwa zamani, dhambi—naam, hata ghadhabu yako—na atoe kiumbe kipya atakayemletea sifa.[99]

---

99. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Julai–Agosti–Septemba 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 13. Imetumiwa kwa idhini (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

# Inafaa

*Urefu wa kila pazia ulikuwa ni dhiraa ishirini na nane, na upana wa kila pazia ulikuwa ni dhiraa nne; mapazia yote yalikuwa ya kipimo kimoja. Naye akaunganisha mapazia matano hili na hili; na mapazia matano mengine akayaunganisha hili na hili. Kisha akafanya matanzi ya rangi ya buluu katika ncha za pazia moja, katika upindo wa kiungo chake; akafanya vivyo hivyo katika ncha ya pazia lililokuwa upande wa nje katika kiungo cha pili. Akafanya matanzi hamsini katika pazia moja, na matanzi hamsini katika upindo wa pazia lililokuwa katika kiungo cha pili; hayo matanzi yalikuwa yakabiliana hili na hili. Kisha akafanya vifungo hamsini vya dhahabu, na kuyaunganya hayo mapazia hili na hili kwa vile vifungo; hivi ile maskani ilikuwa ni moja.*
*Kutoka 36:9-13*

Kuna nafasi gani ambazo ungetengeneza pazia zenye urefu wa futi arobaini na mbili na upana wa futi sita, uweke matanzi hamsini katika kila moja, uunganishe tanzi na tanzi na vifungo hamsini vya dhahabu, na uvifanye *vyote viingiane*? Inashangaza kama Mungu kuwaita wanaume kumi na wawili kwa majina kutoka katika wanaume wengi watu wazima wa idadi ya zaidi ya elfu mia sita wasaidie kuwahesabu watu (tazama Hesabu 1:5–7).

Kwa nini aeleze bayana maelezo ya kina ya ujenzi changamani namna hii? Mungu mtakatifu aliyekuwa ametoa amri kumi takatifu sasa anatoa maagizo kwa ajili ya hema takatifu litakalojengwa na wafanyakazi watakatifu. Naam, Mungu aliwachagua kwa kuwaita majina hata wale wafanyakazi: "BWANA amemwita kwa jina lake Bezaleli . . . naye amemjaza roho ya Mungu, katika hekima, na akili, na ujuzi, na kazi ya ustadi kila aina" (Kutoka 35:30–31).

Musa anapokuwa anaunda hilo hema, matini inatwambia, "Musa akafanya hayo yote; kama yote BWANA aliyoagiza ndivyo alivyofanya" (40:16). Hatua kwa hatua, utiifu unawekewa mkazo, na kirai "kama yote BWANA aliyoagiza ndivyo alivyofanya" inaonekana katika Kutoka 40:19, 21, 23, na 25.

Tunaona utiifu wa Musa na wale wafanyakazi unaojitokeza bila kutajwa, kwa maagizo ya Mungu yaliyo wazi, ambamo hata maelezo ya ujenzi ni muhimu. Hata matanzi hamsini na vifungo hamsini—vyote vinaingiana.

Mchungaji wetu wakati mmoja alitoa kielezo kifuatacho: “Je, umewahi kujaribu kufunga vifungo vya sweta au shati baada ya kupata kifungo cha kwanza katika tundu lisilokuwa lake? Kufikia wakati unapofikia kifungo cha mwisho, unatambua hakuna mahali pa hicho kifungo cha mwisho—hakifai hapo.” Alisisitiza kwamba uhusiano wetu sahihi na Yesu Kristo ndio msingi wa vipengele vyote vya maisha kuweza kuingia katika mahali pake sahihi. Mchungaji alipokuwa bado anazungumza, msichana mmoja aliyekuwa mpya katika kanisa letu aliinamisha kichwa chake kwangu na kusema, “Nafikiri nina kifungo kisichoingia.” Huyo msichana na mumewe baadaye walimtafuta Kristo.

Fikiri—kama Mungu aliweza kuongoza wafanya kazi watengeneze mapazia hata matanzi hamsini ya “pazia ya kwanza” yalikutana kikamilifu na matanzi hamsini ya “pazia ya pili,” na yote yakashikiliwa pamoja na vifungo hamsini vya dhahabu—anaweza kufanya nini katika maisha yako uliyoyatoa kwake? Yeye peke yake ndiye anayeweza kuyafanya yafae.

JULAI 12 **193**

# Miujiza Katikati ya Uovu

*Ahabu mwana wa Omri akafanya yaliyo mabaya machoni*
*pa BWANA kuliko wote waliomtangulia.*
*1 Wafalme 16:30*

*Neno la BWANA likamjia, kusema, Ondoka hapa, geuka, uende upande*
*wa mashariki, ujifiche karibu na kijito cha Kerithi kinachokabili Yordani.*
*Itakuwa utakunywa maji ya kile kijito; nami nimewaamuru*
*kunguru wakulishe huko.*
*1 Wafalme 17:2-4*

Majeshi mabaya ya Nazi yaliivamia nyumba ya Mdachi mmoja na familia yote wakaitia korokoroni. Uhalifu wao ulikuwa nini? Walikuwa wakiwaficha Wayahudi katika vyumba vyao vya siri mle nyumbani mwao ili wawaokoe dhidi ya mateso.

Muda si muda katika kambi ya mateka, Corrie ten Boom akajua kuwa babake alikuwa amekufa katika jela. Baadaye aliomwona dadake Betsie akifa. Corrie peke yake ndiye aliyenusurika. Je, kungeweza kuwa na muujiza wowote katikati ya uovu kama huo?

Uovu wa aina hiyo ulikuwa umefanyika awali—Ahabu anashikilia rekodi ya kuwa mfalme wa Israeli mbaya zaidi. Kama jibu la huo uovu, Mungu alimtuma mwakilishi wake Eliya kutangaza hukumu ya ukame wa muda mrefu. Katikati ya huo uovu, ukame, na mateso, Mungu alifanya muujiza. Alimhifadhi huyo nabii na akamtuma aende Kijito cha Kerithi, ambako angekunywa kutoka kwa kile kijito. Mungu aliwaamuru kunguru wamlishe Eliya asubuhi na jioni.

Miezi ikapita, na hakukuwa na mvua. Kijito kikakauka, na Mungu akachukua hatua tena kwa ajili ya Eliya kwa kumpeleka kwa mjane kule Sarepta. Eliya alipomwomba yule mjane maji kidogo na mkate, alieleza kwamba alikuwa na unga na mafuta ya kutosha kutengeneza chakula cha mwisho chake yeye na mwanawe—baada ya hilo, wangekufa kwa njaa. Eliya alimhakikishia unga wake usingepungua na mafuta yake yasingeisha mpaka mvua inyeshe. Kwa hakika kabisa, kulikuwa na chakula kila siku kwa ajili ya Eliya na familia ya yule mjane—muujiza mwingine.

Baadaye mwana wa yule mjane aliposhikwa na ugonjwa na kufa, Eliya alimwombea yule mvulana, na Mungu akamfufua. Ni miujiza! Ufunguo katika maisha ya Eliya ulikuwa, "Basi akaenda akafanya kama alivyosema Bwana" (17:5). Naam, hata katikati ya uovu na hukumu, Mungu anaweza kuingilia kati kwa njia maalum kwa wale walio wake.

Jinsi walivyofanyiwa Corrie na dadake Betsie katika gereza la kambi ya Nazi lingeweza kukufanya ulie. Lakini hata hapo, waliona miujiza. Betsie alikuwa mgonjwa, na Corrie akampa dawa kutoka kwenye chupa ndogo ya vitamini za maji kila siku. Lakini wengine pale kambini pia walikuwa wagonjwa. Punde, wanawake kumi na wawili walikuwa wanainywa; punde, ishirini na watano. Lakini, kila wakati Corrie alipotikisa hiyo chupa, tone lingine lilitokea. Alisema ilikuwa kama yule mjane wa Sarepta.[100]

Hata katikati ya kufungwa kwao gerezani, Corrie na Betsie walimshukuru Bwana kwa mambo yote. Kufikia mahali fulani, hawekuweza kuelewa ni kwa nini walinzi walikuwa wameacha kuja chumbani mwao—muda si muda wakajua ni kwa sababu kitanda chao na chumba chao kilikuwa kimejaa viroboto. Na kwa hiyo, wakamshukuru Mungu hata kwa wale viroboto.

Wale madada kumi wa familia ya ten Boom wakajifunza kuwa hakuna shimo lenye kina kirefu sana ambalo Mungu hayupo humo. Kabla ya kufa kule gerezani, Betsie aliona maono ya nyumba nzuri ambapo wangehudumia

---

100. Corrie ten Boom, Elizabeth Sherrill, na John L. Sherrill, *The Hiding Place* (Washington, CT: Chosen Books, 1971), 184.

watu wanaoteseka baada ya vita. Akamwambia Corrie, “Ni lazima tuwaambie [watu] kile tulichojifunza.”[101]

Kimiujiza, baadaye Corrie aliachiliwa kutoka katika kambi ya mateka kwa sababu ya kosa la kikarani. Kule Uholanzi, tajiri Bi. de Haan alimpa Corrie nyumba yake kama mahali pa kuhifadhi watu walionusurika kule kambini.

Aliposikia hilo, Corrie alianza mara moja kueleza hivyo vitu vilivyo katika hiyo nyumba. “Basi umekuwa hapa!”[102] Bi. de Haan akasema kwa mshangao.

Corrie alikuwa hajawahi kuwa pale—lakini alijua kutoka kwenye maono ya Betsie vile ilivyokuwa. Nyumba hiyo ya vyumba hamsini ya vinne muda si mrefu ikawa inawahudumia watu wengine.

Baadaye, katika ibada ya kanisa kule Munichi, Corrie alikutana na mmoja wapo wa waliokuwa walinzi wake kule gerezani. Akijua kwamba asingeweza kufanya hivyo kwa nguvu zake mwenyewe, alimwomba Yesu amsaidie kumsamehe. Baadaye Corrie alitoa ushuhuda ambao ulikuwa kama mkondo wa umeme uliopitia mkononi mwake, na upendo ukachipuka katika moyo wake kwa ajili ya yule mwanamume aliyekuwa amemtesa yeye na familia yake.[103]

Corrie alianza kuwaambia watu yote ambayo Mungu alikuwa ameyafanya. Kufikia umri wa miaka themanini, alikuwa amefanya kazi na kufundisha katika nchi sitini na moja.[104] Kitabu chake cha mwaka 1971 *The Hiding Place* na kugeuzwa filamu kwake kulikofuata kulieneza uwezo wa msamaha kwa mamilioni wengi zaidi.

Katika hadithi ya Corrie ten Boom, katika hadithi ya Eliya, katika hadithi ya Mungu—tunaona miujiza katikati ya uovu.

101. Ten Boom, Sherrill, na Sherrill, *The Hiding Place*, 211.
102. Ten Boom, Sherrill, na Sherrill, *The Hiding Place*, 213.
103. Ten Boom, Sherrill, na Sherrill, *The Hiding Place*, 215.
104. Ten Boom, Sherrill, na Sherrill, *The Hiding Place*, 219.

# Mambo Chanya Kutoka katika Maradhi ya Ubongo ya Kupoteza Kumbukumbu (Alzheimer's)

*Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno.*
*Yakobo 1:2-4*

Siku moja, mimi na mke wangu, Nancy tulikula mlo wa mchana pamoja. Kisha, kama saa moja baadaye, akaniuliza, "Je, unataka nikutengenezee mlo wako wa mchana?" Inahuzunisha hakuweza kukumbuka tulikuwa tumekula tayari.

Changamoto zaidi zikaanza kuongezeka. Akaja nyumbani na kuniambia, "Mpenzi, nimeacha vyakula vyangu kwenye kijigari cha ununuzi kule dukani bila kuvilipia. Sikuweza kuipata kadi yangu ya mkopo." Siku tano baadaye, tukaipata hiyo kadi ya mkopo nyumbani mwetu.

Mke wangu amekuwa akiugua maradhi ya ubongo ya kupoteza kumbukumbu (Alzheimer's) kwa kama muongo mmoja sasa. Hata ingawa tumekuwa tukikumbwa na mambo magumu, pia tumepata matukio chanya katika kukabiliana na huu ugonjwa.

Yakobo anazungumza kuhusu majaribu. Baadhi ya majaribu yetu yanaweza kuwa mateso kwa sababu ya imani yetu; mengine yanaweza kuwa tu changamoto zinazokuja na akili zetu au miili yetu kuisha. Vivyote vile, matokeo yanaweza kuwa majaribu ambayo hujaribu imani yetu, ambayo huleta saburi, ambayo huleta ukomaavu. Lakini havifanyiki tu vyenyewe—tunaamua. Yakobo anasema, "Saburi na iwe na kazi kamilifu."

Nimeangalia ninavyokuwa na mwelekeo wa kutokuwa mvumilivu kuwa ndio udhaifu wangu mkubwa zaidi wa maisha yangu ya Kikristo. Unajua nini? Matukio mengi yaliyoletwa na maradhi ya ubongo ya kupoteza kumbukumbu (Alzheimer's) katika familia yetu yananifundisha uvumilivu ambao sikuujua awali. Ninaamini ninakomaa.

Hapa kuna mawazo ambayo yamenisaidia:

1. Maneno yake au vitendo vyake vinatoka katika akili iliyoharibika.
2. Hakusudii kuniumiza.

3. Tunanena kwa uhuru kuhusu hali yake na tunaweza kuchekelea mambo mengine pamoja.
4. Nina heshima ya kuishi kiapo changu cha ndoa "katika ugonjwa na afya, kwa mazuri au kwa mabaya."

Mara ya kwanza Nancy alipokuwa mgonjwa wa maradhi ya ubongo ya kupoteza kumbukumbu (Alzheimer's), alifadhaika, akakasirika, akawa na wasiwasi, na akagadhibika (ambayo ilikuwa tofauti kabisa na kawaida yake). Nilipokuwa ninajaribu kumwelekeza, akanikatiza, "Unajaribu kunisimamia katika kila kitu."

Nikasema, "Ndiyo, ninafanya hivyo kwa sababu unapitia matatizo yanayohitaji usaidizi maalum."

Tukaanza kufanya kazi pamoja kushughulikia ugonjwa wake. Kupitia madaktari wazuri, vyama vya maradhi ya ubongo ya kupoteza kumbukumbu (Alzheimer), madawa, maombi ya watu, na neema ya Mungu, mambo yamebadilika kwa ajili ya wema. Huo ugonjwa haujawa na nafuu—bado unaendelea—lakini mwitikio wetu kwake umekuwa bora.

Kama mwaka mmoja na nusu uliopita, mimi na Nancy tulikuwa tumelala kitandani, tukishikana mikono na kuzungumza tu. Nancy akasema, "Nafikiri ninafuraha zaidi kuliko nilivyowahi kuwa. Na ninakupenda zaidi kuliko nilivyowahi kupenda!"

Waa! Hiyo ni kweli kabisa. Tunakuwa na baadhi ya siku tamu zaidi za ndoa yetu. Ninaamini majaribu yananifanya mimi niwe Mkristo bora zaidi.

Unakabiliwa na majaribu gani?

**JULAI 14** **195**

# Watu Wawili na Roho Mtakatifu Mmoja

*Wakati Simoni alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, "akataka kuwapa fedha akisema, Nipeni na mimi uwezo huu, ili kila mtu nitakayemweka mikono yangu, apokee Roho Mtakatifu."*
*Matendo 8:18-19*

*Roho akamwambia Filipo, "Sogea karibu na gari hili, ukaribiane nalo."*
*Matendo 8:29*

"Siendi kanisani kwa sababu huko kuna wanafiki wengi sana" ni kisingizio kilichoenea katika jamii ya leo. Unajua nini? Ni kweli—kuna wanafiki kanisani. Biblia inakiri hili; kwa kweli, Biblia iko wazi kabisa kuhusu hili, kiasi kwamba inawaeleza baadhi ya wanafiki kama Simoni. Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kwamba wajibu wetu kwa wanafiki si kujiepusha na kanisa, bali *upambanuzi* kuhusu wale walio kanisani.

Katika Matendo 8:9–40 (ambayo ninapendekeza usome), watu wawili wanahusishwa. Wote wanavutiwa na huyo Roho Mtakatifu. Unaposoma simulizi ya Matendo, unaweza kutambua mkweli ni nani na mwongo ni nani. Piga kura yako kwa watu wakweli.

Hili fungu limejaa masomo muhimu:

- "Na yeye Simoni mwenyewe aliamini akabatizwa" (8:13). Anaweza kuwa aliamini ukweli fulani kuhusu Yesu, lakini hakujitoa kwake kwelikweli. Ubatizo hauwezi kukuokoa.
- Simoni alipowaona wale mitume wanawapa waumini wapya Roho Mtakatifu, akataka kuwapa pesa ili aununue huo uwezo. Peter akamkemea Simoni na akamwambia moyo wake haukuwa mnyofu mbele ya Mungu. Akamwambia Simoni atubu huo uovu wake, kwa kuwa alikuwa amejaa "uchungu kama nyongo, na tena u katika kifungo cha uovu" (8:21–23).
- Kisha Simoni akasihi aombewe ili apate kulindwa na hukumu (8:24). Nia ni muhimu kwa Mungu, na ni wazi kwamba Simoni alitaka Roho kwa ajili ya utukufu wake mwenyewe; alitaka kumtumia huyo Roho.
- Filipo ni mshiriki kiongozi mcha Mungu, na mmoja wa wale waliochaguliwa katika bodi ya kanisa la kwanza. Mitume walikuwa wamesema wachague wale pekee "walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima" (Matendo 6:3, 5). Hili fungu linatofautisha kati ya waumini waliojazwa Roho, na waumini ambao hawajajazwa Roho—ni Wakristo "waliojazwa Roho" peke yake ndio waliokuwa wanaweza kuchaguliwa katika hii nafasi.
- Filipo alikuwa amejazwa Roho na alikuwa anaongozwa na Roho (8:29). Roho alimtumia.
- Filipo alimwongoza yule Mkushi kwa neema inayookoa katika Kristo (8:38). Ushuhuda wake binafsi uliongozwa na Roho.
- Filipo alitegemea uwezo wa Roho katika maisha yake ili aweze kuwasaidia wengine na kumtukuza Mungu.

Simoni na Filipo, wote wawili walivutiwa na huyo Roho Mtakatifu. Mmoja alikuwa sahihi; na mwingine alikuwa amekosea. Wote waliacha urithi.

Katika hadithi ya Simoni, tunaona dhambi ya simoni—kutoa pesa ili apate kuchaguliwa katika cheo cha nguvu cha kidini.

Filipo alimwongoza yule Mkushi kwa Kristo. Huyu mwanamume alikuwa katibu wa hazina ya malkia wa Kushi (8:27), na huyo mtu akapeleka Ukristo Kushi. Miaka elfu moja mia kenda baadaye, katika Mkutano wa Uinjilisti wa 1966, kule Berlini, Ujerumani, Mfalme Haile Selassie wa Ethiopia alitoa hotuba ya ufunguzi na akamkiri Kristo kama Mwokozi wake.

Unataka nini kwa Roho Mtakatifu? Je, utaacha kumbukumbu gani?

JULAI 15 **196**

# Mkushi

*Naye akaondoka, akaenda; mara akamwona mtu wa Kushi, towashi, mwenye mamlaka chini ya Kandake malkia wa Kushi, aliyesimamia hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu.*
*Matendo 8:27*

*Je, hili linamaanisha vile ninavyofikiri?*

Ndiyo, "towashi" maanake ni mwanamume aliyehasiwa.

Hawa wanaume mara nyingi walihudumu kama watunzaji wa nyumba za harimu, na mara nyingi walipanda na kupata vyeo vikuu vya serikali. Kwa sababu yule Mkushi alikuwa towashi, asingeweza kujua furaha za ndoa, asingeweza kupata watoto wala wajukuu. Labda alikuwa mtumwa. Hali yake ya kimwili alifanyiwa bila kutaka; halikuwa chaguo lake. Ijapokuwa alikuwa ameenda katika hekalu la Wayahudi, asingeweza kuwa mshiriki kamili wa Dini ya Kiyahudi. Hiyo ilikuwa nafasi iliyoje ya kuhisi uchungu.

Hivyo ndivyo Lisa alivyokuwa—alikuwa amepitia talaka haribifu kabisa ambamo mumewe alimwacha na kiti kimoja na watoto wawili. Alitembelea kanisa Jumapili, na katika muda wa wiki moja, kanisa lilikuwa limempa samani—alisema hata rangi ilikuwa nzuri. Lisa alisema, "Mungu amekuwa mwema sana. Ninaweza kuhisi mikono yake ikinikumbatia. Je, ningekuwa nimeagizia hili? La—lakini Mungu analitumia."

Lisa na yule Mkushi, wote wawili walichagua: badala ya kuwa na uchungu, wangeendelea kuwa bora zaidi.

Mkushi alikuwa na changamoto nyingine. Yeye alikuwa katibu wa hazina ya malkia wa Kushi, jambo linalomaanisha kuwa alisimamia pesa nyingi

zaidi kuliko mtu yeyote katika hilo taifa. Angekuwa amefikiri, "Nimefika," na akawa na majivuno. Angekuwa ameshikana na mfanyabiashara wa Yerusalemu ambaye alikuwa rais wa kampuni yake mwenyewe na kusema, "Nilikuwa na shughuli nyingi sana kutafuta riziki, sikuwa na wakati wa kuwa na maisha." Huyo mfanyabiashara na huyo Mkushi waliamua kuwa kiburi na cheo havitoshi; wangemtafuta Mungu.

Yule Mkushi alikuwa ametafuta—alikuwa amesafiri kutoka Kushi, hadi Yerusalemu, kwenye hekalu la Wayahudi apate kuabudu. Alipokuwa njiani kwenda nyumbani, aliegesha gari lake la farasi katika Ukanda wa Gaza, na alikuwa anasoma Agano lake la Kale. Bado moyo wake haukutosheka.

Lakini Mungu alikuwa anamtaka huyo Mkushi. Mungu akamtuma malaika wake kwa yule mshiriki aliyejazwa Roho, Filipo ateremkie hiyo njia ya jangwani kutoka Yerusalemu kwenda Gaza. Roho akamwambia Filipo, "Sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo" (Matendo 8:29).

Mkushi na Filipo wakaaza mazungumzo. Filipo alipomwuliza yule Mkushi kama alikuwa anaelewa hilo fungu alilokuwa anasoma, akajibu, "Nitawezaje . . . mtu asiponiongoza?" (8:31) Jibu lake linadokezea wazi hitaji la kuwa na shahidi.

Filipo alimwongoza yule Mkushi kwa Kristo, na akambatiza. Yule mwongofu mpya alifurahi alipokuwa anaendelea na safari yake ya kurudi Kushi, ambako angeeneza ujumbe wa Kristo.

Si uchungu wala kiburi kingeweza kumzuia yule Mkushi—wala visikuzuie wewe.

**JULAI 16** **197**

# Usiwe na Tashwishi katika Giza na Kile Ambacho Mungu Amekwambia Katika Nuru

*Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*
*Matendo 28:20*

Marsha alikuwa na ugomvi mkubwa na mchumba wake. Alikuwa analia alipokuwa anaendesha gari kupitia mjini ili aepukane na hilo kabisa. Kisha akakumbuka kifungu kilichojitokeza kwake katika darasa lake la shule ya

Jumapili: “Msihuzunike; kwa kuwa furaha ya BWANAni nguvu zenu” (Nehemia 8:10). Marsha akajituliza na akaendesha gari akaenda nyumbani.

Sote tutakumbana na mahali penye giza maishani. Unapotafuta kukabiliana na changamoto kama hizo na hekima, kumbuka kile Mungu amekwambia, amekuonyesha, amekuongoza, katika wakati wako mzuri zaidi na yeye. Ukweli mkuu zaidi unaodumu kutuendeleza ni ahadi ya Yesu Kristo aliyefufuka, kwa wanafunzi wake: “Mimi nipo pamoja nanyi siku zote.” Hii ni zaidi ya kauli ya kweli—anaahidi uwepo binafsi kwa wote wamfuatao.

Hata saa iwe na giza namna gani, ushindi wako wote wa zamani pamoja na Bwana na kwa Bwana unaweza kuwa ngazi yako ya kupata ushindi mpya. Ushindi wa waumini wengine unaweza pia kukutia moyo. Yoshua alipokabiliana na changamoto kubwa zaidi za maisha yake—kuongoza Waisraeli milioni mbili wavuke Mto Yordani na waingie nchi ya ahadi—Bwana alimpa ahadi: “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe; sitakupungukia wala sitakuacha” (Yoshua 1:5).

Ni nyakati gani ambazo Mungu alikuonyesha nuru? Pengine zinajumuisha baadhi ya zile zifuatazo:

- Mungu alipokuokoa na kukupa maisha mapya (2 Wakorintho 5:17)
- Mungu alipokutakasa kabisa na kukupatia moyo safi (1 Wathesalonike 5:23)
- Mungu alipokuokoa dhidi ya hitaji kubwa la kifedha (Wafilipi 4:19)
- Mungu alipokuongoza ulipokuwa unafanya uamuzi mkubwa (Zaburi 32:8)
- Mungu aliposuluhisha uhusiano uliokuwa unatatiza (Wafilipi 4:2)

Baadhi ya nyakati zangu mbaya zaidi zimekuwa wakati babangu alipoacha kunipa fedha kwa sababu nilikuwa nimekuwa Mkristo; wakati gari ilitugonga upande tulipokuwa tunapita mahali njia zilipokutana na kulikuwa na taa ya kijani; wakati binti yetu alipomwacha mumewe na Bwana; nilipopokea kura pinzani nilipokuwa ninaitwa tena kama mchungaji wa kanisa; Mke wangu aliposhikwa na maradhi ya ubongo ya kupoteza kumbukumbu (Alzheimer’s); na mwanangu alinambia kuhusu upasuaji wa tano wa saratani, wakati huu wa kukata kitoa sauti . Lakini, katika kila kisa, tulitumia zana ambazo Mungu alikuwa ametupa aliposema nasi katika nuru. Matokeo yake, tuliyapitia yote na ushindi wake mpya.

Mwana wetu aliposema kwamba sehemu yake ya kutunzia sauti ingeondolewa, tulienda Wafilipi 4:6–7. Papo hapo, amani ya Mungu ikashuka juu yangu kule Mississippi; juu ya mke wangu Nancy, kule Leawood, Kansas; na juu ya mwana wetu kule Muncie, Indiana. Na haikuondoka kamwe—sote tunaishi katika baraka ya leo.

Kumbuka kile ambacho Mungu amekwambia Katika Nuru!

JULAI 17 — 198

## Kwa Wale Wanaomtii

*Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wanaomtii.*
*Matendo 5:32*

Waumini wanaweza kuona kina kikubwa cha maisha ya Kikristo kama wanavyotamani. Baadhi wanaweza kuishi katika kiwango cha dakika tano za maombi kila siku: "Oo Mungu, wabariki watoto wangu na ufanye hii siku iwe ya kupendeza."

Kuna wengine wanaoenda katika viwango vya kina na Mungu. Mamake Mama Chiang Kai-shek alitumia wakati mwingi sana na Bwana, kwa mfuatano, kiasi kwamba alikuwa ukimtaka ushauri, angesema, "Ni lazima ungojee mpaka kesho ili niweze kumwuliza Bwana yote kuhusu hilo, na nipate mwongozo wake."[105]

Wale wafuasi wa Yesu 120 waliungana katika maombi ya kila mara kwa siku arobaini, na siku ya Pentekoste, wote wakajazwa Roho Mtakatifu (Matendo 1:3, 15; 2:4). Matokeo yake, vuguvugu la kiroho lenye uwezo lilitapakaa Yerusalemu yote. Watu wengi zaidi walimwamini Bwana, na wengi wakaponywa. Mamlaka ya Wayahudi, walijawa na wivu, waliwashika na kuwatia wanafunzi gerezani.

Siku iliyofuata, wanafunzi waliitwa mbele ya Sanhedrin, na kuhani mkuu akawaamuru waache kufundisha kuhusu Yesu. Petro akajibu, "Petro na mitume wakajibu, wakisema, Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu" (Matendo 5:29). Kwa mara nyingine akamhubiri Yesu kwa viongozi.

Kisha Petro akaongeza, "Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtiio" (5:32).

Wanafunzi walikuwa mashahidi wa Yesu aliyefufuka na ushahidi mwingine mwingi. Zaidi ya hayo, Mungu Baba alikuwa anashuhudia kweli hizi kupitia utendaji wa Roho Mtakatifu—uponyaji, miujiza, kuokolewa. Ilikuwa

105. Mrs. Charles E. Cowman, *Streams in the Desert: 366 Daily Devotional Readings* (Grand Rapids: Zondervan, 1996), 169.

kama Petro alivyokuwa amehubiri awali: "Siku zile nitawamwagia . . . Roho yangu . . . Nami nitatoa ajabu katika mbingu juu, na ishara katika nchi chini" (Matendo 2:18–19).

Tafadhali kumbuka katika 5:32 kwamba huyu Roho Mtakatifu hupewa wale wamtiio. Mtu aliyempokea Kristo, amezaliwa kwa Roho, na sasa anamfuata Yesu Kristo na anamtii ndiye anayeweza kumpokea Roho Mtakatifu kikamilifu.

Rafiki yangu Chad alikuwa amemkubali Kristo lakini alikuwa anaishi kiwango cha juujuu, maisha ya Kikristo ya hobelahobela. Hatimaye alipofahamu hali yake, akafanya upya uhusiano wake na Kristo na akaanza kuenenda katika utiifu. Kisha akaelewa hitaji lake la kazi ya ndani ya Roho–kusafisha nia zake za ndani, kutakasa moyo wake, na kumjaza na Roho. Katika siku maalum, ilikuwa wazi alikuwa amejazwa Roho Mtakatifu.

Je, umempokea Kristo? Je, unaishi katika ruwaza ya utiifu? Basi nyakua haki yako ya kuwa Mkristo aliyejazwa Roho (5:32)!

JULAI 18 **199**

# Moyo wa Upendo

*Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; 18 ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina.*
*Waefeso 3:17-18*

Mkristo akiwa amejazwa na Roho, na hiyo kazi ya kiroho imeleta utakaso—au kama Petro anavyosema, "katika kutakaswa na Roho" (1 Petro 1:2)—kinachofuata ni nini? Tunafahamu kwamba kazi ya Roho wakati mwingine inaelezwa kama utakaso. Kumbuka Matendo 15:8–9: "Na Mungu, ajuaye mioyo ya watu, akawashuhudia, akiwapa Roho Mtakatifu vilevile kama alivyotupa sisi. Wala hakufanya tofauti kati yetu sisi na wao, akiwasafisha mioyo yao kwa imani." Kama nimejazwa na Roho, na nimetakaswa, na moyo wangu umesafishwa, nafasi ya ukuaji wa kiroho uko wapi?

Rudi huko katika fungu la Waefeso ukapate jibu—hakikisha kwamba kufahamu upana wa upendo wa Kristo ni "pamoja na watakatifu wote." Katika kuungana na watakatifu wa Bwana wengi zaidi na zaidi, moyo wangu umepanuliwa, na uwezo wangu wa upendo umepanuka.

Ninawaza juu ya watakatifu fulani maalum—kama Petro, aliyetumia saa kadhaa akinambia jinsi ningeweza kumjua Kristo. Kama Ralph na Bernice, waliokuja katika bweni langu la chuo na mlo wa mchana wa pikiniki na kutiwa moyo kwa nguvu niendelee kumfuata Yesu. Kama Clyde, aliyenipeleka kwa gari maili ishirini na sita nyumbani, baada ya ibada kanisani nilipokuwa mwanafunzi na sikuwa na gari. Kama Ralph na Mabel, aliyenialika mlo wa jioni wakati nilipokuwa mtoto mpya katika ile nyumba. Kama Bengt, aliyehimiza kanisa lake la Kibaptisti linitumie fedha za kunisaidia kumaliza masomo katika seminari. Kama Bill, anayeniombea mimi na mke wangu kila siku. Kama Juanita, anayeendelea kuwasiliana na Bwana kikamilifu sana na kuniruhusu kuzijua siri zake. Kama Phil na Joy, waliopanga utondoti wa kustaafu kwangu kutoka katika kufundisha darasa lile lile la shule ya Jumapili kwa miaka arobaini na mitano, ili nihisi kupendwa. Kama Alan na Martha, wanaoendelea kunishukuru kwa kuwaonyesha Yesu wanapokabiliana na changamoto zao za kimwili na upasuaji. Kama mke wangu Nancy, anayesema, "Ninakupenda zaidi kuliko nilivyowahi kupenda." Na wengine wengi zaidi.

Hawa watakatifu wote wanadumu kuniambukiza tabia zao—kupitia kwao, ninajua upendo wa Kristo kwa kina zaidi kuliko awali. Kwa hivyo, ninakua. Fikiri kuhusu baadhi ya watakatifu wa Mungu unaowajua; wataje kwa majina; na uruhusu hilo likukuze.

Mara tu unapojazwa na Roho wa Mungu, na kutakaswa, na kusafishwa, huo si mwisho—badala yake, huo ndio mwanzo wa ukuaji mkubwa katika neema. Unamwona Mungu akisafisha hulka na haiba yako.

Hiyo tarehe 2 Septemba, wakati Roho wa Mungu alipoujaza na kuutakasa moyo wangu wenye umri wa miaka ishirini na mmoja, moyo wangu wote ulifanywa kuwa safi na kujazwa na Mungu kwa 100%. Hata hivyo, ulikuwa moyo mdogo. Sasa, kwa kuchangamana na watakatifu wengi na kupitia kuvunjwa moyo, maumivu, na huzuni, jambo la kushangaza linatokea. Mungu anapolimbikiza upendo zaidi juu yangu kupitia watakatifu wake na kuiponya huzuni yangu, ninatambua kwamba anaendelea kupanua moyo wangu. Kwa hivyo leo, nina moyo uliopanuliwa.

Mjao wa Roho na usafi wa moyo haukomeshi ukuaji katika neema; huiongeza. Kwa hivyo ungana nami katika klabu cha mioyo iliyopanuliwa.

# Ushindi kwa Roho

*Uchungu wa mauti ni dhambi, na nguvu za dhambi ni torati. Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.*
*1 Wakorintho 15:56-57*

Unakuwa na furaha ya namna gani wakati timu yako uipendayo inapopata ushindi? Ninapofikiri juu ya ushindi wa kushangaza wa michezo, ninakumbuka jinsi Wamarekani walivyofurahi wakati Marekani ilipoishinda Urusi katika mchezo wa magongo katika mashindano ya Olimpiki, ya majira ya baridi kule Lake Placid, New York 1980.

Je, unaweza kufurahi namna hiyo kuhusu kupata ushindi juu ya dhambi? Mungu anataka uwe na ushindi kamili, na Roho Mtakatifu ndiye wakala maalum anayekuletea huo ushindi.

Fikiria ahadi hizi:

- " . . . Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu, ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema" (Tito 2:13–14).
- "Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu . . . Maana Mungu hakutuitia uchafu, bali tuwe katika utakaso. Basi yeye anayekataa, hakatai mwanadamu bali Mungu, anayewapa ninyi Roho wake Mtakatifu" (1 Wathesalonike 4:3, 7–8).
- "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu. Na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu" (Wagalatia 2:20).
- "Ili niwe mhudumu wa Kristo Yesu kati ya watu wa Mataifa, niifanyie Injili ya Mungu kazi ya ukuhani, kusudi Mataifa wawe sadaka yenye kibali, ikiisha kutakaswa na Roho Mtakatifu" (Warumi 15:16).
- "Nakutuma kwao [Mataifa] uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi" (Matendo 26:17–18).

Hapa kuna ushuhuda wa wakati huu tulio kutoka kwa Maridel:

Mamangu alikufa kutokana na saratani ya wengu mwaka wa 2003. Akaniomba nimwahidi kwamba tungekutana mbinguni. Nikafanya hivyo na nilimaanisha. Nilikuwa mtu ninayesadiki kuwa hatuwezi kujua habari za Mungu lakini nikaanza kutafiti. Nikaenda katika maduka ya vitabu vya Kikristo na kununua na kusoma vitabu vya Lee Strobel. Nikauliza watu kama walijua mtu yeyote aliyewahi kwenda mbinguni na kurudi. Mbinguni kulipoendelea kuwa halisi zaidi kwangu, niliamini kwamba ni lazima kulikuwa na Mungu wa kukuendesha. Nikamwomba Mungu aniruhusu nihisi uwepo wake. Nikajipata katika kanisa kule Phoenix. Ushirika mtakatifu ulikuwa unagawanywa, na nikahisi sikuwa nastahili kuula. Uwepo wa Mungu ukaja juu yangu, na nikalia sana nilipokuwa ninamkubali Bwana. Nilijua ni lazima niingie ndani zaidi. Nikatafuta utakaso wote. Siku moja Novemba 2003, niliifia nafsi, na Mungu akanijaza Roho wake. Kusema kweli naweza kusema tangu wakati huo sijakosa furaha na amani. Na sijawahi kuwa na tashwishi. Ni mageuzi yaliyoje, kutoka kuwa mtu asadikiye hatuwezi kujua kuhusu Mungu hadi kuwa na imani chanya inayotakasa![106]

Roho Mtakatifu naazae ushindi wa Mungu ndani yako.

**JULAI 20** **201**

# Kumfuata Roho, Sehemu ya 1

*Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti.*
*Warumi 8:2*

*...ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho.*
*Warumi 8:4*

Kwa kuvunjika moyo kuliko wazi mtu mmoja alinambia, "Mm, huwezi kuwa mtakatifu ukiwa bado unaishi, sivyo?"

106. Awali ilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Machi 2016).

Nilipokuwa ninafikiri kuhusu hilo, nikahitimisha, “Ndiyo, unaweza. Kama ukweli ulivyo, hiyo ndiyo aina pekee ya mtakatifu unayoweza kuwa—mtakatifu aliye hai—maana Warumi 8:4 inasema ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho.”

Safari ni mwendo wa hatua moja moja. Wengine wanachanganyikiwa wanapofikiri juu ya maisha ya Mkristo kama safari—hawawezi kuona mahali pa kilele cha hatari cha pili cha neema. Hata hivyo, matukio mawili ya kilele yanachukuliwa na kuashiriwa katika Warumi 8. Katika kifungu cha 1, Paulo ananena juu ya uhuru dhidi ya hukumu inayokuja kwa kufanya makosa—yaani, amani inayokuja pamoja na kuhesabiwa haki (5:1).

Lakini Paulo pia ananena kuhusu kilele cha pili: “Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima itakuweka huru dhidi ya sheria ya dhambi na mauti” (8:2). Hapa Paulo anaelezea ukombozi dhidi ya kuwa *kiumbe* wa dhambi. Alikombolewa namna gani? Jibu ni la mara moja, kwa kilele cha neema, kama njeo ya Kiyunani inavyomaanisha hapa. Paulo anatumia neno lilohilo kwa “kuwekwa huru” hapa kama ilivyo katika 6:18 na 22. “Na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki”; na, “Lakini sasa mkiisha kuwekwa huru, na kuwa mbali na dhambi, na kufanywa watumwa wa Mungu, mnayo faida yenu, ndiyo kutakaswa, na mwisho wake ni uzima wa milele.”

Mwenendo wetu na Mungu ni kama uhusiano wetu mwingi wa kibinadamu. Chukua uhusiano wa ndoa. Kuna wakati wa uchumba wakati mto mmoja anaomba uchumba—hicho ni kilele kweli—na yule mwingine anasema, “Nimekubali.” Kisha, kwenye madhabahu ya ndoa, katika kuwekana wakfu kamili, hao wawili wanatamka, “Ninakubali.”

Siku moja, baada ya mimi na mke wangu kuoana kwa kama miaka mitano, alinambia, “Mpenzi, je, unanipenda?”

Nikiwa ninashangaa kwamba aliuliza hilo, nikajibu, “Bila shaka. Nilikwambia ninakupenda tulipooana. Je, ninatakiwa kukwambia tena?”

Je, hakuuliza swali la kuchekesha? Unafikiri *mimi* ndimi ninayechekesha—na, kwa hakika, uko sahihi. Sote tunatambua kwamba katika ndoa ya maana na yenye mafanikio, ni lazima siku baada ya siku na wakati kwa wakati tudumua katika kupendana. Kutokuwako kwa makosa hakutoshi—ninapaswa nionyeshe kuwa upendo wangu na imani yangu vinaendelea kila siku, la sivyo, huo uhusiano utaumia. Wakristo wengi sana hufanya makosa ya kufikiri kwamba mara tu wanapopokea tukio la kilele cha utakaso wote, wamefika kiroho. Lakini utakaso wote ni mwanzo tu wa uhusiano wa kila

siku na Mungu. Utakatifu si mwisho bali ni mwanzo wa kile ambacho Mungu anataka tuwe.[107]

JULAI 21 202

# Kumfuata Roho, Sehemu ya 2

*Ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho.*
*Warumi 8:4*

*Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa mhuri hata siku ya ukombozi.*
*Waefeso 4:30*

Utakaso si uzoefu peke yake, au hata kimsingi, uzoefu wa kupatikana bali ni uhusiano ambao ni lazima uendelezwe. Ni hatari kunena kuhusu "kuhifadhi" au "kushikilia" uzoefu wako. Kuna maana ambayo ndani yake haya maneno yanakubalika—lakini hayana usahihi kamilifu. *Tunahifadhi uzoefu*, lakini *tunatembea* na *mtu*—na Mungu. Paulo, anataka tusijue tu wakati maalum tulipofanywa tuwe "huru kutoka kwa sheria ya dhambi na mauti" (Warumi 8:2) lakini pia kwa wakati huu na kawaida tumfuate Roho Mtakatifu, kama njeo ya sasa ya hicho kitenzi inavyopendekeza (8:4).

Uhusiano wetu na Mungu lazima uwe hai kila siku. Ni lazima tutulie ndani yake kabisa ndipo tutakapoendelea kuwa wazuri katika kila hali inayotujaribu. Kutakaswa si jambo la kimitambo linalowashwa—linamaanisha kuingia katika uhusiano wenye nguvu na Mungu ambao ni lazima uwe unaendelea. Kuufanya uhusiano wetu na Mungu kuwa jambo la kila wakati kunaonyeshwa katika mfano wa Yesu mzabibu na matawi katika Yohana 15:1–8. "Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu" (kif. 4).

Uhusiano ni jambo nyeti ambalo linaweza kuharibiwa kirahisi. Kupuuzana tu kunatosha kuharibu urafiki mzuri. Lakini kutoaminiana kunaweza kuharibu uhusiano wetu na Mungu, kwa maana hili huonyesha kutaka kwake na uwezo wake wa kutusaidia. "Wala msimhuzunishe yule

107. Awali ilichapishwa katika Charles "Chic" Shaver, *Keeping Spiritual Victory* (Kansas City, MO: Beacon Hill Press of Kansas City, 1972), 5, 8–10.

Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi" (Waefeso 4:30,); na "Msimzimishe Roho" (1 Wathesalonike 5:19), "ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho" (Warumi 8:4).

JULAI 22 **203**

# Fuata Hatua

*Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho.*
*Wagalatia 5:24–25*

Mwendo wa kujisukuma mwenyewe nyuma ya mashine ya kukatia majani ndiyo njia ya kufanya ua wangu ufekwe vizuri. Utaratibu ni rahisi: jaza tangi mafuta, washa mashine, weka vizuri kidude kinachodhibiti kiasi cha mafuta na kasi ya mota, weka vizuri kasi ya mwendo, gandamiza kidhibiti utendaji—kisha unafyeka. Mafuta yataendesha mashine, nami ninatembea.

Ninapofyeka kwenye ukingo mbele ya vichaka vyetu vilivyo kijani siku zote, matawi yaliyojitokeza wakati mwingine hushika kidude kinachodhibiti matumizi ya mafuta na kukibonyeza hata kikakatisha mafuta. Kisha mota inazima, na mashine ya kukatia majani inasimama. Hili linapotokea, ni lazima nisimame.

Katika ulimwengu wa maisha yaliyojazwa na Roho, ni lazima kuwe na *kuendelea* kumwegemea, kumtegemea, na kumsikiliza Roho Mtakatifu. Yeye ndiye chanzo cha uwezo wa kiroho, na ugavi wake unadumu ilimradi tunadumu kutembea naye. Toka nje ya hatua, vunja muungano, na mambo magumu huibuka. Kuna wakati ambapo unakuwa umejazwa Roho, lakini unatakiwa uendelee kumtegemea Roho na kutulia ndani yake ili uendelee kupata ushindi.

Maandiko huwekea mkazo ukweli huu kwa njia nyingi. Wakolosai 1:22–23 inasema, "Katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu, wasio na mawaa wala lawama—mkidumu tu katika ile imani." Tambua hilo neno kuu: "mkidumu."

Angalia mlinganisho wa mzabibu na matawi katika Yohana 15:5–6: "Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi. Akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.

Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea."

Katika Matendo 2:4, wanafunzi walijazwa Roho katika kipindi cha wakati. Wakati hawa hawa wanafunzi walipokuwa katika shinikizo na kutishwa, waliomba na wakapokea ujazo mpya wa Roho wa kuwapa ujasiri (Matendo 4:31). Baadaye, katika onyo la Paulo kwa Wakristo wa Efeso 5:18—"Mjazwe Roho"—anatumia njeo ya sasa, kumaanisha "*Endeleeni* kujazwa Roho."

Wengine wanaweza kujiuliza kama wametakaswa, moyo wako umesafishwa, na umejazwa Roho, je, kuna nafasi ya ukuaji? Oo ndiyo, hata zaidi! Tafadhali angalia hizi glasi mbili, na uchukulie kuwa zote zimejaa maji.



Glasi zote zimejaa pomoni—lakini glasi kubwa huwa na maji mengi. Je, ina maana kusema kwamba Mkristo mchanga anaweza kujaa Roho wa Mungu? Ndiyo—lakini kisha fikiri kwamba kupitia majaribu, changamoto, na mambo magumu, mioyo imepanuliwa. Mioyo yao bado imejaa pomoni, lakini uwezo wao ni mkubwa zaidi—wamekua.

Hudson Taylor, mmishenari mkuu wa Kiingereza aliyeanzisha China Inland Mission mwaka 1865, alivumbua na kuwa na tabia ya kuendelea kumtegemea Mungu. Aliona hii kanuni ikielezwa katika Yohana 6:35, iliyoelezwa hivi: "Yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe."[108] Au, kunena kwa njia nyingine—fuata hatua za Roho.

108. Dkt. na Bi. Howard Taylor, *Hudson Taylor's Spiritual Secret* (Chikago: Moody Press, n.d.), 182.

# Alikuwa na Miaka Kumi na Miwili Pekee

*Basi katika nyumba kubwa havimo vyombo vya dhahabu na fedha tu, bali na vya mti, na vya udongo; vingine vina heshima, vingine havina. Basi ikiwa mtu amejitakasa kwa kujitenga na hao, atakuwa chombo cha kupata heshima, kilichosafishwa, kimfaacho Bwana, kimetengenezwa kwa kila kazi iliyo njema.*
*2 Timotheo 2:20-21*

Mmishenari alipiga simu ili atoe ripoti juu ya huduma mpya zilizokuwa zimeanzishwa katika miji mipya mitano katika nchi tano tofauti—ambazo zote zilikuwa sehemu ya iliyokuwa muungano wa Sovieti. Kisha akaniambia kuhusu binti yake Bekah.

Bekah siku zote alikuwa macho kiroho. Alipokuwa na miaka mitatu, familia ilipokuwa inatazama onyesho la *Sinema ya Yesu* kule Houston, aliona maeneo ya matukio ya ubatizo wa Yesu. Aliposikia Baba akinena kuhusu Yesu, “Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu,” aliuliza, “Yesu ni Mungu, sivyo? Ilikuwaje Mungu akanena?” Alikuwa tayari anajaribu kuelewa Utatu.

Akiwa na miaka minne, Bekah na mamake walianza kujadili dhambi. Kwa ombi la Bekah, mamake akaegesha gari lao, wakaomba pamoja, na Bekah akampokea Yesu. Wazazi wake wakatambua mabadiliko ya mara moja katika mwenendo wake—tabia yake ya awali ya ukaidi hasi iliweza kuonekana kwamba imebadilika na kuwa azimio la kumfuata Yesu.

Muda mchache hapo nyuma, katika ibada yake ya kila siku, Bekah alisoma kuhusu tajiri aliyemwuliza Yesu kile ambacho ni lazima afanye ili aurithi uzima wa milele. Alielewa jibu la Yesu kuwa, “Ni lazima unipe kila kitu.” Alifikia alikuwa amesikia mnong’ono: *Unatakiwa kunipa kila kitu*.

Muda mchache baadaye, Bekah alionyesha hitaji lake la kutakaswa. Yeye, mamake, na babake wote walipiga magoti na wakaomba, na Mungu akamtakasa Bekah. Baadaye, babake akauliza, “Ni kitu gani kilikufanya uhisi hili hitaji?”

Bekah akajibu, “Ninataka moyo wangu uwe tayari kwa chochote kile anachoniitia Mungu.”

Ndiyo, "chombo cha kupata heshima, kilichosafishwa, kimfaacho Bwana, kimetengenezwa kwa kila kazi iliyo njema"—na alikuwa na miaka kumi na miwili pekee.

JULAI 24 **205**

# Hubiri kwa Nguvu za Roho, Sikiliza kwa Nguvu za Roho

*Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.*
*Matendo 2:4*

*Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti yake, akawaambia, Enyi watu wa Yudea, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu.*
*Matendo 2:14*

*Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?*
*Matendo 2:37*

Ilikuwa siku ya kukumbukwa—Roho wa Mungu aliyemwagwa juu ya wafuasi 120 wa Yesu. Matukio ya miujiza yaliambatana na uwepo wa Roho—uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukiashiria *uwezo*; ndimi za moto, zikiashiria *usafi*; watu kuanza kunena kwa lugha nyingine, kukiashiria *kutangaza*. Wale 120 wakatangaza maajabu ya Mungu; watu wa mataifa mengi walisikia hizi shuhuda katika lugha zao wenyewe; na katika mazingira yenye upako wa Roho, Petro akahubiri. Kundi likamsikiliza na, wakisadikishwa na Roho huyo huyo, wakauliza "Tutendeje?"

Na hili bado linatokea leo. Hapa kuna ripoti ya Nancy kuanzia wakati alipoenda kanisani kwa kualikwa na ndugu yake, Craig:

> Katika mahubiri yako yote, nimehisi kama ambaye ulikuwa unanena na mimi binafsi—ni kama kulikuwa hakuna mtu mwingine yeyote hapo. Ninakumbuka ujumbe wako ukinipiga kwa nguvu sana kiasi kwamba nikalazimika kuzuia machozi. Hatimaye, mwisho wa ibada, ulipowaalika watu waje waombe, moyo wangu ulianza kudunda . . . Nilikuwa ninatetemeka kila mahali, machozi yakimwagika, na nikamtazama kaka yangu. Akasema, "Je, unataka niende na wewe?"

> Kwa kweli hata siwezi kukumbuka kwenda mbele na kuomba, lakini . . . nilipoanza kuomba lile ombi la wokovu, nilisikia mzigo mzito sana ukiepuliwa kutoka mabegani mwangu. Kusema kweli siwezi kueleza jinsi nilivyoendesha gari usiku ule—nilikuwa nimetulia sana na katika amani na Bwana. Ninakumbuka kuingia ndani na kumwambia mume wangu kile kilichokuwa kimefanyika kwangu . . . Akasema, "Ni vizuri. Ninaona utakuwa ukienda katika hilo kanisa sasa."
>
> Miezi sita baadaye, mimi na mume wangu tulikuwa tumekaa katika safu ya mwisho ya kanisa, na sote tulikuwa tunaimba "Amazing Grace" baada ya ujumbe wa nguvu sana. Na akaanza kulia. Akanambia mzigo mzito sana ulikuwa umeepuliwa kutoka kwake na akahisi ana amani iliyomzunguka . . . Tarehe 4 Oktoba, mume wangu akamfungulia Bwana moyo wake.

Watoto wao wakahusika katika shule ya Kikristo ya kanisa. Tarehe 19 Januari, binti yao aliandika huu ujumbe kwa wazazi wake: "Leo ilikuwa siku yangu ya pili katika shule ya Kikristo, ni nzuri sana. Kwa kweli wana watoto wazuri sana. Jumapili iliyopita, katika kanisa la watoto, nilimkaribisha Yesu moyoni mwangu. Kwa kweli ninawapenda yote wawili. Asante tena kwa kuniweka katika shule ya Kikristo."

Hubiri kwa Nguvu za Roho. Sikiliza kwa Nguvu za Roho.

JULAI 25 **206**

## Lengo Lake ni Nini?

*Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake. Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.*
*Warumi 8:28-29*

Lengo *lako* ni nini? Katika madaraja tofauti maishani mwangu, nimekubali malengo tofauti tofauti. Kule chuo, lengo langu lilikuwa kujifunza vizuri katika kila darasa na nimalize shule nikiwa nimefanikiwa. Nilipokuwa nafikiri maisha yangu ya kazi yatakuwaje, nilikuwa na lengo la kupata kazi inayonifaa. Lengo langu kuu zaidi maishani mwangu lilikuwa kufanya kitu

cha kuwasaidia wengine. Kuhusu ndoa, kukutana na mwanamke sahihi na niingie katika ndoa itakayokuwa na mapatano, ikitukamilisha sote wawili, mapenzi ya kweli—hilo ndilo lililokuwa lengo.

Hebu geuza mawazo yako kwa dakika moja: Lengo *la Mungu* ni nini? Katika fungu la Warumi, tunajifunza kwamba Mungu huchukua mambo yote yanayotujia, mabaya na mazuri, na huyafanyia kazi katika mpangilio kwa ajili ya wema wetu. Hata hivyo kuna masharti: Hufanya hivi kwa wale wampendao, ambao wameitwa *kulingana na lengo lake*. Maana wale aliowajua tangu asili (wale alijua wataitikia neema yake), aliwachagua tangu asili *wafananishwe* na *mfano* wa *Mwana wake*. Kwa maneno mengine, anataka kukufanya wewe ufanane na Yesu zaidi. Hata hilo tamanio mzizi wake umo katika muktadha wa kuleta utukufu zaidi kwa Yesu, ili Kristo asiwe peke yake—badala yake, awe mzaliwa wa kwanza kati ya watu wengi waliofanywa wafanane na Kristo na neema ya Mungu.

Hebu fikiri kuhusu hilo! Mungu anataka kukufanya wewe na mimi tufanane na Yesu zaidi. Petro wa Pili 1:3–4 inawekea mkazo hili: "Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa." Tunaweza kushiriki katika asili ya uungu ili tupate kufanana na Yesu.

Samuel Logan Brengle alikuwa ofisa katika Jeshi la Wokovu. Zaidi ya nakala milioni moja za vitabu vyake vimebariki ulimwengu. Hapa kuna sehemu ya hadithi yake:

> Tarehe 9 Januari, 1885, kama saa tatu za asubuhi, Mungu aliitakasa roho yangu. Wakati huo nilikuwa katika chumba changu, lakini kwa dakika chache nikatoka na nikakutana na mtu na nikamwambia kile ambacho Mungu alikuwa amenifanyia. Asubuhi iliyofuata, nikakutana na rafiki mwingine barabarani na nikamwambia hiyo hadithi ya baraka. Akapiga kelele na akamsifu Mungu na akanihimiza nihubiri wokovu kamili na kuukiri kila mahali. Mungu alimtumia kunihimiza na kunisaidia. Kwa hivyo siku iliyofuatia nikahubiri juu ya hiyo mada kwa uwazi na kwa nguvu kama nilivyoweza, na nikamalizia na ushuhuda wangu.
>
> Mungu alibariki hilo neno kwa nguvu kwa wengine, lakini nafikiri alilibariki zaidi sana kwangu mimi mwenyewe. Kuungama huko kuliniweka katika rekodi. Kulivunja madaraja nyuma yangu. Ulimwengu wa mara tatu sasa ulikuwa unanitazama kama mtu aliyeungama kwamba Mungu alikuwa amempa moyo safi. Sasa nisingeweza kurudi nyuma.

Nililazimika kwenda mbele. Mungu aliona kwamba niliazimia kuwa mkweli hadi kifo. Kwa hivyo asubuhi mbili baada ya hilo, nilipokuwa tu nikitoka kitandani na nilikuwa ninasoma baadhi ya maneno ya Yesu, alinipa baraka ambayo sikuwa nimewahi kuota kwamba mwanadamu angeweza kuwa na upande huu wa mbinguni. Ilikuwa mbingu ya upendo iliyokuja moyoni mwangu. Nikatembea Boston Common kabla ya kifungua kinywa, nikilia kwa furaha na kumsifu Mungu. Oo, jinsi nilivyopenda! Katika saa hiyo nilimjua Yesu na nikampenda mpaka ikaonekana kama moyo wangu ungepasuka kwa upendo. Nilipenda shomoro, nikapenda mbwa, nikapenda farasi, nikapenda watoto wadogo barabarani, nikapenda wageni walionipita upesi, nikapenda wapagani—nikaupenda ulimwengu wote.

Je, unataka kujua utakatifu ni nini? Ni upendo safi. Je, unataka kujua ubatizo wa Roho mtakatifu ni nini? Si hisia za moyoni tu. Si hisia za furaha zinazopita katika usiku mmoja. Ni ubatizo wa upendo huteka nyara kila fikira ipate kumtii Bwana Yesu (2 Kor. 10:5); huitupa nje hofu (1 Yohana 4:18); huchoma mashaka na kutoamini kama moto unavyounguza nguo; unaomfanya mtu awe "mpole na mnyenyekevu wa moyo" (Mat. 11:29); hilo linamfanya mtu achukie uchafu, kudanganya na uongo, ulimi wa kusifu mno, na kila njia mbaya yenye chuki kamili; inayofanya mbinguni na jehenamu kuwa uhalisi wa milele; hilo linamfanya mtu awe mvumilivu na mpole kwa wale wa mbele na watenda dhamb; hilo linamfanya mtu awe "safi, . . . mpole, . . . rahisi kusihiwa, aliyejaa rehema na matunda mema, bila ubaguzi, na bila unafiki" (Yakobo 3:17); hilo linamleta mtu katika huruma kamili na isiyoisha na Bwana Yesu Kristo katika jitihada zake na taabu ili apate kuuleta ulimwengu uliopotea na ulioasi kwa Mungu.

Mungu alinifanyia hayo yote, nalisifiwe jina lake takatifu![109]
Kufananishwa na mfano wa Mwana wake! Akufanye uwe kama Yesu!

109. S. L. Brengle, *Helps to Holiness* (London: Salvationist Publishing and Supplies, Ltd., 1955), 9–10.

JULAI 26 **207**

# Bado Kuna Tatizo

*Mvue mwenendo wenu wa kwanza, utu wa zamani unaoharibika, kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; na mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.*
*Waefeso 4:22-24*

Wanaosha vyombo vyao kwa mikono kwa sababu mashine yao ya kuoshea vyombo imeharibika. Wakati mwingine wanasema juu ya kukarabati au kununua nyingine lakini siku zote amua kungojea kwa sababu kuna tatizo lingine: mfumo wa maji taka wa hiyo nyumba haufanyi kazi vizuri sana. Mizizi ya miti imekuwa na kuingia katika bomba lililofunikwa mchangani linalobeba maji machafu kutoka kwenye hiyo nyumba. Mara kwa mara, maji yanayopaswa kutoka nje ya nyumba hurudi kwenye msingi wa nyumba. Hata wakipata mashine mpya ya kuoshea vyombo, bado kuna tatizo.

Vivyo hivyo, katika maisha ya Wakristo wengi, kuna tatizo la kina la ndani linaloziba baraka kamili za Mungu katika maisha yao. Mkristo mmoja alilalamika, "Hasira mbaya ilikuwa inapanda kutoka ndani ya roho yangu." Paulo akawahimiza Wakristo kule Efeso wauvue utu wao wa zamani unaotenda dhambi pia mwenendo wa kwanza. Walipaswa kuvaa utu mpya ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu.

Paulo anawaonya Wakristo kule Korintho: "Hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana, ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je! Si watu wa tabia ya mwilini ninyi?" (1 Wakorintho 3:3). Alishangaa kwamba hawakuwa wanaishi kwa kumfuata Roho (3:1).

Paulo aliwaonya Wakristo wa Galatia juu ya vita vya ndani vya kiroho: "Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili. kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka" (Wagalatia 5:17). Baadaye anaonekana kupendekeza suluhisho: "Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake" (5:24). Katika 5:16, aliandika, "Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili."

Katika Waefeso 2:2–3, Paulo alinena kuhusu wale ambao zamani walikuwa wamekufa katika dhambi. Aliandika, "Sisi sote nasi tulienenda

kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili" (2:3). Anaonekana kusema kwamba nyuma ya hizo dhambi kuna uchu na tamaa mbaya na nyuma yake kuna "mwili"—au, kama tafsiri nyingine zinavyosema, "utu wa dhambi."

Mara nyingi, Wakristo wanaonyesha mabadiliko chanya katika tabia zao lakini bado wanaweka mtazamo au msimamo ambao bado unatakiwa kubadilika. Labda hiyo ndiyo sababu Yakobo alisema, "Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili" (4:8).

Labda tungeelewa hili suala kwa njia hii: Kama Mkristo, unaweza kuapa, lakini unanung'unika na kulalamika wakati unapokosa kupata kile unachotaka. Kama Mkristo, pengine hutaweza kuiba, lakini una wivu kwamba rafiki yako ana kitu kipya na wewe huna. Kama Mkristo, hutamwangusha hadharani, lakini inakuudhi kwamba rafiki yako alitambuliwa lakini wewe hukutambuliwa.

Pengine tukitazama maisha ya John Allan Wood itatusaidia. Ijapokuwa ni wazi aliokoka na anatayarisha maisha yake kwa ajili ya huduma, Wood alipata utu wake wa zamani (kujipenda mwenyewe) kuwa ndiko kizuizi kikubwa zaidi. Aliandika kuhusu pambano lake:

> Wakati huu mara nyingi nilikuwa ninasadikishwa juu ya uharibifu wa moyo uliokuwa umebaki na hitaji langu la usafi. Mara nyingi . . . nilikuwa ninafahamu kuhusu uovu wa ndani uliokuwa umekitamizizi . . . . Uliharibu amani yangu. Ulivuruga maono yangu ya kiroho. Ulikuwa chombo cha majaribu makali. Uliingilia ushirika wangu na Mungu. Ulidhoofisha jitihada zangu za kufanya mema . . . . Ulichukua sehemu moyoni mwangu ambayo nilijua ilikuwa inapaswa kumilikiwa na Roho Mtakatifu . . . . Mara nyingi nilikuwa ninasadikishwa kwa nguvu juu ya hitaji langu la usafi wa ndani kuliko nilivyowahi kusadikishwa juu ya hitaji langu la kusamehewa.[110]

Hatimaye, Wood akafanya uamuzi. Akashuhudia: "Atukuzwe Mungu! . . . Wakati wa kufanya uamuzi ndio uliokuwa wakati wa ushindi. Ghafla nilihisi kutoa katika moyo wangu niko macho na mwenye nguvu kiasi kwamba ilionekana kimwili kuliko kiroho; muda mfupi baadaye nilihisi utamu usioweza kuelezeka ukiingia katika nafsi yangu yote."[111]

John Allan Wood alipata kusafishwa na kujazwa kwa Roho Mtakatifu moja kwa moja, pia uwezo wa Roho wa kushinda dhambi. Sasa angeweza

---

110. V. Raymond Edman, *They Found the Secret* (Grand Rapids: Zondervan, 1960), 131–132.

111. Edman, *They Found the Secret*, 133.

kujumuishwa katika kirai cha mtume Paulo, “Kusudi Mataifa wawe sadaka yenye kibali, ikiisha kutakaswa na Roho Mtakatifu” (Warumi 15:16)—jibu la eneo lolote ambamo bado tuna matatizo.

JULAI 27 **208**

# Vita Vya Ndani vya Roho Yako

*Basi nasema, Nendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka.*
*Wagalatia 5:16-17*

Alikuwa rafiki yangu wa karibu sana na yule mtu aliyenipeleka kwa Kristo. Alikuwa anaendesha gari lake, na nilikuwa nimekaa katika kiti cha abiria, nikipendekeza wazo muhimu sana. Hata hivyo, hakuonekana kufurahishwa sana. Ghafula, hisia ya chuki iliinuka ndani yangu. Alipoona onyesho la hisia usoni mwangu, aliuliza, “Kuna nini?” Ukweli kwamba alikuwa amenigundua kulifanya nimfikirie vibaya zaidi.

Ngoja kidogo—huyu mtu alikuwa chombo cha kibinadamu cha wokovu wangu. Kwa nini nilikuwa ninaweka hizi hisia dhidi yake? Ijapokuwa nilikuwa nimemjua Kristo, kulikuwa na vita vya ndani vilivyokuwa vinaendelea ndani yangu—mwili (au utu wa dhambi) dhidi ya Roho.

Wakristo wa Galatia walikuwa wanapitia hivi vita, na Paulo akaviweka katika maneno. Nyuma ya matendo ya mwili (5:19) ni mwili wenyewe—si hiyo nyama juu ya mifupa ya mwanadamu, lakini ubinafsi, nguvu ya kutenda dhambi ambayo wakati mwingine ilibadilika na kuwa “utu wa dhambi.” Paulo aliwaagiza Wagalatia wapigane na huo utu kwa kuusulibisha mwili (5:24), kuishi kwa kuongozwa na Roho, na kufuata hatua za Roho (5:25).

Mtu mmoja wakati mmoja alisema juu ya maisha ya Mkristo, “Maombi yatasukuma dhambi nje, au dhambi itasukuma maombi nje.” Vivyo hivyo vinavyoweza kusemwa kuhusu mwili na Roho. Kuishi katika Roho, kuishi huu uhusiano, ni lazima uuingie—utamjua Roho katika ukamilifu wake wakati anakuongoza kikamilifu. Vita hivi vinapowaka ndani yako, utafanya uamuzi wa wazi kuhusu mahali utiifu wako utakapokuwa.

Bud alikuwa kijana mtendaji mwenye uwezekano mkubwa wa mafanikio, na kama mtu wa laini ya umeme mwenye kifua kikubwa alijitokeza kwa namna ya kuvutia. Hata hivyo, alikuwa na historia ya panda shuka. Wakati mmoja amewahi kuwa na leseni ya mhudumu wa kanisa mahalia, lakini haikuhuishwa na kanisa lake. Humo njiani, alikuwa amekuwa Askari wa Majini wa ujenzi, alikuwa amekarabati nyumba, na alikuwa amechimbia vigingi vya ukigo. Alikuwa katika kila ibada ya uamsho, lakini pamoja na nguvu zake zote za kimwili, kiroho alishindwa—mwili ulikuwa unamshinda vita.

Akasema alikuwa anamngojea Mungu amtakase. Kisha mtu mmoja akamwambia, "Bud, yuko tayari. Anakungojea wewe uwe tayari."

Usiku ule, Bud akaja madhabahuni. Huku akiwa analia, akaupeleka "mwili" wake msalabani, na Roho akatembea. Baadaye, akatamka kwa kushangilia kwa mke wake, "Niko huru, niko huru."

Kisha akarudia maneno hayo kwangu: "Chic, niko huru, niko huru." Hatimaye Roho alikuwa ameshinda.

**JULAI 28** **209**

# Tendo la Mungu

*Ili niwe mhudumu wa Kristo Yesu kati ya watu wa Mataifa, niifanyie Injili ya Mungu kazi ya ukuhani, kusudi Mataifa wawe sadaka yenye kibali, ikiisha kutakaswa na Roho Mtakatifu.*
*Warumi 15:16*

Kuna vitu unavyoweza kufanya—unaweza kuomba, ukatoa maisha yako, ukaomba usafishwe ndani yako, na kumfikia Mungu katika imani. Lakini unapofika wakati wa kutakaswa, ni Mungu anayefanya hivyo—ni *tendo la Mungu* la kimiujiza.

Maandiko yanatwambia hili. Kwa mfano, katika ombi lake la kuhani mkuu kwa niaba ya wafuasi wake, Yesu aliomba, "Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli" (Yohana 17:17). Tambua kwamba alimwomba *Mungu* akamilishe hili tendo kubwa. Katika matini asili, pia tunaona kwamba neno "takasa" ni kitenzi kinachoashiria kitendo cha papo hapo.

Kisha Yesu anaomba, "Na kwa ajili yao najiweka wakfu mwenyewe, ili na hao watakaswe katika kweli" (17:19). Tunajua kwamba Yesu asingeweza

kuwa mtakatifu kuliko vile alivyokuwa tayari—aliposema kuhusu kujitakasa mwenyewe, alimaanisha alikuwa anajitenga kwa ajili ya kifo cha kujitoa sadaka pale msalabani. Na wakati aliposema kwamba wanafunzi wake "watakaswe katika kweli," alikuwa na maana zote mbili "kutengwa" na "kusafishwa." Kwetu sisi leo, neno "takaswa" pia linarejelea hali au uhusiano wa kuendelea.

Waebrania 13:12 inanena kuhusu sadaka kuu ya Yesu: "Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango." Hapa, kwa mara nyingine tena, "takasa" ni kitendo cha papo hapo anachokifanya Yesu.

Katika 1 Wathesalonike 5:23–24,Paulo aliomba, "Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa. Nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya." Tambua kwamba ni wazi kwamba ni Mungu mwenyewe atakayewatakasa kabisa. Kisha Paulo anaomba kwa ajili ya nguvu za Mungu za kuhifadhi ili ziwadumishe waumini mara tu wanapotakaswa. Hatimaye, anasisitiza kwamba Mungu atakamilisha huo utakaso ambao amewaitia. Paulo yuko wazi: *naye atafanya*. Na sasa, wale waliotakaswa wanaweza kufurahia ukuaji mkuu katika neema.

Katika Matendo 26:17–18, Paulo anaeleza mwito wa kiungu anaoishi chini yake: "Nakutuma kwao [Mataifa] uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi." Sehemu ya mwanadamu ya kupokea hii neema ni kitendo chetu cha kumwamini Yesu, lakini Mungu bado anafanya utakaso.

Kwa kuwa utakaso ni tendo la Mungu la kimiujiza, hufanyika papo hapo. John Wesley, kiongozi wa uamsho wa utakatifu mkuu ulioenea Uingereza yote na sehemu nyingi za ulimwengu katika miaka ya 1700, alithibitisha hili: "Baada ya kuwahoji watu 652 wa hiyo jamii waliokuwa na udhihiri zaidi katika yale yaliyowatokea, na ambao sikuona sababu ya kuwa na tashwishi na ushuhuda wao . . . wote wanaoamini kwamba wametakaswa hutangaza kwa kauli moja kwamba mabadiliko yalitokea papo hapo. Sina lingine ila kuamini kwamba utakaso kawaida, kama si siku zote, ni kazi ya papo hapo."[112]

Hapa kuna ushuhuda wa Danielle, kijana mwanamke aliyekuwa mgeni katika kanisa:

112. John Wesley, "On Patience," *Great Holiness Classics, Vol. 2: The Wesley Century*, T. Crichton Mitchell, ed. (Kansas City, MO: Beacon Hill Press of Kansas City, 1984), 147.

Nilipokuwa na miaka mitano, nilitoa moyo wangu kwa Kristo. Nilipokuwa na miaka kumi na mitatu, niliyatoa upya maisha yangu kwa Kristo. Bado nilihisi kama kulikuwa kuna kitu kilichokuwa kinakosekana maishani mwangu. Jumapili, ya tarehe 13 Oktoba, 2019, nilitakaswa. Kila kitu kuhusu utakaso kilinitisha na kuniogofya. Baada ya kumsikia Kasisi Shaver akihubiri, nikaelewa kile kilichokuwa kinakosekana katika maisha yangu ya Kikristo. Hiyo Jumapili jioni, hatimaye nilitoa yote kwa Kristo na kila kitu kimekuwa dhahiri zaidi na kimeng'aa zaidi. Mtazamo wangu na msimamo wangu juu ya vitu ulibadilika na kuwa bora zaidi. Nimehisi kuwa huru zaidi, karibu na Mungu zaidi, na safi zaidi kuliko nilivyowahi kuhisi awali katika maisha yangu. Hatimaye ninahisi kuwa kamili na nina lengo maishani mwangu.

Tambua kauli yake iliyo wazi: "Jumapili, ya tarehe 13 Oktoba, 2019, nilitakaswa." Tendo la Mungu la ajabu kabisa. *Naye atafanya!*

**JULAI 29** **210**

# Usisimame Tu Hapo—Tembea!

*Bali tukienenda katika nuru, kama yeye alivyo katika nuru,*
*tunashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake,*
*yatusafisha dhambi yote.*
*1 Yohana 1:7*

Je, unaweza kuamua kununua gari mpya inayopendeza, uilete nyumbani, uiegeshe kwenye gereji yako, kisha uiache tu ikae hapo? Je, utaweza kujivuna mbele ya rafiki zako, "Nina gari mpya nzuri!" lakini usiitoe kwenye gereji kamwe? Kwa hakika huwezi—utaiendesha! Hiyo ndiyo kazi ya gari.

Bado, watu wengine wanachukulia Ukristo namna hiyo: wanamkubali Kristo kwa muda tu na hata huwaambia watu wengine kuhusu hilo. Lakini, baadaye huo uhusiano unakwama kwa sababu hawafanyi chochote. Yohana anasema, "Usisimame tu hapo—tembea. Tembea katika nuru." Nuru ni kweli yoyote anayokuonyesha Mungu—chochote kinachomfunua yeye, kinachoifunua dhambi, au kuleta upendo, ukuaji, usafi, haki, utakatifu. Unapaswa kuishi katika uhusiano unaoendelea na Bwana anayeishi.

Wakati fulani nilimjua mwanafunzi mmoja wa chuo cha Kikristo aliyekuwa amepoteza mng'ao wa kukutana na Mungu. Lakini siku moja,

Roho wa Mungu akaangaza nuru akilini mwake na akamkumbusha kwamba alipokuwa ameuza Biblia ili alipie ada za shule mpaka akamaliza, hakutuma yale malipo ya mwisho kwa kampuni. Akaungama dhambi yake kwa Mungu mara moja, akatuma hayo malipo, na akaanza kuenenda katika amani, furaha, na ushindi.

Huu mwendo unahitaji moyo mwaminifu. Kama tutasema hatuna dhambi na iwe ni uongo, tunajidanganya wenyewe. Nimesikia hilo awali: "Mimi ni mtoto wa Kikristo—ninafanya upumbavu kidogo, ninakunywa pombe kidogo, ninatumia mihadarati kidogo, ngono kidogo—lakini huyo si mimi halisi. Moyoni mwangu mimi ni mzuri sana." Uongo kama huo!

Matokeo ya mwenendo kama huo ni hakika: "unatutakasa dhambi zote." Usiutie maji—kusafishwa huku kunataka kuenenda katika nuru kila mara, na kwa furaha. Anatufanya tuwe safi, anatufanya tuendelee kuwa safi, anaendelea kutusafisha, anatuosha kila wakati tunapohitaji kuoshwa—tena, tukienenda katika nuru.

Kwa hivyo ukianguka katika dhambi unapaswa kufanya nini?

Mvulana mdogo wakati mmoja alimwuliza mzee, "Ukianguka majini utazama?"

Huyo mzee akasema, "La, utakaa humo."

Kwa maneno mengine, ukifanya dhambi, mpelekee Mungu jambo hilo katika maombi na kuungama.

Charles alikuwa amekuzwa katika nyumba ya Kikristo, lakini kama mtu mzima, akawa hajali. Alihisi alilazimika kupeleka dau lake nyumbani kwake katika siku za wikiendi, na akawaweka watoto wake nje ya kanisa kwa muda mrefu hata wakashika mtindo wake wa maisha. Akakubali kwamba kwa kweli hakuamini katika majibu ya maombi. Katika fikira zake, alisema, unaenda madhabahuni mara moja, na kuanzia hapo na kwendelea, unajaribu tu kuishi maisha mazuri. Lakini wiki iliyopita, Charles alipokea uthibitisho wa ugonjwa wake wa figo na upasuaji unaokuja.

Baada ya kupokea majibu ya kupimwa kwake, Charles akaniambia, "Nimekuwa nikiomba sana. Nilimpa Mungu mashua yangu, nyumba yangu, wikendi yangu, mimi mwenyewe. Hatimaye, akaniokoa, na Mungu ni halisi. Nimepata uponyaji wa muda, nimeweza kuhudhuria wiki ya uamsho, rafiki yangu Eugene aliokolewa Jumatano, Fred alirejeshwa Jumapili, na mimi niko tayari kwenda hospitali. Nimeona majibu mengi zaidi ya maombi hii wiki kuliko katika maisha yangu yote ya awali."

Ndiyo, Charles, Ukristo ni maisha, si wakati tu mchache. Kwa hivyo, litoe hilo neno nje: "Usisimame tu hapo—tembea!"

# Njia Sahihi

*Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza Katika njia z*
*a haki kwa ajili ya jina lake.*
*Zaburi 23:3*

Nilipokuwa darasa la saba, nilisailiwa kwa ajili ya tamthiliya ya darasa. Baada ya kujaribu kwa mara chache, mkufunzi wa uigizaji alinivuta kando na kusema, "Unarudiarudia kitu kilekila. Hakuna tumaini kwako."

Ninashangaa kwa nini sikuvunjwa moyo na hilo. Nilikuwa mtoto ambaye nilikuwa mwepesi kuumia, lakini kwa namna fulani, maneno yake hayakunisumbua.

Katika darasa la nane, nilijaribu tena kwa ajili ya tamthiliya nyingine. La kushangaza, nilipata sehemu ya kuongoza. Mkufunzi yule yule wa uigizaji akasema, "Nini kilikutokea?" Alishangazwa na ubora nilikuwa nimeupata, lakini sikuweza kutoa sababu ya hilo. Kujiamini kwangu kukaongezeka.

Kule shule za upili, nilikuwa na sehemu kubwa katika mchezo mwingine. Huo mchezo ulishinda viwango vya juu katika mashindano ya uigizaji ya mkoa, kisha katika mashindano ya jimbo, kisha katika mashindano ya uigizaji ya New England.

Hatimaye, huo mchezo ulitupeleka katika mkoa wa Dartmouth College. Mwanafunzi aliyefuzu katika shule yetu ya upili ya Connecticut ambaye sasa alikuwa mwanafunzi wa Dartmouth akatuonyesha hayo maeneo ya chuo. Nilikuwa nikifikiri kupeleka ombi kule Yale, lakini baada ya kuona chuo cha Dartmouth, nilijua hapo ndipo nilipotaka kwenda.

Nilipokuwa mwanafunzi wa Dartmouth, nilishangazwa na mafanikio ya yuleyule mwanafunzi aliyefuzu kule shule ya upili ya Connecticut, aliyeitwa Peter. Kama rais wa jumuia yake, mchezaji wa kandanda wa timu ya chuo, mwanachama wa chama cha Green Key, na mwanafunzi wa kupata A katika kila somo (alipojaribu), alikuwa anaacha alama yake katika hiyo shule. Kisha taarifa zikafika: Unywaji pombe wa Peter ulikuwa umemharibu. Alifeli huko shule na akaondoka kwa sababu ya aibu.

Katika mwaka wangu wa kwanza kule Dartmouth, nilipokuwa naendelea kutafuta lengo la maisha yangu, nilijiuliza kama ningeweza kupata uhusiano binafsi na Mungu. Katikati ya utafiti wangu, Peter alijitokeza katika ibada

ya kanisa dogo la chuo. Akanipa mkono halafu akasema, "Chic, niko tofauti na vile nilivyokuwa kwa sababu nilimpata Bwana!" Punde baadaye, Peter akatoa ushuhuda wake wa kuvutia pamoja namimi na akanikaribisha kanisani kwake, ambapo nilikutana na kumpokea Yesu aliye hai.

Kama mtu niliyetaalimikia sheria katika matayarisho yangu, nilifikiri ningeenda katika shule ya sheria na kuwa wakili. Lakini nilipokuwa nakaribia mwisho wa chuo, Mungu akaniita katika huduma. Kisha nikaenda seminari kule Kansas City. Katika muda mfupi, nilikuwa ninapokea mialiko ya kuhubiri. Ijapokuwa rafiki zangu wengi wa seminari walikuwa wanaogopa kunena katika hadhara, mimi sikuogopa, nashukuru kwa mafunzo yangu na uzoefu wangu katika uigizaji.

Sasa ninatazama nyuma kwa furaha juu ya maisha katika huduma kama mchungaji, profesa wa seminari, mwinjilisti, na mwandishi.

Hata kabla ya kumjua binafsi, Mungu alikuwa ananiongoza. Hii ndiyo tunayoiita "neema ya kulainisha"—neema kabla ya kuokoka. Na kwa kuwa nimemjua, Mungu anaendelea kuniongoza.

Na hata wewe anaweza kukuongoza. Mungu anatamani kukuongoza wewe "katika njia za haki kwa ajili ya jina lake." Na kuhusu hilo je?

JULAI 31 **212**

# Ninamwamini Yesu Kristo

*Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho.*
*Yohana 6:40*

Ninamwamini Dkt. Carter. Yeye ni daktari wangu wa macho, na hii wiki, alinifanyia upasuaji wa mtoto wa jicho wa jicho langu la kulia. Kwa miaka mingi, Dkt. Carter ameisaidia familia yetu na vipimo vya macho, miwani, na matibabu ya magonjwa ya macho. Kwa sababu ninamwamini, nilikubali ushauri wake wa kufanyiwa huu upasuaji—nilimwamini atumie vifaa vinavyohitaji uangalifu zaidi, kutoa mtoto wa jicho jichoni mwangu na aweke lenzi mpya.

Dkt. Carter alinipa maagizo mengi ili nipate kujitayarisha kwa ajili ya huu upasuaji. Yalijumuisha:

- Kabla ya upasuaji, tumia tone moja la kiua vijasumu ya steroidi katika jicho lako, mara tatu kwa siku, ukiendelea katika vipindi vya kupunguzwa taratibu, kwa wiki nne baada ya upasuaji.
- Osha uso sawasawa usiku kabla ya upasuaji na asubuhi ya upasuaji
- Usile chakula wala kunywa maji baada ya saa 5.59 usiku kabla ya upasuaji (isipokuwa kwa dawa muhimu sana)
- Mwone daktari siku moja baada ya upasuaji, kisha wiki moja baada ya upasuaji, kuhakikisha kwamba kuna maendeleo katika mchakato wa uponyaji.

Kwa sababu, ninamwamini Dkt. Carter, nilitii maagizo haya kwa furaha.

Kulikuwa na kiasi cha muda cha wakati wa matayarisho katika kituo cha upasuaji—kupimwa shinikizo la damu, uchunguzi wa moyo na mapafu, kutuliza, oksijeni, matone kwa ajili ya upanuzi, sindano ya dawa ya ganzii kuzunguka jicho. Upasuaji wenyewe ulichukua dakika thelathini.

Kulikuwa na wakati katika historia ambapo hakukuwa na urekebishaji wa mtoto wa jicho uliojulikana. Sasa, ni vigumu kuamini kwamba jicho linaweza kufanyiwa upasuaji, kifaa kinaingizwa ili kuvunja mtoto wa jicho, kisha mtoto wa jicho anaondolewa kwa kuvutwa kutoka kwenye jicho na lenzi mpya inaingizwa ndani ya dakika thelathini! Ni ajabu sana!

Katika uchunguzi wa siku iliyofuata, nilikuwa ninampa Dkt. Carter shukrani nyingi sana na sifa. Nilikuwa ninaanza kuona vile ambavyo nilikuwa sijaona kwa miaka. Ninamwamini Dkt. Carter.

Ninamwamini Yesu Kristo. Watu wengi huchukua ushauri wa kumwamini Kristo kuwa unamaanisha tu, "Ninaamini yuko." Lakini "amini," kama lilivyotumiwa na Kristo, linamaanisha mengi zaidi ya hilo:

- Yakobo 2:19—"Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka."
- Yohana 6:36—"Lakini niliwaambia ya kwamba mmeniona wala hamwamini."
- Yohana 8:31—"Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli."
- Yohana 14:23—"Yesu akajibu, akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake."

Kwa hivyo, "kuamwamini" Yesu Kristo maana yake ni kumheshimu, kumtumaini yeye, kumpenda, kumtii, na kufuata maagizo yake. Hata unakuwa na kuonana naye kila mara (kunaitwa ibada) baada ya wewe kumkubali kwanzaa. Na kama inashangaza kwamba Dkt. Carter angeweza

kuondoa mtoto wa jicho na aweke lenzi katika dakika thelathini, inashangaza zaidi sana kutambua kwamba Yesu anaweza kufanya miujiza. Na kwa kweli unapokuja *kumwamini* Yesu, ni kawaida kwamba ungemshukuru, kumsifu, na kuishi kwa furaha pamoja naye milele.

**AGOSTI 1** **213**

# Kawaida

*Akatoka katika sinagogi, akaingia katika nyumba ya Simoni. Naye mkwewe Simoni, mamaye mkewe, alikuwa ameshikwa na homa kali, wakamwomba kwa ajili yake. Akasimama karibu naye, akaikemea ile homa, ikamwacha; mara hiyo akainuka, akawatumikia.*
*Luka 4:38-39*

*Na alipokwisha kunena, "alimwambia Simoni, Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki." Simoni akajibu akamwambia, "Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu." Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika.*
*Luka 5:4-6*

Katika picha kubwa, tatizo letu lilikuwa dogo sana. Lakini bado lilionekana kubwa kwetu.

Tuna TV tatu nyumbani kwetu. Hakuna TV hata moja iliyofanya kazi kwa zaidi ya wiki tatu. Tulibonyeza vidude vyote sahihi (na baadhi ambavyo havikuwa sahihi) katika vifaa vyetu vya kuendesha TV kwa mbali. Tulifanya kila kitu tulichojua. Hatimaye, tukapigia simu Geek Squad watume mtu aje avitengeneze. Nilimsihi mwakilishi wa simu atume mtu ambaye atakuwa mwelewa kwa wazee.

Baada ya kuomba ili nipate mtu sahihi wa kukarabati, suluhisho sahihi kwa kila TV, na jibu bora zaidi kwa ajili ya kile kilicho rahisi zaidi na wakati, Dominic akapiga simu akasema atakuwa fundi wetu wa matengenezo.

Kabla tu ya Dominic kufika, tuligundua kwamba hilo boksi la waya la TV ya kwanza lilikuwa limechomolewa kutoka kwenye umeme. Katika sekunde sitini, ilikuwa inafanya kazi tena.

Dominic, mtu mwelewa sana alirekebisha kitu kimoja katika hilo boksi la waya la TV ya pili, na katika dakika tano, hiyo nayo ikawa inafanya kazi.

TV ya tatu ilikuwa ina laini zilipopita juu ya kioo na zilikuwa zinatoa harufu isiyokuwa ya kawaida ya kemikali zilizokuwa zinaoungua. Dominic akasema hii TV mzee itakakuwa ghali sana kukarabati—ingekuwa vizuri tununue nyingine. Tukaeleza kwamba, kwa sababu ya onyo la serikali la kuhusu kufanya ununuzi katika makundi makubwa ya watu wakati huu wa tandavu ya korona, hatukutaka kwenda kuchangamana na watu hadharani.

Nikauliza, "Dominic, tukikwambia kile tunachotaka, utakinunua na utuwekee?" Dominic akasema ndio.

Mara tu tulipochagua ile ya $149.99 iliyokuwa kwenye punguzo maalumu, Dominic alirudi dukani, akachukua hiyo TV na vifaa muhimu, na akaiweka katika muda wa saa mbili. Hata aliondoa hiyo TV yetu ya zamani bila malipo. Hiyo ilikuwa ni afueni kubwa kwetu—na jibu maalum kwa maombi yetu. Asante Bwana! Si vigumu kumfuata na kumtumikia Mungu anayejali hata mambo ya kawaida ya maisha yetu.

Kama unafikiri ninajiamini mno, tafadhali kumbuka mafungu yetu ya Maandiko: Yesu alimponya mkwe wa Simoni aliyekuwa na homa kali. Pia alimwongoza Simoni na wavuvi wenzake hadi mahali pazuri zaidi pa kuvua baada ya kukesha usiku wote bila kupata kitu. Kwa mwongozo wa Yesu, walishika samaki wengi sana hata wakajaza mitumbwi miwili. Katika visa hivi, Yesu alitatua shida za familia, afya, na za kazi za mtu mmoja, simoni. Zilikuwa shida za kibinafsi katika picha kubwa—lakini zilikuwa shida zilizokuwa na maana kwa moyo na maisha ya huyu mwanamume.

Punde tu baada ya wale wavuvi kufanikiwa, "Yesu alimwambia Simoni, 'Usiogope; tangu sasa utakuwa ukivua watu.' Hata walipokwisha kuviegesha pwani vyombo vyao, wakaacha vyote wakamfuata" (Luka 5:10–11). Simoni, ambaye baadaye aliitwa Petro, alikuwa mmoja wapo wa viongozi wakubwa zaidi wa kanisa la kwanza.

Je, unaelewa ni kwa kiasi gani Yesu anavyojali kuhusu matukio ya kawaida maishani mwako? Basi kwa nini usimfuate? Au, kwa maneno mengine, kama unatafuta chakula au kinywaji au nguo, "Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33).

# Alivuka Mpaka

*Sauti ikamjia mara ya pili, ikimwambia, "Vilivyotakaswa na Mungu, usiviite wewe najisi."*
*Matendo 10:15*

Miaka iliyopita, tulikuwa na maandamano ya ubaguzi wa rangi katika mji wetu, na nilifadhaika.

Petro alikuw Myahudi mwangalifu sana lakini alikuja kumjua, kumpenda, na kumfuata Yesu Kristo. Usuli wake wa Kiyahudi ulikuwa umemfundisha kujitenga na watu wa Mataifa mengine. Sasa, katika maono, Mungu alikuwa anamwongoza apate kuvuka mpaka—na awafikie watu Mataifa, pia Wayahudi, na injili. Petro alipokuwa bado anajaribu kutafakari kile alichokiona, wanaume watatu wakabisha mlangoni pake kumwita aende nyumbani kwa mtu wa Mataifa, akida wa kirumi aitwaye Kornelio. Roho akamwambia Petro, "Ni mimi niliyewatuma" (Matendo 10:20). Kwa hivyo, Petro akaenda, na kwa kufanya hivyo, akavuka mpaka pamoja na injili (10:23–48).

Wakati wa maandamano ya ubaguzi wa rangi katika mji wetu, nilijiuliza ninaweza kufanya nini. Sikufikiri maandamano ya kupinga hayo kuwa suluhisho. Kwa hivyo nilikuwa na wazo: je, nikifanya tu jambo rahisi? Kinyozi wangu alikuwa Mwafrika Mmarekani, na nilikutana na yeye tu kwa sababu ya kunyolewa nywele. Je, mimi na Nancy tukimkaribisha Arby (kinyozi wangu) na mkewe, Joyce, kwa ajili ya mlo wa jioni? Tukafanya hivyo, na tukafurahia jioni iliyojaa chakula kizuri, ushirika wenye upendo, na kuelewana na kuheshimiana. Kilikuwa kitu kidogo sana—lakini ingekuwaje kama raia elfu kumi wa mjini kwetu wangefanya jambo hilo kwa kipindi cha wiki mbili?

Maisha yangu yamejawa na kuvuka mipaka ya kitamaduni. Imekuwa baraka kuingiliana na wanafunzi wa huduma, na kuwa na urafiki wa kukuza, katika maisha yangu yote, na watu wenye usuli tofauti tofauti. Kuvuka mipaka ni baraka.

# Wengine

*Akajibu akasema, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.*
*Luka 10:27*

Ukifanya vile andiko la leo linavyoagiza, utaurithi uzima wa milele (Luka 10:25–27). "Kumpenda Mungu" na "kumpenda jirani yako" kote ni muhimu. Hebu natufikiri kuhusu hiyo sehemu kuhusu "Mpende jirani yako."

Tim alipokuja kanisani kwetu na katika darasa la shule yetu ya Jumapili, alikuwa tayari amekamatwa kwa sababu ya uhalilifu wake na alikuwa anangojea kuhukumiwa. Mara ya kwanza alikuwa anasitasita na mwangalifu, lakini upendo wa watu, ushahidi wa wengi, na mahubiri yenye nguvu vilishinda siku hiyo. Alikuwa ametubu dhambi zake na akapokea msamaha siku chache awali katika gereza la jimbo. Mara ya kwanza, alitoa maisha yake kikamilifu kwa Mungu na akakua kiroho. Hatimaye, akahukumiwa kwenda gerezani na amefungwa kwa miaka sita.

Kila Krismasi, darasa letu la shule ya Jumapili hutuma zawadi za kifedha kwa watu thelathini au zaidi. Tim alipokea dola mia moja katika akaunti yake ya kamisheni. Akiwa na vitu vichache sana vya faraja vya maisha, nilichukulia angeitumia kwa mahitaji yake. Lakini sasa nikapokea barua ifuatayo kutoka kwake.

> *Mimi ni mtu niliyebarikiwa! Si hicho ni kirai cha ajabu kutoka kwa mfungwa katika taasisi ya urekebishaji? Kuna nyakati ambapo mashaka huingia katika akili yangu. Kisha ninapokea barua, mafunzo ya Biblia, kutembelewa, au hata pesa, na hayo mashaka yanaondoka.*
>
> *Ninataka kushukuru darasa la shule ya Jumapili kwa kunikumbuka wakati wa Krismasi. Darasa lilitoa, kwa hivyo niliweza kutoa. Kulikuwa na wachache wetu waliochangia sherehe ya Krismasi kwa ajili ya sisi sote hamsini katika kitengo chetu. Kulikuwa na jamaa wengine ambao hawakuitaka, lakini wengi walishukuru. Nimejumuisha barua ya itikio la bwana mmoja. Tafadhali hakikisha kwamba hilo darasa linajua kuwa ninashukuru na ninafurahia sana hiyo zawadi.*

*Mtu anayeendesha ibada ya kanisa dogo ninalohudhuria mara nyingi husema, "Hatukukamatwa; tuliokolewa." Wakristo wote wanaweza kusema Mungu aliwaokoa, na Mungu yuko tayari kuokoa kila mtenda dhambi anayeomba aokolewe.*

Hapo chini ni sehemu ya hiyo barua ambayo Tim alipokea kutoka kwa mfungwa mwingine:

*Mimi binafsi ningependa kuwashukuru ninyi jamaa kwa jitihada zenu zote mlizofanya kumpa kila mtu sherehe nzuri namna ile. Ninakumbuka mwaka jana mlifanya vivyo hivyo. Ninyi jamaa kwa kweli mmeishi vile ninavyoamini Biblia inasema Mkristo wa kweli ni nani . . . . Ninyi jamaa mmethibitisha kuwa nuru inayong'ara ninayoamini Biblia inazungumzia. Ninamshukuru na ninawaombea mwendelee vyema.*

Earl kutoka katika darasa letu la shule ya Jumapili ni kielelezo cha maana ya kumpenda jirani yako ni nini. Karibu kila wiki sita, Earl huendesha gari hadi upande ule mwingine wa nchi, hulala huko katika hoteli, kisha huenda kumwona Tim na, akiruhusiwa na gereza, humpelekea Tim chakula cha nyumbani.

Kwa hivyo, iwe ni darasa linalotuma zawadi kwa wahitaji, au Tim aliyefungwa kuonyesha kuwajali wale wafungwa wengine hamsini kwawa kitendo chao, au Earl kusafiri katika wikiendi zake kwenda kumwona Tim, kule nje kuna Wakristo wanaowapenda wengine. Ni nani anayehitaji upendo wako leo?

**AGOSTI 4** **216**

# Je, Mungu Akiniuliza . . .

*Nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?*
*Luka 10:25*

Kijana mmoja wa Kidachi alikuwa karibu kupanda ndege ya Malaysian Flight 17 kutoka Amsterdam hadi Kusini Mashariki mwa Asia wakati ghafla, alipohisi kuhangaika na akamrudia mamake mbio. Akaropoka, "Ninaogopa hiyo ndege itaanguka. Je, nikifa?" Mamake akamhakikishia kwamba alikuwa ameenda na ndege awali na kwamba kakake angekuwa pamoja naye.

Akaendelea kuuliza maswali mengi zaidi:

1. Je, nikifa?

2. Je, Mungu Akiniuliza swali?

3. Je, ninapaswa kumwambia nini?

Hii hadithi ilikuja kutoka katika mahojiano ya televisheni yaliyofanywa na mamake huyo kijana baada ya hiyo ndege ya Malasia kudenguliwa katika anga ya Ukraini—hiyo ndege iliingia katika mashambuliano kati ya waasi wa Urusi wanaotaka kujitenga na wanajeshi wa Ukraini mwaka 2014. Kila abiria aliyekuwamo—kama watu mia tatu—alikufa.

Hii ni hadithi ya kuhuzunisha sana! Na ni swali muhimu sana kutoka kwa huyo kijana: "Je, Mungu Akiniuliza swali?"

Je, Mungu akikuuliza *wewe* swali? Dkt. James Kennedy aliandika, "Tuseme unapaswa kufa leo usiku na usimame mbele ya Mungu naye akwambia, 'Kwa nini nikuruhusu uingie kwangu mbinguni?' Ungemwambia nini?"[113]

Hilo swali ni la kina sana kuliko unavyoweza kufikiri. Katika Luka 10, mwalimu wa sheria ya kidini kwa kweli alimwuliza Yesu, "Nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" Yesu akamwambia jibu: Mpende Mungu utu wako wote na jirani yako kama nafsi yako.

Uzima wa milele ni zaidi ya mbinguni, lakini kwa sababu ni wa "milele," unajumuisha mbinguni. Yesu akasema, "Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma" (Yohana 17:3). Uzima wa milele ni *kumjua* Mungu Baba na *kumjua* Yesu Kristo—uhusiano.

Kumpenda Mungu na kumpenda jirani yako ndilo sharti ambalo Yesu analiweka ili mtu aurithi uzima wa milele. Lakini ni nani anayeweza kufanya hivyo kwa jitihada za kibinadamu pekee? Upendo wa aina hiyo unawezekana tu peke yake kwa msaada wa kiungu. Kwa hivyo Paulo anatwambia katika Warumi 5:5, "Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi."

Swali kuhusu kuingia mbinguni linajibiwa na kifungu maarufu Yohana 3:16: "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Ni lazima tuelewe kwamba neno "amini" hapa lina maana zaidi ya kukubali kiakili; linamaanisha kujitoa kwa Yesu. Hili linatuelekeza katika uhusiano wa kwendelea, na Kristo.

Ninashukuru, unaweza kuwa na *hakikisho* na *kujua* kwamba uko sahihi na Mungu. Warumi 8:16 inaahidi, "Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu."

---

113. Dkt. James Kennedy, *Evangelism Explosion* (Wheaton, IL: Tyndale House, 1996), 33.

Tom Phillips, aliyekuwa rais wa Raytheon Corporation, alijua hili kwa hakika. Alimsimulia Charles Colson hadithi yake, msaidizi wa aliyekuwa rais Richard Nixon, baada ya Colson kufungwa gerezani kwa uhalifu uliokuwa unahusiana na Watergate. Baadaye, Colson alikuwa mfuasi wa Kristo na mpiganiaji wa mageuzi ya gerezani. Hili ndilo alilosema Phillips:

> Sikuonekana kuwa na chochote cha maana. Yote yalikuwa hapo juujuu. Vitu vyote maishani havina maana yoyote kama mwanadamu bado hajavumbua kile kilicho chini yao.
>
> . . . Usiku mmoja nilikuwa kule New York kwa ajili ya biashara na nikatambua kwamba Billy Graham alikuwa na injili katika Madison Square Garden . . . Nikaenda—nikitaka kujua, nakisia—nikitumaini labda ningepata majibu fulani. Kile alichosema Graham usiku ule kiliweka kila kitu mahali pake kwangu. Niliona kile kilichokuwa kinakosekana—uhusiano wa wa kibinafsi na Yesu Kristo, ukweli kwamba nilikuwa sijawahi kamwe kumwomba aingie maishani mwangu, nilikuwa zijayatoa maisha yangu kwake. Kwa hivyo nikafanya hivyo—usiku uo huo pale katika injili.
>
> . . . Nikamwomba Kristo aingie maishani mwangu, na niliweza kuhisi uwepo wake pamoja nami. Amani yake ndani yangu. Niliweza kuhisi Roho wake akiwapo pamoja nami. Kisha nikaenda nje kwa ajili ya matembezi mimi peke yangu katika barabara za New York. Sikuwa nikipenda New York awali, lakini huu usiku ulikuwa mzuri. Nilitembea nikipita nyumba hadi nyumba. Kila kitu kilionekana tofauti kwangu. Kulikuwa na manyunyu ya mvua, na mataa ya jiji yalitoa mng'ao wa dhahabu. Kuna kitu kilichokuwa kimenitokea, na nilikijua.[114]

AGOSTI 5 **217**

## Natushikilie wa Nguvu

*Na mlishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke;*
*maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu.*
*Waraka kwa Waebrania 10:23*

114. Charles W. Colson, *Born Again* (Old Tappan, NJ: Fleming H. Revell, 1977), 110.

Akiwa amekuzwa chini ya mahubiri ya mikutano ya kambi katika kanisa la Kimethodisti, alijua umuhimu wa uhusiano wa kibinafsi na Kristo. Lakini, kwa miaka, alimwacha nje ya maisha yake. Kisha, alipokuwa amekaribia umri wa miaka hamsini, alimpokea Mwokozi.

Kila kitu kilichokuwa karibu naye kilimshinikiza amwache Yesu Kristo. Akaangalia hali yake. Akiwa amepewa ujasiri wa kuingia Patakatifu pa Patakatifu (Waebrania 10:19) na kuhani mkuu (10:21), alijua kulikuwa na *upaji* wa kutosha kwa ajili ya ushindi wake. Kwa hivyo akamsongelea Mungu (10:22), akashikilia imani yake (10:23), na hata akawachochea na wengine wawe na upendo na kazi njema katika ushirika wao wa kusaidiana (10:24–25). Kwa maneno mengine, aliweka neema ya Mungu katika *utendaji*.

Hata hivyo hilo suala liligonga mwamba, wakati watu wengine walipoanza kumshinikiza arudi katika mtindo wa maisha wa kuendelea kuasi (10:26). Watu hawa walipokuwa wanamhimiza amwache Kristo, akakataa kujadiliana nao na akaweka wazi azima yake kwa kunena wazi, "Sitaasi niende Jehanamu!" Aliishi katika ushindi wa kiroho.[115]

AGOSTI 6 **218**

# Mungu Anapojitokeza

*Yakobo akashika njia yake na malaika wa Mungu wakakutana naye.*
*Mwanzo 32:1*

Baba mkwe wake alikuwa amemkasirikia, kakake alikuwa amemkasirikia, na Yakobo alikuwa amekwama katikati, akijaribu kulinda mifugo yake, watoto wake, wake zake, na yeye mwenyewe. Akiwa katikati ya Labani aliyemkasirikia na Esau aliyemkasirikia, Yakobo akazidi kuwa dhahiri kwa Mungu, akazidi kuwa macho zaidi kuliko awali. Akiwa katika hali hiyo mbaya, malaika wa Mungu wakakutana naye.

Kufikia wakati wa Matendo ya Mitume, kanisa la kwanza lilimtarajia Mungu ajitokeze—apate kuingilia kati, anene kila mara. Katika kitabu cha Matendo, kuna visa ishirini na tisa ambapo tunaona uongozi wa kiungu

115. Awali ilichapishwa katika *Come Ye Apart* Machi–Aprili–Mei 1971 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 87. Imetumiwa kwa ruhusa (Chapisho hili likawa *Reflecting God*.)

wa Roho. Matendo 13:2 ni mfano wa hivi visa: "Roho Mtakatifu akasema, 'Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia.'"

Mara nyingi ninaomba na kuomba na sipokei jibu. Wakati mwingine ninatamani Mungu ajitokeze na kunena nami nipokuwa ninaomba. Rees Howells alikuwa akisema, "Maana ya maombi ni majibu." Hata hivyo, Howells pia alisema, "Maombi ya kuleta matokeo lazima yawe maombi ya kuelekezwa."[116] J. G. Morrison aliandika juu ya "imani ya kupata" na akafananisha na waya "inayounganisha roho na Mungu, kupitia hiyo yeye hufanya kazi apate kutoa uwezo wake juu ya muumini, kwa kitu kile kile ambacho kwa hicho imani yake inasimama."[117]

Tulipokuwa katika kazi yetu ya kwanza ya uchungaji, kanisa lilokuwa limeanzishwa, mapato yetu yalikuwa kidogo sana. Nikaomba, "Bwana, ninahitaji gari mpya. Mimi ni maskini sana hata siwezi kununua gari nyingine na mpumbavu sana kuweza kutengeneza hii niliyo nayo." Baada ya hilo ombi, Roho wa Mungu akanipa imani, na nikahakikishiwa kwamba gari imo njiani inakuja. Katika dakika chache tu simu ikaita, na mamangu akanambia kwamba rafiki alikuwa ameamua kunipa gari yake mpya.

Wakati mwingine Roho huweka mzigo au ndoto juu ya moyo wako ambao hautaondoka. Nilikuwa nimemwona Shahrzad, mwanamke Mwislamu, akimkubali Kristo kama Mwokozi na Bwana mbele ya macho yangu. Yeye na mumewe, Albert, wakawa rafiki zangu wapendwa. Katika mwaka wao wa ishirini wa ndoa yao (kuweka mpya nadhiri zao kwa kuwa sasa ni Wakristo), nilikutana na rafiki zao Waislamu. Kwa miezi kadhaa baadaye, mzigo ulitua moyoni mwangu: "Ongoza mafunzo ya Biblia kwa ajili ya hawa rafiki zako Waislamu." Baada ya kama miaka mitatu, siku ya Jumanne usiku, watu kumi na watatu kati yetu tulikutana kwa ajili ya mafunzo ya Biblia. Isipokuwa mimi na mke wangu, kila mmoja alikuwa ametoka katika usuli wa Kiislamu au alikuwa ameoana na mtu kutoka katika usuli wa Kiislamu.

Oo, naomba nimtarajie Mungu ajitokeze—na naomba Roho aniongoze ili niwe na imani katika majibu ya Mungu.

---

116. Norman Grubb, *Rees Howells, Intercessor: The Story of a Life Lived for God* (Philadelphia: Christian Literature Crusade, 1952), 43.

117. J. G. Morrison, *Achieving Faith* (Titusville, PA: The Allegheny Wesleyan Methodist Connection, n.d.), 34–35.

# Kuzaa Matunda

*Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; na mti mwovu huzaa matunda mabaya. Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua.*
*Mathayo 7:17, 20*

Ndiyo, alisema hivyo! Yesu alisema matendo tunayoona katika maisha ya watu hudhihirisha hali halisi ya mioyo yao. Maneno ya kiungu hayataonekana yanapolinganishwa na matendo yasikuwa ya kiungu.

Joe na Carol walikuwa wamehudhuria darasa letu la shule ya Jumapili. Siku moja, nikaenda kuwatembelea nyumbani kwao, na nilipokuwa hapo, tukaingia katika majadiliano kuhusu maisha yao ya kiroho. Kwa njia mwafaka, nikamwuliza Joe kama alikuwa na hakika angeenda mbinguni.

Akajibu kitu kama hiki, "Oo ndiyo, ninajua nitaenda mbinguni. Kama miaka ishirini na saba iliyopita, nilimkubali Kristo kama Mwokozi wangu. Kwa hakika, ninakubali nimekuwa nikizini na wanawake wengine, nina midomo michafu, ninalitaja jina la Mungu bure, ni—" Akasita. "Huniamini, sivyo?"

Nilikuwa nimeshtuka. Nilikuwa sijasema neno lolote. Nakisia mwonekano usoni mwangu ulionyesha kutoamini. Hatimaye, nikasema, "Joe, si kama ninakuamini. Unasema kwamba unaenda mbinguni, na kisha unanipa orodha ya matunda ya maisha yako. Yesu alisema, 'Mtawatambua kwa matunda yao.' Ni kitu gani kingine ninaweza kudhania?"

Hebu linganisha hilo na hili tukio. Kasisi wa Kiprotestanti aliyekuwa mgeni kwetu alikuwa anafanya kazi katika hospitali ya jamii ya Kikatoliki na akapitia ofisi yetu ya kanisa kutuarifu kwamba Jack Wilson alikuwa katika nyumba ya wagonjwa mahututi. Jack alikuwa amemwambia huyo kasisi kwamba kanisa letu ndilo kanisa lake. Yule kasisi akafikiri tungependa kuwasiliana na Jack.

Wafanyakazi wa ofisi walifadhaika. Hilo jina halikuwakumbusha chochote. Wakaanza kufanya utafiti. Mhudumu aliyestaafu akakumbuka hilo jina. Mara ya mwisho Jack alipohudhuria ilikuwa zaidi ya miaka kumi na mitano awali. Kabla siku kuisha, mhudumu kutoka kanisani kwetu alikuwa kando ya kitanda cha Jack akiwa na Maandiko, maombi, na faraja.

Huyo kasisi baadaye alisimulia kile alichokiona. Alisema, “Mle ofisini mlikuwa na wanawake watatu. Walifanya kazi nzuri. Vizuri kabisa! Mmoja alitoka nyuma ya kaunta na akaomba pamoja nami. Huu ndio Ukristo halisi! Ninaenda makanisa mengine na kuwaomba wamwangalie mtu. Wanasema, ‘Hayuko katika nakala yetu ya utoaji.’ Wanaonekana hawana mambo mengine wanayojua kuhusu huyo mtu. Nimefurahishwa sana na kanisa lenu.”

“Kazi nzuri”—“vizuri kabisa”—“Ukristo halisi”—“nimefurahi sana.” Hayo ni matunda mema. Hayo ni matunda ya kumcha Mungu. Huo ni uthibitisho kuwa huo Ukristo ni wa dhati.

Wewe unazaa matunda ya aina gani?

**AGOSTI 8** **220**

# Kutoka Kuwa Mhalifu hadi kwa Kristo

*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Mgiriki pia.*
*Warumi 1:16*

Uwezo wa Mungu kwa ajili ya wokovu—huo ni mkubwa namna gani? Ni mkubwa wa kutosha kumbadilisha Joe!

Joe alilelewa akiwa Mkatoliki. Wakati mwingine, Mungu alijaribu kunena naye. Mara moja, Mungu alimwonyesha maono ya Joe kuwa nyuma ya mimbari. Joe, akaitikia kwa kumkimbia Mungu. Tangu umri wa miaka tisa hadi wa arobaini na mitano, alitumia mihadarati, akauza mihadarati, na kuiba. Alikubali, “Maisha yangu yote, nilikuwa mhalifu wa kupindukia.”

Alipoteza nyumba yake kwa sababu ya mtindo wake wa maisha. Alipoteza ndoa yake. Baada ya wakati wa kuwa huru dhidi ya mihadarati, alirudia umalaya na kuuza mihadarati kwa sababu alihitaji pesa.

Mwaka 2009, Joe alikamatwa kwa kosa la utakatishaji pesa. Polisi walipovunja mlango wake, walikuta heroini nyingi nyumbani kwake, na wakampeleka gerezani. Siku moja usiku, aliamshwa ghafla kutoka usingizini katika selo yake. Alimsikia Mungu akimwuliza, *“Je, umetosheka? Je, uko tayari kunifuata?”* Katika wakati huo, alijitoa kumfuata Kristo, na tangu miaka hiyo, maisha yake yamebadilika.

Joe alimaliza kifungo chake cha nje Agosti 2017. Amewekwa wakfu na kanisa lake na akawa mshauri wa kibiblia katika utume wenye nguvu wa

kuokoa jiji. Sasa Joe huwaonyesha mamia ya watu waliokata tamaa nguvu kuu: "Uwezo wa Mungu uletao wokovu." Je, hiyo nguvu inatosha kukuokoa wewe dhidi ya changamoto unazokabiliana nazo leo?

AGOSTI 9 **221**

# Laiti Watu Wangu Wangenisikiliza!

*Mimi ndimi BWANA, Mungu wako, Niliyekupandisha toka nchi ya Misri; Fumbua sana kinywa chako nami nitakijaza. Lakini watu wangu hawakuisikiliza sauti yangu, Wala Israeli hawakunitaka.*
*Zaburi 81:10-11*

Alimkubali Yesu, na Mungu akamkomboa dhidi ya mambo mengi sana:

- Mzigo wa hatia
- Ghasia ya kununua mikopo bila nidhamu
- Kupiga kelele kwa ukali kwa roho ya ugomvi
- Chupa mia za bia kwa wiki
- Uchungu wa neva zilizofika ukingoni

Hebu fikiri mshangao wangu alipoanza kwenda mbali na Mungu aliyekuwa amemfanyia mambo mengi sana. Alikuwa ameniambia, "Niambie kama utaniona nikirudi nyuma." Lakini nilipomfuata kwa hayo maneno yake, hakuweza kukubali.

Hatimaye, akachukua maisha yake mikononi mwake kabisa. Alienenda katika ushauri wake mwenyewe. Hatimaye, kwa kuwa alisisitiza kufanya hivyo, Mungu akamwacha aende katika tamaa za moyo wake (Zaburi 81:12).

Kisha siku moja usiku, simu ikalia, na akaomba niende kwake mara moja—alikuwa ametiwa korokoroni.

Laiti angekuwa amesikiliza![118]

118. Awali ilichapishwa katika *Come Ye Apart* Machi–Aprili–Mei 1971 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 84. Imetumiwa kwa idhini. (Chapisho hili likawa *Reflecting God*.)

# Je, Uso Wako Hung'aa?

*Hata ikawa, Musa aliposhuka katika mlima Sinai, na zile mbao mbili za ushuhuda zilikuwa mkononi mwa Musa, hapo aliposhuka katika mlima, Musa hakujua ya kuwa ngozi ya uso wake iling'aa kwa sababu amesema naye.*
*Kutoka 34:29*

Hatimaye, baada ya kukabiliana na Farao kupitia yale mapigo kumi ya hukumu dhidi ya Misri, Musa alipokea ruhusa na kuondoa Misri. Aliongoza watu wake waliokuwa zaidi ya milioni 1.5 kupita katika maji ya Bahari ya Shamu yaliyofunguliwa, na jeshi la Misri lililojaribu kuvuka baada yao lilizama. Kwa miaka arobaini, aliwaongoza Waisraeli kupitia jangwani na utoaji wa Mungu wa kimiujiza wa mana, kware, na maji kutoka mwambani. Mwishowe, Musa akawafikisha Yordani na akamwachia Yoshua uongozi awaongoze waingie katika nchi ya ahadi.

Uongozi wote wenye nguvu wa Musa ulikuwa kwa sababu ya *uhusiano wake wa karibu* na *Mungu*. Musa alikutana na Mungu juu ya Mlima Sinai kwa ajili ya kupewa zile Amri Kumi kwa mara ya pili. Hapa kuna maelezo ya ule mkutano wao:

> BWANA akashuka ndani ya lile wingu, akasimama pamoja naye huko, akalitangaza jina la BWANA. Bwana akapita mbele yake, akatangaza, "BWANA, BWANA, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli, mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi. Wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne" (Kutoka 34:5–7).

Kisha Bwana akamwahidi Musa, "Nitatenda miujiza, ya namna isiyotendeka katika dunia yote, wala katika taifa lo lote" (34:10).

Kwa hivyo tunaweza kuelewa ni kwa nini uso wa Musa ulikuwa unang'aa aliposhuka kutoka Mlima Sinai: "uso wake uling'aa kwa sababu amesema NAYE."

Je, kuna mtu yeyote mwenye uso wa kung'aa baada ya kuja kwa Kristo? Je, baadhi ya watu bado wanaweza kung'aa, hata ingawa si wakuu kama Musa?

Stefano ni mmoja wa washiriki saba waliochaguliwa kugawa chakula kwa wajane katika kanisa la awali. Alisimama kwa ujasiri mwingi sana kwa ajili ya Yesu hata wale waliopinga Ukristo wakampiga mawe hadi akafa. Siri yake ilikuwa ni nini? Kuhusu kuchaguliwa kwake kuwa mmoja wa wale Saba, rekodi inasema, "Wakamchagua Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho Mtakatifu" (Matendo 6:5).

Kabla ya kifo chake tu, watu walipokuwa wanabishana kuhusu Stefano na kuita mashahidi wa uongo dhidi yake, rekodi inaarifu, "Watu wote walioketi katika ile baraza wakamkazia macho yao, wakamwona uso wake kuwa kama uso wa malaikal" (Matendo 6:15). Alikuwa anang'aa.

Hatimaye, alipokuwa karibu kupigwa mawe, tunasoma, "Lakini yeye akijaa Roho Mtakatifu, akakaza macho yake, akitazama mbinguni, akauona utukufu wa Mungu, na Yesu akisimama upande wa mkono wa kuume wa Mungu" (7:55).

Wakati mmoja niliingia katika nyumba iliyomcha Mungu na nikaona ilikuwa inang'aa. Nimemjua Peter, Juanita, Kelli, na wengine ambao nyuso zao za kumcha Mungu ziling'aa. Je, wewe hunena na Bwana, na je umejazwa Roho Mtakatifu? Je, uso wako hung'aa?

**AGOSTI 11** **223**

# Mito ya Maji Yaliyo Hai

*Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.Na neno hilo alilisema kuhusu Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa*.
*Yohana 7:38-39*

"Je, ni kweli?" Akamwuliza huyo mhudumu, "Je, kwa kweli inasema mto wa maji yaliyo hai itatoka?" Akamjibu kwamba haukuwa mto tu, bali *mito*. Katika Yohana 4:14, Yesu alikuwa ameahidi "chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele." Sasa anaongeza wingi na kuwa "mito."

Roger alipopiga magoti kwenye madhabahu ya Filipino na kumwomba Mungu amtakase kabisa na amjaze Roho Mtakatifu, Mungu alijibu. Kwa uso uliong'aa, Roger baadaye alishuhudia, "Moyo wangu umesafishwa. Nina

furaha. Ninaweza kuimba, ninaweza kupiga kelele. Ninataka kuwa na ndugu zangu Wakristo."

Wiki iliyofuata, Roho aliyetiririka kupitia kwake aliendа mbali zaidi ya wale rafiki zake Wakristo. Kwa miaka kumi, kaka yake Roger alikuwa amekuwa adui yake kwa sababu ya kutoelewana kuhusu mpango wa biashara. Tangu ajazwe Roho, Roger alikuwa anamwombea kaka yake. Siku moja, alipofika nyumbani, alimkuta kaka yake anamngojea. Kaka yake akaomba msamaha, na wakapatana. Kisha Roger akamshuhudia, na kaka yake akamkubali Kristo. Wiki iliyofuata, Roger alikuwa katika mlo wa jioni nyumbani kwa kaka yake.

Roger akatoa taarifa ya mabadiliko mengine katika kuingiliana kwake na watu wengine: "Awali, nilikuwa naogopa kunena na watu kuhusu Kristo. Sasa nina ujasiri. Ninashangaa—nimenena na watu watatu kuhusu Bwana, na wote wameokolewa. Ninahisi kana kwamba mimi ni mshindi nikiwa na Bwana wangu."

Mito ya maji yaliyo hai inatiririka. Hakikisha unaingia katika huo mtiririko huo!

AGOSTI 12 — 224

# Ni Jozi Gani ya Mikono?

*Daudi akauliza kwa BWANA, akasema, "Je! Nikiwafuata jeshi hili, nitawapata?" "Naye akamjibu", Fuata; kwa kuwa hakika utawapata, nawe "hukosi utawapokonya wote."*
*1 Samweli 30:8*

Kabla Jim Elliot hajawa mmishenari jasiri kwa kabila la Huaorani au kutia madoadoa ya damu yake ya mfiadini katika Mto Kurarai, alikuwa mwanafunzi wa chuo. Wakati huo, wakati mmoja alitoa hutoba kwa wanafunzi wapya waliokuwa wameingia ambayo aliieleza kuwa "kile ambacho, mimi kama mtu ninayemaliza, ninatamani mtu angeniambia nilipokuwa mwanafunzi mpya." Katika hiyo hotuba, Jim alisema kile alichokuwa amejifunza: zaidi ya kuamini na kutenda, kuna kuwa ulivyo, na unaweza *kuwa ulivyo* unapokuwa umejifunza kuweka maisha yako yote mikononi mwa Mungu. Ukweli huu unatakiwa ushikiliwe dhidi ya moja wapo ya sababu inayowafanya watu wengi zaidi washindwe: "Nililichukua katika mikono yangu mwenyewe."

Sauli alimwona Daudi kuwa tisho. Ijapokuwa Daudi alikuwa ameituliza roho ya Sauli kwa muziki wake na kuwaua majitu wa kwa ajili ya ushindi wa Israeli, Sauli alimdanganya Daudi mara nyingi na kujaribu kumwua.

Mfalme wa Wafilisti alikuwa amemtoa Daudi katika cheo chake cha kijeshi na kumwacha aende zake. Baada ya kusafiri kwa siku tatu (maili hamsini), Daudi aliwarudisha watu wake Ziklagi. Huko aligunuda kwamba Waamaleki walikuwa wamechoma mji na wakachukua mateka wake wao wote na watoto wao Watu wa Daudi walikuwa na uchungu sana dhidi ya Daudi, lakini Daudi hakuenda katika njia hiyo; aliona ni vyema kutafuta nguvu katika Bwana (1 Samweli 30:6). Akamwendea Bwana katika maombi na akaliweka hilo tatizo mikononi wa Mungu. Aliposikia kutoka kwa Mungu, Daudi alifuata maelekezo ya Mungu. Matokeo yake, Daudi na jeshi lake wakarejesha jamaa zao wote na nyara (kif. 18–20). Kufikia sura ya 31, Sauli, aliyekuwa mara nyingi amechukua masuala katika mikono yake mwenyewe alikuwa amejiua.

Rhonda alikuwa amelia alipokuwa anamrudia Mungu, lakini alikuwa na wasiwasi kuhusu mijibizo ya watu wengine kule kazini kwake, ambako alikuwa amejulikana kama mwanamke wa ulimwengu. Atakabiliana vipi na sifa zake za kunywa na za kuaibisha? Je, achukue hiyo hali mikononi mwake mwenyewe na aridhiane? Hatimaye, alichagua kuweka hilo mikononi mwa Mungu, akitazama ahadi ya Wafilipi 4:6–7: "Msijisumbue . . . haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu . . . itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu." Akafanya hivyo, na Mungu akatenda.

Ann alitambua wauguzi kama Ruth na Cathy katika hospitali aliyofanya kazi. Ubora wa maisha yao ulikuwa chanzo cha nguvu. Kisha akatambua Dkt. John Cashman, alikuwa mwenye akili, mnyenyekevu, na mcha Mungu. Alikuwa daktari peke yake ambaye wauguzi walitia sahihi zao katika kadi zake za kustaafu—walimwita mtakatifu aliye hai. Ann alijiunga na kanisa lao kwa sababu alikutana na watu katika mahali pake pa kazi walioweka kazi yao mikononi mwa Mungu.

Umejiweka katika jozi gani ya mikono? Mother Teresa wakati mmoja alisema, "Niombeeni ili nisilegeze mikono yangu katika kuishika mikono ya Yesu, hata katika kisingizio cha kuwasaidia maskini."

AGOSTI 13 **225**

# Ni Mimi Peke Yangu—Oo Hapana!

*Hata baba yangu na mama yangu wakiniacha, Bali BWANA atanikaribisha kwake.*
*Zaburi 27:10*

Hajiri alikuwa mke wa pili, na alikuwa mjamzito. Sarai, mke wa kwanza alikuwa amekuwa tasa hata kufikia hapa. Hajiri alipoanza madharau, Sarai hakuweza kumvumilia—hata kwanza, Hajiri alikuwa mtumwa wa Sarai. Sarai alimtesa Hajiri, na Hajiri akakimbia.

Chochote kile ambacho Hajiri alikuwa amekosea, sasa alikuwa mahali pabaya. Akiwa njiani kwenda Shuri, akikimbia kutoka Kanaani kwenda Misri, alisimama karibu na chemchemi huko jangwani. Ilikuwa nadra kwa mwanamke kusafiri peke yake; alikuwa mjamzito; alikuwa mtumwa kutoka Misri. Familia yoyote aliyokuwa nayo katika uhusiano wake na Ibrahimu na Sarai ilikuwa imesambaratika. Je, mtu yeyote angemsaidia? Alikuwa peke yake—peke yake.

Hapo hapo, katika sehemu hiyo, hilo tatizo, kukata tamaa huko, alijitokeza: “Malaika wa Bwana akamwona” (Mwanzo 16:7). Malaika akamwambia arudi kwa Sarai, lakini pia akamwahidi mwana—Ishmaeli—na uzao “mwingi usiohesabika” (16:10). Hapo awali alihisi kuwa peke yake, sasa akatamka, “Wewe U Mungu uonaye,” na, “Nimemwona yeye anionaye” (16:13).

Nilikutana na Yesu Kristo, nikiwa mwanafunzi wa chuo; nilifurahi, nikaanza kumfuata. Chini ya miezi mitatu baada ya kuingia katika uhusiano wangu na Bwana, nilimtembelea mpenzi wangu. Hata hivyo, maswali kuhusu msichana niliyepanga kumwoa yalikuwa yamenichochea nimtafute Kristo. Nilipomwambia jinsi maisha yangu yalivyobadilika, akasema, “Baadhi ya mabadiliko nayapenda—baadhi ya mabadiliko siyapendi.” Nilipoenda nyumbani kumwambia mama yangu na baba yangu, mama yangu alifadhaishwa; baba yangu akakasirika. Tafadhali elewa kwamba watu watatu muhimu zaidi maishani mwangu wakati huo walikuwa mama yangu, baba yangu, na mpenzi wangu.

Siku moja, nilipokuwa nimerudi chuo, nikapokea barua mbili. Ile ya kutoka kwa mpenzi wangu ilisema, “Nafikiri una wazimu. Sitaki kukuona tena.”

Kwa mshtuko nikafungua barua iliyotoka kwa mama yangu na baba yangu. Maneno ya baba yangu yalikuwa, "Kwa sababu ya msimamo uliochukua, hutapata tena msaada wa kifedha kutoka kwangu."

Nililia. Nilikuwa peke yangu—peke yangu.

Nikiwa bado mpya katika imani yangu, sikujua Biblia yangu vizuri, lakini bado nilijua ilinibidi nirudi katika Neno. Bila kujua kwamba mstari kama huo umo katika Biblia, nilisoma Zaburi 27:10: "Baba yangu na mama yangu wameniacha, bali Bwana atanikaribisha kwake" . Saachache baadaye, nilikuwa katika ibada ya kila siku ya kanisa dogo. Nilishangaa nilipomsikia msomaji wa Andiko akisoma, "Baba yangu na mama yangu wameniacha, bali Bwana atanikaribisha kwake". Baadaye huo mchana, nilihudhuria mkutano wa maombi wa wanafunzi wa kila siku. Mwanafunzi mmoja (aliyekuwa hajui chochote kuhusu hali yangu) alisema alihisi anaongozwa kusoma, "Baba yangu na mama yangu wameniacha, bali Bwana atanikaribisha kwake" .

Si Hajiri—si mimi—si wewe. Chochote kile unachopitia leo, hauko peke yako!

**AGOSTI 14** **226**

# Mungu Aliiweka Hapa

*Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; na asiyeaminika katika lililo dogo, huwa haaminiki pia katika lililo kubwa. Basi, kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya duniani, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli? Na kama hamkuwa waaminifu katika mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?*
*Luka 16:10-12*

Ilikuwa kazi yangu ya kwanza ya uchungaji. Watu walipokuwa wanakuja kwa Kristo, niliazimia kuwaongoza katika maisha yenye nidhamu kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Katika wakati mwafaka, niliwahimiza baadhi ya hawa Wakristo wapya zaidi waachane na uraibu wao wa tumbaku.

Bw. Mitchell alikuwa mmoja wa wahudhuriaji wetu. Alikuwa anasema sana kuhusu imani yake kwa Yesu lakini hakuwa mwangalifu katika tabia zake binafsi. Nilikuwa sijanena naye kuhusu matumizi yake ya tumbaku, lakini ni wazi kwamba alijua kile nilichokuwa ninawafundisha wale waumini

wengine. Siku moja, alinifuata akasema, “Mchungaji Shaver, ninajua Mungu aliweka tumbaku hapa. Ni zawadi ya kutumiwa. Kwa hivyo uvutaji wangu uko sawa.”

Nilishtuka kwa huo urazini wake. Kisha nikaanza kufikiri juu ya mambo niliyopitia zamani nilipokuwa kijana mdogo. Wakati huo, tuliruhusiwa kufanya ukulima kule Connecticut kabla ya kufika miaka kumi na sita. Huu ulikuwa wakati katika maisha yangu kabla mtu yeyote katika familia yangu hajamjua Yesu. Niliajiriwa kazi ya majira ya joto ya kuchuma tumbaku. Tumbaku la kutengenezewa biri linalokuzwa katika mahema yenye joto na unyevu unyevu ilikuwa tasnia kubwa. Nilifuata utaratibu sahihi wa kuchuma majani—nikikaa kwenye mistari katikati ya miti ya tumbaku na kuchuma majani yaliyo chini zaidi peke yake kulia na kushoto. Nilipokuwa ninachuma, utomvu wa tumbaku uliingia katika sugu nyingi nilizokuwa nazo mikononi mwangu. Katika siku chache, sugu hizo zilianguka, na ngozi yangu ikawa safi.

Mwisho wa hayo mavuno ya majani ya tumbaku, wakulima walirudi kule mashambani na kuvuna visiki vyake. Hivi vilikatwa na katika urefu wa futi mbili na kuuzwa kwa wenye nyumba wapate kuweka katika nyua zao. Sumu kali katika hivyo visiki (hasa nikotini) iliuwa wadudu wasiotakiwa kama funza na wadudu wengine walio katika hizo nyua, na hivyo visiki vilipooza hizo nyua zilipata mbolea.

Kwa hivyo nikarudi kwa Bw. Mitchell nikasema, “Lengo la Mungu kuweka tumbaku hapa halikuwa kutengeneza sigara mpate kuvuta. Lilikuwa kuondoa sugu kutoka miilini mwetu, na kuua funza na wadudu, na kutia mbolea katika nyua. Ukiamua kulitia mdomoni mwako, hilo ni chaguo lako.”

Nikakumbushwa kwa nguvu kwamba kwa sababu kitu kinapatikana haimaanishi kwamba ninapaswa kukitumia kwa njia yoyote nitakayo. *Siwezu kuamua* kutumia kitu kwa njia haribifu na nidai kwa uongo kwamba Mungu alikibariki—au ninaweza kukitumia kwa wema.

Yesu alifundisha mfano katika Luka 16 juu ya msimamizi aliyekuwa anaharibu mali ya bosi wake. Msimamizi mjanja aliona mapema atafukuzwa kazi na akafanya mipango na wadeni wa bwana wake ili apate fadhila zao. Yesu alisema juu ya busara yake na akasema wana wa nuru wanapaswa kufanyia utajiri wao kwa njia ambayo watakaribishwa katika makao ya milele. Kisha Yesu akafundisha kanuni inayotumiwa na Bw. Mitchell na sisi: “Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; na aliye dhalimu katika lililo dogo, huwa dhalimu katika lililo kubwa pia” (Luke 16:10).

Kwa hivyo, uwepo tu wa tumbaku, malipo yako ya kila wiki, mazingira yako, maarifa yako, mke au mume wa mwenzako, mashine ya kufyekea majani

ya jirani yako, miaka ya maisha yako—vyote lazima visimamiwe kwa njia ambayo inamtukuza Mungu na inafanya wema kwa wanadamu. Kwa maneno mengine, ni lazima tufanye maamuzi ya busara kuhusu fursa zote zilizo mbele yetu. Na kama tunaweza kuaminiwa katika lililo dogo sana, tunaweza pia kuaminiwa kwa mengi pia, Je, utatumia zawadi za Mungu kwa hekima?

**AGOSTI 15** **227**

# Yesu Anarudi Tena . . . Kwa hivyo?

*Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na makabila yote ya dunia yataomboleza kwa ajili yake. Naam. Amina.*
*Ufunuo 1:7*

*Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwizi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea.*
*2 Petro 3:10*

Ndiyo, ninaamini kwamba Yesu aliyezaliwa kwenye hori anarudi tena duniani kama Mfalme mwenye nguvu. Ninalihubiri hilo.

Ninapata wazo kwamba baadhi ya wale wanaonisikia nikihubiri hilo wanahitimisha, "Nitakaa na kungojea." Au, wanaponisikia nikihubiri juu ya uaminifu, utumishi, na huduma, wanafikiri, "Hilo linafaa namna gani? Wiki iliyopita tu ulituambia Yesu anarudi tena."

Huyo huyo Petro aliyesema siku ya Bwana itakuja kama mwivi, pia alisema, "Imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa, mkitazamia hata ije ile siku ya Mungu na kuihimiza" (2 Petro 3:11–12).

Katika 1 Petro 4:7–11, anaandika:

> Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia. Basi, iweni na akili, mkeshe katika sala. Zaidi ya yote iweni na juhudi nyingi katika kupendana; kwa sababu upendano husitiri wingi wa dhambi. Mkaribishane ninyi kwa ninyi, pasipo kunung'unika. Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu. Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu.

Mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo.

Kama ningekuwa mtu wa kawaida na ninajua Yesu anakuja tena, ningeishi kwa hayo maneno ya 1 Petro hapo juu. Siku yangu inaweza kujumuisha mafunzo ya Biblia na maombi mapema sana, kifungua kinywa, maombi na familia yangu, na kuwatia moyo watoto wangu wanapoondoka kwenda shule. Kule kazini kwangu, ningefanya kazi vizuri ili tupate kufanikiwa. Ninaweza kunena maneno ya ushuhuda kwa mtu, nimwombee mwingine, nionyeshe kumjali mwingine ambaye mwana familia wake ni mgonjwa. Nikirudi nyumbani, ningewasaidia na kuwatia moyo mke wangu na watoto wangu. Ningeweza kumpigia simu mgeni aliyekuja kanisani hivi karibuni, au ningeweza kutembelea hospitali kwa mmoja wapo wa washiriki wa kanisa letu.

Yesu anarudi tena. Kwa hivyo ningeishi kwa ajili yake hapa na sasa, siku baada ya siku, wakati baada ya wakati, kama Petro alivyosema—penda kwa kina, mkaribishane, watumikie wengine. Na ningekuwa tayari.

AGOSTI 16 **228**

# Ishara Nne za Mkatoliki Mwenye Nguvu

*Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao.*
*Waraka kwa Waebrania 12:14*

Katika kitabu cha Matthew Kelly chenye kichwa kilicho hapo juu, anasema:

- "Ishara Nne za Mkatoliki Mwenye Nguvu ni:
  1. Maombi
  2. Kujifunza
  3. Ukarimu
  4. Kuhubiri injili" (18).
- "Kubadilisha watu mmoja baada ya mwingine ndilo jambo lililo kuu katika mpango wa Mungu kwa ajili ya ulimwengu" (36).
- Kelly anaandika kwamba alikabiliana na wazo moja lililoyageuza maisha yake juu chini: "Mungu anakuita uwe mtakatifu, na kila kitu kinachofanyika maishani mwako, ushindi wako, majaribu, na mikasa ni nafasi ya kukua katika utakatifu" (77).

- Kelly anatumia kirai kingine kueleza kiu ya utakatifu: “kiu ya wewe binafsi kuwa bora zaidi” (78).[119]



# Utando wa Buibui na Panzi

*Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.*
*Waefeso 2:8-9*

Wakati mwingi ninapotembea katika bustani yangu, ninakutana na utando mmoja wa buibui. Sijui kama ulisalia baada ya utando kuharibiwa, au kama ni buibui anajitayarisha kujenga mwingine. Bila kujali hayo, huwa unanisimamisha njiani mwangu, na ninajaribu kuuondoa kwa hasira na kuhakikisha haujashikana na huyo buibui.

Siku moja, Mungu alinambia, *“Watu wanatoa mjibizo gani wanapokutana na utando wako? Je, wanajaribu kuzitoa kwa kuzivuta? Unatumia nini kusuka utando huo? Je, unausuka kwa umbeya au wivu au husuda? Au, wanapokutana na utando wako, je, kuna upendo mwingi na neema kiasi kwamba wanafungwa na kuvutwa kwako? Ni aina gani ya utando unayosuka na unayoacha? Rachel, ukitumia wakati katika bustani ya roho yako, utasuka utando wa neema na rehema ambazo zitawavuta watu wengine kwangu.”*

Mpaka hapo, ninaelewa kila kitu alichoniambia Mungu. Lakini sasa nilishindwa kabisa kuhusu hawa panzi. Nililala pale kwa muda mrefu, lakini sikuweza kuelewa maana ya panzi. Jibu lilinijia siku chache baadaye wakati shemegi yangu, Charlie, aliponiambia kwamba alipokuwa katika bustani yangu, alikuwa ametupa panzi katika utando wa buibui. Yule buibui akateremka mbio na kumshika huyo panzi, akimfungafunga na kumsokota ili apate kumla baadaye. Yule panzi alining’inia pale, akiwa amenaswa kwenye huo utando, bila matumaini, akingojea kufa kama buibui atakavyopenda. Ghafla, Charlie alipata wazo kwamba hii haikuwa haki, kwa hivyo akachukua kitawi kidogo na akamfungua yule panzi, akauvuta ule utando, na akamweka huru. Punde tu niliposikia hili, nilijua maana ya yule panzi.

---

119. Awali ilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Juni 2014).

Mimi ndiye panzi. Wakati mmoja nilikuwa nimenaswa kwenye utando wa dhambi, lakini Yesu akaja na kwa upendo akaniondoa katika utando wa Shetani na akaniweka huru. Yule panzi aliona neema siku ile. Ninaona neema ya Mungu, na ananiita nitumie wakati mwingi zaidi katika bustani ya roho yangu.

Nilijua kwamba Mungu alikuwa ananiita niwe mtu ninayeweza kudhuriwa vya kutosha kuweka hili somo kwenye karatasi na kumwambia mtu mwingine. Kisha akaniambia nijitoe kutumia wakati zaidi na yeye katika bustani ya roho yangu. Katika kukushirikisha wewe katika huu mfano leo, ninakupa ruhusa ya kuniwajibisha mimi—kuniuliza kama ninatumia wakati katika bustani ya roho yangu.

Na ninaleta mwaliko huu kwako pia. Hii wiki, tumia wakati kiasi na Mungu katika bustani ya moyo wako.

Rachel Rowley

**AGOSTI 18** **230**

# Katika Bustani ya Moyo Wako

*BWANA, asubuhi utaisikia sauti yangu, Asubuhi nitakupangia dua yangu na kutazamia.*
*Zaburi 5:3*

Kama umewahi kunitembelea nyumbani kwangu, yamkini umeona buibui mkubwa kwenye bustani. Ana rangi nyeusi na manjano, na hutandaza utando wake katikati ya mti wa kijani kibichi wakati wote na kichaka cha lilaki. Chanzo cha utando kilikuwa na upana wa kama futi tatu, na kilikuwa na vitu kama nanga katika pembe zilizoenda kama futi sita. Buibui alikuwa ameshika panzi kadhaa, alikuwa buibui mkubwa, mnene, na mwenye furaha. Baada ya kutazama huyo buibui kwa kama siku kumi, nilikuwa na hali ya kipekee ambayo kwa namna fulani ilinisumbua. Ilikuwa Alhamisi saa 9.00 alfajiri nilipoamka na kuhisi uwepo wa Mungu usiokuwa wa kawaida kabisa. Kwa saa moja, Mungu alinena nami katika mfano kuhusu buibui, utando wake, na panzi.

Ninapenda kutoka nje katika ua wangu asubuhi na kikombe cha moto cha kahawa ya mdalasini na hazelnati na kutazama uumbaji wa Mungu. Kufikia wakati wa kuingia katika nyumba hii, nilikuwa ninaogopa sana buibui. Bado

hawako katika orodha ya kumi bora, lakini ninajifunza kuwatazama kwa macho tofauti. Ninawatazama wakisokota tando zao—yale mapambo changamani kila moja likiwa na muundo asili. Wazo langu la kwanza kuhusu tando ni kiasi cha kazi kinachohusika. Wale buibui husokota tando zao na kushika mlo wao wa jioni kisha, kufikia asubuhi, upepo mkali au tawi limesonga na kuharibu huo utando, au baadhi ya buibui huvunja tando zao wenyewe makusudi. Kwa hivyo husuka utando mwingine—muundo mwingine asili—na hadithi hujirudia tena. Kusema kweli, huwa nachoka kufikiri tu kuhusu jinsi wanavyofanya kazi kwa bidii, jinsi kazi yao inavyochukua siku moja pekee au kitu kama hicho, kisha jinsi wanavyolazimika kuanza tena.

Hivyo ndivyo nilivyokuwa ninafikiri kuhusu wakati Mungu alipokatisha fikira zangu na kusema, *"Buibui hawafikiri juu ya hilo kama kazi; hawachoki kufanya kile walichoumbwa kufanya. Rachel, unapokuwa na upendo kwa ajili ya mtu, je, hilo hukuchosha wakati unapowekeza wakati kwao? Je, wewe huchoka kuwapikia hawa chakula? Je, ni bure unapokuwa nao nyumbani kwako?"*

"La, hasha."

*"Kwa nini?"*

"Kwa sababu ninawapenda. Kwa sababu nimebarikiwa na ninataka kugawa hizo baraka kwa wengine."

Mungu akaendelea, *"Rachel, ukitumia wakati katika bustani ya roho yako, nitakufundisha jinsi ya kuunda tando ambazo hazitakufanya uhisi uchovu au kuchoka. Tando zako zitametameta kama umande kwa sababu zitatiririka kutoka kwenye moyo wa upendo."*

Ndiyo, Bwana. Ninahitaji kutumia wakati zaidi katika bustani ya roho yangu.

Rachel Rowley

AGOSTI 19 **231**

# Kutotii Huleta Msiba

*Kwa sababu hiyo hasira ya BWANA imewaka juu ya watu wake, naye amenyosha mkono wake juu yao; akawapiga, navyo vilima vilitetemeka, na mizoga yao ilikuwa kama takataka katika njia kuu.*
*Pamoja na hayo yote hasira yake haikugeukia mbali, lakini mkono wake umenyoshwa hata sasa.*
*Isaya 5:25*

Kama wavuvi wawili waoga, tulijaribu kuwa kuzoeana. Jim alikuwa na mengi ya kujivunia—alipata alama za juu zaidi kule shule za upili, na katika wiki chache, akawa kiongozi katika timu ya kandanda ya wanafunzi wapya.

Hata hivyo, mtindo wake wa maisha haukuwa na nidhamu kama desturi zake za kiakili au kimwili. Alikuwa "hodari wa kunywa mvinyo" (Isaya 5:22), na akichanganya na kucheza kadi kwake, kunywa kwake kungeweza "kuendelea hata usiku wa manane" (5:11). Alikuita tu "kunywa kiasi." Alijivuna juu ya mambo yake ya ngono, akitazamia "maadili mapya" kwa miaka kumi. Alikuwa kati ya "wale waitao uovu wema, na wema uovu" (5:20). Nilipomkubali Kristo, itikio lake lilikuwa dhihaka, kwa maana hakuithamini "kazi ya BWANA" (5:12).

Nilitazama tu mwili wake ulipokuwa unadhoofishwa na kukaa muda mrefu usiku, muda si muda ukavunjika. Wakati wa wiki ya mtihani, asubuhi moja aliamka na hakuweza kutoka kitandani—alikuwa na homa ya viungo. Ilimfanya akose mwaka mzima wa masomo. Moyo wake uliharibiwa na huo ugonjwa—yule nyota wa kandanda hakuweza kupanda ngazi za ghorofa. Kufikia umri wa miaka thelathini na mitatu alikuwa amekufa. Ingawa kuna vyanzo vingine vya majanga binafsi kuliko dhambi ya mtu mwenyewe, uasi binafsi siku zote huleta majanga binafsi (5:25).[120]

AGOSTI 20 **232**

# Ilionekana Kuwa Kitu Kidogo Sana

*Basi binti Farao akashuka, aoge mtoni, na vijakazi wake wakatembea kando ya mto; naye akakiona kile kikapu katika nyasi, akamtuma kijakazi wake kwenda kukileta. Akakifungua, akamwona mtoto, na tazama, mtoto yule analia. Basi akamhurumia, akasema, Huyu ni mmojawapo wa watoto wa Waebrania.*
*Kutoka 2:5-6*

Katika akili ya Farao, kuuawa kwa watoto wa kiume wote lilikuwa ndilo suluhisho la pekee kwa hilo tatizo la Waebrania. Waebrania walikuwa wamekuja Misri wakati Yusufu alipoileta familia yake huko ili awaokoe dhidi ya njaa kule Israeli. Farao wa awali aliyemteua Yusufu kama waziri wake

120. Awali ilichapishwa katika *Come Ye Apart* Machi–Aprili–Mei 1971 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 83. Imetumiwa kwa ruhusa.

mkuu alikuwa na huruma kwa familia ya Yusufu. Sasa kulikuwa na mfalme mpya aliyeogopa ukuaji wa haraka haraka wa idadi ya Waebrania.

Huyu Farao mpya aliwahimiza wakunga wa Waebrania wawaue watoto wa kiume wanapozaliwa. Hata hivyo, wale wakunga waliikwepa amri yake na hawakuitekeleza. Kisha Farao akatoa amri: "Kila mtoto mwanamume atakayezaliwa mtamtupa mtoni, na kila mtoto mwanamke mtamhifadhi hai" (Kutoka 1:22).

Siku moja binti Farao akashuka, aoge mtoni, naye akakiona kile kisafina kikielea katika majani. Akamtuma kijakazi wake aende akichukue. Binti Farao alipokifungua kile kisafina na kumwona mtoto wa Kiebrania akilia, akamhurumia na akaamua kumwokoa.

Hiki kitendo alichokifanya binti Farao kilikuwa ni kitendo cha neema na rehema. Siku zote ni jambo kubwa wakati mtu yeyote anapookoa maisha ya mwanadamu. Hata hivyo, kwa kuwa idadi ya Waebrania ilikuwa imeongezeka sana, na Farao alikuwa ametoa amri yake ya uuaji hadharani, tunaweza kuchukulia kwamba mamia ya watoto wa kiume walikuwa wanatupwa mtoni. Kwa hivyo, katika maisha ya jumla ya taifa, ni lazima ilikuwa imeonekana kama jambo dogo tu—mtoto mmoja ameokolewa.

Mtoto alikuwa anaelea ndani ya hicho kisafina kwa sababu baada ya kumficha kwa miezi mitatu, mama yake aliamua asingeweza kumficha tena. Akatengeneza kisafina cha nyasi, akakifanya kisiingie maji kwa kukipaka lami, na kukiweka katika majani kando ya mto, mtoto akiwa ndani. Umbu lake mtoto akasimama mbali ili ajue yatakayompata.

Mara tu binti Farao alipomvumbua yule mtoto mle safinani, dadake yule mtoto akamwendea na kumwuliza kama alitaka mwanamke wa Kiebrania wa kumlea huyo mtoto. Binti Farao aliposema ndiyo, yule dada yake akamleta mama yao. Cha kushangaza zaidi katika mgeuko huo wa matukio, binti Farao akamlipa huyo mama kwa kumlea mtoto wake. Yule mtoto alipokuwa kidogo, mama yake akampeleka kwa binti Farao, na akamwita Musa (Kutoka 2:1–10).

Kisha Musa akawa mtu mzima. Na ni kitu gani kilichofuata?

- Mungu akasema, "Bila shaka mimi nitakuwa pamoja nawe;" (Kutoka 3:12).
- Musa akawa kiongozi wa Waebrania.
- Akamkabili Farao, akamwambia awaachie watu wake, na akamwakilisha Mungu wakati wa yale mapigo kumi makubwa ya hukumu juu ya Misri.
- Akawaongoza Waisraeli kutoka Misri na kuvuka Bahari ya Shamu, ambapo jeshi la Farao lililowafuata lilizama majini.
- Alipokea Amri Kumi za Mungu juu ya Mlima Sinai kwa ajili ya watu wake na ulimwengu.

- Aliongoza Waisraeli kuvuka jangwa hadi nchi ya ahadi.
- Akawafikisha Mto Yordani na akawatayarisha kuingia nchi ya ahadi.
- Akiwa na umri wa miaka 120, baada ya kumchagua Yoshua awaongoze Waisraeli kuingia nchi ya ahadi, Musa akaenda kukaa na Bwana (Kumbukumbu la Torati 34:7–12).

Mara ya kwanza kilionekana kuwa kitu kidogo sana ambacho binti Farao alichukua dakika chache kutoa kisafina mtoni. Lakini Mungu alipotumia hiyo hali kuyachonga maisha ya watu wake, tunaona matokeo yake ya mwisho. Kuna wimbo unaosema, "Kidogo ni kingi sana Mungu anapokuwa ndani yake." Unaona Mungu anaweza kufanya nini maishani mwako katika kitu kinachoonekana kuwa kitu kidogo sana?

**AGOSTI 21** **233**

# Kututoa Huko ili Kututia Huku

*Akatutoa huko ili kututia huku, apate kutupa nchi aliyowaapia babu zetu. BWANA akatuamuru kuzifanya amri hizi zote, tumche BWANA, Mungu wetu, tuone mema sikuzote ili atuhifadhi hai kama hivi leo. Tena itakuwa haki kwetu, tukizingatia kufanya maagizo haya yote mbele ya BWANA, Mungu wetu, kama alivyotuagiza.*
*Kumbukumbu la Torati 6:23-25*

Maisha yamejaa hali ambazo unatolewa nje ili uweze kutiwa ndani.

Ilinibidi nitolewe nje ya mpango wangu wa shule ya sheria ili nitiwe katika seminari. Mungu alikuwa ameniita katika huduma.

Ilinibidi nitolewe nje ya uhusiano wangu na mpenzi wangu fulani ili nitiwe ndani ya uhusiano wangu na Nancy, ambaye akaja kuwa mke wangu.

Yamkini utakubali kwamba huu mpangilio ni sehemu ya maisha yako pia.

Ilibidi Waisraeli watolewe utumwani ili watiwe katika nchi ya ahadi. Kutoka katika vitunguu, na vitunguu saumu hadi katika nchi itiririkayo maziwa na asali; kutoka kwa kupigwa mijeledi na wasimamizi wakali hadi kushinda vita vikali kama vile Yeriko, kutoka kutengeneza matofali katika jua kali hadi kumiliki mali zao wenyewe binafsi. Kwa "kuwatoa" ili "awaweke," Mungu aliwafanyia Waisraeli kile ambacho wasingeweza kujifanyia wenyewe. Ili alitimize hili, Mungu alitenda miujiza—aliachilia mapigo kule Misri; akagawanya Bahari ya Shamu; akawaongoza Waisraeli kupitia jangwani kwa

nguzo ya wingu na nguzo ya moto; akawapa mana kuwa kifungua kinywa na kware kuwa mlo wa jioni. Hii nchi mpya ingewapa mafanikio ili mradi wamtii yule Mungu aliyewapatia hiyo nchi. Kwa kweli, utiifu wao kwa Bwana ungekuwa haki yao.

Na kwetu sisi tulio katika mwongo mpya chini ya Yesu Kristo, kanuni ni iyo hiyo. Petro alihubiri, "Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana" (Matendo 3:19). Tumetolewa katika dhambi zetu na kutiwa katika uhusiano wa kuburudisha na Mungu. Yesu alimwambia Paulo, "Nakutuma kwao uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi" (Matendo 26:17–18). Tumetolewa gizani tukatiwa kwenye nuru. Tumetolewa katika mikono ya Shetani tukaletwa kwa Mungu—na hata zaidi, tukaletwa katika utakaso ndani ya Yesu kwa imani.

Je, kutoa nje ili uwekwe ndani kunafanya kazi katika maisha yako ya kiroho?

**AGOSTI 22** **234**

# Sauti ya Roho Inasikika Kama Kitu Gani?

*Na Petro alikuwa akiyafikiri yale maono. Roho akamwambia,*
*Wako watu watatu wanakutafuta.*
*Matendo 10:19*

Wakati wa kipindi maalum kilichokuwa changamoto maishani mwangu, nilipokea huu ujumbe kutoka kwa aliyekuwa mwanafunzi wangu na mfanyakazi mwenzangu: "Natumaini na kuomba kwamba wewe na Nancy ni wazima. Katika wiki kadhaa zilizopita nimekuwa nikifikiri kuhusu ninyi, kwa sababu kadhaa, na nikaona ni afadhali hayo mawazo niyachukulie hatua (kama tu ulivyotufundisha) na nifikie watu."

Earl Lee alinifundisha, "kama wazo haliondoki, huwa ninachukuliwa kuwa ni uongozi wa kiungu." Earl Lee alikuwa Mkristo mcha Mungu, mwenye urari, aliyeendelea kwenda mbele katika huduma ya nguvu na ushawishi. Agano Jipya, hasa kitabu cha Matendo, kimejaa marejeo mengi ya uongozi wa kiungu—hivi visa vinaweza kuvutia, kama vile maono au sauti ya Mungu

inayosikika. Kumbuka katika maandiko ya leo ambayo Petro alikuwa bado anafikiri kuhusu maono ya kuvutia ambayo Mungu alikuwa amemwonyesha ndipo alipomsikia Roho akinena. Petro alipokuwa anafikiri kuhusu hayo maono, je, ilikuwa kama vile rafiki yangu alivyokuwa anafikiri kuhusu mimi na kunitia moyo, hata ingawa hakuna mtu aliyemwambia kwamba ninapitia wakati wenye changamoto? Haya matukio yote yanasikika kama wazo la Earl Lee la dhana ambayo haiondoki.

Wakati mwingine tunapokea wazo ambalo linaweza kuwa kile ambacho Wakristo wengine wanakiita sauti ya Roho Mtakatifu. Kwa kukubali, ni lazima tufuate baadhi ya maelekezo na tahadhari inapofika wakati wa kuamua ikiwa wazo *linatoka* kwa Roho—la sivyo mtu anaweza kujiingiza katika matatizo makubwa. (Hizi tahadhari zitajadiliwa baadaye.)

Mapema katika majira ya joto, tulihimizwa kuweka miadi kwa daktari maarufu aliyekuwa mtaalamu wa hali tuliyokuwa tunaitibu. Tulipopiga simu ofisini kwa huyo daktari ili tuweke miadi, tulijua kwamba siku ya mapema zaidi atakayofungua ni tarehe 9 Disemba. Hata hivyo, mratibu alitwambia kwamba tunaweza kupiga simu kila baada ya muda kuona kama kuna mtu aliyefutilia mbali miadi yake ili tupate nafasi ya mapema.

Miezi michache baadaye, tarehe 4 Agosti, nikapata wazo kwamba ninapaswa kupiga simu kule ofisini na niulize kama kuna mtu aliyefutilia mbali miadi yake (na huo ndio wakati pekee niliofanya hivyo). La kushangaza, huyo daktari alikuwa na nafasi moja. Yule mratibu akaniuliza kama tungeweza kuwa pale saa 2.30 ya asubuhi iliyofuata. Kwa hivyo tuliweza kuingia kwa ajili ya hiyo miadi ya mtaalamu tuliyoihitaji sana, miezi minne kabla ya ile tuliyokuwa tumeweka awali.

Wakati mmoja mtu mmoja alisema, "Sauti ya kiungu mara nyingi haitamkwi katika maneno ya kusikika; inajulishwa kwa ufahamu wa moyoni." Oo, Bwaba, fanya moyo wangu na akili yangu iwe macho kwa uongozi wako katika mfumo wowote ule utakaoutoa!

# Kutoka Katika Imani ya Mkana Mungu Hadi kwa Kristo

*Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenituma; nami nitamfufua siku ya mwisho.*
*Yohana 6:44*

Angela alikuwa mhudhuriaji mwaminifu katika kanisa lake la nyumbani, lakini mumewe, Steffen, hakuwa anapenda kanisa. Kwa kweli, alidai kwamba yeye ni mkana Mungu. Hatimaye, ndoa yao ilipokuwa inadidimia na walionekana kutengana, Steffen alikubali kupata ushauri wa ndoa kutoka kwa mchungaji wa Angela. Ushauri wao ulipokuwa unaendelea, alikubali kwenda kanisani, ili avijaribu, na kufikiri tena kuhusu msimamo wake.

Steffen akasema, "Nataka kuja kanisani, lakini sina uhakika nitaamini."

Hata hivyo, Steffen alianza kusoma Biblia, Mark Cahill's *One Heartbeat Away—Your Journey into Eternity*, na Lee Strobel's *The Case for Christ*. Alipokuwa akihudhuria ibada kanisani, mtazamo wa Steffen ulianza kulegea. Hata aliungana na Angela katika uhudhuriaji wa ibada za uamsho wa majira ya machipuo.

Jumatano moja, mchungaji alimwalika Steffen kwa ajili ya mlo wa mchana. Nikajumuika nao, na wakati wa huo mlo, niliweza kumwambia Steffen safari yangu kutoka kuwa na imani ya agnostiki hadi kumwamini Yesu. Hatimaye, Steffen akatambua kwamba hakuwa na haja ya kupata jibu la kila swali ndipo afanye uamuzi. Pia alitambua kwamba, hakuwa na haja ya kuwa mkamilifu mara moja.

Punde tu, Steffen alishawishika alikuwa tayari. Mwishowe, katika ofisi ya mchungaji, Steffen aliomba ampokee Kristo. Akahisi afueni mara moja, kama mzigo wa ulimwengu ulikuwa umeondoka mabegani mwake. Alijua kwamba mtu fulani alikuwa pamoja naye; kwamba yule mtu ambaye angeweza kumtegemea alikuwa anasikiliza. Kwa kweli alihisi kwamba Kristo alikuwa ameingia moyoni mwake.

Alipomwambia Angela kile kilichotokea, alishangaa na kufurahi. Usiku ule wa kufunga hizo ibada za uamsho, walikuja madhabahuni pamoja. Watu

wengine wakawazunguka, na Steffen akahisi msaada wao. Akasema, "Nilijua nilikuwa nimefanya jambo sahihi. Hili ni halisi—Yesu ni halisi."

Leo, miaka thelathini na mitano baada ya kuokolewa, nimenena na Steffen kwenye simu. Amenambia kwamba ndoa yake imegeuka kwa nyuzi 180 kuanzia wakati yeye na Angela walipoanza ushauri mara ya kwanza—sasa ndoa yao iko karibu na ukamilifu kadiri iwezekanavyo.

Steffen amefanya *Basic Bible Studies for New and Growing Christians* na watu kutoka kanisani kwake, na amesoma Mathayo, Marko, Luka, na Matendo. Amesanifu bustani yenye miti mipya na mandhari mpya kwa ajili ya kanisa. Yeye na Angela wameanza kutoa fungu la kumi kwa sababu wametambua kwamba hata kwanza hizo pesa zote ni za Mungu. Amekuwa akimshuhudia rafiki yake.

Mchungaji wake anasema kwamba Steffen sasa anatabasamu kubwa zaidi na kawaida yeye ndiye wa mwisho kutoka mlangoni mwa ibada yoyote ya kanisa. Hebu fikiri—kutoka kuwa na imani ya mkana Mungu hadi kwa Kristo. Na wa mwisho kutoka kanisani, si kidogo![121]

**AGOSTI 24** **236**

# Mwokozi Atafutaye na Kifungu Kimoja cha Biblia

*Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta*
*na kuokoa kile kilichopotea.*
*Luka 19:10*

*Bali utafuteni kwanza ufalme wake,*
*na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*
*Mathayo 6:33*

Yesu ni Mwokozi atafutaye!

Baba yangu hakuwa na baraka ya kukuzwa katika nyumba ya Kikristo au kwenda kanisani. Alipokuwa kijana, mara nyingi aliona bango karibu na mji wao wa nyumbani na kifungu cha Biblia, "Mathayo 6:33—Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa." Alijiuliza maswali kuhusu haya maneno kwa miaka mingi. Hivyo basi, kabla baba yangu

121. Awali ilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Juni 2009).

hajaanza kumfuata Yesu, alijua kifungu *kimoja* cha Biblia—na hakikuwa Yohana 3:16! Kilikuwa Mathayo 6:33.

Katika majira ya kuchipua ya mwaka 1972, katika mwaliko wa jirani aliyeitwa Mike, baba yangu aliingia kanisani mara ya kwanza. Wakati huo, baba yangu alikuwa amepotea, amevunjika moyo, na anaishi katika dhambi. Mwinjilisti mmoja alikuwa anahubiri hiyo Jumapili. Baba yangu anasema alihisi kana kwamba huyo mnenaji alikuwa amemfuata katika maisha yake yote na alikuwa anamhubiri *yeye tu* siku hiyo. Je, unajua yule mwinjilisti alikuwa anahubiri kutoka fungu gani kuanzia hiyo Jumapili ya kwanza ambayo baba yangu alienda kanisani? Mathayo 6:33—hicho kifungu kimoja alichokuwa anakijua baba! Yesu alikuwa anamtafuta baba!

Mwisho wa hiyo ibada ya kwanza, baba yangu alikutana na Yesu madhabahuni. Dhambi zake zilisamehewa. Akawa mtu aliyeponywa. Aibu yake na fedheha vikabadilishwa na rehema na neema ya Mungu. Nilikuwa na baba mpya!

Yesu ni Mwokozi atafutaye!

Dkt. Scott Rainey
Mkrugenzi Mkuu wa Huduma za Kimataifa za Shule ya Jumapili na Uanafunzi Ulimwenguni
Kanisa la Nazarene
Mkrugenzi Mkuu Mwenza wa The Chic Shaver Center for Evangelism [122]

AGOSTI 25 — 237

## Sijawahi Kuwa na Siku Mbaya

*Furahini siku zote; ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo;*
*maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.*
*1 Wathesalonike 5:16-18*

Kuna kitu kuhusu wafuasi wa Kristo—hasa wale Wakristo waliojazwa Roho na kutakaswa—anayewawezesha kuishi kwa ushindi hata ingawa wanapitia mambo magumu katika maisha. Hawatoi shukrani *kwa* kila jambo, bali wanawezeshwa kutoa shukrani *katika* kila jambo. Sisemi kwamba Wakristo

122. Awali ilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Juni 2020).

wote wanaishi katika huo ushindi—bali wengine hufanya hivyo, na hayo maisha yapo kwa ajili ya kila mtu.

Nimeona maisha ya ushindi kwa mwanangu, Paul. (Unaweza kusoma zaidi kuhusu yeye katika ibada ya #20 na #21 katika hiki kitabu.) Mume na baba wa watoto wanne, amepitia upasuaji kadhaa wa saratani: madaktari walitoa nyama kubwa kutoka begani mwake alipokuwa kijana; seli ya saratani ya ngozi kutoka kifuani mwake alipokuwa katika miaka yake ya thelathini; seli ya saratani ya ngozi karibu na sikio lake na chini ya utaya mwanzoni mwa umri wake wa miaka ya hamsini; na seli ya saratani ya ngozi haribifu sana katika shingo yake mwanzoni mwa miaka yake ya hamsini. Upasuaji wa mwisho ulijumuisha kutoa kitoa sauti chake na sehemu kubwa ya shingo.

Upasuaji wa nne wa Paul wa saratani ulichukua saa kumi na tatu na ndio uliokuwa mkubwa kuliko mwingine wote. Akiwa na upasuaji wa ziada, hatimaye aliweza kunena katika sauti ya chini, ya kusitasita. Tulipokuwa na wakati na yeye kama miezi sita baada ya upasuaji wake, tulikuwa na maswali mengi kuhusu yeye. Akatupa majibu yafuatayo:

"Uwanja wangu umepunguzwa, kwa hivyo nachagua maneno kwa uangalifu."

"Mara kwa mara daktari alisema 'saratani' na 'kitoa sauti vinaweza kutakiwa kutolewa,' nilikuwa na hii amani, na nikahisi hilo ndilo nililolazimika kufanya. Nilihisi ningeweza kulistahamili."

Tulipomwuliza kuhusu ukubwa ulio shingoni mwake kwa sababu ya kuundwa upya na misuli ya kifuani, alisema, "Nilitamani kwamba pasiwe na ukubwa mwingi sana, na sasa inaonekana kuwa kidogo sana."

Maswali ambayo alikuwa hana jibu, alisema mara nyingi, "Bado Mungu anajua jina langu."

Kisha akalia.

Kufikia wakati wa likizo za familia miezi michache baadaye, kitu fulani katika koo yake kilikuwa hakifanyi kazi vizuri, na Paul akapoteza ile sauti dhaifu aliyokuwa nayo. Alikuwa anakabiliana na upasuaji mwingine. Lakini alikuwa mtu aliyeweza kuona tumaini mbele ya kila jambo gumu. Dada yake Miriam alimwuliza, "Unahisi namna gani baada ya upasuaji wa saratani mara nne, kupoteza kiungo chako cha kutunzia sauti na sasa sauti yako, na yote yaliyofanyika kwako?"

Kwa sababu hakuweza kuongea, akaandika jibu lake: "Sijawahi kuwa na siku mbaya."

Ukimshinikiza, Paul angesema, "Nilipoteza kiungo changu cha kutunzia sauti, lakini bado ninaishi."

Furahini siku zote; ombeni bila kukoma; shukuruni *katika* kila jambo.

# Kuishi chini ya Mapatano

*Yesu aliposikia hayo alimwambia, Umepungukiwa na neno moja bado; viuze ulivyo navyo vyote, ukawagawie maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha, njoo unifuate. Lakini aliposikia hayo alihuzunika sana, maana alikuwa na mali nyingi.*
*Luka 18:22-23*

*Petro akasema, Tazama, sisi tumeviacha vitu vyetu vyote na kukufuata. Akawaambia, Hakika nawaambia, hakuna mtu aliyeacha nyumba, au mke, au ndugu, au wazazi, au wana, kwa ajili ya ufalme wa Mungu, asiyepokea zaidi mara nyingi katika wakati huu, na katika ulimwengu ujao uzima wa milele.*
*Luka 18:28-30*

Sukari ya kuganda juu ya keki ilikuwa kitu kikubwa nilipokuwa mtoto. Mlo wa jioni ya familia yetu mara nyingi ulijumuisha nyama, viazi, na mboga, pongezi kwa mama yangu, aliyekuwa mpishi mzuri. Baada ya kuosha sahani zetu, siku zote kulikuwa na kitindamlo kizuri sana—pai au keki ya kutengenezwa nyumbani. Kitindamlo nilichopenda sana kilikuwa keki nyeupe iliyokuwa imewekewa chokoleti nzito. Mara nyingi nilitoa hiyo chokoleti, kisha nikala keki kwanza, halafu mwisho nikala hiyo chokoleti, nikifurahia kila funda. Sina hakika ilitoka wapi, lakini nilikuwa nimekuza hii falsafa ndogo: *iliyo bora zaidi ile mwisho*.

Nilileta hiyo falsafa katika maisha ya utu uzima. Hata hivyo, sasa ninaishi katika muongo wa kutoshelezwa papo hapo. Baadhi ya watu leo bila shaka wangekula sukari iliyoganda kabla ya kula sehemu moja ya nyama au mboga. Lakini ninaamini falsafa yangu inafanya kazi vizuri—imeniwezesha kufanya uchaguzi tukilenga mbali.

Mtu mkubwa tajiri alimwendea Yesu na akamwuliza, “Nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?” (Luka 18:20).

Yesu alijibu kwa kuorodhesha amri tano kati ya zile Amri Kumi. Yule mkubwa alisema alikuwa amezifuata zote, Yesu akajibu, “Umepungukiwa na neno moja bado. Viuze ulivyo navyo vyote, ukawagawanyie maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni. Kisha, njoo unifuate” (18:22).

Itikio la yule mtawala lilikuwa nini? "Alihuzunika sana." Je, tunapaswa kufikiri kwamba Yesu anawauliza Wakristo wote wauze vyote walivyo navyo na wawagawie maskini? Yamkini la, ingawa baada ya muda mrefu Wakristo wamejifunza kuwapa maskini msaada maalum. Katika haya mazungumzo, Yesu aligusa mahali panapouma zaidi katika maisha ya yule kijana mkubwa kitu alichokipenda zaidi—utajiri wake—na akamwambia atoe hata huo. Vivyo hivyo, Kristo pia atatuomba tutoe upendo wetu wa ghali zaidi kwa wema wetu na kwa utukufu wake.

Kisha Kristo anampa yule mtawala agizo lingine: "Kisha njoo, unifuate." Kwa maneno haya, Yesu alimwomba huyo kijana mtawala asitoe tu utajiri wake, bali pia maisha yake yote.

Kwa kutazama kile kilichokuwa kinatokea, watu wengine wakamwuliza Yesu, "Ni nani basi awezaye kuokoka?" (18:26)

Kristo aliwahakikishia kwamba kwa Mungu, wokovu unawezekana. Petro akasema, "Tazama, sisi tumeviacha vitu vyetu vyote na kukufuata!" (18:28).

Kisha Yesu akajibu kwamba kila mfuasi wake, na kujitoa kwake kokote kule, atapokea "zaidi mara nyingi katika zamani hizi, na katika ulimwengu ujao uzima wa milele" (18:30). Waa! Mapatano mazuri sana—ya kipindi kirefu.

Ninasitasita kutumia neno "mapatano" inapofika upande wa kumfuata Kristo. Naweza kusema ukweli kwamba maisha yangu ni ushirika wa kila siku na Kristo, wa binafsi, wa kudumu, wa furaha, uliojaa upendo, unaoleta amani; na huu uhusiano wa pande mbili una utajiri mwingi, kiasi kwamba ni furaha kumwabudu, kumtumikia, na kumtii. Kwa hivyo, ni nadra kwa dhana ya zawadi kuja kwenye fikira zangu. Je, hili linapaswa kuwa namna hiyo kwa sisi sote?

Mwanangu, Paul, kila mara husema juu ya maisha yake, "Ninaishi chini ya baraka." Ninaona tunaweza kuongeza, "Ninaishi chini ya mapatano." Hata ingawa ni lazima tuwe na uhakika kwamba nia zetu ni safi, Yesu anatuhakikishia kwamba anaweka ile iliyo bora kwa ajili ya wakati wa mwisho.

239

# Umuhimu wa *Ikiwa*

*Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekeza, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao.*
*2 Mambo ya Nyakati 7:14*

Hebu dhania kwamba ninamwahidi binti yangu wa kwanza kwamba siku ya kuzaliwa kwake kwa mwaka wa kumi na sita, nitampeleka kwa gari hadi kwenye Idara ya Magari afanye mtihani wa udereva na apate leseni yake. Halafu, wiki moja kabla ya siku yake ya kuzaliwa, aje na dalili za homa ya uti wa mgongo na, kwa wiki mbili nzima, analazwa hospitalini katika hali mahututi.

Ninakosa hiyo tarehe niliyoahidi kwa sababu, kwa upendo wangu kwake, hakuna namna ninamtoa huyo mtoto wangu hospitali ili nimlazimishe kufanya mtihani wake wa udereva. Hakuna mtu atakayenishitaki kwa kuwa mvunjaji wa ahadi kwa kufanya mtihani ukawie—kumekuwa na mabadiliko muhimu katika hali zilizo karibu nasi. Kwa hivyo, hulka yangu ya upendo inaamua kubadilisha tarehe. Na miezi michache baadaye, binti ana furaha kuwa dereva mwenye leseni.

Mungu ana hulka takatifu isiyobadilika. Kama Yakobo 1:17 inavyotangaza, Mungu "kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka." Mungu anamwambia Sulemani kwamba hata atakapozuia mvua au akituma nzige au mapigo katika hukumu takatifu anaweza kubadilisha matendo yake *ikiwa* watu wake watafanya yafuatayo:

- Watajinyenyekeza
- Wataomba
- Watautafuta uso wake
- Wataacha njia zao mbaya

Haya mabadiliko yanaweza kutokea namna gani? Kwa mabadiliko makubwa katika hali ya watu—yaani, mabadiliko ya mtazamo wao na msimamo wao dhidi ya Bwana.

Kwa sababu Mungu ni mtakatifu ni lazima ahukumu dhambi. Kama Warumi 6:23 inavyoonya, "Mshahara wa dhambi ni mauti." Lakini hali ya mwanadamu ambayo si takatifu inapobadilika kwa maombi na kutubu na

kusamehewa na kuishi maisha ya utakatifu, Mungu hufanya mambo tofauti: “atawasamehe dhambi yao na kuiponya nchi yao.”

Kwa maana yote tunayojua kuhusu Mungu mtakatifu, kumbuka umuhimu wa *ikiwa*!

Bwana mwenye nguvu alitangaza kupitia kwa nabii wake Yeremia, “Yerusalemu utakuwa kama mahali palipoinuka msituni” (Yeremia 26:18). Kisha kulitokea nini? Yeremia 26:19 inasema, “Je! Hezekia, hakumcha Bwana na kumwomba Bwana awafadhili? Naye Bwana akaghairi, asiyatende mabaya yale aliyoyatamka juu yao?” Ni kitu gani kilibadilika hapa? Mtu mmoja aliomba.

Weka usikivu unapoona neno “ikiwa” katika Maandiko (mkazo ni wangu):

- “*Ikiwa* tutaziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote” (1 Yohana 1:9).
- “Bali tu*ki*enenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote” (1 Yohana 1:7).
- “Katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu, wasio na mawaa wala lawama—m*ki*dumu tu katika ile imani, hali mmewekwa juu ya msingi, mkawa imara; msipogeuzwa na kuliacha tumaini la Injili” (Wakolosai 1:22–23).

Ndio! *Ikiwa*!

**AGOSTI 28** **240**

# Uwezo wa Sentensi

*Mpenzi, usiuige ubaya, bali uige wema. Yeye atendaye mema ni wa Mungu, bali yeye atendaye mabaya hakumwona Mungu.*
*3 Yohana 1:11*

Inashangaza kile ambacho sentensi moja au mbili zinaweza kuleta—hasa zinapotumika kutoa ushauri. Jambo muhimu zaidi kuliko hayo maneno yenyewe ni hatua zinazochukuliwa kulingana na maneno hayo. Kwa hakika, watu wanaosikiliza hayo maneno lazima waangalie, waamue, na wajichukulie hatua wenyewe. Bado, kuna uwezo fulani na ushawishi katika hayo maneno asili.

Akamwambia mwanamke, “Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, ‘Msile matunda ya miti yote ya bustani?’” (Mwanzo 3:1). Ijapokuwa haya maneno yalikuwa swali, yaliashiria kwamba Hawa alipaswa kula kama alivyotaka. Hawa, na kisha Adamu, hawakutii amri ya Mungu aliyoitoa moja kwa moja kwa kula tunda lililokatazwa. Kisha wakaona aibu, wakajificha Mungu asiwaone, na wakajiletea laana wao wenyewe na dunia yote.

Akiwa na wasiwasi kuhusu uwezo wake wa kisiasa, Mfalme Herode alisema sentensi chache kwa mamajusi waliyemtafuta mfalme wa Wayahudi aliyekuwa amezaliwa: “Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto. Na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie” (Matthew 2:8). Wale mamajusi wakampata yule mtoto kule Bethlehemu lakini, baada ya kuonywa katika ndoto, hawakurudi kwa Mfalme Herode (2:12). Huu ni mfano wa kukataa maneno ya mapendekezo kwa sababu yataishia katika uovu.

Lidia, mwanamke mfanyabiashara tajiri, alikuwa amefungua moyo wake kwa ujumbe wa Kristo tu aliposema sentensi moja kwa Paulo na timu yake: “Kama mmeniona kuwa mwaminifu kwa Bwana . . . ingieni nyumbani mwangu mkakae” (Matendo 16:15). Wakakubali, na ushirika wa kumcha Mungu ukanawiri. Lidia akawa kiongozi mwenye nguvu kwa Yesu.

Paulo akamtia moyo rafiki yake kijana na mbia wake Timotheo kwa maneno yafuatayo: “Bali wewe, mtu wa Mungu, uyakimbie mambo hayo; ukafuate haki, utauwa, imani, upendo, saburi, upole” (1 Timotheo 6:11). Timotheo alifuata na akaushikilia uzima wa milele. Sasa, barua mbili za Paulo kwa Timotheo zimekuwa sehemu ya Biblia yetu Takatifu.

Ilianza kwa sentensi rahisi. Phil alinambia, “Unapaswa kumwalika Scott aje seminari.” Basi nikampigia Scott na kumwalika ahudhurie seminari. Pia nikampa msaada wa masomo ya uinjilisti na nafasi ya kunisaidia katika majukumu yangu katika kanisa la nyumbani. Alihudhuria, akahudumu, na akastawi.

Baada ya kufuzu, Scott akachukua nafasi kama mhudumu wa uinjilisti katika kanisa imara. Kisha, akahudumu kama mchungaji mkuu wa kanisa lingine kwa miaka minane. Wakati wa uongozi wake, mahudhurio yalikuwa kuanzia mia nne hadi mia saba.

Kisha Scott, mke wake, na binti yake wakasikia wito wa Mungu watoke Marekani na wawe wamishenari. Scott akawa mratibu wa mikakati wa uwandani na akasimamia uanzishaji wa makanisa katika nchi nane tofauti.

Hatimaye, viongozi wa dhehebu lake wakamwita awe mkurugenzi wa shule ya Jumapili na uanafunzi, wa kimataifa kwa makanisa yote ya hilo dhehebu kote ulimwenguni.

Ninajua watu wengi na ushawishi wa kiungu umemkuza Scott, lakini bado, ninafurahi sana kwa sababu ya ile sentensi moja kutoka kwa Phil. “Unapaswa kumwalika Scott aje seminari.”

Kisha kuna ushauri wa Yohana kwa rafiki yake Gayo: “Mpenzi, usiuige ubaya, bali uige wema. Yeye atendaye mema ni wa Mungu” (3 Yohana 1:11).

Ni sentensi gani ambayo mtu alikwambia hivi karibuni? Ni sentensi gani ambayo umemwambia mtu mwingine? Ni kitu gani kitatokea siku za usoni kama matokeo?

AGOSTI 29 **241**

# Chukua Mzigo wa Mwingine

*Mchukuliane mizigo na hivyo kuitimiza sheria ya Kristo.*
*Wagalatia 6:2*

*Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna*
*kwa wakati wake, tusipozimia roho.*
*Wagalatia 6:9*

Urithi alioacha Harry Rich ni maisha ya huduma yenye nguvu na ya kuheshimik—kuanzia kuanzisha kanisa mara tu alipotoka chuo; hadi kuhudumu kama mishenari kule Haiti kwa miaka kumi na minne; hadi kuwa mchungaji wa makanisa mengine mawili; hadi kuhudumu kama mwangalizi wa wilaya wa kanisa lake kule Quebec; hadi kuanzisha huduma za nchi zinazozungumza Kifaranza kule Rwanda na Kongo. Katika vita, baada ya waumini 6,500 kuuawa kwa sababu ya dini, Harry Rich alijenga shule, akaanza chuo cha kitheolojia, na akaanzisha makanisa arobaini na manne katika kambi za wakimbizi. Sasa amestaafu, anaishi kule Waynesburg, Pennsylvania.

Kule Waynesburg, Harry alisaidia mtu na mkewe katika kanisa lake mahalia aliyekuwa na changamoto za kutembea—akajenga mahali mlango wao wa mbele ili wapate kutoka na kuingia kirahisi. Baada ya mumewe kufariki, yule mke akaenda kuishi katika nyumba za kuwasaidia watu wasiojiweza. Alipolazwa hospitalini, wasimamizi wa hiyo nyumba walimhamishia nyumba nyingine. Kwa namna fulani, katika uhamisho huo, chakula chake na vyombo vyake vya jikoni vilipotea. Harry alikuwa amekuwa akihudumu katika hiyo nyumba kwa kuwa na ibada za kila mara za Jumapili mchana. Alipokuwa akifanya hivyo, alihisi kwamba ni lazima amsaidie rafiki yake.

Mara ya kwanza, Harry alipanga kwenda dukani kumnunulia vyombo vya fedha na chakula. Hata hivyo, huu ulikuwa ni wakati wa zuio la kutotoka nje kitaifa mwaka 2020 kwa sababu ya kuenea virusi vya korona. Badala yake, Harry akaamua kwamba nyumbani kwake mwenyewe alikuwa na vitu vya kutosha mahitaji yake. Akachukua baadhi ya vyombo vyake na chakula akampelekea.

Nilisikia hii hadithi kutoka kwa mwana wa Harry aitwaye Dwight, ambaye pamoja na mkewe, Carolyn, wamehudumu kama wamishenari kule Ekwado kwa miaka thelathini iliyopita. Harry Rich—maisha yaliyoje. Ni urithi ulioje wa kuchukua mizigo ya wengine bila kuchoka kutenda mema. Harry ana miaka tisaini na miwili—mzee kuliko mkazi yeyote wa nyumba za maisha ya kusaidiwa alipokuwa akihudumu.

Kila mara ninashangazwa na mamia ya wafuasi wa Kristo wanaoishi maisha yao kwa uaminifu wa namna hiyo. Wewe, pia, unaweza kuwa sehemu ya hili kundi la mashujaa.

**AGOSTI 30** **242**

# Kwa Kweli Mungu Hubadilisha Watu

*Basi yule mtu akajibu, Kwamba yeye ni mwenye dhambi sijui. Najua neno moja, kuwa mimi nilikuwa kipofu na sasa naona.*
*Yohana 9:25*

Ushuhuda ufuatao ulitolewa katika ibada ya uamsho kule Boise, Idaho, tarehe 31 Oktoba, 2010:

> *Karibu miaka mitatu iliyopita, maisha yangu yalikuwa yamemalizwa na mihadarati na pombe. Nilikuwa katika uhusiano wa dhuluma, nilikuwa nimeacha chuo mara kadhaa, nilikuwa kila mara ninachelewa au kukosa kazini, na nilikuwa ninaishi tu. Nilikuwa peke yangu. Wakati nilipokuwa nimekata tamaa, nikaenda katika kanisa karibu na nyumbani na nikamwomba mhudumu aniombee nipate uhuru dhidi ya uraibu wangu. Usiku huo nilienda nyumbani na nikahisi vilevile, kwa hivyo nikaendelea kuishi maisha yangu kama nilivyokuwa nikiishi hapo awali. Nikaendelea kuishi hayo maisha ya kutisha, bila kujua kwamba Mungu amesikia maombi yangu. Miezi sita baadaye, nikakamatwa. Hilo lilikuwa tukio la kwanza kati ya matukio mengi ambayo yalinirudisha kwa Mungu. Serikali*

*ikaniambia ni lazima niende AA na ushauri la sivyo niende gerezani. Niliogopa.*

*Kisha Mungu akamweka mtu maishani mwangu (ambaye sasa ni mume wangu) aliyenishika mkono na tukaenda zaidi ya mikutano hamsini ya AA mpaka nikawa naweza kwenda peke yangu bila shida.*

*Kisha, kupitia kwa hiyo mikutano, Mungu akamwingiza mwanamke maishani mwangu aliyenifundisha jinsi ya kujipenda na kujisamehe mimi mwenyewe na kuomba kila siku.*

*Kisha Mungu akamwingiza mtu mwingine maishani mwangu aliyenitia moyo niache kuvuta sigara, na mwingine aliyenifanya nifikiri kuhusu kurudi shule.*

*Mimi na Andrew tulipoamua kuoana, tulitaka kufanya hivyo kanisani. Kisha Mungu akamwingiza mchungaji maishani mwangu aliyekuwa mvumilivu na mwelewa, na ambaye ananisaidia kuelewa neno la Mungu. Mungu ameendelea kufanya kazi maishani mwangu katika njia nyingi zaidi kuliko ninavyoweza kuhesabu. Kwa neema ya Mungu, sijanywa pombe wala kutumia mihadarati tangu tarehe 22 Aprili, 2008. Na sijavuta sigara tangu tarehe 19 Machi, 2009. Niliyatoa maisha yangu kwa Kristo tarehe 27 Agosti, 2010.*

*Kwa hivyo labda Mungu hakujibu maombi yangu kwa njia ile niliyofikiri kwamba angejibu—lakini akayajibu vilevile alivyohitaji mimi nipate kupona. Kisha akaendelea kuwaweka watu maishani mwangu walionisaidia kuendelea namna hiyo.*

*Sasa ninatumaini siku moja ninaweza kumhamasisha mtu kwa kumsimulia hadithi yangu na kumsaidia kumjua Mungu vilevile watu wengine walivyonisaidia. Ninajua maisha yangu ya awali si mazuri, lakini yalinileta mahali nilipo leo, na ninashukuru kwa hilo.*

Trish Thomas[123]

---

123. Awali ilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Machi 2011).

# Manufaa Yetu ya Kushangaza

*Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia.*
*Warumi 1:19*

Bila kujali haiba, historia, au usuli, wakati watu wengi wanapofikiri kuhusu uinjilisti, itikio lao la kwanza kwa kawaida ni hofu, wasiwasi, kukosa uhakika, na mfadhaiko.

Hata hivyo, Maandiko yanatupa makali ya kutayarisha njia kwa wanafunzi katika kazi yao ya uinjilisti. Makali ya kiroho ni kile ambacho Wa-Wesley wanaita "neema ya kulainisha," inayolainisha moyo wa mtu kabla hajakuwa Mkristo na ufahamu wa Mungu. Katika Warumi 5:8, Paulo anaandika, "Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi." Katika Warumi 1:19–23, inatukumbusha kwamba uumbaji wote unafahamu uwepo wa Mungu. Kulingana na Paulo, ufahamu huu wa Mungu upo hata katika mahali penye giza zaidi na penye dhambi zaidi. Zaidi ya hayo, katika Yohana 6:44, Yesu anatukumbusha kwamba hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka.

Binafsi, kabla kuja kwa imani, nilihisi huu ufahamu mkali wa Mungu na milele. Niliuhisi nilimpokuwa ninamwomboleza kaka yangu, aliyekufa akiwa na umri wa miaka kumi na tisa pekee. Huku tukiwa tunaishi katika huu wakati mgumu, nilitambua kwamba nilikuwa na uchaguzi kuhusu jinsi nitakavyoishi maisha ya milele—nilijua kwamba nilihitaji kumwitikia Mungu. Nilikuwa na tamanio la kuelekea kwa Mungu. Aidha, ninakumbuka kwamba wakati wa shida, "ningeweza" kusikia mhudumu katika redio au kuona ilani ya kanisa inayonikumbusha milele. Kila wakati, roho yangu ilivutwa na wazo la Mungu. Huu ulikuwa ni wakati wa neema ya kulainisha!

Ninamsifu Mungu kwa neema yake ya kulainisha iliyonitayarisha kwa muda mwaka 1976 wakati kijana mmoja aliponiuliza kama nitaweza kuingia mbinguni. Katika wakati uliofuata, kuendesha gari kwa dakika arobaini kutoka Virginia Beach hadi Williamsburg, Virginia, matukio haya yote ya neema ya kulainisha yalikuja mbele ya kumbukumbu yangu. Katika wakati huo muhimu sana, yule Mkristo kijana alihatarisha na akanifikia mimi. Ikawa wazi kwangu kwamba kuanzia wakati wa kuzaliwa kwangu, Roho wa Mungu

amekuwa akitayarisha roho yangu kwa ajili ya kukutana huko. Niliendesha gari, zile kumbukumbu za alama za vidole vya Mungu maishani mwangu za utotoni zilikuwa halisi zaidi kila maili. Nilipofika nyumbani, uwekezaji wa Roho na hatari iliyochukuliwa na Mkristo kijana vyote vilifika kilele katika wakati wa amani ulioyabadilisha maisha yangu milele.

Ninaamini Mungu ni mwaminifu na atafanya kazi yake katika njia zifuatazo:

- Alitupa Neno lake.
- Alituletea Mwanawe.
- Alitupa Roho wake Mtakatifu.
- Katika wakati huu, neema yake lainishi inafanya kazi katika mioyo na maisha ya kila mtu ambaye bado hajawa Mkristo, kumtayarisha kwa ajili ya kukutana na mashahidi.
- Yesu anatuomba twende tukafanye wanafunzi.

Inatia moyo kiasi gani kujua kwamba neema ya Mungu ya kulainisha inatutangulia. Nenda ukawaambie wengine kuhusu imani yako na uvune mavuno ukijua kwamba Mungu ametutangulia na anaenda pamoja nasi!

Mark Bane
Mkurugenzi Mukuu wa Uinjilisi na Ukuzaji wa Kanisa Jipya
Jimbo la USA/Canada
Kanisa la Nazarene[124]

**SEPTEMBA 1** **244**

# Ukweli Kutoka kwenye Misheni ya Uokoaji

*Kwa maana nilikuwa na njaa, mkanipa chakula; nilikuwa na kiu, mkaninywesha; nilikuwa mgeni, mkanikaribisha; nilikuwa uchi, mkanivika nilikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nilikuwa kifungoni, mkanijia.*
*Mathayo 25:35-36*

Kule Amerika, hakuna kundi kubwa zaidi la watu waliotengwa kuliko watu ambao wanaunda idadi ya watu wasio na makazi. Zingatia takwimu zifuatazo:

124. Awali ilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Disemba 2019).

- Asilimia 90–95 ya wanaume wasio na makazi na asilimia 60 ya wanawake wasio na makazi ni watumiaji wa dawa za kulevya.
- Umri wa wastani wa mtu mzima asiye na makazi ni thelathini na mitano.
- Zaidi ya asilimia 60 ya watu wasio na makazi ni wanawake na watoto.
- Zaidi ya nusu ya watu wazima wasio na makazi waliingizwa katika pombe au dawa za kulevya kabla ya umri wa miaka kumi na miwili
- Wengi wa wasio na makazi walinyanyaswa kimwili na/au kingono wakiwa watoto.

Kila siku, Misheni ya Sunday Breakfast hutoa zaidi ya milo mia nane kwa wanaume, wanawake na watoto wenye njaa. Baadhi ya usiku, zaidi ya wanaume mia tatu, wanawake, na watoto huwa kwenye makazi yetu. Takriban wanaume na wanawake mia mbili wamehitimu kutoka kwa programu yetu ya ufuasi ya miezi kumi na minane. Lakini tunapata furaha yetu kuu katika karibu watu elfu kumi ambao wamekabidhi maisha yao kwa Kristo katika miaka kumi na minne iliyopita.

Kasisi Tom Laymon, Sr.
Mkurugenzi, Sunday Breakfast Mission
Wilmington, Delaware[125]

**SEPTEMBA 2** **245**

# Si Mzee Sana

*Sasa basi, angalia, yeye BWANA ameniweka hai, kama alivyosema, miaka hii arubaini na mitano, tangu wakati huo BWANA alipomwambia Musa neno hilo, wakati Israeli walipokuwa wanapitia jangwani; na sasa tazama, hivi leo nimetimiza umri wa miaka themanini na mitano. Hata sasa mimi nina nguvu zangu hivi leo kama nilivyokuwa siku hiyo Musa aliyonituma; kama nguvu zangu zilivyokuwa wakati huo, na nguvu zangu ndivyo zilivyo sasa, kwa vita na kwa kwenda na kurudi.*
*Yoshua 14:10-11*

125. Awali yalichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Juni 2017).

Mark ni mume kijana, baba, na mfanyakazi wa muda kama mchungaji katika kanisa lake. Miaka mitano tu iliyopita, yeye na mke wake hawakuhudhuria hata kanisa. Kila kitu kilibadilika wakati, siku moja katika kukutana kibahati katika Applebee ya mtaani, mwanamume katika miaka yake ya sabini aliwaalika kwenye ibada.

Enoch ni mkandarasi kijana ambaye amejenga au kurekebisha makanisa kumi na mawili katika miaka kadhaa iliyopita. Anajitolea kwa kazi yake ya "kidunia" kutumikia makanisa. Akiwa kijana anayekaribia utu uzima, Enoch aliacha kanisa. Aliporudi, mtu mmoja alimfundisha kwa kutumia *'Basic Bible Studies for New and Growing Christians'*. Mtu huyo, aliyekuwa katika miaka yake ya sabini, baadaye alisimama kama mtu bora zaidi kwenye harusi ya Enoch.

Baada ya mke wake kufa akiwa kijana sana, Terry aliamua kumfuata Kristo kwa mara ya kwanza maishani mwake. Alimfikia mwalimu wake wa zamani wa darasa la sita, ambaye sasa alikuwa amestaafu, katika miaka yake ya sabini. Mwalimu huyu aliyestaafu alimwongoza Terry kwa Bwana kisha akamwongoza kupitia *Basic Bible Studies for New and Growing Christians*.

Vijana hawa watatu wanafanana kivipi? Tayari unajua—mwalimu yuleyule aliyestaafu ambaye hana sifa za kuhudumu alitekeleza wajibu wa kuzipata roho na kuwa mchungaji katika kila maisha ya mmoja wao. Je, ni lazima tuwe vijana ili tuwapate vijana? Usipendekeze hilo kwa baba yangu, John P. Sherwood—hafahamu vizuri zaidi. Naomba Mungu atusaidie tuinue jeshi lisilosahaulika kama Yohana.

Dkt. Scott Sherwood
Mrakibu wa Wilaya, Wilaya ya Kaskazinimagharibi mwa Illinois
Kanisa la Nazarene[126]

---

126. Awali yalichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Machi 2018).

# Je, ulimwacha Yesu Kwenye Maegesho?

*Wala si kwa utumwa wa macho tu kama wajipendekazao kwa wanadamu bali kama watumwa wa Kristo, mkitenda yampendezayo Mungu kwa moyo; kwa nia njema kama kumtumikia Bwana wala si mwanadamu.*
*Waefeso* 6:6-7

Keith Miller alikuwa ameenda seminari, akahudumu katika bodi mbili za kanisa, na kufundisha shule ya Jumapili. Siku moja, mfanyakazi mwenza aliyekuwa katika ofisi moja na Keith kwa zaidi ya mwaka mmoja alisema, “Keith, sikujua wewe ni Mkristo.” Keith alitambua kwamba, ingawa alikuwa amemkubali Kristo, alimwacha Kristo kwenye maegesho alipoingia eneo lake la kazi.

Maneno ya maandiko ya leo yalielekezwa kwa watumwa—hebu tushughulikie hilo. Kulikuwa na watumwa milioni sitini katika Dola ya Kirumi. Wengine walikuwa madaktari au walimu; wengine walikuwa vibarua wa kawaida. Ushawishi wa Ukristo hatimaye uliwaweka huru watumwa, lakini katika hatua hii ya historia, suala la haraka zaidi lilikuwa jinsi ya kufanya kazi mahali pa kazi. Tunaweza kujifunza kutokana na kifungu hiki tunapokisoma kwa kuzingatia muktadha wawafanyakazi na mabosi: Wafanyakazi, fanyeni kazi yenu vizuri—sio tu wakati bosi anapokutazama—kana kwamba mnamfanyia Kristo kazi, si bosi wenu. Mapenzi ya Mungu ni wewe ufanye kazi yako vizuri. Acha uhusiano wako na watu wenye mamlaka udhihirishe Kristo. Tangamana na mtu huyo mwenye matatizo kwa upendo na maombi.

Fanyeni kazi zenu kama kumtumikia Bwana; onyesheni kazi hiyo kwa Bwana. Mfanyakazi wa mstari-kusanyiko ambaye aliweka kiyoyozi kwenye gari langu lazima awe anajua. Maji yakiwa yanamwagika kwenye miguu ya mke wangu na kulowesha sakafu ya gari, nililazimika kwenda tena na tena kwa muuzaji ili kurekebisha tatizo hilo. Kazi mbaya ya mfungaji ilinipora muda wangu.

Ombea wafanyakazi wenzako unapoelekea kwenye mashine ya kahawa au chemchemi ya maji ya kunywa. Omba kwamba Mungu awafanye wakuulize swali sahihi ili uweze kushiriki habari njema za Kristo.

Mabosi, mnawajibika kwa jinsi mnavyowatendea wafanyikazi wenu. Kumbuka, Bwana yuko juu yako, na yeye hawachezei wapendwa (6:9).

Linapotukia suala la hali mbaya ya kazi, huwezi kuwa na uwezo wa kuziepuka, lakini unaweza kuzishinda. Kuhusu mamlaka, tii kama mtumishi wa Kristo. Kwa wale walio chini yako, usiwatendee kwa faida yako.

Huko India, C. T. Venugopal alimleta Kristo katika kazi yake kwenye barabara ya reli ya serikali. Hatimaye, akawa kiongozi wa juu katika barabara hiyo ya reli. Aliwaambia wafanyakazi wenzake, "Mimi ni Mkristo, lakini ninataka mnisaidie kuwa mtu bora zaidi." Aliwataka wamwambie alipokosea.

Wakati huo huo, kulikuwa na mvutano kati ya India na Pakistani. Mbinu ya India ilikuwa kuipa Pakistani rekodi moja kwa kila rekodi ambayo Pakistani iliwapa. Lakini Ndugu Venu, kama alivyoitwa, aliipa Pakistani rekodi zote, bila masharti yoyote.

Baada ya kupokea rekodi hizo kutoka kwa Venu, Waislamu nchini Pakistani walisema, "Hatuwezi kuwaacha Wahindu wawe bora kutuliko sisi." Kwa hivyo waliipa India rekodi zaidi.

Venu alipofichua kwamba Pakistani inadaiwa na India rupia 2,200,000 katika mpango huo, mtu fulani alisema, "Itazame."

Mwingine akasema, "Ikiwa Bw. Venu anasema hivyo, ni hivyo."

Sifa yake na tabia ya Kikristo ilimtangulia.

Acha hii iwe ukumbusho: Usimwache Yesu kwenye maegesho.

**SEPTEMBA 4** **247**

# Mkono wa Bwana Ulikuwa Pamoja Nami

*Nami nikatiwa nguvu, kwa kadiri mkono wa BWANA, Mungu wangu, ulivyokuwa pamoja nami, nikawakusanya wakuu wote katika Israeli, ili wakwee pamoja nami.*
*Ezra 7:28*

Nilipokuwa kijana, maneno mazuri zaidi niliyopata kuyasikia kutoka kwa baba yangu yalikuwa, "Mwanangu, ninajivunia kuwa nawe." Kwa maneno hayo, nilipata ujasiri wa kusonga mbele kwa ajili ya changamoto nyingine maishani. Kiajabu, maneno yale yalinifanya nihisi mkono wake ulikuwa begani kwangu, kana kwamba kusema, *Kazi njema, au, Umefanya vizuri*; kana kwamba kusema, *Unaweza kuifanya*, au, *Nitakupa mwelekeo*; kana kwamba kusema, *Hii ndiyo njia ya kwenda kusikojulikana*.

Ezra, pia, alihisi mkono usioonekana begani mwake—mkono wa Bwana. Bwana alikuwa ameusukuma moyo wa Cyrus, mfalme wa Uajemi, kuamuru kujengwa upya kwa hekalu huko Yerusalemu na kutoa kibali kwa wakimbizi warudi (Ezra 1:2–4). Sasa, Mfalme Artashasta alimwagiza Ezra achukue fedha, dhahabu, vyombo vya hekalu, na watu wa kuandaa hekalu na kufundisha sheria ya Mungu. Baada ya safari ya miezi minne, Ezra alifika Yerusalemu. Katika utume wake wote, Ezra alihisi mara kwa mara mkono wa Mungu alipopokea yafuatayo: Yote ambayo Ezra aliuliza (7:6); safari salama (7:9); ujasiri wa kukusanya viongozi (7:28); viongozi wenye uwezo (8:18); ulinzi barabarani (8:22); ulinzi dhidi ya majambazi (8:31).

Niliandika ingizo lifuatalo katika shajara yangu ya ibada binafsi: *Kuishi katika uwepo wako wenye upendo na wenye nguvu ndiyo furaha yangu kuu. Mara nyingi, nasema, "Weka mkono wako juu yangu." Sitaki kupunguza furaha kuu ya uwepo wako kamili; ni njia yangu ya mkato ya kusema, "Bwana, uwe nami katika jambo fulani. Mkono wako juu yangu unazungumza juu ya uthabiti, nguvu, kuinuliwa, kutia moyo, mwongozo."*

Bwana angependa kuweka mkono wake juu *yako*.

**SEPTEMBA 5** **248**

# Dola Moja Tu

*Maana, upendo wa Kristo watuongoza.*
*2 Wakorintho 5:14*

*Katika neno la kweli, katika nguvu ya Mungu; kwa silaha za haki za mkono wa kulia na za mkono wa kushoto; kwa utukufu na aibu; kwa kunenwa vibaya na kunenwa vema; kama wadanganyao, bali tu watu wa kweli; kama wasiojulikana, bali wajulikanao sana; kama wanaokufa, kumbe tu hai; kama wanaorudiwa, bali wasiouawa.*
*2 Wakorintho 6:7-9*

Ilikuwa karibu Krismasi, na fedha zetu zilikuwa chache. Tungenunua zawadi kwa ajili ya watoto wetu watatu, lakini mimi na Nancy tulikubali kutumia dola moja tu kwa ajili ya kila mmoja wetu.

Nilikuwa nimeingia katika uinjilisti wa wakati wote, ambao ulimaanisha kusafiri hadi jiji tofauti na kanisa kila juma. Mara nyingi, sikujua ni kiasi gani

kanisa fulani lingenilipa. Kama ishara ya kujisalimisha kwangu kikamilifu kwa Mungu, sikuwapa kiwango mahsusi.

Kama mkristo, najua kuna nyakati ambapo ni lazima nipiganie haki za wengine. Lakini kwangu, nikiwa msemaji wa Mungu, niliamini kwamba ikiwa ni lazima nipiganie haki yangu, huenda Mungu akaniacha nifanye hivyo. Hata hivyo, niliamini pia kwamba ikiwa ningesalimisha haki yangu ili niwe mtumishi wa wote, basi Mungu aliyeniita angenipigania. Ninaamini sana maneno ya Yohana 12:25: "Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza; naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele."

Muda mfupi kabla ya Krismasi yetu yenye changa moto ya kifedha, nilisafiri masafa marefu hadi kwenye kanisa dogo kwa ajili ya mkutano wa uamsho. Niliingia kwenye mkutano, na kulikuwa na uamsho wa kweli. Nilipokuwa nikitoka kanisani usiku wa mwisho, kasisi alinipa hundi ambayo baadaye niliona ilikuwa chini ya gharama zangu halisi za juma hilo. Nilimshukuru. Mapema katika huduma yangu, nilijitolea kushukuru kwa kila toleo nililopewa, hata liwe dogo kiasi gani. Hakuna wakati wowote katika wiki ambapo nilitoa maoni yoyote kuhusu mahitaji yangu binafsi ya kifedha.

Nilipokuwa nikielekea kwenye gari langu, mwanamke aliyekuwa amepata msaada wa kiroho juma hilo alinisimamisha. Alibonyeza kipande cha karatasi mkononi mwangu na kuniambia nitazame nyuma ya gari langu. Nyuma ya gari, nilipata gunia la mboga na matunda, sanduku la mboga, sanduku lililofungwa kwa karatasi ya Krismasi iliyosema, "Kwa Nancy, kutoka kwa Chic," na sanduku lililofungwa, "kutoka kwa Nancy." Tulipofungua masanduku hayo baadaye, tuligundua kwamba sanduku la Nancy "kutoka" kwangu lilikuwa na nguo mbili maridadi, na sanduku langu "kutoka" kwake lilikuwa na Biblia ya gharama kubwa ambayo nilitamani lakini sikuweza kuinunua. Nilipoikunjua karatasi aliyonipa mwanamke huyu, nilikuta hundi binafsi ikiwa imetolewa kwa kiasi ambacho kilikuwa thuluthi mbili ya kiasi ambacho kanisa lilikuwa limenilipa.

"Dola moja tu." Hiyo tu ndiyo ningeweza kutumia kwa Nancy kwenye Krismasi, na Nancy angetumia kwangu kiasi hicho hicho. Hakuna mtu katika kanisa aliyejua kuhusu hili. Bado "ulinzi wetu pekee, silaha yetu pekee, ni maisha ya uadilifu." Na, "Siku zote 'tunaipitia' lakini kamwe 'hatuendi chini.'"

# Mwajiri Mcha Mungu

*Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu, na Timotheo aliye ndugu yetu, kwa Filessmoni mpendwa wetu, mtenda kazi pamoja nasi, na kwa Afia, dada yetu, na kwa Arkipo askari mwenzetu, na kwa kanisa lililo katika nyumba yako.*
*Filemoni 1:1-2*

*Naomba ili kwamba ushirika wa imani yako ufanye kazi yake, katika ujuzi wa kila kitu chema kilicho kwetu, katika Kristo.*
*Filemoni 1:6*

Biashara yake haikuwa kubwa, lakini ilikuwa yake binafsi. Na kutoka katika biashara hiyo ya kituo cha mafuta, Clyde aliiacha nuru yake imuangazie Yesu.

Kama vile Filemoni wa zamani, mtindo wa maisha wa Clyde ungeweza kuwa na sifa ya maneno mawili: "kanisa linalokutana nyumbani kwako" (1:2), na "ushirikiano wako pamoja nasi katika imani" (1:6). Filemoni alimpenda Kristo sana kiasi kwamba alitoa bila choyo nyumba yake nzuri kwa ajili ya ibada ya kila Siku ya Bwana.

Ingawa Clyde hakuwa amepanga ibada za kanisa nyumbani kwake, yeye na mke wake mrembo waliwakaribisha watu wa Mungu kwa ukarimu baada ya ibada nyingi za kanisa. Baadhi ya maombi yaliyofanyika katika nyumba hiyo yalitakasa mahali pale kana kwamba palikuwa kanisa.

Huduma ya Clyde inaweza pia kuelezewa kwa maneno "kanisa linalokutana katika kituo chako cha mafuta." Alipofunga kituo chake kwa mara ya kwanza Jumapili, watu walisema ni mjinga; lakini Clyde alifurahi kumtii Mungu. Kwa bahati nzuri, faida yake ilikuwa kubwa katika siku sita akiwa na Mungu kuliko katika siku saba alizokuwa bila Mungu.

"Ushirika katika imani"—Clyde alidhihirisha hivyo pia. *Aliangaza* kwa ajili ya Yesu; aliwaambia watu kuhusu Kristo; hata akaingiza familia ya mmoja wa wafanyakazi wake kanisani.

Inapokuja kwa Filemoni au Clyde, akina Paulo wa kila zama hufurahi katika uaminifu wao. Ee, Bwana, ongeza idadi yao.[127]

127. Awali yalichapishwa katika *Come Ye Apart* October–Novemba–Disemba 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 75. Imetumiwa kwa idhini. (Chapisho hili

# Vipi kama Wangetaka Sandwichi za Siagi ya Karanga?

*Na jua likaanza kushuka; wakamwendea wale Kumi na Wawili, wakamwambia, Uage mkutano, ili waende katika vijiji na mashamba ya kandokando wapate mahali pa kulala na vyakula, maana hapa tulipo ni nyika tupu. Akawaambia, Wapeni ninyi chakula. Wakasema, Hatuna kitu zaidi ya mikate mitano na samaki wawili, tusipokwenda tukawanunulie watu hawa wote vyakula. Kwa kuwa wanaume waliokuwako walikuwa kama elfu tano. Akawaambia wanafunzi wake, Waketisheni watu kwa safu, kila safu watu hamsini. Wakafanya hivyo, wakawaketisha wote. Akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni akavibariki, akavimega, akawapa wanafunzi wake ili wawaandalie mkutano. Wakala, wakashiba wote; na katika vile vipande vilivyowabakia walikusanya vikapu kumi na viwili.*
*Luka 9:12-17*

Mlei mmoja mwerevu sana alikuwa akifanya kazi na mchungaji wake kwenye wikendi ya mashahidi wa kawaida. Kwa namna fulani walianza kujadili muujiza wa kulisha watu elfu tano (Kumbuka, *wanaume* elfu tano wanaweza kumaanisha kitu zaidi kama *watu* elfu kumi au kumi na tano elfu tunapohesabu wanawake na watoto.) Kwa uwezo wake wa kiungu, Yesu aliwahudumia wote kwa sandwichi za samaki.

Katika hatua hii ya majadiliano, mlei aliongea kwa sauti, "Itakuwaje kama wangetaka sandwichi za siagi ya karanga?"

Alisema hivyo kwa mzaha, lakini maneno yake yanaeleza mtazamo wa watu wengi kuelekea kazi ya Yesu yenye neema. Tamaa zao ndogo hupewa kipaumbele juu ya matendo ya Mungu, na hukosa baadhi ya baraka kuu ambazo Mungu anataka kutia katika maisha yao. Fungua moyo wako uelewe hadithi hii.

Hebu tuchunguze baadhi ya ujumbe tunaouona katika maelezo haya ya maandiko:

1. Wanafunzi wakasema, "Uage umati ..." (Wacha watu wafanye wawezavyo.)
2. Akasema, "Ninyi wapeni chakula" (Wajibikeni kwa ajili ya umati.)

---

lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

3. Wakasema, “Tunayo mikate mitano tu…na samaki wawili.” (Nyenzo zetu ni chache sana—hili haliwezekani!)
4. Akasema, “Waketishe…” (Nina jibu. Tazama!)
5. “Wanafunzi wakafanya hivyo.” (Hii ilikuwa hatua nzuri zaidi kwa wanafunzi—walimtii Yesu. Na walifanya hivyo bila kufahamu lolote.)
6. Alichukua mkate na samaki na, “akatazama juu mbinguni,” akashukuru. (Aliwaonyesha jibu pekee lilikuwa kwa uwezo wa Mungu.)
7. Aliwapa chakula “wanafunzi wawagawie watu.” (Ni vyema hatimaye kupatana na mapenzi ya Mungu.)
8. “Wote wakala wakashiba, na wanafunzi wakaokota vikapu kumi na viwili” vya masalio. (Kama mhubiri mmoja alivyosema, “Hakuna uhaba, hakuna upotevu, hakuna takataka.”)

Katika hadithi hii, tunaona tofauti kati ya njia ya wanafunzi na njia ya Kristo. Je, umefika mahali ambapo umegundua kwamba njia ya Kristo ndiyo bora zaidi? “Wote walikula na kushiba,” na ilikuwa baraka nyingi sana hivi kwamba kulikuwa na mabaki.

**SEPTEMBA 8** **251**

# Ah! Pumzika!

*Maana kama Yoshua angaliwapa pumziko, asingaliinena siku nyingine baadaye. Basi, limesalia pumziko la sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika pumziko lake amepumzika mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyopumzika katika kazi zake. Basi, na tufanye bidii kuingia katika pumziko lile, ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.*
*Waraka kwa Waebrania 4:8-11*

Ninapomwona Dan mara tu baada yake kutoka kazini, naona uchovu. Vifurushi anavyoinua vinaweza kuwa na uzito wa hadi pauni 75, na atashughulikia vifurushi 1,200 katika zamu yake. UPS hutoa takriban vifurushi 160,000 kutoka kwenye ghala lake maalum katika kipindi cha saa ishirini na nne. Dan anaporudi nyumbani, kitu kitamu zaidi anachoweza kupata ni kupumzika. Ah! Pumzika!

Neno la Mungu hutoa pumziko kwa watu wa Mungu. Katika Waebrania 4:1–11, tunasoma juu ya aina nne za mapumziko: pumziko la uumbaji,

pumziko la Sabato, pumziko la Kanaani, na pumziko la kiungu. Matatu ya kwanza ni vielelezo na mifano ya pumziko la kiungu.

Mafanikio makubwa mawili ya Israeli yalikuwa ni kuvuka Bahari Nyekundu na kuvuka Mto Yordani. Walikodhamiria, nchi ya ahadi, ilikuwa pawe makao yao. Mara baada ya kuvuka Bahari Nyekundu, walikuwa karibu kuingia katika nchi ya ahadi. Lakini katika wakati huo tatanishi, walichagua shaka badala ya imani—wakakataa ripoti ya wapelelezi wawili waaminifu waliowahimiza waingie nchini. Kutokana na kutotii kwao, walitangatanga jangwani kwa muda wa miaka arobaini hadi mwishowe Yoshua akawaongoza.

Mungu aliitoa Israeli kutoka Misri ili aweze kuipeleka katika nchi ya ahadi. Wasomi wengi wa Biblia wanaamini kwamba kuachiliwa kutoka katika utumwa wa Misri kunaashiria wokovu, na kuingia katika nchi ya baraka kunaashiria utakaso. Wakati Yoshua akiwapa watu pumziko la kutoka katika kutangatanga jangwani, bado kuna pumziko jingine kwa watu wa Mungu leo—pumziko la kimungu; pumziko la Sabato. Hili ni muhimu sana kiasi kwamba Mungu anatusihi, "fanya bidii ili ushiriki katika pumziko hilo" (4:11).

Ni Wakristo wangapi leo, wakiwa wamemkubali Kristo kwa dhati na kumfuata kwa kiasi fulani, wanajikuta wakihangaika, wasiwasi, kukosa raha, na kulemewa?

Hebu somo kutoka katika historia litusaidie. AB Earle alikuwa mwinjilisti wa Kibaptisti ambaye huduma yake ilianzia mwaka 1830 hadi 1880 huko Marekani, Kanada, na Visiwa vya Uingereza. Alisafiri maili 325,000 kote Marekani na Kanada, alihubiri mahubiri 19,780, na kuona watu 150,000 wakidai kuwa wameongoka katika mikutano yake. Ingawa Earle alipenda kazi ya huduma, aliripoti kwamba "kwa muda mrefu nilihisi machafuko ya ndani, pengo katika nafsi yangu ambalo halikuwa limejazwa... kama ningekuwa na amani, nilihofia kwamba isingeendelea, na haikutimia." Wakati huohuo, maisha yake ya Kikristo yalikuwa pandashuka—mara ya furaha, kisha ya huzuni. Alisema, "Pumziko ndani ya Yesu ambalo nilitamani lilikuwa bado halijapatikana." Dhambi moja iliyomsumbua sana ni azimio lake la kuwa na njia yake mwenyewe. Alitambua kwamba, "kabla ya kujazwa na utimilifu wa upendo wa Kristo, lazima niwe mtupu wa nafsi yangu." Wakati wa mkutano huko Cape Cod, baada ya miaka mingi ya maombi, kutafuta, na kuwekwa wakfu tena, Earle alitoa ushuhuda ufuatao: "Nilikuwa chumbani kwangu peke yangu, nikiomba utimilifu wa upendo wa Kristo, ghafla amani tamu ya mbinguni ilijaza utupu katika nafsi yangu, bila kuacha kutamani, machafuko, wala hisia zisizoridhika kifuani mwangu... Kisha kwa mara ya kwanza maishani mwangu, nikapata pumziko ambalo ni zaidi ya amani... Badiliko hili lilitokea karibu saa kumi na moja, siku ya pili ya Novemba

1863… Mbingu ya amani na pumziko kujaza roho yangu. Mchana na usiku Mwokozi anaonekana kuwa nami."[128]

AB Earle aliendelea katika huduma yake kwa nguvu mpya na ushindi mkubwa zaidi. Maisha yake ya kibinafsi yaliwekwa alama ya amani ya ndani na pumziko. Hata aliandika kitabu kiitwacho *The Rest of Faith*. Si ajabu!

Ah! Pumzika! Jua kwamba wewe pia unaweza kuipitia.

**SEPTEMBA 9** **252**

# Kurudi Kutawala

*Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani.*
*Waefeso 3:16*

Andy na Heather walipokuwa wakikabili matatizo katika kazi yao ya kwanza kwa kanisa, Heather alinitumia ujumbe ufuatao:

> *Bila ya kusema, mabadiliko mengi yametokea katika maisha yetu na yametumika kunivuruga kutoka katika lengo letu kuu hapa—kulifanya kanisa hili kuwa hai tena. Hata hivyo, tangu kusikia ujumbe wako, nimegundua kwamba, ingawa kweli nilitakaswa miaka kadhaa iliyopita, tangu wakati huo nimemsukuma Kristo kutoka kwenye kiti cha enzi cha moyo wangu na kukirukia, tayari kujitawala mwenyewe. Nilianza kuhisi matokeo ya kufanya hivyo: huzuni, wasiwasi, kutokuwa na tumaini, na hisia ya kweli ya kushindwa kuhusu kanisa kabla hata halijaanza!*
>
> *Ujumne wako ulitoka kwa Roho Mtakatifu moja kwa moja ndani ya moyo na akili yangu, na nimemwomba Bwana Yesu atawale zaidi moyoni mwangu kwa mara nyingine tena. Nimeanza kuomba na kusoma Biblia yangu, na bado sijui jinsi Bwana atakavyopuliza uhai katika kanisa hili au jinsi gani tutafanya kila jambo linalohitajika kufanywa, najua kwa hakika amerudi kutawala, kama anavyopaswa kuwa, na tunajikaza kwa mara nyingine tena kusikia mwelekeo wake. Kwa mara nyingine tena ninawaka moto kwa ajili ya Bwana, na nina shauku kuhusu kile atakachofanya katika huduma hii.*

---

128. James Gilchrist Lawson, *Deeper Experiences of Famous Christians* (Anderson, IN: Warner Press, 1911), 301–09.

Hebu tuwe na hakika kwamba Bwana Yesu ni mtawala mkuu katika mioyo yetu! [129]

SEPTEMBA 10 **253**

# Katika Shinikizo

*Akamwambia, Jina lako hutaitwa tena Yakobo, ila Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu, nawe umeshinda.*
*Mwanzo 32:28*

Je, umewahi kuhisi shinikizo?

Yakobo aliwahi kuhisi.

Mjanja; asiye mwaminifu; mdanganyifu. Alizaliwa akiwa ameshika kisigino cha ndugu yake pacha, anaitwa Yakobo, kumaanisha "mshikaji wa kisigino," au kwa njia ya kitamathali, "mdanganyifu" (Mwanzo 25:26). Akiwa kijana anayekaribia utu uzima, anamuuzia Esau, ndugu yake mwenye njaa na mzembe, bakuli la maharagwe kubadilishana na haki ya mzaliwa wa kwanza ya Esau. Haki hii ya mzaliwa wa kwanza inajumuisha sehemu kubwa zaidi ya urithi kutoka kwa baba yao. Baadaye, baba yao Isaka alipokuwa mzee na kipofu, Yakobo na mama yake wanamdanganya ili ampe Yakobo baraka za Esau.

Esau anapopata habari hiyo, anapaaza sauti kwa hasira, "Je! si kihalali anaitwa Yakobo? Hii ni mara ya pili amenitumia vibaya: Alichukua haki yangu ya mzaliwa wa kwanza, na sasa amechukua baraka yangu!" (Mwanzo 27:36). Kwa hasira yake, Esau anatishia kumuua Yakobo. Anapopata taarifa hizo, Yakobo anakimbia.

Kufikia hapa, ingawa Isaka alikuwa ametamka baraka juu ya Yakobo, hakuna jambo linaloonyesha kwamba Yakobo ana uhusiano wa kibinafsi na Mungu. Kwenye shinikizo la vitisho vya kaka yake, Yakobo anasimama usiku kucha huko Betheli. Hapo, Mungu anajidhihirisha kwa Yakobo, akimwambia, "Mimi nipo pamoja nawe." Kwa mara ya kwanza, Yakobo ana uhusiano na Mungu mweza yote.

129. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Juni 2006).

Yakobo anawasili Padan Aramu na kupata wake wawili kwa kufanya kazi kwa miaka kumi na minne kwa mjomba wake Labani. Hatimaye, Labani alimtendea Yakobo na familia yake kwa ukali sana kiasi kwamba Yakobo anaamua kuwachukua wakewe, watoto, na mifugo yake arudi nyumbani. Labani anamfuata Yakobo, hatimaye, wanafikia makubaliano.

Sasa, anapokaribia nchi ya kwao, Yakobo anapaswa kukabiliana na ndugu ambaye ametishia kumuua. Usiku kucha huko Penueli, Yakobo anashindana mweleka na Mungu, akidhamiria kupokea baraka za Bwana. Mwishowe, Mungu anagusa sehemu ya ndani kabisa ya moyo wake na kubadilisha jina lake kutoka kuwa "Yakobo" na kuwa "Israeli," kumaanisha, "anashindana na Mungu." Mabadiliko haya ya jina yanaashiria mabadiliko ya tabia.

Baada ya pambano hilo la kimungu, Israeli na Esau wanaungana tena katika msamaha na upendo. Yakobo anakuwa kiongozi wa kiroho wa familia yake na baba wa makabila kumi na mawili ya Israeli.

Matukio mawili makuu ya Israeli na Mungu ni ishara ya safari yetu ya kiroho leo. Kwanza, mkubali Kristo na uingie katika uhusiano na Mungu. Baadaye, Mungu huchunguza hadi viwango vya ndani kabisa vya moyo wako na kufichua ubinafsi unaohitaji utakaso na kujisalimisha kikamilifu. Kama katika hadithi ya Yakobo, shinikizo la hali mara nyingi hutuleta mahali hapo.

Ndiyo, shinikizo! Na katika siku zetu!

Akiwa kijana, Dick Fields alienda kufanya kazi katika Nazarene Publishing House. Alikuwa mfuasi wa Kristo, lakini sehemu ya kazi yake ilikuwa ngumu na ilimtia shinikizo. Hapo nyuma, mitambo mikubwa ya uchapishaji ilivuta karatasi kupitia mtambo wa kuchapa kwa kitambaa. Wakati mwingine kitambaa kilichanika. Dick angelazimika kutambaa chini ya mtambo wa kuchapa, alale chali kwenye uchafu, na kushona kitambaa huku mafuta yakimwagika kwenye mwili wake. Alisema, "Sitaki kufanya hivi maisha yangu yote!" Kisha akasita. Dick aliomba, "Bwana, ikiwa unataka nifanye hivi maisha yangu yote, nitafanya."

Baadaye, Dick alisema, "Ninaamini ndipo Mungu aliponitakasa."

Dick aliendelea kufanya kazi kwa miaka hamsini na minne akiwa Nazarene Publishing House (ambayo ilikuja kuwa The Foundry Publishing mnamo mwaka 2018). Hatimaye aliinuka na kuwa meneja wa uzalishaji. Kazi yake ilichangia utoaji wa machapisho ya Kikristo kwa mamilioni ya watu. Chini ya shinikizo, chini yam tambo wa kuchapa, chini ya mafuta, kujisalimisha kwake kamili kwa Mungu kulileta uwepo wa utakaso kwa tabia yake. Katika mazishi yake, Dick Fields alielezewa kwa kutumia maneno yafuatayo:

1. Joto linaloambukiza
2. Heshima, usikivu, uaminifu

3. Utiifu wa kudumu
4. Mchungaji wa zamani alisema, "Katika miaka ishirini na mitatu, sijawahi kuona Dick akiyumbayumba katika kufanana na Kristo."
5. Mtu mwingine alishuhudia, "Mungu alitupa Dick Fields ili uweze kujua jinsi Mungu alivyokuwa."

Je, utaruhusu shinikizo unalokumbana nalo likusukume kumtafuta Mungu hadi abadilishe jina lako; tabia yako; moyo wako; mipango yako; Mustakabali wako?

**SEPTEMBA 11** **254**

# Yesu Alikuwa Amechoka

*Na hapo palikuwa na kisima cha Yakobo. Basi Yesu, kwa sababu amechoka kwa safari yake, akaketi vivi hivi kisimani. Nayo ilikuwa yapata saa sita.*
*Yohana 4:6*

Pengine rais mkuu zaidi katika historia ya Marekani alikuwa Abraham Lincoln. Tuna ripoti zifuatazo kuhusu Lincoln katikati ya Vita vya wenyewe kwa wenyewe: "Lincoln alilala kwa dhiki usiku baada ya mwingine alipokuwa akijaribu kutafuta migawanyiko na kufuata wimbi la vita linaloenda kwa kasi."[130] "Lincoln aliona jeshi la Muungano likipigwa vibaya, sifa ya jenerali ilivunjwa, Washington ikitishwa na adui."[131]

Mnamo Mei 6, 1863, Ikulu ya White House ilipokea habari kwamba Jeshi la Potomac lilikuwa limepigwa vibaya katika Vita vya Chancellorsville. Ripota wa gazeti ambaye alikuwa katika Ikulu ya Marekani wakati huo aliona kwamba "uso wa rais uligeuka kuwa kijivu; hakuwa amewahi kuonekana amevunjika moyo na kukata tamaa. Akiinamisha Kichwa, mikono imetundikwa kwa nguvu mgongoni mwake, alitembea ofisini kwake, akiguna, 'Mungu wangu! Mungu wangu! Nchi itasema nini? Nchi *itasema* nini?'"[132]

Ndiyo, hata walio bora na wakuu zaidi miongoni mwetu hupitia nyakati zao za kibinadamu—nyakati zao za shinikizo na mahangaiko, akili na miili

130. Benjamin Thomas, *Abraham Lincoln* (New York: Alfred A. Knopf, 1952), 336.
131. Thomas, *Abraham Lincoln*, 338
132. Thomas, *Abraham Lincoln*, 369–70.

yao inapoathiriwa sana. Yesu Kristo, Mwokozi na Bwana wa ulimwengu, alipitia nyakati hizi pia.

Katika Yohana 4, Yesu anaposafiri (pengine kutembea) kutoka Yudea kwenda Galilaya, anapitia Samaria, eneo hasidi la Wayahudi. Katika mji wa Sikari, akiwa amechoka kwa sababu ya safari yake, anaketi kando ya kisima. Akiwa kawaida sana—Yesu Kristo mwenye nguvu amechoka, kwa hiyo anaketi. Waandishi wa Biblia wako makini kueleza kwamba Yesu ni mwanadamu kamili na Mungu kamili. Waraka kwa Waebrania 4:14-15 "Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa kama sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi."

Ni muhimu kuelewa baadhi ya maumivu na mapungufu ambayo Yesu anapitia. Katika Mathayo 13:57, anadharauliwa na mji wake mwenyewe. Katika Mathayo 26:38–40, anahisi huzuni kuu anapokabili kifo msalabani na anafadhaika kwa kukosa kuungwa mkono na wanafunzi wake. Katika Luka 4:1–2, ibilisi anamjaribu wakati ana njaa kutokana na kufunga. Katika Luka 19:45, anakasirishwa na kufanywa biashara katika hekalu. Katika Yohana 11:35, analia juu ya kifo cha rafiki mpendwa. Katika nyakati hizi zote, tunahisi ubinadamu wake na ufahamu wake kwetu. Amekuwa amechoka, kudharauliwa, huzuni, taabu, kujaribiwa, njaa, hasira—uzoefu sawa tunaokuwa nao kila siku.

Hata akiwa amechoka na kuketi kando ya kisima, bado Yesu anatoa ushawishi wake kwa wengine. Anakutana na mwanamke Msamaria mwenye kiu na mwenye dhambi na kumpa maji ya uzima. Anarudi katika mji wake, akitangaza kwamba amempata Masihi. Wasamaria wengine wanatoka katika mji huo, wanakuwa waumini, na kusema, "Mtu huyu hakika ndiye Mwokozi wa ulimwengu" (Yohana 4:42).

Vivyo hivyo, je, hatuwezi, ingawa tumechoka na kujaribu katika njia nyingi, bado tuwe na ushawishi wetu wa kiroho kwenye ulimwengu unaotuzunguka? Ndiyo, tunaweza—kwa sababu ya uhusiano wetu na Mwokozi wa ulimwengu.

# Je, Mungu Anaweza Kukuamini kwa Kiasi Gani?

*Ni nani basi yule mtumwa mwaminifu mwenye akili, ambaye bwana wake alimweka juu ya nyumba yake, awape watu chakula kwa wakati wake? Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo. Amin, nawaambieni, atamweka juu ya vitu vyake vyote.*
*Mathayo 24:45-47*

Yesu alituambia kuwa "Kwa maana watatokea Makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, ikiwezekana, hata walio wateule" (Mathayo 24:44). Hivyo, uaminifu kamili kwa kazi uliyopewa na Mungu ndiyo hakikisho pekee la utayari wako wa kukutana na Kristo. Zaidi ya hayo, uaminifu katika majukumu madogo ndio mlango wa majukumu makubwa zaidi katika siku zijazo.

Ed alikuwa mshiriki mwaminifu wa kanisa lake la mtaa. Mchungaji wake, alivutiwa na utauwa wake na talanta yake, alitabiri hatimaye angekuwa makamu wa rais wa US Steel. Kwa hakika, kampuni yake ilimpa kazi kubwa na nyongeza ya malipo. Hata hivyo, kituo kichanga cha kanisa ambacho Ed alikuwa amejitolea kilimhitaji sana, kwa hivyo akakataa kupandishwa cheo kwa ajili ya ufalme. Kutokana na hayo, kanisa lake likawa na nguvu zaidi.

Baadaye, US Steel ilimwomba Ed asimamie kiwanda huko Italia ambapo angekuwa na wafanyakazi 3,500 chini yake. Wasimamizi waliona ulikuwa wakati wa kuteua meneja mwenye maadili ya Kikristo—hasa kwa vile wasimamizi wengi wenye maadili madogo hawakuwa wamefanya vyema. Dhehebu la Ed pia lilikuwa limeanzisha kanisa katika jiji ambalo Ed angekuwa akitumikia. Je, ni aina gani ya matokeo ya kiroho ingeleta kwa wafanyakazi 3,500 kuona meneja wao Mkristo akimtumikia Mungu katika kanisa mahalia?

Ijapokuwa hawakuwahi kamwe kukosa ibada, Ed na mke wake, Evelyn, walikamilisha uuzaji wa nyumba yao, wakafunga virago vyao, na kujitayarisha kwa ajili ya safari yao ya kuelekea Italia huku kanisa lao mahalia likifanya ibada za uamsho.

Jumapili hiyo asubuhi, Evelyn alinijia akilia. Mwana wao na mke wake walikuwa hawamtumikii Bwana na hawakuwa wamemjibu Mungu katika ibada ya asubuhi. Nilimsihi Evelyn awe na subira kwa Bwana.

Hakika, katika ibada ya usiku huo, mtoto wa Ed na Evelyn na binti-mkwe walimpata Bwana. Zawadi nzuri sana ya kuwaaga.

Ed na Evelyn walikuwa waaminifu katika jambo dogo, na Mungu alikuwa akiwakabidhi mambo makubwa zaidi. Mada ya Mathayo 24:47 — "atamweka juu ya mali yake yote"—inarudiwa mahali pengine katika Maandiko:

- Mathayo 25:21 — "Umekuwa mwaminifu katika mambo machache; nitakuweka juu ya mambo mengi."
- Luka 16:10 — "Yeyote anayeweza kuaminiwa katika kidogo sana anaweza kuaminiwa pia katika mengi."
- Luka 19:17 — "Kwa kuwa umekuwa mwaminifu katika jambo dogo sana, simamia miji kumi."

Je, unaelewa maana yake? Kama vile Bwana alivyoniambia siku moja, "Kama ninaweza kukuamini kwa jambo dogo leo, ninaweza kukuamini kwa jambo kubwa zaidi kesho." Je, Mungu anaweza kukuamini hadi lini?

**SEPTEMBA 13** **256**

# Chukua Hatua Inayofuata

*Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.*
*Wagalatia 6:9*

Jimmy Carter alikuwa rais wa Marekani, shah wa Iran alilazimika kuondoka kwenye nafasi yake, na Wairani wengi waliikasirikia serikali ya Marekani. Umati wa vijana Wairani ulivamia Ubalozi wa Marekani mjini Tehran na kuwakamata wanadiplomasia wote wa Marekani. Muda si muda, Earl na Hazel Lee, makasisi wa kanisa lenye nguvu huko Pasadena, California, waliambiwa kwamba mwana wao, Gary, alikuwa miongoni mwa wafungwa. Lakini hawakuwa na mawasiliano na Gary. Hazel hakujua kama mwanawe alikuwa hai au amekufa, aliteswa au alikuwa salama, alikuwa na njaa au kalishwa. Alipata msongo, wasiwasi, na unyogovu.

Ilikuwa Jumapili asubuhi. Afanye nini? Alipokuwa akiomba, alisikia sauti ya Bwana ikisema, "Chukua hatua inayofuata." Kwa Hazel, hiyo ilimaanisha kufanya kile ambacho kwa kawaida angefanya Jumapili asubuhi—kumaliza somo lake la shule ya Jumapili; nenda kwenye jengo la kanisa; fundisha darasa

lake; kumwabudu na kumheshimu Mungu. Huenda alihisi unyogovu, na hakujua mustakabali, lakini angeweza kuchukua hatua inayofuata.

Kwa miezi iliyosonga hadi mwaka mmoja, Earl na Hazel bado hawakujua ni nini kilikuwa kimempata Gary. Lakini waliendelea kumtegemea Mungu na "kuchukua hatua inayofuata." Kituo cha TV cha ndani kilipendezwa na hali ya Earl na Hazel na kumteua mtangazaji Janine Tartaglia kuangazia hadithi hiyo. Janine alifikiri kwamba, ili kuripoti hadithi hiyo kikamilifu, alipaswa kuhudhuria kanisa lao ili kuona jinsi walivyostahimili shinikizo katika mazingira ya umma. Aliposikia Dk. Lee akihubiri, alihisi Mungu akizungumza na moyo wake. Janine Tartaglia alimkubali Yesu kama Mwokozi na Bwana wake.

Siku mia nne na arobaini na nne baada ya dhoruba ya Ubalozi, wakati Rais Ronald Reagan alipoingia madarakani, wafanyakazi wote wa kidiplomasia wa Marekani waliokuwa wametekwa nyara waliachiliwa. Baada ya siku chache, Gary alikuwa nyumbani. Earl na Hazel walifurahi na kumshukuru Mungu.

Si kila siku katika uhusiano wetu na Mungu itakuwa ya kuvutia. Lakini kama Oswald Chambers alivyoandika, "Lazima tuishi siku tatanishi kulingana na kile tulichoona mlimani."[133]

Kwa njia hiyo, siku za giza ambazo ziliwakutanisha Janine Tartaglia na Lees zimezalisha matunda zaidi. Kijana huyo mwongofu alikua, na leo Janine Tartaglia Metcalfe ni mhubiri mwenye nguvu, mwalimu, na mhudumu wa injili—yote kwa sababu mtu fulani alichukua "hatua inayofuata."

**SEPTEMBA 14** **257**

# Kwenye Uongo Weka Kutia Moyo

*Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia.*
*Waefeso 4:29*

*Maneno!* Je, ni muhimu kiasi gani? Je, tunayaapa nguvu kiasi gani? Ulimwengu wako unakuambia nini? Je, ni maneno ya hasira, ya hukumu kuhusu wewe kutopima? Je, unawaamini? Je, yanakuzuia usiwe vile ambavyo

133. Oswald Chambers, *My Utmost for His Highest* (Toronto: McClelland and Steward Limited, 1935), 107.

Mungu alikusudia uwe? Je, yanakuzuia yakikuweka katika udongo usio na rutuba ya kukua?

Ni wakati gani unaposema "hapana" na kurudisha nguvu zako? Je, unawafundishaje watu kwamba unataka kutendewa kwa kuthaminiwa na kuheshimiwa?

Kwa upande mwingine, labda ulimwengu wako umejaa uthibitisho mzuri. Labda mtu anakutia moyo kwa subira na kukufundisha jinsi ya kucheza mchezo wa maisha hadi upate kukimbia nyumbani. Labda umegubikwa na upendo usio na masharti na neema ya Baba yetu aliye juu, ambapo ni sawa kujaribu mambo mapya, na ni sawa kufanya makosa. Ikiwa ndivyo, umebarikiwa, na mtu huko nje anahitaji kusikia maneno hayo ya uzima.

Wakati mmoja, siku ya kuzaliwa ya binti yetu, badala ya maua, tulimpa wosia wa maneno na maandishi ambao uliujaza moyo wake kwa siku nyingi. Unazungumza maneno gani katika ulimwengu wako?

Nancy Shaver[134]

**SEPTEMBA 15** **258**

# Alijali Kupanda

*Na tazama, palikuwa na mtu, jina lake Zakayo, mkubwa mmoja katika watoza ushuru, naye ni tajiri. Huyu alikuwa akitafuta kumwona Yesu ni mtu wa namna gani, asiweze kwa sababu ya umati wa watu, maana ni mfupi wa kimo. Akatangulia mbio, akapanda juu ya mkuyu apate kumwona, kwa kuwa atakuja kuipitia njia ile.*
*Luka 19:2-4*

Alikuwa mtoza ushuru mkubwa, kwa hiyo watu wengi hawakumpenda. Pengine alifanya kazi kwa serikali ya Kirumi, na katika Israeli, hilo halikuwa maarufu. Zaidi ya kodi iliyotakiwa ya Waroma, watoza ushuru wangejipatia ada nyingi zaidi wawezavyo. Kwa sababu hii, *hawakuwa* maarufu. Pia walichukuliwa kama wenye dhambi (Luka 19:7).

134. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* Septemba–Oktoba–Novemba 2001 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 81. Imetumika kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa Reflecting God.)

Huna budi kumpa Zakayo sifa. Licha ya jinsi wengine walivyohisi kumhusu, hakuruhusu uharibifu wowote kwa taswira yake umzuie kutafuta mtu muhimu zaidi ulimwenguni. "Alitaka kuona Yesu ni nani"—alikuwa na udadisi mzuri na unaofaa. Zaidi ya hayo, alichukua hatua - alikimbia mbele na, kwa kuwa alikuwa mfupi, alipanda mti.

Inaonekana kwamba Yesu aliona jambo la pekee kutoka kwa Zakayo—moyo wenye kukubali—na akamchagua kutoka kwa umati. Yesu alijialika nyumbani kwa Zakayo kwa chakula cha jioni. "Zaki"—wacha nimwite jina la utani—alikuwa mwerevu vya kutosha kuchukua fursa ya kumkaribia Yesu. Bila shaka, watu wengine walipomwona akikaribia zaidi kwa Mwokozi, walianza kunung'unika na kukosoa.

Zakayo lazima alikuwa ametubu kutoka moyoni—kumaanisha alijuta kwa ajili ya dhambi zake, na akajuta vya kutosha kuziacha. Alitangaza kwamba angetoa nusu ya mali yake kwa maskini na kumlipa mtu yeyote ambaye alikuwa amemlaghai mara nne zaidi (19:8)—hii inaitwa kurejesha. Mungu anaweza kukusamehe dhambi zako zote, lakini bila shaka, baadhi ya dhambi hizo zinahusisha kuwakosea wengine. Unafaa kurejea kwa wale uliowaumiza na kurekebisha mambo. Unapofanya hivyo, wapokeaji wa urejesho wako watajua kuwa kweli umepata haki na Mungu.

Yesu alipokutana na Zakayo alikuwa akipitia Yeriko akielekea Yerusalemu kufa msalabani kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Katika usemi mdogo wa kile ambacho angetoa hivi karibuni kwa ulimwengu wote, Yesu alisema, "Wokovu umefika katika nyumba hii" (19:9). Kwa sababu ya mwitikio wake kwa Yesu, Zakayo na familia yake yote walibarikiwa. Kwa kumjibu Yesu jinsi alivyomjibu, Zakayo akawa mwana wa Ibrahimu katika kuzingatia maana bora zaidi ya neno hilo.

Kisha, Yesu anaeleza utume wake mkubwa zaidi: "Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa waliopotea" (19:10). Msomi wa Agano Jipya na mtafsiri wa Bibilia Dk. Ralph Earle alisema kwamba huu ulikuwa mstari mkuu wa Injili ya Luka. Inapendeza tukiitikia wito huu; inapendeza sana tukiungana na Yesu anapoleta waliopotea kwake.

Mama yangu mwenyewe alimkubali Kristo kama Mwokozi na Bwana wake alipokuwa na umri wa miaka arobaini na tisa. Alifanya tofauti iliyoje ndani yake! Miongoni mwa changamoto nyingi katika maisha yake ni ile ya tangu utotoni mwake.

Mama yangu alilelewa katika umaskini kaskazini mwa New York. Alipokuwa katika darasa la sita, darasa lake lilisafiri kwenda jiji la New York. Alimwendea mwalimu wake na kuomba mkopo wa dola tano za kumsaidia kulipia safari hiyo. Mnamo mwaka 1919, hizo zilikuwa pesa nyingi. Sasa, akiwa

Mkristo mpya, mama yangu alitambua kwamba hakuwahi kurejesha mkopo huo. Alisafiri mara kwa mara hadi kaskazini mwa New York ili kutembelea familia, kwa hiyo katika mojawapo ya safari hizo, alienda kumwona mwalimu wake wa zamani na kulipa mkopo huo wa dola tano—miaka arobaini na sita baadaye. Hii ilikuwa urejeshaji, na watu waliamini kwamba Vera Shaver alikuwa na kitu halisi.

Hebu hadithi ya Zakayo na Yesu iwe kielelezo kwako:

- Bila kujali nafasi yako maishani, usiruhusu mtu yeyote au kitu chochote kikuzuie kumtafuta Yesu.
- Fuata udadisi wako wa kiroho kwa vitendo; fanya kile kinachohitajika ili kuungana na Yesu.
- Jua kwamba Yesu anaona kitu cha pekee ndani yako. Jibu hatua inayofuata anayokualika kuchukua.
- Geuka kabisa kutoka kwa dhambi zako na urekebishe mambo na wale uliowadhulumu.
- Yesu anataka kutafuta na kuokoa—mwamini yeye atakuokoa. Waambie wengine jinsi wanavyoweza kumjua Kristo ambaye umemjua.

Asante, Zakayo, kwa kujali kupanda. Kutambua ni kiasi gani Yesu anatutafuta kulifanya kule kupanda juu kudhihirisha thamani yake.

**SEPTEMBA 16** **259**

# Mtumishi kwa Neema ya Mungu

*Injili hiyo ambayo nilifanywa mhudumu wake, kwa kadiri ya kipawa cha neema ya Mungu niliyopewa kwa kadiri ya utendaji wa uweza wake.*
*Waefeso 3:7*

Sauli alikuwa na kazi ya kufanya Pamoja na Mungu ambaye hakuwa amewahi kukutana naye. Safari yake ya kuwaangamiza Wakristo hao wasio na hatia ilikomeshwa ghafla na nuru yenye upofu iliyomkabili, ikamfanya awe hatarini, na kumbadilisha milele. Sasa alikuwa mmoja wao, na Mungu kwa fadhili alimtuma Anania awe mtumishi wake wa uponyaji.

Paulo, kama alivyokuwa anajulikana sasa, alikuwa na msukumo mkubwa wa ndani na shauku ya kufidia maisha yake ya zamani na wakati uliopotea. Alikuwa amechaguliwa kufunua siri kuu ya upendo wa Mungu kwa kila mtu. Alikuwa mtenda dhambi aliyefanikiwa, na sasa alikuwa mtakatifu

aliyefanikiwa. Aliunda ruwaza ya kutumikia ambao hauwezekani bila nguvu za kiroho kuusukuma.

Je, tumeunganishwa na nguvu hizo ili tuweze kutumika pale tulipowekwa? Je, tunastaajabishwa na kunyenyekea Mungu anapotumia watu wa kawaida kama sisi kujenga madaraja ya upendo ili neema iweze kuvuka? Na iwe hivyo.

Nancy Shaver[135]

SEPTEMBER 17 260

# A Man Called Peter

*Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji. Vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu.*
*Zaburi 42:1*

*A Man Called Peter* ni jina la kitabu (na, baadaye, sinema inayotokana na kitabu hiki) iliyoandikwa na Catherine Marshall kuelezea hadithi ya mume wake mhubiri maarufu, Peter Marshall. Mhamiaji Mskochi aliyehamia Marekani, Peter alihudhuria seminari na hatimaye akawa mchungaji wa Kanisa la kihistoria la New York Avenue Presbyterian huko Washington, DC. Kisha akateuliwa kuwa kasisi wa Seneti ya Marekani. Alikufa mapema akiwa na umri wa miaka arobaini na sita.

Peter alishuhudia kuhisi "mguso begani." Alifafanua hivi: "Mguso begani ni uweza mkuu wa Mungu unaotenda kazi bila msaada au kizuizi juu ya mteule aliyeanguka dhambini ili kuzalisha kiumbe kipya, na kumwongoza katika kazi fulani ambayo Mungu ameweka kwa ajili yake yeye."[136]

Kulikuwa na mtu tofauti aitwaye Peter katika maisha yangu. Alikuwa miaka michache mbele yangu katika shule yetu ya upili huko Manchester, Alikuwa rais wa bodi ya wanafunzi; mwanafunzi wa kupata A; na, ingawa alikuwa mlemavu tangu utotoni, alicheza kama golikipa wa shule kwenye timu ya soka. Vilevile, huko Dartmouth, alikuwa rais wa udugu wake, alicheza soka ya shule, na alikuwa sehemu ya Green Key, shirika la juu zaidi

135. Awali kilichapishwa katika in *Come Ye Apart* September–October–November 1998 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 92. Imetumika kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa Reflecting God.)

136. Dr. Peter Marshall, *Mr. Jones, Meet the Master: Sermons and Prayers of Peter Marshall* (Westwood, NJ: Fleming H. Revell Company, 1950), 31.

la heshima katika shule hiyo. Hatimaye, Peter alipata tatizo la kunywa sana pombe hadi kwamba akaacha chuo.

Nilisomea Dartmouth pia, na huko, nilianza kuhisi njaa ya Mungu. Sikujua jinsi ya kumpata, na hakuna aliyeonekana kuwa na uwezo wa kuniambia—hivyo nilienda kwenye kanisa. La kushangaza Peter alionekana kwenye kanisa pia. Alikuwa amerudishwa chuoni baada ya kutokuwepo kwa zaidi ya mwaka mmoja. Tulipoonana, aliniambia, "Chic, mimi ni mtu tofauti na nilivyokuwa zamani kwa sababu nilimpata Bwana." Alikuwa mtu wa kwanza niliyekutana naye ambaye alizungumza kama Mungu alikuwa halisi.

Wiki chache baadaye, Peter alikuja kwenye bweni langu na akaniambia hadithi kuu zaidi kabla na baada ya hadithi ambayo nimewahi kusikia. Hapo awali, alikuwa amelala nyuma ya gari lake na alikuwa na shida na polisi katika majimbo sita tofauti. Lakini alikutana na Mungu kibinafsi kupitia Yesu alisamehewa dhambi zake zote; aliokolewa mara moja kutoka kwa pombe; na kupata furaha kubwa na amani. Peter alinialika kwa kanisa la karibu, ambapo Kristo alifanyika halisi kwangu na kunipa maisha mapya. Nilipokua kiroho, Peter alinifundisha jinsi ya kuomba na kusoma Biblia, na kunisaidia katika mapambano yangu.

Sote wawili hatimaye tuliishia Kansas City kwenye seminari. Nilipofika Kansas City, mtu pekee niliyemjua alikuwa Peter, ambaye alikuwa amekuwa msimamizi wa Misheni ya Uokoaji ya Jiji la Kansas. Alinipa mahali pa kulala, na mara nyingi tulienenda pamoja, tukihubiri pamoja. Andiko alilopenda sana Peter lilikuwa Zaburi 42:1—na kwa kweli, ameiga mfano huo wa kumtamani Mungu. Mimi na Nancy tulipooana, alitia sahihi cheti cha ndoa yetu ili kutoa ushahidi—na kuongeza Wafilipi 4:19.

Peter alioa mwanamke mzuri anayeitwa Mary, na walikuwa na watoto wanne ambao mara nyingi sana alinisimulia juu yao kwa upendo. Peter alipitia wakati wa mapambano ya kiroho, lakini tuliendelea kuwasiliana. Alirudi akiwa na nguvu kwa ajili ya Bwana na kufundisha shule ya Jumapili, akawafunza wachungaji wa baadaye, na alikuwa na ushawishi mkubwa katika kanisa lake la mtaa. Anang'aa na uwepo wa Mungu na kuendeleza kwa uthabiti kazi ya utakaso ya Roho Mtakatifu. Katika miaka ya mwisho ya Mary, alimtunza kwa upendo mkubwa.

Wakati wa janga la COVID-19, Peter alipata virusi, ambavyo vilisababisha nimonia. Alikuwa kwenye oksijeni na hospitalini kwa wiki saba. Hatimaye, Jumapili moja, alipiga simu na kuripoti kwamba alikuwa ametolewa hospitalini—ilikuwa mojawapo ya siku zenye furaha zaidi maishani mwangu. Ingawa bado alikuwa mdhaifu, aliuliza jinsi gani angeweza kuniombea.

Peter ni mmoja wa watu wanaomcha Mungu sana ninaowajua, na mimi ni Mkristo leo kwa sababu ya ushuhuda wake. Hii ndiyo sababu ninazungumza kuhusu "mtu aitwaye Peter."

**SEPTEMBA 18** **261**

# Malaika Wawili

*Hamjui ya kuwa mtawahukumu malaika,*
*basi si zaidi sana mambo ya maisha haya?*
*1 Wakorintho 6:3*

*Je! Hao wote si roho watumikao, wakitumwa*
*kuwahudumia wale watakaourithi wokovu?*
*Waraka kwa Waebrania 1:14*

Waebrania 1:14 inawaelezea malaika kama "roho watumikao wakitumwa kuwahudumia wale watakaourithi wokovu."

Ninaamini kwamba hawa ni malaika "fulani" ambao siku moja tutawahukumu: "Je, hamjui kwamba tutawahukumu malaika?" (1 Wakorintho 6:3).

Wakati fulani, wakati Misheni ya Uokoaji ya Jiji la Kansas ilipokuwa na takriban watu tisini kwa kila ibada ya usiku, kikundi cha kanisa kilichopangwa kilishindwa kujitokeza kuendesha ibada. Hiyo ilimaanisha kwamba mmoja wetu tulioishi Misheni alihitajika kuhubiri. Kwa hivyo nilichukua kitabu changu cha nyimbo na Biblia na kwenda mbele.

Kutaniko lilikuwa wanaume, na mwanamume mmoja aliendelea kuvuruga uimbaji. Nilipuuza hili. Lakini kabla ya kusoma maandiko kwa ajili ya mahubiri, aliendelea na usumbufu wake. Nilimwomba "tulia tafadhali na kuliheshimu Neno la Bwana." Bado, aliendelea. Baada ya jitihada tatu zaidi za kumtuliza mtu huyo, nilishuka na kumwambia aondoke kwenye mkutano.

Alikuwa mtu mkubwa. Nilimsaidia kusimama na kumpeleka mlangoni. Nikiwa pembeni, alishika viganja vyangu vyote viwili na kuvizungusha. Maumivu yalipita kwenye mkono wangu, na magoti yangu yakagongana. Muda huohuo, gari la kijani la kubeba abiria wawili lilisimama kwenye ukingo karibu nasi.

Majitu mawili yalijaza gari. Yalivalia kofia kubwa za cowboy, na bunduki yenye uwezo mkubwa ilisimama wima kati yao. Wote wawili walitazama mbele, hawakututazama sisi wawili tuliokuwa kando ya barabara.

Bila kuonekana kwa harakati za kutoka kwa wanaume kwenye gari, dirisha la upande wa abiria lilishuka kidogo. Mwanamume aliyeketi kwenye kiti cha abiria, akiwa bado anatazama mbele, alifungua kinywa chake na kusema maneno matatu: “Mwache aende zake.”

Mwanaume huyo mara moja aliniacha na kuondoka. Nilirudi ndani ya Misheni na kukamilisha ibada. Sikuwahi kuliona gari lile la kijani likiwa na wale watu wawili wakubwa waliovalia kofia za cowboy tena. Lakini kwa miaka mingi, aghalabu nimefikiria kuwahusu na kuhitimisha kuwa walikuwa malaika.

Mwaka mmoja baadaye, yule mtu aliyevikunja viganja vyangu alirudi na kuniomba nimpeleke nyumbani kwa dada yake, nami nilifanya hivyo. Nilimshusha huku nikitabasamu, kushikana mikono na sala. Natumaini kumuona mbinguni. Sote tunakumbuka kipindi hiki na jinsi kilivyotufanya tuhisi. Je, inawezekana kwamba malaika mmoja alikuwa anamwangalia na malaika mwingine alikuwa akiniangalia mimi? Kila mmoja wetu ana sifa za kustahili kuhukumu jinsi malaika hawa walivyojiendesha.

Peter Gunas
(Huyu ndiye mtu aliyeleta Chic Shaver kwa Kristo)

**SEPTEMBA 19** **262**

# Je, Unapanda Mbegu Gani?

*Mimi nilipanda, Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu. Hivyo, apandaye si kitu, wala atiaye maji, bali Mungu akuzaye. Basi yeye apandaye, na yeye atiaye maji ni wamoja, lakini kila mtu atapata thawabu yake mwenyewe kulingana na taabu yake mwenyewe. Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu.*
*1 Wakorintho 3:6-9*

*Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika*

*Roho atavuna uzima wa milele. Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.*
*Wagalatia 6:7-9*

Lafudhi zake za Kiingereza na Welsh zilituvutia mimi na Nancy. Tulifurahi kwamba familia ya wamishenari ya Heap ilikuwa imeamua kukodisha nyumba ya wamishenari ng'ambo ya eneo takatifu la kanisa la kwanza tulilochunga. Samuel na Gladys Heap walikuwa na watoto watatu: Christiana, mwenye umri wa miaka kumi na sita; Steven, mwenye umri wa miaka kumi na tatu; na Philip, mwenye umri wa miaka minane.

Tulishangazwa na jinsi familia hii inavyofanya kazi. Tulijua wazazi walikuwa wamepanda mbegu za utauwa, utakatifu, na upendo kwa watoto wao. Wazazi waliwaacha watoto kwa wiki kadhaa wakati fulani ili wasafiri kwenda Marekani kuripoti kile kilichokuwa kikitendeka kwenye uwanja wa misheni katika huduma za uwakilishi. Christiana aliongoza nyumba, akapika chakula, akalipa bili, akawapeleka wale wavulana shuleni, na kusoma shuleni kwa njia ya barua. Watoto hawakukosa kamwe shule ya Jumapili au ibada ya kanisa, na Christiana alilipa zaka. Wazazi walituambia watoto wangeweza kufanya kazi kwa njia hii kwa sababu walikuwa wamejifunza imani na kutegemewa katika misheni.

Miaka ilipita, na Samuel na Gladys wote wakachukuliwa kwenda mbinguni. Christiana akawa mke wa mchungaji, na walikuwa na huduma nzuri makanisani. Steven na mke wake, Brenda, wakawa wamishenari huko Brazili na kukaa huko baada ya kustaafu. Philip ni mchungaji katika eneo la Washington, DC, ana kutaniko lake la kimataifa, na mara kwa mara huhudumu kwa makutaniko mengine ya Kihispania katika eneo hilo. Ni mavuno makubwa sana ambayo Samuel na Gladys wamevuna katika maisha ya watoto wao.

Kasisi na Bi. Heap waliendesha huduma yao ya umishenari huko Kolombia na Peru. Kuanzia mwaka 1940 hadi mwaka 1954, miaka yao ya Colombia ilishuhudia kifo cha mwana wao wa kwanza; kupigwa kwao na kundi la watu; na matatizo ya kimwili na kifedha. Walipohamia mgawo wao wa Peru, waliacha jumuiya ndogo huko Kolombia. Songa mbele kwa haraka kwenye mstari wa McDonald's huko Indianapolis, ambapo mtoto wao Steven alikuwa akingoja kuagiza:

> Wenzi wa ndoa waliokuwa mbele yangu walikuwa wakizungumza Kihispania na kujaribu kuamua watakachoagiza. Waliona jina langu na kuniuliza kama namfahamu Don Samuel e Doña Gladys Heap. Nilipojibu kwamba walikuwa wazazi wangu, nilikumbatiwa sana kiasi

kwamba ningeelekea waliko wazazi wangu. Waliendelea kuniambia kwamba babu na nyanya wa mwanamke huyo walikuwa wamekuja kumwamini Kristo kwa sababu ya ushuhuda mwaminifu wa wazazi wangu. Niliwauliza walikuwa wakifanya nini huko Kolombia. Jibu lao halikupaswa kunishangaza, kwa kutegemea ahadi za Neno la Mungu—mmoja anapanda, mwingine anamwagilia, na Bwana anatoa ongezeko—lakini nilishangaa waliponiambia kwamba walikuwa wachungaji wa kanisa moja huko Cali, Kolombia.

Haya yalikuwa matunda zaidi kutoka katika mbegu iliyopandwa na Heaps kuanzia mwaka 1940 hadi 1954. Nataka kupanda mbegu nyingi kwa ajili ya kazi ya Yesu. Je, unakusudia kupanda mbegu gani katika maisha yako yote?

**SEPTEMBA 20** **263**

# Upendo wa Mume na Mke

*Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na dosari wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa.*
*Waefeso 5:25-27*

*Lakini kila mtu ampende mke wake kama nafsi yake mwenyewe; wala mke asikose kumstahi mumewe.*
*Waefeso 5:33*

*Mpende kama Kristo alivyolipenda kanisa na kujitoa kwa ajili yake*. Hiyo ina maana ya upendo wa kujitolea; upendo unaozaa utakatifu. Ninajitahidi sana kumtunza, kumsaidia, kumtia moyo, na kumtegemeza. Ninamtendea kwa njia ambayo haitamkasirisha, kumshushia hadhi, au kumdharau bali itamwezesha, kumkuza, kuzalisha moyo na maisha matakatifu, na kumfanya awe kama Kristo zaidi.

"Umfanye kuwa mtakatifu..." inasema, "ili amtakase na kumsafisha" The American Standard Version huifasiri, "itakase, ukiisha kuisafisha."

Paulo anatumia uhusiano wa mume na mke kama mlinganisho wa upendo wa Kristo kwa kanisa na dhabihu yake ili kumtakasa na kumfanya mtakatifu. Anatumia upendo na dhabihu ya Kristo kwa kanisa kuwafundisha waume na wake jinsi ya kupendana.

Katika kiapo changu cha harusi na Nancy, niliahidi "kumpenda, kumfariji, kumheshimu, na kumtunza, katika ugonjwa na afya; na kuwaacha wengine wote, nijilinde naye peke yangu, maadamu sisi sote tunaishi." Niliahidi kuwa ningekuwa naye na kumshikilia "kwa mema—kwa mabaya, kwa utajiri—kwa umaskini, katika ugonjwa na afya, kumpenda na kumthamini hadi kifo kitakapotutenganisha."

Afya ya sasa ya Nancy inaathiriwa na Alzheime's. Kwa namna fulani, katikati ya utunzaji wote wa ziada, Bwana anatuwezesha kuwa na upendo mzuri kwa kila mmoja wetu. Nancy ananiachia maandishi mengi kando ya kiti ambapo mimi husomea Biblia yangu kila asubuhi. Hapa kuna barua niliyopata mnamo Machi 15, 2020:

> *Asante kwa safari yetu nzuri kwenda kw Paul na uamsho—Mungu alibariki kweli, na watu wengi walimkaribia Mungu zaidi.*
>
> *Wewe ni wa ajabu—kufanya kazi zote unazofanya na kunitunza pia!*
>
> *Nimefurahia sana na bado ninakupenda—jamaa wangu wa kupendeza!!*
>
> *XXOO*
>
> *Nakupenda siku zote,*
>
> *Nan*

Kwa sababu Mungu anakusaidia, unaweza kumpenda mwenzi wako katika ndoa yako yote—si kwa urahisi tu, bali kwa nguvu.

**SEPTEMBA 21** **264**

# Dhabihu Yako Iliyo Hai

*Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu,*
*itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu,*
*ndiyo ibada yenu yenye maana.*
*Warumi 12:1*

Dottie alimtazama kazini. Henry alikuwa mkuu wa shule ya umma, na aliona kwamba alikuwa mzuri kwa maswali ya uhasama katika mikutano ya hadhara na wazazi na raia. Dottie alifurahi sana hivi kwamba alitoa maisha yake kwa yule yule Kristo Henry aliyewahi kumtumikia. Hapa palikuwa na mtu kazini kama dhabihu iliyo hai.

Sio dhabihu iliyokufa, kama katika Agano la Kale - lakini dhabihu iliyo hai. Paulo anahimiza kwamba kwa kuwa Mungu ametupa rehema kwa uhuru

na ukamilifu, jambo dogo tuwezalo kufanya ni kutoa miili yetu kwa Mungu kama dhabihu. Ni wito kwa ndugu na dada Wakristo.

Je, umewahi kuhisi kwamba Mungu amekuita ili kumrudishia kitu fulani? Mungu wetu hastahili tu "mambo fulani"—anastahili vyote. Sio tu mikono au miguu au sauti au nguvu au moyo au akili... mpe mwili wako wote. Ni dhabihura moja kwa yote, wakati wa maamuzi.

Dhabihu iliyo hai hutokeza katika hatua yenye nguvu, inayoendelea ambapo sisi sote ni wake—bado tuko hai, wachangamfu, na daima tunafanya maamuzi na kuishi maisha ili kumpendeza Mungu.

Ilikuwa usiku wa Juni huko North Carolina wakati Linda alipoyasalimisha maisha yake yote ya Kikristo kwa Mungu. Alikubali kujisalimisha kwake na kuukabidhi utimilifu wake wa utakaso kwa moyo wake uliojitolea. Mume wake alishangaa na kusema, "Una furaha sana."

Linda alihudhuria ibada zote za kanisa wiki hiyo maalum. Alisema, "Nimekuwa nikiomba zaidi tangu Alhamisi usiku kuliko nilivyofanya katika miaka minne iliyopita. Na unamjua huyo mpuuzi kazini? Naam, nimeacha kumlalamikia." Hata alinihakikishia kwamba angeshughulikia fedha zake siku zijazo kwa uaminifu mbele za Bwana. Alikuwa akifurahia na kukubali "mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na makamilifu" (12:2) kama dhabihu yake iliyo hai.

**SEPTEMBA 22** **265**

# Usiiruhusu Dunia Ikubane

*Wala msifuate kanuni za dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*
*Warumi 12:2*

Nilikuwa nachukua kipimo cha MRI. Kabla ya kuniingiza ndani ya mashine, mtalaam alisema, "Je, una hofu ya kufoka?"

Nikasema, "Hapana."

Lakini baada ya kumalizika, nilitambua kwamba nilipaswa kusema ndiyo. Tao la juu la bomba lilikuwa karibu kugusa pua yangu - nilihisi kubanwa sana.

Bila shaka, katika Warumi, Paulo alipowaonya Wakristo kwamba ulimwengu ungezibana akili zao, alimaanisha jambo lisiloweza kungundulika

kwa urahisi. Ulimwengu (nguvu zinazoishi bila Mungu) haziwezi kusimama kwa ajili ya wewe kuishi kwa ajili ya Mungu—tofauti yako inawatia mashakani. Ulimwengu unataka kuthibitisha akili yako. Lakini Mungu anataka kuyabadilisha mawazo yako.

Katika karamu ya kanisa, daktari Denny Kinlaw, mtoto wa waziri Dk. Dennis Kinlaw, alishuhudia nguvu za ulimwengu kubana:

> Nilipokuwa na umri wa miaka saba, mama yangu aliomba pamoja nami ili kumpokea Kristo. Nina kumbukumbu za thamani sana baada ya hapo, za Yesu kujidhihirisha kwangu. Lakini nilipoanza kukaribia pengo lile kubwa la hali duni ambalo tunaliita ujana—wakati tufaha la Adamu lilikuwa kubwa sana na misuli yangu kuwa mikubwa—nilianza kuwa na ufahamu wangu mwenyewe zaidi kuliko yeye...
>
> Hatimaye, niliingia chuo kikuu. Niliamua, *Ah, sasa niko na watu wenye fikra nzuri na huru*. Nilishtuka kukuta hazikuwa nzuri wala wala huru... Walitaka kuniwekea maoni ya ukweli ambayo hayapatani na yale niliyojifunza katika familia yangu wala yale niliyojifunza kivyangu.
>
> Nilianza tena kufungua maisha yangu kwa Mungu, naye akarudi kituoni. Niliamua kwamba nilitaka maisha yangu yawe yake kabisa.
>
> Kisha nilianza mafunzo yangu ya hospitali na makazi. Niliona ningeweza kufanya kazi kwa saa thelathini na sita bila kupumzika, bila kulala, jinsi watu wengine wangeweza. Lakini sikuwa na wakati wa Mungu. Pia niligundua kwamba nilipokosa kuzungumza na Mungu, hakuzungumza nami. Alihamia ukingo wa maisha yangu tena.
>
> Aliposogea pembeni, nafasi iliyobaki haikuwa tupu. Mahali alipokuwa akikaa kukajaa hamu na matamanio. Taratibu nikagundua wapo na wananidhibiti. Nilianza kujionea huruma. Niliwatazama hawa madaktari wengine wakiwa na ndege zao za kibinafsi na nyumba za majira ya kiangazi na zile za majira ya baridi kali na mahali penye ufuo na magari makubwa na maisha ya anasa, nikawaza, *Acha nitoke nje kwenye kitongoji, nami nitajitengenezea pesa na nafasi ya kufurahia baadhi ya mambo hayo.* Niligundua kwamba, bila muujiza, nilikuwa tayari nimepangwa kwa msiba.[137]

Kuwa na hekima sana. Usiuruhusu ulimwengu ukumiize!

137. Dennis Kinlaw, *Preaching in the Spirit* (Grand Rapids: Francis Asbury Press, 1985), 56–57.

# Kubadilishwa kwa Kufanywa Upya Nia Yako

*Wala msifuate kanuni za dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*
*Warumi 12:2*

Chukulia malighafi ya akili yako, kile unachoweka ndani yake huamua bidhaa itakayokamilishwa. Ingawa kutoa mwili wako kwa Mungu kama dhabihu iliyo hai lilikuwa tukio katika wakati fulani, kufanywa upya kwa akili yako ni mchakato unaoendelea. Utachagua mawazo ya kiakili ambayo yanadumaa, kupotosha, kuchafua, kushusha hadhi—*au* ambayo hujenga, kukua, kupanuka, kufanya upya. Unaamua!

Mojawapo ya maamuzi bora niliyowahi kufanya ni kuanza kila siku kwa Biblia na sala. Tunaweza kuwezesha mabadiliko chanya kwa ibada, ushirika wa Kikristo, kusoma nyenzo za kiroho, na kushiriki imani yetu. Wafilipi 4:8 inatuambia tuzingatie yaliyo ya kweli, ya kiungwana, ya haki, safi, ya kupendeza, yenye kupendeza, bora, na yenye kusifiwa. Changanua maisha yangu, Bwana, na unitahadharishe kuhusu mabadiliko yoyote katika halijoto yangu ya kiroho.

Daktari Denny Kinlaw anaelezea kufanywa kwake upya:

> Majuma sita baadaye, mkono wa yule daktari wa upasuaji mwingine uliteleza, nami nikapewa wakati mwingi kwa ajili ya Mungu. Watatu kati yetu tulikuwa tukimfanyia upasuaji msichana ambaye alikuwa mraibu wa dawa za kulevya. Wakati daktari mwingine wa upasuaji... chombo kilipenyeza glavu yangu na kukata kwenye nyama ya mkono wangu... Niliambukizwa aina mbaya zaidi ya hepatitis.
>
> Miezi hiyo iliyofuata ilikuwa wakati wa maumivu makubwa na huzuni... Bwana alirudi katikati ya maisha yangu. Na aliporudi, aliniweka huru...
>
> Nilimwomba aniponye, naye akaniponya, lakini si kwa jinsi nilivyotarajia. Nilifikiri angeniponya kwa namna ambayo ningekuwa na uhakika kuhusu kesho... Lakini hilo halikutokea... Alisema, “Sikumpa mtume Paulo dhamana ya kesho; kwa nini nikupe wewe?”

... Uzoefu huo ulibadilisha njia yangu ya kuishi. Sichukulii kila siku kwa ukawaida tena. Simchukulii mke wangu, watoto wangu, au kazi yangu kwa ukawaida tena. Namchukulia kila mmoja wao kama zawadi maalum kutoka kwake, zawadi ya neema yake. Kuna baadhi ya asubuhi ninapoendesha gari kwenda kazini kule Lexington ambapo mimi hutazama jua likichomoza na kujipata nikiwa na shukrani kwa siku mpya... Unajua, si njia mbaya ya kuishi. [138]

Matunda mengi ya upya huo ni haya: "mtaweza kupima na kuthibitisha mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu" (Warumi 12: 2).

**SEPTEMBA 24** **267**

# Tendo la Msamaria Mwema

*Lakini, Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipokuwa; na alipomwona alimhurumia.*
*Luka 10:33*

Msamaria alichukua sehemu ya maisha yake na kuitoa ili kuokoa mwingine. Ingawa wengi wetu hatutaenda msalabani na kutoa maisha yetu yote ili kuokoa mwingine, wengi wetu tutatoa "kiasi" cha maisha yetu.

Msamaria alimpa mtu aliyejeruhiwa yafuatayo (Luka 10:34–35):

- Huduma ya matibabu: "alifunga vidonda vyake"
- Utoaji wa usafiri: "alimweka mtu huyo juu ya punda wake mwenyewe"
- Kuandaa mahali pa kulala: "kumleta kwenye nyumba ya wageni"
- Kutoa fedha: "alichukua dinari mbili"
- Kufuatilia hali: "Nitakulipia"

Kumbuka kwamba Msamaria huyo alimwacha mtu aliyejeruhiwa kwa mtunza nyumba ya wageni kwa muda alipokuwa akishughulikia shughuli zake binafsi. (Kwa wengi wetu, hii inafanya iwe halisi zaidi kwetu kufuata mfano wa Msamaria Mwema.) Kisha, anarudi kwa ajili ya rehema na huduma zaidi. Msamaria huyu anajulikana daima kwa kanuni ya "mpende jirani yako kama nafsi yako" ambayo Yesu alifundisha.

Ingawa haijawasilishwa kama hadithi ya Kikristo ya moja kwa moja, mkulima alifanya tendo la Msamaria Mwema kwa kuacha kazi yake ili

---

138. Kinlaw, *Preaching in the Spirit*, 57–58.

kuokoa maisha. Jina lake lilikuwa Fleming, na alikuwa mkulima maskini wa Kiskochi. Siku moja, alipokuwa akijaribu kutafuta riziki kwa ajili ya familia yake, alisikia kilio cha kuomba msaada kutoka kwenye kilindi cha mchanga ulio karibu. Aliziacha zana zake na kukimbilia kwenye dharura.

Huko, akiwa amezama hadi kiunoni kwenye tope jeusi, alikuwa mvulana mwenye hofu, akipiga kelele akijitahidi kujiweka huru. Mkulima Fleming alimwokoa kijana huyo kutokana na kile ambacho kingeweza kuwa kifo cha polepole na cha kutisha. Siku iliyofuata, gari la kifahari lilifika kwenye maskani finyu ya Mskochi. Mtukufu aliyevalia mavazi ya kifahari alitoka nje na kujitambulisha kuwa baba yake mvulana ambaye aliokolewa na Mkulima Fleming.

"Nataka kukulipa," mheshimiwa huyo alisema. "Uliokoa maisha ya mwanangu."

"Hapana, siwezi kukubali malipo kwa nilichofanya" mkulima wa Kiskochi alijibu, akipuuza ofa hiyo.

Wakati huo, mtoto wa mkulima mwenyewe alifika kwenye mlango wa geti la familia. "Huyo ni mwanao?" mheshimiwa aliuliza.

"Ndiyo," mkulima akajibu kwa kujivuna.

"Nitakufanyia mpango. Niruhusu nimchukue nimpe elimu nzuri. Ikiwa mvulana huyo ni kama baba yake, atakua na kuwa mwanamume unayeweza kujivunia."

Na kwamba alifanya. Baada ya muda, mwana wa Mkulima Fleming alihitimu kutoka Shule ya Matibabu ya Hospitali ya St. Mary's huko London na kujulikana ulimwenguni kote kuwa Sir Alexander Fleming, aliyegundua penicillin. Miaka mingi baadaye, mwana wa mheshimiwa huyo alipatwa na nimonia, na penicillin ikamwokoa.

Jina la mtukufu huyo lilikuwa Lord Randolph Churchill. Mwanawe alikuwa Sir Winston Churchill, ambaye alikuwa waziri mkuu wa Uingereza wakati wa Vita vya II vya Ulimwengu na, wengi wangesema, kiongozi wa ulimwengu huru katika vita dhidi ya Ujerumani ya Nazi.

Tazama pande zote! Ni Nani anayehitaji mguso wa Mungu kupitia kwako? Huwezi kujua ni nani unaweza kuwa unamwokoa!

# Maisha yako ni Mto

*Katika siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama, akapaza sauti yake akisema, Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema kuhusu Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa.*
*Yohana 7:37-39*

Maisha yako yanapaswa kuwa mto, mfereji. Kila mto lazima uwe na chemchemi ya kuujaza—iwe chemchemi yenye nguvu, kuyeyuka kwa theluji nyingi, au mvua. Kiroho, chemchemi yako ni kuja kwa Yesu Kristo na kushiriki. Ikiwa ni kama maisha ya kimwili, hii haimaanishi kushiriki mara moja tu—inamaanisha kushiriki mara kwa mara. Maji haya yanayotiririka kutoka ndani ni kazi ya Roho.

Tunapojazwa na Roho, hatupaswi kuingia katika mtego wa kudhania sisi ni hifadhi na chemchemi iko ndani yetu. Hapana, sisi ni mto. Unadumisha utimilifu kwa kushiriki mara kwa mara, kwa Yesu Kristo. Atakuweka kamilifu.

Myron Augsburger, kiongozi katika Kanisa la Mennonite, amesema kwamba huwezi kuweka ujalizo wa Roho isipokuwa kama wewe ni mtu wa sala. Ikiwa kizuizi chochote kinatokea kwenye mto wako—dhambi, kwa mfano—shughulikia kuondolewa kwake mara moja.

Kwa hivyo, endelea kuwasiliana mara kwa mara na chemchemi yako, Yesu Kristo. Maisha yako ni mto, sio hifadhi. Fukwe zako zinaweza kujaa. Na baraka ya ziada ni kwamba mwisho wa mito mingi kuna mavuno mengi.

# Toa Upendo na Utoe Injili

*Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wezi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi. 1 Wakorintho 6:9-10*

Tulia. Kumekuwepo na mijadala mingi ya hivi majuzi kuhusu hali ya kiroho ya watu wanaofuata mtindo wa maisha ya ushoga. Niruhusu nieleze uzoefu binafsi.

Binafsi nimeshughulikia mamia na mamia ya watu katika miaka yangu sitini na mitano ya maisha na huduma ya Kikristo. Nimekuwa rafiki wa karibu na mpendwa wa watu ambao walishiriki ukosefu wa maadili, uzinzi, au kufanya ngono na watu wa jinsia moja.

Mmoja wa marafiki hawa, mtaalamu katika sekta yake, alipanga miadi nami ya chakula cha mchana. Huku akitokwa na machozi mengi, alinieleza kwa zaidi ya saa moja kwamba alikuwa amefanya ngono na wanaume kadhaa. Kwa nini aliomba kuzungumza nami? Kwa sababu alijua ninampenda.

Nilikuwa nikihubiri kwa juma moja katika mojawapo ya majiji makubwa ya Marekani, na mchungaji alikuwa akinitambulisha kwa wafanyakazi wake. Alisema jambo kama hili alipozungumza kuhusu mchungaji na mke wake: "Jim alihusika katika tabia ya ushoga hapo awali. Lakini alimpata Yesu Kristo na akabadilishwa na kuokolewa. Leo yeye ni mhudumu aliyewekwa wakfu na kanisa. Madeline alikuwa kahaba awali. Amebadilishwa na Yesu Kristo. Wamefunga ndoa yenye furaha, na huyu ni Celeste, msichana wao mdogo mrembo."

Kwa simu isiyotarajiwa, Monica aliniambia hadithi yake, ambayo ilikuwa hivi: "Miaka kadhaa iliyopita, katika mkutano wa kambi, nilikusikia ukihubiri mahubiri yanayoitwa, Watu, Ngono, na Mungu. Msagaji mwenzangu alikuwa ameketi karibu nami. Mwishoni mwa ujumbe huo, alinigeukia na kusema, 'Nadhani nimenufaika na wewe kwa ubinafsi, na tunapaswa kuachana. Wakati fulani baadaye, nilikutana na mwanaume mzuri sana, na tukapendana. Tuna ndoa yenye furaha na tumesherehekea kumbukumbu ya miaka ishirini na sita. Nilidhani nikupigie simu ili nikupe ripoti hii."

Watu wote niliokuwa karibu nao na kuwapenda—wote ambao walipata au wanatafuta maisha mapya ya furaha katika Yesu Kristo.

Baada ya mtume Paulo kutaja baadhi ya dhambi za Wakorintho, anaongeza, "Na baadhi yenu ndivyo mlivyokuwa. Lakini mlioshwa, mlitakaswa [kutengwa], mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu" (1 Wakorintho 6:11). Walisamehewa, wakabadilishwa, na wakawa sehemu ya kanisa.

Si ajabu ninasema, "Toa upendo na utoe injili."

SEPTEMBA 27 **270**

# Kiwango cha Nguvu Kinachohitajika

*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.*
*Matendo 2:42*

*Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*
*Matendo 2:46-47*

Huenda alikuwa mtu aliyejulikana sana nchini Marekani, angalau kwa kuona—Francis Asbury, ambaye Wesley alimtuma kuhubiri injili huko Amerika.[139] Kuanzia 1771 hadi 1816, Asbury alisafiri kwa farasi na gari hadi miji na majiji akielezea juu ya Yesu. Pamoja na Washington, Jefferson, Adams, na Lincoln, alitambuliwa kama mmoja wa Waamerika sitini na sita ambao wanachukuliwa kuwa muhimu kwa maendeleo ya Amerika kama taifa. Kufikia 1813, mmoja kati ya kila Waamerika wanane alikuwa akihudhuria mikutano ya kambi ya Wamethodisti kila mwaka. [140]

Siri moja ya mikutano ya kambi ilikuwa wiki yao ya kuhubiri na kufundisha kwa umakini ambayo ilisababisha aina ya mafanikio ya kiroho ambayo hayakutokea kwa kawaida katika ibada moja. Hii ni sawa na uzito

139. Darius Salter, *America's Bishop: The Life of Francis Asbury* (Nappanee, IN: Francis Asbury Press, 2003), 294.

140. Salter, *America's Bishop*, 9.

unaoelezewa katika kifungu chetu cha Matendo—kukusanyika pamoja na mafanikio makubwa ya kiroho.

Dk. Richard Taylor alisema kuwa kuna kiwango cha nguvu kinachohitajika kwa kila ngazi ya mafanikio. Nguvu ya ndege isiyofanya kazi inatosha kusukuma gari la watoto, lakini haitoshi kutikisa ndege kubwa kutoka kwa hali yake ya hewa. Makanisa mengi huweka injini zao zikifanya kazi mwaka mzima na zina kiasi cha nguvu, lakini haitoshi kabisa kutimiza mambo ambayo yanahitaji sana kufanywa. Wakristo wengine watatakaswa pale tu watakapowekwa wazi kwa msukumo endelevu wa kiroho.

Vijana wengi huhudhuria kanisa lao la kawaida kila Jumapili, lakini wanapoondoka kwa wiki moja ya kambi ya vijana, hurudi wakiwa wamebadilishwa. Kufunga kwa kiroho, mkutano wa kambi, na uamsho hutimiza hitaji la ibada iliyokolea.

Katika uamsho wa Kimethodisti wa Florida niliokuwa sehemu yake, niliona matokeo ya mkusanyiko huu. Watu themanini na sita walihudhuria semina ya mashahidi wa Jumamosi. Ibada za kanisa Jumapili hadi Jumatano zilishuhudia jumla ya mahudhurio ya 1,221, na watu 112 walimtafuta Mungu madhabahuni. Hii hapa ripoti ya mchungaji:

> Mwaka huu wa 2006 utakuwa mwaka wetu wa uinjilisti wa kibinafsi. Dk. Shaver amehubiri mahubiri yenye nguvu, yaliyotolewa umaizi wa ajabu, akitufundisha "njia bora zaidi kuwahi kutokea" ya kuleta kwa uwazi maarifa ya kweli ya Yesu Kristo na uhakikisho wa wokovu. Tunahimiza kila mtu kuingia katika *Mafunzo ya Msingi ya Bibilia* ya Dk. Shaver ili kuhakikisha imani yako ya kibinafsi. Kwa sasa tunatengeneza mipango kupitia ushirika wetu mpya wa nyumbani ili kutumia mwongozo huu wa utafiti, pamoja na nyenzo nyingine ambazo Dk. Shaver ameshiriki nasi. Hakika hii ni siku ya mwanzo mpya. Labda uwazi wa uamsho huu utawatia moyo Wamethodisti wengine wengi kurudi kwenye mizizi yao ya Kiwesley. Katika uchunguzi mmoja, Dakt. Shaver alinukuu ujumbe wa John Wesley kwa wahudumu wake: "Hatuna kazi nyingine ila kuokoa nafsi." Je, umeokolewa? Je, unafahamu kwa uhakika? Ni furaha iliyoje kutambua kuwa unajua kwamba wewe ni mtoto wa Mungu. [141]

Tafuta matukio ambayo hutoa ukoleo wa kiroho unaoongoza kwa ushindi wako binafsi, ikiwa ni pamoja na utakaso wako wote.

141. Awali yalichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Machi 2006).

# Mpe Nafasi Ndogo

*Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu,*
*utu wema, fadhili, uaminifu, 23 upole, kiasi;*
*juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.*
*Wagalatia 5:22-23*

*Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu;*
*upendo hautakabari; haujivuni.*
*1 Wakorintho 13:4*

Kwa wakati! Ndio, ningefika kazini kwa wakati. Ilinibidi kuendesha kwa mitaa miembamba ya makazi kwa kikomo—mwendo cha maili ishirini na tano kwa saa na fursa ndogo ya kupita gari jingine. Gari lililokuwa mbele yangu lilianza kupunguza mwendo, ishirini, kumi na tano, kumi, kisha maili tano kwa saa. Mtu aliyekuwa akiendesha gari aliendelea kuchungulia nje ya dirisha la upande wa abiria. Alikuwa anatafuta nini? Hatimaye, alisimama katikati ya barabara bila ishara yoyote. Bila kujali madereva wengine wote, hatimaye alipata alichokuwa akitafuta—uuzaji wa gereji.

Kwa muda sasa, nilikuwa nikifurahia maisha yaliyojazwa na Roho. Usinielewe vibaya—nilikuwa na changamoto zangu. Lakini niliona mojawapo ya udhaifu wangu mkubwa kuwa ni mwelekeo wangu wa kukosa subira. Nilikuwa kwenye misheni kwa ajili ya Mungu na nilikuwa na mengi ya kufanya—hakuna vizuizi barabarani, tafadhali.

Nilitia nanga gari langu nyuma ya gari la mtafutaji wa kuuza gereji. Ni nini kingine ningeweza kufanya? Sikumfokea; Sikupiga honi yangu; na, kwa sababu fulani, kutovumilia kwangu hakukuwa kumejidhihirisha.

Kisha nikasikia sauti hiyo: *"Mpe nafasi kidogo!"*

Ndiyo, hiyo: "Mpe nafasi kidogo!" Ni kana kwamba maneno hayo yalinifungulia sura mpya. Misheni yoyote, maisha yangu yote, nitakutana na kuzungumza na watu ambao wanaishi maisha *yao* wenyewe kwa maslahi *yao* wenyewe, changamoto, matunzo, matumaini, na mizigo yao. Roho wa Mungu na upendo wote huniambia niwape nafasi kidogo.

Ni miaka imepita tangu niisikie sauti hiyo ya siku hiyo. Dereva mwingine hatimaye akasogea pembeni, akaniruhusu nipite, nikafanya kazi kwa wakati. Lakini muhimu zaidi, nilijifunza kitu kutoka kwa Roho siku hiyo. Angalau

mara mia katika miaka tangu hapo, chini ya hasira na vikwazo, maneno hayo yamenirudia. Na mara mia moja, nimeweza "kumpa nafasi kidogo." Ninashukuru jinsi gani kwamba Roho ambaye huvamia mioyo yetu kikamilifu wakati wa utakaso huzungumza na kutuongoza na kutukuza katika kufanana zaidi na Kristo—hata katika udhaifu.

Mpe nafasi kidogo!

**SEPTEMBA 29** **272**

# Kuongozwa na Roho: Rob na Barbara

*Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili;*
*Matendo 6:3*

*Neno hili likapendeza machoni pa mkutano wote; wakamchagua Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho Mtakatifu, na Filipo, na Prokoro, na Nikanori, na Timoni, na Parmena, na Nikolao mwongofu wa Antiokia.*
*Matendo 6:5*

*Roho akamwambia Filipo, Sogea karibu na gari hili, ukaribiane nalo.*
*Matendo 8:29*

Ilianza kwa karamu—ya mashindano ya mapishi ya chili cook-off yaliyofadhiliwa na darasa la shule ya Jumapili. Lenny aliwaalika jamaa zake Rob na Barbara. Huko, Rob na Barbara walishiriki chakula, ushirika, na kujivinjari. Walisema ulikuwa mlipuko.

Asili ya Barbara ilikuwa ya Kikatoliki na ile ya Rob Mprotestanti, lakini hawakuwa wanaenda kanisani mahali popote. Walikuwa wakisema walihitaji kutafuta kanisa. Baada ya mashindano ya mapishi ya pilipili, simu iliyofuata iliwaalika kwenye shule ya Jumapili na ibada Walikuja.

Rob na Barbara walikuwa wameoana kwa miaka mitatu. Walikuwa na mabinti wanne kutoka kwa ndoa za awali. Rob alikuwa meneja wa duka la usambazaji wa mabomba, na Barbara alikuwa meneja wa mradi wa utafiti wa kitaasisi katika Chuo cha Jumuiya ya Barton County.

Ingawa mwanzoni walifikiri shule ya Jumapili ya watu wazima ilikuwa ya kijinga, walifurahishwa na urafiki na kadi ya ukaribishaji ya ufuatiliaji

waliyopokea. Waligundua kuwa ibada ilikuwa nzuri. Na hivyo wakaanza kuhudhuria kwa ukawaida.

Hatimaye, baadhi ya watu katika darasa ambao wangejenga uhusiano na Rob na Barbara waliuliza kama wangeweza kukutana nao, kuwafahamu vyema, na kushiriki kile ambacho kanisa liliamini. Rob na Barbara walikuwa wazi kwa hilo.

Siku moja ya Februari, Roho akifungua milango, marafiki kutoka kanisani walishiriki injili na Rob na Barbara na kuwapa changamoto ya kumpokea Kristo maishani mwao. Usiku huo, walimpokea.

Rob anaeleza mabadiliko hayo, akisema, "Nilifundishwa kushinda sikuzote—baseball, kandanda, mpira wa vikapu. Karibu niwe baba wa watoto kumi na mmoja katika familia yangu. Nilikuwa kwenye pedestal. Lilikuwa shinikizo kubwa, na sikulipenda. Niliposali, nilihisi kufunguliwa kihisia."

"Mabega yake yaliinuliwa," Barbara anathibitisha. "Uzito ulimtoka. Amekuwa tofauti tangu wakati huo."

Rob anaendelea, "Sasa ninaweza kuomba. Inamaanisha kitu—nina mazungumzo na Yesu. Maisha yangu yamebadilika. Watu wa kazini wananiona tofauti."

Barbara anaelezea mwitikio wake wa kiroho kwa injili kwa njia hii: "Sikubadilika sana mwanzoni. Niliogopa kidogo. Kisha, nilipomtazama Rob, nilianza kukua. Mwanzoni, nilijiona kuwa mzuri; baadaye nilijua sikuwa mzuri kama nilivyofikiria. Nilikuwa nikijificha. Sasa ninafanya zaidi ya kupitia mwendo. Tunapojifunza, *Basic Bible Studies for New and Growing Christians* ninahisi kama ninakula Neno. Linanilisha. Mimi na Rob tunaposhiriki masomo yetu ya Biblia, tunafahamiana vizuri zaidi, na tunakuwa karibu zaidi. Inanisaidia kupona. Yesu sasa yuko mbele na katikati. Lazima ashike usukani wa meli yangu."

Je, ubadilishaji kama huu hutokeaje? Katika Matendo, mlei Filipo alijazwa na Roho na kuongozwa na Roho. Roho alipomwongoza kwenye gari, alimwongoza Mhabeshi kwa Kristo. Yesu alikuwa amewaahidi wafuasi wake kwamba watakapojazwa na Roho Mtakatifu, wangewezeshwa kushuhudia (Matendo 1:8).

Zaidi ya miaka elfu mbili baadaye, watu waliozungumza na Rob na Barbara siku hiyo ya Februari pia walijazwa na kuongozwa na Roho Mtakatifu. Wewe pia unaweza kujazwa na Roho na kuongozwa na Roho. Kumbuka, mwishoni mwa uongozi huo, kutakuwa na Rob na Barbara mwingine.

# Upendo, Ukweli, na Amani

*Haya ndiyo mtakayoyatenda; kila mtu na aseme ukweli na jirani yake; katika malango yenu toeni hukumu za kweli na ziletazo amani.*
*Zekaria 8:16*

Je, wewe ni mtafuta-ukweli? Je, unauliza swali, "Je, nimesema uongo leo?" Ikiwa unayo, una nguvu ya kutosha kukubali? Watu wanaosema uongo ni waoga. Najua hili kwa sababu nilikuwa mmoja.

Watu hawakuhitajika kunipenda, lakini kukataliwa kuliniuma sana hivi kwamba nilikuwa tayari kujidanganya ili niepuke. Niligundua kuwa nilipojidanganya, haikuwezekana kusema ukweli. Nilikuwa adui mbaya zaidi wa nafsi yangu. Kisha nikapata mahali salama pa kuwa halisi, pa kuponya, na kudai nguvu za Mungu katika maisha yangu ya kibinafsi. Ukweli ni hitaji la mabadiliko yote—kwa ajili ya wokovu, uponyaji, na ukuaji.

Aibu ni kizuizi kikubwa katika ukweli. Siri nyingine ambazo zimezikwa ndani hutuharibu na kuondoa nguvu zetu. Mara moja tu, tafuta mtu mmoja salama wa kushiriki naye siri yako na utakuwa njiani kuelekea kupata uhuru.

Ukweli huugonga uhalisia wangu hadi ninafungua mlango. Je, ninakataa mwongozo isipokuwa ukiwa katika namna ninayoidhinisha? Ninapoinama na kujisalimisha, ninapojihatarisha kwa ajili ya Mungu, huwa ninapata amani na upendo, hata nikianguka kifudifudi.

Analoniulizia Yesu zaidi ni kumpenda Bwana Mungu wangu kwa moyo wangu wote, roho yangu yote, nguvu zangu zote na akili zangu zote, *na* kumpenda jirani yangu kama ninavyojipenda mimi mwenyewe. Je, ninaweza kufanya hivyo bila kusema ukweli?

Nancy Shaver[142]

142. Awali kilichapishwa katika *Come Ye Apart* September–October–November 2001 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 80. Imetumika kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

# Asubuhi, Bwana

*BWANA, asubuhi utaisikia sauti yangu,*
*Asubuhi nitakupangia dua yangu na kutazamia.*
*Zaburi 5:3*

Sikuthubutu kutoka chumbani kwangu ili kukabiliana na watu au matatizo hadi nilipomkabili Bwana kwanza. Hali ya anga ya chuoni nilikoishi ilikuwa yenye changamoto.

Mapema katika safari yangu ya Kikristo, nilijikuza katika maisha ya ibada ya kila siku. Kwa kuwa tunasoma kuhusu kuishi maisha yenye kuendelea katika Roho, ilionekana inafaa kuweka muundo wa ibada ambao ungetegemeza maisha hayo.

Acha nieleze muundo ulionifaa. Ondoka na chochote kitakachokusaidia kukuza wakati wako maalum na Bwana:

- Nilichagua wakati maalum kila siku. Kwangu, ilikuwa asubuhi. Ikiwa wewe si mtu wa asubuhi, chagua wakati katika siku ambao unaweza kumpa Mungu akili yako yote. Usimpe tu mabaki ya nguvu zako.
- Ninapata kikombe cha kahawa, naenda kwa kiti ninachokipenda, na kuketi kwa muda nikiwa na mtazamo huu: *Bwana, ungependa kuniambia nini leo?* Wakati mwingine ananiambia neno lililo wazi; mara nyingi, nahisi tu kuna uwazi kati yetu.
- Husoma ukurasa mmoja kutoka katika kitabu cha ibada cha kila siku, nikiongozwa na tarehe. Vitabu ambavyo nimetumia ni pamoja na *My Utmost for His Highest*, cha Oswald Chambers; *Take Time to Be Holy*, cha Samuel Logan Brengle; *This Day with the Master*, cha Dennis Kinlaw; Siku hii na Mwalimu, na Dennis Kinlaw; na *Streams in the Desert*, cha Lettie Cowman.
- Nilisoma kutoka *The One Year Bible*, ambayo inajumuisha sura mbili za Agano la Kale, zaburi, mistari mitatu kutoka Mithali, na kifungu cha Agano Jipya kila siku. Kwa kusoma kila siku, mimi hupitia Biblia nzima katika mwaka mmoja. Ninaweka alama kwenye maandiko muhimu kwa kiangazio ninapondelea.
- Mimi huandika katika shajara nafuu. Katika kuandaa shajara yangu, ninataja andiko muhimu ambalo nimetoka kulisoma, kisha kuandika

mchanganyiko wa mazungumzo na Bwana, maingizo ya shajara, na mipango ya siku hiyo. Mara nyingi mimi hupitia maombi yaliyojibiwa kutoka kwa ingizo la shajara ya siku iliyopita.
- Kisha ninaenda kwenye chumba changu cha maombi ninachokipenda—ofisi kubwa katika ghorofa yangu ya chini. Ninaweka orodha ya kina ya maombi mbele yangu na kuweka karatasi na kalamu karibu na uongozi wa kushajiishwa au kiungu. Ninaomba nikitembea kwa miguu kwa sababu hivyo niko macho zaidi kuliko kupiga magoti. Wakati huu, ninapitia ushirika halisi na Bwana na kumpa sifa nyingi.

Wakati nilipojaribiwa kuwa mlegevu katika wakati wangu wa ibada, Bwana alinikumbusha kwamba, kwa kuwa alikuwa amekuja duniani kote na kufa kwa ajili yangu, ilikuwa na maana kubwa sana kwake kwamba ningetumia muda pamoja naye kila siku. Kwa zaidi ya miaka sitini, nimekuwa nikikutana naye kwa uaminifu asubuhi, na nimekosa mkutano huo mara chache sana.

Fanya uamuzi kuhusu wakati wako wa kawaida wa ibada na Bwana—thawabu ni kubwa sana.

**OKTOBA 2** **275**

## Wachungaji wenye Upendo

*Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo*
*kwao waaminio, katika usemi na mwenendo,*
*na katika upendo na imani na usafi.*
*1 Timotheo 4:12*

Wachungaji wenza Ben na Kelly walikuwa wachanga walipoanza kuchunga kanisa lao la Maryland. Sasa wamewekeza zaidi ya miaka thelathini na mmoja katika kutaniko lao lililo hai na lenye shangwe. Nilikuwa mgeni nyumbani mwao kwa juma la ibada za uamsho, na walikuwa vielelezo vya usemi wa kimungu na upendo kama wa Kristo hivi kwamba roho yangu iliinuliwa. Ingawa kuna mazungumzo mengi kuhusu kasoro za baadhi ya wachungaji, ninavutiwa na idadi kubwa ya wachungaji wenye upendo ambao nimekutana nao katika takriban uamsho elfu moja. Katika wiki moja, haya ndiyo niliyoona kwa Ben na Kelly:

- Walitayarisha kanisa lao kikamilifu kwa ajili ya juma la uamsho.
- Waliniweka katika chumba kizuri chenye bafu langu.

- Ben alibeba mzigo wangu mzito hadi chumbani kwangu.
- Kelly alinilisha chakula kitamu.
- Ben alituma ujumbe mwingi kuwaalika watu kwenye ibada.
- Ben alikuwa amejenga uhusiano na kikundi cha wavulana vijana kutoka katika nyumba za mzazi mmoja kwa kucheza nao mpira wa vikapu .Alikuwa kama baba kwao.
- Kelly aliwakaribisha wavulana wa mpira wa vikapu kwa ajili ya chakula cha jioni siku moja, na wote walikuwa kanisani usiku huo.
- Ben alikuwa ameanzisha biashara ya kupasua mbao na kuajiri wavulana wa mpira wa vikapu ili kuwasaidia kustawisha maadili ya kazi na kupata mapato.
- Kila usiku, mwisho wa kila ibada, Ben na Kelly walikuwa madhabahuni wakiomba na au kuwashauri watu waliokuwa wakimtafuta Mungu.
- Siku nilipoondoka kuendesha gari maili 1,100 hadi shughuli yangu iliyofuata, Ben na Kelly waliamka saa 5:00 asubuhi ili kunisaidia kupakia vitu kwenye gari langu na kuomba pamoja nami.
- Walinijulia hali kwa simu na ujumbe ili kuhakikisha kuwa nimefika nyumbani salama.

Nilipowazia wiki hiyo, nilihisi kupendwa sana. Ndiyo, kuna wachungaji wengi wenye upendo huko nje.

**OKTOBA 3** **276**

# Hakika—Mweza Yote

*Tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake.*
*Ufunuo 1:5*

Dola la Kirumi lilikuwa limetandaza mahema yake yenye nguvu kuzunguka makanisa ya Kristo, na Ufunuo 1 inatuchorea tukio la kushangaza. Katika sura hii, Yohana na wanafunzi wengine wanaohusika wanapokea neno lenye nguvu kutoka kwa kiti cha enzi—lakini ni kiti cha enzi cha Kristo, si cha Kaisari (1:4). Kristo ndiye "mtawala wa wafalme wa dunia" (1:5).

Mashaka yoyote tunayokumbana nayo maishani, tunaweza kuwa na uhakika juu ya hili katika Kristo: Dhambi zetu zote *zilizopita* zimesamehewa (1:5); "kazi yetu ya *sasa* ni kumtumikia Mungu kama "ufalme na makuhani" (1:6); *mustakabali* wetu ni kumkaribisha atakapokuja mawinguni (1:7).

Ili kuwatia moyo watumishi wake wapate ushindi, Yohana anawatumia "neema na amani" (1:4). Kwa hivyo, wakati bonasi ya kampuni ni ndogo sana kuliko ilivyotarajiwa na mipango ya likizo inapaswa kughairiwa; wakati mtu tuliyefikiri tunaweza kumtegemea anatoka nje; wakati kimbunga au tetemeko la ardhi au tufani kupiga ardhi na watu kufa - ndipo tunapohitaji mtu. Bado kuna mmoja ambaye atakuwa na neno la mwisho, ambaye bado anakuja, ambaye ana nguvu kwa siku yetu.

Yohana, akiteseka lakini akiwa imara, alipokea ujumbe alipokuwa "katika kisiwa cha Patmo" (1:9). Kama vile mhubiri mmoja alivyosema, "Yohana *alikuwa* Patmo; Patmo haikuwa juu yake."

Samuel na Gladys Heap walikuwa wamishenari wanaomcha Mungu, walioongozwa hadi Amerika Kusini na Kati. Niliishi kando ya barabara kutoka kwao wakati wa likizo yao. Miaka ilipita, na walianza kupata matatizo ya afya. Nilimpigia simu Bi. Heap siku moja na kumuuliza, "Dada Heap, unaendeleaje kwenye mazingira haya?"

Alijibu kwa haraka na kwa nguvu, "Oh, Ndugu Shaver, siko kwenye mazingira hayo. Niko juu yake."

Ni kiwango cha ajabu cha ushindi! Ni kwa sababu alijua "Alfa na Omega... aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi" (1:8). [143]

OKTOBA 4 **277**

# Anaweza

*Na mmojawapo wa wale wazee akaniambia, Usilie; tazama, Simba aliye wa kabila la Yuda, Shina la Daudi, yeye ameshinda apate kukifungua kile kitabu, na ile mihuri yake saba.*
*Ufunuo 5:5*

Awali, mimi na Nancy tulimtembelea mwanasheria ili kuandaa utaratibu wa urithi na wosia wetu wa mwisho. Ndani ya kurasa za utaratibu huo kuna

143. Awali yalichapishwa katika *Standard* Agosti 2009 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 4. Imetumiwa kwa idhini.

mpango wa kuondoa mali zetu zote za duniani ili kusiwe na mkanganyiko. Nakala asilia ya utaratibu wa urithi imefungwa kwenye sanduku la kufuli kwenye benki ya ndani, amoj mmoja tu anayestahili kuifungua. Mtekelezaji aliyetajwa atatumia ufunguo uliofichwa kufungua kisanduku cha kufuli, kufungua utaratibu huo, na kutekeleza matakwa yetu.

Ufunuo 5 inasimulia juu ya hati kama hiyo—hati iliyokunjwa yenye mihuri saba. Ni hati ya ahadi, agano, na Yohana analia kwa sababu hakuna anayestahili kuifungua.

Ghafla, mbingu yasema: "Simba wa kabila la Yuda... *yaweza* kukifungua hicho kitabu na mihuri yake saba" (5:5). Hii inaongoza kwa ujio wa ufalme.

Viumbe wanne, wazee ishirini na wanne, maelfu ya malaika, na kila kiumbe hai wanaanza kumsifu. Anastahili kwa sababu...

- Alitoa vyote: "kwa damu yako" (5:9)
- Aliwafikia wote: "kila kabila na lugha na jamaa na taifa" (5:9)
- Aliwafanya wote: "Ufalme na makuhani wamtumikie Mungu wetu" (5:10)
- Atatuweka sisi kutawala juu ya wote: "watatawala juu ya nchi" (5:10)

Mwanakondoo anastahili kwa sababu alimwokolea Mungu binadamu kwa damu yake.

Ninapoandika haya, nilipokea simu kutoka kwa Janell, ambaye alikuja kanisani kwetu akiwa mtu mzima. Watu kadhaa kutoka kanisa letu walimtembelea na kushiriki Kristo naye, na akampokea mwokozi. Aliniambia, "Alinirudisha kwenye uhusiano naye. Sasa maisha yangu ni tofauti."

Ndiyo, tunapaswa kuwa miongoni mwa wale wanaomsifu Mungu, kwa sababu yule anayeweza kufungua kitabu cha kukunjwa kilichotiwa muhuri pia anaweza kutosheleza mahitaji ya maisha yetu binafsi. Naye anawafikia watu wa miji yote: "kila kabila na lugha na jamaa na taifa."[144]

144. Awali yalichapishwa katika *Standard* Agosti 2009 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 4. Imetumiwa kwa idhini.

# Mwenye Haki Kweli

*Wanadamu wakaunguzwa na joto kali, nao wakalitukana jina la Mungu aliye na mamlaka juu ya mapigo hayo; wala hawakutubu wala kumpa utukufu.*
*Ufunuo 16:9*

Ufunuo 16 inaonyesha matokeo ya kutisha ya dhambi. Sheria za Mungu ni zilezile kwetu sote, na kutotii huleta matokeo mabaya sana. Katika sura hii, matokeo haya yanawakilishwa na mabakuli saba ya ghadhabu ya Mungu.

Wengine hufikiri kwamba Mungu huwapeleka watu kuzimu. Ukweli ni kwamba Mungu anajaribu kutuzuia tusipotee milele, lakini anaturuhusu kwenda huko ikiwa tunasisitiza—ni chaguo letu.

Kwangu mimi, mtu anayechagua kwenda kuzimu ni kama kijana mwenye hasira anayejitosa ndani ya nyumba ya marafiki zake, na kutishia kuruka kutoka kwenye dirisha la ghorofa ya sita kusababisha kifo chake. Rafiki yake wa kwanza anamsihi, "Usifanye hivyo!" Anampita kwa kasi.

Rafiki wa pili, akiwa amenyoosha mikono, anamhakikishia kwamba atamsaidia kutatua matatizo yake—ikiwa tu atazungumza. Kijana huyo anakazana kuelekea dirishani.

Rafiki wa tatu anajaribu kumzuia kimwili, lakini kijana huyo anamsukuma kando na kuruka.

Akielekea chini, anapiga kamsa, "Kwa nini hakuna mtu aliyenisaidia? Kwa nini hamkunizuia? Nimewakasirikia sana kwa kutoniokoa!"

Hapa kuna mtu ambaye amelipita Neno la Mungu kwa haraka; wito wa Baba; damu ya Kristo; kusihi kwa Roho; ushuhuda wa marafiki; kuhubiri injili; upendo wa Wakristo; ibada ya kanisa. Mtu huyu ni kama wale waliotajwa katika aya ya 9 na 11: "Walikataa kutubu."

Hata hivyo, hatupaswi kamwe kukatia tamaa wokovu wa mtu au kuacha kuwaombea. Kwa mfano, siku moja, Haruni alipiga magoti kwenye madhabahu, akalia, na kusali. Niliuliza kwa nini alikuwa na maumivu, na akasema, "Nilikuwa nimekata tamaa juu ya baba yangu, lakini Mungu alinihukumu. Nimeubeba mzigo wake tena."

George Mueller, mtu aliyejulikana sana kwa yake ya maombi, aliombea wokovu wa marafiki wawili kwa miaka arobaini na minane. Baada tu ya Mueller kufa wawili hao walipata wokovu.

Hatupaswi kukata tamaa. Mungu hataki "mtu yeyote apotee, bali kila mtu afikie toba" (2 Petro 3:9). [145]

OKTOBA 6 **279**

# Yesu Hushinda

*Na tazama, naja upesi; heri yeye ayashikaye maneno ya unabii wa kitabu hiki.*
*Ufunuo 22:7*

Mke wangu, Nancy, alikuwa na mwaka mgumu. Aliandika hivi: *Ikiwa ningelazimika kuupa mwaka huu jina, ningeuita "Mwaka wa Dhoruba." Adui alikuja kupasua na kurarua, na Yesu anakuja kutushona tena… Usimwambie Mungu jinsi yako ilivyo kubwa, Iambie jinsi Mungu wako alivyo mkubwa*.

Na mwishowe, ameshinda.

Katika Ufunuo 22, tuna uthibitisho wa ujumbe wa tumaini ambao unasikika katika kitabu chote." Mara tatu katika sura hii, Yesu anarudia, "Ninarudi karibuni" (22:7, 12, 20). Kwa wote wanaopitia majaribu, misukosuko na dhiki—shikilieni! Ufunuo ni kitabu cha wale wanaopitia nyakati ngumu.

Sura hii ya mwisho pia inatupa tumaini la mbinguni. Yesu anatuhakikishia kwamba wote "wanaosafisha mavazi yao" katika damu ya Kristo "watakuwa na haki ya kuuendea mti wa uzima" (22:14). Hakuna dhambi itakayoruhusiwa mahali hapo. Patakuwa tu kwa ajili ya wale ambao tabia na mienendo yao imebadilishwa na Yesu.

Kisha, kuna mshangao. Baada ya kusema kwa uthabiti kwamba dhambi haitaruhusiwa mbinguni (22:15), Mungu mwenye upendo, Kristo mwenye neema, anatoa mwaliko mmoja: "Yeye anayetaka na ayatwae maji ya uzima bure" (22:17). Mpaka mwisho wa kitabu, mwisho wa Biblia, mwisho wa dunia kama tujuavyo, Kristo bado anasihi kila mtu apokee wokovu.

---

145. Awali yalichapishwa katika *Standard* Agosti 2009 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 4. Imetumiwa kwa idhini.

Ujumbe wa Ufunuo unafupishwa katika simulizi ya kijana mmoja ambaye alikuwa amemaliza kujifunza kitabu hicho na alikuwa na uhakika kwamba alikifahamu chote. Alipokuwa akiingia darasani jioni moja, alimwona mzee akisoma. Akiwa tayari kumfundisha, alisema, "Mzee, unakielewa?" mzee alijibu, "Yup. Yesu anashinda."

Ni hayo tu! Yesu anashinda! Na naye, sisi pia. [146]

OKTOBA 7 **280**

# Bali Mjazwe Roho

*Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana. Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho.*
*Waefeso 5:17-18*

Alirudi kutoka likizoni na wanafamilia na akaendesha gari moja kwa moja hadi kituo cha kurekebisha uraibu wa pombe kurekebishwa kwa wiki tatu. Baadaye, nilimuuliza kilichomfanya anywe pombe

Alisema, "Kijamii, nilihisi kama sikufaa. Bia chache zilinilegeza. Lakini nilipoenda sehemu moja hadi nyingine jioni, ningeweza kunywa bia kumi na mbili. Kilichonizindua ni kwamba, nilipokuwa nikirudi nyumbani kutoka Memorial Day kunywa pombe, niligonga nguzo nikiwa nimeshikilia dari juu ya njia yangu ya kuingia."

Wiki iliyofuata, baada ya kusherehekea siku yake ya kuzaliwa, hakukumbuka kuendesha gari kwenda nyumbani, na aligonga nguzo ileile ya dari.

Alikuwa amemkubali Kristo, lakini sasa alikuwa ameazimia kutatua tatizo lake la unywaji pombe. Alishtuka mgonjwa mwenzake alipomuuliza ikiwa alipanga kuanza kutumia tena—tayari alikuwa na miadi na muuzaji wake wa dawa za kulevya. Lakini mtazamo wake ulikuwa, "mimi ni mmoja na nimemaliza."

Ni kweli kwamba wafuasi wa Yesu walikunywa divai. Hata hivyo, haikuwa sawa na divai ya leo au vileo vingine. Uwiano wa siku hizo ulikuwa sehemu tatu za maji kwa sehemu moja ya divai. Pombe ilisafisha maji, na maji

146. Awali yalichapishwa katika *Standard* August 2009 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 4. Imetumiwa kwa idhini.

yakapunguza divai.[147] Zaidi ya hayo, Maandiko yana msimamo mkali dhidi ya ulevi. Warumi 13:13: "Na tuenende kwa adabu, kama wakati wa mchana, si kwa ulafi na ulevi." Na Wagalatia 5:21 inafuata kauli yake juu ya ulevi na, "watu wa namna hii hawataurithi ufalme wa Mungu."

Ninawasihi watu wajizoeshe kuepukana na pombe. Walevi wa kijamii mara nyingi hudai kwamba hakuna shida—watakuwa na kinywaji kimoja tu. Lakini mojawapo kati ya athari za kwanza za pombe ni kupunguzwa kwa vizuizi vya afya—ambavyo bila shaka hurahisisha kunywa kinywaji cha pili na cha tatu. Maandiko pia yanatuhimiza kuzingatia ushawishi wetu kwa wengine: "Ni afadhali kutokula nyama au kunywa divai au kufanya kitu kingine chochote kitakachosababisha ndugu yako kuanguka" (Warumi 14:21). Kwa wale wanaokunywa ili kupunguza msongo, Waefeso 5:18 hutoa jibu bora zaidi: "Badala yake, mjazwe Roho."

Rafiki yangu alipomaliza marekebisho ya uraibu, aliacha pombe. Aliniambia kwamba, tangu uamuzi huo, wasiwasi na dhiki yake imepungua. Alipoteza pauni kumi na tano na anahisi afadhali kimwili. Mara chache tu ndio yeye hufikiria juu ya kunywa tena. Kwa ujumla, yeye amejengeka zaidi katika mwingiliano wake na wengine. Rafiki mmoja alitambua, "Sasa anatabasamu. Ametulia na mwenye furaha sana—mwenye furaha zaidi."

Sasa, baada ya miaka miwili ya urazini, amerejea katika sehemu ile ile ya likizo ambayo alisafirishwa kwenda kwenye marekebisho miaka miwili iliyopita. Alisema anahisi ukaribu na Roho Mtakatifu.

Wakati wa maandishi haya, mwanamke mlevi alitolewa kutoka kwa maji kwenye ufuo wa karibu, amekufa.

OKTOBA 8 **281**

# Je, Unaamini Kuzimu?

*Ikawa yule maskini alikufa, akachukuliwa na malaika mpaka kifuani kwa Abrahamu. Yule tajiri naye akafa, akazikwa. Basi, kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Abrahamu kwa mbali, na Lazaro kifuani mwake. Akalia, akasema, Ee baba*

---

147. Robert H. Stein, "Wine Drinking in New Testament Times," *Christianity Today*, Juni 20, 1975, 9–16.

*Abrahamu, nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, aupoze ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika moto huu.*
*Luka 16:22-24*

Watu wengi wangekuambia, "Siamini kuzimu!" Hata hivyo wengi wao, wakati wa hasira au katika jaribio la kusisitiza kauli, watairejelea kuzimu. Kwa mfano, ikiwa mtu ameghadhabishwa na jinsi anavyozungumziwa, anaweza kujibu, "Unafikiri wewe ni nani, unazungumza nami hivyo? Nenda kuzimu."

Hebu tufikirie hili kwa muda. Je, ungejaribu kusisitiza kauli kwa kutumia mahali au wazo ambalo hata halipo? Bila kujua, je, inawezekana kwamba mtu anayetumia neno "kuzimu" anaamini kweli kwamba ipo?

Zingatia maandiko yanasema nini kuhusu kuzimu:

- Luka anaeleza Yesu akizungumza kuhusu tajiri mwenye ubinafsi ambaye anateseka kuzimu (Luka 16:22–24).
- Mathayo anaeleza kuwa Yesu akisema, "Ondokeni kwangu, ninyi mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika wake" (25:41). Kumbuka kusudi la awali la moto wa milele: "uliotayarishwa kwa ajili ya Ibilisi na malaika wake."
- Petro anaandika, "Kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika walipokosa, bali akawapeleka kuzimu, akawaweka katika minyororo ya giza ili walindwe hadi ije hukumu; ikiwa hakuuhurumia ulimwengu wa kale alipoleta gharika juu ya watu wake wasiomcha Mungu, bali alimlinda Nuhu, mhubiri wa haki, na wengine saba; ikiwa aliihukumu miji ya Sodoma na Gomora kwa kuiteketeza na kuwa majivu, na kuifanya iwe mfano wa mambo yatakayowapata waovu; na ikiwa alimwokoa Loti, mtu mwadilifu, ambaye alihuzunishwa na mwenendo mpotovu wa wale waovu (maana mtu huyo mwadilifu, akiishi kati yao siku baada ya siku, aliteseka katika nafsi yake ya haki kwa matendo ya uasi-sheria aliyoyaona na kuyasikia)—ilivyo, basi, Bwana anajua jinsi ya kuwaokoa watauwa na majaribu, na kuwaweka wasio haki wapate adhabu siku ya hukumu" (2 Petro 2:4–9). Kumbuka jinsi Mungu anavyojali kuwaokoa watu wanaomcha.
- Kwenye maono yake katika Ufunuo, Yohana anaandika maneno yafuatayo: "Akaniambia, Imekwisha; Mimi ndimi Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Kwa wenye kiu nitawapa maji kutoka katika chemchemi ya maji ya uzima bila gharama. Washindi watarithi haya yote, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watoto wangu. Lakini waoga, wasioamini, wachafu, wauaji, wazinzi, wachawi, waabudu

sanamu na waongo wote, watatupwa kwenye ziwa la moto la kibiriti. Hiki ndicho kifo cha pili" (21:6–8).

Pamoja na kauli hizi zote kali kuhusu kuzimu, hebu tukumbuke kwa nini Mungu alimtuma Yesu Kristo hapa duniani na kwa kila moyo:

- Luka 19:10 inasema, "Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa waliopotea."
- Yohana 3:17–18 inasema, "Kwa maana Mungu hakumtuma Mwanawe ulimwenguni ili auhukumu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi, bali asiyeamini amekwisha kuhukumiwa kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu."
- Ufunuo 3:19–20 inasema Yesu: "Kwa hiyo uwe na bidii na utubu. Niko hapa! Ninasimama mlangoni na kubisha. Yeyoteakiisikia sauti yangu na kuufungua mlango, nitaingia na kula pamoja na mtu huyo, na wao pamoja nami."

Yesu Kristo anafanya kila juhudi kuniokoa mimi na wewe na wale wanaotuzunguka kutokana na maisha yaliyovunjika, yaliyotawaliwa na dhambi hapa na kuzimu baadaye. Ni sababu iliyoje ya kuwafikia wengine kwa upendo wa Mungu na uweza wa kuokoa wa Yesu Kristo.

**OKTOBA 9** **282**

# Gharama ya Ukweli

*Bali kama si hivyo, ujue, Ee mfalme, ya kuwa sisi hatukubali kuitumikia miungu yako, wala kuisujudia hiyo sanamu ya dhahabu uliyoisimamisha.*
*Danieli 3:18*

Ni rahisi kwangu kufuata "fanya" badala ya "usifanye," na ndivyo walivyofanya vijana hawa watatu. Walimwabudu Mungu aliye hai kwa mioyo yao yote, nafsi na akili zao zote, kwa hiyo hapakuwa na chochote kilichosalia kwa miungu ya uwongo. Walikuwa wamejitolea sana kwa kweli kiasi kwamba hata iweje, wasingesalimisha imani yao au kusujudu na kumwabudu mungu mwingine yeyote—na kwa hakika si mungu aliyetengenezwa kwa dhahabu baridi isiyo na uhai. Hata tishio la kifo halikuwatikisa.

Hawakuwa tayari kujifanya kuabudu sanamu ili kujilinda. Hawakuwa na karamu ya huruma, kumsihi Mungu, au kusema, "Hii si haki! tazama jinsi tulivyokuwa waaminifu—unawezaje kuruhusu hili litendeke?" Mambo

yalipokuwa hayaendi sawa, hawakukimbia. Hawakujaribu kudhibiti kitu ambacho hawakuwa na nguvu juu yake. Walitumaini tu kwamba, katika maisha au katika kifo, "Mapenzi yako yatimizwe."

Ninaweza kuandika mambo haya kwa sababu ndivyo ningejaribiwa kufanya. Ninaweza kuwa mbaya katika kusikiliza. Ninaweza kuwa na shughuli nyingi wakati sitaki kusikia ukweli kuhusu kazi inayofuata. Hata hivyo katika mapambano yangu, Mungu yupo, akinielekeza. Ananifungulia njia ya kusimama kwa ujasiri na kujifunza kwamba ninaweza kufanya hivyo—naweza kumtumaini.

Je, Mungu ananong'onezana ukweli nawe leo? Je, utajiruhusu kusikia na kutii?

Nancy Shaver[148]

OKTOBA 10 **283**

# Barua kutoka Gerezani

*Na wengi wa hao ndugu walio katika Bwana, wakapata kuthibitika kwa ajili ya kufungwa kwangu, wamezidi sana kuthubutu kunena neno la Mungu pasipo hofu.*
*Wafilipi 1:14*

Kuhubiri na kutoa ushuhuda kulimletea nini mtume Paulo? Muda gerezani, miongoni mwa mambo mengine. Kushtakiwa pasipo haki; kujaribiwa pasipo haki; kufungwa jela pasipo haki; sasa katika minyororo na kulindwa kwa ukaribu—ilionekana kuwa maisha yasingeweza kuwa mabaya zaidi. Tafadhali kumbuka mtazamo wa mfuasi huyu wa Kristo aliyejitoa kikamilifu, aliyetakaswa kabisa na aliyemilikiwa na Roho. Anaandika kutoka gerezani kwa kanisa alilolianzisha huko Filipi:

- "Kama vile nilivyotazamia sana, na kutumaini, kwamba sitaaibika kamwe, bali kwa uthabiti wote, kama sikuzote na sasa vivyo hivyo Kristo ataadhimishwa katika mwili wangu; ikiwa kwa maisha yangu, au ikiwa kwa mauti yangu" (Wafilipi 1:20).

148. Awali yalichapishwa katika *Come Ye Apart* September–Octoba–Novemba 2001 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 77. Imetumiwa kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

- "Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yoyote niliyo nayo" (Wafilipi 4:11).
- "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu" (Wafilipi 4:13).
- "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu" (Wafilipi 4:19).
- "Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu" (Wafilipi 4:6-7).

Hata leo tunapata barua kutoka gerezani. David alihudhuria wiki ya ibada za uamsho katika kanisa dogo la Illinois. Alikuwa akikabiliwa na matatizo ya kisheria na, akimtafuta Bwana usiku baada ya usiku, aliondoa tabaka za dhambi. Wiki kadhaa baadaye alipata kifungo chake gerezani. Haya ndiyo aliyotuandikia kutoka gerezani:

> *Nilipendekezwa na mahakama na kuahidiwa kwenda kwenye kambi ya mafunzo (IIP), ambayo ni programu ya miezi minne, lakini Capitol ya Illinois ilinikataa. Kwa hivyo nimekwama kufanya miaka miwili ya kifungo cha miaka minne. Mungu wangu ni mwaminifu na ana mpango. Siku moja baada ya kujua, ingawa nilikandamizwa, nilibaki mwaminifu, na jambo la ajabu lilitokea. Mwanaselo mwenzangu mpya, ambaye alikuwa akinitazama nikisoma Biblia yangu na kusali kwa bidii licha ya kila jambo, alizungumza nami. Nilihisi hisia hii nzito kuifanya, na ingawa nilikuwa na hofu na woga (sijawahi kufanya kitu kama hiki hapo awali), nilifanya.*
>
> *Nilimuuliza tu Bradley S. Peters, "Je, ungependa kuokolewa?"*
>
> *Cha kushangaza, kwa sura hii laini ya kijibwa katika macho ya kijana huyu mgumu, alisema, "Ndiyo."*
>
> *Kwa hiyo, mnamo Juni 30, katika jumba la X huko Hillsboro, Illinois, DOC, tukiwa tumepiga magoti pale pale kwenye sakafu hiyo chafu ya selo huku mikono yetu ikiwa imekunjwa, nilimwongoza Bradley katika sala ya wokovu, naye akamkubali Kristo. Kwenye sakafu hiyo chafu akawa msafi kama theluji. Alikuwa mtu wa kwanza ambaye nimemwongoza kwa Yesu, na ilikuwa mojawapo ya mambo yenye nguvu zaidi ambayo nimekuwa sehemu yake. (Atukuzwe Mungu!)*
>
> *Ni vigumu kufikiria kwamba lile gamba hatari, la kuuza dawa za kulevya, uraibu wa dawa za kulevya, jeuri, lenye uovu, na kuharibu maisha ya watu nililokuwa zamani sasa linafanya kazi kubwa kwa ajili ya Yesu Kristo. Wewe na mimi sote tunajua niliokolewa na kuwekwa huru kutokana na uraibu wangu kabla ya kufungwa kwangu. Ningeweza kutumia mahali hapa kuongeza IQ yangu na hadhi yangu na kuwa mbaya zaidi*

*kuliko nilivyokuwa. Lakini, kwa neema ya Mungu na Mwokozi wangu, Yesu Kristo, nimegeuza mahali hapa kuwa kambi ndefu ya Biblia.*

Paulo hakuweza kuwakimbia walinzi wake—lakini, kwa upande mwingine, mlinzi hakuweza kumkimbia. David hakuweza kumtoroka mfungwa mwenzake—lakini mwenzake pia hakuweza kumkimbia. Katika hali zote mbili inaweza kusemwa, "Yale yaliyonipata yamesaidia kuendeleza injili" (1:12).

Je, unamruhusuje Mungu aitumie hali yako?

**OKTOBA 11** **284**

# Baba na Yesu Wanafanya Kazi, Sehemu ya 1

*Akawajibu, Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi.*
*Yohana 5:17*

Je, mama na baba yangu wangenipa zawadi ifaayo kwa ajili ya kufuzu kwangu katika shule ya upili? Baba yangu alinipa saa nzuri nilipofuzu darasa la nane, lakini shule ya upili—hilo lilikuwa kubwa zaidi. Sikujua kilichokuwa kikifikiriwa, kupangwa, kulipwa, na kufanya kazi kilivyokuwa kikiendelea nyuma ya pazia. Nikiwa na wasiwasi, alifanya kazi. Punde niligundua kuwa zawadi yangu ilikuwa safari ya maili elfu kumi, ya siku thelathini kote Marekani na walimu wawili wa shule ya upili na wanafunzi kumi na wanne, wakipiga kambi usiku. Hadi leo ninakumbuka Yellowstone, Glacier, Grand Canyon), Badlands, Crater Lake, Redwoods, Mount Shasta, vinginevyo. Baba yangu alikuwa akifanya kazi yote, na ilikuwa nzuri sana.

Katika usemi unaoonekana kuwa wa kustaajabisha kwa mtazamo wa kwanza, Yesu asema, "Baba yangu huwa katika kazi yake siku zote… na mimi pia ninafanya kazi." Siku ya Sabato, Yesu alimponya mtu ambaye alikuwa mlemavu kwa miaka thelathini na minane. Viongozi wa Kiyahudi baadaye walianza kumtesa kwa ajili ya "kufanya kazi" kwake siku ya Sabato. Yesu aliwajibu kwa kauli kuhusu kazi yake na ya Baba yake.

Usikose, Yesu alikuwa mwaminifu kwa ibada ya Sabato. Hata hivyo, alikuwa akiipanua maana ya Sabato kujumuisha kazi za dharura na matendo ya upendo na huruma. Baba yuko kazini mwake. Kazi zake ni pamoja na upendo, huruma, rehema, kujali, uponyaji, kuokoa, utakaso. Kulikuwa na

nyanja ya kiroho ya kazi ambayo ilienda zaidi ya kile walichokielewa viongozi wa Kiyahudi.

Kanuni hii inakwenda zaidi ya Sabato. Katika masuala yote ya maisha yako, au mambo makubwa ya taifa au dunia, tuone au tusione, Baba daima anafanya kazi, na Kristo pia. Baba na Mwana wanashughulika na watu binafsi na wanafanya kazi katika mambo ya kimataifa, kwa manufaa yetu na utukufu wake.

Kazi hii inaonekana katika maisha ya mtu binafsi. Katika Yohana 4:49–50, ofisa wa kifalme alimwomba Yesu amponye mwanawe, ambaye alikuwa karibu kufa. Yesu akajibu, “Nenda, mwanao ataishi.”

Yule ofisa alipokuwa akirudi nyumbani, watumishi wake walikutana naye na kumpa taarifa kwamba mtoto wake amepona. Yule ofisa akauliza ni lini jambo hili limetukia, nao watumishi wakasema, “Jana saa saba alasiri homa ilimwacha.” Ndipo yule baba akatambua kwamba huo ulikuwa ndio wakati hasa ambao Yesu alikuwa amemwambia, “Mwanao ataishi.” Kwa hiyo yeye na jamaa yake yote wakaamini” (Yohana 4:52–53). Matukio mengi kama haya ya kimungu yanayotukia kwa wakati ni uthibitisho kwamba Baba na Mwana wanafanya kazi pasipo kuonekana.

Wakati mwingine tunafadhaika kwa sababu ya uwepo wa hali mbaya. Dk. Orval Nease alipitia hali ya kufadhaisha na yenye maumivu. Alisoma katika Biblia yake, “Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake” (Warumi 8:28). Kauli hiyo ilikuwa ya kutatanisha kutokana na uzoefu wake. Dk. Nease alikuwa mwanafunzi wa Kigiriki, lugha ya asili ya Agano Jipya. Kwa hiyo alifungua Agano lake Jipya la Kigiriki kwenye Warumi 8:28 na kusoma, “Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake.” Dk. Nease ghafla alitambua kwamba Mungu angeweza kuchukua vitu vyote, hata vile ambavyo shetani anaweza kutuma, na kuvifanya kuwa muundo kwa ajili ya wema. Kitulizo cha ajabu! Kumbuka kusudi la Mungu katika 8:29: kwamba ‘tufanane na mfano wa Mwana wake.

# Baba na Yesu Wanafanya Kazi, Sehemu ya 2

*Akawajibu, Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi.*
*Yohana 5:17*

Baada ya Yesu kuwaambia viongozi wakosoaji kwamba yeye na Baba wanafanya kazi, anaingia katika majadiliano marefu, yenye kina kuhusu uhusiano wa karibu wa Baba na Mwana (Yohana 5:19–30). Miongoni mwa miradi ambayo Baba na Mwana wanafanya ni wakati "wale wote waliomo makaburini mwao wataisikia sauti yake na kutoka—wale waliofanya mema watafufuliwa waishi, na wale waliofanya yaliyo maovu watafufuliwa wahukumiwe" (5:28–29). Ingawa Baba na Mwana wote wanafanya kazi katika mpango huu wa wakati wa mwisho, kuna kipengele kimoja cha ukomo: "Lakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake" (Mathayo 24:36).

Catherine Marshall alipambana na ugonjwa mbaya. Aliona shida. Mumewe, Peter Marshall, kasisi wa Seneti ya Marekani kutoka 1947 hadi 1949, alikufa akiwa na umri wa miaka arobaini na sita. Baada ya Peter kupelekwa hospitalini kwa gari la wagonjwa, Catherine akiwa nyumbani na mtoto wao mdogo walijitosa sakafuni na kutafakari jinsi ya kuomba. Alisema, "Ghafla kulikuwa na hisia ya kuzungukwa na upendo wa Mungu Baba—uliofunikwa ndani yake, ukiwa umejaa upole usio na kikomo. Nilipigwa na butwaa, ikifuatiwa na imani kwamba haikuwa lazima *kuulizia* chochote. Nilichopaswa kufanya ilikuwa kujikabidhi mimi na Peter na mustakabali wetu kwa upendo huu mkuu.[149]

Aligundua kwamba Mungu angeweza kufanya hata matatizo hatimaye yageuzwe kuwa wema. Baada ya Peter kufa, kwa wakati wake na neema ya Mungu, Catherine aliandika *A Man Called Peter* (ambacho baadaye kilifanywa kuwa filamu) na kitabu kingine kuhusu safari yake ya kiroho, *Beyond Our Selves*. Kwa hiyo, mamilioni ya watu wameletwa karibu zaidi na Mungu. Baba na Mwana wamekuwa wakifanya kazi.

149. Catherine Marshall, *Beyond Our Selves* (New York: McGraw Hill Book Company, 1961), 24–25.

Katika ulimwengu wetu wenye matatizo, unaoonekana kutoweza kudhibitiwa, Baba amekuwa akifanya kazi hadi leo hii. Mwana amekuwa akifanya kazi. Na katika maisha yako mwenyewe, Baba na Mwana wanafanya kazi.

**OKTOBA 13** **286**

# Rudi Kutokea Nyuma

*Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu. Pande zote twateseka, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; siku zote twabeba katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu.*
*2 Wakorintho 4:7-10*

Patrick Mahomes na Wakuu wa Jiji la Kansas walifanya hivyo tena. Kwa mechi ya tatu mfululizo, walijizatiti kutoka kuwa nyuma kwa pointi kumi au zaidi na mwishowe wakashinda. Walishinda Super Bowl ya 2020 huko Miami kwa miguso mitatu katika dakika nane za mwisho-alama ya mwisho ilikuwa 31-20. Inafurahisha kuona timu yako ikirudi kutoka nyuma na kutwaa ushindi!

Kwa njia yenye maana zaidi, wewe ni mpokeaji wa ahadi ya Yesu ya kurudi ukitokea nyuma na ukashinda. Kumbuka kwamba unaweka hazina yako ya kiroho katika mtungi wa udongo wa kawaida—"kitungi cha udongo," katika fasiri nyinginezo. Ni vyema kukumbuka kwamba neema ya ajabu ya Mungu inakubali kwamba tumefungwa katika miili ya kibinadamu. Lakini mapungufu yetu yanatupa nafasi zaidi ya kukoleza nguvu za Mungu.

Kumbuka kwamba mtume Paulo mkuu, mcha Mungu, mwenye nguvu za kiroho anakiri mipaka yake mwenyewe: amekuwa mlemavu, amechanganyikiwa, ameteswa, hata kuangushwa chini. Lakini kila kikwazo kinafuatwa na kurudi tena—licha ya hayo yote, hatuchanganyikiwi, hatukati tamaa, hatujatolewa kamwe. Ndiyo, nguvu ya maisha ya Yesu inatiririka kupitia kwako. Yohana alisema hivi: "Aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika ulimwengu" (1 Yohana 4:4).

Kwa hiyo shinikizo lolote ambalo unaweza kuwa unapitia leo—matatizo ya afya, changamoto za kifedha, migogoro ya mahusiano, maombi

yasiyojibiwa, ukosoaji, upinzani, uchovu, kuvunjika moyo, hujaza nafasi iliyo wazi—kumbuka mwisho wa ujumbe wa Paulo. Daima kuna majibu, jibu, Jibu linalosababisha kujirudi tena. Kama vile Yohana anavyoandika, "Yeye [Kristo] aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye [Shetani] aliye katika ulimwengu" (1 Yohana 4:4, KJV).

Baadaye katika barua yake ya pili kwa Wakorintho, Paulo anakazia ukweli huu: "Chemchemi ya matendo yetu ni upendo wa Kristo… Ulinzi wetu pekee, silaha yetu pekee, ni maisha ya uadilifu… Kamwe hatuko mbali na kifo, lakini hapa tuko hai, siku zote 'tukiyapitia' lakini 'hatuzami" (2 Wakorintho 5:14; 6:7, 9, FILIPI).

**OKTOBA 14** **287**

# Endelea Kutembea na Roho

*Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake.Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho.*
*Wagalatia 5:24-25*

Ushuhuda wa wazi wa Dkt. David unaonyesha hitaji la kuendelea kuishi katika utimilifu wa Roho Mtakatifu. Unasisitiza umuhimu wa kufanywa upya kiroho wakati wowote tunapopotea kutoka kwa ahadi hiyo inayoendelea na maisha katika Roho.

Wakati wake katika chuo kikuu, David alimkubali Yesu moyoni mwake, akaanza kwenda kanisani, na akaomba Mungu amwongoze kwa mwanamke mzuri wa Kikristo. Sasa, kwa zaidi ya miaka ishirini na minne, mke wake, Fay, amekuwa furaha ya maisha yake.

Dk. David anaeleza kilichofuatia:

> *Nilihangaika kiroho kwa miaka ishirini. Nimefundisha shule ya Jumapili kwa miaka kumi iliyopita na nimekuwa kwenye bodi ya kanisa mara kadhaa tofauti katika miaka kumi na mitano iliyopita. Nilifahamu tu kazi ya kwanza ya neema hadi miaka saba iliyopita, nilipojazwa na Roho Mtakatifu. Biashara yangu ilikaribia kuanguka, na nilichoka kimwili na kihisia. Hatimaye nilipiga magoti mbele ya Mungu na kukabidhi kila kitu kwake. Kuna kitu kilitokea siku hiyo ambacho huenda nisiweze kabisa kukieleza. Nilikuwa siku zote nikihisi kwamba nilipaswa kupata kibali na upendo wa Mungu. Sikuwa mzuri vya kutosha, ingawa nilikuwa nimesoma*

*Biblia mara kadhaa na hata kufundisha darasa la shule ya Jumapili. Nilihisi Mungu akinikumbatia siku hiyo, na nilihisi upendo tofauti na niliowahi kuhisi. Ndani ya miezi kadhaa, nilikuwa nimewaongoza watu kadhaa kwa Bwana.*

Lakini mapambano ya kiroho yalifuata. Dkt. David anaendelea:

*Nilikuwa na shughuli nyingi sana, na nilijua maisha yangu ya maombi yalikuwa magumu. Kidogo kidogo nilipanda tena kwenye kiti cha enzi. Hakuna mtu hata mmoja ambaye ameokolewa kwa karibu miaka miwili. Miezi miwili iliyopita, nilipata nimonia na nilikuwa mgonjwa sana. Vipimo vyangu ya damu vilifanana na vile vya lymphoma. Mungu alikuwa akiyashika makini yangu.*

Na hivi majuzi zaidi, Dkt. David anasema:

*Hili linanileta kwa usasa. Baada ya kusikiliza jumbe zako, nilijua nilitaka Mungu arudi kuyatawala maisha yangu. Niliomba Jumapili usiku baada ya ibada. Nilikuwa na usingizi mzuri zaidi wa usiku kabla ya kufanya upasuaji ambao nimekuwa nikifanyiwa tangu nilipotakaswa. Nilikuwa na saa kumi na mbili za upasuaji kwenye ratiba yangu siku iliyofuata. Nakumbuka nilimwomba Mungu anisaidie hasa kupata kitu. Nilipoangalia kwa mkono wa C, nilikuwa katika nafasi nzuri ingawa sikuweza kuiona kwa macho yangu. Nilihisi Mungu akielekeza mikono yangu kama alivyofanya nilipomfuata kwa karibu hapo awali.*

Hakuna kitu duniani kinacholingana na kutembea karibu na Bwana na kufanya mapenzi yake katika kuwarudisha nyumbani watenda-dhambi waliopotea.[150]

Chukua muda wako kuyapitia maisha yako na Bwana. Ikiwa unahitaji kutafuta kufanywa upya na Roho Mtakatifu, fanya hivyo.

**OKTOBA 15** **288**

# Mlinikusudia Mabaya, Bali Mungu . . .

*Nanyi kweli mlinikusudia mabaya, bali Mungu aliyakusudia kuwa mema, ili itokee kuokoa taifa kubwa, kama ilivyo leo.*
*Mwanzo 50:20*

150. Awali yalichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Disemba 2007).

Bila shaka, Yusufu alikuwa shujaa! Alikuwa akiwakera ndugu zake kumi na mmoja na baba yake. Lakini pia hakuna shaka kwamba suluhisho la ndugu zake kwa hasira yao lilikuwa baya sana. Israeli baba yao alipomtuma Yusufu kwenda kuwaangalia ndugu zake mifugo yao ya malishoni, ndugu hao walimkamata, wakamtupa shimoni, na kumuuza kwa wafanyabiashara Wamidiani. Wafanyabiashara kwa upande wao wakamuuza Yusufu kwa Mmisri aitwaye Potifa, mkuu wa walinzi chini ya Farao.

Ingawa Potifa alimwamini mwanzoni, Yusufu alituhumiwa kwa utovu wa nidhamu, kisha kufungwa gerezani pasipo haki. Hata hivyo, kama Maandiko yanavyotuambia, "Yusufu alipokuwa gerezani, BWANA alikuwa pamoja naye" (Mwanzo 39:20–21).

Hata alipokuwa gerezani, Yusufu ndiye pekee aliyeweza kufasiri ndoto za Farao. Baadaye Farao alimtoa gerezani na kumteua kuwa waziri mkuu. Katika wadhifa huu, Yusufu aliweka nafaka za ziada wakati wa shibe na kuitayarisha nchi kwa msimu wa njaa.

Njaa ilipokuja, ilifika kwa baba yake Israeli na ndugu zake kumi na mmoja. Ndugu hao walikuja kwa Yusufu, waziri mkuu anayesimamia ugawaji wa chakula, akitafuta msaada. Kadiri muda ulivyopita hawakumtambua. Hatimaye walipotambua ni nani waliokuwa wakizungumza naye, walimwomba awahurumie na hata wakajitolea kuwa watumwa wake. Kisha Yusufu akasema, "Mlikusudia kunidhuru, lakini Mungu alikusudia... kuokoa maisha ya watu wengi" (Mwanzo 50:20). Yusufu aliwasamehe ndugu zake na kuwaandalia mahitaji yao ya kimwili.

Tangu siku za Mwanzo hadi sasa, Mungu bado ana njia ya kubadilisha uovu wa wengine kuwa wema kwa wale wanaomfuata. Niliiona katika uchungaji wangu wa kwanza. Kanisa dogo linalojitegemea ambalo lilikuwa limeanzishwa awali majuma matano liliniomba niwe kasisi wake. Mfanyabiashara wa huko alikuwa amekusanya kikundi hicho, na wakakutana katika kibanda chake cha farasi kilichofanyiwa marekebisho. Mfanyabiashara wa huko alikubali kwamba tungeweza kuliendeleza tukiwa Kanisa la Nazarene, nasi tukamlipa kodi ya kawaida sana. Mara tu kanisa lilipoanzishwa na mimi na mke wangu tukiwa tumejitolea sana, mfanyabiashara huyo alituambia ghafla kwamba lazima tununue eneo hilo—kanisa, nyumba mbili, jengo dogo la shule ya Jumapili, na ekari nne—katika muda mfupi. Vinginevyo, angewauzia dhehebu jingine. Wakati huohuo, tuligundua kwamba kila mtu ambaye alikuwa amekusanyika ili kuhudhuria kanisani alikuwa anadaiwa na mfanyabiashara huyo. Si vizuri!

Tulikuwa na watu wapatao arobaini katika kusanyiko wakati huo. Halmashauri yetu ya kanisa ilikusanyika kujadili ofa hiyo (au tishio). Mjumbe mmoja wa bodi alisema, "Nadhani alituhusisha hapa tu ili auze nyumba yake."

Nilikuwa na uhakika kwamba Mungu alikuwa ametuongoza kuchunga kanisa kiasi kwamba nilijibu, “Huenda umesema kweli. Huenda alikusudia mabaya, lakini Mungu aliyakusudia kuwa mema.” Tuliafikiana kununua nyumba hiyo.

Baada ya hapo, kanisa lilikua, tukajenga eneo takatifu zuri na kitengo cha mafunzo kwenye ekari hiyo, na tuliona watu wengi wakimpata Kristo. Kutokea katika kanisa hilo alikuja kuwepo kasisi mashuhuri wa gereza; mwimbaji ambaye alikuja kuwa sehemu ya kikundi cha injili kinachosafiri; mwanamke aliyejipatia sifa za utumishi; mchungaji wa kanisa la chuo; msimamizi wa wilaya; watu mashuhuri, walei; na wengine wengi.

Itakuwa hivyo pia wewe ambaye umejitolea yote kwa Yesu na unaishi maisha ya kujazwa na Roho na kuongozwa na Roho: watu wanaweza kukusudia kukudhuru, lakini Mungu anakukusudia kwa wema. Tunaweza hata kuokoa maisha mengi kupitia hilo. Mungu wa ajabu!

**OKTOBA16** **289**

## Hawakutaka Shauri Kinywani mwa Bwana

*Basi wakuu hao wakatwaa katika vyakula vyao, wala wasitake shauri kinywani mwa BWANA.*
*Yoshua 9:14*

Wanajeshi wa Israeli walikuwa wanawachokoza wapinzani. Mungu aliwaongoza kwenye ushindi huko Yeriko, ambako kuta zilianguka. Baada ya kushughulika na kutotii huko Ai, Israeli walifanya shambulizi la pili kwa mwongozo wa kimungu, na kupata ushindi mkubwa.

Habari za mafanikio ya kijeshi ya Israeli zilipoenea, raia wa Gibeoni wa karibu waliamua kwamba lazima wafanye udanganyifu ili kujilinda. Walituma wajumbe kwenda Israeli ambao punda wao walikuwa wamebebeshwa magunia yaliyochakaa na ambao watu wao walivaa viatu vilivyotiwa viraka na nguo kuukuu. Mkate wao ulikuwa mkavu na wenye ukungu. Walijifanya kuwa wametoka nchi ya mbali, na wakaomba mapatano ya amani.

Kama Maandiko yasemavyo, “Waisraeli waliiga vyakula vyao, lakini hawakuuliza kutoka kwa BWANA.” Badala yake, walikubali hadithi ya wajumbe na kufanya nao mapatano ya amani. Siku tatu baadaye, waligundua

kuwa walikuwa wamedanganywa. Matatizo makubwa yalifuata—Yoshua 9 inakuelezea zaidi.

Kwa sisi tunaomfuata Bwana leo, ni muhimu kumwuliza Bwana kuhusu maamuzi makuu ya maisha. Haya ni pamoja na:

- Ni aina gani ya elimu utakayopokea
- Kama kuwa mseja au ni nani wa kuoa
- Mahali pa kuishi
- Ni aina gani ya kazi au kazi utakayofuatilia
- Utahudhuria kanisa gani

Kuna njia tano za kujua mapenzi ya Mungu:

- Neno la Mungu (Biblia)
- Uongozi wa Roho katika maombi
- Milango iliyofunguliwa na kufungwa
- Ushauri wa marafiki Wakristo wakomavu
- Sababu takatifu

Israeli walifikiri mazingira (mlango wazi) yalithibitisha kwamba Gibeoni ilikuwa mbali, kwa hiyo walifanya uamuzi wa kuandaa mapatano ya amani. Laiti wangemwomba Bwana kwanza.

Kathy aliniambia alimwalika mwanamke asiye na makao kuja kuishi naye, akichukulia tu kwamba lilikuwa jambo la huruma kufanya—hakuuliza mwelekeo wa Bwana. Muda si muda, ilimbidi kumwomba mwanamke huyo aondoke.

Charles aliniambia aliamua kununua nyumba ya wikendi kwenye ufuo wa bahari kwa sababu mara kwa mara alipeleka familia yake huko kwa wikendi. Hakuutafuta mwongozo wa Bwana. Matokeo yake, alitambua, mara kwa mara aliwatoa watoto wake kanisani, na sasa walikuwa mbali na Mungu.

Kwa upande mwingine, mimi na Nancy tuliona uhitaji wa kuhamia nyumba nyingine. Tulidumu kuomba kuhusu hilo. Siku moja katika maombi, nilimsikia Bwana akisema, *"Sasa ni wakati wa kuhama*." Tulifanya hivyo, na kwa njia nyingi, nyumba yetu mpya ikawa chanzo cha baraka nyingi.

Tafadhali muulize Bwana.

# Je, Unaweza Kufanya Nini Unapokuwa Na Umri Wa Miaka Themanini Na Mitano?

*Sasa basi, angalia, yeye BWANA ameniweka hai, kama alivyosema, miaka hii arubaini na mitano, tangu wakati huo BWANA alipomwambia Musa neno hilo, wakati Israeli walipokuwa wanapitia jangwani; na sasa tazama, hivi leo nimetimiza umri wa miaka themanini na mitano. Hata sasa mimi nina nguvu zangu hivi leo kama nilivyokuwa siku hiyo Musa aliyonituma; kama nguvu zangu zilivyokuwa wakati huo, na nguvu zangu ndivyo zilivyo sasa, kwa vita na kwa kwenda na kurudi. Basi sasa unipe mlima huu, ambao BWANA alinena habari zake siku hiyo; kwani wewe ulisikia siku hiyo jinsi Waanaki walivyokuwa huko, na miji ilivyokuwa mikubwa yenye boma; yumkini yeye BWANA atakuwa pamoja nami, nami nitawafukuza watoke nje, kama BWANA alivyonena.*
*Yoshua akambariki, akampa Kalebu, huyo mwana wa Yefune, Hebroni kuwa urithi wake.*
*Yoshua 14:10-13*

Umri wa miaka themanini na mitano na tayari kwenda vitani tena—Mungu alikuwa amempa Kalebu ahadi, na sasa alimsukuma Yoshua ili aweze kuidai. Naye Yoshua akampa Kalebu Hebroni kuwa urithi wake.

Miaka arobaini na mitano mapema, Kalebu na Yoshua walikuwa wapelelezi wawili pekee waaminifu kati ya kumi na wawili walipoipeleleza nchi ya ahadi. Wakati huo, watu wa Israeli walikuwa nyikani wakingoja kuingia katika nchi hiyo.

Wapelelezi kumi walirudi na kusema, “Hatuwezi kuingia katika nchi hiyo.”

Lakini Kalebu na Yoshua walisema, “Kwa Mungu, tunaweza.”

Mwishowe, Israeli waliwaamini wale kumi na kutangatanga jangwani kwa miaka arobaini. Hatimaye, wakiwa na Yoshua kama kiongozi wao mpya, walikuwa wameingia katika nchi na walikuwa wamewaondoa adui na kudai eneo kwa miaka mitano. Na sasa Kalebu, akiwa na umri wa miaka themanini na mitano, alidai ahadi nyingine na akapokea Hebroni kama urithi wake.

Dkt. Paul Rees na Dkt. Edward Lawlor wote walikuwa wakihubiri kwa nguvu walipokuwa katika miaka yao ya sabini, labda miaka yao ya themanini.

Alipokuwa karibu miaka themanini, Ernie Loganbill alichukua majuma mawili kunichongea fimbo. Amechonga vijiti kwa ajili ya watu kama Mama Teresa na Seneta Bob Dole—na yangu ilikuwa nambari 283.

Kalebu alidai ahadi na akapokea urithi wake akiwa na umri wa miaka themanini na mitano. Wewe pia unaweza kufanya vivyo hivyo uwe wewe una miaka themanini na mitano, mkubwa zaidi, au mdogo.

Nimekuwa nikifikiria baadhi ya ahadi ambazo Yesu na wafuasi wake walitoa. Hapa kuna baadhi:

- "Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33).
- "Kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa" (Mathayo 7:8).
- "Yesu akawaambia, Mimi ndimi chakula cha uzima; yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe" (Yohana 6:35)
- "Mwizi huja tu kuiba, kuua na kuharibu; mimi nilikuja ili wawe na uzima, tena wawe nao tele" (Yohana 10:10).
- "Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu" (Yohana 10:27-28).
- "Mkiniomba neno lolote kwa jina langu, nitalifanya" (Yohana 14:14).
- "Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu" (Wafilipi 4:6-7).
- "Basi, limesalia pumziko la sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika pumziko lake amepumzika mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyopumzika katika kazi zake" (Waraka kwa Waebrania 4:9-10).
- "Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe muwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. 24 Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya" (1 Wathesalonike 5:23-24).

Jana usiku saa 1:00, nilianza kuomba kwa ajili ya hitaji. Nilitaja ahadi katika jina la Yesu, kwa urahisi sana na bila kuigiza. Ilipofika saa 2:30 usiku, jibu lilikuwa mkononi mwangu. Kama Kalebu, nina umri wa miaka themanini na mitano.

Themanini na mitano, au zaidi, au mdogo—unaweza kufanya nini? Dai ahadi zako; miliki urithi wako.

# Mungu Hajajifungia

*Angalieni, mimi leo ninakwenda njia ile waendayo watu wote wa ulimwengu; nanyi nyote mnajua mioyoni mwenu, na rohoni mwenu, ya kuwa halikuwapungukia ninyi hata neno moja katika mambo hayo mema yote aliyoyanena BWANA, Mungu wenu, katika habari zenu; yote yametimia kwenu hapana neno lolote mlilopungukiwa.*
*Yoshua 23:14*

Ninapoandika haya mnamo mwaka 2020, jamii imefungwa. Kwa sababu ya janga la COVID-19, mataifa ulimwenguni kote yamefunga mabohari, viwanda, shule, maduka, viwanja vya michezo na zaidi. Lakini chochote kitakachofuata katika ulimwengu wetu, tunajua Mungu hajafungiwa.

Yoshua alikuwa mwisho wa maisha yake ya kimwili. Alikuwa amewaongoza Israeli kuvuka Yordani na kuingia katika nchi ya ahadi, na alikuwa amewaongoza katika kuiteka nchi hiyo kwa miaka ishirini na mitano hadi thelathini. Aliwakumbusha kwamba Mungu alitimiza kila ahadi aliyowapa Israeli. Kisha Yoshua akaweka bayana na kuorodhesha ushindi, ahadi zilizotimizwa:

- Alimwongoza Ibrahimu hadi Kanaani.
- Aliwatumia Musa na Haruni kuwaongoza Waisraeli kutoka Misri.
- Alifungua Bahari ya Shamu kwa ajili ya Israeli na kulizamisha jeshi la Wamisri lililokuwa likiwafuatia.
- Aliwapa Waisraeli ushindi dhidi ya wafalme wa Waamori mashariki mwa Yordani.
- Aliwavusha Israeli Yordani na kuwapa Yeriko.
- Aliwapa Waisraeli ushindi dhidi ya wakaaji wengi wa nchi.

Bwana alihitimisha: "Niliwapa nchi ambayo hamkuifanyia kazi kwa taabu, wala miji hamkuijenga" (Yoshua 24:13). Kwa maneno mengine, licha ya changamoto zote, Mungu hakufungwa.

Fikiria juu ya maisha yako kwa muda; fikiria ahadi zilizotolewa na ahadi zinazotekelezwa. Hapa kuna baadhi kutoka kwa maisha yangu, ambayo yote Mungu amehifadhi:

- "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kututakasa na udhalimu wote" (1 Yohana 1:9). Alitenda!
- "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami" (Ufunuo 3:20). Alitenda!
- "Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe muwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya" (1 Wathesalonike 5:23-24). Alitenda! Na yeye hutenda!
- "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu" (Wafilipi 4:19). Alitenda! Na yeye hutenda!
- "Hata baba yangu na mama yangu wakiniacha, Bali BWANA atanikaribisha kwake" (Zaburi 27:10). Alitenda!
- "Kwa hiyo, hebu kila akuaminiye Akuombe awapo katika dhiki. Hakika maji makuu yafurikapo, Hayatamfikia yeye" (Zaburi 32:8). Yeye hutenda!
- "Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele" (1 Wathesalonike 4:16-17). Atatenda!

Hata iweje, Mungu hajafungwa!

**OKTOBA 19** **292**

# Zawadi ya Mungu

*Naye Samweli akamwambia Sauli, Umefanya upumbavu; hukuishika amri ya BWANA, Mungu wako, aliyokuamuru; kwa maana BWANA angaliufanya ufalme wako kuwa imara juu ya Israeli milele. Lakini sasa ufalme wako hautadumu; BWANA amejitafutia mtu aupendezaye moyo*

*wake, naye BWANA amemwamuru yeye kuwa mkuu juu ya watu wake, kwa sababu wewe hukulishika neno lile BWANA alilokuamuru.*
*1 Samweli 13:13-14*

Sauli alikuwa mtu wa kipekee. Alikuwa mrefu na mwenye sura nzuri, na Mungu alimchagua na kumtia mafuta awe mfalme wa kwanza wa Israeli (9:2, 16). "Mungu akaubadili moyo wa Sauli," na "Roho ya Mungu ikaja juu yake kwa nguvu" (10:9–10). Mwanzoni, Sauli alisitasita kwa hoja kwamba, katika kutambulishwa kwake hadharani kama mfalme, alijificha kati ya vifaa (10:22). Ustadi wake wa kijeshi, akiwa amewezeshwa na Mungu, ulikuwa kiasi kwamba kampeni yake ya kwanza ilisababisha kushindwa kabisa kwa kambi ya Waamoni iliyokuwa hatari (11:11). Sauli alikuwa na miaka thelathini alipoanza kutawala, akatawala miaka arobaini na miwili (13:1).

Mungu alikuwa amempa zawadi ya ajabu—ufalme juu ya Israeli, mali iliyochaguliwa na Mungu. Hata hivyo, mahali fulani njiani, kielelezo kilianza kutokea kwa Sauli. Angefanya *sehemu* ya yale ambayo Mungu aliamuru, lakini si *yote*—kwa maneno mengine, alikuwa mtiifu kwa kiasi (13:8–10; 15:9–10). Zaidi ya yote, maisha yake yalihusu kutunza utawala wake.

Baada ya muda, Sauli akawa mtu wa kuhangaika, mwenye wivu, mwenye machungu, muuaji ambaye aliwakasirikia wale waliotaka kumtendea mema. Mwishowe, baada ya kujeruhiwa vitani, Sauli alijiua (31:4). Hatima ya kimungu ilikuwa hiii: "Hukushika amri ambayo Bwana, Mungu wako, alikuamuru" (13:13).

Ni nini kilitukia vibaya? Ingawa Mungu alikuwa amembariki Sauli kwa zawadi za kiasili—zaidi ya yote, zawadi kubwa ya kutawala Israeli—alishindwa kufuata Mithali 4:23: "Linda moyo wako kuliko yote uyatendayo." Tatizo la Sauli lilikuwa kwamba alihamisha kipaumbele jambo moja la kwanza: Alikuja kuthamini zawadi ya Mungu kuwa kuu kuliko Mungu aliyeitoa.

Nina hakika kila mmoja wetu atakabiliwa na suala hili. Fikiria zawadi zote ambazo Mungu anaweza kukupa—afya, elimu, kazi, wapendwa, nyumba, akaunti ya benki, mali, ujuzi, ukubwa, mamlaka—na uwe mwangalifu. Linda moyo wako. Mungu ni mkuu kuliko zawadi yoyote anayokupa. Ingawa zawadi nyingi zitakuwa za muda, Mungu ni wa milele. Zingatia uhusiano wako na Mungu leo kwa kuzingatiazawadi yoyote aliyokupa.

# Amani kwa ajili ya Ukuta wa Uadui Unaotenganisha

*Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga.*
*Waefeso 2:14*

Mafarakano kati ya Wayahudi na Wamataifa ulikuwa mkubwa; kwa miaka mingi, walikuwa wamechukiana wao kwa wao. Na sasa, Yesu Kristo anajitokeza. Anaiweka kando sheria ya Wayahudi na badala yake anamleta Myahudi na Mmataifa kwake; anawafanya wote wawili kuwa waadilifu mbele za Mungu kwa kifo chake msalabani. Anawapa wote wawili njia ya kumfikia Baba kwa Roho Mtakatifu. Anaumba ubinadamu mmoja mpya kati ya hao wawili, na hatimaye, kuna amani (Waefeso 2:14–18).

Katika jamii ya leo, pia, kuna mengi ambayo huwakera watu. Kuna ukuta wa uadui unaowatenganisha. Katika jitihada ya kuonyesha jinsi ya kubomoa ukuta wa uadui kati ya watu, acheni niwaambie hadithi ya Kathy na Carolee.

Kathy alikuwa amejaribu kwa miaka mingi kumsaidia kaka yake Dave. Mara nyingi sana, alimsihi yeye na wenye mamlaka ambao wangeweza kumsaidia. Dave alikuwa mraibu wa tembe za maumivu na pombe, na alikuwa mwenye hasira na mjeuri. Ilikuwa mbaya sana kiasi kwamba Kathy alianza kulala kichwa-chini tofauti na hali yake ya kawaida kwenye kitanda chake. Akihofia kwamba kaka yake anaweza kumpiga risasi kwenye dirisha la chumba cha kulala, alisema "afadhali miguu yangu kuliko kichwa changu."

Siku moja, akiwa na hasira, Dave alimpiga jirani yake hadi kufa, akaiba bunduki, na kuelekea kwenye maduka. Alimpiga risasi na kumuua msichana mdogo kwenye gari lake na kijana katika gari lake, na hatimaye, maafisa wa polisi walimuua. Baadaye, polisi walifika nyumbani kwa Carolee na kumwambia kwamba Dave alikuwa amemuua binti yake wa miaka thelathini na mitatu, Leslie.

Siku iliyofuata, Kathy alisimama mbele ya kanisa lake mahalia pamoja na mchungaji wake na wanafamilia kando yake ili kueleza fadhaiko na huzuni yake kwa jamii. Wakati habari za runinga za eneo husika zikipeperusha kanda hiyo kote jijini, Carolee alitazama. Ingekuwa rahisi kwa Carolee kuwa na uchungu na hasira dhidi ya Kathy kwa kile kaka yake alikuwa amemfanyia Leslie. Angeweza kusema kwa urahisi, "Sitaki kumwona, kuzungumza naye,

au kuwa na uhusiano wowote naye"—uhasama uliotengana. Lakini badala yake, Kathy aliposimama mbele ya kamera za TV siku hiyo, akizungumzia hali ya Dave na kumpa rambirambi, samahani, na majonzi, Carolee alijua kwamba alipaswa kukutana na Kathy.

Miezi mitatu baadaye, Carolee alikutana na Kathy katika ofisi ya mchungaji na akamweleza kwamba tayari alikuwa amemsamehe Dave. Wanawake hao wawili walikumbatiana. Baadaye, walikwenda pamoja kwenye eneo la mauaji. Hapo, walikumbatiana, wakalia, na kueleza na kupokea msamaha.

Mungu alianza kuushughulikia msiba huo. Punde, Kathy na Carolee walikuwa wakisimulia hadithi yao pamoja kwenye habari za TV na vikundi vya kanisa. Kathy alianza kusoma na kuongoza vikundi katika kupona dhidi ya huzuni. Wote wawili walikuwa na nakala zilizochapishwa katika C*hicken Soup for the Soul*.

Carolee alisema, "Ingawa moyo wangu ulivunjika, nina marafiki wapya, urafiki wa zamani ni wa kina zaidi, nimekuwa mwenye upendo na kujali zaidi, familia yangu ina uhusiano mkubwa zaidi, na nimekua katika uhusiano wangu na Mungu."

Ikiwa ungetembelea darasa lao la shule ya Jumapili, ungewaona Kathy na Carolee wakiwa wameketi kando kama marafiki wa dhati. Haya yote yanawezekana kwa sababu wanawake wote wawili wana uhusiano na Yesu Kristo—yeye ndiye amani yao, anaharibu ukuta wowote wa uhasama na kuwaleta wawili hao pamoja. Anaweza kufanya hivi katika ulimwengu wako pia.

**OKTOBA 21** **294**

# Upendo wa Mungu Unaweza Kupotezwa

*Akawaambia, Sasa tekeni, mkampelekee mkuu wa sherehe. Wakapeleka.*
*Yohana 2:8*

Je, unaweza kuwachukulia watu kuwa bidhaa yetu ya thamani zaidi; mali yetu muhimu zaidi; hazina yetu ya thamani zaidi? Ikiwa ndivyo, kwa nini wajitengenezee maisha yasiyo na maana kwa kutumia dawa za kulevya na pombe, wakibadilisha haki yao ya mzaliwa wa kwanza kwa upotovu wa kitunguu au dhambi iliyopakwa sukari? Sisi ni wa thamani sana kuishi bila

kupata kusudi letu la kuwa hapa; sisi ni wa thamani sana kuishi chini ya kiwango alichokusudia Mungu.

Kwa miaka mingi, nilibeba mizigo tangu utotoni ambao ulinifanya nisionekane. Niliishi maisha yangu kupitia familia yangu hadi maumivu kutokana na ndoto zilizovunjika yalipodai kwamba nitumie muda kushughulikia maisha yangu ya zamani. Uponyaji katika mwili wa Kristo uliniruhusu kuwa mwaminifu; na katika usalama huo, nilifungua majeraha ili kuruhusu mwanga na upendo kufanya kovu la kupendeza. Nilibadilisha sanamu ya aibu na hofu kwa uhusiano na Mungu halisi, ambaye hunipa ujasiri, ushujaa, kujiamini, na uaminifu wa kuwa mimi mwenyewe na kumtumikia popote nilipo.

Usiogope kubadilisha sanamu yako isiyo na thamani kwa kitu halisi.

Nancy Shaver[151]

## OKTOBA 22 — 295

# Mtumainie Bwana

*Kwa ajili ya hayo BWANA atangoja, ili awaonee huruma, na kwa ajili ya hayo atatukuzwa, ili awarehemu; kwa maana BWANA ni Mungu wa hukumu; heri wote wamngojao.*
*Isaya 30:18*

*Wakati alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kutoka kwangu;ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache.*
*Matendo 1:4-5*

Nataka ujue ninakaza kwa ajili yako. Sasa umesoma masomo mengi ya ibada binafsi kuhusu utakaso na kujazwa kwa Roho Mtakatifu. Pengine umekuwa ukimwomba Mungu afanye kazi hii ya neema ndani yako lakini bado huna uhakika alionao. Ninawasihi mtumainie Bwana. Wanafunzi wa kwanza waliomba kwa muda wa siku arobaini katika maombi mazito (Matendo 1:14; 2:1) hadi walipojazwa na Roho (2:4).

151. Awali yalichapishwa katika *Come Ye Apart* Julai–Agosti–Septemba1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 94. Imetumiwa kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

Dkt. Wes Tracy aliandika kuhusu umuhimu wa kutumia muda muhimu mbele za Bwana unapomngoja akujibu maombi haya. Hapa kuna maoni yake kadhaa:

- Kuna mengi ya kufanya ili kuutayarisha moyo wa mwongofu kwa ajili ya utakaso. Kwanza, hata mwongofu mwenye kushangilia kwa kawaida hana taswira sahihi ya jinsi dhambi ilivyo katika utu wake
- Wakati kati ya uongofu na utakaso, Mungu kwa uaminifu anafunua hitaji la mtu la neema ya utakaso na kuunda moyoni hamu ya Kristo. Hili linachukua muda. Wakati wa uamsho wa Wesley kiasi cha kawaida cha muda ambacho mwongofu alitumia kutafuta neema ya utakaso ilikuwa miaka mitano. Wale Wawesley wa mapema wanatoa kielelezo muhimu. Walikuwa *wepesi kutafuta* neema ya utakaso lakini *wagumu kuikiri*.
- Wesley aliwafundisha "wasifadhaike," "wasichukie," wala "kunung'unika dhidi ya Mungu kwa sababu bado hamjatakaswa," wala mtu hapaswi kutumia wakati "kujitesa bila faida kwa sababu wakati haujafika kikamili." Badala yake, Wesley aliwashauri "waingojee kwa utulivu na kwa utulivu, wakijua kwamba itakuja."

Utafutaji wangu wa utakaso kamili ulichukua muda. Kuongoka kwangu kulikuwa wazi, na siku zangu za mapema za Ukristo zilionyesha uthibitisho wa maisha yaliyobadilika. Lakini karibu miezi mitano katika maisha yangu ya Kikristo, nilianza kuhisi hasira mbaya zikitoka chini ya sakafu ya nafsi yangu. Nilijifunza kwa kina kuhusu maisha ya Kikristo yanayoitwa utakaso. Nilianza kumtafuta Mungu kila siku kwa ajili ya baraka hiyo. Baada ya miezi mitano, Mungu alijibu. Mungu alikuwa akitumia muda huo kuchunguza viwango vya ndani vya moyo wangu na kunitayarisha kwa ajili ya kumpokea Roho kikamilifu. Kwa hivyo moyo wangu unaungana nawe katika kungoja na kutafuta. Kama vile Wesley alivyosema, "Atazungumza mara ya pili, 'Uwe safi.'" [152]

152. Habari zimetoka kwa Wesley Tracy, "Entire Sanctification and Uncertain Trumpets," *Herald of Holiness* Octoba 1990 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 6–7. Imetumiwa kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Holiness Today*.)

# Ushuhuda wa Dkt. Bresee

*Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango.*
*Waraka kwa Waebrania 13:12*

Dk. Phineas Bresee anachukuliwa kuwa mwanzilishi wa Kanisa la Nazarene. Mnamo 1884, alishangazwa na kazi ya Roho Mtakatifu. Alielezea yaliyotokea kwa maneno yake mwenyewe:

> *Ulisikika kama moto kwenye midomo yangu, na hisia inayowaka haikuwaacha kwa siku kadhaa. Ingawa haya yote yenyewe yasingekuwa chochote, yalikuja nayo moyoni mwangu na kuwa, hali iliyobadilishwa ya maisha na baraka na upako na utukufu, ambayo sikuwahi kujua hapo awali. Nilihisi kwamba hitaji langu lilitolewa. Siku zote nilikuwa kimya sana nikirejelea uzoefu wangu wa kibinafsi. Sijawahi kujisahaulisha, na nimewaeleza jamaa wachache sana kwa hili; lakini kulikuja katika huduma yangu kipengele kipya cha maisha ya kiroho na nguvu. Watu walianza kupokea baraka ya wokovu kamili; kukawa na watu zaidi walioongoka; na mwaka wa mwisho wa huduma yangu katika kanisa hilo ulikuwa wa fanaka zaidi, nikiwa nimetawazwa na ufufuo wa karibu kila mara. Wakati mwaka wa tatu ulipofika mwisho, kanisa lilikuwa limeongezeka karibu maradufu, na kuimarika.*

Dkt. William Greathouse, katika kitabu chake bora kabisa cha *Wholeness in Christ*, akimnukuu John Wesley:

> *"Lakini ni imani gani ambayo kwayo tunatakaswa... Kwa uhakika huu, kwamba Mungu anaweza na yuko tayari kututakasa sasa, panahitajika kuongezwa jambo moja zaidi, uthibitisho wa kimungu na usadikisho kwamba anafanya hivyo... Ukitafuta kwa imani, unaweza kutarajia jinsi ulivyo; na kama ulivyo, basi tarajia sasa! Itarajie kwa imani, itarajie jinsi ulivyo, na itarajie sasa!*
>
> *Jiunge na wale wanaoombea ukweli huu wa utakatifu kuusafisha ulimwengu wetu!*[153]

153. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Disemba 2008).

# Vita vya Kiroho

*Kwa maana mwili hutamani yale yaliyo kinyume cha Roho, na Roho hutamani kushindana na mwili. Wanagombana wao kwa wao, ili usifanye chochote unachotaka. Wagalatia 5:17*[154]

Ni tabu iliyoje! Ikiwa uko tayari kumfuata Yesu Kristo nusu, pambano hili linapaswa kuvunja nafsi yako. Maneno yaliyo hapo juu yaliandikwa kwa Wakristo wa Galatia, lakini wengi leo ambao ni wa Yesu Kristo bado wanapitia vita kati ya Roho Mtakatifu na kubaki ubinafsi.

Katika barua yake kwa Wakristo wa Efeso, Paulo anathibitisha kwamba walikuwa *wakiishi* katika makosa na dhambi, lakini sasa wameokolewa dhidi ya mtindo huo wa maisha kwa neema ya Yesu Kristo (2:1–2, 5). Lakini anaacha kidokezo. Nyuma ya utume wa dhambi, kuna nguvu ya ndani inayochochea matendo hayo: "kuzitimiza tamaa za mwili wetu na kuzifuata tamaa zake na mawazo yake" (Waefeso 2:3). Nyuma ya dhambi, matamanio; nyuma ya tamaa, asili ya dhambi-au kile tunaweza kuita ubinafsi.

Wagalatia walikabili suala hilohilo. Sheria haikuweza kutatua tatizo hili. Kuna kutoa na kuongeza kunakohusika:

Kutoa: "Wale walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake" (Wagalatia 5:24). "Kusulubiwa" inaonekana kama kifo.

Kuongeza: "Kwa kuwa tunaishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho" (5:25). Ni wazi huu ni uhusiano unaoendelea, lakini ili kuishi uhusiano huu, lazima uingie - ili kushiriki ndoa, lazima uwe na harusi. Na, mara tu unaposhiriki, uhusiano huo ni mzito kiasi gani: "*Endelea* katika *hatua* na Roho."

Ni kweli—kuania wakati unamkubali Kristo na kuanza kumfuata, unakuwa "umezaliwa kwa Roho" (Yohana 3:8) na una Roho Mtakatifu (Warumi 8:9). Lakini unaweza kosa "kujazwa na Roho."

Pindi unapoingia kwenye sebule yako na kuwasha swichi ya mwanga, mwanga husambaa kwa kawaida kila kona ya chumba. Sio lazima kusimama

154 It Mei be helpful to know that the 1984 version of the NIV used the term "sinful nature" instead of "flesh."

kwenye kiti, kufikia balbu zako, na kuelekeza mwanga kwenye sakafu na sehemu za mwisho wa chumba.

Hata hivyo, ukaguzi wa makini wa chumba hutambua vivuli-samani huzuia miale ya mwanga. Ili mwanga *ujaze* chumba, itabidi usogeze samani nje kama katika kusafisha kwa makini. Kwa hivyo, si jambo la kushangaza kwamba katika ulimwengu wa kiroho, ili ujazwe na Roho na kutembea katika Roho, asili ya dhambi lazima kwanza isulubishwe.

David alikuwa akihudhuria kanisa lake kwa uaminifu kwa miaka kumi na mitatu. Alikuwa ameongoka, lakini alikuwa amesikia kuhusu maisha ya kina ya Kikristo yanayoitwa "utakaso." Alifikiri angeweza kufikia hatua hiyo. Mara kwa mara, alikuwa akienda mbele ya kanisa lake na kusali, lakini hakuna kilichotokea. Alihitimisha, "Hili si kwa ajili yangu."

Hata hivyo, katika kujiandaa kwa ajili ya wiki ya ibada ya uamsho, kanisa lake lilitoa changamoto ya kuwaombea wengine watano ili wapate msaada wa kiroho. Daudi aliishia kujiombea mwenyewe. Usiku mmoja wakati wa uamsho, alihisi kwamba kama asingechukua hatua hiyo usiku huo, asingeweza kamwe. Alikwenda mbele, akapiga magoti, na kutiwa nguvu ya kumtumainia Mungu apate jibu. David alisimulia, "Nilihisi amani sana. Vita vimekwisha. Muda mrefu sana, roller coaster."

Baadaye, alituma barua pepe ifuatayo kwa mchungaji wake: "Ninataka tu ujue kwamba una mshiriki mpya wa kanisa, na ni mimi."

David alianza kuomba, kusoma Biblia, na kufuata hatua kwa kuongozwa na Roho kila siku, akisema, "Kwa nini sikufanya hivi mapema?"

Kwa Wagalatia, kwa David kwa ajili yako na kwangu—vita vinaweza kushindwa kwa kusulubishwa kwa asili ya dhambi na kujazwa na kuongozwa na Roho Mtakatifu.


**OKTOBA 25** **298**

# Kipaumble cha Leo

*Ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni,*
*na vya duniani, na vya chini ya nchi.*
*Wafilipi 2:10*

*Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki.*
*Warumi 6:13*

Mpangilio sahihi wa vipaumbele vya Mkristo umejadiliwa kwa muda mrefu. Agizo moja linasema, "Mungu kwanza; mengine nafasi ya pili; mimi mwenyewe wa tatu." Mwingine anasema, "Kristo, familia, huduma ya Kikristo, kazi." Ninaamini kuna njia thabiti zaidi ya kuelewa vipaumbele vyetu vya kila siku.



Kama kitovu cha gurudumu, Kristo ndiye nguvu inayotawala shughuli zote za maisha; kila sehemu ya maisha yetu inapaswa kuwa chombo chake cha haki. Hii inaonyeshwa katika mahusiano ya familia zetu; wito au huduma yetu ya Kikristo; kazi yetu; na mengineyo. Unaposafiri kwenye barabara ya uzima, kwa wakati mmoja, familia ilizungumza juu ya gurudumu kugusa ardhi kwa sababu, wakati huo, familia yako inahitaji uangalifu zaidi. Wakati mwingine, masuala ya fedha yangezuka. Wakati mwingine, inaweza kuwa huduma ya Kikristo iliyozungumzwa au jukumu la kazi lililozungumzwa.

Acha nihusishe hili na maisha yangu mwenyewe. Nilipokuwa nikizuru nchi nzima nikiwa mwinjilisti wa muda wote, mwanangu alikuwa na matatizo shuleni. Nilipoalikwa kufundisha katika seminari yetu ya karibu, jambo moja kuu katika uamuzi wangu wa kuchukua kazi hiyo lilikuwa kumpa mwanangu umakini zaidi. Wakati huo, familia ilizungumza juu ya gurudumu ambalo lilikuwa na uangalizi maalum na matumizi kwenye barabara yangu ya maisha.

Nilipokuwa nikiandaa mradi wangu wa mwisho wa shahada yangu ya udaktari, nilijiondoa kwenye kazi yangu ya kawaida (ya kufundisha) ili kutenga muda wa kutosha kwenye mradi huo. Niliafiki makataa, na Bwana alizungumza nami, akisema, *"Hili litachapishwa."* Kwa hakika, mradi huo

ukawa wa *Kuishi katika Nguvu za Roho*, ambao nao ulisababisha *Mafunzo ya Msingi ya Biblia ya Maisha yaliyojazwa na Roho na Kutakaswa*.

Nilipokuwa mchungaji, wenzi wa ndoa walioitwa Roy na Nora walikuwa watendaji katika kanisa letu. Nora alikuwa amekatwa miguu yake yote miwili na bado alikuwa amelazwa hospitalini. Ilikuwa asubuhi ya Krismasi, na watoto wetu watatu walikuwa na hamu ya kufungua zawadi. Lakini nilipigiwa simu na kufahamishwa kwamba Roy alikuwa amepata mshtuko mkubwa wa moyo na alikuwa katika hospitali moja na Nora. Niliwaomba watoto wangu wasubiri kwa saa chache kupata zawadi za Krismasi ili niwape faraja wanandoa hawa waliokata tamaa. Wakati huo, huduma ya Kikristo, ikawa ndiyo kipaumbele .

Hivi majuzi, baada ya miaka arobaini na mitano ya kufundisha darasa langu pendwa la shule ya Jumapili, ilibidi nirudi nyuma ili niweke mkazo zaidi kukamilisha kitabu hiki cha ibada (kazi ilipewa kipaumbele) na kutoa muda wa dhati zaidi kwa mke wangu, ambaye anapambana na Alzheimers (familia ilipewa kipaumbele).

Katika matukio haya yote, Kristo alikuwa kitovu cha vipaumbele hivi tofauti. Katika nyakati tofauti za maisha, kujitolea kwetu kwa Kristo kutaonyeshwa kwa mikazo tofauti. Ni maongezi gani ambayo ni kipaumbele chako leo?

**OKTOBA 26** **299**

# Kidole Gumba Kilichoharibika

*Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele.*
*Wagalatia 6:7-8*

Ngozi iliyo mwisho wa vijipicha vyangu ilikuwa imepasuka na kusalia wazi. Majira ya baridi katika Jiji la Kansas yanaweza kuwa baridi sana. Wengi wetu hupasha joto nyumba zetu kwa gesi ya kiasili, ambayo ni ya bei nafuu lakini ina athari ya kukausha hewa ya nyumba. Na bila shaka, ukavu mwingi huathiri ngozi.

Nilijaribu kutibu kidole gumba changu kilichoharibika kwa losheni nilipokuwa nyumbani na kwa glavu nilipotoka nje. Hili lilinipa nafuu kidogo,

lakini muda mwingi nilikuwa bado naumwa. Hatimaye, suala hili halikuwa kidole gumba changu tu—niligundua kwamba kila kitu kilichoguswa na gumba changu kiliathiriwa pia. Kufunga vifungo ikawa changamoto mahususi. Je, unaweza kupatisha kifungo kwenye tundu la shati bila kutumia kidole gumba?

Nilitambua kuwa shida ya kidole gumba iliunda shida kwenye vifungo. Ni kielelezo cha dhana ya kisababishi na athari. Kanuni hii pia ni kweli katika ulimwengu wa kiroho: ikiwa utaendelea kuwa na asili ya dhambi, kila tendo linalotokana na asili hiyo na kila kitu unachogusa kitaathiriwa, hata kuchafuliwa—kitasababisha hata "kuvuna uharibifu." Matendo ya asili ya dhambi yatazalisha mambo kama vile "uasherati, uchafu na ufisadi; kuabudu sanamu na uchawi; chuki, fitina, wivu, hasira, ubinafsi, misukano, mafarakano na husuda; ulevi, na mengine kama hayo" (Wagalatia 5:19–21). Kwa hivyo, ninahitimisha, ni muhimu sana kuwekwa huru dhidi ya asili ya dhambi.

**OKTOBA 27** **300**

# Ninawezaje Kuja Hekaluni?

*Yesu akajibu, akawaambia, Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha. Basi Wayahudi wakasema, Hekalu hili lilijengwa kwa muda wa miaka arubaini na sita, nawe utalisimamisha katika siku tatu? Lakini yeye alinena habari za hekalu la mwili wake. Basi alipofufuka katika wafu, wanafunzi wake wakakumbuka ya kuwa alisema hivi, wakaliamini lile andiko na lile neno alilolinena Yesu.*
*Yohana 2:19-22*

Ingawa zaidi ya watu elfu nne walihudhuria Kongamano la mwaka 1989 la Lausanne II la Uinjilishaji Ulimwenguni huko Manila, tulikuwa na mikutano mingi ya vikundi vidogo. Wakati wa mlo mmoja mdogo wa kikundi, nilimuuliza Mchina aliyekuwa karibu nami kile alichofanya. Aliniambia yeye ni mchungaji na alikuwa ametoka gerezani. Alipanga kurudi China kuhubiri na baada ya hapo, angefungwa tena. Alikuwa mtulivu sana aliponiambia hivi—vipi? Ndugu yangu Mchina alijua kwamba, hata katika selo ya gereza, bado angeweza kuabudu na kuwa na uhusiano hai na Yesu Kristo.

Maandiko ya leo yanaanza mara tu baada ya Kristo kulisafisha hekalu kwa kuwafukuza wabadili fedha. Viongozi wa Wayahudi walipompinga, Yesu

alisema, "Livunjeni hekalu hili, nami nitalijenga tena kwa siku tatu." Alikuwa akirejelea ufufuo wake, akimaanisha kwamba yeye mwenyewe angekuwa hekalu jipya la ibada.

Kwenye hatua nyingine katika kitabu hiki cha ibada binafsi, nilieleza umuhimu wa Wakristo kujumuika pamoja kwa ajili ya ibada. Nilinukuu andiko la Waebrania 10:25, linalozungumzia "kutokuacha kujumuika pamoja." Ninasimama kwa yote niliyoandika. Bado, wakati wa kuandika haya, watu wengi hawajumuiki katika umati mkubwa kwa sababu ya hatari ya kueneza COVID-19. Baadhi hushiriki ibada kwa kutazama kupitia Facebook au Zoom na wanafamilia wachache. Wengine wamefungiwa na serikali hasimu. Hata hivyo, kwa sababu wana uhusiano wa kibinafsi na Yesu Kristo, watu hao bado wanaabudu kwa njia ya kweli.

Hekalu la kale limekwisha; Kristo sasa ndiye hekalu letu la ibada. Hata wakati hatuwezi kwenda kwenye jengo, bado tunaweza kwenda kwenye hekalu, Yesu Kristo. Wakati Yesu alipokufa msalabani, pazia la eneo takatifu zaidi hekaluni lilipasuka kutoka juu hadi chini, kwa nguvu kuashiria kwamba sasa tuna uwezo kamili wa kumfikia Mungu mtakatifu na utakaso kamili dhidi ya dhambi zote (Mathayo 27:51). Yeye ndiye tunayemwomba msamaha wa dhambi zetu; yeye ndiye uhusiano kati ya mbingu na dunia. Mafarisayo walipomlaumu Yesu kwa matendo yake siku ya Sabato, alijibu, "Lakini nawaambieni, kwamba hapa yupo aliye mkuu kuliko hekalu" (Mathayo 12:6).

Katika kueleza kuhusu Jiji Takatifu, Yerusalemu, likishuka kutoka mbinguni, Yohana aliripoti, "Sikuona hekalu ndani ya jiji hilo, kwa sababu Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo ndio hekalu lake" (Ufunuo 21:22). Mwana-Kondoo ni Kristo.

Uhusiano huu wa sasa wa kibinafsi na hekalu letu, Yesu Kristo, unawezeshwa na huduma ya Roho Mtakatifu. Yesu alieleza haya kwa wanafunzi wake hivi: "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari. Na yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo nilisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo yangu, na kuwapasheni habari" (Yohana 16:13-15).

Mchungaji Chen, mzungumzaji mkuu katika Kongamano la Lausanne, alikuwa amekaa miaka kumi na minane katika kambi za magereza za Wachina. Hata hivyo, kama mwinjilisti, anaendelea kurudi nyuma. Katika miaka hiyo kumi na minane, askari wa magereza walifanya kila wawezacho kumdhalilisha na kumsumbua Mchungaji Chen. Walimpa kazi ya kusafisha

kinyesi cha gerezani. Kwa kawaida, walinzi hawakupenda Mchungaji Chen awe peke yake, lakini alipokuwa akifanya kazi kwenye bwawa la maji taka, walinzi hawakutaka kuwa karibu naye. Kisha Mchungaji Chen angeweza kuomba kwa sauti, kuimba, na kunukuu Maandiko bila bughudha. Mchungaji Chen alisema, "Nilitazamia kwa hamu wakati wangu katika shimo la uchafu wa binadamu. Ningeweza kuimba wimbo ninaoupenda." Haya hapa ni baadhi ya maneno kutoka katika wimbo Mchungaji Chen alipenda kuimba alipokuwa akisafisha bwawa la maji:

> Ninakuja kwenye bustani peke yangu,
> Wakati umande bado upo kwenye maua;
> Na sauti naisikia,
> Ikianguka kwenye sikio langu,
> Mwana wa Mungu anafichua.
> Na anatembea nami,
> Na anatembea nami,
> Na ananiambia mimi ni wake.
> Na furaha tunayoshiriki tunapokaa hapo,
> Hakuna mwingine aliyewahi kujua. [155]

Yote yanawezekana kwa sababu Yesu Kristo ndiye hekalu letu la kweli—kimbilio letu ambamo tunaweza kumwabudu Mungu mweza yote.

**OCTOBER 28** **301**

# Ugavi wa Chakula: Wanaume Waliojaa Roho

*Hata siku zile wanafunzi walipokuwa wakiongezeka hesabu yao, palikuwa na manung›uniko ya Wayahudi wa Kigiriki juu ya Waebrania kwa sababu wajane wao walisahauliwa katika huduma ya kila siku. Wale Kumi na Wawili wakawaita jamii ya wanafunzi, wakasema, Haipendezi sisi kuliacha neno la Mungu na kuhudumu mezani. Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili; na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno.*
*Matendo 6:1-4*

155. C. Austin Miles, "In the Garden," 1912, *Sing to the Lord: Hymnal* (Kansas City, MO: Lillenas Publishing Company, 1993), #606.

Wajane katika kanisa walihitaji chakula—hata hivyo, wahubiri hawakuweza kufanya kila kitu. Badala yake, waliamua kuchagua walei saba kupanga, kusimamia, na kutoa chakula. Kanisa lilikuwa limekua tangu ujio wa Roho kwenye Pentekoste miaka mitano iliyopita—walihesabiwa katika maelfu kuzunguka Yerusalemu. Walikuwa na wengi ambao walikuwa wamemkubali Mwokozi na kuzaliwa kwa Roho, lakini wale waliowachagua kwa ajili ya kazi hii walipaswa kuwa watu wa nguvu za kipekee za kiroho. Mitume waliagiza kanisa kuchagua wale tu "wanaojulikana kuwa wamejaa Roho na hekima" (Matendo 6:3).

Alipokuwa na umri wa miaka kumi na tisa, Robert Nicholas alihama kutoka Ontario, Kanada, kutafuta kazi huko Chicago. Alikuwa amejifunza kufanya bidii kwenye shamba la familia yake huko Kanada, na alikuwa amejifunza njia ya wokovu kutoka kwa Kanisa la Methodisti. Alipofika Chicago, alianza kufanya kazi katika duka la vifaa vya ndani na kutoa zaka kwa uaminifu juu ya mshahara wake wa kila wiki. Punde, akawa mtendaji katika shule ya Jumapili na uinjilisti katika kanisa la Methodisti alilohudhuria. Alipata marafiki wapya. Mwanamke mmoja mbichi mrembo akawa mke wake.

Ndani ya miaka mitano, Robert alikuwa ameanzisha biashara yake ya vifaa vya ujenzi karibu na Oak Park. Alijenga duka lake katika mojawapo ya biashara kubwa zaidi ya vifaa, samani za nyumba, na vifaa vya umeme huko Illinois. Alikuwa na ushawishi mkubwa katika kukuza biashara ya wilaya ya Lake Marion, ambayo hatimaye ikawa kituo cha biashara cha jiji hilo.

Lakini moyo wa Robert haukuridhika. Ingawa biashara yake ilikuwa ikiongezeka na alikuwa na furaha na mke wake na watoto watatu wachanga, bado alihisi kana kwamba kuna kitu kilikosekana. Siku moja, alipokea habari kutoka kwa dada yake huko Saskatchewan kwamba alimhitaji. Robert alipokuwa akimtembelea, aliendesha gari kuvuka tambarare ili kumtembelea mwanafamilia mwingine. Akiwa anaendesha, upepo ulizidi kuwa mkali kiasi kwamba aligeuza gari lake na kurudi nyumbani kwa dada yake. Robert alipofika nyumbani kwa dada yake, alimtambulisha kwa mwinjilisti ambaye alikuja kwa ziara fupi na alikuwa akifanya ibada za mahali hapo.

Mwinjilisti akamuuliza, "Bw. Nicholas, umetoa maisha yako kabisa kwa Mungu?"[156]

Mara moja, Robert alianguka kwa magotini na kuomba kuwekwa wakfu kabisa kwa Bwana. Alimuahidi mwinjilisti kwamba angehudhuria ibada ya jioni.

---

156. V. Raymond Edman, *They Found the Secret* (Grand Rapids: Zondervan, 1960), 101.

Wito wa madhabahu ulipotolewa, Robert Nicholas alikwenda mbele. Baadaye alishuhudia: *Nilitoa maisha yangu yote kwa Mungu. Hatimaye nilipokuwa nikiomba, nilianza kumsifu Mungu; ndipo Roho Mtakatifu akajaza moyo wangu hadi sikuweza kuizuia furaha hiyo... Niliinuka kutoka kwenye madhabahu ya maombi nikiwa mtu mpya, na maisha yangu, licha ya kushindwa na mapungufu yangu, hayajawahi kuwa kama awali tangu mkutano huo na Mungu. Kwa miaka mingi kumekuwa na shinikizo kubwa sana la biashara na wajibu mkubwa katika jumuiya na kanisa, na misukumo hii hii inaweza kuwa ilinielekeza mbali na Mwokozi lakini kwa ukweli kwamba daima kulikuwa na ujuzi wa Roho anayekaa ndani yake ambaye alikuwa amekuja kukaa moyoni mwangu.* [157]

Robert alipofika nyumbani, mke wake alikuwa chumbani akifua nguo. Mara tu aliposhuka kwenye ngazi, alijua jambo fulani lilikuwa tofauti—maneno yake ya kwanza kwake yalikuwa, “Rob, ni nini kimekupata?” [158]

Alishuhudia na kulia, na yeye na mke wake walipiga magoti pamoja, na yeye akasalimisha yote kwa Yesu na pia akajazwa na Roho.

Baadaye, Robert Nicholas aliuza duka lake la vifaa vya ujenzi. Kwa miaka kumi, alikuwa rais wa chama cha ujenzi na mikopo. Kisha akawa mdhamini wa Chuo cha Biblia cha Moody na Chuo cha Wheaton, alihudumia kanisa lake, na akachangia biashara huko Oak Park.

Alikuwa mtu kama watu walioelezewa katika 1 Wathesalonike 3:10: “usiku na mchana tunapoomba kwa juhudi tupate kuwaona nyuso zenu, na kuurekebisha upungufu wa imani yenu?” Lakini baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu, akawa kama watu walioelezwa katika 2 Timotheo 2:21: “Basi ikiwa mtu amejitakasa kwa kujitenga na hao, atakuwa chombo cha kupata heshima, kilichosafishwa, kimfaacho Bwana, kimetengenezwa kwa kila kazi iliyo njema.”

Kwa nini Wakristo wengi sana hukosa shangwe hiyo na sifa nyingi? Kulingana na Robert Nicholas, “Lazima kuwe na kusalimisha Maisha kikamilifu kwa Mwokozi ili kupata ujalizo wa Roho Mtakatifu.” [159]

Ee Bwana, tunaweza kujisalimisha! Tunaweza kupata utimilifu wa Roho!

157. Edman, *They Found the Secret*, 102.
158. Edman, *They Found the Secret*, 103.
159. Edman, *They Found the Secret*, 104.

# Ninaamini

*Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na kote katika Yudea, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*
*Matendo 1:8*

Kwa miaka kumi iliyopita, Roho wa Mungu amesisitiza mara kwa mara mambo manne makuu moyoni mwangu: ushuhuda, uinjilisti, uamsho, na utakatifu. Ninaamini katika yote manne.

*Shahidi:* Ni fursa na wajibu wa kila Mkristo kushiriki na wengine kile ambacho Kristo amefanya katika maisha yao (Matendo 1:8).

*Uinjilisti:* Kwa kuwa maana ya kibiblia ya neno "injilisti" ni "kuhubiri habari njema," ni lazima tushiriki ukweli wa injili na kutafuta kuwashawishi watu kumkubali Kristo, kama Petro katika Matendo 2:38 na Paulo katika 2 Wakorintho 5:11, 20.

*Uamsho*: Kwa kuwa ni asili ya mwanadamu kuhitaji kufanywa upya katika nyanja zote za maisha (kimwili, kiakili, kijamii, na kiroho), ni wajibu wa kanisa kuendeleza uamsho—msururu wa mikutano wa injili unaowaita watu kujitolea. Zaidi ya hayo, tunapaswa kuomba kwa ajili ya uamsho ulioenea—vuguvugu kubwa la kiroho ambalo litafagia idadi kubwa ya watu katika ufalme, kama katika Matendo 4:4 na Uamsho wa Hebrides huko Scotland (1949–52).

*Utakatifu:* Kwa kuwa kuna kiwango cha ndani zaidi cha maisha ya Kikristo zaidi ya kuzaliwa upya, ni lazima tujitahidi kuwaongoza watu katika maisha yaliyojazwa na Roho na kuongozwa na Roho (Wagalatia 5:25). Maisha haya huanza na utakaso kamili (1 Wathesalonike 5:23–24; 1 Petro 1:2) na kukua katika neema hadi maisha ya utimilifu mwingi na matukio ya ajabu kwa Mungu (2 Petro 3:18).

Ninaamini! Je wewe? [160]

160. Awali yalichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Disemba 2017).

# Usikivu kwa Roho Mtakatifu

*Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho.*
*Wagalatia 5:25*

Ninapoandika maneno haya mwaka 2020, ulimwengu uko kwenye vita vikubwa dhidi ya COVID-19. Kwa majuma na miezi sasa, tumekumbushwa mara kwa mara kunawa mikono yetu, kujiweka mbali na wengine, na kuvaa barakoa hadharani.

Katika mazungumzo ya hivi karibuni na mkazi wa kituo cha kusaidiwa, aliniambia, "Hatupaswi kuondoka kwenye vyumba vyetu. Milo yote inaletwa hadi kwenye mlango wetu. Hata barua zetu zinaletwa kwetu."

Viongozi, wanasayansi, wafanyakazi wa matibabu, na watu wa kawaida wanafanya juhudi kushinda virusi hivi. Wengi wanasali na kutafuta uingiliaji kati wa Mungu mweza yote.

Hivi majuzi, nilipokuwa nikizungumza na mtu niliyemfahamu, alisema, "Tunafahamu sana kile tunachopaswa kufanya—kama vile kunawa mikono na kujiweka mbali na wengine. Je, ingekuwaje kama tungezingatia sana kuhusu Roho Mtakatifu?"

Mwanzoni nilichanganyikiwa kwa maneno yake. Lakini nilianza kufikiria yale ambayo Biblia inafundisha kuhusu Roho Mtakatifu. Roho ana kazi nyingi, lakini mojawapo kuu ni kumwakilisha Yesu. Yesu alisema, "Ajapo huyo Msaidizi, nitakayewaletea kutoka kwa Baba—Roho wa kweli atokaye kwa Baba—yeye atanishuhudia" (Yohana 15:26).

Yesu pia alisema, "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote. Hatasema peke yake; atanena tu kile anachosikia, na atawaambia yale ambayo bado yanakuja. Yeye atanitukuza mimi kwa kuwa atapokea kutoka kwangu kile atakachowajulisha ninyi" (Yohana 16:13–14).

Ona kwamba Yesu alisema Roho "atakuongoza." Agano Jipya limejaa ripoti za Roho akizungumza na, kuwaelekeza, na kuwaongoza Wakristo. Kwetu sisi, changamoto ni kuzingatia vya kutosha kusikia na kutii.

Hapa kuna baadhi ya maarifa:

- Wagalatia 5:18 "Lakini mkiongozwa na Roho, hampo chini ya sheria."

- Waefeso 4:30: "Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa mhuri hata siku ya ukombozi."
- 1 Wathesalonike 5:19: "Msimzimishe Roho."
- Warumi 8:4: "Ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho."
- Matendo 9:31: "Basi kanisa likapata raha kote katika Yudea na Galilaya na Samaria, likajengwa, likiendelea na kuongezeka katika kicho cha Bwana, na faraja ya Roho Mtakatifu."
- Matendo 20:22: "Basi sasa, angalieni, nashika njia kwenda Yerusalemu nikiwa nimefungwa rohoni, nisiyajue mambo yatakayonikuta huko"
- Matendo 8:29: "Roho akamwambia Filipo, Sogea karibu na gari hili, ukaribiane nalo."

Tafadhali kumbuka maelezo ya awali ya hali ya kiroho ya Paulo na Filipo:

- Matendo 13:9: "Lakini Sauli, ambaye ndiye Paulo, akiwa amejaa Roho Mtakatifu, akamkazia macho."
- Matendo 6:3, 5: "Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili. Neno hili likapendeza machoni pa mkutano wote; wakamchagua Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho Mtakatifu, na Filipo, na Prokoro, na..."

Ee Bwana, nijaze na Roho wako Mtakatifu. Niongoze kwa Roho wako. Nifanye nizingatie sana Roho ili kwamba nisikose maelekezo yake.

**OKTOBA 31** **304**

# Sijakasirika

*Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya.*
*1 Wakorintho 13:4-5*

Nilikutana na Lou huko Ohio aliponijia akilia baada ya semina ya Jumamosi.

"Nimekuwa nikitafuta kutakaswa kwa miaka kumi," aliniambia. Unaweza kunisaidia? Kwa hivyo nilimshauri Lou.

Siku ya Jumapili, alienda madhabahuni na kutoa ushuhuda wa wazi kwamba Mungu alikuwa amemtakasa. Siku ya Jumatatu, nilimuuliza kama ameona tofauti yoyote katika maisha yake tangu kutakaswa kwake.

Alijibu, "Sijakasirika, nilimsaidia mke wangu, na ninaendelea kumwambia kwamba ninampenda."

Siku ya Jumatano usiku, ibada za uamsho zilipokuwa zikiisha, Lou aliniambia, "Sijakasirika tangu Jumamosi. Nina uhakika kwa asilimia mia. Ninajua ninakoenda—mbinguni!" [161]

## NOVEMBA 1 — 305

# Je, unaweza kuwa mwema kwa kiasi gani?

*Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe muwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo.*
*1 Wathesalonike 5:23*

Hapo awali watoto wetu walipokuwa bado nyumbani, Jumapili moja asubuhi tulikuwa tukijiandaa kuondoka kwenda kanisani na ibada ya watoto kanisani. Kwa kuwa tulitoa kahawa na donati kabla ya ibada kuanza, mimi na mke wangu, Nancy, mara kwa mara tulibeba birika letu kubwa la kahawa hadi kanisani na kurudi kila juma. Siku hiyo, watoto wetu watatu walipokuwa pembeni kabisa ya nyumba wakivaa, nilimwambia Nancy, "Tutaacha birika letu la kahawa kanisani leo kwa sababu kanisa limeomba litumie usiku wa leo kwa ajili ya tafrija ya jioni."

Baadaye, baada ya shule ya Jumapili na ibada ya asubuhi, tulikuwa tukiendesha gari kuelekea nyumbani, na kila mtu alikuwa na furaha. Wasichana hao walikuwa kwenye kiti cha nyuma na Nancy. Mwana wetu, Paul, ambaye alikuwa na umri wa miaka tisa hivi, alikuwa kweny kiti cha mbele pamoja nami. Alinitazama kwa tabasamu kubwa na kusema, "Nimekusaidia leo, Baba. Ulipokuwa ukisalimiana na watu baada ya ibada, nilikuwekea birika la kahawa kwenye buti."

Nikiwa nimechanganyikiwa, nilijibu, "Kwa nini ulifanya hivyo? Nilitaka kuiacha kanisani."

161. *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Juni 2014).

Unafikiri nilipaswa kumwadhibu mwanangu? Alifanya jambo lisilofaa, baada ya yote—alileta birika la kahawa nyumbani wakati nilitaka kuliacha kule kanisani.

Nina uhakika ungepiga kura dhidi ya kumwadhibu kwa sababu bila shaka hakujua nilitaka kuiacha kanisani, na alikuwa ametenda kwa nia ya upendo—alikuwa akijaribu kusaidia.

Je, unaweza kuwa mwema kwa kiasi gani?

Paulo hakuwa mtu asiyekuwa na dosari, lakini alikuwa timilifu—huwa tunatofautisha maneno hayo katika lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo, usijiwekee kiwango kisichowezekana. Mungu hakuahidi "bila dosari." Badala yake, aliahidi kukuweka "ukiwa timilifu"—ili kutakasa nia za moyo wako ili utamani kumpenda na kumpendeza nyakati zote.

**NOVEMBA 2** **306**

# Tabia Endelevu ya Nafsi

*Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msifuate kanuni za dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*
*Warumi 12:1-2*

Hata baada ya uongofu wangu wa ajabu, uliobadili maisha, niligundua kwamba chuki, hasira, na roho ya kuhukumu vilikuwa bado vinaninyemelea moyoni mwangu. Kwa miezi kadhaa niliomba na kutafuta kazi ya Roho ya kusafisha, na utakaso. Kisha, wakati wa ibada ya Jumapili usiku, Roho wa Mungu akanitakasa. Ilikuwa ni uzoefu wa wazi, dhahiri, na wa kweli—nilihisi utakaso na nilijawa na upendo mwingi ambao ulijaa na kusukwa sukwa hadi siku iliyofuata.

Kazi zangu za siku iliyofuata zilijumuisha kufanya kazi katika biashara ya familia yangu kwa kuondoa vitu ndani ya vyumba vya hoteli baada ya wageni kuondoka. Nafasi ya kuhifadhi ilikuwa ya bei ghali, na tulikuwa katika harakaharaka. Nilichukua kitanda cha ziada kutoka kwa chumba kimoja na kujaribu kukiweka kwenye nafasi pekee ya kuhifadhi. Lakini vipande vya fremu ya chuma vilinaswa kwenye viunzi vya kitanda vilivyohifadhiwa pande zote

mbili—hakingeweza kuingia na kukaa mahali pake. Hili lilinikasirisha sana hivi kwamba *nilikirusha* kitanda hicho juu ya vitanda vingine viliyohifadhiwa.

Kwa kweli, hilo halikusuluhisha shida yangu, lakini muhimu zaidi, nilishangazwa na hasira yangu iliyopita kiasi. Nilikuwa tu nimetakaswa usiku uliopita—je utakaso haukushughulikia hili?

Baadaye, nilitumia miezi kadhaa kufikiria, kusoma, na kusali kuhusu tatizo hili. Nilianza kufikiria juu ya mazoea ambayo nilikuwa nimekuza katika miaka ishirini na moja ya maisha yangu. Tunaelewa nguvu ya tabia za kimwili kama vile uraibu wa tumbaku. Vipi kuhusu mazoea ya kihisia-moyo? Nilitoka katika familia iliyojaa vurugu za mara kwa mara, na kwa miaka mingi, nilikuwa nikitenda kwa hasira kali. Kulikuwa na ushahidi mkubwa wa mabadiliko chanya katika maisha yangu baada ya tukio langu la kutakaswa—je, inaweza kuwa Mungu alikuwa ameusafisha moyo wangu kweli, lakini bado nilikuwa na mazoea ya kihisia na kiakili yaliyokita mizizi sana ambayo yalihitaji kupangwa upya?

Nilipata msaada katika kuyasoma maisha ya Hudson Taylor, mmisionari mkuu aliyeanzisha Misheni ya China Inland. Taylor alikuwa na wongofu wa wazi, na baadaye, tukio la utakaso lisilopingika. Hata hivyo, miaka mingi baadaye, chini ya mkazo mkubwa wa huduma yake inayokua, alibadilika na kuwa mwenye kufadhaika. Kisha akakubali ushauri wenye hekima kutoka kwa rafiki yake na kufanya upya uhusiano wake uliotakaswa pamoja na Kristo.

Baadaye, Taylor aliandika, "Lakini yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele" (Yohana 4:14). Sio rasimu moja pekee anazungumza, au hata nyingi, lakini ya *tabia endelevu ya nafsi*" (msisitizo ni wangu).[162]

Nilihitaji kupanga upya mazoea ya kiakili na kihisia-moyo. Ninahitaji kunywa neema mara kwa mara, hata katikati ya changamoto kuu za maisha.

Katika Warumi 12:1-2, Paulo alitoa changamoto kwa Wakristo kujisalimisha mara moja-kwa-wote: "Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai . . . kwa Mungu." Lakini kumbuka kuwa pia aliamuru, "bali mgeuzwe kwa kufanya upya nia zenu," akimaanisha mchakato unaoendelea.

Na kwa hivyo ninatafuta tabia mpya- tabia endelevu ya nafsi. Vipi kuhusu wewe?

---

162. Quoted in Charles "Chic" Shaver, *Basic Bible Studies for the Spirit-Filled and Sanctified Life*, Lesson 6 (Kansas City, MO: Beacon Hill Press of Kansas City, 2009).

# Kosa Kubwa Sana, Sehemu ya 1

*Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi.*
*Wakolosai 3:12-14*

Nilifanya kosa kubwa, ninamaanisha kosa kubwa *kweli!* Nilipata habari kwamba kiongozi mtukufu, mcha Mungu wa kanisa letu la kimataifa amefariki. Wakati fulani, alikuwa amewahi kuwa kasisi mpendwa wa familia yetu. Nilipochunguza ili kutathmini ikiwa ripoti hiyo ilikuwa ya kweli, chanzo chenye ujuzi kilithibitisha, "Ndiyo, alifarikai jana."

Moyo wangu ulimhurumia sana mke wake, ambaye alikuwa mwanamke wa ajabu, mwenye upendo, mcha Mungu. Nilinunua kadi na kuandika ujumbe ndani yake nikionyesha huruma yangu na kuelezea baadhi ya kumbukumbu nzuri nilizokuwa nazo katika maisha yake. Siku hiyo, niliituma kadi ile.

Usiku huo, nilipokea simu kutoka kwa mfanyakazi mwenzangu—alikuwa amegundua kutoka kwa watu wengine kadhaa kwamba kiongozi huyu *hakuwa* amefariki. Kiongozi mwingine wa kimataifa alikuwa amefariki, na kwa namna fulani majina yalikanganya—ripoti ya awali haikuwa sahihi.

Rafiki yangu mtukufu hakuwa amefariki, na tayari nilikuwa nimemtumia mkewe kadi yenye ujumbe wa huruma. Niliona aibu sana. Nilijua ningempigia simu mke wake na kumuomba msamaha. Nilikuwa na wasiwasi juu ya kufanya hivi—ni mshtuko na huzuni gani ambayo ningemletea! Lakini bado, nilijua lazima nipige simu.

Kwa hiyo nilimpigia simu mwanamke huyu mcha Mungu niliyemfahamu kwa miaka mingi. Aliniambia jinsi alivyofurahi kuisikia sauti yangu. Mara moja, niliungama kwake, "Nimefanya kosa kubwa." Nilielezea ripoti ya uwongo na kadi yangu ya huruma. Nilipokuwa nikiomba msamaha, nilipendekeza labda angeweza kupata faraja katika kumbukumbu nilizoeleza kwa kina katika ujumbe wangu.

Kwa sauti iliyotulia, na yenye uelewa zaidi, alisema, "Chic, usijali kuhusu hili hata kidogo. Naelewa." Alisema yeye na mumewe walithamini familia yangu na mimi, naye akatoa shukrani zake kwa huduma na mchango wangu.

"Na usimruhusu shetani akufanye ujilaumu kwa hili," aliongeza.

Nilifarijika sana, kutiwa moyo, na kuchangamshwa na kukubali kwake kwa upendo. Nilisema, "Siku zote umekuwa katika nafasi ya kwanza katika orodha yangu ya watu ninaowatamani—lakini umezidi kukaa katika nafasi ya *juu zaidi* kwenye orodha hiyo!"

NOVEMBA 4 **308**

# Kosa Kubwa Sana, Sehemu ya 2

*Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi.*
*Wakolosai 3:12-14*

Nilifikiria nyuma juu ya kile nilichokifanya katika kutuma ile kadi ya huruma. Katika kuandika kadi, nilikuwa nikifanya hivyo kwa upendo, huruma, na kujali. Ingawa niliaibishwa na kosa hilo, simu ya kukiri kosa langu ilikuwa uthibitisho wa uaminifu na uadilifu. Nilikuwa nimefanya kosa, nilikosea katika ufahamu wangu, na nilifanya jambo la kutatanisha. Hata hivyo, nia yangu ilikuwa upendo na kujali; Nilikuwa nikijaribu kumfariji na kumtia moyo mke wa rafiki yangu. Hili lilikuwa kosa—si dhambi. Nilikumbushwa kwamba, ingawa utakaso hukupa moyo safi na kukujaza na upendo, hauahidi uelewa kamili au ujuzi kamili wa mawasiliano.

Nilipomaliza kumpigia simu mke wa rafiki yangu, niliketi. Nilihisi kitulizo kikubwa—hata kupendwa. Niligundua kuwa nilikuwa nimezungumza na kiongozi mkuu ambaye alikuwa amenionyesha huruma, wema, upole, na subira. Alikuwa tayari amemsamehe mtu ambaye angeweza kuwa na malalamiko dhidi yake—alikuwa amesamehe kama Yesu. Na, juu ya yote, alionyesha upendo. Tabia yake ilijumuisha ndani maagizo ya Paulo kwa Wakolosai (3:12–14).

Ninamjua mwanamke huyu kuwa ni muumini aliyetakaswa, aliyejazwa na Roho, na kile alichonionyesha kilikuwa ni kielelezi cha waliotakaswa kweli. Na tuwe na zaidi kama yeye!

# Ushahidi Wa Wazi, na aa Moja kwa Moja

*Katika hili tunafahamu ya kuwa tunakaa ndani yake, naye ndani yetu, kwa kuwa ametushirikisha Roho wake.*
*1 Yohana 4:13*

*Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya.*
*1 Wathesalonike 5:24*

Mnamo Oktoba 29, 1789, John Wesley alimwandikia maneno yafuatayo mwanamke kwa jina Betsy: "Je, umepokea ushuhuda wa wazi na wa moja kwa moja kwamba [uliokolewa] dhidi ya dhambi ya asili? Saa ngapi? Kwa namna gani? Na unauona wazi kama ilivyokuwa mwanzoni? Je, unahisi ongezeko?"

Hata leo, watu wanashuhudia matukio wazi ya utakaso kamili. Huu hapa ni ushuhuda wa mwanamke anayeitwa Nancy:

> *Katika miaka yangu ya awali nilikuwa—nilifikiri—nimeokolewa na kutakaswa. Niliamini ulihitaji kwenda madhabahuni mara mbili—mara moja ili kuokolewa, na mara ya pili kutakaswa. Ilionekana haikudumu.*
>
> *Jumapili jioni, mahubiri yalikuwa juu ya utakaso—kile tu nilichohitaji na nilitaka. Wakati wa wito wa madhabahuni, nilienda mbele kupokea tukio hili la ajabu. Ilikuwa rahisi sana. Alinisamehe dhambi zangu zote, na nilijua nilikuwa mgombea tayari. Kama vile andiko linavyosema katika 1 Wathesalonike 5:23, alinitakasa siku zote usiku wa Jumapili, Oktoba 19.*
>
> *Siwezi kueleza furaha na amani niliyo nayo moyoni mwangu! Nimekuwa nikifurahia Roho yake tangu wakati huo na nina hamu kubwa ya kumwambia kila mtu ninayeweza kuhusu tukio langu ili aweze kulipata pia!*
>
> *Lisifuni jina lake!*

Katika barua nyingine mwaka 1790, Wesley aliandika juu ya "jinsi haiwezekani kudumisha upendo safi bila kukua ndani yake."

Kwa hivyo kwa akina Nick na Nancy kila mahali, tunawasihi mtafute "shahidi wa wazi na wa moja kwa moja" wa utimilifu wa utakaso wa Mungu.

Mara tu Mungu akishakupa neema hiyo kwa neema, hakikisha *unaendelea kukua*.[163]

## NOVEMBA 6 — 310

# Viongozi Wanapobadilika na Masomo Yanapofunzwa

*Baada ya kufa kwake Musa, mtumishi wa BWANA, BWANA akamwambia Yoshua, mwana wa Nuni, mtumishi wa Musa, akasema, Musa mtumishi wangu amefariki; sasa ondoka, vuka mto huu wa Yordani; wewe na watu hawa wote, mkaende hadi nchi niwapayo wana wa Israeli. Kila mahali zitakapopakanyaga nyayo za miguu yenu, nimewapa ninyi, kama nilivyomwapia Musa. ..... Hakuna mtu yeyote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe; sitakupungukia wala sitakuacha. Uwe hodari na moyo wa ushujaa, maana ni wewe utakayewarithisha watu hawa nchi hii niliyowaapia baba zao ya kwamba nitawapa.*
*Yoshua 1:1-3, 5-6*

Ilikuwa ni hasara kubwa sana, yenye kuhuzunisha—Musa, kiongozi wa Israeli kwa miaka arobaini, na mtu mwenye nguvu zaidi kiroho waliyepata kumjua, alikuwa amefariki. Siku thelathini za maombolezo kwa ajili yake zilifaa (Kumbukumbu la Torati 34:8).

Lakini kifo cha Musa hakikuweza kuwapooza Waisraeli. Mungu alikuwa amewaita; walikuwa kwenye misheni, na utimilifu ulikuwa karibu.

Kifungu chetu kinaanza na kifungu hiki cha maneno, "BWANA akamwambia Yoshua" (Yoshua 1:1). Ni mara ngapi Bwana alikuwa amezungumza—tunamtumikia Mungu anayezungumza. Ni fursa yetu kumsikiliza. Bila shaka, lazima tuwe na nia katika kukuza usikivu wetu wa kiroho. Ni muhimu sana kusikia mwongozo wa Mungu nyakati za mabadiliko ya uongozi.

Yoshua alipaswa kuwa kiongozi mpya wa Israeli. Huu haukuwa mshtuko; Mungu alikuwa akimtayarisha Yoshua kwa ajili ya jambo hili, na vivyo hivyo Musa. Hata wakati wa kifo cha Musa, Maandiko yanasisitiza jambo

---

163. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Machi 2009).

hili: “Na Yoshua mwana wa Nuni, alikuwa amejaa roho ya hekima; maana Musa alikuwa amemwekea mikono yake juu yake” (Kumbukumbu la Torati 34:9). Na kwa sababu ya maandalizi ya kiongozi mpya, “wana wa Israeli wakamsikiliza, wakafanya kama BWANA alivyomwamuru Musa.” (34:9). Ilikuwa ni busara kumwandaa kiongozi anayefuata.

Kisha Mungu akaamuru, “Sasa ondoka, vuka mto huu wa Yordani; wewe na watu hawa wote” (Yoshua 1:2). Sehemu yoyote ambayo Mungu alikuwa nayo, Israeli pia walikuwa na sehemu. Kitabu cha Hesabu kinaripoti kwamba kulikuwa na wapiganaji 600,000 kati yao. Uhasibu wa wanawake na watoto, lazima tuwe tunazungumzia zaidi ya watu milioni 1.5—pamoja na mifugo na nyara za ushindi wao. Yoshua alitumia mfuatano wake wa mamlaka na kuamuru maofisa wake kupita katika nchi ili kuwaambia watu wajitayarishe (1:10–11). Kuwa na muundo wa kufanya kazi ili kushughulikia mabadiliko ya viongozi ilikuwa muhimu.

Lakini, zaidi ya yote, hii ni kazi ya Bwana: “Kila mahali zitakapokanyaga nyayo za miguu yenu” (1:3). Nakumbuka mmoja wa viongozi wa dhehebu langu wazuri zaidi akisema, “Ilikuwa mojawapo ya maamuzi yaliyoongozwa na Roho ambayo nimewahi kufanya.”

Mungu anasema, “Nitafanya.” Tunamheshimu Bwana na kumpa utukufu. Tunakumbuka yeye huja kwanza; na sisi tunafuata. Ni lazima tushirikiane naye na kutenda kwa ajili yake. Yeye hutoa mahali; lazima tuingie ndani yake. Ni mara ngapi Mungu tayari ametutayarishia njia lakini hatuna kile ambacho kinapaswa kuwa fursa yetu? Inapatikana—imiliki!

Akijua kwamba kuhama huko kunaleta changamoto kubwa sana, Mungu anaamuru watu wake, “Iweni hodari na moyo wa ushujaa” (1:6), akiwapa maneno ya kutia moyo waliyohitaji.

Mungu ni mkuu katika kutimiza ahadi na kukumbuka historia. Elewa kwamba anasema hapa, “nchi niliyoapa kwa babu zao kwamba nitawapa” (1:6). Mara nyingi, Mungu huwataja mababu hao—Abrahamu, Isaka, na Yakobo. Marejeleo haya yanaibua historia nyingi, ahadi nyingi, na mpango wa muda mrefu wa Mungu. Hata baada ya Yesu kuja duniani, masuala hayo yalikuwa yakiendelea. Kristo alitoa onyo lifuatalo kwa watu waasi wa siku zake: “Ndipo kutakapokuwa na kilio na kusaga meno, mtakapomwona Abrahamu na Isaka na Yakobo na manabii wote katika ufalme wa Mungu, nanyi wenyewe mmetupwa nje” (Luka 13:28). Kumweka Mungu kama Bwana ndilo suala muhimu sana katika misimu ya mabadiliko ya uongozi.

Kuzingatia mabadiliko kama haya ya uongozi hubariki sisi tunaotazama yakitokea. Hadi leo, tunamiliki ardhi ya kiroho ambayo imeundwa na

kujengwa na watangulizi wetu wa kiroho. Ninawafikiria walimu katika maisha yangu na masomo waliyonifundisha.

1. Petro: Mungu ni wa kweli
2. Ralph na Bernice: Jinsi ya kuomba na wanaotafuta
3. Earl na Hazel: Uongozi wa Kimungu
4. Jinsi ya kufanya wanafunzi ambao watafanya wanafunzi ambao watafanya wanafunzi
5. Ralph: Kutegemewa kwa Neno la Mungu
6. Mendell na Gertrude: Ukarimu
7. Rees: Jinsi ya kuomba kupitia hali
8. Scott: Uongozi imara

Na wapo wengi zaidi.

Ninapata wakati mwema wa maisha yangu ninapotembea nje na katika nchi ya ahadi ya maisha yangu, nikiweka miguu yangu kwenye maeneo yaliyobarikiwa ambayo yaliundwa na wengine wengi ambao siwezi kamwe kuwalipa. Na nina uwezekano mwingine ulio wazi kwangu kwa sababu ninaishi katika enzi ya Yesu Kristo: "Kwa maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo" (1 Wakorintho 3:11). Mungu asifiwe!

Uwezekano huu uko wazi kwako pia. Je, utamiliki nchi gani ya ahadi wiki hii?

**NOVEMBA 7** **311**

# Shujaa Ndani ya Mhalifu

*Basi Eliya akaenda ili ajioneshe kwa Ahabu. Na njaa ilikuwa nzito katika Samaria. Ahabu akamwita Obadia, aliyekuwa juu ya nyumba yake; (na huyu Obadia alikuwa mwenye kumcha BWANA sana; wa kuwa ikawa, Yezebeli alipowaua manabii wa BWANA, Obadia akatwaa manabii mia moja, akawaficha hamsini hamsini katika pango, akawalisha chakula na kuwapa maji).*
*1 Wafalme 18:2-4*

Usingeweza kuwazia mfalme asiyemwogopa Mungu na mwovu kuliko Ahabu (I Wafalme 16:33). Obadia alifanya kazi chini ya mfalme huyu mwovu kama meneja wake wa ikulu. Nakala hiyo inasema kuwa, "Na huyu Obadia alikuwa

*mwenye kumcha Mungu* sana" – na kwa hakika, tunaona kwamba Obadia alidhihirisha imani hiyo katika matendo yake. Lakini Ahabu mwovu alikuwa na nguvu; Obadia mwadilifu alikuwa mtumishi wake. Je, Obadia aliamini kwamba angeweza kuwa na ushawishi wa kimungu kwa mfalme?

Licha ya kuogopa kuuawa, Obadia alipanga mkutano kati ya Ahabu na nabii Eliya. Mkutano huo ulisababisha shindano kati ya manabii wa Baali na Mungu wa Eliya—ambalo lilifuatiwa na Mungu kuonyesha nguvu zake kwa moto na kuangamizwa kwa manabii waovu 450 wa Baali. Ninafurahi kwamba Obadia hakuacha, hakukata tamaa, au kuamua kuwa asingeweza kuwa na ushawishi wa kimungu.

Ilikuwa wakati wa hatari nchini Marekani: watu 100,000 walikuwa wameandamana huko Washington, DC, kupinga Vita vya Vietnam, na Rais Nixon alipaswa kuhutubia kikao cha pamoja cha Congress. Wakati huo, nilikuwa DC nikihubiri katika kanisa la mtaa kwa juma moja. Mwandishi mkuu wa mjadala wa Baraza la Seneti la Marekani alikuwa mshiriki wa kanisa hilo la mtaa, na alinipatia kiti katika kikao cha pamoja. Sikumbuki maneno ya rais, lakini sijawahi kusahau kile ambacho kinara mkuu alisema baadaye: "Nimeona uovu kama huo kwenye chumba cha mavazi kwenye jingo la Seneti. Wakati fulani natamani ningerudi katika eneo langu la Wyoming. Lakini basi nafikiri, *Nini kitatokea kwa serikali yetu ikiwa watu wacha Mungu wataondoka?"*

Iwe chini ya mfalme mwovu au katikati ya uovu katika Seneti, watu wacha Mungu bado watafanya athari zao. Unajipata wapi leo? Usikose nafasi yako ya kufanya athari ya kimungu! Hata chini ya uongozi wa mhalifu, unaweza kuwa shujaa.

**NOVEMBA 8** **312**

## Je, Kuna Kitu Kingine?

*Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu*
*iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu,*
*ndiyo ibada yenu yenye maana.*
*Warumi 12:1*

Kwa miaka mingi nimekutana na watu ambao wameyasalimisha yote kwa Mungu na kupokea utimilifu wa utakaso wa Roho. Hapa kuna hadithi ya Kathy:

*Kwa miaka mingi, nilimpuuza Mungu aliyekuwa pamoja nami—hakuna sala, hakuna usomaji wa Bibilia, hakuna kanisa. Niliishi tu.*

*Mnamo Julai mwaka 2000, mume wangu, Gary, aligunduliwa na ugonjwa wa kansa huku kukiwa na ubashiri wa kwamba ulikuwa umesalia kwa miezi kadhaa tu, na kufikia Februari 2001, alikuwa amefariki. Siku zangu za kuishi tu zilikuwa zimekwisha. Mungu sasa alikuwa na usikivu wangu—Mungu na huzuni. Walikuwa nami kila mahali na katika mambo yote niliyokuwa nikifanya.*

*Nilialikwa kujiunga na kikundi kidogo cha kujifunza Bibilia na mwalimu wangu wa shule ya Jumapili, Dkt. Chic Shaver. Nilianza mafunzo katika kitabu cha Yohana na baada ya muda mfupi nikakumbana na kizuizi—kizuizi kikubwa—katika safari yangu ya kiroho. Hakikuwa na uhusiano na nyenzo; kilikuwa na uhusiano na mwalimu. Nilikuwa mwangalifu kutoruhusu mwanaume yeyote, hata mume wangu, kuwa mtu mwenye mamlaka katika maisha yangu baada ya dhuluma niliyoipata kutoka kwa baba yangu. Dkt. Shaver alikuwa anataka kuwa mtu mwenye mamlaka, kwa kuwa alitarajia niwepo, niwe tayari, na nishiriki. Nilikuwa nikifikia wakati mgumu wa kiroho nilipotambua kwamba Mungu pia alitarajia zaidi kutoka kwangu, na alikuwa mtu mwenye mamlaka! Lazima kungekuwa na makubaliano.*

*Nilihamia katika somo lingine nikifundishwa na Dkt. Shaver—somo la kina zaidi na la kujichunguza—linaloitwa Kuishi katika Nguvu za Roho. Yote yalikuwa juu ya kuhamia na kudumisha uhusiano wa kina wa kibinafsi na Roho Mtakatifu-kitu kinachoitwa utakaso. Nilijifunza, katika kipindi cha majuma mengi ya kujifunza kwa kina, maombi, na majadiliano ya kikundi, kwamba Mungu alitaka yaliyo bora zaidi—yale yaliyo bora zaidi—kwangu, na hilo lingepatikana kwa kuachilia kwa hiari mamlaka. Juu ya maeneo yote ya maisha yangu na kuyakabidhi. Kwake. Polepole, nilifika mahali nilipoelewa kwamba Baba yangu wa mbinguni hatawahi kunidhuru, na ningeweza kuamini mamlaka yake juu yangu. Kwa kweli, ni kitu nilichotamani! Kilichobaki ni maelezo tu. Nakumbuka niliuliza kwenye madhabahu, "Je, kuna kitu kingine chochote unachotaka nikupe?" Niliendelea kuuliza swali hilo mpaka ukimya wa Mungu na amani yangu kubwa ikanihakikishia hakuna kingine.*

*Nilipata utakaso kamili kama uamuzi wa mara moja, wa mgogoro wa kiroho na ninaeendelea kuupitia kama uamuzi endelevu wa kuishi maisha*

*yangu jinsi Mungu anavyotaka mimi niishi. Jambo kuu kuhusu hayo yote ni kwamba kwa ushirika wa karibu, wa upendo tulio nao, pia ndivyo ninavyotaka kuishi!*

*Sikuweza kamwe kuota mahali ambapo Mungu angenipeleka na njia ambazo angenipenda na kuniongoza kutumikia. Maisha yangu ndani yake ni safari yenye miadi ya kimungu iliyotapakaa njiani. Nimebarikiwa sana kuwa mali yake!*

**NOVEMBA 9** **313**

# Hapana Mwingine, Ila Yeye, Sehemu ya 1

*Wewe umeoneshwa haya, ili upate kujua ya kuwa*
*BWANA ndiye Mungu, hapana mwingine ila yeye.*
*Kumbukumbu la Torati 4:35*

Mungu aliuzungushia moyo wangu mfululizo wa mistari katika Maandiko. Ungana nami katika kuchunguza mfululizo huu wa ripoti za Biblia. Unaposoma, Mungu akutengenezee moyo wako kama alivyoufanya wangu.

Musa alipokuwa akipokea Amri Kumi kwenye Mlima Sinai—amri ambazo zilijumuisha, "Usiwe na miungu mingine ila mimi. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, wala kilicho majini chini ya dunia" (Kutoka 20:3-4)—Israeli walikuwa wakitengeneza na kuabudu ndama wa dhahabu chini ya mlima huo huo.

Mungu alinena, na Musa akajibu:

> "Mimi nimewaona watu hawa," Mungu akamwambia Musa, "ni watu wakaidi. Basi sasa niache, ilihasira zangu ziwake juu yao, niwaangamize, name nitakufanya wewe uwe taifa kuu."
>
> Lakini Musa akatafuta kibali cha BWANA, Mungu wake. "BWANA," akasema, "kwa nini hasira zako kuwaka juu ya watu wako uliowaleata kutoka nchi ya Misri, kwa uweza mkuu, na mkono wenye nguvu? Kwa nbini Wamisri waseme, kuwa, 'Amewatoa ili awatende mabaya, apate kuwaua milimani na kuwaangamiza watoke juu ya uso wa nchi?' Geuza katika hasira yako kali, ughairi uovu huu ulio nao juu ya watu wako. Mkumbuke Abrahamu na Isaka, na Israeli, watumishi wako, amabao uliwaapia kwa nafsi yako, na kuwaambia: 'Nitazidisha kizazi chenu mfano wa nyota za mbinguni; ten nchi hii yote niliyoinena nitakipa kizazi

chenu nao watairithi milele.'" Na Bwana akaughairi ule uovu aliosema ya kwamba atawatenda watu wake. (Kutoka 32:9—14)

Kisha Musa akawaombea watu hao:

Hata asubuhi yake Musa akawaambia watu, "Mmetnda dhambi kuu; na sasa nitakwenda juu kwa Bwana, labda nitapa upatanisho kwa jaili ya dhmabi yenu."

Musa akarejea kwa Bwana akasema, "Aa, watu hawa wametenda dhambi kuu wamejifanyia Miungu ya dhahabu. Lakini sasa ikiwa utasaemehe dhambi yao – na kama sivyo, unifute, nakusihi, katika kitabu chako ulichoandika" (Kutoka 32:30-32).

Hatimaye, Mungu akamwambia Musa aende kwenye nchi ya ahadi:

BWANA akasema na Musa uso kwa uso, kama mtu asemavyo na rafiki. Kisha Musa angerudi kambini, lakini mtumishi wake kijana Yoshua mwana wa Nuni hakutoka mle hemani.

Musa akamwambia Bwana, "Angalia, wewe waniambia, wachukue watu hawa,' nawe hukunijulishja ni nani utakayemtuma pamoja nami. Lakini umesema, nakujua jina lako, nawe umepata neema mbele yangu.' Basi, sasa nakuomba, ikiwa nimepata neema mbele zako, unioneshe njia zako, nipate kukujua, ili nipate neema mbele zako; ukakumbuke ya kwamba, taifa hilo ndilo watu wako."

Naye Bwana akasema, "Uso wangu utakwenda pamoja nawe, name nitakupa raha."

Naye Musa akamwambia, "Uso wako usipokwenda pamoja nami, usituchukue kutoka hapa" (Kutoka 33:11—15).

Nimefurahishwa na vipengele vifuatavyo vya hadithi:

- Musa aliomba heshima ya Mungu na sifa yake katika Misri (32:12).
- Musa aliomba ahadi za Mungu kwa baba wa kiroho wa Israeli (32:13).
- Mungu alikubali kuitikia maombi ya Musa (32:14).
- Musa alilemewa sana na watu wake hivi kwamba alikuwa tayari kuhatarisha kufutwa katika kitabu cha Mungu (32:32).
- Uwepo wa Mungu ungeenda pamoja na Musa hadi nchi ya ahadi (33:14).

# Hapana Mwingine, Ila Yeye Sehemu ya 2

*Wewe umeoneshwa haya, ili upate kujua ya kuwa BWANA ndiye Mungu, hapana mwingine ila yeye.*
*Kumbukumbu la Torati 4:35*

Musa anawapatia Waisraeli maji kutoka kwenye mwamba lakini si kwa njia sahihi:

> "Twaa ile fimbo, ukawakusanye mkutano, wewe na Haruni ndugu yako, ukauambie mwamba mbele ya macho yao utoe maji yake, nawe utawatokezea maji katika mwamba, na hivyo utawanywesha maji mkutano na wanyama wao."
>
> Musa akaitwaa hiyo fimbo kutoka mbele za BWANA kama alivyomwamuru. Musa na Haruni wakawakusanya kusanyiko mbele ya mwamba, akawaambia, "Sikieni sasa, enyi waasi; je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu?" Musa akainua mkono wake akaupiga ule mwamba kwa fimbo yake mara mbili; maji yakatoka mengi, mkutano wakanywa na wanyama wao pia.
>
> BWANA akamwambia Musa na Haruni, "Kwa kuwa hamkuniamini mimi, ili kunistahi mbele ya macho ya wana wa Israeli, basi kwa sababu hiyo, hamtawaingiza kusanyiko hili katika ile nchi niliyowapa" (Hesabu 20:8-12).

Israeli walifika kwenye Mto Yordani, baada ya miaka arobaini, bado umbali mfupi wavuke kuingia nchi ya ahadi. Musa na Bwana wana mazungumzo ya uhusiano binafsi:

> Nikamnyenyekea Bwana wakati huo, nikamwambia: "Ee Bwana Mungu, umeanza kumwonesha mtumishi wako ukubwa wako, na mkono wako wa nguvu, kwa kuna Mungu gani mbinguni au duniani awezaye kufanya mfano wa kazi zako, na mfano wa matendo yako yenye nguvu? Nami nakuomba nivuke, nikaione hiyo nchi nzuri iliyoko ng'ambo ya Yordani, mlima ule mzuri, na Lebanoni."
>
> Lakini BWANA alikuwa amenikasirikia kwa ajili yenu, asinisikize; BWANA akaniambia, "Na ikutoshe." Usinene nami zaidi jambo hili. "Kwea katika kilele cha Pisga ukainue macho yako upande wa magharibi, na kaskazini, na kusini, na mashariki, ukatazame kwa macho yako, kwa

maana huuvuki mto huu wa Yordani. Lakini mwagize Yoshua, mtie moyo na nguvu, umtie na nguvu; kwani ndiye atakayevuka mbele ya watu hawa, na nchi utakayoiona atawarithisha yeye" (Kumbukumbu la Torati 3:23-28)

Musa anawasihi watu wake:

Tazama siku zilizopita, zilizokuwa kabla yako, tangu siku ile Mungu aliyoumba mwanadamu juu ya nchi, na kutoka pembe hii ya mbingu hadi ile, kama kumetukia neno lolote kama neno hili kubwa, au kwamba kumesikiwa habari ya neno kama hili? Je! Kuna wakati wowote watu wameisikia sauti ya Mungu ikinena toka kati ya moto, kama wewe ulivyosikia, na wakaendelea kuishi? Au Mungu amekwenda wakati gani akajitwalia taifa kutoka kati ya taifa lingine, kwa majaribu, ishara, maajabu, vita, mkono hodari, mkono ulionyoshwa, na vitisho vikuu, kama vile BWANA, Mungu wenu, alivyowatendea ninyi katika Misri, mbele ya macho yenu?

Wewe ulioneshwa haya, ili upate kujua ya kuwa BWANA ndiye Mungu, hapana mwingine ila yeye. Kutoka mbinguni amekufanya usikie sauti yake, ili akufundishe; na juu ya nchi alikuonesha moto wake mkuu; ukasikia maneno yake kutoka katika moto. Na kwa sababu aliwapenda baba zenu, kwa sababu hiyo aliwachagua wazao wao baada yao, akakutoa katika Misri kwa kuwako pamoja nawe, kwa uweza wake mwingi, ili kufukuza mbele yako mataifa, walio wakubwa, wenye nguvu kukupita wewe, ili kukuingiza, na kukupa nchi yao iwe urithi, kama ilivyo leo.

Kwa hiyo ujue, leo hivi, ukaweke moyoni mwako, ya kuwa BWANA ndiye Mungu katika mbingu juu, na katika nchi chini; hapana mwingine. Basi, zishike sheria zake, na amri zake, ninazokuamuru leo, upate kufanikiwa, wewe na watoto wako baada yako, na siku zako ziwe nyingi katika nchi ile akupayo BWANA, Mungu wako, milele. (Kumbukumbu la Torati 4:32-40)

Nimefurahishwa na maelezo yafuatayo ya hadithi hii:

- Katika hasira yake na Israeli, Musa alikosa kutii maagizo ya Mungu, akakiuka utakatifu wa Mungu na kupoteza fursa ya kuwaongoza Waisraeli katika nchi ya ahadi (Hesabu 20:11–12).
- Mungu alimruhusu Musa kuiona nchi ya ahadi lakini akamwagiza Yoshua kuwaongoza watu kuingia humo (Kumbukumbu la Torati 3:25–28).
- Musa alisimulia ukuu wa Mungu na kuwaagiza Israeli watii (Kumbukumbu la Torati 4:35, 40).

Bwana ndiye Mungu; pasipo yeye, hakuna mwingine!

# Ni Nini Hufanya Dhambi "Ikakosa Mamlaka"?

*Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema.*
*Warumi 6:14*

Neema ilinifikia nikiwa kijana nilipokuwa bado nikimtumikia bwana wangu wa zamani, dhambi. Yule bwana aliniacha nimepotea, peke yangu, na kuogopa kwamba ningeachwa tena na tena na wale niliowapenda. Nilibeba woga huu kama mzigo mzito, na nilikuwa nikitafuta mahali pa kuuweka nilipomsikia Yesu akiniita kupitia familia yake yenye upendo: "Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha" (Mathayo 11:28).

Hii ilikuwa habari njema kwangu, kwa kuwa ilinipa tumaini. Nikiwa na woga fulani moyoni mwangu, nilipiga magoti na kumtolea Mungu nafsi yangu iliyokuwa na ugonjwa wa dhambi. Kwa upole sana, nilifungua mlango na kumkaribisha Kristo wa msalaba ndani. Wakati huo mabadilishano makubwa yalifanyika, mzigo wangu ulinitoka, na Kristo alikuwa nyumbani moyoni mwangu.

Dhambi si bwana wangu tena kwa sababu siku moja nilimchagua Yesu, na kila siku ananipa uwezo wa kuchagua. Siisikii sauti ya bwana wangu wa zamani, kwa sababu Yesu anawapenda wasiopendeka. Anasamehe asiyesameheka. Anapata kisichoweza kupatikana, na tunajikuta tumekumbatiwa katika mikono ya Mungu.

Nancy Shaver[164]

164. Awali yalichapishwa katika *Come Ye Apart* Julai–Agosti–Septemba 1964 (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House), 89. Imetumiwa kwa idhini. (Chapisho hili lilikuja kuwa *Reflecting God*.)

# Kuwekwa Huru

*Na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi,*
*mkawa watumwa wa haki.*
*Warumi 6:18*

Patrick alikua kama asiyeamini kwamba kuna Mungu na aliamini kwamba Biblia ilijipinga yenyewe. Baada ya kukumbana na changamoto, alianza kusoma Agano la Kale na kulimaliza mwaka 2003. Mwaka huo huo alioa. Mnamo mwaka 2008, alianza kusoma Agano Jipya. Mnamo Oktoba 2009, Patrick alitazama tovuti kuhusu kuzimu. Alikuwa na wasiwasi baada ya kutambua kwamba umilele hautimiziki kamwe.

Mnamo Oktoba 28, 2009, aliachana na ponografia, akaanza kusali, na kiakili akaanza kumwamini Yesu. Mnamo Novemba 1, Patrick na mkewe walihudhuria kanisani kwa mara ya kwanza. Alianza kukutana na mchungaji.

Mnamo Novemba 28, wakati mwanawe, Eric, alikuwa hospitalini, Patrick alisoma Matendo na kuombea maono ya Sauli (Paulo). Patrick alilala na kushtuka akaamshwa na mwanga mweupe—Yesu akasimama mbele yake. Patrick akasema, "Asante."

Yesu alisema, *"Katika ufuasi naenda."*

Patrick alijua hatua yake ya kwanza ilikuwa kubatizwa. Baada ya hafla ya kubatizwa kwake, alianza kumpenda mke wake zaidi. Eric, mwanawe, alisema, "Ulianza kuwa mzuri." Sasa Patrick anapanga kuhudhuria shule ya Bibilia.

Kwenye mkutano wa kambi, baada ya mahubiri yaliyoitwa "Nimesulibiwa pamoja na Kristo," Patrick aliumia madhabahuni juu ya ubinafsi wa kina uliokuwa umebaki ndani yake. Siku chache baadaye, Patrick alisali na kupata uhakikisho wa kina na kwamba aliwekwa huru.[165]

---

165. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Septemba 2010).

NOVEMBA 13 **317**

## "Uwe Mkamilifiu" – C. S. Lewis

*Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu,*
*kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye*
*hofu hakukamilishwa katika pendo.*
*1 Yohana 4:18*

Ifuatayo ni sehemu ya kitabu cha *Mere Christianity* cha CS Lewis:

> *[Kristo] hakuwahi kuzungumza maneno yasiyo sahihi na yasiyoeleweka na yasiyo na maana. Aliposema, "uwe mkamilifu," alimaanisha hilo. Anamaanisha lazima tuingie tupate matibabu kamili. Ni vigumu, lakini aina ya maelewano tunayotafuta ni vigumu zaidi - kwa kweli, haiwezekani. Inaweza kuwa vigumu kwa yai kugeuka kuwa ndege; itakuwa vigumu kwake kujifunza kuruka huku akisalia kuwa yai. Sisi ni kama mayai kwa sasa. Na huwezi kuendelea kwa muda usiojulikana kuwa yai la kawaida tu. Lazima tuanguliwe au tuoze kwa kuharibika.*
>
> *Je, naweza kurudi kwa yale niliyosema hapo awali? Huu ni Ukristo wote. Hakuna lingine lolote . . . . Kanisa halipo kwa ajili ya kitu kingine ila kuwavuta [watu] ndani ya Kristo, kuwafanya wawe Kristo wadogo. Kama hawafanyi hivyo, makanisa yote makuu, makasisi, misheni, ibada, hata Biblia yenyewe, ni kupoteza muda tu. Mungu alifanyika [mwanadamu] bila kusudi lingine.*[166]

NOVEMBA 14 **318**

## Malipo kwa Huduma

*Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna*
*kwa wakati wake, tusipozimia roho.*
*Wagalatia 6:9*

166. C. S. Lewis, *Mere Christianity* (New York: McMillan, 1952), 169–70.

"Lazima niseme tu asante kwako, Dkt. Shaver."

Najua nilionekana kushangaa kabisa Christine aliponisalimia kwa njia hiyo kwenye mkutano wa kambi ya Ohio Mashariki. Kisha akaniambia kisa chake.

Christine alikuwa na umri wa miaka kumi mama yake alipompeleka kwenye ibada za ufufuo katika kanisa moja huko Plattsburgh, New York. Alikwenda mbele kuomba, na Mungu akautakasa moyo wake mchanga kabisa. Baada ya hapo, alimwomba mama yake ampeleke kwenye ibada zote za ufufuo. Kila usiku, aliketi kwenye safu ya kwanza ya roshani na kutazama ukingoni ili kuingiza yote ambayo Mungu alikuwa akifanya.

Sasa Christine ameolewa na Neil, ambaye ameitwa kwenye huduma. Wako njiani kuelekea Niagara Falls, New York, ambako wataanza uchungaji wao wa kwanza. Akiwa na umri wa miaka kumi, Christine alipata neema ya Mungu—na sasa yeye na mume wake wanafanya kazi ya uchungaji. Malipo yaliyoje?

Baada ya ibada ya usiku huo kwenye mkutano wa kambi ya Ohio Mashariki, Kristi, mke wa mchungaji mwingine, alinitazama kwa tabasamu kubwa na kusema, "Nilitakaswa katika darasa lako la uinjilisti katika Jiji la Kansas."

"Je, lilileta mabadiliko?" Niliuliza.

"Oh, ndiyo," akajibu. "Sijawahi kutambua jinsi nilivyokuwa mbinafsi."

Malipo mengine!

Laura Fitzsimmons alinitumia ujumbe wa pongezi nilipopokea tuzo. Katika kadi yake, alitafakari wakati fulani mwaka 1993 wakati yeye na mume wake walimkubali Kristo baada ya mimi na wengine kadhaa kushiriki injili pamoja nao. Aliandika hivi: "Hebu fikiria—maisha hayo yote ambayo yamebadilishwa kwa sababu ya moyo wako kwa ajili ya waliopotea. Mungu asifiwe kwamba familia yangu ilikutana nawe! Ninakuandikia kutoka katika kambi ya darasa la tatu na la nne wiki hii huko Augusta, Kansas. Ninawapikia watu mia tatu! Umewahi kufikiria ningefanya kitu kama hiki? Nimetoka mbali sana baada ya kukutana nawe karibu miaka kumi na tano iliyopita. Msifu Mungu, msifu Mungu. Asante rafiki yangu kwa kunipenda."

Bado malipo mengine. Fikiria malipo ambayo yatakuja katika maisha yako.[167]

---

167. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Septemba 2008).

# Yohana na Dhambi

*Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki.*
*1 Yohana 2:1*

Yohana alikuwa na tatizo kubwa kuhusu wazo kwamba Wakristo wa kweli (wafuasi wa Kristo) wanaendelea kutenda dhambi. Tazama baadhi ya kauli zake kuu katika 1 Yohana 3:

- "Dhambi ni uasi" (3:4).
- "Yeye [Kristo] alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi zetu." (3:5)
- "Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi" (3:6).
- "Atendaye dhambi ni wa Ibilisi . . . . Kwa kusudi hili mwana wa Mungu alidhihirishwa ili azivunje kazi za Ibilisi" (3:8).
- "Hakuna mtu aliyewzaliwa na Mungu [na bado anaishi] ambaye ataendelea kutenda dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake" (3:9).

Baadhi ya ufafanuzi wa kimsingi utatusaidia:

- Dhambi (asili ya dhambi)—Hali ya dhambi ya moyo ambayo matendo ya dhambi huchipuka. Inaweza pia kuitwa ubinafsi au kujifikiria mwenyewe.
- Kutenda dhambi—Kuvunja kwa makusudi sheria ya Mungu inayojulikana.
- Dhambi isiyokusudiwa—Kuvunja sheria ya Mungu kwa wakati usiotarajiwa, lakini si kwa hiari au kwa kusudi lililowekwa.
- Kosa—Kitendo ambacho kinapungukiwa na mapenzi makamilifu ya Mungu lakini ni bila kukusudia na kinafanywa kwa kutojua.

Haya yote yanahitaji damu ya Kristo itakasayo. Hata hivyo, kufanya kosa si sawa na kutenda dhambi. Dhambi zote zinahitaji msamaha. Ubinafsi, kwa upande mwingine, huwezi kusamehewa, unahitaji kutakaswa.

Baadhi ya watu wa wakati wa Yohana walidai kuwa hawana dhambi (1:8). Yohana alihubiri, "Bali tukienda katika nuru, kaka yeye alivyo katika nuru, tunashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, *yatusafisha*

*dhambi yote*" (1:7). Kumbuka kwamba suala si msamaha, lakini usafishaji au utakaso.

Hii si kudai kwamba Mkristo hawezi kutenda dhambi. Ni kudai kwamba Mkristo *hahitaji* dhambi. Katika hali hii, haiwezekani kimwili kwa mtu kutofanya dhambi; badala yake, ni nje ya tabia ya mtu kimaadili. Kama vile mtu mwaminifu hawezi kusema uongo, vivyo hivyo Mkristo hawezi kutenda dhambi. Kutenda dhambi hakupatani na kuwa mfuasi wa Yesu Kristo.

Unaweza kujiuliza, "Itakuwaje nikitenda dhambi baada ya kuwa Mkristo?" Katika maandiko ya leo, Yohana anasema kusudi lake zima la kuandika ni "ili kwamba msitende dhambi." Hata hivyo, anaendelea zaidi: "Na *kama* mtu akitenda dhambi tunaye mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo." Gundua kwamba Yohana anasema, "kama," si "utakapo." Na *kama* dhambi itatokea, tunapaswa kuungama mara moja kwa Mungu kupitia Yesu Kristo kwa ajili ya msamaha, utakaso, na urejesho.

Curt na Jan walipompokea Kristo, ilimaanisha kuungama na kugeuka kutoka katika dhambi zao zilizopita. Ilimaanisha kumpokea Yesu kama msamehevu wa dhambi zao (Mwokozi) na kiongozi wa maisha yao (Bwana). Ilimaanisha mabadiliko ya mara moja ya mtindo wa maisha, pamoja na kukombolewa kutoka kwa matumizi ya pombe na tumbaku.

Pia ilimaanisha kurejeshwa kwa ndoa yao iliyovunjika. Walitazama ndoa za Wakristo wengine na kusema, "Hilo huenda likawezekana kwetu." Muda si muda, Curt na Jan walianza kulea watoto wao kwa ushawishi wa kimungu.

Walipoanza kuhudhuria ibada za kanisa kwa uaminifu, waligundua kwamba kwa kuwa Mungu alikuwa amewabariki kwa rasilimali za kifedha, ilikuwa sawa tu kwamba walipe zaka (kumpa Mungu asilimia kumi ya mapato yao).

Hatimaye, Curt na Jan walianza kuwaleta wengine kwa Kristo. Walikuja kuelewa kwamba kulikuwa na kiwango cha kina cha utakaso kutokana na kubaki na ubinafsi, na hatimaye, walipata utakaso wa Mungu. Walijihusisha na madai ya Paulo katika Wagalatia 2:20: "Nimesulubiwa pamoja na Kristo."

Jan alisema hivi: "Tuliamini tunaweza kuwa washindi."

Je, huu si aina ya Ukristo unaoutaka pia?

# Mito Ya Maji Yaliyo Hai Tena

*Katika siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama, akapaza sauti yake akisema, Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema kuhusu Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa.*
*Yohana 7:37-39*

"Je, kweli inasema, mito ya maji yaliyo hai? Alimuuliza mchungaji wake.

*"Ndiyo," alisema, "inasema mito."*

Neno "mito" linaashiria ugavi mwingi. Na Wakristo wengi wanashuhudia "mito." Maisha haya ni kwa ajili ya Roho Mtakatifu.

Wakati wa uandishi huu (2020), shule nyingi, biashara, na majengo ya makanisa yamefungwa. Watu wengi hawana kazi. Maelfu wamekufa.

Leo, nilipokea barua kutoka kwa mwanamke Mkristo ambayo imeandikwa hivi: "Hakika Mungu anasonga na kuunda njia mpya za kuwafikia watu wake na kuwavuta wafuasi wapya kwake. Ni wakati mzuri sana wa kuwa hai na kushuhudia kazi ya mikono yake." Ninahisi mto unatiririka.

V. Raymond Edman alikuwa mchungaji mmisionari, na rais wa Chuo cha Wheaton. Akiwa ameathiriwa na maisha ya Hudson Taylor na wengine, aliandika kuhusu wazo la Taylor "la maisha yaliyobadilishwa:" "Ni maisha mapya badala ya zamani. Ni furaha badala ya uchovu, na mng'aro badala ya kufadhaika. Ni ushindi hata kwa machozi, na huruma ya moyo badala ya kuguswa. Ni unyenyekevu wa roho badala ya kujikweza, na uzuri wa maisha kwa sababu ya uwepo wa Yeye aliye Mpenzi kabisa."[168]

Katika kitabu cha *They Found the Secret*, Edman aliandika juu ya Wakristo ishirini ambao waligundua maisha ya kina ya Ukristo: "Ruwaza ya matukio yao ni sawa. Walikuwa wamemwamini Mwokozi, bado walikuwa na mizigo na kuchanganyikiwa, wasio waaminifu na wasiozaa matunda. Kisha wakaja kwenye shida ya kujisalimisha kwa moyo kabisa kwa Mwokozi, mkutano

168. V. Raymond Edman, *They Found the Secret* (Grand Rapids: Zondervan, 1960), 7.

pamoja naye katika kina cha ndani kabisa cha roho zao; nao wakamwona Roho Mtakatifu kuwa chemchemi isiyokwisha ya uzima na burudisho."[169]

Hudson Taylor alikuwa mwanzilishi wa Misheni ya China Inland na mmisionari mkuu. Hata hivyo, akiwa na umri wa miaka thelathini na saba, alimwaga moyo wake kwa mama yake katika barua. Aliandika, "Sikujua kamwe jinsi nilivyokuwa na moyo mbaya," na akaomba, "Ombeni kwamba Bwana aniepushe na dhambi, atanitakasa kabisa, anitumie kwa sehemu kubwa zaidi katika utumishi wake."[170]

John McCarthy, mmishenari mwenzake, alimwandikia Taylor kuhusu tukio lake yeye mwenyewe: "Kumruhusu Mwokozi wangu mwenye upendo afanye kazi ndani yangu mapenzi yake, utakaso wangu ndio ningeishi kwa neema yake. Kudumu, sio kujitahidi au kupambana; mwangalie mbali; kumwamini kwa uwezo wa sasa; kumwamini atawatiisha ufisadi wote wa ndani; kupumzika katika upendo wa Mwokozi mwenyezi."[171]

Taylor alipokuwa akiisoma barua hiyo, moyo wake uliguswa. Alisema, "Niliposoma, niliona yote. Nilimtazama Yesu; na nilipoona, oh jinsi furaha ilitiririka."[172]

Mtu ambaye alimtazama Taylor baada ya tukio hili alisema, "Alikuwa mtu mwenye furaha sasa, Mkristo mwenye furaha na mwenye furaha. Alikuwa akifanya kazi ngumu, aliyelemewa hapo awali, na mwishowe hakuwa na mapumziko mengi ya roho. Ilikuwa ikipumzika ndani ya Yesu sasa, na kumwacha yeye afanye kazi—ambayo inaleta tofauti kubwa."[173]

Ndiyo, Hudson Taylor alikunywa—na mito ya maji yaliyo hai ilitiririka kutoka kwake kwa Roho.

## NOVEMBA 17 — 321

# Kutakaswa kwa Imani Iliyo Ndani Yangu

*Nikikuokoa na watu wako, na watu wa Mataifa, ambao nakutuma kwao; uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu;*

169. Edman, *They Found the Secret*, 9.
170. Edman, *They Found the Secret*, 18.
171. Edman, *They Found the Secret*, 18
172. Edman, *They Found the Secret*, 19.
173. Edman, *They Found the Secret*, 17.

*kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.*
*Matendo 26:17-18*

Mnamo mwaka 1917, wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia, wanajeshi wa Uingereza walipiga kambi katika jangwa la Misri. Waliogopa. Vita viliendelea kuwazunguka, na marafiki zao walikuwa wakiuawa.

Wakati huohuo, kasisi alihamia kati vikosi vya askari. Alishauri, alitia moyo, aliomba, alihubiri, alifundisha, na kufanya mazishi. Hakuwa maarufu, lakini kila mtu aliyemfahamu alijua kwamba alikuwa mtu wa Mungu—mtu wa imani.

Siku moja, kasisi huyo aliugua na kupata maumivu ya tumbo. Lakini alichelewesha kutafuta matibabu kwa sababu alihisi kuwa wanajeshi ndio wanapaswa kutanguliza. Alipofika kwa daktari, alikuwa amechelewa sana - ugonjwa wa uvimbe kwenye kibole ulichukua maisha yake. Alikuwa na umri wa miaka arobaini na tatu tu.

Mke wake alikuwa mwaminifu. Kila alipohubiri au kufundisha, aliandika yote aliyoyasema, na mwaka 1927, alichapisha kitabu chake cha kwanza. *My Utmost for His Highest, kilichoandikwa na* Oswald Chambers, bado kinachapishwa leo na kinachukuliwa kuwa kitabu maarufu zaidi cha ibada binafsi ulimwenguni. Sasa, zaidi ya miaka mia moja baada ya kifo chake, Oswald Chambers, kupitia imani yake, bado anazungumza (Waebrania 11:4).

Kama mtume Paulo, Oswald Chambers alitumwa kuyafungua macho ya watu, kuwageuza kutoka gizani na kuingia kwenye nuru, kutoka kwa nguvu za Shetani hadi kwa Mungu, "Kisha wapate msmaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa Imani iliyo kwangu mimi [Kristo]" (Matendo 26:18). Zaidi ya hayo, hakuishia kwenye msamaha wa dhambi, bali alichukua wasikilizaji wake ndani zaidi. Katika kitabu chake, anaandika juu ya utakaso katika matukio ishirini na moja tofauti; pia hufanya marejeo mengine mengi kwa kweli zinazohusiana.

Baada ya kuzungumzia ondoleo la dhambi, Chambers alitangaza, "Kisha inafuata ile kazi kuu ya pili ya neema 'urithi miongoni mwao waliotakaswa.'"[174] Chambers alitoa changamoto kwa watu katika siku zake na katika siku zetu:

> Tunapoomba kutakaswa, je, tumejiandaa kukabiliana na kiwango cha vifungu hivi? . . . . Itatugharimu kupunguzwa sana kwa maslahi yetu yote duniani, na upanuzi mkubwa wa maslahi yetu yote kwa Mungu. Utakaso unamaanisha kuzingatia sana mtazamo wa Mungu. Utakaso unamaanisha

---

174. Oswald Chambers, *My Utmost for His Highest* (Uhrichsville, OH: Barbour Publishing, 1963), Januari 10.

kufanywa kitu kimoja na Yesu ili tabia iliyomtawala itatutawala . . . . Je, tuko tayari kusema—Bwana, nifanye kuwa mtakatifu jinsi unavyoweza kumfanya mwenye dhambi aokolewe kwa neema?[175]

Katika sehemu nyingine, Chambers anaandika, "Utakaso sio wazo langu la kile ninachotaka Mungu anifanyie; utakaso ni wazo la Mungu la kile anachotaka kunifanyia, naye hana budi kuniingiza katika mtazamo wa akili na roho ambapo kwa gharama yoyote nitamwacha anitakase kabisa."[176]

Niko tayari! Je, wewe?

NOVEMBA 18 **322**

# Hatazidi Sana

*Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu zawadi nzuri,*
*je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa*
*Roho Mtakatifu hao wamwombao!*
*Luka 11:13*

Miezi tisa baada ya kukutana na Yesu Kristo, Richard Halverson, chaplaini wa zamani wa Seneti ya Marekani, alianza kusoma kitabu cha Oswald Chambers '*My Utmost for His Highest*.' Kuanzia hapo na kuendelea, Halverson alisoma mara kwa mara kitabu hiki cha ibada kwa maisha yake yote. Kuhusu kitabu hicho alisema, "Hakuna kitabu isipokuwa Biblia ambacho kimeathiri maisha yangu na Kristo katika viwango vya kina na vya kukomaa hivi."[177]

Oswald Chambers alikuwa amemkubali Kristo kama mtoto. Akiwa mtu mzima, alipokuwa akifundisha katika Chuo cha Dunoon, Chambers alisikia F. B. Meyer akizungumza kuhusu Roho Mtakatifu. Baadaye, alienda kwenye chumba chake na kuomba kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, lakini hakuna jibu lililoonekana kuja. Kwa miaka minne alijitahidi.

Kisha Luka 11:13 ikamjia. Siku moja, katika mkutano wa hadhara, Chambers alisimama na kudai kipawa cha Roho Mtakatifu, akitoa mfano kutoka kwa Luka 11:13. Hakuwa na maono ya kipekee, lakini siku chache baada ya kuzungumza kwenye mkutano, watu arobaini walijitokeza. Wakati

175. Chambers, *My Utmost*, Februari 8.
176. Chambers, *My Utmost*, Agosti 14.
177. Richard Halverson, "Introduction," Oswald Chambers, *My Utmost for His Highest* (Uhrichsville, OH: Barbour Publishing, 1963).

rafiki yake alimkumbusha kwamba alikuwa amedai Roho Mtakatifu, na kwamba Yesu alisema, “Mtapokea nguvu” kutoka kwa Roho, ghafla, baada ya kipindi kifupi, jambo fulani lilitokea ndani yake. Alibadilishwa. Alishuhudia, “Upendo ni mwanzo, upendo ni kati, na upendo ni mwisho. Baada ya yeye kuingia, unachokiona ni ‘Yesu pekee, Yesu milele.’’’[178] Athari ya kazi hii ya Roho inatiririka kupitia maneno ya Chambers katika kitabu chake *‘My Utmost for His Highest:* “Yesu alisema, ‘Wakati yeye, roho wa kweli, atakapokuja . . . atanitukuza.’ Ninapojikabidhi kwa ufunuo unaofanywa katika Agano Jipya, ninapokea kutoka kwa Mungu kipawa cha Roho Mtakatifu ambaye anaanza kunifasiria kile ambacho Yesu alifanya; na anafanya ndani yangu kwa upendeleo yote ambayo Yesu alinifanyia bila upendeleo.” [179]

Katika kitabu kingine cha ibada, Chambers anasema, “Taratibu tunapaswa kuunda matembezi yetu na mazungumzo katika mstari wa kanuni za Yesu Kristo jinsi Roho Mtakatifu anavyozitumia katika hali zetu. Mahubiri ya Mlimani sio kifungu cha sheria na kanuni: ni taarifa ya maisha tutakayoishi wakati Roho Mtakatifu anapata njia yake pamoja nasi.”[180]

Kwenye sehemu nyingine katika kitabu hicho, Oswald anasisitiza tena, “Kamwe huwezi kufika mbali zaidi mpaka uwe tayari kufanya jambo hilo moja. Roho Mtakatifu atakipata ndani yako kitu kimoja kisichoweza kuzuilika, lakini hawezi kukishika isipokuwa kama uko tayari kumruhusu.”[181]

Jinsi alivyokuwa makini kwa Roho Mtakatifu. Jiwe la msingi katika makaburi ya kijeshi huko Cairo, Misri, huashiria kaburi la Chambers. Maneno yafuatayo yameandikwa juu ya jiwe lake la msingi: “Je! Ni kiasi gani zaidi Baba yenu wa mbinguni atawapa Roho Mtakatifu kwa hao wamwombao.”[182]

**NOVEMBA 19** **323**

# Glasi Imejaa

*Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna*
*ufisadi; bali mjazwe Roho.*
*Waefeso 5:18*

178. V. Raymond Edman, *They Found the Secret* (Grand Rapids: Zondervan, 1960), 47.
179. Chambers, *My Utmost*, Novemba 29.
180. Chambers, *My Utmost*, Julai 25.
181. Chambers, Oktoba 8.
182. Edman, *They Found the Secret*, 49.

Fikiria kwamba ninakuja kwenye mlango wako wa mbele na glasi ya maji mkononi mwangu na kuomba maji. Unanijua vyema, kwa hivyo unasema, "Bila shaka. Ingia ndani."

Unaniongoza kuelekea kwenye sinki yako ya jikoni, na mimi nafungua bomba. Glasi inajaa—kujaa nusu, kujaa theluthi-mbili, kujaa kabisa hadi pomoni. Ninafunga bomba.

Lakini basi, kwa sababu fulani, ninafurahi sana. Baada ya kuiweka glasi iliyojaa kwenye kaunta, ninaanza kusema kwa hamaki, "Glasi mejaa! Glasi imejaa!"

Tukio hili linanisisimua sana hivi kwamba ninampata mmoja wa jamaa zenu akitazama runinga sebuleni na kuripoti, "Glasi imejaa!"

Haionekani kuwa sawa kuzuia kusambaa kwa habari, kwa hivyo ninaenda katika eneo la majirani wako. Kwa juma moja, ninamwambia kila mtu ninayekutana naye, "Glasi imejaa!"

Hatimaye, ninarudi nyumbani kwako, jikoni yako, kaunta yako, glasi yangu, nikiwa bado nikisema kwa sauti yenye hamaki, "Glasi imejaa!"

Lakini kwa mshtuko, naona glasi haijajaa tena. Wakati nilitumia juma moja nikifurahi juu ya tukio mmoja hapo awali wakati glasi ilijazwa, mchakato wa polepole wa uvukizi ulipunguza kiwango cha maji. Glasi haijajaa tena!

Hebu turudie tukio hili la awali. Nimerudi kwenye sinki yako ya jikoni, nikijaza glasi nyingine ya maji, sawa kabisa na glasi ile ya kwanza. Glasi inajaa—imejaa–nusu, imejaa theluthi mbili, imejaa hadi pomoni. Lakini basi, badala ya kuzima bomba, niliiacha iendelee kutiririka.

Sasa glasi imejaa- na inafurika hadi kumwagika. Haijalishi ni kiasi gani uvukizi huondoa baadhi ya maji, bomba linalotiririka—chanzo—siku zote ni kikubwa kuliko uvukizi. Nafurahi. Glasi imejaa-na inafurika!

Glasi hizi ni kama aina mbili za Wakristo. Wengine huja kwa Mungu na kujazwa na Roho Mtakatifu lakini wanaonekana kuweka msisitizo wao wote katika kipindi cha nyuma walipokuwa wamejazwa. Wakati huo huo, wamevukiza.

Wakristo wengine huja kwa Mungu, wamejazwa na Roho, na *wanaendelea* kutumia rasilimali za kimungu. Waumini hawa hawakujazwa tu bali pia kufurika. Kwa maneno mengine, mara Roho atakapokujaza:

- Weka wazi; endelea kupokea kutoka kwa chanzo.
- Endelea kuomba, kutii, na kusoma Neno.
- Kama 1 Wathesalonike 5:19 inavyosema, "Msimzimishe Roho."
- Kama Waefeso 4:30 inavyosema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu."

- Kama Wagalatia 5:25 inavyosema, “Kwa kuwa tunaishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho.”
- Kama vile mtu fulani alisema, “Kaa kimaya asu useme machache pale ambapo utukufu unatoka!”

Paulo katika Waefeso 5:18 ni, “Mjazwe Roho.” Je, umejazwa? Je, umeyeyuka? Umebaki kujazwa? Je, unafurika? Ikiwa umejazwa na Roho, ukiendelea kuishi katika Roho, na kama unafurika, utakuwa na vya kukutosha wewe na wengine pia. Ni kama mwanamke aliyemwendea mchungaji wake kwa furaha, akisema, “Kikombe changu kinafurika! Kikombe changu kinafurika! Nifanye nini?”

Akajibu, “Nenda ukamgawie yeyote!”

Imejaa - na inafurika!

**NOVEMBA 20** **324**

# Kufurika

*Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho; mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu; na kumshukuru Mungu Baba sikuzote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo. Hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo.*
*Waefeso 5:18-21*

Ikiwa una ziwa au bwawa kwenye shamba lako na maji hutiririka ndani lakini hakuna maji yanayotoka, basi unajua kuwa maji yatasimama na hayatakuwa na afya. Vivyo hivyo, katika maisha ya kiroho, mara Mkristo anapojazwa na Roho, lazima kuwe na njia za kufurika kiroho. Kulingana na kifungu chetu cha Waefeso, pindi tu Mkristo anapojazwa na Roho, kuna njia tatu za asili za kufurika huko: sifa, shukrani, na utii.

Miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa nikipitia kipindi kigumu maishani mwangu. Sikuwa nikikabiliana inavyofaa na mafadhaiko—nililalamika kwa wengine kuhusu mzigo wangu wa kazi nyingi. Mara nyingi nilishikilia juu ya kujitolea kwangu na malipo duni. Nilijigamba juu ya wengine kwa sababu ofisi ya nyumbani haikuthamini thamani kubwa ya kazi yangu. Hatimaye, nilizinduka. Nilitambua kwamba, badala ya kulalamika, nilipaswa kusifu; badala ya kulalamika, ningepaswa kutoa shukrani; badala ya kujiinua,

ninapaswa kuwa nikitii n kujitoa. Kwa hakika, mara tu nilipoanza kusifu, kushukuru, na kutii, njia za kufurika zilifunguliwa katika nafsi yangu.

Baada ya Paulo kutaja utii katika 5:21, anaeleza yote juu ya mada:

- Enyi wake, watiini waume zenu (5:22).
- Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa (5:25).
- Watoto, watiini (au nyenyekeeni) wazazi wenu (6:1).

Lo, huo ni utii mwingi. Tunawezaje kushughulikia madai mengi hivyo? Katika utamaduni wa Marekani, watu hawashughulikii mahitaji kama haya vizuri. Baada ya kutoka kazini, mtu ambaye amekuwa chini ya shinikizo kutoka kwa bosi wake anaweza kuingia kwenye nyumba na kumfokea mke wake, "Nipatie bia!"

Paulo ana jibu bora zaidi: "Msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi. Bali mjazwe roho" (5:18). "Mjazwe" inarejelea sasa—*endelea* kujazwa na Roho. Ushuhuda wa jambo hili la lazima ni kwamba Wakristo wa Agano Jipya mara nyingi walipokea ujazo mpya wa Roho katikati ya hali zenye shinikizo kubwa (Matendo 4:31).

E. Stanley Jones alikuwa mmoja wa majitu ya kiroho ya kanisa la Methodisti. Aliongoka kwa Kristo akiwa kijana. Baadaye, baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu, alijitoa kwa ajili ya utumishi wa kimisionari. Kazi yake ya kwanza ilikuwa India, ambako aliwekwa kuwa msimamizi wa kituo cha misheni na wafanyakazi mia tano. Angestahiki kustaafu tu baada ya miaka kumi ya huduma. Baada ya muda, Jones alipata shida ya neva. Alijaribu kuchukua likizo, kutumia muda huko milimani, na kurudi nyumbani huko Baltimore. Bado, baada ya haya yote, bado aliugua. Lakini, kwa hisia ya wajibu, alirudi kwenye kazi yake ya misheni. Huko Lucknow, alihudhuria ibada za ufufuo zilizoongozwa na Tamil David. Wakati Jones alipokuwa amepiga magoti nyuma ya kanisa, Mungu alimwuliza, *"Je, uko tayari kwa kazi ambayo nimekuitia?"*

Jones akajibu, "Hapana, Bwana, nimekwisha maliza. Nimefikia mwisho wa rasilimali zangu, na siwezi kuendelea."

Mungu akajibu, *"Ikiwa utanikabidhi tatizo hilo na usijali kulihusu, nitalishughulikia."*

"Bwana," akasema, "nimewacha kulalama juu ya hilo papa hapa."

Ghafla, Jones alijazwa na kufurika kwa nguvu, amani, uwezo, na hisia ya kutosheka.[183] Mtu ambaye hapo awali alikuwa amejazwa Roho alijazwa tena

183. E. Stanley Jones, *A Song of Ascents* (Nashville: Abingdon Press, 1968), 89–90.

upya na Roho. Tangu wakati huo na kuendelea, aliendelea kujazwa na kuingia katika kipindi tajiri zaidi cha huduma yake.

Rafiki Mkristo, ujazwe na Roho, na uendelee kujazwa na Roho. Furika kwa sifa, shukrani, na utii.

NOVEMBER 21 **325**

# Upendo katika Alhzeimer's

*Wapenzi, na mpendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu.*
*1 Yohana 4:7*

*Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno.*
*Waefeso 5:25-26*

Wakati wa maandishi haya, Nancy, mke wangu, amekuwa na ugonjwa wa Alzheimers kwa karibu muongo mmoja. Kufikia sasa, kumbukumbu yake ya muda mfupi ni fupi sana, na sisi huhudhuria mikutano ya chama chetu cha Alzheimer kwa kawaida. Kuna tofauti nyingi sana kati ya wagonjwa waliougua ugonjwa huu; hivyo, sidai kwamba ninachoshiriki ni kweli kwa wagonjwa wote na walezi wao.

Kwa namna fulani, kwa maombi, neema ya Mungu, na imani yetu ya Kikristo, Nancy na mimi tumeshuhudia uhusiano maalum, wa upendo na wa kushiriki. Mara kwa mara, ninapokuja kwenye meza ya kiamsha kinywa, napata barua ambayo ameniachia usiku uliopita. Hapa kuna moja ambayo nimepata hivi karibuni:

> *Kwa kijana wangu mtanashati, mzuri anayenitunza kwa upendo na huruma.*
>
> *Asante kwa njia nyingi ambazo unanifanya nihisi kuwa ninapendwa na kujaliwa. Tazamia safari zetu. Mshukuru Mungu kila siku kwa maisha yetu yenye matokeo kwa baraka na mwongozo wa Baba yetu wa mbinguni. Ninakupenda zaidi kila siku.*
>
> *Nan, mpenzi wako*

Kwa hiyo Nancy anaposema kuwa haipati simu yake na najua itabidi nimsaidie kuitafuta, naendelea kumuonyesha upendo licha ya kukata tamaa. Na, kwa sababu ya jinsi anavyonipenda tena, si vigumu kufanya.

Je, kuna hali ngumu katika maisha yako ambayo inaweza kusaidiwa na kipimo kipya cha upendo?

NOVEMBA 22 **326**

# Sema tu Asante

*Furahini siku zote; ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.*
*1 Wathesalonike 5:16-18*

Alisikitishwa na jinsi mtu fulani alivyokuwa akimtendea. Tulipokuwa tukizungumza, alisimulia jinsi, zamani, mtu huyu alivyobadilika na kuwa bora kama jibu la sala. Alipokuwa anakumbuka haya, uso wake ukachangamka, akatabasamu. Kwa pamoja, tulimshukuru Mungu kwa majibu yaliyopita huku pia tukiomba mapya.

Ona kwamba maagizo ya Paulo ni kwamba tunapaswa kuomba na kushukuru si *kwa* hali zote bali *katika* hali zote. Hata katika hali ngumu ya sasa, unaweza kuhisi kitu kizuri katikati yake. Zaidi ya hayo, "tunajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema" (Warumi 8:28)—na, kama mtu mmoja alivyosema, "mambo yote" yanajumuisha "hata kile ambacho hutumwa na Ibilisi." Kutoa shukrani kwa Mungu huleta utukufu ufaao kwa Mungu. Zaidi ya hayo, kumshukuru Mungu kwa majibu ya zamani kwa maombi hujenga imani ya kumtumaini kwa majibu ya wakati ujao.

Na kutoa shukrani kwa watu. Katika enzi iliyoandaliwa na mtazamo wa kustahiki na, "Nitafaidika na nini?" jinsi inavyofaa kusema "asante." Kusema asante huonyesha kwamba mtu mwingine ni muhimu, amechangia katika maisha yangu, na anathaminiwa.

Paulo alipoliandikia kanisa la Filipi, alisema, miongoni mwa mambo mengine, "Lakini ilikuwa vyema kwenu kushiriki katika taabu zangu"; "Mlinitumia msaada zaidi ya mara moja nilipokuwa mhitaji"; na, "Nimeshibishwa tele, kwa kuwa sasa nimepokea kutoka kwa Epafrodito

zile zawadi mlizotuma" (Wafilipi 4:14, 16, 18). Unafikiri Wafilipi walihisije waliposoma hilo?

Hivi sasa, ninayo barua ya shukrani nami hapa. Inasema hivi, kwa sehemu: "Umefanya mambo haya yote ya nje, lakini kuna mambo ya ndani pia. Umenitia imani kama mume, baba, mchungaji na kiongozi. Umeathiri sana safari yangu ya kiroho na Mwokozi wetu. Asante."

Unafikiri nilihisije nilipousoma ujumbe huo? Je, ungehisije?

Sasa lazima nipumzike ili niandike ujumbe shukrani. Je, unahitaji kuandika moja pia?

**NOVEMBA 23** **327**

# Kufichwa Pamoja na Kristo Katika Mungu

*Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa*
*pamoja na Kristo katika Mungu.*
*Wakolosai 3:3*

Niliogopa kuwa nimefanya kosa kubwa. Hakukuwa na shaka kwamba Mungu alinitakasa kabisa (1 Wathesalonike 5:23) usiku huo wa Septemba. Moja ya kweli kubwa za tukio hilo ni kwamba Chic Shaver wa zamani alikufa. Mahali pa utu wangu wa kale palikuwa na usafi wa ndani, amani, na upendo kupita vile nilivyowahi kupata kujua—mkuu sana kiasi kwamba niliimba wimbo wa Charles Wesley "Upendo Mtakatifu, Upendo Wote Hushinda" mara ishirini katika saa ishirini na nne zilizofuata. Aya ya pili hasa ilizungumza nami:

*Nipulizie, Nipulizie Roho wako wa upendo*
*Katika kila titi lisumbukalo!*
*Hebu sisi sote ndani yako turithi;*
*Hebu tupate pumziko hilo la pili.*
*Ondoa asili yetu ya kufanya dhambi;*
*Uwe Alfa na Omega.*
*Mwisho wa imani, kama ulivyo mwanzo wake,*
*Iweke huru mioyo yetu.*[184]

184. Charles Wesley (words) and John Zundel (music), "Love Divine, All Loves Excelling," *Sing to the Lord: Hymnal* (Kansas City, MO: Lillenas Publishing Company, 1993), #507.

Kwa miezi kadhaa, nilitafuta ujazo wa Roho Mtakatifu kama tiba ya dhambi zangu za ndani na ukosefu wa nguvu za kiroho. Na sasa - jibu!

Lakini basi kosa langu likaja. Lilikuwa hila. Nilidhani kimakosa kwamba, kwa sababu Mungu alinikomboa wakati huo, ningekuwa na ushindi wa moja kwa moja katika kila hali ya siku zijazo yenye changamoto niliyopitia. Nilikosea jinsi gani! Niligundua nilipaswa kumtegemea Kristo dakika baada ya muda na kumtegemea Mungu sana katika kila jaribu la maisha. Huu ulikuwa uhusiano wenye nguvu, unaoendelea! Kujazwa na Roho, naam, lakini pia:

- "Ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho" (Warumi 8:4).
- "Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa mhuri hata siku ya ukombozi" (Waefeso 4:30).
- "Msimzimishe Roho" (1 Wathesalonike 5:19).
- "Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho" (Wagalatia 5:25).

Au, kama Everett Lewis Cattell alivyosema kwa hekima sana, "Sasa silaha kuu ya majaribu inayotumiwa na Ibilisi dhidi ya moyo uliojisalimisha na mtakatifu ni kujaribu kuivuta nafsi kutoka mahali pake pa siri na, kwa namna fulani, angalau, kuipata. Kuanzisha tena kwa kujitegemea kutoka kwa Mungu."[185]

**NOVEMBA 24** **328**

# Aonekane Kuwa Mwaminifu

*Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili,*
*ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu.*
*1 Wakorintho 4:2*

Kitaaluma, alikuwa mwalimu wa shule na mwalimu wa ibada za chekechea kanisani kwa wito wa Mungu. Sikuwahi kumsikia akifundisha darasa la kuchosha—aliwaombea washiriki wa darasa lake, akawatembelea, wakati mwingine alilia alipokuwa akifundisha, na mara nyingi alifurahi. Aliishi katika furaha ya utimilifu wa utakaso wa Roho. Ndiyo, tunda la Roho linajumuisha si tu upendo, furaha, na amani bali pia uaminifu (Wagalatia 5:22).

185. Everett Lewis Cattell, *The Spirit of Holiness* (Grand Rapids: Eerdmans, 1963).

Jim na Anita walipohama kutoka kwenye jimbo, hawakutulia kanisani, na walianza kuyumba-yumba kiroho. Mwalimu wa ibada ya shule ya Jumapili Ferne hakuweza kulikubali hili—aliwafuata kwa sala, upendo, kujali, na mawasiliano ya mara kwa mara. Aliendelea hivyo hadi aliposikia kwamba Jim na Anita wamerudi kwa Mungu na kanisani.

Ferne alipokuwa na wasiwasi kuhusu mmoja wa wasichana wadogo katika darasa lake la shule ya umma, aliamua kupiga simu nyumbani ili kukutana na wazazi wa msichana huyo. Alipokuwa akiongea na wazazi, alitambua kwamba sehemu ya kile ambacho nyumba hiyo ilihitaji ni maisha ya kiroho. Alisimulia hadithi yake mwenyewe ya kuwa mwasi mwenye umri wa miaka ishirini na moja, alipogundua kwamba mtindo wake wa maisha usingefaa, kumjua Yesu Kristo, na hatimaye kuona sehemu za maisha yake zikiendana.

Baada ya wazazi kusikia hadithi yake, walisema, "Ferne Long, umepata tunachokihitaji. Tutakuja katika kanisani lako Jumapili hii."

Hii ilikuwa wikendi ambayo angeenda likizo. Alikuwa na uhakika kwamba, kama angewaambia hangekuwa pale, familia hiyo changa isingekuja kanisani. Alijua kwamba maisha, wakati ujao, na nafsi ya mtu vilikuwa hatarini. Kwa hiyo Ferne aliamua kuahirisha likizo yake ili akae na familia hiyo mpya kanisani Jumapili hiyo. Zungumza juu ya uaminifu!

Haikushangaza wakati, kwenye mkusanyiko wa kila mwaka wa makanisa sitini au zaidi yaliyofanyiza wilaya hiyo, Ferne alipotunukiwa kuwa Mwalimu Bora wa Mwaka wa ibada ya chekechea ya watotom kanisani. Hilo linaonekana kuendana na kile ambacho Wakristo wengi wangependa kusikia wanapovuka kutoka ulimwengu huu hadi mwingine: "Vyema, mtumwa mwema na mwaminifu! Umekuwa mwaminifu kwa machache; Nitakuweka juu ya mambo mengi. Njoo ushiriki katika furaha ya bwana wako!" (Mathayo 25:21).

Bila shaka utatamani kuthibitishwa kuwa mwaminifu pia.

**NOVEMBA 25** **329**

# Uhuru na Utumwa

*Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli.*
*Yohana 8:36*

Huonyesha dhihaka usoni mwake anaposema kuhusu aina mbalimbali za watu wanaokera kwa sababu wana tabia ya kujiona kama wanajua kila kitu: "Unamaanisha nini hufanyi shughuli hiyo au huendi sehemu hizo? Je, dini yako haikupi uhuru wowote?" Na anajiona bora kwa sababu anaenda mahali ambapo hujali kwenda.

Baadhi ya Wayahudi wa siku za Yesu walikuwa na jamii ya hadhi ya juu pia. Lakini si Wayahudi wa kale wala wakosoaji wa upotovu wa leo wanaokaribia kuelewa maana ya uhuru. Wakristo wanaishi jinsi wanavyoishi kwa tamaa, huku wenye dhambi wakiishi chini ya mjeledi mkali wa bwana wao, yaani dhambi. Mpaka Mwana atakapomweka mtu huru, asili ya mwanadamu inakuwa utumwa wa dhambi.

Huniamini? Muulize Starr Daily. Starr alikuwa akioza "katika shimo" (kifungo cha upweke) la gereza, ambapo alikuwa na mkate na maji kama chakula na mawe kama kitanda. Chuki tu kwa mlinzi wake na mkuu wa gereza ndio ilimfanya aendelee kuwa hai. Kisha, katika usingizi wake usiku mmoja, Starr alikabiliwa na Yesu Kristo, mtu ambaye siku zote alikuwa amejaribu kuepuka. Kristo alipenyeza ndani kabisa ya nafsi ya Starr, na upendo wake ukatoa sumu yote ya dhambi nje. Alipoamka, kuta za kijivu karibu naye zilionekana tofauti. Lakini ilikuwa Starr ambaye alikuwa tofauti — kwa mara ya kwanza katika maisha yake, alikuwa na uhuru ndani.

**NOVEMBA 26** **330**

# Kukwazwa

*Busara ya mtu huiahirisha hasira yake;*
*Nayo ni fahari yake kusamehe makosa.*
*Mithali 19:11*

Amekwazwa! Ni rahisi kiasi gani watu hukwazika. Baadhi huonekana kana kwamba wamekuwa wakiisubiria nafasi ili wakwazwe.

Nilishangazwa na ripoti kutoka kwa mwanangu, Paul, kuhusu tukio la hivi majuzi katika maisha yake. Hapa ni baadhi ya maelezo kwanza.

Paul amekuwa na saratani nyingi mwilini mwake na kufanyiwa upasuaji mara nyingi ili kuzishughulikia. Upasuaji uliokuwa hatari zaidi ulikuwa wa kuondoa saratani kwenye shingo yake, ambayo pia ilihusisha kuondolewa kwa kitunza sauti chake. Sasa ili azungumze ni lazima afunike tundu la shingo

analotumia kupumua na kulazimisha hewa kupitia kinywa chake kuunda maneno. Kila maneno mengi, lazima asite, afunue tundu, na kuvuta pumzi. Matokeo yake, sauti yake ina kigugumizi, sauti mbaya. Halalamiki juu ya hili, lakini amekuwa akipokea matibabu ili kuboresha ubora wa sauti yake.

Hivi majuzi, Paul aliingia kwenye mazungumzo na kocha kwenye mchezo wa mpira wa wavu ambao Paul alikuwa refarii. (Anafanya hivi kwa filimbi ya kielektroniki.) Kocha alimwuliza Paul, “Unaendeleaje?”

Paul alijibu kwa sauti yake ya unyonge, na kocha akasema, “Inaonekana kama umepatwa na hali mbaya” (ikimaanisha homa mbaya).

Paulo alisema tu, “Hapana.”

Lakini muda kidogo baadaye, kocha alirudi na kumpa Paul dawa ya kupunguza makali ya kikohozi.

Nilipomsikia Paul akisimulia hadithi hii, nilijiuliza iwapo alihisi kukwazwa na kitendo kisichofaa kutoka kwa kocha huyo. Ilikuwa mbaya vya kutosha kuwa na saratani, sembuse kupoteza kitunza sauti chake—na sasa mtu ambaye hata hakujua ukweli alikuwa akimtolea dawa ya kupunguza makali ya kikohozi kwa mafua ambayo hakuwa nayo!

Lakini Paul hakukwazika—kwa kweli, alishukuru. Alifikiri ilikuwa vyema kwamba, kutokana na matibabu yake ya hivi karibuni, ubora wake wa sauti *ulipanda* hadi kiwango cha maumivu ya koo au homa. Hii ilikuwa ni uboreshaji! Paulo alikuwa na furaha na mtazamo chanya juu ya hilo.

Kwa muda mrefu, Paulo amekuwa akiishi chini ya baraka za Mungu. Mungu alimpa amani kubwa wakati madaktari waliposema kwamba wangemtoa kikoromeo chake. Anaangalia maisha kwa mtazamo tofauti na ule wa wengi. Anaishi katika maandiko yafuatayo: “Furahini katika Bwana siku zote” (Wafilipi 4:4); “Furahini siku zote, ombeni bila kukoma, shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu” (1 Wathesalonike 5:16–18). Amejifunza kwamba “Atakayekuza upendo husitiri kosa” (Mithali 17:9).

Zingatia yale ambayo umelazimika kukumbana nayo katika wiki iliyopita. Na kumbuka kwamba “ni kwa utukufu wa mtu kupuuza kosa.”

NOVEMBA 27 **331**

# Uovu Ndani Yangu, Sehemu Ya 1

*Basi kama lile nisilolipenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu.*
*Warumi 7:20*

Nilipokuwa mdogo, wazazi wangu hawakuniruhusu niwe na uhuru wa kuingia katika chumba chochote katika nyumba yetu. Lakini siku moja mahususi, niliruhusiwa kuingia sebuleni, ambayo ilikuwa na vitu vingi vinavyoweza kuvunjika. Mara moja nilivutiwa na trei nzito ya kioo (hizi zilikuwa siku kabla hatujamruhusu Yesu adhibiti sana nyumba yetu).

Nilichukua trei hiyo nzito ya majivu na kuiinua juu ya kichwa changu. Mama yangu aliona na kuamuru kwa ukali, "Usiiangushe trei hiyo ya majivu!"

Mara moja, niliiangusha na ikatapakaa kwenye chumba. Na niliilipia.

Ni nini kilinifanya nifanye hivyo? Paulo alikuwa amekwisha fahamu. Katika Warumi 7:9, aliandika, "Nami nilikuwa hai hapo, kwanza bila sheria; ila ilipokuja ile amri, *dhambi ilihuika*, nami nikafa." Kando na Mungu na neema yake, ninashangazwa na jinsi ninavyojionea maovu mengi ikiwa nitakuwa mwaminifu bila ukamilifu. Kando na uovu wa kimfumo na matendo maovu ya wengine, sina budi kushindana na uovu ulio ndani. Na hakika, uovu wa kimfumo ni matokeo ya kukusanya na kuzidisha ubaya wa mioyo mingi ya watu binafsi.

Warumi 7:19-20 inatuambia, "Kwa maana lile jema nilipendalo silitendi, bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo —ndilo ninaloendelea kutenda. Basi kama nisilolipenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile *dhambi ikaayo ndani yangu* ndiyo inayolitenda." Kuzingatia baadhi ya matukio katika maisha yangu kunathibitisha ukweli huu.

Nilipokuwa katika shule ya upili, mtu fulani alinipa kazi katika msimu wa kiangazi katika duka lake la samani. Hata hivyo, mwaka uliofuata, niliposoma katika gazeti kwamba bosi wangu wa zamani alikuwa na matatizo ya kifedha, nilifurahia sana kuripoti habari hizo kwa wengine. Je, kueneza habari hizo kulinifanya nijihisi bora zaidi kuliko yule aliyekuwa mkuu wangu? Je, hilo lilikuwa tatizo la moyo wangu? Yesu alisema, "Kwa maana mawazo mabaya hutoka ndani ya moyo wa mtu . . . wivu, kashfa, kiburi na upumbavu. Maovu haya yote hutoka ndani na kumtia mtu unajisi" (Marko 7:21–23).

Kama kijana, nilihisi kwamba nilikuwa nimesitawisha viwango fulani vya juu. Unyoofu ulikuwa jambo la kwanza kwangu, na nilikasirishwa na ukosefu wa uaminifu kutoka kwa wengine. Bado, nilipokuwa kwenye msongamano mkali, nilijikuta nikidanganya ili niondokane nao. Sikuthamini kile Paulo alisema: "Kwa hiyo, wewe mtu uwaye yote uhukumuye, huna udhuru; kwa maana katika hayo umhukumuyo mwingine wajihukumu mwenyewe kuwa na hatia; kwa maana wewe uhukumuye unafanya yale yale" (Warumi 2:1).

Nilianza kuhisi misukosuko ya kidini ndani yangu. Mtu fulani alipopendekeza kwangu kwamba njia ya kuelekea kwa Mungu ilikuwa kwa kupitia Yesu Kristo, nilishangaa sana. Niliwaza, *nitamfikia Mungu kwa njia yoyote nipendayo!* Nilijaribu-na sikufanikiwa. Katika ubinafsi wangu, bado sikuelewa maneno ya Yesu: "Mimi ndiye njia na kweli na uzima. Mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6).

NOVEMBA 28 **332**

# Uovu ndani Yangu, Sehemu ya 2

*Basi kama lile nisilolipenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu.*
*Warumi 7:20*

Kwa kushangaza, kama wanafunzi wawili vijana wa seminari, tulialikwa kuhubiri na kutoa ushuhuda wetu katika hafla ya uamsho wa wikendi kwenye kanisa kubwa. Mambo ya ajabu yalitendeka. Wengi walimtafuta Mungu hadharani, na mke wa kasisi alizungumza juu ya wenzi sita waliopokea msaada wa kiroho, akisema, "Ninathubutu kusema kwamba kila ndoa itaokolewa."

Nikiendesha gari kuelekea nyumbani, nilijiambia, "Jamani, sikutoa wito mzuri wa madhabahuni!"

Mara moja, Roho Mtakatifu akauambia moyo wangu, *"Mimi ni BWANA; ndilo jina langu; na utukufu wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa zangu"* (Isaya 42:8). Nilikemewa na kulazimishwa kutazama ndani kabisa ya moyo wangu.

Siku chache zilizopita, nilikuwa nikimwambia mke wangu juu ya zaidi ya miaka sitini ya kupendeza kuhusu kutoridhika kwangu juu ya suala fulani. Alisema, "Unanifokea." Neno lake lilionekana kuwa na nguvu kama la Roho.

Alikuwa sahihi; Nilimwomba msamaha, na niliomba msamaha wa Bwana, kutakaswa, na kutembea upya katika Roho.

Oswald Chambers alisema,

> Mwanzoni mwa jamii ya wanadamu, dhana ilikuwa kwamba Adamu angetawala kila kitu isipokuwa yeye mwenyewe. Alipaswa kuwa na mamlaka juu ya uhai duniani na angani na baharini, lakini hakupaswa kuwa na mamlaka juu yake mwenyewe—Mungu alipaswa kuwa na mamlaka juu yake. Jaribio lilikuja kwenye mstari huu—"Usitii, nawe utakuwa kama Mungu." Mwanadamu alichukua mamlaka juu yake mwenyewe na kwa hivyo akapoteza mamlaka yake juu ya kila kitu kingine. Kulingana na Biblia, tabia ya dhambi ni dai langu la haki yangu kwangu.[186]

Tunaweza pia kuelezea "dai langu la haki yangu kwangu"; kama "dhambi inayokaa ndani yangu" (Warumi 7:20). Nimepata majibu mawili tu kwa suala zima kama hilo. Tunahitaji msamaha kwa yale tuliyofanya hapo awali, lakini ni lazima tuende kwa undani zaidi.

Ninapata jibu la kwanza katika maneno ya Paulo katika Wagalatia 2:20: "*Nimesulubiwa pamoja na Kristo*; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu."

*Kusulubishwa* tu kwa nafsi yangu—"dai langu la haki yangu kwangu" au "dhambi inayoishi ndani yangu"—ni ya kina vya kutosha kushughulikia suala hili. Lakini mara nitakaposulubishwa pamoja na Kristo, nitahitaji jibu la pili, kutoka kwa Wagalatia 5:25: "*Tuenende* katika *Roho*." Nahitaji kutembea kwa kila dakika katika Roho.

## NOVEMBA 29 — 333

# Nimesulubishwa Pamoja na Kristo

*Maana mimi kwa njia ya sheria niliifia sheria ili nimwishie Mungu.*
*Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena,*
*bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili,*

186. Oswald Chambers, *My Utmost for His Highest* (Toronto: McClelland and Steward Limited, 1935).

*ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda,*
*akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*
*Wagalatia 2:19-20*

Kukamata kwa kuvutia—miguu chini juu ya mstari—funga bao. Kisha dansi la ushindi - au, kwa usahihi zaidi, dansi la ushindi. Yenye upekee. Mchezaji huyo anaonyesha mafanikio yake: "Nilikudanganya; Nilikushinda; mimi navutia; Ninashinda, unashindwa." Sote tumeiona hapo awali—kuinuliwa kwa "Kujigamba mwenyewe."

Kile ambacho wachezaji fulani hufanya kwenye mpira wa miguu, mtume Paulo (wakati angali Sauli) alifanya na dini. Akiwa Mfarisayo mkuu, mnyofu kabisa, na mdini sana, angeweza kujisifu, "Nalikuwa nikiendelea katika Dini ya Kiyahudi kuliko Wayahudi wengi wa rika langu mwenyewe" (Wagalatia 1:14). Huku kulikuwa ni "Kujigamba" kabisa. Hata hivyo, katika nyakati zake nzuri, Sauli alijua hakuwa ameishika sheria ya Mungu kwa mafanikio. Kama mtume Paulo, hatimaye alimalizia, "Kupitia sheria niliifia sheria." Lakini kushindwa huko kulifungua mlango wa jambo lililo bora zaidi: "ili nipate kuishi kwa ajili ya Mungu" (2:19).

Umewahi kufurahia katika "Kujigamba"?

- Nilifaulu mtihani huo.
- Nilimdanganya.
- Nilimwambia jambo moja au mawili.
- Nilimpata vizuri zaidi.
- Nilimwonyesha.
- Nilimwambia pa kushuka.

Huko "Kujigamba" ni kukali, kuna msukumo, ni dhahiri, na si kuzuri sana. Paulo alijua tatizo lake lilikuwa kubwa kuliko sheria; ilikuwa nguvu inayotawala ya "Kujigamba." Baada ya uongofu wake kwa Kristo, aligundua kwamba, kati ya maisha chini ya dhambi na maisha chini ya ukuu wa Kristo, kuna nchi ya maisha isiyo na mwanadamu chini ya udhibiti wa pamoja—na haifaulu. Kwa hiyo Paulo aliupeleka msalabani: "Nimesulubishwa pamoja na Kristo" (2:20). Kifo cha "Kujigamba" kilikuwa jibu pekee—hapo ndipo Kristo angeweza kuishi kwa wingi na kwa ukamilifu kupitia kwake. Kusulubishwa kulikuwa kusalimu amri kwa shida. Ilikuwa imefanyika huko nyuma, lakini ilikuwa bado inafanya kazi. Haikuwa imepoteza nguvu zake.

Jim, mwanafunzi wa huduma, aliketi kando ya dawati kutoka kwa profesa wake. Ingawa alikuwa amemkubali Kristo, nguvu nyingine kuu bado ilikuwa ikifanya kazi ndani yake. Alikiri, "Ninapenda kupata pesa. Kichwani mwangu najua nilipaswa kujisalimisha, lakini kihisia nimeunganishwa nayo.

Huwa natoa zaka yangu, lakini sipendi kufanya hivyo." Profesa alimhimiza ayakabidhi maisha yake yote yaliyosamehewa kwa Mungu (kuweka wakfu); kuomba utakaso kamili au kusulubiwa kwa ubinafsi wake uliobaki (kusafisha au kusulubisha); na kutoa msaada kwa imani na kumwamini Roho kufanya hivyo (kudai). "Kujigamba" kwa Jim kulitawaliwa sana na pesa hivi kwamba alisali, "Ee Mungu, nisaidie niwe tayari kuwa tayari." Aliweka kichwa chake kwenye dawati na kulia. Tena na tena alisema, "Sawa, sawa, sawa," huku akisalimisha suala baada ya suala. Ghafla, alitazama juu na kumwambia profesa wake, "Tamaa ya pesa imetoweka!"

Profesa akauliza, "Ni nani anayekudhibiti?"

"Roho Mtakatifu," Jim akajibu.

Profesa aliagiza, "Andika hivi: Mei 9, saa 4:15 jioni, Jim alikufa."

Jim aliendelea kufurahi, akisema, "Roho Mtakatifu anasisimua zaidi kuliko pesa. Sijisikii nimefungwa tena."

Si ajabu Jim na Paulo wote wawili wangeweza kushuhudia, "Nimesulubishwa pamoja na Kristo." Wote wawili wakawa njia zenye tija kwa injili.

**NOVEMBA 30** **334**

# Ndugu katika Kristo

*Tokea sasa, si kama mtumwa, bali zaidi ya mtumwa,*
*ndugu mpendwa; kwangu mimi sana, na kwako*
*wewe zaidi sana, katika mwili na katika Bwana.*
*Filemoni 1:16*

Paulo aliandika maneno haya kuhusu Onesimo, mwongofu wa hivi karibuni ambaye alikuwa akirudi kwa bwana wake wa zamani, Filemoni. Ni nini kilicho na nguvu zaidi ya kuwainua wasio na uwezo ("bora kuliko mtumwa, kama ndugu mpendwa") kuliko hadithi ya injili? Ni nini kinachoweza kufanya zaidi katika kutatua machafuko ya wafanyakazi na ghasia za ubaguzi wa rangi kuliko kuwaleta wakuu na mfanyakazi, mweusi na mweupe, katika undugu kwa kumjua Yesu Kristo?

Walimwita "malaika aliye katika mpingo"—mwana wa mfalme, alitekwa na kabila la Waafrika lililopigana, akauzwa utumwani, na kushikiliwa ili wapate fidia. Vipigo vyake vya kila siku vikawa vikali sana hadi kijana

huyo akakimbia. Baadaye, alipata kazi kwenye shamba la kahawa, na hapo akampata Kristo. Muda si muda, aliita maombi kuwa ni "kuzungumza na Baba yangu." Alisafiri hadi Marekani kutafuta mtu wa kumwambia kuhusu Roho Mtakatifu. Aliishi karibu sana na Mungu kiasi kwamba, katika usiku wake wa kwanza huko Marekani, aliwaongoza watu kumi na saba kwa Kristo. Aliwahi kutekwa nyara, kufanywa mtumwa, na kukandamizwa, lakini mwishowe, Sammy Morris alikuwa ndugu yangu katika Kristo.

**DESEMBA 1** **335**

# Mungu Alinitakasa!

*Tokea sasa usinywe maji tu lakini tumia mvinyo kidogo, kwa ajili ya tumbo lako, na magonjwa yakupatayo mara kwa mara.*
*1 Timotheo 5:23*

Hakuna shaka kuhusu hilo—nilijua Mungu alikuwa ameniokoa! Usiku wa Novemba 20, dhambi zangu zilisamehewa; Kristo aliingia katikati ya maisha yangu; Mungu akawa halisi; upendo, furaha, na amani vikawa hisia zangu kuu. Niliendelea na uhusiano wa siku baada ya siku, kuishi na Yesu. Bibilia ikawa kitabu chenye kusisimua; Nilikuwa nikipokea majibu ya maombi; kwa neema, nilipinga majaribu ya zamani. Nilikuwa kanisani kila wakati milango ilikuwa wazi. Nilikuwa nikiwaambia wengine kile ambacho Yesu alikuwa amenifanyia na kuwaleta marafiki zangu kanisani.

Miezi sita baadaye, nilikuwa katika hali mbaya. Licha ya kuendelea kuwa na uhusiano na Mungu na baraka alizonipa, hasira mbaya ilianza kutokea kwenye sehemu ya chini ndani kabisa katika nafsi yangu. Watu fulani, hata marafiki Wakristo, walinitendea kwa njia isiyofaa. Nilijua kwamba Wakristo wanapaswa kuwa wenye upendo, kwa hiyo niliuma meno yangu, nikakunja taya yangu na kusema, "Jifanye umpende mtu huyu!" Lakini sikuweza kufanya hivyo.

Uchungu, chuki, kukosa subira, wivu, na kiburi vilianza kupanda kutoka ndani yangu. Pamoja na hayo, nilihisi ukosefu wa nguvu za kiroho—ingawa nilikuwa nikishiriki imani yangu na wengi, wachache walikuwa wakibadilishwa. Nilijiuliza, "Je, huu ndio Ukristo wangu bora zaidi ambao naweza kuwa?"

Kisha, baadhi ya mwanga ulianza kunijia. Niliisikia kwenye mahubiri; soma katika Bibilia; nikaisikia katika wimbo; niliupata katika ushuhuda wa kibinafsi. Nilianza kusikia misemo kama "utakaso mzima"; usafi wa moyo"; "aliyesulubishwa pamoja na Kristo"; "pumziko la imani"; "utakaso kamili." Kila siku, kwa kufuatanisha, niliomba ili nipate jibu la Mungu kwa pambano langu.

Kisha, katika ibada moja ya Jumapili usiku, Mungu alizungumza na moyo wangu na kunisukuma kwenda madhabahuni kwa maombi. Mungu akaniuliza, "Umekuwa ukiomba nini kwa muda wote huu?"

Nilijibu, "Bwana, nitakase."

Ghafla, kile nilichohisi kama mshtuko wa kupigwa na umeme kilipita mwilini wangu wote na nilikuwa nimeinama chini. Ingawa nilikuwa na afya kamili mwenye umri wa miaka ishirini na mmoja, nilihisi dhaifu sana hivi kwamba nilifikiri nitakufa. Kisha nikagundua, "Hicho ndicho hasa kitakachotokea. 'Chic Shaver mzee' atakufa."

Kuyatoa maisha yangu yote yaliyosamehewa kwa Mungu na kumwomba asulubishe msingi uliobaki wa ubinafsi, nilijaribu kutoa msaada kwa imani na kumwamini Mungu kwa jibu. Kwa kuhimizwa na marafiki Wakristo, nilikusanya imani yangu yote na kumwamini Mungu atanitakasa.

Nilipofanya hivyo, amani na furaha ya ajabu ilijaza moyo wangu. Nguvu zangu zilirudi ghafla. Na oh, upendo! Nilisimama na kushuhudia Mungu alikuwa amenitakasa kabisa. Mara moja, mtu mmoja katika kusanyiko la waumini aliharakisha kumtafuta Mungu. Kulikuwa na nguvu za kiroho katika chumba hicho. Nilienda nyumbani nikiimba wimbo wa Charles Wesley "Love Divine, All Loves Excelling," na nikauimba kwa kurudia-rudia kwa muda wa saa ishirini na nne zilizofuata.

Ubinafsi wangu ulikuwa umeenda msalabani; Mungu alikuwa amenitakasa kabisa. Roho alikuwa amenijaza, na maisha yangu ya Kikristo yalipanda hadi kiwango kipya kabisa. Bado nilikuwa na masomo mengi ya kujifunza kuhusu kuendelea "kutembea katika Roho"—na bado najifunza. Lakini nilikuwa nimeingia katika nchi inayoitwa "ushindi." Bado ninaishi huko na kuzuru eneo jipya.

## DESEMBA 2 336

# Kutakaswa Kabisa na Kuenenda kwa Roho

*Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa.*
*1 Wathesalonike 5:23*

*Tukiishi kwa roho, na tuenende kwa Roho.*
*Wagalatia 5:25*

Wengi wanadai kwamba huduma ya John Wesley huko Uingereza katika karne ya kumi na nane iliokoa taifa dhidi ya mapinduzi. Kwa kuwajali maskini na ushawishi wa matajiri, kazi yake ilifikia makundi yote ya jamii. Wesley alikuwa na nguvu hasa kwa sababu mahubiri na mafundisho yake yaliwaongoza watu zaidi ya kuongoka na kuingia katika uzoefu wa ndani zaidi na Mungu. Utakaso huu wote ulitakasa mioyo ya waumini kikamilifu kutoka kwa asili ya dhambi. Lakini Wesley alikuwa mwangalifu kuwahimiza Wakristo kwamba kama hitaji la ushindi wa kiroho, lazima wabaki katika neema ya Mungu, waendelee katika upendo mkamilifu, na watembee katika Roho kila dakika. Barua zake mbili zinaangazia masuala haya.

Kwa Bi. Cook, Septemba 24, 1785:

> *Na je, ni kwa muda gani unaweza kufanywa mshiriki wa utakaso! Na sio tu kwa ukuaji wa polepole na usio na hisia katika neema, lakini kwa uweza wake Aliye juu zaidi akikufunikia kama kivuli, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, ili kukomesha dhambi kabisa, na kuwafanya upya katika sura yake yote! Ikiwa wewe ni rahisi wa moyo, ikiwa uko tayari kupokea zawadi ya mbinguni, kama mtoto mdogo, bila hoja, kwa nini usiipokee sasa? Yuko karibu anayetakasa; yu pamoja nawe; Anabisha hodi kwenye mlango wa moyo wako!*[187]

Na kwa Adam Clarke, Novemba 26, 1790: *"Kuhifadhi neema ya Mungu, ni zaidi ya kuipata: Ni vigumu labda mmoja kati ya watatu anayefanya hivi. Na hili linapaswa kusisitizwa kwa nguvu na kwa uwazi kwa wote ambao wameonja upendo mkamilifu."*[188]

---

187. John Wesley, *The Works of John Wesley* (Kansas City, MO: Nazarene Publishing House, n.d.), vol. XIII, 94.

188. Wesley, *Works*, 104.

Kwa hiyo mtafute mpaka ujue ameutakasa moyo wako kabisa. Lakini usiwe mwenye kiburi—kuwa na bidii kutumia rasilimali zote za kimungu na kuhifadhi hatua ya kila siku pamoja na Roho. Kama Wagalatia 5:25 inavyosema, "Na tuenende katika Roho." Ukifanya hivyo, "roho yako yote na nafsi na mwili" zitahifadhiwa bila lawama wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye anayewaita ni mwaminifu, naye atafanya" (1 Wathesalonike 5:23–24).

**DESEMBA 3** **337**

# Utakaso Muhimu, Sehemu ya 1

*Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu,*
*kutakaswa kwenu.*
*1 Thessalonians 4:3a*

Utakaso ni muhimu kwa sababu ya:

1. **Wito wa Neno la Mungu**
   "Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati" (1 Thessalonians 4:3).
   "Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe muwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo" (1 Thessalonians 5:23).
2. **Haja ya Watu**
   Bado kuna hali ya kutisha ya ubinafsi katika mioyo ya watu walioongoka, pamoja na ukosefu wa nguvu za kiroho. Hili linahitaji kutatuliwa kwa kuingilia kati kwa Mungu.
3. **Moyo uliotakaswa unavutia**
   Sherwood Wirt, mhariri wa zamani wa gazeti la *Decision,* alishuhudia juu ya tukio lake la kutakaswa: "Sijui jinsi upendo ulivyoingia, lakini ninajua kwamba uchungu wote niliokuwa nao dhidi ya wengine . . . . ulitoweka. Kinyongo—uadui—hisia zenye kuumiza—yote hayo. Yote yaliyeyuka. Yalivukizwa. Alienda."
4. **Watu wanatafuta**
   Katika miezi kumi na miwili kuanzia Juni 1, 2015, hadi Mei 31, 2016, katika uamsho mara kumi na nne kutoka Florida hadi Michigan, na

kutoka Texas hadi Idaho, watu 146 walimtafuta Mungu hadharani baada ya mahubiri juu ya utakaso.[189]

DESEMBA 4 **338**

# Utakaso Muhimu, Sehemu ya 2

*Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu.*
*1 Wathesalonike 4:3a*

Waumini wanashuhudia ukweli juu ya hitaji la utakaso.

*Isabel:* Siku chache baada ya kuona rafiki yake akimkubali Kristo, Isabel alishuhudia, "Nilipoanzisha darasa hili, niliogopa kuwasilisha injili. Sasa kwa kuwa Mungu amenitakasa, siogopi tena. Ninajiamini, ninachangamkia, na niko makini zaidi kuhusu fursa zangu."

*Kathy:* Polepole, nilifika mahali nilipoelewa kwamba Baba yangu wa mbinguni asingenidhuru kamwe na kwamba ningetumaini mamlaka yake juu yangu. Kwa kweli, ni kitu nilichokitamani! Kilichobaki ni maelezo tu. Nakumbuka niliuliza kwenye madhabahu, "Je, kuna kitu kingine chochote unachotaka nikupe?" Nakumbuka niliuliza kwenye madhabahu, "Je, kuna kitu kingine chochote unachotaka nikupe?" Niliendelea kuuliza swali hilo mpaka ukimya wa Mungu na amani yangu kubwa ikanihakikishia hakuna kingine. Nilipitia utakaso mzima kama uamuzi wa wakati mmoja wa mgogoro wa kiroho, na ninaendelea kuupitia kama uamuzi endelevu wa kuishi maisha yangu jinsi Mungu anavyotaka niishi. Jambo kuu kuhusu hayo yote ni kwamba kwa ushirika wa karibu, wa upendo tulio nao, pia ndivyo ninavyotaka kuishi!

*Keith:* Ningewezaje kuwa muumini na mfuasi wa Kristo ikiwa silika yangu ya asili ilikuwa kulaani na kunung'unika? Kwa hivyo nilianza kutafuta kile ambacho kilikosekana. Niliyatafuta majibu, lakini ilionekana kana kwamba nilikuwa na misingi yote: amini, zaka, tumikia—lakini hakuna kilichobadilika katika asili yangu. Kisha, karibu na mwisho wa Julai 2008, kanisa letu lilihitaji usaidizi wa ulezi huku baadhi ya waumini wa kawaida wakiwa wametoka. Nakumbuka nikifikiri hiyo ilikuwa chini sana ya hadhi yangu, lakini nilijitolea kuchukua zamu kwa kinyongo. Wakati wa ibada ya

189. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Septemba 2016).

Jumapili Julai 27, 2008, nilikutana na aliyekuwa mtunzaji mkuu aliyestaafu. Nilimwambia kwa mzaha ningechukua kazi yake ya zamani na kumuuliza, "Unashughulikiaje hili?

Aliniambia kwamba aliona kazi yake ya utunzaji kuwa huduma na kwamba alikuwa akimfanyia Mungu kazi: "Ikiwa Kristo anaweza kufa msalabani kwa ajili yangu, bila shaka ninaweza kusafisha kanisa kwa ajili yake."

Maneno yake yalining'inia hewani na kunizunguka. Kisha ikawa. Nilihisi joto, baridi, mtupu, na nimejaa ndani kwa wakati mmoja. Nilijua nilihitaji kuwa mtunzaji. Matatizo yakawa hali ya kusaidia; hali zikawa fursa za kufanya jambo; kazi zangu zikawa matendo ya utumishi. Nilitambua kwamba Mungu alitumia mtunzaji kuyafungua macho na moyo wangu kwa utimilifu wake. Kwa hiyo watu wanaponiuliza jinsi ninavyo "simama na Bwana," ninawaambia nimejazwa na Roho, na ninamwacha Mungu ayatawale mambo.[190]

**DESEMBA 5** **339**

# Utakaso Muhimu, Sehemu ya 3

*Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu,*
*kutakaswa kwenu.*
*1 Wathesalonike 4:3a*

Mwanafalsafa Mkristo Dallas Willard alisema kwamba kitabu pekee kilichomshawishi zaidi kuliko Bibilia kilikuwa *Deeper Experiences of Famous Christians* cha James Gilchrist Lawson. Kitabu hiki kimejaa ushuhuda wa wale ambao wametakaswa na kujazwa na Roho.

Matthew Kelly, katika kitabu cha *Four Signs of a Dynamic Catholic*, anawaita Wakatoliki wafanye uamsho. Anauliza swali, "Je, ni njia gani bora zaidi ya kuishi?" Anasema jibu ni kuwa mfano bora zaidi wa mtu mwenyewe kwa kuufia ubinafsi mdogo ili nafsi bora iibuke katika Kristo. Kutafuta utakatifu ni kutafuta mfano bora zaidi wako mwenyewe.

Kitabu cha ibada kinachouzwa sana kwa wakati wote ni cha Oswald Chambers, *My Utmost for His Highest*. Ulimwenguni kote, Wakristo wa kutoka pande mbalimbali wanakisoma. Katika kitabu hicho, Chambers

190. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Septemba 2016).

anatumia neno “utakaso” mara ishirini na moja, na kuna matukio mengi zaidi ya maneno yanayohusiana. Katika somo la Februari 8, anaandika hivi: “Tunaposali ili kutakaswa, je, tunajitayarisha?... Utakaso unamaanisha kuzingatia sana mtazamo wa Mungu . . . Utakaso unamaanisha kufanywa kitu kimoja na Yesu ili tabia iliyomtawala itatutawala. Je, tuko tayari kusema, ‘Bwana, nifanye kuwa mtakatifu jinsi unavyoweza kumfanya mwenye dhambi aokolewe kwa neema?’” Katika ingizo la Oktoba 20, anaandika hivi: “Si swali la ikiwa Mungu yuko tayari kunitakasa; Je, ni mapenzi *yangu*? Je, niko tayari kumwacha Mungu afanye ndani yangu yote ambayo yamewezeshwa na Upatanisho?”[191]

Ikiwa Neno la Mungu; mahitaji ya watu; mvuto wa moyo uliotakaswa; kutafuta watu; watu wanaoshuhudia; vilevile Sherwood Wirt, Dallas Willard, Matthew Kelly, na Oswald Chambers wote wanatuita—je, hatupaswi kusonga mbele ili kupata utakaso wa Mungu kibinafsi na kuwaambia wengine ukweli?[192]

**DESEMBA 6** **340**

# Hofu na Nguvu za Kiroho

*Akawaambia, “Ndivyo ilivyoandikwa, kwamaba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu, na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya. Tazama nawaletea juu yenu ahadi ya baba yangu; lakini kaeni humu mjini hadi mvikwe uwezo utokao juu.”*
*Luka 24:46-49*

Walikuwa wafuasi wa Kristo, kwa kiwango fulani—lakini walikimbia na kujificha shinikizo lilipokuwa kali. Kisha Yesu akawapa ahadi ya uwezo utokao juu—rejeleo la Roho Mtakatifu (Matendo 1:4–5). Na kwa hakika, Roho alishuka kwa wafuasi 120 wa Kristo walipokuwa wakiomba (1:14 na 2:4). Petro, pia, alijazwa na Roho—sasa yule aliyekana akawa mshawishi, na watu

191. Oswald Chambers, *My Utmost for His Highest* (Toronto: McClelland and Steward Limited, 1935).

192. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Septemba 2016).

elfu tatu walimpokea Kristo. Yohana alijazwa na Roho na akalihubiri neno la Mungu kwa ujasiri (4:31). Stefano, akiwa amejaa Roho (7:55), aliona mbingu na Yesu, na kuwasamehe wale waliomwua. Mshiriki wa kanisa asiyekuwa rasmi aliyejazwa na Roho, Filipo (6:5), akiongozwa na Roho (8:29), aliongoza Mwethiopia kwa Kristo. Na Dwight Moody, Charles Finney, Samuel Logan Brengle, na E. Stanley Jones wote walishuhudia kujazwa na Roho wakati baada ya kumjua Kristo kama Mwokozi kwa muda. Wote walisema kwamba uhusiano huu na Roho ulitia huduma zao nguvu.

Labda hii ni kwa viongozi wa dini, watu wenye mamlaka Lakini vipi kuhusu watu wa kawaida? Je, hofu inatuzuia kushuhudia (kuwaambia wengine kile ambacho Yesu anamaanisha kwetu)?

Tulikuwa tumemaliza darasa la mafunzo ya uinjilisti wa kibinafsi ya wiki kumi na mbili katika kanisa moja huko Houston. Mshiriki mmoja katika darasa hilo alikuwa Isabel—kijana, aliyefunga ndoa hivi karibuni, kutoka Venezuela, na alikuwa amekuwa Mkristo kwa zaidi ya miaka miwili hivi. Darasa lilikuza ujuzi wake hadi pale ambapo angeweza kushuhudia kwa ujasiri na kushiriki ujumbe wa injili. Muda mfupi baadaye, alishiriki injili, na mtu huyo akamkubali Kristo. Lazima pia nikuambie kwamba wakati ule ule wa mafunzo yake ya uinjilisti, Isabel alitakaswa kabisa (1 Wathesalonike 5:23) na kujazwa na Roho Mtakatifu. Siku chache baada ya kuona rafiki yake mpya akimkubali Kristo, alishuhudia, "Nilipoanzisha darasa hili, niliogopa kuwasilisha injili. Sasa kwa kuwa Mungu amenitakasa, siogopi tena. Ninajiamini, nina furaha, niko makini zaidi kwa fursa zangu."

Kwa uwezo wa Roho wa utakaso, na tushinde hofu zetu.[193]

**DESEMBA 7** **341**

# Mvuto wa Sumaku

*Mvue mwenendo wenu wa kwanza, utu wa zamani unaoharibika, kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; na mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.*
*Waefeso 4:22-24*

193. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Juni 2005).

Uliwahi kucheza na sumaku ulipokuwa mtoto? Nilikuwa na sumaku iliyo na upinde na sumaku ya chuma kimoja. Ningeweza kumwaga vichuma vidogo kwenye kipande cha karatasi, kushikilia sumaku ile yenye upinde chini ya karatasi, na papo hapo, mvuto wa sumaku uliweka vipande vya chuma katika sehemu mbili tofauti kuzunguka nguzo za sumaku. Baadhi ya vichungi vya chuma vilikuwa na wakati mgumu kuamua ni upande gani wa kutua. Walakini, nikiweka sumaku ya upau mmoja chini ya karatasi, vichungi vya chuma huwekwa katika sehemu moja, moja kuzunguka nguzo hiyo ya sumaku.

Katika maisha ya Wakristo wengi walioongoka kweli, bado kuna pande mbili kuu—Mungu na nafsi—ambayo huunda mifumo miwili ya utendaji inayopishana. Watu hawa kwa sehemu wana ubinafsi na wanamzingatia Mungu kwa kiasi—hii ni kusema kuwa, wana "nia mbili" (Yakobo 1:8).

Jinsi andiko katika Wagalatia 5:24 linavyoshughulikia suala hili ni kali sana: "Wale walio wa Kristo Yesu *wameusulibisha* mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake." Ikiwa mwili umesulubishwa, ikiwa utu wa kale (ubinafsi) umetupiliwa mbali, basi nguzo moja iliyobaki inaweza kutawala moyo na maisha: "asili yako mpya, iliyoumbwa kufanana na Mungu - ya haki na takatifu kweli" (Waefeso 4:24).

Unahisi mvutano gani? Kumbuka kwamba hutateleza na kuanguka hadi mahali pa ushindi—lazima uamue. Kwa hiyo, kama vile Paulo aandikavyo, "uvueni utu wenu wa zamani na . . . mkavae utu mpya" (Waefeso 4:22, 24,).[194]

**DESEMBA 8** **342**

# Kazi ya Pili ya Neema

*Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu.*
*1 Wathesalonike 4:3a*

"Ni wakati gani nimtazamie Mungu anitakase?" ni swali kubwa kwa Wakristo wengi wanyofu. Wathesalonike walikuwa Wakristo halisi, wa kweli na wazuri. Walikuwa waigaji wa Bwana (1 Wathesalonike 1:6) na vielelezo kwa waumini wote katika eneo lao (1:7). Paulo na viongozi wengine waliwaagiza

194. Adapted from Everett Lewis Cattell, *The Spirit of Holiness* (Grand Rapids: Eerdmans, 1963), 24–28.

"jinsi ya kuishi ili kumpendeza Mungu," na walikuwa wakifanya hivyo (4:1). Lakini Paulo aliwaambia, "Ni mapenzi ya Mungu kwamba mtakaswe" (4:3)—ambayo, pamoja na mambo mengine, ingemaanisha kuwezeshwa kwa usafi wa kingono.

Rafiki yangu Paul ni mfano muhimu wa ugunduzi huo wa kiroho. Kufikia wakati alifika kwenye chuo cha Kikristo, alikuwa Mkristo kwa jina tu. Mtindo wake wa maisha ulikuwa wa kutenda dhambi na kutubu, kutenda dhambi na kutubu. Wakati huohuo, aliwaona Wakristo waliokuwa karibu naye waliokuwa wakisitawi kiroho. Aligundua kwamba Mungu alizungumza nao lakini si yeye.

Paulo alimwuliza Mungu juu ya hili, akiuliza, "Mbona husemi nami?"

Mungu akajibu, "*Sijaacha kusema nawe. Umeacha kunisikiliza. Huwezi kunisikia kwa sababu ya mambo mengine yote unayosikiliza.*"

Kwa hiyo Paulo alitubu na kupata kile alichokiita "kuongoka kwake kwa watu wazima." Wafilipi 4:8 (ambayo inatoa mwongozo kwa maisha ya mawazo ya Mkristo) ikawa chujio lililomwongoza. Tokeo likawa kwamba, akiwa na umri wa miaka kumi na tisa, ukuaji wake wa kiroho ulikuwa wa kiwango cah juu zaidi.

Sasa Mungu alikuwa akizungumza naye. Alikuwa mkuu wa haki ya jinai, lakini Mungu alimwambia, *"Nina jambo bora zaidi kwa maisha yako."* Paulo alijiuliza angejuaje kama ameitwa kwenye huduma. Ndani ya wiki chache, alipata uthibitisho wa wito wake, na kazi yake ikaanza.

Paulo aliendelea kusikia watu wakizungumza kuhusu utakaso. Walizungumza juu ya uongofu wa kweli kwa Kristo, lakini kisha tukio la pili, la kina zaidi na Mungu—kazi ya pili ya neema. Alifikiri, *niliokolewa nikiwa mtoto wa miaka saba, na sasa nimeongolewa kama mtu mzima. Hiyo lazima iwe ni kazi ya pili ya neema.*

Lakini kulikuwa na matatizo. Paulo alikuwa na roho ya kuwahukumu Wakristo ambao hawakuwa na bidii kidogo kuliko yeye. Alikwenda kwenye uamsho na kumsikia mwinjilisti akisema kwamba, ili kutakaswa, unapaswa kutembea katika nuru yote ambayo Mungu amekupa. Baadaye alishuhudia: "Tangu nilipomkubali Kristo utotoni wangu nikiwa na umri wa miaka saba hadi kumi na tisa, nilikuwa katika dini yenye dhambi. Uongofu wangu wa mtu mzima haukuwa utakaso wangu; ulikuwa ni urejeshaji wangu wa uhusiano uliohifadhiwa. Nimeokolewa, sijatakaswa. Mungu alinionyesha roho yangu ya kuhukumu na moyo wangu usio kama wa Kristo ambao ulihitaji kusafishwa. Nilienda madhabahuni na kuutoa na kuufungua moyo wangu. Nikasema, 'Je, nimedanganywa?'"

Wakati huo, profesa mmoja alimjia Paulo na kumshauri kwa hekima. Paulo aliomba tena, na imani yake ikaanza kuinuka. Akasema, “Ndiyo, ninaamini.” Hisia za joto zilipita kifuani mwake, mikononi na miguuni mwake.

Kisha, alimsikia Mungu akisema, *“Paulo, nimependezwa nawe.”* Alijua basi kwamba Mungu alikuwa amemtakasa.

Karibu kila mtu alikuwa ametoka mahali patakatifu alipomaliza kuomba. Kisha Ibilisi akasema: *“Hili ndilo jambo kuu zaidi ambalo limewawahi kukupata, na hakuna anayejali.”*

Lakini Mungu hakuwa amemaliza. Alisema, *“Haijalishi wengine wanasema nini kukuhusu. Nimefurahishwa na wewe.”* Na hisia ya joto ikapita tena kwenye mwili wake.

Siku iliyofuata, Paulo alimwendea profesa ambaye alikuwa akimchambua na kumuomba msamaha. “Nilikosea,” alisema. “Nilitakaswa jana usiku.” Baada ya hayo, wakawa marafiki wa dhati.

Njia ya maisha ya Paul ilichukua mkondo mpya. Leo, yeye ni mhudumu mwenye nguvu wa injili na mmoja wa watu wacha Mungu sana ninaowajua.

**DESEMBA 9** **343**

# Jamani, Yuko Polepole Sana!

*Mtu ajaribiwapo, asiseme, “Ninajaribiwa na Mungu.” maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu. Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti. Ndugu zangu wapenzi, msidanganyike.*
*Yakobo 1:13-16*

Ndiyo, alisema hivyo—mwinjilisti mmoja, aliyekuwa akingojea kiamsha kinywa chake katika nyumba ya mchungaji, alisema hivi kuhusu mke wa mchungaji, “Jamani, hakika yuko polepole!”

Baadaye mchungaji huyo aliniambia, “Hilo lilinikasirisha.” Hata hivyo nilipoamua kumuuliza mchungaji kama alikuwa na kinyongo, alijaribu kulipiza kisasi, au alikuwa na mtazamo mbaya kumuelekezea muinjilisti huyo, alisema hapana.

Hasira ya mchungaji ilikuwa ya kawaida hata kwa mtu aliyetakaswa. Ilikuwa ni mwitikio wake wa Kikristo *unaoendelea* na mtazamo wake baadaye ambao ulionyesha utakaso wake.

Je, tunapaswa kulichukuliaje tatizo la majaribu? Kwanza, ni lazima tutofautishe kati ya majaribu na dhambi. Yakobo 1:14–15 inasema, "Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha." Yakobo anaonekana kusema kwamba tamaa zetu za ndani huleta majaribu kwa mapenzi yetu. Ikiwa, kwa upande mwingine, tamaa zetu za ndani *zinadhibiti* au kuelekeza nia yetu, hiyo ina maana kuwa huwa tunatenda dhambi.

Ni rahisi kutofautisha kati ya majaribu na dhambi tunaposhughulika na matendo ya nje badala ya tamaa za ndani (dhambi za roho). Kutokuwa na subira, wivu, majivuno, kinyongo, na kukasirika (1 Wakorintho 13) ni mifano ya dhambi za ndani. Ikiwa, wakati wa shinikizo au majaribu, Mkristo aliyetakaswa hushuhudia *hali* ya kukosa subira au kuudhika kwa muda, je, hilo lamaanisha kwamba hajatakaswa kabisa? La. Hisia hiyo ya muda sio dhambi bado, kwa sababu zifuatazo:

1. Ili jaribu liwe halisi, lazima kuwe na "mvuto wa kweli . . . tamaa za ndani".
2. Hali ya shinikizo la juu itazalisha kuchanganyikiwa kwa ndani hata kwa watu watakatifu zaidi, na hili ni jambo la kawaida. Dt. Richard Taylor anasema kwamba hata kwa watu waliotakaswa, kuna majibu ya kawaida, ya kupingana na hali ambazo hawazipendi. Mwitikio wa mchungaji kwa kukosolewa kwa mke wake ni mfano wa hili.
3. Labda Warumi 8:7— "Nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii" —inatupatia tofauti kati ya mambo ya kimwili na ya kibinadamu. Katikati ya fadhaa au hamu ya ndani, uliza, "Je, hii iko chini ya sheria ya Mungu?" Wanyama hawako chini ya sheria ya Mungu; binadamu yuko.
4. Tamaa au hisia mbaya ya muda si dhambi maadamu wosia unasema tu, "Nitaitikia wakati wa kufadhaika kwa sheria ya upendo." Kama msemo unavyosema, "Huwezi kuwazuia ndege wasiruke juu ya kichwa chako, lakini unaweza kuwazuia wasifanye kiota kwenye nywele zako."[195]

195. Charles "Chic" Shaver, *Keeping Spiritual Victory* (Kansas City, MO: Beacon Hill Press of Kansas City, 1972), 13–16.

# Kuna Amani

*Amani nawaachieni; amani yangu nawapa.*
*Yohana 14:27*

Katika ibada ya uamsho ya Jumapili asubuhi huko Illinois, Jack alichukua mkono wa mke wake na kuja madhabahuni huku akilia. Alirudi kwa Kristo.

Hii ndio hadithi ya Jack:

> Nilitoa udhuru kila juma kwa nini singeweza kwenda kanisani. Kisha, wiki mbili zilizopita Jumamosi, nilikunywa bia yangu ya mwisho. Nilihitaji kuwa mfano mzuri kwa wajukuu wangu kumi na watatu.
>
> Siku ya Jumapili, mwanamume mkaidi aliingia kanisani. Nilikuwa nimedumaa kiroho. Sikuwa nimechukua Bibilia kwa mwaka mmoja. Mtu huyu mwenye kiburi, mpumbavu alifika madhabahuni akiwa na magoti dhaifu. Yeye [Kristo] alichukua mizigo yote niliyokuwa nayo. Alinitoa kwenye ukali na kuniweka kwenye Mwamba.
>
> Usiku huo, nilipata usingizi wa amani wa kwanza ambao sikukwa nimeupata kwa muda mrefu. Hakukuwa na matatizo akilini mwangu.
>
> Siku iliyofuata, sikubishana na mke wangu kuhusu siku ya malipo au jinsi ya kutumia pesa hizo. Tumekuwa tukigombana kila wakati.

Hivi ndivyo Jack alivyosimulia kwa kifupi tukio lake na Yesu asubuhi hiyo ya Jumapili: "Sikuwa nimewahi kuvuliwa mzigo kama huo."

Mke wake alitoa muhtasari wa jambo hilo namna hii: "Kuna amani katika nyumba yetu."[196]

---

196. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Juni 2014).

# Krisimasi: Mwenye Hofu au Mwaminifu

*Malaika akawaambia, Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote.*
*Luka 2:10*

Katika maisha yangu ya miaka themanini na mitano, sikumbuki wakati ambapo mambo ya kitaifa au ya kimataifa yamekuwa yakiharibika zaidi kuliko ilivyo sasa. Yesu Kristo alitabiri hivi: "Tena, kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota; na katika nchi dhiki ya mataifa wakishangaa kwa uvumi wa bahari na msukosuko wake; watu wakivunjika mioyo kwa hofu, na kwa kutazamia mambo yatakayoupata ulimwengu. Kwa kuwa nguvu za mbinguni zitatikisika" (Luka 21:25–26). Uchungu, fadhaa, woga, na woga vyote vinazungumza juu ya ulimwengu uliojaa hofu. Hivi majuzi, niligundua kwa uwazi kwamba aina mbili kuu za woga zinaonekana katika Maandiko.

Jambo la kwanza ni kumcha Mwenyezi-Mungu na matendo yake ya kiungu. Kuna hofu yenye afya au heshima kwa Bwana ambayo Maandiko yanaeleza (Mithali 9:10). Halafu kuna hofu kwamba, nikimwacha Mungu awe karibu nami sana, atayaingilia maisha yangu. Mfano juu ya hilo ni yule mtawala kijana tajiri aliyemwacha Yesu kwa sababu aliogopa madai ya Yesu juu ya mali yake na maisha yake (Mathayo 19:21–22). Kinyume chake, hadithi hiyo ya Krismasi inayojulikana sana inasimulia juu ya mjumbe wa kimalaika kutoka kwa Mungu akiripoti kuzaliwa kwa Yesu Kristo. "Na malaika aliwaambia nini wachungaji? Ninawaletea habari njema ambayo italeta furaha kubwa" (Luka 2:10). Pia tunasoma kwamba Mungu alipomkaribia Musa, "Musa akaufícha uso wake, kwa sababu aliogopa kumwangalia Mungu" (Kutoka 3:6).

Zaidi ya kumcha Bwana, aina ya pili ya woga tunayoiona katika Maandiko ni woga unaotokana na shinikizo katika maisha yetu binafsi na jamii. Mungu anazungumza na hilo kwa nguvu. Kama mtunzi wa zaburi alivyoandika, "BWANA ni nuru yangu na wokovu wangu—nimwogope nani?" (Zaburi 27:1). Vivyo hivyo, katika Zaburi 56:3, tunasoma, "Ninapoogopa, nakutumainia wewe." Na Waebrania 13:6 inasema, "Bwana ndiye msaidizi wangu." Inashangaza! Mungu ambaye mara nyingi tunaogopa kumkaribia anataka kuwa karibu nasi na kutusaidia na hofu zetu.

Mnamo 2014, niliandika katika jarida letu la Krismasi kuhusu upasuaji wa saratani wa saa kumi na tatu wa mtoto wetu (Paul) ambao uliondoa sehemu yake ya kutunzia sauti na sehemu kubwa ya shingo yake. Tuliweza kuripoti kwamba, katika maombi kabla ya upasuaji, amani ya Mungu ilikuwa imenishukia huko Mississippi; juu ya Nancy huko Kansas; na juu ya Paul huko Indiana (Wafilipi 4:6–7).

Tangu upasuaji huo wa saa kumi na tatu, Paul amekuwa na upasuaji wa kujenga upya mara nne. Wakati wote huo, Paul amekuwa akifanya kazi yake ya muda wote pamoja na kazi mbili za ziada. Wakati wa ziara pamoja na Paul, Nancy alimwuliza maswali mengi kuhusu hali yake, hisia zake, na siku zake zijazo. Alijibu tena na tena, "Mungu analijua jina langu." Hata kama Paul asingeweza kutoa majibu ya kina kuhusu siku zijazo, alikuwa na uhakika katika Mungu ambaye anamjua kibinafsi kwa jina.

Katika tukio lingine, binti zetu walimwuliza Paul jinsi alivyokuwa akishughulikia upasuaji huo mbaya, kupoteza kikoromeo chake, na upasuaji uliofuata. Alijibu kwa urahisi, "Sijawahi kuwa na siku mbaya." Ujasiri! Nguvu! Furaha!

"Anajua jina langu," na "Sijawahi kuwa na siku mbaya." Kwa majibu yake, tunaona kwamba Paulo haogopi lakini ni mwaminifu kwa Mungu anayesikia maombi ya mtu binafsi, anayetusaidia, anayetupenda.

Katika hali ya ulimwengu wetu wenye matatizo Krismasi hii, tuwe waaminifu kwa ujumbe, "Usiogope. Ninawaletea habari njema ambayo italeta furaha kubwa."[197]

**DESEMBA 12** **346**

# Utakaso Kamili

*Nikikuokoa na watu wako, na watu wa Mataifa, ambao nakutuma kwao;*
*uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru,*
*waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate*
*msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao*
*waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.*
*Matendo 26:17-18*

197. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Disemba 2015).

John Wesley alimwandikia Kasisi Freeborn Garrettson haya mwaka 1785: “Kadiri unavyowasisitiza kwa uwazi na kwa nguvu waumini wote kutamani utakaso kamili, unaoweza kupatikana sasa kwa imani sahili, ndivyo kazi yote ya Mungu itakavyofanikiwa zaidi.”

Mshiriki wa kawaida kutoka Alabama aliniandikia haya baada ya wiki ya ibada za uamsho katika kanisa mahalia: “Umefanya jambo la maana sana kutokana na mambo ambayo nimehangaika nayo. Ninahisi nguvu ya upendo wa Mungu zaidi ya hapo awali . . . Ninaomba utakaso huo zaidi sasa kwa sababu umenisaidia kutamani hilo.”

Baada ya ibada za kipekee, mchungaji wa Ohio alinitumia barua iliyokuwa na ujumbe huu: “Asante kwa . . . jumbe zilizopelekea asilimia kubwa ya . . . watu wa kanisa wakisonga mbele kiroho . . . Mkazo wako juu ya uinjilisti wa kibinafsi utasababisha watu wengi kuongezwa kwenye ufalme. Katika miaka yangu ishirini na tatu ya uchungaji sijawahi kushuhudia watu wengi wakiomba utakaso.”

Ninawasihi Wakristo wote wasonge mbele hadi kwa utakaso kamili.[198]

DESEMBA 13 **347**

# Nafsi, Sehemu ya 1

*Mpende jirani yako kama nafsi yako.*
*Mathayo19:19b*

“Yeye si mpumbavu atoaye asichoweza kuhifadhi ili kupata kile ambacho hawezi kukipoteza”[199] ni maneno ya kushangaza ambayo Jim Elliot aliandika alipokuwa na umri wa miaka ishirini na miwili. Alikuwa mmoja wa wanaume watano ambao wangetoa maisha yao kama wafia imani kwa ajili ya wokovu wa kabila la Huaorani la Ekuado—kama vile Yesu Kristo alivyotoa maisha yake kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu.

Yesu Kristo alikuwa na mazungumzo mazito na mtu tajiri ambaye alikuwa akijaribu kupata uzima wa milele. Walijadili amri, kisha Yesu akasema maneno maarufu, “Mpende jirani yako kama nafsi yako.” Bila shaka,

198. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Machi 2008)

199. Elisabeth Elliot, *Shadow of the Almighty* (New York: Harper and Brothers, 1958), 247.

kusudi kuu la Yesu lilikuwa kuondoa ubinafsi wa mtu huyo na kumchochea kuwapenda wengine. Hata hivyo, kwa kufanya hivyo, Yesu alikiri kwamba kuna kujipenda kwa njia halali.

Nafsi yako ni zawadi kutoka kwa Mungu. Yesu anataka uwe na thamani, kujistahi, kujiheshimu, kujitambua, kujijali, kujitunza, kujidhibiti na mengine mengi. Huo ni upendo halali kwako mwenyewe.

Nafsi yako ndio gari ambalo Mungu hutumia kufanya kazi. Mungu anapokutakasa na kukujaza kwa Roho wake, yeye haibatili nafsi yako—utakuwa nafsi yako daima.

Badala yake, Mungu anapokutakasa, anaisafisha na kuitakasa nafsi yako. Mungu anaondoa ubinafsi wako kujifikiria kwako. Kuna maneno mengine ya ubinafsi—mwili, asili ya dhambi, Adamu wa kale, asili ya Adamu, asili ya kimwili, nia ya kimwili, na mengine. Lazima uelewe unaweza ukawa nafsi bila kujifikiria mwenyewe. Mara nyingi, nitahubiri, "Unajua dhambi zako zimesamehewa; umemjua Kristo; lakini bado unapambana na kiini cha ubinafsi katika utu wako. Mungu ana jibu laako."

Mojawapo ya maonyesho ya wazi zaidi ya ukweli huu ni ushuhuda wa mtume Paulo: "Nimesulubishwa pamoja na Kristo lakini ni hai wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu" (Wagalatia 2:20).

Katika maandishi ya asili ya Kigiriki, "mimi" ambaye amesulubishwa ni neno "kujiona." Tunaelewa maana yake wakati mtu anaposema, "jamani, ana majisifu makubwa." Inamaanisha mtu huyo anajiona kupita kiasi, anajiona kuwa juu ya wengine, na anapaswa kusifiwa sana. Hiyo ni nafsi yenye ubinafsi—aina inayohitaji kusulubishwa, na kuuawa.

Kristo anapokuja kuishi katika maisha ya mtu huyo, mtu huyo bado anaishi katika mwili ambao wenyewe si wenye dhambi. Baada ya kusulubishwa, mtu huyu anaishi kwa njia mpya; "Ninaishi kwa imani katika Mwana wa Mungu." Anaishi kwa wingi zaidi kuliko hapo awali. Kristo yuko kwenye kiti cha enzi cha maisha yake, ambapo hapo awali, ubinafsi ulikuwa kwenye kiti cha enzi.

# Nafsi, Sehemu ya 2

*Mpende jirani yako kama nafsi yako.*
*Mathayo 19:19b*

Maandiko yanafundisha, "vijana wa kiume uwaonye kuwa na kiasi" (Tito 2:6), hayahamasishi *kijitafutia makuu* "[Upendo] haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya" (1 Wakorintho 13:5).

Tunaonywa tusiwe na "wivu wenye uchungu na ubinafsi mioyoni [mwetu]" (Yakobo 3:14). Badala yake, Maandiko yanatualika kuishi maisha yaliyojaa matunda matamu: "Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi" (Wagalatia 5:22–23).

Wakristo wote wanaombwa kupeleka ubinafsi wao msalabani na kuruhusu Roho Mtakatifu wa Mungu kusafisha, kuunganisha, na kutakasa utu wao wote. Nafsi lazima ijue bwana wake.

Watu wanakuwaje wanapomruhusu Mungu asulubishe ubinafsi wao na *kujitolea* kumpenda na kumtumikia? Ili kujua, hebu tusome zaidi kutoka kwa Jim Elliot:

> Katika tukio langu mwenyewe nimeona kwamba ndoto zenye kupita kiasi za ujana hazijapita tukio kuu la kuwa katika mapenzi ya Mungu, na ninaamini kwamba hakuna kitu kinachoweza kuwa bora zaidi. Hiyo sio kusema kwamba sitaki vitu vingine, na njia zingine za kuishi, na mahali pengine pa kuona, lakini katika akili yangu timamu najua kuwa matumaini yangu na mipango yangu juu yangu haiwezi kuwa bora zaidi kuliko alivyoipanga na kuitimiza. Hivyo na sisi sote tupate, na kujua ukweli wa Neno linalosema, "Yeye atakuwa kiongozi wetuhatakufa."[200]

Baadaye, anaandika juu ya "hazina moja, jicho moja, na bwana mmoja."[201]

Zaidi ya hayo, anaandika, "Mungu, nakuomba, uwashe vijiti hivi vinavyokaa tu vya maisha yangu na niwake kwa ajili yako. Teketeza uhai

200. Elisabeth Elliot, *Shadow of the Almighty* (New York: Harper and Brothers, 1958), 196.

201. Elliot, *Shadow*, 247.

wangu, Mungu wangu, maana ni wako. Sitafuti maisha marefu bali maisha kamili, kama wewe, Bwana Yesu."[202]

Haya ni maneno ya "nafsi" inayotawaliwa na Mungu na iliyobarikiwa.

DESEMBA 15 — 349

## Ninayokutakia Wakati wa Krismasi

*Malaika akawaambia, Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana.*
*Luka 2:10-11*

Ikiwa Yesu alikuja nyumbani kwako na kubisha mlango wako
Je, ungekimbilia kumruhusu aingie ndani na uchangamkie jambo hilo?
Je, moyo wako ungeshtuka anapoingia ndani ya mlango?
Je, ungemshukuru na kumsifu, kisha ungeimba nyingine zaidi?
Kujua alikuokoa, kisha akakusamehe, na amani ikaja mchana kutwa
Kwa hivyo sasa unashiriki upendo wake na neema na msamaha kwa makosa
Unawaombea wale wanaomhitaji kuwa na mtazamo wa mbinguni
Kuishi maisha yao kwa upendo na neema kwa moyo unaopiga mapya kabisa
Tunamshukuru na kumsifu kwa siku zetu zote duniani
Kujua kwamba yuko pamoja nasi na hubariki njia zetu zote
Inalipa kumtumikia Yesu—inalipa kila siku—inalipa kila hatua ya njia
Ingawa njia ya utukufu wakati mwingine inaweza kuwa mbaya
Nitamwamini kwa kila hatua.

Nancy Shaver[203]

202. Elliot, *Shadow.*
203. Awali kilichapishwa katika the Shaver Christmas letter, 2017.

# Fikia Lengo

*Usiku na mchana tunapoomba kwa juhudi tupate kuwaona nyuso zenu, na kuurekebisha upungufu wa imani yenu?*
*1 Wathesalonike 3:10*

*Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati.*
*1 Wathesalonike 4:3*

*Basi yeye anayekataa, hakatai mwanadamu bali Mungu, anayewapa ninyi Roho wake Mtakatifu.*
*1 Wathesalonike 4:8*

Keith ni mkurugenzi wa uhasibu wa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Kansas Medical Center, ambapo anasimamia mkopo wa wanafunzi na fedha za masomo—dola milioni 75 hadi 110 kwa mwaka. Yeye na mke wake, Laura, pia wana huduma ya ushuru wa mapato wanaousimamia kutoka kwenye nyumba yao. Keith na Laura wameoana tangu mwaka 1986, wana mtoto wa kiume mtu mzima, Andy, na ni washiriki wa kanisa lao. Hapa kuna hadithi ya Keith kwa maneno yake mwenyewe:

*Nikawa mfuasi wa Kristo kama kazi ya mbinguni ya Mungu na kazi ya duniani ya Mchungaji Chic Shaver. Usiku huo, nilijua kuwa kuna kitu kilikuwa kimetokea, lakini kwa kuwa hakuna kitu kilichoonekana tofauti, nilianza kutafuta uhakikisho kwamba chochote ambacho kilipaswa kutokea kweli kilitokea. Maadili yangu, tabia, na nia yangu ya kutumikia ilibadilika kabisa. Mabadiliko hayo yalikuwa uthibitisho kwangu kwamba jambo lilitokea—nilibadilishwa.*

*Hili lilionekana kuwa sawa, na nilikubali kwa miaka kadhaa. Nilikuwa na shughuli nyingi katika kufanya kazi za kanisa na jumuiya sikuwa nimegundua kwamba pengine kuna kitu kilichokosekana—mpaka siku moja, wakati mke wangu mpendwa, Laura, nami tulipokuwa tukizunguka kwenye sehemu ya kuegesha magari tukitafuta nafasi kwenye kituo cha ununuzi cha eneo tulipo. Nilipopata nafasi, nilianza kuegesha gari langu nilipoona alama ya kiti cha magurudumu iliyochorwa kwenye lami. Nilirudi*

*nyuma na kuanza kulaani na kunung'unika kuhusu usumbufu huo Laura aliposema, "Vyema, huo ni mtazamo mzuri wa Kikristo."*

*Hapo ndipo nikajua kuna kitu kinakosekana. Ningewezaje kuwa muumini na mfuasi wa Kristo ikiwa silika yangu ya asili ilikuwa kulaani na kunung'unika? Kwa hivyo nilianza kutafuta kile ambacho kilikosekana. Nilitafuta majibu, lakini ilionekana kana kwamba nilikuwa na misingi yote: amini, zaka, tumikia—lakini hakuna kilichobadilika katika asili yangu. Ilikuwa ni kama kujaribu kugonga shabaha inayosonga wakati hata sikujua jinsi ya kulenga!*

*Nakumbuka nilimwambia Mungu kwamba nilikuwa tayari kujua la kufanya, lakini nadhani ilikuwa ni takwa zaidi kuliko sala: "Mungu, unangoja nini? Tuendelee na hili!"*

*Ilichukua muda, lakini niligundua kwamba marafiki wengi wa kanisa langu siku zote walionekana kuwa wenye fadhili na wenye subira wakati jambo fulani lilipoenda vibaya. Waliwafikia watu kwa huruma badala ya lawama. Walitoa msaada au usaidizi kama inahitajika. Na walikuwa wakiomba daima.*

*Hayo yote yalionekana kuwa na maana kwangu, lakini nilifanya jaribio la harakaharaka kulibaini. Kama unavyoweza kutarajia, hakuna kilichobadilika kabisa.*

*Kisha, karibu na mwisho wa Julai 2008, kanisa letu lilihitaji usaidizi wa utunzaji na ulezi huku baadhi ya waumini wa kawaida wakiwa wametoka. Nakumbuka nikifikiri hiyo ilikuwa chini sana ya hadhi yangu, lakini nilijitolea kwa moyo mkunjufu kuchukua zamu. Wakati wa ibada ya Jumapili Julai 27, 2008, nilikutana na aliyekuwa mlinzi mkuu aliyestaafu. Nilimwambia kwa mzaha ningechukua kazi yake ya zamani na kumuuliza, "Huwa unashughulikiaje hili?"*

*Aliniambia aliona kazi yake ya ulezi kama huduma, na kwamba alikuwa akifanya kazi kwa ajili ya Mungu: "Ikiwa Kristo anaweza kufa msalabani kwa ajili yangu, bila shaka ninaweza kumsafishia kanisa."*

*Maneno yake yalining'inia hewani na kunizunguka nilipoyasikia. Na kisha ikawa. Nilihisi joto, baridi, mtupu, na nimejaa ndani kwa wakati mmoja. Nilijua kwamba nilihitaji kuwa mtunzaji. Nilizungumza na mmoja wa wachungaji kuhusu jambo hilo, naye akasema, "Hili ni jibu la kweli kwa maombi."*

*Nilitoka kwa kujitolea hadi kwa mlinzi wa kudumu na nimekuwa huko tangu wakati huo. Huduma yangu kanisani ilikuwa rahisi na yenye kuridhisha. Wakati huo huo, matatizo yakawa hali ya kusaidia; hali zikawa fursa za kufanya jambo; kazi zangu zikawa matendo ya utumishi. Watu*

*walianza kuthamini na kutegemeamsaada wangu kanisani, na matatizo mengi yalitoweka nilipokuwa na mtazamo mzuri.*

*Niligundua Mungu alikuwa amemtumia mtunzaji kufungua macho na moyo wangu kwa utimilifu wake. Sihitaji tena kuwa katika udhibiti au kufuata Mpango wa Keith—si kanisani tu, bali katika maeneo yote. Ni furaha ya kweli kumngoja Mungu atawale tatizo kisha kufuata mwongozo wake.*

*Kwa hivyo, watu wanaponiuliza jinsi "nimejiweka sawa na Bwana," ninawaambia nimejazwa na Roho, na ninamwacha Mungu ayatawale mambo. Kisha mimi hukubali kwa shukrani anapoomba msaada wangu.*

*Sikuwahi kufikia lengo hilo lililokuwa linasongala. Ilinipiga.*

**DECEMBA 17** **351**

# Uinjilisti na Mahitaji ya Kibinadamu

*Naam, imewapendeza, tena wamekuwa wadeni wao. Kwa maana ikiwa Mataifa wameyashiriki mambo yao ya roho, imewabidi kuwahudumia kwa mambo yao ya mwili. Basi nikiisha kuimaliza kazi hiyo, na kuwatilia mhuri tunda hilo, nitapitia kwenu, kwenda Spania.*
*Warumi 15:27-28*

Maneno ya Doris yalizungumziwa kwa uhuru. Yeye na binti yake Sylvia walikuwa wakihudumu katika misheni ya uokoaji, na huko, walikuwa wamekutana na Fidel. Wakati mmoja alifanya kazi katika mkahawa wa ndani na aliishi katika chumba huko. Lakini katika umri wa miaka arobaini na sita, ugonjwa wa kisukari uliongezeka, na mguu mmoja wa Fidel ulilazimika kukatwa. Kwa hiyo, alipoteza kazi yake na nyumba yake. Siku hiyo, Doris aliuliza ikiwa darasa letu la shule ya ya Jumapili lingeweza kuungana na wengine kuchangisha dola 4,400 ili kumnunulia Fidel mguu wa bandia.

Darasa letu, ambalo linalenga kuwaleta watu katika uhusiano na Kristo na kuwasaidia kukua kama wanafunzi wake, lilikuwa limemaliza kutoa sadaka yetu ya Krismasi. Zaidi ya utoaji wao wa kawaida, washiriki wa darasa walichangisha zaidi ya $2,600 kwa ajili ya elimu ya watoto nchini Peru, Bangladesh, na Ethiopia. Je, wangeweza kutoa tena?

Baadaye juma hilo, Doris na Sylvia walimwambia Fidel kwamba darasa lilikuwa tayari limechangisha dola 674 kwa ajili ya mguu wake, Fidel alilia na kusema, "Asante, asante."

Paulo, katika safari yake ya uinjilisti hadi Uhispania kupitia Roma, alipata shangwe katika kukidhi mahitaji ya kimwili ya Yerusalemu kwa huduma ya upendo. Vivyo hivyo, darasa letu la shule ya Jumapili, katika safari yake ya uinjilisti na ufuasi, lilipata furaha katika kukidhi hitaji la Fidel. Leo, Doris, Sylvia, Fidel, nesi wa misheni ya uokoaji, na washiriki wa darasa letu wote wanafurika kwa shukrani kwa Mungu.[204]

**DESEMBA 18** **352**

# Ametumwa Ili Kuuokoa Ulimwengu

*Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.*
*Yohana 3:17*

Wazazi wangu walienda kanisani mara chache sana, lakini walifikiri nilipaswa kuhudhuria shule ya chekechea ya Jumapili kwa watoto. Msichana jirani alienda shule ya Jumapili, kwa hiyo mama yangu akatuacha sisi wawili kanisani, na jirani akatuchukua baada ya shule ya Jumapili. Wiki iliyofuata, akina mama hao wawili wangebadilisha majukumu. Jumapili fulani mama mmoja angefanya yote mawili—kutupeleka na kutuchukua.

Jumapili moja, tulipotoka shule ya Jumapili, hakuna mama aliyekuwepo kutuchukua. Msichana huyo mdogo, ambaye alikuwa na umri wa miaka sita, alijiona kuwa mtu mzima kabisa. Alisema, "Ninajua njia ya kurudi nyumbani." Nilikuwa na umri wa miaka mitano tu, na sikujua njia ya kurudi nyumbani.

Nyumba zetu zilikuwa maili mbili katika upande wa mashariki mwa kanisa. Alinishika mkono na kuanza kutembea kusini kwenye Barabara kuu, katikati ya jiji. Wakati huohuo, mama yangu alianza kujiuliza kwa nini nilichukuwa muda mrefu sana kufika nyumbani. Alimpigia simu jirani na kumuuliza, "Je, bado hujawachukua watoto?"

"Hapana," jirani akajibu, "nilifikiri ulienda kuwachukua."

---

204. Awali kilichapishwa katika *Reflecting God* June–July–August 2010 (Kansas City, MO: WordAction Publishing Co.), 17. Imetumika kwa idhini.

Mama yangu alienda katika kituo cha polisi kuripoti watoto wawili waliopotea. Mama yangu aliyechanganyikiwa alipokuwa amesimama kituoni akitoa ripoti yake, alichungulia dirishani na kuona watoto wawili wadogo wakitembea kwenye Barabara Kuu. Alitoka nje kwa kasi, akatuita, akaja haraka na kutukumbatia. Hakutuhukumu bali alitupenda na kutushikilia. Alituokoa. Ndani ya dakika ishirini, kila mtu alikuwa nyumbani salama na akifurahia.

Katika kitabu cha Mungu, hakuna siri kuhusu mpango wake kwa ajili yako, mimi, au ulimwengu: "Kwa maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye." Mungu alimtuma Mwana wake ili kuokoa ulimwengu.

Isaya, Yeremia, na manabii wengine wa Agano la Kale walihubiri. Sheria ilinguruma kutoka mlimani; hukumu ilitokea watu walipoasi. Ulimwengu ulioharibiwa na dhambi na uliopotoshwa na dhambi ulivurugika kurusha mawimbi makubwa au upepo mkuu; wanadamu, ambao walikuwa wamemwacha Mungu nje, walifanyiana uovu, wakionyesha ubaya wa dhambi. Yohana Mbatizaji alizungumzia hilo. Wafuasi wakuu wa Kristo kama Petro na Paulo walijitokeza kuongoza. Mungu alitumia kila kipengele alichoweza kututahadharisha, kutuamsha, kuweka alama za kupotoka, kutuzuia tusiendeshe kutoka kwenye jabali, na kutuelekeza kwa Kristo. Yeye ndiye njia, na kweli, na uzima (Yohana 14:6). Kristo anajaribu kuokoa ulimwengu, na yeye ni mpango wa Mungu kufanya hivyo. Mungu hana mpango mbadala—huu ndio wenyewe. "Hapana jina jingine chini ya mbingu..... litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12)—Yesu Kristo pekee.

Kristo alikuja kwa unyenyekevu, akakua hadi kukomaa, na akaanza kuhubiri na kufundisha. Aliwaponya vipofu na viwete; alitoa pepo; aliwafufua wafu; alitufundisha kupenda, kujali, kusamehe, kutumikia. Alikufa msalabani kwa ajili ya ondoleo la dhambi zetu na alifufuka kutoka kwa wafu. Sasa anatuombea akiwa kwenye mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu mbinguni, na anarudi duniani.

Sasa, anatuagize tufanye yafuatayo:

- Tuache dhambi zetu za uharibifu na laana
- Tufungue mioyo na maisha yetu kwake
- Tumpokee kama msamehevu wa dhambi zetu zote
- Tumfuate yeye kama kiongozi wa maisha yetu
- Kutoa maisha yetu yote kwake
- Tujazwe na kutakaswa na Roho wake Mtakatifu
- Tuyafurahie maisha ya maana, utele, furaha, umuhimu, upendo, na utimilifu

- Tuwaambie wengine kuhusu njia
- Kuwaleta watu pamoja nasi katika mbingu yake tukufu

Watu wanaweza kujitoa wenyewe kwa dhambi na hukumu, lakini Mungu anafanya kila awezalo kuwaleta watu kwa Kristo anayeokoa. Kwa mara nyingine tena: "Kwa maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye."

Ikiwa unashangaa kwa nini, hili jibu hapa: "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

**DESEMBA 19** **353**

# Uwepo wa Mungu

*Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine ili kuwasaidia na kuwa pamoja nanyi milele, huyo Roho wa kweli... Siku hiyo mtatambua ya kuwa mimi niko ndani ya Baba yangu, nanyi mko ndani yangu, nami niko ndani yenu.*
*Yohana 14:16–20*

Kama inavyofunuliwa katika vifungu vingi vya Agano la Kale, uwepo wa Mungu ulikuja kwa watu wake kwa njia za ajabu na hata za kutisha. Kwa mfano, sanduku la agano lilipoletwa katika hekalu la Sulemani, jambo hili lilitokea: "Ikawa, makuhani walipotoka katika patakatifu, nyumba ya BWANA ikajaa wingu; hata makuhani hawakuweza kusimama ili kufanya huduma yao, kwa sababu ya wingu lile; kwa kuwa nyumba ya BWANA ilikuwa imejaa utukufu wa BWANA" (1 Wafalme 8:10-11).

Mungu alikuja kwa njia isiyotisha sana Yesu alipokuja duniani. Hata wakati huo, hapakuwa na upungufu wa utukufu wa Bwana. Wachungaji wa kawaida walijionea wenyewe: "Malaika wa Bwana akawatokea, na utukufu wa Bwana ukawaangazia pande zote, wakaingiwa na hofu. Lakini malaika akawaambia, 'Msiogope. Nawaletea habari njema . . . Mwokozi amezaliwa kwenu . . . . Mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo na amelala kwenye hori" (Luka 2:9–12). Mtoto—wangeweza kushughulikia hilo.

Mtoto alipokua na kuwa mtu mzima, tuliona huduma yenye upendo na nguvu ya Yesu Kristo. Alitumia muda mwingi kujaribu kuwasaidia wanafunzi wake wamwelewe Mungu Baba. Alipokuwa akijiandaa kuondoka duniani,

alimwambia Filipo, "Husadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu? Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake" (Yohana 14:10).

Kisha Yesu akaahidi kwamba hatawaacha wanafunzi yatima. Aliahidi kutuma mwakilishi, Roho wa kweli, kuwa pamoja nao milele: "Siku hiyo mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi mko ndani yangu, nami ndani yenu" (14:20). Wakati Roho Mtakatifu, Mwakilishi, anapotawala moyo wako, Baba na Mwana wapo pia.  Mwana, na Roho—uwepo wa Mungu—huishi *ndani* yako.

Si ajabu Yesu alisema, "Yeyote anipendaye atayashika mafundisho yangu" (14:23). Ni kawaida kiasi gani kwamba uwepo wa kukaa ndani wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu husababisha maisha ya utii.

**DESEMBA 20** **354**

# Krisimasi, Waovu, na Wema

*Ndipo Herode, alipoona ya kuwa amedhihakiwa na wale majusi,*
*alighadhibika sana, akatuma watu akawaua watoto wote wa kiume*
*waliokuwako huko Bethlehemu na viungani mwake kote,*
*kuanzia wenye miaka miwili na chini yake,*
*kwa muda ule aliouhakikisha kwa wale majusi.*
*Mathayo 2:16*

Krismasi ya kwanza ilijumuisha mchanganyiko usio wa kawaida wa waovu na wema. Mathayo 2:11–12 inasimulia hadithi ya watu wenye hekima waliomjia Yesu Kristo: "Walipofika nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Maria mama yake, wakainama na kumsujudia. Kisha wakafungua hazina zao na kumpa zawadi za dhahabu, ubani na manemane. Nao wakiisha kuonywa katika ndoto wasirudi kwa Herode, wakarudi katika nchi yao kwa njia nyingine."

Lakini basi hakukuwa na mwitikio mzuri wa kuzaliwa huku kwa furaha. Mathayo 2:16 inaandika, "Herode alipojua ya kuwa amedanganywa na Mamajusi, alikasirika sana, akatoa amri wauawe wavulana wote katika Bethlehemu na jirani zake, waliokuwa na umri wa miaka miwili na waliokuwa na umri chini ya miaka miwili."

Vita hivi vinaendelea leo—hata Krismasi hii, katika ulimwengu wetu. Niliiona huko Newport, Oregon, wakati wa ibada za ufufuo. Tulipitia msukumo usio wa kawaida wa Roho Mtakatifu, na idadi kubwa ya watu

walijitokeza kuomba. Mwanamke mmoja aitwaye Gail alikuwa mmoja wao. Gail alikuwa na fikra bunifu. Aliunda sehemu akilini mwake ambapo angeweza kwenda kuomba. Ikiwa alikuwa na mawazo ambayo hapaswi kuwa nayo, aliyaweka kwenye "shimo" la akili yake. Tatizo ni kwamba, baada ya muda, shimo hilo linaweza kujaa uchungu, kuumizwa, maumivu, na chuki. Wakati wa ibada ya Jumatatu usiku aliniambia, "Jana usiku nilimpa shimo na akalisafisha. Nililala usingizi mzito zaidi niliowahi kuwa nao kwa muda mrefu. Niko huru zaidi leo."

Namjua Gail ni mtu mmoja tu katika ulimwengu mkubwa na wenye matatizo, lakini wiki baada ya wiki, katika ibada maalum za kuwasilisha habari njema za Kristo, na kwa huduma na ushuhuda wa Wakristo wengi, watu wanabadilishwa. Kujumlisha yote kunaleta tofauti kubwa.

Leo Mfalme Herode amekufa na amevunjiwa heshima, huku Yesu, Mwokozi, yu hai milele na kuabudiwa na mamilioni. Na Gail yuko huru—na wengi kama yeye pia wako huru.

Licha ya magumu ambayo unaweza kukutana nayo, kumbuka Krismasi hii kwamba Yesu atakuwa na neno la mwisho.[205]

**DESEMBA 21** **355**

# Krisimasi . . . kama "Ilivyotimizwa"

*Akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti; ili litimie neno lililonenwa na manabii, Ataitwa Mnazareti.*
*Mathayo 2:23*

Je, haishangazi ni mara ngapi neno "kutimia" ni sehemu ya hadithi ya Krismasi? Hapa kuna mifano michache:

- Mathayo 1:22-23 — "Hayo yote yamekuwa, ili *litimie* neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema, Tazama, bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake Imanueli; Yaani, Mungu pamoja nasi."

205. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Disemba 2008).

- 2:15 — "Akakaa huko hadi Herode alipokufa; ili *litimie* neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii, akisema, Kutoka Misri nilimwita mwanangu."
- 2:17-18 —"Ndipo *lilipotimia* neno lililonenwa na nabii Yeremia, akisema, 18 Sauti ilisikiwa Rama, Kilio na maombolezo mengi, Raheli akiwalilia watoto wake, Asikubali kufarijiwa, kwa kuwa hawapo tena."
- 2:23 — "Akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti; ili *litimie* neno lililonenwa na manabii, Ataitwa Mnazareti."

Matukio haya ni ushahidi wa ukweli wa kuzaliwa na maisha ya Yesu, ukweli wa Maandiko, uaminifu wa Mungu, na mamlaka ya ujumbe wa Bibilia. Bado ninatazamia *utimiligu* mwingine wa Yesu:

- 24:44 — "Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyotazamia Mwana wa Adamu yuaja."

Tunatimizwa tunapomfanya Kristo awe kitovu cha maisha yetu. Krismasi hii, na ufurahie faida zote za ahadi zilizotimizwa mara ya kwanza na uwe tayari kwa ile ambayo bado inakuja.[206]

**DESEMBA 22** **356**

# Mtoto Ndani ya Hori: Mfalme Katika Utukufu Wake

*Kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu.*
*Waraka kwa Waebrania 9:28*

Ikiwa Krismasi ya kwanza ilikuwa mtoto kwenye hori, je, Krismasi hii inaweza kuwa Mfalme katika utukufu wake?

Katika usomaji wa kawaida wa Bibilia, nimeathiriwa na idadi ya matangazo kuhusu kurudi kwa Kristo. Tazama hapa chini baadhi ya aya hizi:

- Waebrania 9:27-28—"Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu; kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu."

206. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Disemba 2010).

- Tito 2:11-14—"Maana neema ya Mungu iwaokoao wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa; tukilitazamia tumaini lenye baraka na kufunuliwa kwa utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wake mwenyewe walio na bidii katika matendo mema."
- 2 Wathesalonike 1:7-10—"na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake, katika muali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake; yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake, na kustaajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile, (kwa sababu ushuhuda wetu ulisadikiwa kwenu)."

Kujifunza zaidi, soma 2 Timotheo 4:1–2, 1 Wathesalonike 4:16–17, na 2 Petro 3:9–13.

Niko tayari![207]

**DESEMBA 23** **357**

# Heri Njema ya Siku ya Kuzaliwa, Yesu!

*Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia; nao walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu, uvumba na manemane.*
*Mathayo 2:11*

Kutoka mashariki, mamajusi walifuata nyota ya Yesu na kuja kumwabudu, wakiwa wamebeba zawadi za bei ghali. Tangu wakati huo, ulimwengu umetoa kidogo kwa Yesu, lakini tazama kile alichotoa kwa ulimwengu:

- "Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka dhambi zao" (Mathayo 1:21).

207. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (December 2016).

- “Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. .... Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia” (Luka 2:11-14).
- Yesu: “Mwizi huja tu kuiba, kuua na kuharibu; mimi nilikuja ili wawe na uzima, tena wawe nao tele” (Yohana 10:10).
- Yesu: “Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali” (Yohana 14:2).
- Yesu: “Mkiniomba neno lolote kwa jina langu, nitalifanya” (Yohana 14:14).
- Yesu: “Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga” (Yohana 14:27).
- Yesu: “lakini yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele” (Yohana 4:14).
- Yohana: “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16).

Ilikuwa siku yake ya kuzaliwa, lakini amegeuka kuwa mtoaji mkubwa wa zawadi. Nimemwona akitoa baadhi ya karama hizi, kama vile uzima wa milele, na uzima kwa ukamilifu. Niliona zawadi hizi zikija kwa Bill, Keith, Laura, Dennis, Frank, Peggy, Rachel, Paul, na Miriam.

**DESEMBA 24** **358**

# Inawezekanaje?

*Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu. Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.*
*2 Wakorintho 5:20-21*

Siku zote nilijiuliza: Inawezekanaje kwamba mwingine anaweza kuchukua gharama na jukumu la dhambi yangu? Sikuwa na tatizo kuhusu ukweli kwamba “wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu” (Warumi 3:23). Niliona hilo katika maisha yangu mwenyewe na katika

ulimwengu unaonizunguka. Na katika mwanga wa utakatifu kamili wa Mungu, nilitambua kwamba "mshahara wa dhambi ni mauti" (Warumi 6:23). Namaanisha, ungetarajia nini kingine? Lakini niliona kuwa vigumu zaidi kukubali jinsi mwingine angeweza kuchukua gharama na wajibu wa dhambi *yangu*.

Mwanangu, Paul, alikuwa na miaka kumi na sita au kumi na saba, na nilikuwa nikilala Jumapili mchana. Nikiwa nimelala, Paul alitoka nje ya nyumba kwa siri, akachukua gari langu bila ruhusa yangu, na kumchukua rafiki yake. Kinyume na ombi langu la kuitakasa Jumapili, walishiriki mchezo wa mpira wa vikapu wa wataalamu. Wakiwa njiani kuelekea nyumbani, Paul aliipita taa ya njano ikiwa inageuka kuwa nyekundu na kugongana na gari lingine.

Alipofika nyumbani, alisema kwa unyogovu, "Baba, nimeliharibu gari, lakini nitalipia." Wakati huo, tulikuwa na bima ya dhima lakini si bima ya mgongano au ajali. Majeraha mengine ya gari na abiria yalilipwa, lakini tungelazimika kutoa pesa nyingi kwa ajili ya ukarabati wa gari letu.

Ikiwa nitakumbuka kwa usahihi baada ya miaka hii yote, nadhani mwanangu alilipa dola tano kwa ajili ya ukarabati wa gari. Nilichukua gharama nyingine zote, mazungumzo ya kisheria, makaratasi, na majadiliano ya bima. Nilichukua gharama na wajibu wote wa dhambi ya mvulana wangu ili aweze kuwa huru, kusonga mbele, na kuwa ushawishi wa wema katika maisha ya wengine.

Ikiwa ninaweza kuyaitikia matokeo ya dhambi za mwanangu, basi ninaelewa (na kufurahi) kwamba Kristo angechukua dhambi yangu juu yake na hivyo kunibadilisha kwamba ningeweza, ndani yake, kuwa haki ya Mungu.

**DESEMBA 25** **359**

# Aliota Ndoto

*Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu.*
*Mathayo 1:20*

Kwa aibu kutokana na ujauzito wa mchumba wake, hakujua afanye nini hasa kwa vile alijua yeye si baba. Kisha akaota ndoto, na malaika wa Bwana

akasema naye: "Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka dhambi zao" (Mathayo 1:20-21).

Je, unajua Yusufu alisubiri kwa muda gani ili kuona ndoto ya Yesu kuwaokoa watu kutoka katika dhambi ikitimia? Wewe na mimi tunaona kile ambacho Yusufu hakuona.

Siku chache zilizopita, katika kanisa la Ohio, nilimwona Samantha akilia na kuomba. Aliniambia, "Nilikuwa na mzigo—sasa ninahisi mwepesi kama manyoya. Nimejitoa kikamilifu kwa Bwana!" Yesu mwenye kubeba mzigo alimwokoa kutoka katika dhambi zake.

Krismasi hii, nina ndoto fulani—ndoto mahususi, ndoto za familia, ndoto za ulimwengu mkubwa. Ndoto yangu kubwa ni kwamba Yesu anayesamehe, anayeweka huru ataleta vuguvugu kuu la kiroho ambalo litazalisha ushuhuda, uinjilisti, uamsho, na utakatifu katika makanisa na ulimwengu wetu uliochanika.

Nina hakika unazo ndoto Krismasi hii pia. Acha ndoto zako kubwa na bora zitimie. Yusufu alifanya hivyo![208]

**DESEMBA 26** **360**

# Atawasha Taa

*Kulikuwako Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu,*
*akija katika ulimwengu.*
*Yohana 1:9*

*Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu,*
*ndio wale waliaminio jina lake.*
*Yohana 1:12*

Ilikuwa ibada ya chuo kikuu—ikiwa utajiunga na kundi fulani, utahitaji kuvumilia kipindi cha mafunzo ya mara ya kwanza. Tukio la kuogofya zaidi lilikuwa ni ndugu walikuchukua kwa "safari." Usiku mmoja, mwenzangu,

208. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Disemba 2009).

Al, alikimbilia kwenye mlango wetu wa bweni na kuufunga. Akapiga kelele, “Wanakuja!”

Haikuwa na manufaa; waliingia kwa njia ya malango wa dharura ya moto. Walitufunga mikono, wakatuwekea foronya juu ya vichwa vyetu, na kutuingiza kwenye gari. Waliendesha gari, wakifanya zamu nyingi njiani, kisha wakasimama. Hatimaye, waliondoa foronya kwenye vichwa vyetu, wakatutoa nje ya gari, kisha wakaondoka.

Tulikuwa kwenye uwanja mkubwa wa wazi kwenye giza-nyeusi, na sikutambua chochote. Nilikuwa na wasiwasi.

Kwa bahati nzuri, Al alisema hivi: “Ninajua tulipo. Nilishawahi kuwa hapa kabla.”

Lo! Nuru kidogo ya matumaini. Mwishoni mwa uwanja, tulianza kwenye barabara mbovu ya changarawe. Tulipopita kila nyumba ya shamba, mbwa wa ulinzi walibweka na kukimbia kuelekea tulipo. Kila wakati, tulisikia mlio wa mnyororo wa kuzuia.

Hatimaye, kulikuwa na mwanga kidogo. Punde tukaona taa za mji wetu. Muda si muda, tulikuwa tumerudi chumbani kwetu, na mwanga mkali ulikuwa umewaka.

Yesu Kristo tayari ndiye Mwokozi wa nuru. Katika Injili ya Yohana, neno “nuru” limetumika mara ishirini na moja. Katika Yohana 8:12, Yesu ndiye “nuru ya ulimwengu; katika Yohana 1:9, Yesu “hutoa nuru kwa kila mtu.” Hiyo inajumuisha wewe.

Ikiwa umewahi kuwa kwenye changamoto maishani mwako, unaweza kuhisi kama hujui la kufanya. Inaweza kuwa uamuzi mkubwa; kifo cha mpendwa; afya mbaya; shinikizo la kifedha; uhusiano uliovunjika; ukosefu wa kazi; wakati ujao usio na uhakika; hali ya jamii; kutengwa na Mungu. Kwa maeneo haya yote ya giza, anatoa tukio kubwa zaidi la kutoa mwanga katika maisha yako: “Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake” (Yohana 1:12).

Nilikuwa nimemjua Yesu siku chache tu tulipoimba “Ewe Mji Mdogo wa Bethlehemu” katika ibada ya chuo kikuu. Mashairi ya nyimbo hizo yalizungumza nami kuliko hapo awali:

*Lakini kuna nuru katika barabara zako zenye giza*
*Nuru ya milele*
*Matumaini na woga wa miaka yote*
*Yanatimia kwako usuku wa leo*

Kisha,

*Ewe Mtoto mtakatifu wa Bethelehemu*
*Tunaomba, ushuke kwetu*

*Ondoa dhambi zetu, na uingie ndani*
*Uzaliwe ndan yetu leo*[209]

Kristo atakuwashia taa.

DESEMBA 27 361


## Taswira Inayoelekea Utakaso

*Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni.*
*1 Wakorintho 2:14*

*Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohoni, bali kama na watu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. Niliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi, kwa maana hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana, ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je! Si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu?*
*1 Wakorintho 3:1-3*

Tutaangalia baadhi ya picha ili kuelewa hatua za maisha ya Kikristo na jinsi ya kuingia katika maisha yaliyotakaswa. Katika maandiko ya leo, Paulo anazungumza na Wakristo katika kanisa la Korintho. Miduara iliyo hapa chini inawakilisha vikundi vitatu vya watu anaowaelezea, pamoja na maisha ya watu leo:

209. Phillips Brooks (words) and Lewis H. Redner (music), "O Little Town of Bethlehem," *Sing to the Lord: Hymnal* (Kansas City, MO: Lillenas Publishing Company, 1993), #169.




Mwanadamu wa asili hakubali kile kitokacho kwa Roho. Badala yake, wanaishi kwa rasilimali zao za asili za kibinadamu. Mduara unawakilisha maisha; kiti cha enzi ni kiti cha udhibiti katika maisha ya mtu. "Kujigamba" kukuu kwenye kiti cha enzi ni ubinafsi. Nyota (maslahi ya maisha) ni maonyesho ya udhibiti wa msingi – "Kujigamba" kukubwa. Zinakusudiwa kuonekana kama miduara potofu, na zinaweza kuwa maisha ya kifedha, maisha ya kijamii, maisha ya kikazi, maisha ya nyumbani, maisha ya kidini, na zaidi. Katika maisha ya mtu mmoja, mwonekano mkubwa wa nje wa dhambi unaweza kuwa ni mambo ya sherehe na anasa; kwa mwingine, inaweza kuwa ni kuabudu pesa. Maneno ya dhambi yatakuwa tofauti kwa watu tofauti. Msalaba unawakilisha Kristo akibisha hodi kwenye mlango wa moyo. Baada ya upinzani, hatimaye mtu huyu anasema ndiyo kwa Kristo na kumwalika moyoni mwake, kama katika Ufunuo 3:20.

Maisha mapya huanza. Kristo anasogea kwenye kiti cha enzi—kituo cha udhibiti. Masilahi ya maisha yanakuwa na usawa zaidi. Hata hivyo, baada ya muda, Mkristo huyu anagundua vita vya ndani. 3"Kujigamba kukubwa" hakutaki kuachilia udhibiti, na vita vya udhibiti vinazuka. Vita hivi vimefafanuliwa katika Wagalatia 5:16–24 na Warumi 8:5–8. Kunaweza kuwa na maonyesho ya ndani ya wivu au ugomvi wa nje. Huyu ni Mkristo wa kilimwengu, au wa kimwili.

Mkristo huyu mwenye matatizo anahisi kwamba lazima kuwe na jambo bora zaidi. Baada ya kusikia kwamba Mungu anaweza kumtakasa mtu kabisa, mtu huyu anamtafuta Mungu. Mtu anapomwamini Mungu wa 1 Wathesalonike 5:23–24, Kristo anachukua udhibiti kamili wa kiti cha enzi, na "kujigamba kukubwa" kwenye ubinafsi kunatupwa nje. Nguvu ya Mungu ya kutunza hudumisha Mkristo huyu. Imejengwa juu ya 1 Wathesalonike 5:23–24, Matendo 15:8–9, Waefeso 3:14–20, Warumi 8:2 na 4, huyu ndiye Mkristo wa kiroho—au aliyetakaswa.

Ni mduara gani zaidi unaowakilisha maisha yako ya sasa? Ni mduara gani unaofanana zaidi na maisha ambayo ungependa kuwa nayo?

**DESEMBA 28** **362**

# Dhiki ya Chad

*Lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka wa ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu.*
*Warumi 7:23*

Je, inafananaje kutakaswa, kujazwa na Roho? Inatokeaje? Hivi ndivyo ilivyotokea kwa kijana mmoja anayeitwa Chad, kwa maneno yake mwenyewe:

> *Nikiwa na umri wa miaka ishirini na minne, nilihitimu shahada yangu ya Udaktari wa Famasia na kuanza kazi yangu ya kwanza kama mfamasia katika mji wangu. Nilikuwa na gari jipya linalong'aa, nilikuwa nikipata pesa nzuri, na nilikuwa na msichana mrembo. Nilihudhuria kanisa mara kwa mara kadiri nilivyoweza, lakini ilikuwa ni wajibu zaidi kuliko kitu chochote. Kwa ujumla, mambo yasingekuwa bora zaidi. Nilikuwa karibu kama nilivyokuwa nimewahi kuishi ndoto ya Marekani; hata hivyo, kitu*

*kikubwa kilikuwa kinakosekana katika maisha yangu, kama nilivyotambua mapama.*

*Uhusiano wangu na rafiki yangu wa kike (sasa ni mke wangu), Celia, ulipozidi kuwa mbaya, tulianza mazungumzo ya kina kuhusu dini. Uligundua kwamba maoni yetu yalikuwa tofauti kidogo: Mimi nilikuwa Mbaptisti, naye alikuwa Mnazarene. Ikiwa mimi ni mwaminifu kabisa, sikuwahi kusikia habari za Wanazarene hapo awali, kwa hiyo mara moja niliona maoni yangu kuwa bora kuliko* yake kutokana na umaarufu wa dhehebu langu. *Niliamini kwa moyo wote kwamba mara tu mtu alipookolewa na Mungu, hakuna kitu ambacho kingeweza kubadili hilo—hata mtindo wangu wa maisha. Katika maisha yangu ya kila siku, nilitangaza kuwa Mkristo; hata hivyo nikiangalia nyuma, ninaona kwamba mawazo yangu, tabia, na vitendo havikuwa tofauti sana na wale wasiokuwa Wakristo karibu nami. Sikuona hili kama jambo kubwa, kwa sababu, "Sisi sote ni binadamu hata hivyo!" Kulikuwa na dhambi iliyo wazi katika maisha yangu, lakini nilikuwa na hisia kwamba hakuna kitu nilichoweza kufanya kuhusu hilo, hivyo niliendelea pamoja bila kufikiri sana. Hata hivyo nilielewa kwamba Celia alihisi tofauti: aliamini kwamba tumeitwa kuishi maisha ambayo ni matakatifu na yanampendeza Mungu na kwamba, kwa msaada wa Roho wa Mungu, tunaweza kuishi kwa kuishinda dhambi ya kukusudia.*

*Bila kusema, kutokubaliana huku haraka kukawa hatua ya ugomvi katika uhusiano wetu. Hapo ndipo nilipogundua kuwa naweza kutatua tatizo hili. Kwa kuwa nilizingatia mambo ya kisayansi, ningeichunguza Bibilia na kukusanya "ushahidi" mwingi kadiri niwezavyo ili kuunga mkono maoni yangu, kisha kuuwasilisha kwa Celia kwa njia isiyopingika. Nilijua kwa hakika kwamba nilikuwa sahihi; Nilihitaji tu kumwonyesha. Mara nilipofanya hivyo, asingefurahishwa tu, lakini kutoelewana kati yetu kungetatuliwa. Hata hivyo, nilipoazimia kuibua "ushahidi" huu, upesi nilipata kitu tofauti kabisa na nilichokuwa nikitafuta.*

*Katika utafutaji wangu, niligundua mada kadhaa ambazo sikuwahi kuziona hapo awali. Nilikutana na maandiko kama haya yafuatayo:*

- *Marko 13:13—"Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kuvumilia hadi mwisho, ndiye atakayeokoka."*
- *Yohana 15:6—"Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea."*
- *Wakolosai 1:22-23—"katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu, wasio na mawaa wala lawama; mkidumu tu katika ile imani, hali mmewekwa juu ya msingi,*

*mkawa imara; msipogeuzwa na kuliacha tumaini la Injili mliyosikia habari zake, iliyohubiriwa kwa viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu; ambayo mimi Paulo nilikuwa mhudumu wake."*

- *Waraka kwa Waebrania 10:26—"Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi."*
- *1 Yohana 3:6—"Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi; kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua."*

*Ningeweza kuendelea na kuendelea, lakini inatosha kusema kwamba nililemewa sana na mada hii kuu iliyo wazi. Kwa miaka mingi nilikuwa nimesoma Maandiko kwa vipande-vipande tu, lakini mara nilipoanza kutafakari kwa kina zaidi, niliona kwamba mada hii ya kuendelea, kubaki, na kuishi bila dhambi ilihusisha Biblia nzima. Ikawa dhahiri kwangu mara moja kwamba Mungu hataki tuendelee kutenda dhambi baada ya kuokolewa—na kwamba kuna mengi zaidi katika mwenendo huu wa Kikristo kuliko kuokolewa kisha kungojea mbinguni. Misheni yangu ya awali ilikuwa imeshindwa. Badala ya kupata uthibitisho wa kwamba nilikuwa sahihi, nilianza kuona kwamba nilikosea—na bila shaka niliogopa kukiri hivyo kwa Celia!*

*Baada ya haya, nilianza kuhisi mwito wa wazi wa Mungu kwa utakatifu na uhusiano wa kina zaidi naye. Si kwa bahati, nilitambua wakati huo kwamba maisha yangu yalihitaji "kusafishwa." Sikuwa mtu mbaya sana katika maoni ya ulimwengu—sikutumia dawa za kulevya au kunywa kileo au kuumiza watu. Lakini nilipambana na hasira, kiburi, na ubinafsi, miongoni mwa mambo mengine. Kwa ufunuo huu kutoka kwa Mungu, mambo yalianza kubadilika katika maisha yangu. Nilianza kuchangamkia mambo ya Mungu kwa sababu kwa mara ya kwanza, nilitambua umuhimu wa kuwa na uhusiano naye. Niliamua kwamba ningeanza kuishi kwa Mungu kweli na kushikilia upande wangu wa uhusiano huu! Hata hivyo, upesi nilichanganyikiwa na kuudhika kwa sababu jitihada zangu zingeshindwa. Ule msemo wa zamani, "Hujui jinsi ulivyo mbaya hadi ujaribu kuwa mzuri," ulionekana kuwa kweli kwangu. Ilionekana kwamba haijalishi jinsi nilivyojaribu sana kubadili njia zangu, mawazo yangu, tabia zangu, mazoea yangu, sikuweza kufanya hivyo kwa uthabiti wowote. Nilisimulia vizuri sana maneno ya Paulo katika Warumi 7:18b–19, ambapo anasema, "Kwa maana nina shauku ya kufanya lililo jema, lakini siwezi kulitimiza.*

*Sitendi jema ninalotaka kufanya, lakini lile baya ambalo sitaki—hilo ndilo ninaloendelea kufanya." Nilishindwa tena na tena na tena.*[210]

DESEMBA 29 **363**

# Ukombozi wa Mungu

*Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu.*
*1 Wathesalonike 4:3a*

*Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti.*
*Warumi 8:2*

Chad anaendelea:

*Siku baada ya siku, nilizidi kutoridhika na kukasirika, hadi siku moja, hatimaye nilifikia hatua ya kukataa tamaa na kufadhaika. Nilipiga magoti ili kuomba na kuanza kulia sana. Nilimwambia Mungu jinsi nilivyochanganyikiwa na jinsi nilivyotaka kuishi kwa ajili yake,* lakini *hata nijitahidi kwa kadiri gani, sikuweza. Nilikuwa nimeamua tu kwamba maisha haya matakatifu niliyokuwa nimesoma kuyahusu hayakuwa jambo ambalo ningeweza kufikia; ni wazi lilikuwa ni agizo lisilowezekana, na, katika majaribio yangu ya bure, moyo wangu ulivunjika.*

*Sitasahau kamwe kilichotokea baadaye. Ilikuwa wakati huu nilipomsikia Bwana akinong'ona moyoni mwangu, "Hapana, huwezi kufanya hivyo—lakini ninaweza."*

*Ghafla, nilishindwa na uwepo wake na kugundua kwa muda kile nilichokuwa nikikosa; Nilikuwa nikijaribu kufanya yote kwa nguvu zangu. Nisingeweza kujibadilisha; Nilimhitaji ili anibadilishe! Na kwa hiyo, katika wakati huo, niliomba ili nimpate zaidi. Nilikubali kwamba nilijaribu kwa nguvu nilizoweza kupata, lakini haikutosha—nilihitaji Roho wake kunisaidia. Nilikuwa nimefika mwisho wangu, na hapo ndipo nilipomkuta akisubiri. Nilisalimisha maisha yangu na mapenzi yangu kwa Bwana siku hiyo—ni wakati ambao sitausahau na nitauthamini daima.*

---

210. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Septemba 2018).

*Baadaye, ningejifunza kwamba "kujisalimisha" huku kunaenda kwa majina mbalimbali: utakaso mzima, ubatizo wa Roho, kazi ya pili ya neema, n.k. Lakini bila kujali unaiitaje, najua haya: tangu wakati huo na kuendelea, nimekuwa mwanaume tofauti kabisa. Kitu chenye nguvu kilinitokea, na, tangu wakati huo, nimekuwa na njaa ya Bwana kwa njia ambazo sikuwahi kuwa nazo hapo awali. Nimewasiliana naye kila siku na bila kukatizwa, na maisha yangu hatimaye "yalisafishwa"—sio kwa kujaribu zaidi, lakini kwa kujisalimisha kwake kila siku na kuruhusu Roho wake kuwa na njia yake maishani mwangu. Mambo ambayo nilihangaika nayo wakati huo sio suala tena. Bado ninatembea kwa ukaribu niwezavyo kwake jinsi ninavyoongozwa na Roho, na imeleta mabadiliko yote katika ulimwengu maishani mwangu. Kwa hakika ninaweza kutafakari nyuma wakati ule wa shida nilipojitoa kikamilifu kwa Mungu; hata hivyo, pia nimekuja kutambua kwamba utakatifu kw asana ni mchakato wa kila siku. Ni muhimu kwamba tufikie wakati wa kujisalimisha—lakini lazima tuendelee kusalimu amri kila siku katika maisha yetu. Ninaweza kusema kwa moyo wote kupitia tukio hili kwamba njia pekee ya ushindi wa kweli na wa kudumu wa kiroho ni kupitia utakaso wa Mungu wa mioyo yetu kupitia utakaso—na yeye ni mwaminifu kufanya hivyo ikiwa tutashirikiana na upendo na neema yake.*

*Miezi kadhaa baadaye, hamu hii ya kuingia ndani zaidi na Mungu ilianza kufikia kilele cha mwito wa huduma. Nilianza kutambua jinsi mambo hayo yote yalivyokuja pamoja kwa njia ambayo Mungu pekee ndiye anayeweza kupanga. Nilikuwa na maswali kwa Mungu, ni wazi, lakini amekuwa mwaminifu kujibu kila moja njiani. Nilipomuuliza jinsi nilipaswa kuwa mchungaji nilipokuwa tu nimefuzu kutoka Chuo cha mafunzo ya ufamasia, Mungu alinitumia mhudumu mstaafu na mfamasia wa zamani ambaye alikuwa mjini kwa miezi michache tu kwa wakati ufaao. Nilipogundua kuwa singeweza tu kuacha kazi yangu kama mfamasia kutokana na mikopo ya wanafunzi niliyokuwa nayo, Mungu alinitambulisha kwa mchungaji wa elimu ya juu. Nilianza kutambua kwa mara ya kwanza kwamba naweza kuwa mfamasia na mchungaji, kwa hiyo niliendelea na harakati zangu. Nilipokuwa nikishindana na gharama za seminari juu ya mikopo ya shule ya mafunzo ya ufamasia, Mungu alinitambulisha kwa mchungaji mwingine ambaye aliniambia kuhusu mpango unaoitwa Course of Study, ambao ungeniongoza kuelekea kuwekwa wakfu kwa njia ya gharama nafuu zaidi kuliko seminari. Wakati wote huo, Mungu amejibu maswali na mashaka yangu.*

*Sasa mimi ni mzee aliyetawazwa kanisani, na kwa sasa ninahudumu kama mchungaji kijana katika kanisa moja katikati mwa Georgia. Sijui*

*Mungu ana mpango gani kwa ajili yangu katika siku zijazo, lakini najua tayari yuko huko. Neema yake inatosha kweli, na, kwa hilo, ninashukuru sana! Utukufu kwa Mungu!*[211]

**DESEMBA 30** **364**

# Jinsi ya Kutakaswa

*Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu*
*na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe muwe kamili,*
*bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo.*
*Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya.*
*1 Wathesalonike 5:23-24*

Alikuwa na furaha kabisa! Mchungaji wake alikuwa amemwomba achukue wadhifa mkubwa katika kanisa lake mahalia wadhifa ambao ungehitaji kujitolea sana na kazi ngumu sana. Sasa hakuwa na furaha tu, bali alisisimka—ilimbidi amwambie mtu.

Kipindi cha nyuma, Keith, ambaye alikuwa akikua katika maisha yake ya Kikristo, alienda ndani zaidi na Bwana, na Mungu akamtakasa kabisa. Alipofika mahali hapa maishani, alikuwa akijionea kusudi kuu la Mungu kwa maisha yake—kama mtu mmoja alivyosema, alikuwa akiishi kama "mtu bora zaidi". Zaidi ya yote, unapotafuta kutakaswa, kumbuka kwamba kiwango hiki kipya cha maisha kitakupa furaha kubwa na utimilifu.

Kwa kuwa tumekuwa tukipitia katika wiki za mawazo ya ibada, tumegundua kwamba kuna idadi ya maneno ya kibiblia ili kuelezea maisha ya kina ya Kikristo:

- Imani iliyosalia (Waebrania 4:9-11)
- Kusulubishwa pamoja na Kristo (Wagalatia 2:20)
- Kutakaswa kabisa (1 Wathesalonike 5:23)
- Kujazwa na Roho Mtakatifu (Matendo 1:8;13:9)
- Kristo kutulia na kujihisi nyumbani moyoni mwako (Waefeso 3:17)

Maneno mengine yanaelezea vipengele vya maisha haya:

- Mito ya maji ya uzima (Yohana 7:38)
- Ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele (Yohana 10:10).

211. Awali kilichapishwa katika *The Good News: The Chic Shaver Center for Evangelism Newsletter* (Septemba 2018).

Labda umekuwa ukitamani kuingia na kufurahia maisha haya ya kina. Umejiuliza unatakiwa kufanya nini ili Mungu afanye kazi hii ndani yako. Utapata idadi ya hatua hapa chini. Tafadhali elewa kwamba hatua hizi hazichukuliwi kwa njia ya kiufundi, lakini badala yake, ni vipengele vya kumtafuta Mungu kwa kina kwa moyo.

- Wasiwasi: Una mahangaiko ya kina kwa Mungu kukuleta katika maisha haya ya ushindi na utimilifu. Unaomba (Matendo 1:12–14; Luka 11:9–10, 13).
- Kujiweka wakfu: Lazima uwe tayari kuwa Mkristo. Sasa unatoa maisha yako yote yaliyosamehewa kwa Mungu asilimia 100, ili yatumiwe naye apendavyo (Warumi 6:13; 12:1–2).
- Utakaso: Unamwomba Mungu akutakase, akusafishe dhidi ya ubinafsi uliosalia au kujifikiria mwenyewe (1 Yohana 1:7; Matendo 15:8–9; Yakobo 4:8).
- Kudai: Kudai ahadi za Mungu, unaomba kwa imani na kumwamini Mungu kukutakasa kabisa (Matendo 26:18; Wagalatia 3:14; 1 Wathesalonike 5:23–24 [hasa tegemea mstari wa 24]).

Ukifuata hatua hizi kwa dhati kwa wakati halisi mbele za Bwana, Mungu atakutakasa na kukujaza kwa Roho Mtakatifu. Kumbuka 1 Wathesalonike 5:23–24: "Mungu mwenyewe, Mungu wa amani, awatakase kabisa.... Yeye anayewaita ni mwaminifu, naye *atafanya*." Mungu anaweza kuuchunguza moyo wako kwa undani sana unapoomba hivi.

Hilo lilikuwa kweli kwa Cheri. Alihudhuria darasa la Jumanne usiku nililofanya kwa wenzi wa wanafunzi wa seminari. Alinijia baada ya darasa jioni moja na kusema anatamani ningetoa wito wa madhabahuni baada ya darasa la juma lililopita kwa sababu alikuwa amehukumiwa sana. Alipokuwa akienda nyumbani na mwanandoa mwingine wa seminari usiku huo, hakusikia neno ambalo mwanamke huyo alisema. Alihisi yuko katika ulimwengu mwingine.

Alipofika kwenye nyumba yake, mume wake alimsalimia, lakini akasema, "Mpenzi, siwezi kuzungumza. Nina kazi ya kufanya."

Huku akitokwa na machozi, alikwenda kwenye chumba cha kulala cha nyuma. Alijifungia ndani na kusali hadi usiku. Ilionekana kana kwamba Roho Mtakatifu alifika ndani kabisa katika moyo wake na kuleta suala mbele yake. Alihangaika juu ya suala hilo, na mwishowe akasema, "Sawa, sawa, sawa, nitakupa."

Ndipo Roho akaingia moyoni mwake tena na kuleta suala jingine. Hii iliendelea na kuendelea hadi akahisi alikuwa ametoa kila kitu kichafu. Lakini Roho alishuka tena na kuibua jambo lingine: *"Cheri, unamwekea kinyongo mume wako mwenyewe. Nimemwita ahubiri, na nilitarajia umfuate. Hata*

*hivyo umemwekea kinyongo kwa sababu, ili kufuata wito huo, ulipaswa kuacha nyumba yako nzuri na kuhamia nyumba ndogo; ulilazimika kuacha kazi zenye faida kubwa na kuchukua kazi za kawaida zaidi; wewe umemwekea kinyongo. Si sawa.*"

Hatimaye, akamwambia Bwana, "Sawa, ninakupa. Na Mungu akamkubali na kumtakasa.

Katika darasa lililofuata, aliniambia, "Loo, Profesa Shaver, wiki hii imekuwa nzuri sana. Najisikia huru sana. Mzigo umekwenda—niko huru."

Alikuwa na furaha kabisa—ndiyo, alikuwa huru. Mungu alikuwa ameondoa kinyongo chake na ubinafsi wake. Alikuwa amefanya muujiza ndani yake. Alikuwa amemtakasa kabisa.

Usiogope Mungu akikuchunguza unapoomba. Matokeo yatakuwa mazuri sana, na yanaweza hata kusababisha utakaso wako.

**DESEMBA 31** **365**

# Wakati wa Kuomba

*Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli.*
*Yohana 17:17*

*Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani. Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.*
*Waefeso 3:16-19*

*Nao waliposikia, wakampazia Mungu sauti zao kwa moyo mmoja, wakisema, Mola, wewe ndiwe Mungu, ndiwe uliyefanya mbingu na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo.*
*Matendo 4:24*

*Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.*
*Matendo 4:31*

*Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho.*
*Waefeso 5:18*

Kwa kuzingatia yote ambayo umesoma na kufikiria unaposoma kitabu hiki, labda ni wakati *wako* wa kuomba . . . .

- Iliutakaswe
- Ili ujazwe na Roho
- Ili kuokea ujazo mpya wa Roho
- Kuweka upya maisha endelevu ya utimilifu wa Roho

Au je, ni wakati wa kumshukuru Mungu kwamba tayari amefanya haya yote kwa ajili yako?

Tuombe!

# Faharasa ya Maandiko

❖

## AGANO LA KALE


**Mwanzo**

| | |
|---|---|
| 2:15–17 | Apr. 28 |
| 15:6 | Jan. 13 |
| 22:2 | Mei 13 |
| 22:9 | Mei 13 |
| 26:24–25 | Feb. 26 |
| 32:1 | Ago. 6 |
| 32:28 | Sept. 10 |
| 39:20–21 | Juni16 |
| 39:21 | Julai 3 |
| 50:20 | Machi. 19, Okt. 15 |

**Kutoka**

| | |
|---|---|
| 2:5–6 | Aug. 20 |
| 2:12 | Julai 10 |
| 3:6 | Juni 28 |
| 4:31 | Juni 14 |
| 20:3, 8 | Feb. 21 |
| 34:29 | Ago. 10 |
| 36:9–13 | Julai 11 |

**Walawi**

**Hesabu**

| | |
|---|---|
| 1:5–7 | Mar. 13 |
| 11:28–29 | Jan. 3 |

**Kutoka**

| | |
|---|---|
| 4:35 | Nov. 9, Nov. 10 |
| 6:6–7 | June 21 |
| 6:23–25 | Agosti. 21 |
| 7:2–4 | Feb. 28 |
| 9:4 | Feb. 28 |
| 33:27 | Jan. 11 |
| 34:1, 4–6, 7, 10–12 | Jan. 23 |

**Yoshua**

| | |
|---|---|
| 1:1–3, 5–6 | Nov. 6 |
| 4:23–24 | Jan. 30 |
| 9:14 | Oct. 16 |
| 14:10–11 | Sept. 2 |
| 14:10–13 | Okt. 17 |
| 23:14 | Okt. 18 |

**Waamuzi**

**Ruthu**

**1 Samueli**

| | |
|---|---|
| 13:13–14 | Okt. 19 |
| 15:13–14 | Mei 10 |
| 30:8 | Machi. 26, Ago. 12 |

**2 Samueli**

**1 Wafalme**

| | |
|---|---|
| 16:30 | Julai 12 |
| 17:2–4 | Julai12 |
| 18:2–4 | Nov. 7 |
| 19:3, 4–5 | Jan. 31 |
| 19:12–13 | Juni 12 |

**2 Wafalme**

**1 Mambo ya Nyakati**

**2 Mambo ya Nyakati**

| | |
|---|---|
| 7:14 | Juni 10, Ago. 27 |

**Ezra**

| | |
|---|---|
| 1:1–2 | Julai 1 |
| 7:28 | Sept. 4 |

**Nehemia**

**Esta**

**Ayubu**

| | |
|---|---|
| 4:8 | Apr. 6 |

**Zaburi**

| | |
|---|---|
| 5:3 | Ago. 18, Okt. 1 |
| 19:1–2 | Jan. 4 |
| 23:3 | Julai 30 |
| 23:4 | Jan. 15 |
| 27:10 | Aug. 13 |
| 32:8 | Juni 4 |
| 34:8 | Mei 9 |
| 40:1 | Juni 11 |
| 42:1 | Jan. 18, Sept. 17 |
| 46:1–3, 11 | Feb. 1 |
| 51:4 | Mar. 23 |
| 62:1–2 | Julai 9 |

81:10–11 Ago. 9
88:13 Jan. 9
121:1–2 Julai 9

**Mithali**
1:3 Jan. 25
11:30 Feb. 7
19:11 Nov. 26

**Mhubiri**
12:1 Mei11

**Wimbo Ulio Bora**

**Isaya**
5:25 Ago. 19
30:18 Okt. 22
40:26 Jan. 12

**Yeremia**

**Maombolezo**

**Ezekieli**
36:25–27 Mei 7
36:26–27 Mar. 16

**Danieli**
3:18 Okt. 9

**Hosea**

**Yoeli**

**Amosi**

**Obadia**

**Yona**
2:8 Okt. 21

**Mika**

**Nahumu**

**Habakkuki**

**Sefania**

**Hagai**

**Zekaria**
8:16 Sept. 30

**Malaki**

## AGANO JIPYA

**Mathayo**
1:6 Apr. 1
1:20 Des. 25
2:11 Des. 23
2:16 Des. 20
2:23 Des. 21
4:19–20 Mar. 17
5:48 Mar. 25
6:8 Jan. 28
6:33 Ago. 24
7:11 Mei 29, Juni 19
7:17, 20 Ago. 7
9:5-8 Jan. 14
13:8 Feb. 7
18:15–16 Mar. 2
19:19 Dec. 13, Des. 14
19:27 Mei 3
21:22 Mar. 21
24:13 Mar. 14
24:45–47 Sept. 12
25:21 Mei 26, Mei 27
25:35–36 Sept. 1
25:36 Apr.26
26:39, 45–46 Apr. 8
28:7 Apr. 5
28:19 Feb. 7
28:20 Juni 11, Julai 16

**Marko**
5:19 Feb. 5, Feb. 6
10:17 Feb. 3

**Luka**
2:10 Des. 11
2:10–11 Des. 15
2:49–52 Jan. 16
3:21–22 Feb. 12
4:38–39 Aug. 1
5:4–6 Aug. 1
5:15–16 Jan. 22
9:12–17 Sept. 7
10:25 Ago. 4
10:27 Ago. 3
10:33 Sept. 24
11:2 Feb. 10
11:13 Mei 29, Nov. 18
15:4, 7 Mar. 7
16:10–12 Ago. 14
16:22–24 Okt. 8
18:22–23 Ago. 26
18:28–30 Ago. 26
19:2–4 Sept. 15
19:10 Ago. 24

21:14–15 Mar. 8
22:31–32 Mei 16
24:46–49 Des. 6
24:49 Mei 31

**Yohana**

1:9 Des. 26
1:12 Des. 26
2:19–22 Okt. 27
3:3 Feb. 22
3:17 Des. 18
4:6 Sept. 11
4:15 Mar. 11
4:34 Feb. 16
5:17 Oct. 11, Okt. 12
5:31–32 Apr. 19
6:40 Julai 31
6:44 Ago. 23
7:37–39 Sept. 25, Nov. 16
7:38–39 Ago. 11
8:12 Mei 15
8:3 Feb. 9
8:34 Nov. 25
8:44 Julai 6
9:25 Ago. 30
12:2–3 Mar. 18
12:25–26 Jan. 29
14:12 Julai 7, Julai 8
14:16–17 Juni 5
14:16–20 Des. 19
14:21 Feb. 13
14:27 Des. 10
15:9–10 Mei 14
15:16 Juni 23, Juni 24
16:7 Mar. 3
16:13 Juni 12
17:17 Des. 31
20:17–18 Apr. 9

**Matendo**

1:4–5 Okt. 22
1:8 Feb. 11, Okt. 29
2:4 Julai 24
2:14 Julai 24
2:17 Mei 20
2:19–22 Okt. 27
2:37 Julai 24
2:38–39 Jan. 10
2:42 Sept. 27
2:46–47 Sept. 27
3:6 Mar. 29
3:19 Jan.6, Mei 17
4:13 Apr. 23
4:12 Feb. 20
4:20 Julai 5
4:24 Des. 31
4:31 Apr. 23, Des. 31
5:32 Julai 17
6:1–4 Okt. 28
6:3 Sept. 29
6:5 Apr. 11, Sept. 29
7:35 Juni 8
7:55, 59–8:1 Mei 28
7:59–60 Apr. 11
8:18–19 Apr. 30, Julai 14
8:27 Julai 15
8:29 Apr. 30, Julai 14, Sept. 29
9:5 Jan. 26
9:26–27 Mar. 15
9:27 Jan. 5
10:15 Ago. 2
10:19 Ago. 22
11:23 Apr. 25
11:24 Juni 20
11:25–26 Jan. 5
16:14 Jan. 26
16:25–26, 29–30 Jan. 19
18:2–3 Juni 26
20:24 Juni 18
26:17–18 Nov. 17, Des. 12
26:18 Jan. 6

**Warumi**

1:4 Apr. 4
1:16 Mar. 9, Ago. 8
1:19 Ago. 31
2:1 Feb. 2
5:3–5 Apr. 16
5:5 Apr. 22, Juni 15
5:15 Juni 27
6:13 Okt. 25
6:14 Nov. 11
6:18 Nov. 12
7:20 Nov. 27, Nov. 28
7:23 Des. 28
8:1 Jan. 7
8:2 Mei 22, Mei 23, Julai 20, Des. 29
8:4 Mei 24, Julai20, Julai 21
8:28–29 Julai 25
12:1 Sept. 21, Nov. 8
12:1–2 Juni 29, Nov. 2

12:2 Sept. 22, Sept. 23
13:10 Apr. 29
15:16 Feb. 14, July 28
15:27–28 Des. 17
15:31–32 Jan. 24

**1 Wakorintho**

1:2 July 2
2:14 Des. 27
3:1–3 Des. 27
3:6–9 Sept. 19
4:2 Nov. 24
6:3 Sept. 18
6:9–10 Sept. 26
6:9–11 Apr. 24
6:19–20 Mei 5, Mei 6
9:26–27 Feb. 27
10:31 Mar. 4
12:12 Mar. 17
13:4 Sept. 28
13:4–5 Okt. 31
15:10 Mei 2
15:56–57 Julai 19

**2 Wakorintho**

2:15 Mei 25
3:3 Apr. 17
4:7–10 Okt. 13
5:8–10 Jan. 17
5:10 Mei 21
5:14 Sept. 5
5:17 Jan. 2
5:20 Juni 17
5:20–21 Des. 24
6:7–9 Sept. 5
6:14 Mar. 8
10:5 Apr. 21

**Wagalatia**

2:19–20 Nov. 29
2:20 Mar. 31
5:16–17 Julai 27
5:17 Okt. 24
5:22–23 Sept. 28
5:24–25 Julai 22, Okt. 14
5:25 Okt. 30, Des. 2
6:2 Ago. 29
6:7–8 Okt. 26
6:7–9 Sept. 19
6:8–9 Feb. 8
6:9 Ago. 29, Sept. 13, Nov. 14

**Waefeso**

1:13–14 Mar. 10
1:18–20 Apr. 12
2:8–9 Ago. 17
2:13 Apr. 3
2:14 Okt. 20
2:19 Mar. 27
3:7 Sept. 16
3:12 Apr. 7
3:16 Mei 18, Sept. 9
3:16–19 Des. 31
3:17 Juni 1, Juni 2
3:17–18 Julai 18
3:17–19 Feb. 17
3:19 Mar. 15
3:19–20 May 30
3:20 Juni 3
4:22–24 Apr. 18, Julai 26, Des. 7
4:29 Sept. 14
4:29–32 Mei 1
4:30 Feb. 10, Julai 21
5:17–18 Oct. 7
5:18 Juni 13, Nov. 19, Des. 31
5:18–21 Nov. 20
5:25–26 Mei 8, Nov. 21
5:25–27 Sept. 20
5:31 Juni 22
5:33 Mwi 8, Sept. 20
6:1 Mei 8
6:4 Mei 8
6:6–7 Sept. 3

**Wafilipi**

1:14 Okt. 10
2:5–8 Mar. 30
2:10 Okt. 25
2:14–16 Feb. 15
4:6–7 Jan. 20, Jan. 21
4:8 Julai 4
4:11–13 Mar. 20
4:12–13 Jan. 25

**Wakolosai**

1:22 Feb. 18
2:6 Mei 9
2:6–7 Mar. 14, Apr. 27
3:3 Nov. 23
3:12–14 Nov. 3, Nov. 4
3:22–24 Mar. 24

**1 Wathesalonike**

3:10 Des. 16

4:3 Mei 12, Des. 3, 4, 5, 8, 16, 29
4:8 Des. 16
5:16–18 Aug. 25, Nov. 22
5:23 Nov. 1, Des. 1, Des. 2
5:23–24 Des. 30
5:24 Juni 7, Nov. 5

**2 Wathesalonike**

**1 Timotheo**
4:12 Mei 4, Okt. 2

**2 Timotheo**
1:9 Mei 4
2:20–21 Julai 23
4:7–8 Apr. 13

**Tito**

**Filemoni**
1:1–2 Sept. 6
1:6 Sept. 6
1:16 Nov. 30

**Wahibrania**
1:14 Sept. 18
4:8–11 Sept. 8
4:15 Juni 25
9:28 Des. 22
10:10 Juni 30
10:14 Juni 30
10:23 Ago. 5
10:23–25 Feb. 19
10:35 Apr. 15
12:1–2 Julai 2
12:14 Ago. 16
13:5 Juni 11
13:12 Okt. 23

**Yakobo**
1:2–4 .Julai 13
1:13–16 Des. 9

**1 Petro**
2:24–25 Apr. 2
4:7–10 Mar. 6

**2 Petro**
3:9 Juni 9
3:10 Ago. 15
3:11–12 Juni 9
3:18 Feb. 22, Feb. 23

**1 Yohana**
1:7 Apr. 20, Julai 29
2:1 Jan. 27, Mar. 12, Nov. 15
3:16–17 Mei 19
4:4 Jan. 1
4:7 .Mar. 1, Nov. 21
4:9 Apr. 22
4:11 Apr. 22
4:13 Nov. 5
4:18 Feb. 4, Nov. 13
5:13 Juni 6

**2 Yohana**

**3 Yohana**
1:11 Ago. 28

**Yuda**

**Ufunuo**
1:5 Okt. 3
1:7 Aug. 15
2:10 Mar. 22
3:19–20 Feb. 25
3:20 Feb. 24
3:21 Jan. 8, Apr. 10
5:5 Oct. 4
11:15 Feb. 10
16:9 Okt. 5
20:12, 15 Mei 21
21:1 Mar. 28
21:2 Mar. 5
21:3–4 Mar. 28
21:7 Mar. 5, Apr. 14
22:7 Okt. 6